
ELLEN G. WHITE ESTATE

# Tumaini Kuu



ELLEN G. WHITE

**A revealing look at the battle between good and evil — and who wins.**

# Tumaini Kuu

**Ellen G. White**

**2013**

**Copyright © 2021**
**Ellen G. White Estate, Inc.**

# Information about this Book

## Overview

This eBook is provided by the Ellen G. White Estate. It is included in the larger free Online Books collection on the Ellen G. White Estate Web site.

## About the Author

Ellen G. White (1827-1915) is considered the most widely translated American author, her works having been published in more than 160 languages. She wrote more than 100,000 pages on a wide variety of spiritual and practical topics. Guided by the Holy Spirit, she exalted Jesus and pointed to the Scriptures as the basis of one's faith.

## Further Links

A Brief Biography of Ellen G. White
About the Ellen G. White Estate

## End User License Agreement

The viewing, printing or downloading of this book grants you only a limited, nonexclusive and nontransferable license for use solely by you for your own personal use. This license does not permit republication, distribution, assignment, sublicense, sale, preparation of derivative works, or other use. Any unauthorized use of this book terminates the license granted hereby. (See EGW Writings End User License Agreement.)

## Further Information

For more information about the author, publishers, or how you can support this service, please contact the Ellen G. White Estate

at mail@whiteestate.org. We are thankful for your interest and feedback and wish you God's blessing as you read.

# Contents


Information about this Book . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . i
Kwa Nini Huna Budi Kusoma Kitabu Hiki . . . . . . . . . . . . . . . . . . . x
Kuufunua Wakati Ujao . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . xii
Sura Ya 1 - Utabiri Wa Hatima Ya Dunia . . . . . . . . . . . . . . . . . . 19
Hekalu Zuri Lakabiliwa na Uharibifu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 21
Uvumilivu wa Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 23
Ilani za Janga . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 24
Sura Ya 2 - Wakristo Wa Awali-Watii Na Wakweli . . . . . . . . . . . 28
Makundi Mawili Kanisani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 30
Sura Ya 3 - Giza La Kiroho Katika Kanisa La Awali . . . . . . . . . 33
Jinsi Sabato "Ilivyobadilishwa" . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 34
Siku za Hatari kwa Kanisa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 37
Jinsi Mafundisho ya Uongo Yalivyoingia . . . . . . . . . . . . . . . . . 38
Sura Ya 4 - Wawaldensia Waitetea Imani . . . . . . . . . . . . . . . . . . 41
Roma Vakabiliana na Dini ya Biblia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 42
Kanuni za Ukweli Zilizokuwa Zinathaminiwa . . . . . . . . . . . . . 44
Vijana Waliofundishwa Kuwa Wamisionari . . . . . . . . . . . . . . . 46
Wenye Dhambi Waelekezwa kwa Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . 47
Kuuvamia Ufalme wa Shetani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 48
Kanisa la Roma Laazimu Kuwaangamiza Wawaldensia . . . . 49
Sura Ya 5 - Nuru Yachomoza Uingereza . . . . . . . . . . . . . . . . . . 51
Mgunduzi wa Uovu Aliyc Makini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 52
Kushambuliwa na Ugonjwa wa Kutisha . . . . . . . . . . . . . . . . . . 55
Wycliffe Akataa Kukanusha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 57
Mpiga Mbiu wa Zama Mpya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 58
Sura Ya 6 - Mashujaa Wawili Wakabili Mauti . . . . . . . . . . . . . . 61
Picha Mbili Zamvutia Huss . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 62
Prague Yawekwa Kwenye Katazo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 63
Hati ya Usalama Kutoka kwa Mfalme . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 65
Ushindi Waonekana Mapema . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 67
Huss Afa kwa Kuchomwa Moto . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 68
Jerome Ajisalimisha kvva Baraza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 69
Jerome Apata Toba na Ujasiri Mpya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 70
Kuamriwa Kwenda Gerezani na Kufa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 72

Kusalitiwa na Diplomasia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 74
Sura Ya 7 - Luther, Mwanamume Kwa Wakati Wake . . . . . . . . 76
Kuitafuta Amani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 77
Ukweli Kwenye Ngazi ya Pilato . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 79
Mauzo ya Vyeti vya Msamaha wa Dhambi . . . . . . . . . . . . . . 80
Kazi ya Luther Vaanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 81
Luther Alikata Rufaa kwenye Biblia Pekee . . . . . . . . . . . . . . 83
Kutoroka Augsburg . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 86
Zahama ya Kutisha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 88
Sura Ya 8 - Mtetezi Wa Ukweli . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 91
Luther Ashitakiwa kwa Uasi wa Kidini . . . . . . . . . . . . . . . . . 92
Luther Aitwa Shaurini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 94
Ujasiri wa Mfia-dini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 95
Luther Asimama Mbele ya Baraza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 97
Luther Mbele ya Mkutano kwa Mara Nyingine . . . . . . . . . . . 99
Ulinzi wa Luther Hatarini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 102
Jitihada za Mapatano na Kanisa la Roma . . . . . . . . . . . . . . . 104
Mungu Amtumia Frederick wa Saxony . . . . . . . . . . . . . . . . 106
Usalama Kule Wartburg . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 106
Sura Ya 9 - Nuru Yaamshwa Nchini Uswisi . . . . . . . . . . . . . . 108
Zwingli Aitwa Kwenda Zurich . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 110
Kuuzwa kwa Hati za Msamaha Nchini Uswisi . . . . . . . . . . 111
Mabishano Na Watawala wa Kanisa la Roma . . . . . . . . . . . 113
Sura Ya 10 - MAENDELEO NCHINI UJERUMANI . . . . . . . 116
Tunda la Mafundisho Mapya Ladhihirika . . . . . . . . . . . . . . 117
Nguvu ya Neno . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 118
Masumbuko Makali Moyoni Sasa Vamshinikiza Luther . . . 120
Kujifunza Biblia Kila Mahali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 121
Sura Ya 11 - Upinzani Wa Wakuu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 123
Msimamo Adilifu wa Wakuu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 125
Mkutano wa Augsburg . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 127
Sura Ya 12 - Pambazuko Nchini Ufaransa . . . . . . . . . . . . . . . 130
Agano Jipya kwa Lugha ya Kifaransa . . . . . . . . . . . . . . . . . 132
Ujasiri wa Berquin . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 133
Berquin Achomwa Moto . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 134
Kuitwa kwa Calvin . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 135
Kushuhudia Mtu Akichomwa Moto . . . . . . . . . . . . . . . . . . 136
Enzi ya Hofu Kuu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 138

Uchapishaji Wapigwa Marufuku . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 139
Froment Mwalimu wa Shule . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 143
Ngurumo ya Apizo la Kanisa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 144
Ushindi kwa Wanamatengenezo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 145
Sura Ya 13 - Uholanzi Na Scandinavia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 147
Matengenezo Nchini Denmark . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 149
Maendeleo Nchini Sweden . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 150
Sura Ya 14 - Maendeleo Ya Ukweli Uingereza . . . . . . . . . . . . 152
Tyndale Atafsiri Agano Jipya kwa Kiingereza . . . . . . . . . . . 153
Maandiko Matakatifu-Mamlaka Isiyokosea . . . . . . . . . . . . . 154
John Knox . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 155
Maelfu ya Wachungaji Watimuliwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 156
Kuhesabiwa Haki kwa Njia ya Imani . . . . . . . . . . . . . . . . . . 157
Moyo wa Wesley Wapata Joto kwa Njia ya Ajabu . . . . . . . 159
Wesley Anusurika Kifo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 160
Kuilinda Sheria ya Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 162
Upatanifu wa Sheria na Injili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 163
Sura Ya 15 - Enzi Ya Hofu Kuu Ufaransa: Chimbuko Lake Halisi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 164
Utimilifu wa Kuvutia wa Unabii . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 166
Ladui Dhidi ya Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 166
Uovu wa Kutisha zaidi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 167
Ushupavu katika Kumtukana Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . 169
Mungu Mke wa Hekima . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 170
Kile Ambacho Kingetokea . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 172
Kuvuna Katika Damu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 173
Kosa Baya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 176
Sura Ya 16 - Kuutafuta Uhuru Katika Ulimwengu Mpya . . . . 178
Mungu Alidhibiti Matukio . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 179
Roger Williams . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 180
Hati ya Uhuru . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 181
Kinga ya Uhakika kwa Ukuu wa Taifa . . . . . . . . . . . . . . . . 182
Sura Ya 17 - Ahadi Za Ujio Wakristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 184
Tetemeko Lililotikisa Dunia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 186
Mwezi Na Jua Vyatiwa Giza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 187
Mwezi Kama Damu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 188
Mmwito wa Kuamka . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 190
Ujumbe Watolewa na Watu Duni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 191

Sura Ya 18 - Nuru Mpya Katika Ulimwengu Mpya . . . . . . . . 195
Miller Apata Rafiki . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 196
Kuja Kwa Kristo Katika Mwili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 197
Maandiko na Matukio ya Miaka . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 198
Kugundua Ratiba ya Unabii . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 200
Vipindi Viwili vya Wakati Vyaanza Pamoja . . . . . . . . . . . 201
Injili Iliyotolevva Kvva Ulimwengu . . . . . . . . . . . . . . . . . 201
Hitimisho la Kushtusha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 202
“Nenda Kauambie Ulimwengu” . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 203
“Nyota Zitaanguka” . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 204
Utabiri Watimia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 205
Shauku na Kutokuamini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 206
Wabishi na Wasioamini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 207
Sura Ya 19 - Kwa Nini Matumaini Yalivunjika? . . . . . . . . . . . 210
“Wakati Umetimia” . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 211
Kukata Tamaa Hadi Uhakika . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 213
Ujumbe wa Wanafunzi Ukilinganishwa na Ujumbe wa Mwaka 1844 . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 213
Sura Ya 20 - Kuupenda Ujio Wakristo . . . . . . . . . . . . . . . . . 216
Katika Nchi Mbalimbali kwa Wakati Mmoja . . . . . . . . . . . . 217
Tofauti na Fasili za Wengi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 219
Uwezo Ndani ya Kitabu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 219
Ujumbe wa Ujio Kule Uingereza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 220
Ufunuo Wadhihirika kwa Bengel . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 221
Wahubiri Watoto wa Scandinavia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 222
Ujumbe Waenea . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 223
Maandiko Sahili Valeta Imani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 224
Ujumbe Wapingwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 224
Sura Ya 21 - Kuvuna Upepo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 228
Wanadamu Waikataa Nuru . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 229
Ujumbe wa Malaika wa Kwanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 230
Ujumbe wa Malaika wa Pili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 231
Uzinzi wa Kiroho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 231
Kuungana na Ulimwengu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 233
Hatua za Kwanza za Kuiacha Injili . . . . . . . . . . . . . . . . . . 234
Sura Ya 22 - Unabii Watimia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 237
Itikadi Kali Zajitokeza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 239
Makosa Yarekebishwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 240

"Kelele ya Usiku wa Manane" . . . 241
Matumaini Yavunjika Tena . . . 242
Ujumbe Uliotolewa kwa Wakati Mwafaka . . . 243
Imani Yadumishwa . . . 244
Sura Ya 23 - Fumbo Lililo Wazi La Patakatifu . . . 246
Patakatifu na Patakatifu Sana . . . 247
Vile Vyumba Viwili . . . 248
Fumbo la Patakatifu Lafumbuliwa . . . 250
Kutakaswa kwa Patakatifu . . . 251
Siku kuu ya Upatanisho . . . 251
Jambo Halisi Mbinguni . . . 252
Kazi ya Hukumu . . . 253
Sura Ya 24 - Yesu Anafanya Nini Sasa? . . . 255
Nani Atasimama? . . . 256
"Haya, Bwana Arusi" . . . 256
Kumngoja Bwana Wao . . . 257
Kazi ya Mwisho ya Patakatifu . . . 258
Sura Ya 25 - Sheria Ya Mungu Haibadiliki . . . 261
Mmwito wa Kumsujudia Mwumbaji . . . 263
Kuinuka Kwa Mamlaka Nyingine . . . 264
Mnyama na Sanamu Yake . . . 268
Ukimya Mkubwa wa Agano Jipya . . . 269
Onyo la Malaika wa Tatu . . . 271
Sura Ya 26 - Watetezi Wa Ukweli . . . 272
Sabato ya Kweli Imekuwa IkishikwaDaima . . . 273
Siyo Mapenzi ya Mungu . . . 274
Sura Ya 27 - Uamsho Wa Kisasa Umefanikiwa Kwa Kiasi Gani? . . . 277
Sheria ya Uhuru . . . 279
Hatia ya Dhambi . . . 280
Utakaso ni Nini? . . . 281
Ni Kwa Njia ya Imani Pekee . . . 282
Utakaso Unaotajwa Kwenye Biblia . . . 283
Sura Ya 28 - Kukabiliana Na Kumbukumbu Ya Maisha Yetu 287
Makusudi ya Siri . . . 288
Kipimo cha Hukumu . . . 289
Bwana Anamkemea Shetani . . . 290
Kuzifuta Dhambi . . . 291

WakatiUIioamuIiwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 291
Ubinafsi Uliofichwa Wafunuliwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 292
Maombezi ya Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 293
Hatima ya Wote Kuamuliwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 294
Sura Ya 29 - Kwa Nini Dhambi Iliruhusiwa? . . . . . . . . . . . . . . 295
Kutoridhika Miongoni mwa Malaika . . . . . . . . . . . . . . . . . 297
Chuki Yakomaa na kuwa llasi Halisi . . . . . . . . . . . . . . . . . . 298
Kufukuzwa Kutoka Mbinguni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 299
Hoja kwa Ajili ya Kumsaidia Mwanadamu . . . . . . . . . . . . . 301
Sura Ya 30 - Shetani Na Mwanadamu Vitani . . . . . . . . . . . . . . 302
Adui Aliye Macho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 303
Sura Ya 31 - Roho Za Uchafu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 305
Malaika Walinzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 306
Sura Ya 32 - Namna Ya Kumshinda Shetani . . . . . . . . . . . . . . 309
Ukweli Unatakasa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 310
Biblia Nzivna ni Kiongozi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 311
Makosa ya Hatari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 312
Mipaka ya Neno . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 313
Ushahidi wa Kutosha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 314
Sura Ya 33 - Baada Ya Kifo Kinachotokea Nl Nini ? . . . . . . . 316
Udanganyifu Mkuu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 317
Fundisho Potovu la Mateso ya Milele . . . . . . . . . . . . . . . . . 318
Wokovu wa Jumla Siyo Fundisho la Maandiko . . . . . . . . . . 319
Masharti Vamewekwa Bayana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 320
Hawajajitayarisha Kuingia Mbinguni . . . . . . . . . . . . . . . . . 321
Mshahara wa Dhambi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 321
Ufufuo wa Kwanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 322
Sura Ya 34 - Roho Nl Nani Katika Imani Ya Mizimu? . . . . . . 326
Ushawishi wa Shetani kwa Wasomi . . . . . . . . . . . . . . . . . . 327
Ushawishi kwa Wanaopenda Anasa . . . . . . . . . . . . . . . . . . 328
Biblia Inawakilishwa Kama Riwaya . . . . . . . . . . . . . . . . . . 329
Sura Ya 35 - Kutishiwa Kwa Uhuru Wa Dhamiri . . . . . . . . . . 332
Maridhiano na Makubaliano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 333
Mlandano wa Kuvutia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 334
Muungano wa Upagani na Ukristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 335
Badiliko Ndani ya Uprotestanti . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 336
Kuishika Jumapili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 337
Mnyama Mwenye Pembe kama za Mwanakondoo . . . . . . . 339

Sura Ya 36 - Pambano Linalokaribia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 342
Kuiweka Pembeni Sheria ya Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 343
Kutokuwa Na Kiasi KumewapumbazaWengi . . . . . . . . . . . . 344
Sura Ya 37 - Usalama Wetu Pekee . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 348
Kuinua Mamlaka Ya Binadamu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 349
Wajibu wa Kwanza wa Muhimu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 350
Matokeo ya Kupuuzia Maombi na Kujifunza Biblia . . . . . . 351
Sura Ya 38 - Ujumbe Wa Mwisho Wa Mungu . . . . . . . . . . . . . 353
Jaribio Kuu la Uaminifu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 354
Dhoruba Inakaribia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 356
Upinzani Kuinuka Katika Viwango vya Juu Zaidi . . . . . . . 356
Sura Ya 39 - Wakati Wa Taabu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 359
Wakati Wa Taabu Ya Yakobo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 360
Mungu Analaumiwa Kwa Sababu ya Maumivu . . . . . . . . . . 362
Kufutwa kwa Dhambi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 362
Imani Inayostahimili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 363
Watu wa Mungu Hawatapotoshwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 365
Makundi ya Malaika Wanalinda . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 367
Sura Ya 40 - Watu Wa Mungu Wakombolewa . . . . . . . . . . . . . 370
Siku ya Bwana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 371
Kutokea kwa Mfalme wa Wafalme . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 372
Katika Mji Mtakatifu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 375
Kukutana kwa Adamu Wawili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 376
Waliokombolewa Wakiwa Kwenye Utukufu . . . . . . . . . . . . 377
Sura Ya 41 - Dunia Ikiwa Magofu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 380
Malaika wa Mauti. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 381
Kifungo Cha Shetani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 382
Sura Ya 42 - Amani Ya Milele: Pambano Lafika Mwisho . . . 385
Shambulizi la Mwisho Dhidi ya Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . 386
Hukumu Yatolewa Dhidi Ya Waasi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 387
Shetani Ameshindwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 389
Mwisho Mbaya wa Waovu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 391
Mambo Yanayotukumbusha Kusulubishwa kwa Mwokozi 392
Kushinda Kwa Upendo Wa Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 393

# Kwa Nini Huna Budi Kusoma Kitabu Hiki

Kwa mamilioni ya watu, maisha ni kama jambo lisilo na maana wala mantiki. Sayansi, teknolojia, hata falsafa na teolojia, huwachukulia watu kama viumbe waliotokea kwa kudra. Lakini watu, wakijua au bila kujua, wameshindwa kukubaliana na maisha yasiyokuwa na malengo. Ghasia, upinzani na uasi, kujaribisha madawa ya kulevya—mambo haya kwa sehemu kubwa, ni namna ya watu kuonesha kuwa wanahangaika katika upotevu wao mkubwa.

Wanalia katika upweke na kukata tamaa kama watoto waliotawanyika kwa sababu ya vita, "Mimi ni nani? Wazazi wangu walikuwa akina nani? Ninawezaje kuwapata?" Wengi tunaigeukia sayansi ili tupate majibu, tukitegesha darubini zetu kubwa zitumiazo mionzi, kutazama mwenendo wa nyota kana kwamba tunauliza, "Kuna mtu ye yote anayenijua huko? Ni nani anayenijali? Lakini sayansi haina jibu. Sayansi ipo kwa ajili ya kuuliza maswali: Atomu imeundwaje, Inawezaje kugawanyika? Akili zetu zinafanyaje kazi? Ulimwengu wetu umeumbwaje?

Sayansi haiwezi kutwambia kwa nini kuna atomu, kwa nini wanadamu wapo, kwa nini ulimwengu upo. Wala haiwezi kujibu maswali ya pekee yanayowasumbua wanazuoni:Kama kuna kusudi jema na haki ulimwenguni, kwa nini waatu wema huteseka pamoja na waovu?

Je, kuna uhai baada ya kifo? Je, haiba ya mtu huwa inaendelea kuishi? Makanisa ya leo ya Kikristo yanamwakilisha Mungu? Ukweli ni nini?

Mustakabali wa ulimwengu ukoje? Je, utakoma huku ukilialia kama mtoto anayehangaika kuvuta hewa ya mwisho katika hali ya hewa iliyochafuka, au kwa mlipuko wa jehanamu utakatokana na makombora? Au, wanadamu-ambao katika historia hawajaweza kuonesha uwezo wa kuudhibiti ubinafsi wao-wataweza ghafla kukomesha uovu, vita, umaskini na hata mauti?

Kitabu hiki kinatoa majibu, tena ya kututoa wasiwasi. Uhai una makusudi! Hatuko peke yetu ulimwenguni. Kuna anayejali

mahali fulani! Yupo kweli, aliyejihusisha na historia ya wanadamu, yeye aliyejiunga na jamii yetu, ili tuweze kumfikia na yeye aweze kutufikia yeye ambaye mkono wake wenye nguvu umekuwa juu ya sayari hii na ambaye ataiongoza kurudi kwenye amani-tena upesi.

Lakini miaka mingi iliyopita, kiumbe mmoja mlaghai ulimwen- [12]
guni aliazimu kuitawala dunia yetu na kuuharibu mpango wa Mungu kwa ajili ya furaha ya familia yake ya duniani. Mwandishi wa kitabu hiki, ametumia lugha ya vielelezo—ambayo maelfu ya watu wameiita lugha iliyovuviwa—anafunua mambo yaliyokuwa hayajulikani sana na kuianika wazi mikakati ya kiumbe huyu mwenye nguvu, asiyeonekana, ambaye mikono yake iko tayari kuitawala wa dunia yetu. Kwa upande wa wanadamu, watawala wa kipagani pamoja na taasisi za kidini wanadhihirishwa kuwa washirika walio na hatia katika njama hizo.

Kitabu hiki kingeweza kuchapwa na kusambazwa katika kipindi chenye uhuru wa kidini tu, kwani kinazianika baadhi ya taasisi zenye nguvu kabisa katika siku zetu. Kinaeleza kwa nini matengenezo yalihitajika, na kwa nini yalisimamishwa; kisa cha makanisa yaliyoasi, juu ya ushirika wa watesi, muungano unaojitokeza wa kanisa na serikali ambao utafanya sehemu yake ya kidhalili kabla pambano kuu kati ya wema na uovu halijaisha. Katika pambano hili kila mwanadamu anahusika.

Mwandishi huyu anaandika hapa kuhusu mambo yaliyokuwa hayapo wakati wa uhai wake. Anaeleza kwa uaminifu usio wa kawaida. Masuala ya pambano ni makubwa na matokeo yake ni nyeti sana kiasi kwamba ilipasa mtu fulani atoe maneno haya ya kuonya na kuelimisha.

Hakuna mtu atakayefiingua kurasa za kitabu hiki kisha akakiweka bila kujiuliza kama haikuwa bahati kukiona.

Wachapaji

[13] ## Kuufunua Wakati Ujao

Kabla ya dhambi kuingia, Adamu alikuwa na fursa ya kuwasiliana moja kwa moja na Mwumbaji wake; lakini tangu mwanadamu alipojitenga na Mungu kwa kukosa, jamii ya wanadamu iliondolewa katika fursa hii kubwa. Hata hivyo, njia imefunguliwa kwa wakazi wa dunia kuwa na uhusiano na mbingu. Mungu amekuwa akiwasiliana na watu kwa njia ya Roho wake, na nuru ya mbingu imekuwa ikitolewa kwa ulimwengu kwa mafunuo yatolewayo kwa watumishi wake. "Wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu." 2 Pet. 1:21.

Katika miaka 2500 ya kwanza ya historia ya mwanadamu, hakukuwa na mafunuo yaliyoandikwa. Wale waliokuwa wamefundishwa na Mungu waliwasilisha ujuzi wao kwa wengine, na ujuzi huo ulikuwa unakabidhiwa toka kwa baba kwenda kwa mtoto, kwa vizazi vingi. Maandalizi ya neno lililoandikwa yalianza wakati wa Musa. Mafunuo yenye uvuvio yaliwekwa katika kitabu kilichovuviwa. Kazi hii iliendelea kwa kipindi kirefu cha miaka 1600—kuanzia kwa Musa, mwana historia wa uumbaji na sheria, hadi kwa Yohana, mwandishi wa ukweli nyeti wa Injili.

Biblia inamtaja Mungu kuwa mtunzi wake; lakini iliandikwa kwa mikono ya wanadamu; na katika mitindo tofauti ya vitabu vyake mbalimbali, inaonesha sifa bainifu za waandishi wake wengi. Ukweli wote uliofunuliwa, ulitolewa kwa "pumzi ya Mungu" (2 Tim.3:16); japo umeelezwa kwa maneno ya watu. Yeye asiye na ukomo aliangaza nuru katika akili na mioyo ya watumishi wake kwa njia ya Roho wake Mtakatifu. Aliwapa ndoto na njozi, vielelezo na mifano; na wale waliooneshwa ukweli huo waliyatafsiri mawazo hayo katika lugha za wanadamu.

Vikiwa vimeandikwa katika kame tofauti, na watu waliokuwa wanatofautiana sana katika nyadhifa na katika kazi, kiakili na kiroho, vitabu vya Biblia wanaonesha tofauti kubwa katika mitindo, na pia tofauti katika aina ya mada zinazoelezewa. Aina mbalimbali za usemi zimetumia na waandishi tofauti; mara nyingi ukweli ule ule

umeelezewa kwa namna ya kuvutia zaidi na mwandishi mmoja kuliko ulivyoelezewa na mwingine. Na kwa vile waandishi mbalimbali huwasilisha mada wakizingatia vipengele tofauti na maelezo ya aina [14] mbalimbali, mambo hayo yanaweza kuonekana kuwa ni tofauti au yanakinzana kwa msomaji wa juu juu, asiye makini au mwenye mtazamo wa kupinga, wakati msomaji makini mwenye utauwa, akiwa na ufahamu wa kina, ataona upatanifu uliomo.

Kama ulivyowasilishwa na watu mbalimbali, ukweli unakuja katika vipengele vyake vinavyotofautiana. Mwandishi mmoja anaguswa zaidi na sehemu moja ya suala fulani; anayashika mambo yanayokwenda sambamba na hali yake au uweza wake wa kutambua; mwingine hushika sehemu nyingine; na kila mmoja, kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, anawasilisha kile kilichogusa zaidi akili yake—kila mmoja akiwa na upande tofauti wa ukweli, lakini kukiwa na mwafaka mkamilifu kote. Na ukweli uliooneshwa kwa njia hiyo huungana kuunda kitu kizima kikamilifu, kinachofaa kukidhi mahitaji ya wanadamu katika hali zote na matukio yote katika maisha.

Mungu aliona vyema kuwasilisha ukweli wake duniani kwa kutumia wanadamu, na yeye mwenyewe, kwa njia ya Roho wake Mtakatifu, aliwapa watu uweza na kuwawezesha kufanya kazi hiyo. Aliongoza akili zao katika kuchagua mambo ya kusema na ya kuandika. Hazina ilikabidhiwa kwa vyombo vya udongo, lakini iliendelea kuwa ya mbinguni. Ushuhuda unatolewa kwa misemo dhaifu ya yenye upungufii wa lugha za wanadamu, lakini ni ushuhuda wa Mungu; na mtoto wa Mungu ambaye ni mtiifu na anayeamini ataona ndani yake utukufu wa uwezo wa Mungu, uliojaa neema na kweli.

Katika Neno lake, Mungu amekabidhi watu ujuzi ulio muhimu kwa ajili ya wokovu. Maandiko Matakatifu yanapaswa kukubaliwa kama ufunuo wa mapenzi ya Mungu ulio na mamlaka, usiokosea. Maandiko ndiyo kiwango cha tabia, chanzo cha mafundisho, na kipimo cha mwenendo. "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema." 2 Tim. 3:16, 17.

Hata hivyo, kitendo cha Mungu kufunua mapenzi yake kwa watu kwa kutumia Neno lake hakipunguzi umuhimu wa uwepo wa uongozi endelevu wa Roho Mtakatifu. Kinyume chake, Mwokozi

[15] wetu aliahidi uwepo wa Roho, ili kufunua Neno kwa watumishi wake, kuangazia na kuyafanyia kazi mafundisho yake. Na kwa kuwa Roho wa Mungu ndiye aliyeivuvia Biblia, haiwezekani kwa mafundisho ya Roho kupingana na Neno.

Roho hakutolewa—na hawezi kutolewa—ili achukue nafasi ya Biblia; kwani Maandiko yanasema wazi kabisa kwamba Neno la Mungu ndiyo kipimo cha mafundisho na mwenendo wote. Mtume Yohana anasema, "msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani." 1 Yoh. 4:1. Isaya naye anasema, "Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Isa. 8:20.

Fedheha kubwa imeletwa katika kazi ya Roho Mtakatifu na makosa ya kundi la watu ambao, wakati wanadai kuwa wamepata maarifa katika katika Neno la Mungu, wanasema kuwa hawahitaji uongozi zaidi wa Neno la Mungu. Wanatawaliwa na hisia ambazo wanadhani ni sauti ya Mungu ndani ya moyo. Lakini roho inayowatawala si yule Roho wa Mungu. Tabia hii ya kufuata hisia na kupuuza Maandiko, inaweza kuleta machafuko, udanganyifu na uharibifu. Inasaidia tu kuendeleza makusudi ya yule mwovu. Kwa kuwa kazi ya Roho Mtakatifu ni ya muhimu kwa kanisa la Kristo, moja ya malengo ya Shetani ni kuifedhehesha kazi ya Roho kwa njia ya makosa ya watu wenye itikadi kali, na kuwafanya watu wakipuuze chanzo hiki cha nguvu ambacho Bwana wetu ametupatia.

Sambamba na Neno la Mungu, Roho wa Mungu alikuwa aendelee kufanya kazi yake katika kipindi chote cha Injili. Wakati Maandiko ya Agano la Kale na Jipya yakitolewa, Roho Mtakatifu hakukoma kuwasilisha nuru katika akili za kila mtu, kando ya mafunuo ambayo yangeingizwa katika Maandiko. Biblia yenyewe inaeleza jinsi watu walipokea, kwa njia ya Roho Mtakatifu, maonyo, makaripio, ushauri na maelekezo katika masuala ambayo hayakuhusika na utoaji wa Maandiko. Na wanatajwa manabii ambao maneno yao hayajaandikwa. Vivyo hivyo, baada ya kumalizika kazi ya kuandika Maandiko, Roho Mtakatifu alikuwa aendelee na kazi yake ya kuelimisha, kuonya, na kuwafariji watoto wa Mungu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.."

"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote: ... na mambo yajayo atawapasha habari yake." Yn. 14:26; 16:13. Maandiko yanafundisha wazi kabisa kuwa, ahadi hizi hazikuwa zimekusudiwa kwa ajili ya kanisa la mitume tu, bali zilikuwa zinaendelea katika kanisa la Kristo katika vizazi vyote. Mwokozi aliwahakikishia wafuasi wake, "mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Mt. 28:20. Paulo pia anasema kuwa karama na kazi za Roho ziliwekwa kanisani "kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili Wakristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu Wakristo." Efe. 4:12, 13. [16]

Mtume Paulo aliwaombea waumini wa Efeso, "Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye; macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mmwito wake jinsi lilivyo; ... na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo." Efe. 1:17-19. Kazi ya Roho wa Mungu katika kuelimisha akili na kuzionesha mambo ya kina ya Neno Takatifu la Mungu ni baraka ambayo Paulo alikuwa akiitafuta kwa ajili ya kanisa la Efeso.

Baada ya udhihirisho wa ajabu wa Roho Mtakatifu katika Siku ya Pentekoste, Petro aliwasihi watu watubu na kubatizwa katika jina la Kristo, kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao; akisema: "nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Mdo. 2:38, 39.

Kwa njia ya nabii Yoeli, Bwana alikuwa ameahidi udhihirisho maalum wa Roho wake sambamba na matukio ya siku kuu ya Mungu. Yoe. 2:28. Unabii huu ilitimia kwa sehemu katika kumwagwa kwa Roho Siku ya Pentekoste; lakini utatimia kikamilifu zaidi katika udhihirisho wa neema ya Mungu itakayoongoza kazi ya mwisho ya Injili. Pambano kuu kati ya wema na uovu litazidi kuwa kali hadi mwisho wa wakati. Katika kame zote hasira ya Shetani imekuwa ikidhihirishwa dhidi ya kanisa la Kristo; na Mungu amewapa watu wake neema na Roho, ili kuwaimarisha wasimame dhidi ya nguvu za yule mwovu. Wakati mitume Wakristo

walipotakiwa kupeleka Injili yake kwa ulimwengu na kuiandika kwa
[17] ajili ya vizazi vya baadaye, walikuwa wanaangaziwa na Roho kwa namna ya pekee. Lakini kanisa linavyokaribia ukombozi wake wa mwisho, Shetani atafanya kazi kwa nguvu zaidi. Atakuja akiwa "mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu." Ufu. 12:12. Atafanya kazi, "kwa uwezo wote, na ishara, na ajabu za uongo." 2 Thes. 2:9. Kwa miaka 6,000 kiumbe huyu mwenye akili nyingi aliyewahi kuwa juu zaidi miongoni mwa malaika wa Mungu amekuwa akifanya kwa bidii kazi ya kudanganya na uharibifu. Na undani wote na ujuzi wa kishetani uliopatikana, ukatili wote aliobuniwa katika wakati wa mapambano haya ya enzi, utatumika dhidi ya watu wa Mungu katika pambano la mwisho. Na wakati huo wa hatari, wafuasi Wakristo watapeleka onyo la ujio wa Bwana; na jamii ya watu itaandaliwa kwa ajili ya kusimama mbele yake wakati wa kuja kwake, wakiwa hawana "mawaa wala aibu mbele yake." 2 Pet. 3:14. Wakati huu, kipawa maalum cha neema ya Mungu na uwezo hakitahitajika kidogo kwa kanisa kuliko kilivyokuwa kinahitajika wakati wa mitume.

Kwa kuangaziwa na Roho Mtakatifu, matukio ya pambano kati wema na uovu, ambalo limedumu kwa muda mrefu yamekuwa yakifunuliwa kwa mwandishi wa kitabu hiki. Mara nyingi nimeruhusiwa kuona mambo ya pambano kuu kati ya Kristo, Mfalme wa uzima, Mwanzilishi wa wokovu, na Shetani, mfalme wa uovu, mwanzilishi wa dhambi, mvunjaji wa kwanza wa sheria takatifu ya Mungu. Uadui wa Shetani dhidi ya Kristo umedhihirishwa dhidi ya wafuasi Wakristo. Chuki ile ile dhidi ya kanuni za sheria ya Mungu, sera ile ile ya udanganyifu, inayofanya uongo uonekane kama ukweli, inayofanya sheria za wanadamu zishikwe badala ya sheria ya Mungu, na watu wamefanywa waabudu kiumbe badala ya Mwumbaji, inaweza kuonekana katika historia yote iliyopita. Juhudi za Shetani za kuwasilisha vibaya tabia ya Mungu, ili kuwafanya watu wang'ang'anie dhana potovu juu ya Mwumbaji, na hivyo kumtazama kwa hofu na chuki badala ya upendo; juhudi zake za kuweka kando sheria ya Mungu, kuwafanya watu wajione kuwa hawafungwi na sheria hiyo; na mateso yake kwa wale wanaothubutuu kuupinga udanganyifu wake, yameonekana katika hisitoria ya wazee, manabii na mitume, hisitoria ya wafia dini na wanamatengeneo.

Katika pambano kuu la mwisho, Shetani atatumia sera hiyo hiyo, atadhihirisha roho hiyo hiyo, na atafanya kazi zake kwa makusudi yale yale aliyokuwa nayo katika kame zilizopita. Kile ambacho kimekuwepo kabla, kitakuwepo, isipokuwa pambano linalokuja [18] litakuwa kali na la kutisha kuliko lo Iote ambalo dunia imewahi kulishuhudia. Udanganyifu wa Shetani utakuwa wa hila zaidi na mashambulizi yake yatakuwa ya ushupavu zaidi. Kama yumkini, atawapotosha wateule. Mk. 13:22.

Kwa kuwa, Roho wa Mungu ameufunua katika akili zangu, ukweli mkuu wa Neno lake na matukio yaliyopita na yajayo, nimeagizwa kuwajulisha wengine mambo niliyooneshwa—kuielezea historia ya pambano katika enzi zilizopita, na hasa kuiwakilisha katika namna ambayo itaangazia pambano lijalo ambalo linakuja upesi. Ili kutimiza lengo hilo nimejitahidi kuchagua na kuweka pamoja matukio katika historia ya kanisa katika njia ambayo itaonesha kufunuliwa kwa ukwei upimao ambao katika vipindi fulani umekuwa ukitolewa kwa ulimwengu, ukawasha hasira ya Shetani na chuki ya kanisa lipendalo ulimwengu, na ambao umeendelea kudumishwa kwa ushuhuda wa wale "ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. Katika maandishi haya tunaweza kupata picha ya pambano lililo mbele yetu. Tukiyaangalia kwa kuzingatia Neno la Mungu, na kwa kuangaziwa na Roho wake, tunaweza kuona hila za yule mwovu zikiwekwa wazi pamoja na hatari ambazo inawapasa kuziepuka wale watakaoonekana "hawana mawaa" mbele ya Bwana siku atakapokuja.

Matukio makubwa yaliyotukia katika maendeleo ya matengenezo katika siku za nyuma ni mambo yaliyotokea kihistoria, yanajulikana vizuri na yanatambuliwa ulimwenguni kote na Waprotestanti; ni ukweli ambao hakuna anayeweza kuupinga. Historia hii nimeielezea kwa ufupi, kulingana na upeo wa kitabu hiki na ufupisho ambao ni lazima uzingatiwe. Ukweli umefupishwa katika nafasi ndogo kama ilivyoonekana inafaa katika kuyaelewa matumizi yake. Wakati mwingine, mahali ambapo mwanahistoria fulani ameyakusanya matukio ili kuwezesha kuwe na mwonekano mpana wa suala zima kwa muhtasari, au kama ameweka muhtasari wa vipengele katika njia inayofaa, maneno yake yamenukuliwa; lakini katika sehemu zingine hakuna nukuu yo yote iliyotajwa, kwa kuwa madondoo yenyewe hayakutolewa kwa ajili ya kumtambua mwandishi

husika kama bingwa, lakini kwa sababu usemi wake unatoa maelezo yaliyo tayari na yenye nguvu katika kuelezea suala husika. Katika kusimulia mambo na maoni ya wale wanaoendeleza kazi ya matengenezo katika siku zetu, kazi zilizokwisha kuchapwa zimetumika kwa njia hiyo hiyo.

[19] Si kusudi la kitabu hiki kuelezea ukweli mpya juu ya misukosuko ya siku za nyuma, bali ni kuelezea mambo na kanuni ambazo zinahusiana na matukio yajayo. Lakini yakitazamwa kama sehemu ya pambano kati ya nguvu za nuru na zile za giza, maandishi yote haya yanayohusu siku za nyuma yanaonekana kuwa na maana mpya; na kwa njia ya maandhishi hayo nuru inayaangazia mambo yajayo, ikiiangazia njia ya wale ambao watatakiwa kushuhudia "kwa ajili ya Neno la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo, " hata kwa hatari ya kukosa mema yote ya nchi, kama ilivyokuwa kwa wanamatengenezo

Lengo la kitabu hiki ni kuelezea matukio ya pambano kuu kati ya ukweli na uongo; kufichua hila za Shetani na mbinu za kuzipinga kwa ufanisi; kuwasilisha ufumbuzi wa kuridhisha wa tatizo kubwa la uovu, kuangazia chanzo cha dhambi na kuondolewa kwa dhambi ili kufanya haki na fadhila za Mungu katika kushughulikia viumbe vyake zidhihirike, na kuonesha hali isiyobadilika ya sheria yake takatifu.

***E.G.W.***

# Sura Ya 1 - Utabiri Wa Hatima Ya Dunia

[20]

Yesu aliutazama mji wa Yerusalemu kutoka katika kilele cha mlima wa mizeituni. Majengo mazuri ya hekalu yalikuwa yanaonekana vizuri. Jua lililokuwa linatua liliuangazia weupe wa kuta zake za marumaru zake uliokuwa kama theluji na kuufanya ule mnara wa dhahabu ung'ae. Hakuna mwana wa Israeli ambaye angeweza kuitazama mandhari hii bila kusisimka kwa furaha na mshangao! Lakini moyo wa Yesu ulikuwa unawaza mambo mengine. "Alipofika karibu aliuona mji, akaulilia." Lk. 19:41.

Yesu alikuwa halii kwa ajli yake, ingawa mbele yake kulikuwa na Gethsemane, mahali pa uchungu mkali ambapo hapakuwa mbali sana, na Kalvari, mahali ambapo angesulubiwa. Lakini matukio hayo siyo yaliyokuwa yanaleta huzuni kwake katika saa hii ya furaha. Alikuwa anawalilia maelfu ya watu wa Yerusalemu ambao wangeangamia.

Historia ya zaidi ya miaka elfu moja ya fadhila maalum za Mungu kwa wateule wake ilionekana machoni mwa Yesu. Yerusalemu ilikuwa imeheshimiwa na Mungu kuliko ulimwengu wote. Bwana alikuwa "ameichagua Sayuni ... akae ndani yake." Zab. 132:13. Manabii watakatifu walikuwa wametoa ujumbe wa onyo kwa muda mrefu. Damu ya wana kondoo ilikuwa ikitolewa kila siku, ikimwakilisha Mwana kondoo wa Mungu.

Kama Israeli, kama taifa, wangedumisha utii wao kwa Mbingu, Yerusalemu ingesimama milele kama mji mteule wa Mungu. Lakini historia ya wale watu waliofadhiliwa ilikuwa ni hadithi ya kurudi nyuma na uasi. Kwa upendo wenye huruma ulio mkubwa kuliko wa baba, Mungu "aliwahurumia watu wake, na makao yake." 2 Nya. 36:15. Kusihi na kukemea kuliposhindwa, alituma zawadi bora kuliko zote kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Mungu mwenyewe, ili ausihi mji huu usiokuwa na toba.

Bwana wa nuru na utukufu alikuwa ameingia na kutoka kati ya watu wake kwa miaka mitatu, "akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi, " akiwaweka huru wale waliokuwa wame-

[21] fungwa, akiwapa kuona waliokuwa vipofu, akiwainua walemavu na kuwawezesha kutembea na kuwapa viziwi kusikia, akitakasa wenye ukoma, akifufua waliokufa, na akihubiri Injili kwa maskini. Soma Mdo. 10:38; Lk. 4:18; Mt. 11:5.

Kama msafiri asiye na makazi, aliishi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya watu na kupunguza tabu zao, akiwasihi waipokee karama ya uzima. Mawimbi ya rehema, yaliyosukumiwa mbali na watu hao waliokuwa na mioyo migumu, yalirudi tena kama wimbi kubwa zaidi la upendo usioelezeka uliojaa huruma. Lakini Israeli ilikuwa imemwacha Rafiki yake mkubwa na Msaada wake wa pekee. Kusihi kwa upendo wake kulipuuzwa.

Saa ya tumaini na msamaha ilikuwa inapita upesi. Wingu ambalo lilikuwa likikusanyika kwa kame nyingi za uasi lilikuwa limekaribia kuinyeshea jamii hii yenye hatia. Yeye ambaye peke yake angeokoa watu kutoka katika hatima iliyokuwa imekaribia sana alikuwa amepuuzwa, ametukanwa, amekataliwa, na alikuwa anakaribia kusulubiwa.

Kristo alipoutazama Yerusalemu, maangamizi ya mji mzima, taifa zima, yalionekana mbele yake. Alimwona malaika anayeangamiza akiwa na upanga ulioinuliwa kuelekea kwenye mji huo ambao kwa muda mrefu ulikuwa makazi ya Mungu. Kutoka mahali ambapo baadaye Tito na jeshi lake walisimama, alitazama hadi ng'ambo ya bonde kwenye nyua takatifu na varanda zenye matao. Kwa macho yaliyojaa machozi aliziona kuta zikiwa zimezingirwa na majeshi ya kigeni. Alivisikia vishindo vya wanajeshi wakijipanga kwa ajili ya vita, na sauti za akina mama na watoto wakililia mkate katika mji uliokuwa umezingirwa. Aliiona nyumba takatifu ya mji huo, ikulu zake na vinara vyake, vyote vikiteketeaa kwa moto, naam, rundo la vifusi vinavyofuka moshi.

Alipoitazama miaka ya baadaye, aliona watu wa agano wakiwa wametawanyika katika kila nchi, "kama vipande vya chombo kilichosambazwa na dhoruba katika jangwa." Huruma ya Mungu, upendo wa kina, vilisikika katika maneno ya huzuni: "Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!" Mt. 23:37.

[22] Alipoitazama Yerusalemu, Kristo aliona kielelezo cha

ulimwengu uliokubuhu kwa kutokuamini na uasi, ukielelekea upesi kwenye hukumu za haki za Mungu. Moyo wake uliguswa na huruma kwa ajili ya watu wanaopata taabu na kuteseka duniani. Alitamani kuwapumzisha wote. Alikuwa radhi kuitoa nafsi yake hadi kufa ili auelete wokovu mahali wanapoweza kuufikia.

Mfalme wa mbinguni akilia! Tukio hilo linaonesha ugumu wa kazi ya kuwaokoa waovu kutoka katika athari za kuvunja sheria ya Mungu. Yesu aliona kwamba ulimwengu ulikuwa katika udanganyifu kama ule uliosababisha maangamizi ya Yerusalemu. Dhambi kubwa ya Wayahudi ilikuwa kumkataa Kristo; dhambi kuu ya ulimwengu itakuwa kuikataa sheria ya Mungu, ambayo ni msingi wa serikali yake ya mbinguni na duniani. Mamilioni ya watu walio katika utumwa wa dhambi, wanaokabiliwa na mauti ya pili, watakataa kusikiliza maneno ya kweli katika siku ya kujiliwa kwao.

## Hekalu Zuri Lakabiliwa na Uharibifu

Siku mbili kabla ya Pasaka, alikwenda tena pamoja na wanafunzi wake katika Mlima wa Mizeituni uliokuwa mkabala na mji. Kwa mara nyingine alilitazama hekalu katika utukufu wake wa ajabu. Lilikuwa kilele cha uzuri. Sulemani, aliyekuwa na hekima kuliko wafalme wote wa Israeli, alikuwa amejenga hekalu la kwanza, jengo lililokuwa la fahari kuliko yote ambayo ulimwengu ulikuwa umepata kuyaona. Baada ya Nebukadneza kuliangamiza, lilijengwa upya takriban miaka mia tano kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

Lakini hekalu la pili halikulifikia la kwanza kwa uzuri. Halikuwa na wingu la utukufu, wala moto ulikuwa haushuki toka mbinguni kuja kwenye madhabahu yake. Sanduku la Agano, kiti cha rehema, na mbao za ushuhuda hazikuwepo. Hakukuwa na sauti toka mbinguni iliyokuwa inamjulisha kuhani mapenzi ya Mungu. Hekalu la pili halikupewa heshima ya kuwa na wingu la utukufu wa Mungu, bali lilipewa heshima ya uwepo wake yeye aliye Mungu mwenyewe aliyedhihirishwa katika mwili. "Shauku ya Mataifa yote" alikuwa amekuja kwenye hekalu lake wakati yule Mtu wa Nazareti [23]
alipokuwa akifundisha na kuponya katika zile nyua takatifu. Lakini Israeli waliikataa karama ya mbinguni iliyokuwa imetolcwa. Kwa kutoka yule Mwalimu mnyenyekevu katika lango la dhahabu la hekalu, utukufu uliondoka moja kwa moja katika lile hekalu. Ma-

neno ya Mwokozi yalikuwa yametimia: "nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa." Mt. 23:38.

Wanafunzi walikuwa wamejawa na mshangao kutokana na utabiri Wakristo kuhusu kubomolewa kwa hekalu, na walitamani kuelewa maana ya maneno yake. Herode mkuu alikuwa ametumia kwa wingi hazina za Kirumi na Kiyahudi kwa ajili ya hekalu hilo. Sehemu ya hekalu hilo ilikuwa imetengenezwa kwa matofali makubwa ya marumaru nyeupe toka Rumi. Hii ndiyo ilipelekea wanafunzi kumwambia Mwalimu wao: "tazama, yalivyo mawe na majengo haya!" Mk. 13:1.

Yesu akatoa jibu zito na la kushtusha: "Amin, nawaambieni, halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa." Mt. 24:2. Bwana alikuwa amcwaambia wanafunzi kwamba atakuja mara ya pili. Kwa sababu hiyo, alipotaja hukumu juu ya Yerusalemu, mawazo yao yalirudi katika suala la kuja kwake, na hivyo wakauliza: "Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?" Mt.24:3.

Kristo alitoa muhtasari wa matukio muhimu yatakayotokca kabla ya mwisho wa wakati. Unabii alioutoa ulikuwa na maana mbili. Wakati ulikuwa unaonesha maangamizi ya Yerusalemu yatakavyotokea, pia ulikuwa unaonesha matatizo ya siku ile kuu ya mwisho.

Hukumu zingewajia Israeli kwa sababu ya kumkataa na kumsulubisha Masihi. "Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu), ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani." Mt. 24:15, 16. Soma pia Lk. 21:20, 21. Bendera za Kirumi zinazoambatana na ibada ya sanamu zingesimamishwa katika nchi takatifu nje ya kuta za mji, ingewapasa wafuasi Wakristo kutafuta usalama kwa kukimbia. Wale waliokuwa wanataka kupona ingewapasa kufanya haraka. Kwa sababu ya dhambi za Yerusalemu, ghadhabu ilikuwa imetamkwa dhidi yake. Kutokuamini kwake kulikokuwa sugu kulifanya maangamizi yawe jambo la uhakika.
[24] Soma Mik. 3:9-12. Wakazi wa Yerusalemu walimtuhumu Kristo kwamba alikuwa chanzo cha matatizo yote yaliyokuwa yanawapata kwa sababu ya dhambi zao. Japo walikuwa wanajua kuwa hakuwa na dhambi, waliona kuwa kifo chake kilikuwa cha lazima kwa ajili ya usalama wao kama taifa. Walikubaliana na uamuzi wa kuhani

wao mkuu kuwa ingekuwa bora mtu mmoja kufa kuliko taifa zima kuangamia. Soma Yn. 11:47-53.

Wakati walikuwa wamemwua Mwokozi wao kwa sababu alikuwa amekemea dhambi zao, walikuwa wanajiona kuwa ni watu wa Mungu na kutarajia Bwana awakomboe kutoka kwa adui zao!

### Uvumilivu wa Mungu

Bwana alichelewesha hukumu zake kwa takriban miaka arobaini. Bado kulikuwa na Wayahudi wengi ambao walikuwa hawajui tabia na kazi ya Kristo. Watoto walikuwa hawajaiona nuru ambayo wazazi wao walikuwa wameikataa. Kwa njia ya mahubiri ya mitume, Mungu alifanya nuru hiyo iwaangazie. Waone jinsi unabii ulivyokuwa umetimia, siyo tu katika kuzaliwa kwa Kristo na maisha yake, bali pia katika kufa na kufufuka kwake. Watoto hawakuhukumiwa kwa sababu ya dhambi za wazazi wao; lakini walipoikataa nuru ya ziada waliyokuwa wamepewa, walikuwa washirika wa dhambi za wazazi wao na kukijaza kipimo cha uovu wao.

Wayahudi waliikataa fursa ya mwisho ya rehema kwa tabia yao sugu ya kutokuwa na toba. Mungu akawaondolea ulinzi wake. Taifa likaachwa chini ya utawala wa kiongozi waliyekuwa wamemchagua. Shetani akaamsha tamaa mbaya katika mioyo. Watu wakafanya mambo bila kutafakari—wakitawaliwa na tamaa, hasira kali, wakawa wakatili kama Shetani. Marafiki na ndugu wakawa wanasalitiana. Wazazi wakawa wanaua watoto wao, na watoto wakawa wanaua wazazi wao. Watawala wakawa hawana uwezo wa kujitawala wenyewe. Hamaki ziliwafanya kuwa watawala dhalimu. Wayahudi walikuwa wamekubali ushuhuda wa uongo kumhukumu Mwana wa Mungu asiye na hatia. Sasa mashtaka yasiyo ya kweli yakafanya maisha yao kuwa ya mashaka. Hofu ya Mungu ilikuwa haiwasumbui tena. Shetani alikuwa analiongoza taifa lao.

Viongozi wa vikundi vilivyokuwa vinapingana walishambulia majeshi ya wapinzani wao na kuua bila huruma. Hata utakatifu wa hekalu haukuzuia ukatili wa kutisha. Hekalu lilinajisiwa kwa [25]
miili ya waliouawa. Licha ya hayo, wachochezi wa mambo haya ya kutisha walikuwa wanadai kuwa walikuwa hawana wasiwasi wa kuangamizwa kwa Yerusalemu, kwani ulikuwa mji wa Mungu. Hata wakati majeshi ya Kirumi yanalizingira hekalu, wengi walikuwa

wanaamini kuwa Aliye juu angeingilia na kuwashinda maadui zao. Lakini Israeli ilikuwa imeukataa ulinzi wa Mungu, na sasa ilikuwa haina ulinzi.

## Ilani za Janga

Utabiri wote uliokuwa umetolewa na Kristo kuhusu maangamizi ya Yerusalemu ulitimia kikamilifu kabisa. Ishara na maajabu yalitokea. Kwa miaka saba, mtu mmoja alikuwa akizunguka katika mitaa ya Yerusalemu, akitangaza taabu iliyokuwa inakuja. Mtu huyu wa ajabu alifungwa na kupigwa, lakini, dhidi ya matusi na ukatili aliokuwa akitendewa alikuwa anajibu, "Ole, ole wake Yerusalemu!" Aliuawa wakati mji umezingirwa kama alivyokuwa ametabiri." [1]

Yerusalemu ilipoangamizwa hakuna Mkristo hata mmoja aliyeangamia. Baada ya Warumi, wakiwa chini ya Cestius kuzingira mji, Warumi waliondoka bila kutarajiwa wakati dalili zote zilikuwa zinaonesha kuwa ulikuwa wakati mwafaka wa kushambulia. Jenerali huyu wa Kirumi alirudisha majeshi yake nyuma bila sababu yo yote. Ishara iliyokuwa imeahidiwa ilikuwa imetolewa kwa Wakristo waliokuwa wakisubiri. Lk. 21:20,21.

Matukio yalidhibitiwa ili Wayahudi au Warumi wasiwazuie Wakristo kukimbia. Cestius aliporudi nyuma, Wayahudi walimfuata, na wakati majeshi hayo yanapambana, Wakristo nchini kote waliweza kukimbia bila kusumbuliwa hadi mahali pa usalama, katika mji wa Pela.

Majeshi ya Wayahudi, yaliyokuwa yakimwandama Cestius na majeshi yake, yalishambulia kutokea nyuma. Warumi walifanikiwa kurudi nyuma kwa shida sana. Wayahudi walirudi Yerusalemu kwa ushindi wakiwa na nyara zao. Hata hivyo hali hii iliiyoonekana kuwa ya mafanikio ilileta madhara zaidi. Ilichochea roho ya upinzani wa kikaidi dhidi ya Warumi, jambo lililoleta shida kwa mji huu uliokuwa hauwezi kuepuka maangamizi.

[26] Maafa yaliyoukuta mji wa Yerusalemu ulipozingirwa na Tito, yalikuwa ya kutisha. Mji huo ulizingirwa wakati wa Pasaka, ambapo mamilioni ya Wayahudi walikuwa wamekusanyika ndani ya kuta zake. Akiba za chakula zilikuwa zimeharibiwa kutokana na visasi kati ya vikundi vilivyokuwa vinapingana. Sasa athari zote

[1] Milman, History of the Jews, Book 13.

za njaa zilikuwa zinawapata. Watu walitafuna ngozi za mikanda na ndala zao na mifuko ya ngao zao. Wengi walikuwa wanatoka usiku kutafuta mimea ya porini iliyokuwa imeota nje ya mji, ingawa wengi waliuawa kwa mateso ya kikatili. Mara kwa mara wale waliokuwa wanarudi salama walikuwa wananyang'anywa kile walichokuwa wamepata. Wanaume walikuwa wanawapora wake zao, na wanawake walikuwa wanawapora waume zao. Watoto walikwapua chakula midomoni mwa wazazi wao waliokuwa wazee.

Viongozi wa Kirumi walikuwa wanataka kuwatia hofu Wayahudi ili wasalimu amri. Wafungwa walichapwa mijeledi, wakateswa na kusulubishwa mbele ya ukuta wa mji. Katika bonde la Yehoshafati na Kalvari, misalaba ilisimikwa kwa wingi. Ilikuwa vigumu kupata nafasi ya kupita kati yake. Kwa hiyo, ile laana iliyotamkwa mbele ya kiti cha hukumu cha Pilato ilitimia: "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu." Mt. 27:25.

Tito alishtuka alipoona marundo ya miili ikizagaa mabondeni. Akiwa kama ametekewa, alilitazama lile hekalu zuri na kutoa amri kuwa lisiguswe hata jiwe moja la hekalu hilo. Aliwasihi viongozi wa Kiyahudi wasimlazimishe kupanajisi kwa damu mahali hapo patakatifu . Kama wangekwenda kupigania mahali pengine po pote, kusingekuwa na Mrumi wa kunajisi utakatifu wa lile hekalu! Josephus mwenyewe aliwasihi wasalimu amri ili wajiokoe wao, mji wao, na mahali pao pa ibada. Lakini, walimrushia mishale, na kumtukana mpatanishi wao wa mwisho wa kibinadamu. Juhudi za Tito kuliokoa hekalu hazikusaidia Aliyekuwa mkuu kuliko yeye alikuwa amekwisha kutamka kwamba lisingesalia hata jiwe moja juu ya lingine.

Hatimaye, Tito aliamua kuliteka hekalu kwa nguvu, akiwa [27]
amekusudia kuliepusha na uharibifu ikiwezekana. Hata hivyo, maagizo yake yalipuuzwa. Kijinga cha moto kilirushwa na askari mmoja kwenye mwanya uliokuwa kibarazani, na mara vile vyumba vya nyumba takatifu, ambavyo kuta zake zilikuwa zimefunikwa kwa mbao za mkangazi vilishika moto.. Tito aliwahi pale na kuamuru askari wauzime. Maneno yake yalipuuzwa. Kwa hasira askari walitupa vijinga vya moto kwenye vyumba vilivyokuwa ndani ya hekalu na kisha wakawachinja wale waliokuwa wamejificha mle. Damu ikamiminika kwenye ngazi za hekalu kama maji.

Baada ya kuangamizwa kwa hekalu, mji mzima ulitekwa na Warumi. Viongozi wa Kiyahudi wakaiacha minara yao iliyokuwa haipenyeki. Tito akatangaza kuwa Mungu alikuwa amewatia Wayahudi mikononi mwake; kwani hakuna injini ambazo zingeweza zingeweza kuzishinda ngome za Wayahudi zilizokuwa imara. Mji pamoja na hekalu viliteketezwa hadi kwenye misingi yake, na ardhi vilipokuwa vimejengwa ililimwa "kama shamba lilimwavyo." Soma Yer. 26:18. Zaidi ya watu milioni waliangamia; waliosalia wakachukuliwa mateka, wakauzwa kama watumwa, wakapelekwa Rumi, wakatupwa waliwe na wanyama wakali katika viwanja michezo, au kutawanyika duniani kote kama wahamiaji wasio na kwao.

Wayahudi wenyewe, walikuwa wamekijaza kikombe cha kisasi. Katika matatizo yote yaliyofuata baada ya kutawanyika kwao, walikuwa wanavuna mavuno ambayo mikono yao wenyewe ilikuwa imeyapanda. "haya ndiyo maangamizo yako, Ee Israeli " Hos. 13:9; "maana umeanguka kwa sababu ya uovu wako." Hos. 14:1. Mara nyingi matatizo yao yanaelezwa kama adhabu kutokana na tamko la moja kwa moja la Mungu. Yule mdanganyifu mkuu huficha yake kwa mji hiyo. Kwa kuwa waliukataa upendo na rehema kutoka mbinguni kwa ukaidi, Wayahudi waisababisha uizo wa Mungu uondolewe kwao.

Hatuwezi kuelewa ni kwa kiasi gani amani na ulinzi tunaofaidi ulitokana na Kristo. Uwezo wa Mungu unaodhibiti, humzuia mwanadamu kuangukia moja kwa moja katika mikono ya Shetani. Waasi na wasio na shukurani wana sababu kubwa ya kuwa na shukurani kwa ajili ya rehema ya Mungu. Lakini wanadamu wanapovuka mipaka ya uvumilivu wa Mungu, udhibiti huo huondolewa. Mungu huwa hasimami kama mtekelezaji wa hukumu dhidi ya makosa. Huwa anawaacha walioikataa rehema yake wavune walichokipanda.
[28] Kila nuru iliyokataliwa ni mbegu iliyopandwa izaayo matunda ya uhakika. Roho wa Mungu akipingwa kwa muda mrefu, hatimaye huondolewa. Hapo huwa hakuna nguvu ya kudhibitii tamaa mbaya za moyo, huwa hakuna ulinzi dhidi ya hiyana na chuki ya Shetani.

Maangamizi ya Yerusalemu ni onyo kali kwa wote ambao wanapinga ushawishi wa rehema ya Mungu. Unabii wa Mwokozi juu ya adhabu kwa Yerusalemu utatimia tena. Katika hatima ya ule mji mteule, tunaona maangamizi ya ulimwengu ambao umeikataa

rehema ya Mungu na kuikanyaga sheria yake. Historia ya dhiki ya wanadamu ambayo ulimwengu umeishuhudia ni ya kutisha. Matokeo ya kuikataa mamlaka ya mbinguni ni ya kutisha. Lakini tukio baya zaidi linaoneshwa katika ufunuo wa mambo yajayo. Roho wa Mungu anayedhibiti atakapoondolewa, asidhibiti tena mlipuko wa hisia za wanadamu na ghadhabu ya kishetani, ulimwengu utaona matokeo ya utawala wa Shetani kuliko ulivyowahi kuona. Siku hiyo, kama ilivyokuwa katika kuharibiwa kwa Yerusalemu, watu wa Mungu wataokolewa. Soma Isaya 4:3; Mathayo 24:30, 31. Kristo atakuja mara ya pili kuwakusanya kwake walio waaminifu wake. "Ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu." Mt. 24:30,31.

Watu wajihadhari wasije wakayapuuza maneno ya Kristo. Kama alivyowaonya wanafunzi wake juu ya kuharibiwa kwa Yerusalemu, ili waweze kukimbia, ndivyo alivyouonya ulimwengu juu ya siku ya maangamizi ya mwisho. Wote wanaotaka wanaweza kuikimbia ghadhabu inayokuja. "Tena, kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota; na katika nchi dhiki ya mataifa wakishangaa kwa uvumi wa bahari na msukosuko wake." Luka 21:25. Soma pia Mathayo 24:29; Marko 13:24-26; Ufunuo 6:12-17. "Kesheni basi, " ndiyo agizo la Kristo. Marko 13:35. Wale watakaotii onyo hilo hawakuwa gizani.

Dunia haiko tayari kuupokea ujumbe wa wakati huu kama vile [29] Wayahudi walivyokuwa hawako tayari kupokea onyo la Mwokozi juu ya Yerusalemu. Vyo vyote itakavyokuwa, siku ya Mungu itakuja bila kutegemea kwa wasiomcha Mungu. Dunia inapoendelea na mzunguko wake usiobadilika; wakati watu wamezama katika anasa, katika biashara, katika kutafuata pesa; wakati viongozi wa dini wanakuza maendeleo ya dunia na watu wanadanganyika na usalama wa bandia—ndipo, kama mwizi wa usiku wa manane aibavyo katika makazi yasiyo na ulinzi, uharibifu wa ghafla utawajia wasiojali na wasiomcha Mungu, "wala hakika hawataokolewa." Soma lThe. 5:2-5.

[30] ## Sura Ya 2 - Wakristo Wa Awali-Watii Na Wakweli

Yesu aliwaeleza wanafunzi wake mambo ambayo watu wake wangeyapitia tangu alipotwaliwa kutoka kwao, hadi atakaporudi katika nguvu na utukufu. Alipokuwa akitazama ndani kabisa katika wakati ujao, jicho lake liliona dhoruba kali ambazo zingewakumba wafuasi wake katika nyakati za mateso zilizokuwa zinakuja. Soma Mt. 24:9, 21, 22. Iliwapasa wafuasi Wakristo kupita katika njia ile ile ya kukataliwa na mateso ambayo Bwana wao aliipitia. Uadui dhidi ya Mkombozi ungedhihirishwa kwa wote ambao wangeliamini jina lake.

Upagani uliona kwamba kama Injili ingeshinda, mahekalu na madhababu zake zingefutiliwa mbali; kwa hiyo, moto wa mateso ukawashwa. Wakristo wakanyang'anywa mali zao na kutolewa katika nyumba zao. Watu wengi, waungwana na watumwa, matajiri na maskini, wenye elimu na wasio na elimu, wakauawa bila huruma.

Tangu wakati wa Nero, mateso yaliendelea kwa kame kadhaa. Wakristo walisingiziwa kuwa vyanzo vya njaa, maafa na matetemeko. Watoa habari walikaa tayari kulipwa kwa kuwasaliti hawa ambao hawakuwa na hatia kwa kusema kuwa ni waasi na wasumbufu katika jamii. Wengi walitupwa mbele ya wanyama mwitu na kuchomwa wakiwa hai katika matanuru. Baadhi walisulubishwa; wengine wakafunikwa na ngozi za wanyama wa porini na kutupwa katika viwanja vya maonesho ili wararuliwe na mbwa. Katika matukio ya sherehe, umati mkubwa wa watu ulikutana kufurahia maonesho hayo na walicheka na kushangilia vilio vya waliokuwa wakifa.

Wafuasi Wakristo walilazimika kutafuta maficho katika sehemu zilizojitenga. Chini ya vilima nje ya mji wa Roma, mapango marefu yalichimbwa katika ardhi na miamba kwa kilometa nyingi nje ya kuta za mji. Ndani ya makimbilio haya ya chini ya ardhi, wafuasi Wakristo walizika wafu wao; huko ndiko walikopata makazi wakati wametengwa. Wengi waliyakumbuka maneno Bwana wao aliyowaambia, kwamba wakati watakapoteswa kwa ajili ya Kristo,

wafurahi kabisa. Tuzo yao ni kubwa mbinguni, kwani ndivyo manabii walivyoteswa kabla yao. Soma Mt. 5:11, 12.

Nyimbo za ushindi zilisikika kutoka katikati ya moto. Kwa imani walimwona Kristo na malaika wakiwaangalia kwa shauku kubwa na kuheshimu uthabiti wao na kuukubali. Sauti ilikuja toka katika kiti cha enzi cha Mungu: "Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima." Ufu. 2:10. [31]

Juhudi za Shetani kuangamiza kanisa la Kristo kwa vurugu hazikusaidia. Watendakazi wa Mungu waliuawa, lakini Injili ilizidi kuenea na wafuasi wake waliongezeka. Mkristo mmoja alisema: "Kadiri mnavyotufyeka, ndivyo tunavyoongezeka; damu ya Wakristo ni mbegu." [2]

Kwa hiyo, Shetani aliweka mipango yake kupambana na Mungu kwa ufanisi zaidi kwa kupandisha bendera yake katika kanisa la Kikristo ili akipate kwa hila kile alichoshindwa kukipata kwa nguvu. Mateso yakakoma. Badala yake kukawa na vishawishi vya mafanikio na heshima ya kidunia. Waabudu sanamu walipewa kupokea sehemu ya imani ya Kikristo, wakati wakiukataa ukweli muhimu. Walidai kuwa wamempokea Kristo lakini walikuwa hawajashawishika kuwa ni wenye dhambi na hawakuwa wanaona haja ya toba wala badiliko la moyo.

Sasa kanisa lilikuwa katika hatari ya kutisha. Jela, mateso, moto na upanga vilikuwa baraka ukilinganisha na jambo hili! Baadhi ya Wakristo walisimama imara. Baadhi walikubali kubadili imani yao. Akiwa na vazi la ukristo wa bandia, Shetani alijipenyeza kanisani na kupotosha imani yao.

Hatimaye, Wakristo wengi walikubali kushusha kiwango. Ukaundwa umoja kati ya Ukristo na upagani. Ingawa waabudu sanamu walidai kuwa wamejiunga na kanisa, bado waliendelea kung'ang'ania ibada zao za sanamu, wakibadilisha tu vitu walivyokuwa wakiviabudu kuwa sanamu za Yesu, Mariamu na hata watakatifu wengine. Mafundisho yasiyokubalika, kanuni za kishirikina, na sherehe za ibada ya sanamu zikaingizwa katika imani na ibada za kanisa. Kanisa la Kikristo likapotoshwa, na kupoteza usafi na nguvu yake. Hata hivyo, baadhi hawakupotoka. Waliendelea kuwa waminifu kwa yule aliye chanzo cha ukweli.

[2]Tertullian, Apology, parag

[32]
## Makundi Mawili Kanisani

Sikuzote huwa kuna makundi mawili miongoni mwa wale wanaodai kumfuata Kristo. Wakati kundi moja linajifunza maisha ya Mwokozi na kutaka kwa dhati kusahihisha dosari zao na kufanana na Yeye aliye kielelezo, kundi lingine linaepuka ukweli uliodhahiri, unaofaa kutumika maishani, ambao unafunua makosa yao. Hata kipindi kanisa lilipokuwa katika hali nzuri kuliko vipindi vingine vyote, sio wote waliokuwa wakweli na waaminifu kanisani. Yuda aliwekwa pamoja na wanafunzi, ili aweze kuona makosa yake kwa njia ya maelekezo na mfano Wakristo. Lakini kwa kuendekeza dhambi alikaribisha majaribu ya Shetani. Alikuwa anakasirika wakati makosa yake yanakemewa na jambo hilo ililimfanya amsaliti Bwana wake. Soma Marko 14:10, 11.

Anania na Safira walijifanya kutoa sadaka yote kwa Mungu huku wakibakiza kiasi fulani kwa ajili yao wenyewe. Roho wa ukweli akawafunulia mitume tabia halisi ya wanafiki hao, na hukumu ya Mungu iliondoa doa baya lililokuwa katika usafi wa kanisa. Soma Matendo 5:1- 11. Mateso yalipokuja kwa wafuasi Wakristo, wale waliokuwa tayari kuyaacha yote kwa ajili ya ukweli, ndio waliotamani kuwa wanafunzi wake. Lakini mateso yalipokoma, waongofu waliongezeka ambao hawakuwa waaminifu sana, na njia ya Shetani kujiimarisha, ikafunguka.

Wakristo walipokubali kuungana na wale waliokuwa wameongoka nusu nusu kutoka kwenye upagani, Shetani alishangilia. Kisha akawaamsha wawatese wale waliokuwa wanaendelea kuwa wakweli kwa Mungu. Wakristo hawa waasi, wakiungana na wale waliokuwa nusu wapagani, walielekeza mashambulizi yao kwenye sehemu nyeti za fundisho la Kristo. Ilihitaji juhudi kubwa kusimama imara dhidi ya udanganyifu na machukizo yaliyokuwa yameingizwa kanisani. Biblia ilikuwa haikubaliki kama kipimo cha imani. Fundisho la uhuru wa kidini liliitwa uasi, na wale waliokuwa wanalifuata walipigwa marufuku.

Baada ya mgogoro wa muda mrefu, waaminifu waliona kujitenga lilikuwa jambo la lazima. Hawakuthubutu kuvumilia makosa yaliyokuwa yanaweza kuangamiza roho zao na kuhatarisha imani
[33] za watoto wao na watoto wa watoto wao. Waliona kuwa amani ingekuwa imenunuliwa kwa gharama kubwa sana kama ingelaz-

imu kuziacha kanuni ili kuipata. Kama umoja ungepatikana kwa kuhafifisha ukweli tu, basi ni heri kuwe na tofauti, na hata vita.

Kwa kweli, Wakristo wa awali walikuwa watu wa pekee. Walikuwa wachache, hawakuwa na mali, vyeo au nafasi za heshima, walikuwa wanachukiwa na waovu, kama Habili alivyokuwa anachukiwa na Kaini. Soma Mwanzo 4:1-10. Tangu siku za Kristo hadi sasa wanafunzi wake waaminifu wamekuwa wakiamsha chuki na upinzani kutoka kwa wale wanaopenda dhambi.

Inawezekanaje basi, Injili iitwe ujumbe wa amani? Malaika waliimba juu ya nyanda za Bethlehemu: "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." Lk. 2:14. Inaonekana kama kuna ukinzani kati ya matamshi haya ya kiunabii na maneno ya Kristo: "Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! Sikuja kuleta amani, bali upanga." Mt. 10:34. Lakini kama yakieleweka vema, matamko haya mawili yanakubaliana kabisa. Injili ni ujumbe wa amani. Kama dini ya Kristo, ingepokelewa na kutiiwa, ingeleta amani na furaha duniani kote. Kazi ya Yesu ilikuwa ni kupatanisha watu na Mungu na pia watu wao kwa wao. Lakini dunia yote imekuwa chini ya utawala wa Shetani, ambaye ni adui mkubwa Wakristo. Injili inawasilisha kanuni za maisha ambazo ziko tofauti kabisa na tabia na tamaa za kidunia, na hivyo dunia inazipinga. Wanaoipenda dunia huchukia usafi ambao unakemea dhambi, na hivyo huwatesa wale wanaowasisitizia madai matakatifu ya usafi huo. Ni katika mazingira haya, Injili huitwa upanga. Soma Mathayo 10:34.

Wengi walio dhaifu katika imani wako tayari kutoendelea kumwamini Mungu kwa sababu huwaruhusu watu wabaya wafanikiwe, wakati walio wema zaidi na walio safi huteswa na mamlaka zao dhalimu. Inawezekanaje Yeye aliye mwenye haki na mwenye rehema na mwenye uwezo usio na mwisho avumilie udhalimu kiasi hicho? Mungu ametupatia uthibitisho wa kutosha wa upendo wake. Haitupasi kuwa na shaka na wema wake eti kwa sababu tumeshindwa kuyaelewa majaliwa yake. Mwokozi alisema, "Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi; ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu." Yn. 15:20. Wale wanao- [34]
lazimika kupata mateso na kifo kwa ajili ya imani wanapita tu katika nyayo za Mwana mpendwa wa Mungu.

Wenye haki hutiwa katika tanuru la mateso ili wasafishwe, ili mfano wao uwafanye wengine waamini juu ya uhalisi wa imani na utauwa na kwamba, mwenendo wao usioyumba, uwahukumu wasio watauwa na wasio amini. Mungu anawaruhusu waovu wasitawi na kuonesha uadui wao dhidi yake ili wote wapate kuona haki na rehema yake watakapoangamizwa. Adhabu itatolewa kwa ajili ya kila tendo la ukatili linalofanywa dhidi ya waaminifu wa Mungu kana kwamba alifanyiWakristo mwenyewe.

Paulo alisema "Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." 2 Tim. 3:12. Kwa nini basi, mateso yanaonekana kuchelewa? Sababu pekee ni kwamba kanisa limekubaliana na kiwango cha dunia, kwa hiyo, haliamshi upinzani. Dini ya wakati wetu, siyo ile dini safi na takatifu ya Kristo na mitume wake. Kwa sababu ukweli wa Neno la Mungu haujaliwi, kwa sababu utauwa wa kweli ni kidogo sana katika kanisa, likristo umechukua sura ya ulimwengu. Kukiwa na uamsho wa imani ya kanisa la mwanzo, moto wa mateso utawaka upya

# Sura Ya 3 - Giza La Kiroho Katika Kanisa La Awali [35]

Mtume Paulo alisema kuwa siku ya Kristo isingekuja "usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." Na tena, "Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi." 2 The. 2:3, 4, 7. Hata wakati huo, mtume aliona yakiingia amakosa mbayo yangeandaa njia kwa ajili ya utawala wa Papa.

"Siri ya kuasi" iliendelea kufanya kazi ya udanganyifu tararibu. Desturi za kipagani zikaingia katika kanisa la Kikristo, zikizuiwa kwa muda na mateso makali yaliyoletwa na upagani; lakini mateso yalipokoma, Ukristo uliuacha unyenyekevu Wakristo na mahali pake pakawa na majivuno ya makuhani na watawala. Kuongoka nusu nusu kwa Konstantino kulisababisha shangwe kubwa. Sasa kazi ya uharibifu iliendelea kwa kasi zaidi. Upagani, ambao ulikuwa umeonekana kushindwa, ukawa umeshinda. Mafundisho na mapokeo potuvu wa kipagani yakajumuishwa katika imani ya wale waliokuwa wanadai kuwa wafuasi Wakristo.

Mwafaka huu kati ya upagani na Ukristo ulizaa "mtu wa kuasi" aliyekuwa ametabiriwa katika unabii. Hiyo dini bandia ndiyo kazi ambayo Shetani alifanya kwa ustadi mkubwa, yaani juhudi zake za kukaa katika kiti cha enzi ili aitawale dunia sawasawa na mapenzi yake.

Moja ya mafundisho makuu katika Kanisa la Roma ni kwamba Papa amepewa mamlaka ya juu kabisa kuliko maaskofu na mapadri duniani kote. Zaidi ya hilo, Papa ameitwa "Bwana Mungu, Papa" na kutangazwa kuwa hawezi kukosea. (Angalia kiambatisho). Hoja ile ile ambayo Shetani alikuwa anaitoa wakati wa kumjaribu Yesu kule jangwani, anaendelea kuitoa kwa njia ya Kanisa la Roma, na watu wengi wanamtii.

Lakini wale wanaomcha Mungu wanaikabili hali hii ya kujitwalia mamlaka kama vile Kristo alivyokabiliana na adui huyo mwc-

nye hila: "Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake." Lk. 4:8.

[36] Mungu hajawahi kumteua mtu ye yote kuwa kichwa cha kanisa. Ukuu wa Papa ni kinyume cha Maandiko. Papa hawezi kuwa na mamlaka juu ya kanisa la Kristo bila kujitwalia mamlaka hayo yeye mwenyewe. Wafuasi wa Kanisa la Roma huwatuhumu Waprotestanti kwa kujitenga kwa makusudi kutoka katika kanisa la kweli. Lakini wao ndio walioiacha "imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Yud. 3.

Shetani alikuwa anajua vema kuwa Mwokozi aliyapinga na mashambulizi yake kwa kutumia Maandiko Matakatifu. Katika kila shambulio, Kristo alitoa ngao ya ukweli wa milele, akisema, "Imeandikwa." Ili Shetani aweze kudumisha utawala wake kwa watu na kuimarisha mamlaka ambayo Papa amejitwalia, lazima aendelee kuwafanya wasijue Maandiko. Ukweli mtakatifu wa Maandiko hayo lazima ufichwe na kuzimwa. Kwa mamia ya miaka usambazaji wa Biblia ulikuwa umepigwa marufuku na Kanisa la Roma. Watu walikuwa wamekatazwa kuisoma. Makasisi na maaskofu waliyafasiri mafundisho ya Biblia ili kulinda hila zao. Kwa namna hiyo, Papa akajulikana karibu dunia yote kama mwakilishi wa Mungu hapa duniani.

## Jinsi Sabato "Ilivyobadilishwa"

Unabii ulisema kuwa utawala wa Papa ungeazimu "kubadili majira na sheria." Dan. 7:25. Ili kupata kitu badala ya ibada ya sanamu, ibada ya vinyago na vitu vya kale iliingizwa taratibu kwenye ibada ya Kikristo. Hatimaye, tamko la baraza kuu likaidhinisha ibada hiyo ya sanamu. Kanisa la Roma lilidiriki kufuta amri ya pili inayokataza ibada ya sanamu, kutoka kwenye sheria ya Mungu, kisha likagawa amri ya kumi ili kudumisha idadi ya amri kumi.

Viongozi wa kanisa wasiotakaswa walibadilisha amri ya nne pia, ili kuiondoa Sabato ya zamani, siku ambayo Mungu alikuwa ameibariki na kuitakasa (Mwa. 2:2, 3) na badala yake wakaitukuza sikukuu iliyokuwa ikiadhimishwa na wapagani kama "siku tukufu ya jua." Katika kame za awali Sabato ya kweli ilikuwa ikishikwa na Wakristo wote, lakini Shetani alijitahidi kutimiza kusudi lake. Jumapili ikafanywa kuwa siku kuu ya kuadhimisha kufufukwa kwa

Kristo. Huduma za kidini zikawa zinafanyika katika siku hii na ikawa inachukuliwa kama siku ya burudani, huku Sabato ikiendelea kushikwa kama takatifu.

Kabla Kristo hajaja, Shetani alikuwa amewafanya Wayahudi [37]
waiwekee Sabato masharti magumu. Sasa, kwa kutumia udhaifu wa mwonekano wa bandia ambao alikuwa ameifanya Sabato iwe nao, aliidhalilisha kwa kuifanya ionekane kama jambo la "Kiyahudi." Wakati Wakristo wakiendelea kuiadhimisha Jumapili kama sikukuu ya furaha, aliwafanya waigeuze Sabato kuwa siku ya huzuni na masikitiko ili kuonesha chuki dhidi ya dini ya Kiyahudi.

Mfalme Konstantino alitoa tamko la kuifanya Jumapili kuwa sikukuu ya serikali katika dola yote wa Kirumi. (Angalia Kiambatisho.) Siku ya jua ilikuwa inatukuzwa na raia wake wa kipagani na kuheshimiwa na Wakristo. Alihimizwa kufanya hivyo na maaskofu wa kanisa. Wakiongozwa na uchu wa madaraka, waliona kuwa kama siku hii ingeshikwa na Wakristo na wapagani, ingekuza mamlaka na utukufu wa kanisa. Lakini wakati Wakristo wengi wacha Mungu walipokuwa wanaongozwa hatua kwa hatua kuichukulia Jumapili kana kwamba ina kiasi fulani cha utakatifu, waliendelea kuishika na kuiadhimisha Sabato ya kweli wakiitii amri ya nne.

Yule mdanganyifu mkuu hakuishia hapo. Aliazimu kutumia uwezo wake kupitia kwa mwakilishi wake, yaani askofu mwenye kiburi wa Kanisa la Roma ambaye alikuwa anadai kuwa ni mwakilishi Wakristo. Mabaraza makubwa yalikaa ambapo wakuu kutoka duniani kote walikutana. Karibu katika kila baraza Sabato ilishushwa chini kidogo, na Jumapili ikainuliwa. Kwa njia hiyo, hatimaye siku kuu ya kipagani ikawa inaheshimiwa kama siku ya Mungu, huku Sabato ya Biblia ikitangazwa kuwa ni jambo la Kiyahudi na ushikaji wake ukatangazwa kuwa umelaaniwa.

Yule mwasi alikuwa amefaulu kujiinua mwenyewe "juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa." 2 Thes. 2:4. Alikuwa amediriki kubadili kanuni pekee katika sheria ya Mungu inayoelezea Mungu wa kweli aliye hai. Katika amri ya nne, Mungu anaelezewa kama Mwumbaji. Kama kumbukumbu ya kazi ya uumbaji, siku ya saba ilitakaswa kama siku ya kupumzika kwa wanadamu, ikiwa imekusudiwa kumfanya Mungu aliye hai akumbukwe kila wakati kuwa ndiye anayestahili kuabudiwa. Shetani anajitahidi kufanya

watu wasitii sheria ya Mungu; kwa hiyo, jitihada zake anazielekeza hasa kwenye ile amri inayomwelezea Mungu kama Mwumbaji.

[38] Sasa hivi Waprotestanti wanadai kwamba kufufuka kwa Kristo siku ya Jumapili kuliifanya Jumapili iwe Sabato ya Kikristo. Lakini Kristo wala mitume walikuwa hawajaipa Jumapili heshima kama hiyo. Chanzo cha kushika Jumapili ni ile "siri ya kuasi" (2 Thes. 2:7) ambayo hata wakati wa Paulo, ilikuwa imeanza kazi yake. Je, sababu gani inaweza kutolewa kwa ajili ya badiliko lisiloungwa mkono na Maandiko?

Katika kame ya sita, askofu wa Kanisa la Roma alitangazwa kuwa kichwa cha kanisa lote. Upagani ulikuwa umeupisha utawala wa Papa. Joka akawa amempa mnyama "nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi." Ufu. 13:2.

Sasa ikaanza ile miaka 1260 ya ukandamizaji wa utawala wa Papa uliotabiriwa katika unabii wa Danieli na Ufunuo. Danieli 7:25; Ufunuo 13:5-7. (Angalia Kiambatisho.) Wakristo walilazimishwa kuchagua ama kuacha unyoofu wao na kukubaliana na sherehe na ibada za utawala wa Papa, au kumalizia maisha yao katika magereza yaliyokuwa chini ya ardhi, au kufa. Sasa maneno ya Yesu yalikuwa yametimia: "Nanyi mtasalitiwa na wazazi wenu, na ndugu zenu, na jamaa zenu, na rafiki zenu, nao watawafisha baadhi yenu. Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu." Lk. 21:16, 17.

Ulimwengu ukawa uwanja mpana wa mapambano. Kwa mamia ya miaka kanisa la Kristo lilitafuta usalama katika maeneo pweke na yaliyofichika. "Yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko muda wa siku elfu na mia mbili na sitini." Ufu. 12:6.

Mwanzo wa zama za giza ulikuwa ni pale Kanisa Katoliki lilipopata nafasi ya kutawala. Imani ilihamishwa kutoka kwa Kristo kwenda kwa Papa wa Roma. Badala ya kumtegemea Mwana wa Mungu kwa ajili ya msamaha wa dhambi na uzima wa milele, watu walimwangalia Papa na mapadri aliokuwa amewakasimisha mamlaka. Papa akawa mpatanishi wao duniani. Kwao, alikuwa badala ya Mungu. Kukiuka matakwa yake kulikuwa sababu ya kutosha kupata adhabu kali. Kwa namna hiyo, mawazo ya watu yakageuzwa kutoka kwa Mungu kwenda kwa watu wenye kukosea na wakatili, na zaidi, kwa mkuu wa giza mwenyewe, aliyekuwa anaonesha uwezo wake kupitia kwao. Maandiko yanapopingwa, na mwanadamu kujichuku-

lia kwamba yeye ndiye mwenye mamlaka yote, matokeo yake ni ulaghai, udanganyifu, na uovu wa kudhalilisha.

## Siku za Hatari kwa Kanisa [39]

Wabeba bendera waaminifu walikuwa wachache. Wakati fulani, ilionekana kana kwamba uovu ungetawala kabisa, na dini ya kweli ingetokomezwa duniani. Injili ilikuwa haionekani, na watu walibebeshwa masharti magumu. Walifundishwa kutegemea matendo yao wenyewe kwa ajili ya upatanisho wa dhambi. Hija ndefu, malipizi, ibada ya vitu vilivyokuwa vinaheshimiwa na vilivyokuwa vinakumbushia mambo ya kale, kuinua makanisa, mahali patakatifu, na madhabahu, malipo ya kiasi kikubwa cha pesa kwa kanisa—haya yaliamriwa ili kutuliza ghadhabu ya Mungu au kukubalika mbele zake.

Ilipokaribia mwisho wa karae ya nane, utawala wa Papa ukatangaza kuwa katika miaka ya awali ya kanisa, maaskofu wa Kanisa la Roma walikuwa na uwezo wa kiroho kama ule waliokuwa wameanza kuwa nao sasa. Maandiko ya kale yakaghushiwa na watawa. Yakagunduliwa mabaraza ambayo yalikuwa hayajawahi kusikika huo nyuma, ambayo yalikuwa yanathibitisha ukuu wa Papa tangu mwanzo kabisa. (Angalia Kiambatisho).

Wajenzi wachache waaminifu waliojenga kwenye msingi imara (lKor.3:10, 11) walikuwa wanafadhaika. Wakiwa wamechoshwa na mahangaiko yasiyokoma dhidi ya mateso, ulaghai na kila kizuizi ambacho Shetani alikuwa anabuni, baadhi ya wale waliokuwa waaminifu walivunjika mioyo. Kwa sababu ya kutaka amani na usalama wa mali zao na maisha yao, waliuacha msingi ulio imara. Wengine hawakutishwa na upinzani wa maadui.

Ibada ya sanamu ikawa jambo la kawaida. Mishumaa ikawa inawashwa mbele ya sanamu na sala zikawa zinatolewa kwa sanamu hizo. Desturi za kipuuzi zikashamiri. Akili ikaonekana kana kwamba imepoteza udhibiti wake. Huku mapadri na maaskofu wenyewe wakiwa wapenda anasa na mafisadi, watu waliokuwa wakitegemea uongozi wao walitumbukizwa katika ujinga na uovu. Katika kame ya kumi na moja, Papa Gregori VII alitangaza kuwa kanisa lilikuwa halijawahi kufanya makosa, na lisingeweza kukosea, kulingana na Maandiko. Lakini dai hilo halikuambatana na ushahidi [40]

wa Maandiko. Askofu huyu mkuu mwenye kiburi, wa Kanisa la Roma alidai pia kuwa alikuwa na uwezo wa kuwaondoa madarakani wafalme. Kielelezo cha tabia hii ya ukatili ya huyu mtetezi wa dhana ya kutokosea kilikuwa jinsi alivyomtendea mfalme Henry IV wa Ujerumani. Mfalme huyu alipodiriki kudharau mamlaka ya Papa, alitengwa na kung'olewa kwenye kiti cha enzi. Wakuu wake wa majimbo walichochewa na mamlaka ya Papa wamwasi.

Henry IV aliona ulazima wa kupatana na Kanisa la Roma. Akiwa na mkewe na mtumishi wake mwaminifu alivuka milima ya Alps katikati ya kipupwe, ili aende kunyenyekea mbele ya Papa. Alipofika kwenye jumba la Gregory, alipelekwa kwenye ua wa nje. Akiwa huko alikaa kwenye baridi kali ya kipupwe, akiwa kichwa wazi na miguu pekupeku, akisubiri ruhusa toka kwa Papa ili aingie kumwona. Papa hakumsamehe mpaka alipoendelea kufunga na kuungama kwa siku tatu. Hata msamaha huo ulikuwa kwa sharti kwamba asubiri kibali cha Papa kuirudia taji yake au kutumia mamlaka ya kifalme. Gregory, akiwa amefurahishwa na ushindi wake, alijivuna akisema kuwa kushusha viburi vya wafalme, ulikuwa ni wajibu wake.

Kuna tofauti kubwa kati ya askofu huyu mwenye kiburi na Kristo, anayejieleza kuwa amesimama katika mlango wa moyo akisihi apate kuingia. Aliwafundisha wanafunzi wake kuwa: "na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu." Mt. 20:27.

### Jinsi Mafundisho ya Uongo Yalivyoingia

Hata kabla ya kuanzishwa kwa utawala wa Papa mafundisho ya wanafalsafa wapagani yalikuwa yameshakuwa na ushawishi kanisani. Wengi bado walikuwa wanang'ang'ania itikadi za falsafa ya kipagani na kulazimisha watu wajifunze falsafa hiyo kama njia ya kueneza ushawishi wao miongoni mwa wapagani. Makosa makubwa yaliingizwa katika imani ya Kikristo kwa njia hiyo.

Katika mafundisho hayo, fundisho lililokuwa maarufu zaidi ni ile imani ya kutokufa kwa mwanadamu na hali ya kuwa na ufahamu akiwa mautini. Fundisho hili liliweka msingi ambapo Kanisa la Roma lilianzisha kuomba kwa watakatifu na kumwabudu bikira Maria. Kutoka katika jambo hilo pia likaibuka fundisho la uongo la

mateso ya milele kwa wale ambao hawatatubu, ambalo liliingizwa mapema katika imani ya Papa.

Njia iliandaliwa kwa ajili ya uzushi mwingine wa upagani - yaani [41]
toharani, ambao uliokuwa unatumika kuwatishia watu wengi wenye mapokeo potovu. Fundisho hili la uongo lilikuwa linadai kuwa kuna mahali pa mateso ambapo roho za watu ambao hawajastahili hukumu ya jehanum hupata adhabu kwa ajili ya dhambi zao, na baada ya hapo zikitakasika, huruhusiwa kuingia mbinguni. (Angalia Kiambatisho.)

Ulikuwa unahitajika uongo mwingine kuliwezesha Kanisa la Roma kunufaika kutokana na hofu na uovu wa wafuasi wake: fundisho la kulipia msamaha. Ahadi ya ondoleo la dhambi, za zamani, za sasa na zijazo ilitolewa kwa wote ambao wangejiandikisha katika vita vya Papa vya kuwaadhibu maadui zake au kuwaangamiza wale waliokuwa wanathubutu kukataa ukuu wake wa kiroho. Kwa kulipa pesa kanisani, watu waliweza kuondokana na dhambi na pia kuzifungulia roho za rafiki zao zilizokuwa zinateseka motoni. Kwa njia hiyo, Kanisa la Roma lilizijaza hazina zake na kuendeleza fahari, anasa, na uovu wa waliokuwa wanajifanya wawakilishi wake Yeye ambaye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa chake. (Angalia Kiambatisho).

Nafasi ya meza ya Bwana ilikuwa imechukuliwa na dhabihu ya ibada ya sanamu, yaani misa. Mapdre wa Kanisa la Roma walikuwa wanajifanya kuwa wanaubadili mkate wa kawaida na divai kuwa "mwili na damu halisi Wakristo." [3] Kwa ufidhuli wenye kufuru, walidai wazi wazi kuwa wana uwezo wa kumwumba Mungu, ambaye ni Mwumbaji wa vyote. Wakristo walikuwa wanalazimishwa, kukiri imani yao katika fundisho hili potovu linalotukana Mbingu, la sivyo wauawe.

Katika kame ya kumi na tatu kilianzishwa chambo cha kutisha kabisa katika mamlaka ya Papa. -Mahakama ya kanisa ya kukomesha uasi. Katika mabaraza yao ya siri Shetani na malaika zake walitawala akili za watu waovu. Malaika wa Mungu alisimama kati yao, bila kuonekana, akichukua taarifa za kutisha za uamuzi
wao mbovu na kuandika historia ya matendo mabaya yasiyofaa [42]
kuonekana katika macho ya wanadamu. "Babeli mkuu" alikuwa

[3] Cardinal Wiseman's Lectures on "The Real Presence, " lecture 8, sec. 3, par.26.

"amelewa kwa damu ya watakatifu." Soma Ufunuo 17:5, 6. Miili iliyokuwa imeharibika, ya mamilioni ya wafia dini ilimlilia Mungu kwa ajili ya kisasi juu ya mamlaka iliyokuwa imeasi.

Utawala wa Papa ulikuwa umekuwa utawala dhalimu wa dunia. Wafalme walikuwa wanatii maagizo ya Papa. Kwa mamia ya miaka, mafundisho ya Kanisa la Roma yalikuwa yanapokelewa bila maswali. Watumishi wake walikuwa wanaheshimiwa na kutunzwa kwa gharama kubwa. Kanisa la Roma lilikuwa halijawahi kufikia ukuu, fahari, na nguvu, kuliko wakati huo.

Lakini "mchana wa utawala wa Papa ulikuwa ni usiku wa manane kwa ulimwengu." [4] Maandiko yalikuwa hayajulikani kabisa. Viongozi wa utawala wa Papa walikuwa wanaichukia nuru ambayo ingefichua dhambi zao. Sheria ya Mungu, ambayo ni kiwango cha haki, ikiwa imeondolewa, walifanya uovu bila kizuizi. Majumba ya Mapapa na maaskofu yalikuwa mahali pa ufisadi mbaya wa kupindukia. Baadhi ya maaskofu walikuwa wanafanya uhalifu wa kuudhi mpaka watawala wa kidunia wakadiriki kuwaondoa kama watu katili wasioweza kuvumiliwa. Kwa kame kadhaa, Ulaya haikuwa na maendeleo yo yote katika elimu, sanaa, au ustaarabu. Ukristo ulikuwa umekumbwa na kudumaa kimaadiali na kielimu. Hayo ndiyo yalikuwa matokeo ya kuliondoa Neno la Mungu.

[4] Wylie, History of Protestantism, book 1, Chap. 4.

# Sura Ya 4 - Wawaldensia Waitetea Imani



Katika kipindi kirefu cha utawala wa Papa, walikuwepo mashahidi wa Mungu ambao walikuwa wanaithamini imani kwa Kristo kama mpatanishi pekee kati ya Mungu na wanadamu. Walikuwa wanaiamini Biblia kama kanuni pekee ya maisha, na kuitakasa Sabato ya kweli. Walikuwa wakiitwa waasi, maandishi yao yalipigwa marufuku, yakapotoshwa na kukataliwa. Lakini bado walisimama imara.

Hawa hawatajwi sana katika kumbukumbu za wanadamu, isipokuwa katika tuhuma kutoka kwa watesi wao. Kanisa la Roma lilikuwa linataka kungamiza kila ambacho lilikuwa linaona kuwa ni "uasi," kiwe ni watu au maandishi. Kanisa la Roma pia liliamua kuharibu kumbukumbu zote za ukatili wake dhidi ya wale waliokuwa na maoni tofauti. Kabla ya kugunduliwa kwa elimu ya uchapaji, vitabu vilikuwa vichache; kwa hiyo kulikuwa hakuna jambo la kulizuia kanisa kutimiza makusudi yake. Mara baada ya utawala wa Papa kupata madaraka lilianza kuwaangamiza wote waliokuwa hawataki kukubaliana na utawala wake.

Katika nchi ya Uingereza, Ukristo wa kale ulikuwa umeota mizizi mapema, bila kuchafuliwa na uasi wa Kanisa la Roma. Zawadi pekee ambayo makanisa ya mwanzo ya Uingereza yalipata kutoka Rumi ni mateso toka kwa wafalme wa kipagani. Wakristo wengi waliokuwa wanakimbia mateso kule Uingereza walipata hifadhi kule Scotland. Toka huko ukweli ulipelekwa Ireland, na katika nchi hizi, ulipokelewa kwa furaha.

Watu wa Saxony walipovamia Uingereza, upagani ulipata nguvu, na Wakristo walilazimika kukimbilia milimani. Kule Scotland, kame moja baadaye, num iling'aa kwenda nchi za mbali. Toka Ireland, alikuja Columba na wafanyakazi wenzake, ambao walikifanya kisiwa cha Iona, kilichokuwa ukiwa, kuwa kituo cha kazi yao ya umisionari. Miongoni mwa walnjilisti hawa alikuwepo mshika Sabato ya kwenye Biblia, na kwa namna hiyo ukweli huu ulifikishwa

kwa watu. Huko Iona ilianzishwa shule ambayo ilitoa wamisionari kwenda Scotland, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na hata Italia.

## [44] Roma Vakabiliana na Dini ya Biblia

Lakini Kanisa la Roma liliazimu kuiweka Uingereza chini ya utawala wake. Katika kame ya sita wamisionari wa Kanisa la Roma walianza kuwaongoa watu wa Saxony waliokuwa wapagani. Kazi ilipoendelea, viongozi wa utawala wa Papa walipambana na Wakristo wa kale-watu wa kawaida, wanyenyekevu na wenye tabia zilizojengwa kwenye Maandiko, mafundisho na uungwana. Viongozi wa Kanisa la Roma walionesha mapokeo potovu, majivuno na kiburi cha utawala wa Papa. Kanisa la Roma lilikuwa linataka makanisa haya ya Kikristo yamtambue Papa. Waingereza walijibu kwamba Papa hakuwa anastahili ukuu katika kanisa na walikuwa wanaweza kumpa heshima anayostahili kila mfuasi Wakristo. Walikuwa hawamjui Bwana mwingine isipokuWakristo.

Sasa roho ya kweli ya utawala wa Papa ilidhihirika. Kiongozi wa Kirumi akasema: "Kama hamtawapokea ndugu watakaowaletea amani, basi mtapokea maadui watakaowaletea vita." [5] Vita na udanganyifu vilitumika dhidi ya mashahidi hawa wa imani ya Biblia, hadi makanisa ya Uingereza yalipoharibiwa na kulazimishwa kumtii Papa.

Katika nchi zilizokuwa nje ya utawala kwa Kanisa la Roma, jumuiya za Kikristo zilibaki zikiwa hazijaguswa sana na uchafu wa Kanisa la Roma. Waliendelea kuichukulia Biblia kama kanuni ya pekee ya imani. Wakristo hawa walikuwa wanaamini kuwa sheria ya Mungu ni ya milele na walikuwa wanaishika Sabato ya amri ya nne. Makanisa yaliyokuwa yanashika imani na desturi hizi yalikuwa Afrika ya Kati na miongoni mwa Waarmenia wa Asia.

Wawaldensia walikuwa mstari wa mbele kati ya wale waliokuwa wanapinga mamlaka ya Papa. Makanisa ya Piedmont yalidumisha uhuru wao katika nchi ambayo utawala wa Papa ulikuwa umeweka kiti chake. Lakini wakati ulifika ambapo Kanisa la Roma lilisisitiza kuwa makanisa hayo yajisalimishe. Hata hivyo, baadhi, walikataa kumtii Papa au maaskofu, wakiwa wameazimu kuhifadhi

[5] J.H Merle D' Aubigne, History of the Reformation of the Sbcteenth Century, kit. 17 sura ya 2.

usafi na usahili wa imani yao. Kulitokea utengano. Wale waliokuwa wameshika imani ya kale sasa walijitoa. Baadhi yao wakiiacha mil- [45]
ima yao ya Alps, waliinua bendera ya ukweli katika nchi za ugenini. Wengine walikimbilia katika maficho ya miamba ya milimani na huko waliendeleza uhuru wao wa kumwabudu Mungu.

Imani yao ya kidini ilikuwa imejengwa kwenye Neno la Mungu. Wakulima hao wa hali ya chini, waliokuwa wametengwa na dunia, hawakugundua wao wenyewe ukweli uliokuwa kinyume na mafundisho ya kanisa lililokuwa limeasi. Imani yao ya kidini ilikuwa ni urithi kutoka kwa baba zao. Walikuwa wanapigania imani ya kanisa la mitume. "Kanisa la jangwani" ndilo lililokuwa kanisa la kweli la Kristo, linalohifadhi hazina ya ukweli ambao Mungu aliwakabidhi watu wake waupeleke kwa ulimwengu, na siyo ule utawala wenye kiburi uliokuwa umetawazwa katika makao makuu ya dunia.

Miongoni mwa sababu kubwa zilizosababisha kujitenga kwa kanisa la kweli na Kanisa la Roma, ni chuki ya Kanisa la Roma dhidi ya Sabato ya Biblia. Kama ilivyotabiriwa katika unabii, mamlaka ya Papa iliikanyaga sheria ya Mungu. Makanisa yaliyokuwa chini ya Papa yalishurutishwa kuiheshimu Jumapili. Wakati uovu huo uliokuwa unaenea ukiendelea, wengi kati ya watu waaminifu wa Mungu walitatizwa kiasi kwamba walikuwa wakiiadhimisha Sabato, na Jumapili waliacha kufanya kazi. Lakini jambo hili halikuwaridhisha viongozi wa Kanisa la Roma. Walitaka Sabato inajisiwe, na waliwalaumu wale waliokuwa wanajaribu kuiheshimu.

Mamia ya miaka kabla ya kipindi cha matengenezo, Wawaldensia walikuwa na Biblia zilizokuwa katika lugha yao ya asili. Jambo hili liliwafanya wawe walengwa maalum ya mateso. Walilibainisha Kanisa la Roma kuwa ndiyo Babeli iliyoasi inayotajwa katika unabii. Walisimama imara kupinga uchafu wa ufisadi wa Kanisa la Roma, huku wakihatarisha maisha yao. Katika enzi zote za uasi, kulikuwa na Wawaldensia waliokuwa wanapinga ukuu wa Kanisa la Roma, waliokuwa wanapinga ibada ya sanamu, na waliokuwa wanashika Sabato. (Angalia kiambatisho).

Wawaldensia walipata mahali pa kujificha nyuma ya milima mirefu. Wakimbizi hawa waaminifu waliwaonesha watoto wao vilele vilivyokuwa vimeinuka juu katika utukufu na kuwaeleza juu ya yule ambaye Neno lakc linadumu kama milima ya milele. [46]

Mungu alikuwa ameweka milima imara; hakuna mkono ambao ungeweza kuiondoa isipokuwa wa yule aliye na uwezo usio na ukomo. Hivyo ndiyo alivyokuwa wamcisimika sheria yake. Mkono wa mtu usingeweza kubadili kipengele kimoja cha sheria ya Mungu kama vile usivyoweza kung'oa milima na kuitupa baharini. Wakimbizi hao hawakuendekeza huzuni kwa sababu ya ugumu wa maisha waliyokuwa wakipitia; hawakuwahi kuwa wapweke katika sehemu zilizojitcnga za milimani. Waliufurahia uhuru wao wa kuabudu. Waliimba nyimbo za sifa wakiwa katika majabali marefu, wala majeshi ya dola ya Kirumi hayakuweza kunyamazisha nyimbo zao za shukurani.

## Kanuni za Ukweli Zilizokuwa Zinathaminiwa

Kanuni za ukweli zilikuwa zinathaminiwa kuliko nyumba, ardhi, marafiki, ndugu na hata uhai wenyewe. Tangu mapema katika utoto, vijana walikuwa wanafimdishwa kuheshimu na kutambua utakatifu wa matakwa ya sheria ya Mungu. Nakala za Biblia zilikuwa adimu; kwa sababu hiyo, maneno haya ya thamani yalikuwa yanakaririwa. Wengi walikuwa wanaweza kukariri sehemu kubwa za Agano la Kale na Jipya.

Tangu utotoni walikuwa wamefundishwa kustahimili matatizo na kufikiri na kutenda wao wenyewe. Walikuwa wamefundishwa kubeba majukumu, kuwa waangalifu katika usemi, na kuelewa hekima ya kuwa kimya. Neno moja tu la siri lingefika masikioni mwa adui zao lingehatarisha maisha ya mamia ya ndugu, kwani maadui wa ukweli walikuwa waawafuatilia kama mbwa mwitu, wale waliokuwa wanathubutu kujipatia uhuru wa imani ya kidini.

Wawaldensia walihangaikia chakula chao kwa uvumilivu mkubwa. Kila eneo la ardhi lililopatikana kati ya milima lilitumiwa vema na kwa uangalifu. Uchumi na kujikana nafsi vilikuwa miongoni mwa elimu ambayo ilitolewa kwa watoto . Mchakato ulikuwa mgumu lakini wenye manufaa, ule ambao mwanadamu anauhitaji katika hali yake ya dhambi. Vijana walikuwa wanafundishwa kwamba nguvu zao zote zilikuwa za Mungu, na kwamba iliwapasa kuziendeleza kwa ajili ya kazi yake.

Makanisa ya wafuasi wa Wawaldensia yalikuwa yanafanana na kanisa la wakati wa mitume. Waliiamini Biblia kama mamlaka

pekee isiyoweza kukosea huku wakipinga mamlaka ya Papa na maaskofu. Kinyume na mapadre wa kimwinyi wa Kanisa la Roma, wachungaji wao walililisha kundi la Mungu, wakilingoza kwenye malisho mabichi na chemchemi hai za Neno lake Takatifu. Watu walikuwa hawakutani kwenye makanisa ya fahari au makubwa, bali kwenye mabonde ya milima ya Alps, na wakati wa hatari, walikuwa wanakutana kwenye ngome za miamba, kusikiliza maneno ya ukweli kutoka kwa watumishi Wakristo. Wachungaji walikuwa hawahubiri Injili tu, lakini pia walikuwa wakiwatembelea wagonjwa, pia walikuwa wanafanya kazi ya kuhimiza umoja na upendo wa kidugu. Kama Paulo, fundi wa mahema, kila mmoja alijifunza ufundi fulani kwa ajili ya kujikimu. [47]

Vijana walipata mafunzo kutoka kwa wachungaji wao. Biblia ndiyo ilikuwa somo lao kuu. Injili za Mathayo, Yohana pamoja na nyaraka nyingine nyingi zilikaririwa.

Maandiko Matakatifu yaliandikwa bila kuchoka, fungu kwa fungu, wakati mwingine wakijimulikia kwa myenge kwenye mapango yenye giza. Malaika toka mbinguni waliwazingira hawa wafanyakazi waaminifu.

Shetani alikuwa amewashawishi mapadre na maaskofu wa mamlaka ya Papa kulifukia Neno la ukweli kwenye takataka za uongo na imani za mapokeo potovu. Lakini kwa namna ya ajabu, lilihifadhiwa bila kuharibiwa katika kipindi chote cha zama za giza. Kama ilivyokuwa safina katika vilindi vya mawimbi makubwa, Neno la Mungu hushindana na dhoruba zinazotishia kuliangamiza. Kama vile mgodi ulivyo na mikondo ya dhahabu au fedha iliyofichika chini ya ardhi, ndivyo Maandiko Matakatifu yalivyo na hazina ya ukweli unaoonekana kwa mtafuataji mnyenyekevu mwenye maombi. Mungu alikuwa amekusudia Biblia iwe kitabu cha kujifunzia kwa wanadamu wote, kama njia ya kujifunua yeye mwenyewe. Kila ukweli unaoonekana ni ufunuo mpya wa tabia ya Mtunzi wa Biblia.

Kutoka katika shule zao kule milimani, baadhi ya vijana walipelekwa kwenye vyuo kule Ufaransa na Italia, ambako kulikuwa na uwanja mpana zaidi wa kujifunza na uchunguzi kuliko katika Milima yao ya Alps. Vijana waliokuwa wanapelekwa huko walikuwa wanakutana na majaribu. Walikuwa wanakutana na mawakala wa Shetani ambao

walikuwa wanashawishi kukubaliana na uasi uliofichika na udanganyifu hatari. Lakini elimu yao kutoka utoto ilikuwa imewaandaa kwa ajili ya jambo hilo.

[48] Katika shule walizokuwa wanakwenda, hawakutakiwa kumwamini mtu ye yote. Mavazi yao yalikuwa yametengenezwa kwa namna ambayo yangeweza kuficha hazina yao kuu—Maandiko. Kila walipoweza, waliweka kwa uangalifu sehemu za Maandiko katika njia za wale ambao mioyo yao ilikuwa tayari kupokea ukweli. Watu waliongolewa kuufuata ukweli katika vyuo hivi, na mara nyingi kanuni za ukweli zilienea shule nzima. Hata hivyo viongozi wa mamlaka ya Papa walishindwa kufuatilia chanzo cha kile walichokiita "uasi" uharibuo.

## Vijana Waliofundishwa Kuwa Wamisionari

Wakristo wa Kiwaldensia waliona kuwa walikuwa na wajibu nyeti wa kuangaza nuru yao. Kwa nguvu ya Neno la Mungu walitafuta njia ya kuondoa utumwa uliokuwa umeletwa na Kanisa la Roma. Iliwapasa wachungaji wa Wawaldensia kutumika kwa miaka mitatu katika maeneo ya kimisionari kabla ya kushika uongozi wa kanisa nyumbani. Hili lilikuwa zoezi murua kwa maisha ya wachungaji katika wakati ambapo roho za watu zilikuwa zinajaribiwa. Vijana hawakuwa wanaona utajiri na heshima ya kidunia mbele yao, bali walikuwa wanaona hatari na pengine kuuawa kwa ajili ya imani. Wamisionari walikuwa wanakwenda wawili wawili, kama Yesu alivyokuwa amewatuma wanafunzi wake.

Kutangaza kusudi lao kungefanya lisifanikiwe. Kila mchungaji alikuwa na ujuzi wa kazi au fani fulani, na wamisionari walifanya kazi zao kwa siri huku wakijulikana kama wafanyabiashara au wachuuzi."Walibeba nguo za hariri, vito, na bidhaa nyingine, ... Na kule ambapo wangekataliwa kuingia kama wamisionari, walikuwa wanakaribishwa kama wafanyabiashara." [6] Walibeba nakala za Biblia kwa siri, wakati fulani Biblia yote au nusu yake. Mara kwa mara shauku ya kusoma Neno la Mungu ilikuwa inaamshwa, na sehemu za Biblia ziliachwa pamona na watu waliokuwa na nia.
[49] Wamisionari hawa, huku wakiwa pekupeku na mavazi yao yakiwa yamechakaa na kuchafuka safarini , walipita katika miji mikubwa

[6] Wyllie, kit. 1, sura 7

na kupenya hadi nchi za mbali. Makanisa yalianzishwa njiani walimokuwa wakipita, na damu ya wafia dini ilikuwa inaushuhudia ukweli. Likiwa limefichwa na kimya kimya, Neno la Mungu lilikuwa likipokelewa kwa furaha katika nyumba na mioyo ya watu.

Wawaldensia walikuwa wanaamini kuwa mwisho wa mambo yote ulikuwa hauko mbali sana. Kadiri walivyoendelea kusoma Biblia waliifurahia sana kazi yao ya kuufanya wa Biblia ukweli unaookoa ujulikane kwa wengine. Walipata faraja, tumaini na amani katika kumwamini Yesu. Mioyo yao ilipoangaziwa nuru hii, walitamani kuiangaza miali yake kwa wale waliokuwa katika giza la uongo wa utawala wa Papa.

Chini ya uongozi wa Papa na mapadre, watu wengi walifundishwa kutegemea matendo yao kuwaokoa. Siku zote walikuwa wanajitumainia wenyewe, akili zao zikiwa zimezama katika hali yao ya dhambi, wakitaabisha roho na miili, lakini walikuwa hawapati nafuu. Maelfu walikuwa wanaishi maisha yao yote katika vyumba vya watawa. Kwa kufunga mara kwa mara na mapigo, kwa kukesha usiku, kwa kulala kifudifudi kwenye mawe ya baridi yaliyomwagiwa maji, kwa safari ndefu za hija—wakisumbuliwa na hofu juu ya ghadhabu ya Mungu ya kulipiza kisasi—wengi waliteseka, mpaka mwili uliochoka uliposhindwa kustahimili. Waliingia kaburini bila hata chembe ya matumaini.

### Wenye Dhambi Waelekezwa kwa Kristo

Wawaldensia walikuwa na shauku ya kuwafunulia watu hawa wenye njaa, ujumbe wa amani ulio katika ahadi za Mungu, na kuwaelekeza kwa Kristo kama tumaini lao la pekee la wokovu. Walikuwa wanaamini kuwa fundisho la matendo mema kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi lilikuwa limejengwa katika uongo. Stahili za Mwokozi aliyekufa na kufufuka ndizo msingi wa imani ya Kikristo. Inampasa mwanadamu kumtegemea Kristo kwa karibu kama mkono au mguu ulivyo karibu na mwili au tawi lilivyo karibu na mzabibu.

Mafundisho ya Mapapa na mapadre yalikuwa yanawafanya watu [50]
wamwone Mungu na hata Kristo kama mkali na wa kutisha, asiye na huruma kwa wanadamu kiasi ambacho ilikuwa inabidi mapadre na watakatifu waombwe ili kufanya upatanisho. Wale ambao akili zao

zilikuwa zimepata nuru walikuwa wanatamani kuondoa vikwazo ambavyo Shetani alikuwa ameviweka, ili watu waweze kwenda moja kwa moja kwa Mungu, watubu dhambi zao, na kupata msamaha na amani.

## Kuuvamia Ufalme wa Shetani

Wamisionari wa Kiwaldensia walikuwa wanatoa kwa tahadhari sehemu za Maandiko Matakatifu. Nuru ya ukweli ilipenya katika akili nyingi zilizokuwa zimetiwa giza, hadi Jua la Haki alipoangaza moyoni kwa uponyaji katika miali yake. Mara nyingi msikilizaji alikuwa anatamani sehemu fulani ya Biblia isomwe tena, kana kwamba anataka kujiridhisha kwamba amesikia vema.

Wengi walikuwa wanaona jinsi upatanisho wa mwanadamu kwa niaba ya mwenye dhambi ulivyokuwa bure. Walikuwa wanasema kwa mshangao: "Kristo ni kuhani wangu; damu yake ni dhabihu yangu; madhabahu yake ndiyo kitubio changu." Nuru iliyowaangazia ilikuwa kubwa kiasi kwamba waliona kama wamepelekwa mbinguni. Hofu yote ya mauti iliondolewa. Sasa walikuwa wanatamani hata kwenda jela kama huko wangeweza kumheshimu Mwokozi wao.

Neno la Mungu lilikuwa linaletwa na kusomwa katika sehemu za siri, wakati fulani lilikuwa linasomwa kwa ajili ya roho moja, na wakati mwingine lilikuwa linasomwa kwa ajili ya kundi dogo lililokuwa linatamani nuru. Mara nyingi usiku mzima ulikuwa ukitumika kwa namna hii. Mara nyingi maneno kama haya yalikuwa yanasemwa: "Je, Mungu ataikubali sadaka yangu? Je, atanifurahia? Atanisamehe?" Jibu lilikuwa linasomwa, "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha." Mt.l 1:28.

Watu hawa waliokuwa na furaha walirudi kwao kueneza ile nuru, kusimulia kwa wengine kadiri walivyokuwa wanaweza juu ya mambo mapya waliyojifunza. Walikuwa wamepata njia mpya na ya kweli! Maandiko yalikuwa yamegusa mioyo iliyokuwa inautamani ukweli. Mjumbe wa kweli alisonga mbele. Mara nyingi wasikilizaji wake walikuwa hawaulizi alikokuwa ametoka na alikokuwa anakwenda. Walikuwa wametekewa kiasi kwamba hawakuwa

wanafikiria kumwuliza. “Je, anaweza kuwa alikuwa malaika kutoka mbinguni?” Walikuwa wanauliza.

Mara nyingi mjumbe wa kweli alikuwa amekwenda kwenye nchi [51] nyingine au alikuwa anateseka kwenye magereza yaliyokuwa chini ya ardhi au alikuwa amekufa pale alipokuwa ameshuhudia ukweli. Lakini maneno aliyokuwa ameyaacha yalikuwa yakifanya kazi.

Viongozi wa utawala wa Papa waliona hatari kutokana na kazi za watu hawa wanyenyekevu waliokuwa wakisafiri huku na kule. Nuru ya ukweli ingeondoa mawingu mazito ya uongo ambayo yalikuwa yamewafunika watu; ingeelekeza mawazo yao kwa Mungu tu na matokeo yake ingeharibu ukuu wa Kanisa la Roma.

Watu hawa, waliokuwa wanashika imani ya kanisa la kale, walikuwa ushuhuda thabiti dhidi ya uasi wa Kanisa la Roma. Na kwa sababu hiyo, waliamsha chuki na mateso. Kukataa kwao kuacha Maandiko lilikuwa kosa ambalo Kanisa la Roma lisingeweza kulivumilia.

### Kanisa la Roma Laazimu Kuwaangamiza Wawaldensia

Sasa vita mbaya zaidi ya kidini ilianza dhidi ya watu wa Mungu katika nyumba zao za milimani. Wapelelezi na watesaji walitumwa kuwafuatilia. Mara kwa mara mashamba yao yenye rutuba yaliharibiwa, makazi na makanisa yao madogo yaliteketezwa kabisa. Hakuna tuhuma ambayo ingeweza kuletwa dhidi ya uadilifu wa kundi hili lilokuwa limepigwa marufuku. Kosa lao kubwa lilikuwa kwamba hawakuwa tayari kumwabudu Mungu kulingana na matakwa ya Papa. Kila aina ya matusi na mateso ambayo wandamu au maShetani wangeweza kuyafikiria, yalielekezwa kwao kwa ajili ya “uhalifu” huo.

Kanisa la Roma Iilipoazimu kuangamiza kundi hili la kidini lililokuwa linachukiwa, tamko rasmi kutoka kwa Papa lilitolewa likiwatuhumu kuwa waasi na kuwatoa ili wanyongwe. (Angalia Kiambatisho.) Hawakuwa wanatuhumiwa kuwa wavivu, au kutokuwa waaminifu, au kwa kutofuata utaratibu; lakini ilidaiwa kuwa walikuwa na mwonekano wa utauwa na utakatifu uliokuwa unapotosha “kondoo wa kundi la kweli.” Amri hii ya Papa ilikuwa inawataka washiriki wote wa kanisa kuungana katika vita vya kidini dhidi ya [52] “waasi” hawa. Kama motisha, amri hiyo, “iliwaondolea nadhiri zao

wote waliokuwa wanajiunga na vita hiyo; iliwahalalishia umiliki wa ardhi yo yote ambayo huenda walikuwa hawakuipata kihalali, na iliwaahidi ondoleo la dhambi zao zote wale ambao wangeua mwasi ye yote. Amri hiyo ilifuta mikataba yote iliiyokuwa imefanywa kwa manufaa ya Wawaldensia, ikawazuia watu wote kuwapatia msaada wa aina yo yote, na iliwaruhusu watu wote kutwaa ardhi zao."[7] Waraka huu unaonesha wazi kabisa kuunguruma kwa joka, na wala siyo sauti ya Kristo. Roho ile ile iliyomsulubisha Kristo na kuwaua mitume, iliyomchochea Nero mwenye uchu wa damu dhidi ya waaminifu katika wakati wake, ilikuwa inajitahidi kuwaondoa duniani wale waliokuwa wanapendwa na Mungu.

Licha ya kukabiliana na vita ya dini dhidi yao na ukatili wa kinyama, watu hawa waliokuwa wanamcha Mungu, waliendelea kutuma wamisionari ili waeneze ukweli huu wa thamani. Waliwindwa hadi kuuawa, na bado damu yao ilimwagilia mbegu iliyokuwa imepandwa na ikazaa matunda.

Hivi ndivyo, Wawaldensia walivyomshuhudia Mungu kame kadhaa kabla ya Luther. Walipanda mbegu za Matengenezo ambayo yalianza wakati wa Wycliffe, yakaendelea kukua na kuenea zaidi katika siku za Luther, na inapasa Matengenezo hayo yaendelezwe mpaka mwisho wa wakati.

[7] *Ibid*. kitabu cha 16, sura ya 1

# Sura Ya 5 - Nuru Yachomoza Uingereza [53]

Mungu hakuvumilia kuona Neno lake likiangamizwa kabisa. Katika nchi mbalimbali za Ulaya watu walisukumwa na Roho wa Mungu kuutafuta ukweli kama kutafuta hazina zilizofichwa. Kwa bahati njema, kwa kuongozwa na Maandiko Matakatifu wao wenyewe walikubali kupokea nuru kwa gharama yoyote. Japokuwa hawakuweza kufahamu mambo yote, waliwezeshwa kugundua ukweli mwingi uliokuwa umefichika kwa muda mrefu.

Ulikuwa umefika wakati Maandiko yafikishwe kwa watu katika lugha zao za asili. Wakati wa giza nene kwa ulimwengu ulikuwa umekwisha kupita. Katika miji mingi kulikuwa na dalili za mapambazuko yaliyokuwa karibu kuja.

Mnamo kame ya kumi na nne, "nyota ya asubuhi ya Matengenezo" ilichomoza Uingereza. John Wycliffe alikuwa anafahamika chuoni kutokana na bidii yake katika kumcha Mungu pamoja na umahiri wake katika masomo. Alipewa elimu ya juu ya falsafa, kanuni za kanisa, na sheria za kiraia, ili kumwandaa kwa ajili ya kuingia katika pambano kubwa la uhum wa kiraia na wa kidini. Alikuwa amepata elimu ya juu ya masomo hayo, na alielewa mbinu za wasomi. Uelewa wake mpana na wa kina ulifanya aheshimiwe na marafiki na maadui zake pia. Adui zake walishindwa kudhalilisha kazi ya matengenezo kwa kuonesha ujinga au udhaifu wa aliyekuwa anaitetea.

Wycliffe alipokuwa bado yuko chuoni, alijiingiza katika kuchunguza Maandiko. Kabla ya hapo, alikuwa ameona hitaji kubwa, ambalo taaluma yake ya uanazuoni wala mafundisho ya kanisa havikuweza kulikidhi. Katika Neno la Mungu alipata kile ambacho alikuwa amekitafuta mahali pengine bila ya mafanikio. Humo alimwona Kristo akioneshwa kama wakili pekee kwa ajili ya mwanadamu. Akaazimu kuutangaza ukweli aliougundua.

Wycliffe alipokuwa anaanza kazi yake, alikuwa hajakusudia kuwa mpinzani wa Kanisa la Roma. Lakini kadiri alivyotambua makosa ya mamlaka ya Papa, ndivyo alivyozidi kudhihirisha kwa

[54] bidii zaidi mafundisho ya Biblia. Aligundua kuwa Kanisa la Roma lilikuwa limeacha Neno la Mungu kwa ajili ya mapokeo ya watu. Aliwashutumu bila hofu makasisi kwa kupiga marufuku Maandiko, na akataka Biblia irejeshwe kwa watu na mamlaka yake yaimarishwe tena kanisani. Alikuwa mhubiri hodari na mwenye lugha ya kushawishi, na maisha yake ya kila siku yalikuwa kielelezo cha ukweli aliokuwa anauhubiri. Ujuzi wake wa Maandiko, usafi wa maisha yake, ujasiri na uadilifu wake vilimpa heshima kubwa. Wengi waliona uovu katika Kanisa la Roma. Wengi bila kuficha furaha yao waliupokea kwa shangwe ukweli uliofunuliwa na Wycliffe . Lakini viongozi wa utawala wa Papa walikasirika sana; huyu mwana matengenezo alikuwa anapata umaarufu kuliko wao.

### Mgunduzi wa Uovu Aliyc Makini

Wycliffe alikuwa mgunduzi makini wa uongo na alikabili bila hofu udhalilishaji uliokuwa umeshinikizwa na Kanisa la Roma. Huku akiwa kasisi wa ikulu, aliamua kusimama kidete dhidi ya malipo ya kodi iliyodaiwa na Papa kutoka kwa mtawala mkuu wa Uingereza. Papa kujitwalia mamlaka juu ya watawala wa dunia ilikuwa kinyume na haki na ufunuo. Matakwa ya Papa yalikuwa yameamsha hasira, na mafundishoya Wycliffe yalivutia mawazo ya watu muhimu katika taifa. Mfalme na wenye vyeo waliungana katika kukataa kulipa kodi.

Watawa maskini walirundikana Uingereza, wakiweka vizuizi katika ukuu na mafanikio ya taifa. Maisha ya watawa ya kutokuwa na kazi na ufukara yalikuwa hayanyonyi tu raslimali za watu, bali pia yalifanya kazi zilizokuwa za maana zidharaulike. Vijana walivunjwa mioyo na kuharibiwa. Wengi walishawishwa kuingia katika maisha ya utawa siyo tu bila kibali cha wazazi wao, lakini pia hata bila utashi wao, na pia ikiwa ni kinyume cha matakwa yao. Kwa kutumia "unyama huu uliopita kiasi," kama Luther alivyoeleza baadaye, "ikiwapendeza zaidi mbwa mwitu na walio dhalimu kuliko Mkristo na mwanadamu," mioyo ya watoto ilifanywa kuwa migumu dhidi ya wazazi wao. [8]

[55] Hata wanafunzi katika vyuo vikuu walidanganywa na watawa

[8] Bamas Sears, The Life ofLuther, pp. 70,69..

na kushawishwa kujiunga na mfumo wao. Mara walipokuwa wanafungwa katika mtego huo ilikuwa vigumu kupata uhuru. Wazazi wengi walikataa kuwapeleka watoto wao kwenye vyuo vikuu. Shule zilidumaa, na ujinga ukatawala.

Papa alikuwa amewapa hawa watawa mamlaka ya kusikiliza toba na kutomsamaha-chanzo cha uovu mkubwa. Watawa, wakiwa wamedhamiria kuongeza mapato yao walikubali kabisa kutoa msamaha kiasi kwamba wahalifu waliamua kukimbilia kwao, na uovu mbaya zaidi ukaongezeka kwa kasi. Zawadi ambazo zingewasaidia wagonjwa na maskini zilipelekwa kwa watawa. Utajiri wa watawa uliendelea kuongezeka, na majumba yao ya kifahari na meza zao za anasa vilifanya ongezeko la ufukara wa taifa kuwa dhahiri zaidi. Lakini watawa hawa waliendelea kutawala fikira za umma huo wenye mapokeo potovu na wakawafanya waamini kuwa wajibu pekee wa kidini ulikuwa kuutambua ukuu wa Papa, kuabudu watakatifu, kuwapa zawadi watawa, na kwamba haya yalikuwa yanatosha kuwapatia nafasi mbinguni.

Wycliffe kwa kutambua vema aligonga kwenye shina halisi la uovu, akatangaza kuwa mfumo wenyewe haukuwa wa kweli na ilikuwa inapasa uondolewe. Mjadala na uchunguzi vilianza. Wengi walifanywa wajihoji kama ilikuwa muhimu kupata msamaha toka kwa Askofu wa Kanisa la Roma badala ya Mungu. (Angalia Kiambatisho.) "Watawa na makasisi wa Kanisa la Roma," walisema, "wanatuangamiza kama saratani. Inapasa Mungu atuokoe, la sivyo watu wataangamia." [9] Watawa hawa waliokuwa ombaomba walidai kuwa walikuwa wanafuata mfano wa Mwokozi, wakatangaza kwamba Yesu na wanafunzi wake walikuwa wanasaidiwa na hisani za watu. Dai hili lilifanya wengi waiangalie Biblia ili wajifunze wenyewe ukweli.

Wycliffe alianza kuandika na kuchapisha vitini kupinga watawa, akiwarejesha watu kwenye mafundisho ya Biblia na Mwandishi wake. Asingekuwa na njia bora zaidi ya hii ya kuuharibu mtego mkubwa huo ambao Papa alikuwa ameuweka, na ambao mamilioni walikuwa wamenaswa nao.

Wycliffe aliyekuwa ameitwa kuitetea haki za ufalme wa Uingereza dhidi ya uvamizi wa Kanisa la Roma, aliteuliwa kuwa balozi [56]

[9] D' Aubigne', bk 17, ch. 7.

wa mfalme kule Uholanzi. Hapa alikutana na viongozi wa kanisa kutoka Ufaransa, Italia na Hispania na akapata fursa ya kuona mambo ambayo alipokuwa Uingereza yalikuwa yamefichika kwake.Ndani ya wawakilishi hawa kutoka kwenye mahakama ya Papa alielewa vema tabia halisi ya uongozi wa kanisa. Kwa shauku kubwa alirejea Uingereza ili arudie mafundisho yake ya awali, akitangaza kuwa kiburi na udanganyifu vilikuwa ni miungu ya Kanisa la Roma.

Baada ya Wycliffe kurudi Uingereza, aliteuliwa na mfalme kwenda kuwa paroko wa Lutterworth. Hii ilikuwa uthibitisho kwamba mfalme hakuwa amechukizwa na uwazi wa Wycliffe. Mvuto wa Wycliffe ulionekana katika kurekebisha imani katika taifa.

Baada ya muda mfupi hasira za Papa zilielekezwa kwake. Kutoka kwa Papa yalitolewa matamko matatu yakiamuru hatua za haraka za kumnyamazisha huyu mwalimu wa "uzushi" [10]

Matamko ya utawala wa Papa yaalipofika Uingereza yalisababisha Uingereza yote kuwekewa amri ya kuwafunga gerezani wazushi. (Angalia Kiambatisho.) Ilionekana dhahiri kuwa lazima baada ya muda mfupi Wycliffe angeangukia katika kisasi cha Kanisa la Roma. Lakini Yeye aliyewahi kumtamkia mtu mmoja zamani, "usiogope....mimi ni ngao yako" (Mwa. 15:1), alinyoosha mkono wake kumlinda mtumishi wake. Mauti ikaja, siyo kwa Mwana matengenezo, bali kwa Papa aliyekuwa ametoa tamko la kuangamizwa kwa Wycliffe.

Kifo cha Gregory XI kilifuatiwa na uchaguzi wa Mapapa wawili waliohasimiana. (Angalia Kiambatisho.) Kila mmoja aliwaambia wafuasi wake wafanye vita dhidi ya wale wa upande mwingine, akishinikiza matakwa yake kwa maapizo ya kutisha dhidi ya wapinzani wake na ahadi za thawabu kule mbinguni kwa wale wanaomuunga mkono. Makundi haya hasimu yalifanya kila yalilokuwa yanaweza kushambuliana, na Wycliffe akapumzika kwa muda.

[57] Pamoja na na kusababisha mvutano na ufisadi , mpasuko huu, uliandaa njia kwa ajili ya Matengenezo kwa kuwawezesha watu kuona uhalisi wa mamlaka ya Papa. Wycliffe aliwaomba watu wachunguze kama Mapapa hawa wawili walikuwa hawasemi ukweli

[10] Augustus Neander, General History of the Christian Religion and Church, kipindi cha 6, kipeng. 2, sehemu 1 kifungu 8..

walipokuwa wakishutumiana kila mmoja na mwenzake kuwa ni mpinga Kristo.

Wycliffe akiwa ameazimu kwamba nuru ipelekwe katika kila sehemu ya Uingereza, aliandaa kundi la wahubiri, wasio na makuu, wenye kumcha Mungu, walioupenda ukweli na kuwa na shauku ya kuusambaza. Watu hawa, kwa kufundisha kwenye masoko, mitaa ya miji mikubwa, na katika njia mashambani, waliwatafuta wazee, wagonjwa na maskini, wakawafunulia habari njema za neema ya Mungu.

Pale Oxford, Wycliffe alihubiri Neno la Mungu kwenye kumbi za Chuo Kikuu. Akapewa sifa ya kuitwa "Daktari wa Injili." Lakini kazi kuu kuliko zote katika maisha ya Wycliffe ilikuwa kutafsiri Maandiko kwa Kiingereza, ili kila mtu nchini Uingereza aweze kusoma matendo ya Mungu ya ajabu.

## Kushambuliwa na Ugonjwa wa Kutisha

Lakini kwa ghafla kazi zake zilisimimamishwa. Ingawa alikuwa hajafikia umri wa miaka sitini, kazi ngumu sana, majifunzo mengi na mashambulio ya maadui vilikuwa vimekula nguvu zake na kumfanya awe mzee kabla ya wakati wake. Alishambuliwa na ugonjwa wa hatari. Watawa walifikiri kuwa angetubu uovu aliokuwa amelifanyia kanisa, na wakaenda upesi kwenye chumba chake ili wasikie ungamo lake. "Mauti yamo midomoni mwako," walisema, "guswa na makosa yako na tangua mbele yetu yote uliyoyasema na kutujeruhi."

Mwanamatengenezo alisikiliza akiwa kimya. Kisha akamwomba mhudumu wake amuinue kitandani mwake. Huku akiwatazama kwa makini, alisema kwa uthabiti, kwa sauti yenye nguvu ambayo mara nyingi iliwatetemesha, "Sitakufa, nitaishi; na kwa mara nyingine nitayataja matendo maovu ya watawa." [11] Wakiwa wameshangazwa na kutahayarishwa, watawa walikimbia kutoka kwenye chumba.

Wycliffe akaishi na kuweza kufikisha mikononi mwa watu wa nchi yake silaha iliyo kubwa kuliko zote dhidi ya Kanisa la Roma - Biblia, wakala aliyeteuliwa na mbingu ili kukomboa, kuelimisha [58]

[11] D' Aubigne', bk. 17, ch. 7.

na kuwafikishia watu Injili. Wycliffe alijua kuwa alikuwa amebakiza miaka michache tu ya kufanya kazi; aliona upinzani ambao ilipasa akabiliane nawo; lakini akiwa ametiwa moyo na ahadi za Neno la Mungu, aliendelea mbele. Huku akiwa na nguvu kamili zilizoonekana katika uwezo wake kiakili, uzoefu wa kutosha, kwa majaliwa ya Mungu aliandaliwa kwa ajili ya kazi hii iliyo kuu kuliko zote alizowahi kuzifanya. Mwanamatengenezo huyu akiwa katika nyumba yake ya Upadre kule Lutterworth, hali akiacha kufuatilia dhoruba iliyoongezeka nje, akazami kwenye kazi hii.

Hatimaye, kazi ilimalizika-tafsiri ya kwanza ya Biblia. Mikononi mwa watu wa Uingereza, mwanamatengenezo aliiweka nuru ambayo kamwe haingezimishwa. Alikuwa amefanya kazi kubwa zaidi katika kuvunja pingu za ujinga na kuikomboa na kuiinua nchi yake kuliko yote yaliyowahi kutekelezeka katika ushindi kwenye viwanja vya mapambano.

Nakala za Biblia zingeweza kuzidishwa tu kwa njia ya kazi ngumu chosha. Shauku ya kupata kitabu hiki ilikuwa kubwa kiasi ambacho watengenezaji wa nakala walipatagumu sana kufikia kiwango cha mahitaji. Wanunuzi waliokuwa matajiri walitaka Biblia nzima. Wengine walinunua sehemu tu. Mara nyingi, familia ziliungana na kununua nakala moja. Kwa muda mfupi, Biblia ya Wycliffe, kwa haraka ilifika majumbani mwa watu.

Wycliffe sasa alifundisha mafundisho yaliyowabainisha Waprotestanti wokovu kwa njia ya imani katika Kristo na kutokukosea kwa Maandiko. Imani hii mpya ilipokelewa na takriban nusu ya watu wa Uingereza.

Kuonekana kwa Maandiko kulileta fadhaa kwa mamlaka za kanisa. Wakati huu Uingereza haikuwa na sheria inayokataza Biblia, kwani ilikuwa haijawahi kuchapwa katika lugha ya watu. Sheria hizi zilipitishwa baadaye na kushinikizwa kwa ukali.

Kwa mara nyingine viongozi wa utawala wa Papa waliandaa mpango wa kuizima sauti ya Mwanamatengenezo. Kwanza, sinodi ya maaskofu ilitamka kuwa mafundishoyake yalikuwa ya kizushi.
[59] Baada ya kufaulu kumshawishi mfalme kijana, Richard II, walipata tamko la kifalme kuwa kila mtu ambaye angeshikilia mafundisho yaliyokatazwa apelekwe gerezani.

Wycliffe akapeleka rufani yake toka kwenye Sinodi hadi kwenye Bunge. Bila ya hofu alishitaki mamlaka ya Papa mbele za baraza

la taifa na kudai badiliko la desturi mbaya sana za ukatili zilizoidhinishwa na kanisa. Adui zake wakapatwa na kiwewe. Ilitegemewa kuwa Mwanamatengenezo, wakati wa uzee wake, akiwa peke yake na bila marafiki, angejisalimisha kwa ufalme. Lakini badala yake, Bunge, likiwa limeamshwa na miito inayoshtua ya Wycliffe, liliondoa sheria, na Mwanamatengenezo akawa huru tena.

Kwa mara ya tatu aliletwa kwenye shitaka, na sasa ikiwa ni mbele ya Mahakama ya kikanisa katika ufalme. Hatimaye hapa kazi ya Mwanamatengenezo ingesimamishwa. Ndivyo wafuasi wa utawala wa Papa walivyodhani. Kama wangekamilisha kusudi lao, Wycliffe angetoka kwenye baraza hilo kuelekea kwenye miali ya moto na sio vinginevyo.

### Wycliffe Akataa Kukanusha

Lakini Wycliffe hakukanusha kauli yake. Alidumisha mafundisho yake, bila hofu na kukataa mashtaka ya watesi wake. Aliitisha wasikilizaji wake waje mbele ya mahakama ya kimbingu na kupima maneno yao ya hila na udanganyifu katika vipimo vya ukweli wa milele. Nguvu ya Roho Mtakatifu ilikuwa kati ya wasikilizaji. Kama mishale itokayo katika podo la Bwana, maneno ya Mwanamatengenezo yalipenya mioyoni mwao. Akawageuzia shitaka la uzushi, ambalo walikuwa wameliweka dhidi yake.

Alisema, "Je, mnadhani mnapambana na nani? Mzee anayekaribia kaburi? La! na Ukweli-Ukweli ulio na nguvu kuliko ninyi, na utawashinda." [12] Baada ya kusema hivyo, aliondoka na hakuna hata mmoja kati ya adui zake waliojaribu kumzuia.

Kazi ya Wycliffe ilikuwa imekaribia kuisha, lakini kwa mara [60]
nyingine tena alikuwa atoa ushuhuda kwa ajili ya Injili. Aliitwa kwa ajili ya shitaka mbele za mahakama ya utawala wa Papa pale Roma, ambayo mara nyingi ilimwaga damu ya watakatifu. Mshtuko uliopelekea kupooza ulifanya isiwezekane kwake kufanya safari hiyo. Lakini, ingawa sauti yake haingesikika Roma, angeweza kunena kwa njia ya maandishi. Mwanamatengenezo alimwandikia Papa barua, ambayo, ikionesha heshima na roho ya Ukristo, ilikuwa kemeo kali kwa ufahari na kiburi cha mamlaka ya Papa.

[12] Wylie, bk 2, ch. 13.

Wycliffe aliwasilisha kwa Papa na makadinali upole na unyenyekevu Wakristo, akionesha siyo tu kwao, bali pia kwa jumuiya yote ya Kikristo, tofauti kati yao na Mkuu ambaye walidai kumwakilisha.

Wycliffe alitegemea kikamilifu kwamba uhai wake ulngekuwa malipo kwa uthabiti wake. Mfalme, Papa na maaskofu waliungana ili kukamilisha maangamizi yake, na ilielekea kuwa isingechukuwa miezi mingi hadi yeye kufikishwa hatua ya kuchomwa moto. Lakini ujasiri wake haukutikisika.

Mtu ambaye katika maisha yake yote alikuwa amesimama imara akitetea ukweli, hangepaswa kuwa mhanga wa hasira ya adui zake. Bwana alikuwa mlinzi wake; na sasa, wakati adui zake walipojisikia kuwa na hakika ya kupata windo lao, mkono wa Mungu ulimwondoa kutoka katika upeo wao. Akiwa kanisani kwake pale Lutterworth, hali akiwa tayari kuongoza katika huduma ya chakula cha Bwana, alipooza na kuanguka, na katika muda mfupi akakata roho.

## Mpiga Mbiu wa Zama Mpya

Mungu alikuwa ameliweka neno la ukweli ndani ya kinywa cha Wycliffe. Uhai wake ulilindwa na kazi zake ziliendelezwa hadi msingi ulipokuwa umewekwa kwa ajili Matengenezo. Wycliffe hakuunda mfumo wake wa matengenezo kutokana na yeyote aliyemtangulia. Yeye alikuwa mpiga mbiu wa zama mpya. Licha ya hivyo, katika ukweli aliouwasilisha kulikuwa na umoja na ukamilifu ambao wanamatengenezo waliofuatia hawakuweza kuupita na pia ambao baadhi yao hawakuufikia. Muundo wake ulikuwa imara na wa kweli, kiasi kwamba haukuhitaji kuundwa upya na wale waliokuja baada yake.

[61] Vuguvugu kubwa ambalo Wycliffe alilianzisha ili kuyaweka huru mataifa yaliyokuwa yamekamatwa kwa muda mrefu na Kanisa la Roma chanzo chake kilikuwa katika Biblia. Hapa ndipo chanzo cha chemchemi ya baraka ambayo ilikuwa imetiririka katika kame kadhaa tangu kame ya kumi na nne kilipokuwepo. Huku akiwa ameelimishwa kuheshimu Kanisa la Roma kama mamlaka isiyokosea na kukubali kwa kicho bila maswali, mafundisho na desturi za miaka elfu, Wycliffe aliyapa kisogo haya yote ili asikilize Neno Takatifu la Mungu. Badala ya kanisa kunena kupitia kwa Papa,

alitangaza sauti ya Mungu anenaye kupitia kwenye Neno lake kuwa mamlaka pekee ya kweli. Alifundisha pia, kuwa Roho Mtakatifu ndiye mfasiri pekee wa Neno.

Wycliffe alikuwa mmoja kati ya Wanamatengenezo wakuu. Ni wachache tu waliokuja baada yake waliolingana naye. Usafl wa maisha, bidii isiyokoma katika kujifunza na kufanya kazi, uadilifu usiombuniwa, na upendo ulio kama Wakristo, ni tabia zilizodhihirika kwa Wanamatengenezo wa awali.

Biblia ndiyo ilimfanya akawa vile alivyokuwa. Kujifunza Biblia kutaadilisha kila wazo, hisia, na shauku kuliko majifunzo mengine yoyote. Inaimarisha nia, inaongeza ujasiri na ustahimilivu. Kama watu wangejifunza Maandiko kwa dhati na unyenyekevu, ulimwengu ungepata watu wenye akili nyingi zaidi, na wenye kanuni za kiungwana zaidi, kuliko zote ambazo zimetokana na majifunzo yanayofikiriwa kuwa bora ambayo falsafa ya mwanadamu imeweza kutoa.

Wafuasi wa Wycliffe, wanaofahamika kama Wycliffites na Waloladi, walisambaa hadi katika nchi zingine, wakibeba Injili. Wakati huu ambapo kiongozi wao alikuwa ameondolewa, wahubiri hawa walifanya kazi kwa ari zaidi kuliko wakati uliopita. Watu wengi walikusanyika ili kusikiliza. Baadhi ya waliokuwa kati ya waungwana, hata mke wa mfalme, ni baadhi yao walioongoka. Mahali pengi, ishara za ibada za sanamu za Kiroma ziliondolewa toka makanisani.

Lakini mara, mateso yasiyo na humma yakafumuka kwa wale waliodiriki kukubali Biblia kama kiongozi chao. Kwa mara ya kwanza katika historia ya Uingereza tamko la adhabu ya kuchomwa moto likatolewa dhidi ya wanafunzi wa Injili. Ufia dini ukafuatiwa na ufia dini. Hali wakiwindwa kama maadui wa kanisa na wasaliti wa ufalme, mawakili wa ukweli waliendelea kuhubiri maeneo yaliy- [62]
ofichika, wakitafuta makazi kwenye nyumba za maskini, na mara kwa mara wakikimbilia hata kwenye matundu na mapango.

Upinzani uliokuja kwa namna tulivu na yenye uvumilivu dhidi ya upotovu wa imani ya kidini uliendelea kunenwa kwa kame kadhaa. Wakristo wa wakati ule wa awali walikuwa wamejifunza kulipenda Neno la Mungu na hivyo wakateseka kwa uvumilivu kwa sababu yake. Wengi walitoa walivyokuwa navyo kwa ajili ya Kristo. Wale waliopata kibali cha kukaa kwenye nyumba zao waliwahifadhi kwa furaha ndugu zao waliofukuzwa, na wakati wao walipofukuzwa wa-

likubali kwa furaha hali ya kutengwa na jamii. Waliobeba ushuhuda wa ukweli bila hofu hadi kwenye magereza ya chini ardhini na kati ya mateso ya moto hawakuwa wachache, wakishangilia kuwa walionekana kustahili kujua "ushirika wa mateso yake."

Chuki ya mamlaka ya Papa haikupozwa na kupumzika kwa mwili wa Wycliffe kaburini. Zaidi ya miaka arobaini baada ya kifo chake mifupa yake ilifukuliwa na kuchomwa hadharani, na majivu yake kutupwa kwenye kijito kilichokuwa karibu. "Kijito hiki,"anasema mwandishi wa kale, "kimepeleka majivu yake hadi Avon, Avon hadi Savem, Savem hadi kwenye bahari ndogo, toka hapo hadi kwenye bahari kuu. Na kwa jinsi hiyo, majivu ya Wycliffe ni kielelezo cha mafundisho yake, ambayo kwa sasa yamesambazwa duniani kote." [13]

Kupitia kwa maandishi ya Wycliffe, John Huss wa Bohemia aliongozwa kujitoa toka kwenye makosa mengi ya Uroma. Kutokea Bohemia, kazi ilipanuka hadi nchi zingine. Mkono wa Mungu ulikuwa ukiandaa njia kwa ajili ya Matengenezo makuu.

[13] T Fuller, *Church History of Britain*, bk. 4, sec. 2, par. 54.

## Sura Ya 6 - Mashujaa Wawili Wakabili Mauti [63]

Karibuni kabisa na kame ya tisa Biblia ilikuwa imetafsiriwa na ibada za hadhara zilikuwa zikiendeshwa katika lugha ya watu wa Bohemia. Lakini Gregory VII alikusudia kuwafanya watu watumwa, na tamko lilitolewa lililokataza ibada za hadhara katika lugha ya Bohemia. Papa alitamka kuwa "ilikuwa inapendeza kwa Yeye aliye na uwezo wote kwamba ibada zake ziadhimishwe katika lugha isiyojulikana." [14] Lakini mbingu ilitoa mawakala kwa ajili ya kulilinda kanisa. Wawaldensia na Waalbijensi wengi, wakiwa wamekimbizwa na mateso, walikuja Bohemia. Walifanya kazi kwa juhudi na kwa siri. Kwa njia hiyo, Imani ya kwel ililllindwa.

Kabla ya siku za Huss walikuwepo watu katika Bohemia waliolaani upotovu kanisani. Hofu ya mamlaka ya Papa iliibuliwa, na mateso yakaanzishwa dhidi ya Injili. Baada ya muda tamko lilitolewa kuwa wale waliotoka katika ibada ya Kanisa la Roma wachomwe moto. Lakini Wakristo walitazamia mbeleni ushindi wa kazi yao. Mmoja wao alisema akikaribia kufa, "Kutokea kati ya watu wa kawaida, atainuka mtu asiye na upanga wala mamlaka, nao hawataweza kumshinda." [15] Yupo ambaye tayari alikuwa akiinuka, ambaye ushuhuda wake dhidi ya Roma ungeamsha mataifa.

John Huss alizaliwa katika mazingira ya kimaskini na akawa yatima mapema katika maisha yake kutokana na kifo cha baba yake. Mama yake ambaye alikuwa mcha Mungu, hali akiithamini elimu na uchaji wa Mungu kama hazina ya thamani zaidi, alitafuta njia za kumpa mtoto wake urithi huu. Huss alisomea kwenye shule ya jimbo, na kisha akajiunga na Chuo Kikuu cha Prague, akipokelewa kama mwanafunzi aliyesomeshwa kwa msaada.

Pale chuoni, Huss alijipatia heshima upesi kwa maendeleo yake [64]
ya haraka. Mvuto ulioonekana katika mwenendo wake wa uungwana ulimpa heshima kwa wote. Alikuwa mfuasi wa dhati wa Kanisa la Roma na mhitaji makini wa baraka za kiroho ambazo kanisa

[14] Wylie, bk. 3, ch. 1

[15] *Ibid*

lilidai kuwa nazo. Baada ya kumaliza mafunzo yake ya chuo, aliingia kwenye upadre. Huku akiongezeka kwa kasi katika umaarufu, aliambatanishwa na makao ya mfalme. Alifanywa pia kuwa profesa na baadaye akawa mkuu wa Chuo Kikuu. Msomi mnyenyekevu aliyesaidiwa akawa fahari ya nchi yake, jina lake lilifahamika Ulaya kote.

Jerome, ambaye baadaye alikuja kuwa karibu sana na Huss, alikuwa amemletea maandishi ya Wycliffe kutoka Uingereza. Malkia wa Uingereza, muongofu wa mafundisho ya Wycliffe, alikuwa ni mzaliwa wa Bohemia. Kupitia kwa mvuto wake, kazi za Mwanamatengenezo zilisambazwa sana katika nchi yake ya asili. Huss alikuwa na mwelekeo wa kukubali matengenezo yaliyokuwa yakitetewa. Ingawa hakujua, alikuwa tayari amekwisha ingia katika njia ambayo ilikuwa inampeleke mbali zaidi na Roma.

### Picha Mbili Zamvutia Huss

Katika kipindi hiki, wageni wawili kutoka Uingereza, wasomi, walikuwa wamepokea nuru na walikuwa wamekuja kuisambaza mjini Prague. Walinyamazishwa baada ya muda mfupi, lakini kwa sababu hawakuwa tayari kuacha kusudi lao, walihamia kwenye mbinu nyingine. Hali wakiwa wasanii pamoja na kuwa wahubiri, walichora picha mbili mahali palipokuwa wazi. Moja iliwakilisha kuingia kwa Kristo Yerusalemu, "Mpole, naye amepanda punda" (Mt.21:5) akifuatwa na wanafunzi wake waliovaa mavazi yaliyochakazwa na safari na miguu isiyo na viatu. Picha nyingine ilionesha msafara wa Papa-Papa katika mavazi yake ya kifahari na taji yenye ngazi tatu, akiwa juu ya farasi huku akiwa amepambwa kwa uzuri wa ajabu, akitanguliwa na wapiga tarumbeta na kufuatiwa na makadinali na maaskofu waliovalia mavazi yanayong'aa.

Umati wa watu walikuja kuangalia michoro hii. Hakuna aliyeshindwa kupata ujumbe uliokuwamo kwenye michoro. Kukawa na ghasia kubwa Prague, na wale wageni wakaona kuwa ilikuwa muhimu waondoke. Lakini picha hizi ziliweka mvuto mkali ndani ya Huss na kumuongoza kujifunza Biblia zaidi na pia maandishi ya Wycliffe.

[65] Ingawa alikuwa bado hajajiandaa kukubali matengenezo yote yaliyopiganiwa na Wycliffe, aliona tabia ya kweli ya utawala wa

Papa, na akashutumu kiburi, tamaa ya makuu na upotovu wa mamlaka ya Papa.

## Prague Yawekwa Kwenye Katazo

Habari zilipelekwa Roma, na Huss aliitwa ili asimame mbele za Papa. Kutii kungepelekea yeye kuuawa bila ya shaka. Mfalme na malkia wa Bohemia, Chuo Kikuu, waungwana, na maofisa wa serikali, waliungana katika mwito kwa Askofu Mkuu wa Roma kwamba Huss aruhusiwe kubaki Prague na kujibu kwa njia ya mjumbe. Badala yake, Papa aliendelea na kesi na kumhukumu Huss, kisha akautangaza mji wa Prague kuwa chini ya katazo.

Wakati huu, hukumu hii ilisababisha mshtuko. Watu walimwangalia Papa kama mwakilishi wa Mungu, akishikilia funguo za mbinguni na kuzimu na akiwa na uwezo wa kuhukumu. Watu waliamini kuwa wafu walifungiwa nje ya makao ya amani hadi Papa alipoondoa amri ya kuwazuia. Huduma zote za kidini zilisitishwa. Makanisa yalifungwa. Huduma za ndoa zilifanyikia kwenye viwanja vya makanisa. Wafu walizikwa bila huduma kwenye mitaro au mashamba.

Mji wa Prague ulijazwa na makelele. Kundi kubwa la watu lilimshutumu Huss na kudai apelekwe Roma. Ili kuituliza dhoruba, Mwanamatengenezo alijiondoa kwa muda na kwenda kijijini kwake alikozaliwa. Hakukoma kufanya kazi zake, lakini alisafiri ndani ya nchi akihubiri kwa makundi yaliyokuwa na shauku. Wakati msisimko wa Prague ulipopoa, Huss alirejea na kuendelea kuhubiri Neno la Mungu. Adui zake walikuwa na nguvu, lakini malkia na waungwana wengine wengi walikuwa rafiki zake, na idadi kubwa ya watu ilipelekana naye.

Huss alikuwa amesimama mwenyewe katika kazi zake. Sasa Jerome alijiunga katika matengenezo. Hawa wawili waliungana katika maisha yao baada ya hapa, na katika kifo hawangetenganishwa. Katika zile sifa ambazo hufanya nguvu ya kweli ya tabia, Huss alikuwa mkuu zaidi. Jerome, akiwa na unyenyekevu wa kweli, alielewa thamani yake na kukubali mashauri yake. Wakiwa katika kutenda kazi pamoja matengenezo yaliendelea kwa haraka. Mungu aliruhusu nuru kuu kung'aa kwenye mawazo ya watu hawa wateule, akiwafunulia makosa mengi ya Kanisa la Roma, lakini hawakupokea [66]

nuru yote ambayo ilikuwa itolewe duniani. Mungu alikuwa akiwaongoza watu kutoka katika giza la Kanisa la Roma, na aliwaongoza, hatua kwa hatua, kadiri walivyoweza kuipokea. Kama ambavyo nuru ya jua la utosini iwezavyo kuwa kwa wale ambao wamekaa gizani kwa muda mrefu, mwanga wote ungesababisha wageukie mbali. Kwa sababu hiyo, aliifunua hatua kwa hatua, kwa kadiri ilivyoweza kupokelewa na watu.

Utengano kanisani uliendelea. Mapapa watatu walikuwa wakishindania ukuu. Ugomvi wao ulijaza vurugu katika Ukristo. Bila kuridhika na tabia ya kutupiana laana, kila mmoja alijitosa katika kununua silaha na kuwa na askari. Bila shaka ilikuwa ni lazima kuwa na fedha; ili kupata hivi, zawadi, ofisi na baraka za kanisa zilitolewa kwa kuuzwa. (Angalia Kiambatisho.)

Kwa ujasiri ambao ulikuwa ukiongezeka, Huss alitoa shutuma dhidi ya machukizo yaliyokuwa yakivumiliwa katika jina la dini. Watu walilikosoa Kanisa la Roma hadharani kwamba lilikuwa chanzo cha mateso yaliyokuwa yanaugubika Ukristo.

Kwa mara nyingine Prague ilionekana ikiwa katika ukingo wa pambano la damu. Kama ilivyokuwa wakati wa zama zilizopita, mtumishi wa Mungu alishtakiwa kama "mtaabishaji wa Israeli." 1 Fal. 18:17. Mji uliwekwa tena chini ya katazo, na Huss akatoka tena kwenda kwenye kijiji chake alikozaliwa. Alikuwa azungumze tena kwa watu wengi, kwa Wakristo wote, kabla ya kukabidhi uhai wake chini kama shahidi wa ukweli.

Baraza kuu liliitishwa ili kukutana pale Constance (Kusini Magharibi mwa Ujerumani), ambalo liliitishwa kutokana na matashi ya mfalme Sigismund na pia mmoja kati ya Mapapa watatu waliokuwa wakishindana, Yohana XXIII. Papa Yohana, ambaye tabia na sera zake visingeweza kufaa hata kuchunguzwa, hakuweza kudiriki kumpinga Sigismund. **(Angalia Kiambatisho.)**

Makusudi makuu ambayo yalikuwa yafikiwe ni kuponya utengano katika kanisa na kuung'oa "uzushi." Hawa Mapapa wawili waliopingana waliitwa kuhudhuria pamoja na John Huss. Mapapa waliwakilishwa na wajumbe wao. Papa Yohana alikuja akiwa na
[67] mashaka makubwa, akihofu kuhojiwa kwa ajili ya maovu ambayo yalikuwa yamedhalilisha taji, pamoja na uhalifu uliotumika kuitunza. Hata hivyo aliingia mjini Constance kwa fahari kubwa, akisindikizwa na msafara wa watumishi wa mahakama. Juu ya kichwa chake

kulikuwa na mfuniko wa dhahabu, uliobebwa na mahakimu wakuu wanne. Mkate wa Bwana ulikuwa umebebwa mbele yake, na mavazi ya kitajiri ya makadinali na waungwana yalifanya mwonekano uwe wa kuvutia.

Wakati huo huo msafiri mwingine alikuwa anakaribia Constance. Huss aliachana na marafiki zake kana kwamba asingeonana nao tena, akihisi kuwa safari yake ilikuwa iishie kwenye kuchomwa moto. Alikuwa amepewa hati ya usalama wakati wa kusafiri kutoka kwa mfalme wa Bohemia vile vile nyingine kutoka kwa Mfalme Sigismund. Lakini alifanya maandalizi yote katika mtazamo wa uwezekano wa kifo chake.

### Hati ya Usalama Kutoka kwa Mfalme

Katika barua aliyowaandikia rafiki zake alisema: "Ndugu zangu,...Ninaondoka nikiwa na hati ya usalama toka kwa mfalme ili nikakutane na maadui zangu walio wengi na ambao ni wanadamu tu....Yesu Kristo aliteseka kwa ajili ya wapendwa wake; kwa hiyo, kwa nini tushangae kwamba ametuachia mfano wake?... Kwa hiyo, wapendwa, kama kifo changu kitaongeza utukufu wake, ombeni ili kije upesi, na pia aniwezeshe kukabili majanga yangu yote nikiwa thabiti.... Hebu tumuombe Mungu...ili nisizuie hata chembe ya ukweli wa Injili, ili niwaachie ndugu zangu mfano ulio bora wa kufuata." [16]

Katika waraka mwingine, Huss alinena kwa unyenyekevu juu ya makosa yake mwenyewe, akijilaumu "kwa kujisikia fahari katika kuvalia mavazi ya kitajiri na kwa kupoteza saa nyingi kwenye shughuli za kipuuzi." Kisha aliongezea, "hebu utukufu wa Mungu na wokovu wa roho ujaze mawazo, na wala isiwe kuwa na vyeo na makazi. Jihadhari na upambaji wa nyumba yako kuliko roho yako: na zaidi ya vyote, wekeza ulivyo navyo katika majengo ya kiroho. Uwe mchaji wa Mungu na mnyenyekevu kwa maskini, na usitumie raslimali zako katika karamu." [17]

Kule Constance, Huss alipewa uhuru kamili. Zaidi ya hati ya usalama aliyopewa na mfalme, aliongezewa uhakika kwake binafsi wa ulinzi kutoka kwa Papa. Lakini, kwa namna iliyokuwa ya kuk- [68]

[16] Bonnechose, vol. l,pp. 147, 148.

[17] *lbid*.,pp. 148, 149.

iuka matamko haya yaliyorudiwa, Mwana matengenezo alikamatwa baada ya muda mfupi kutokana na amri ya Papa na makadinali na akatupwa kwenye gereza la ardhini lenye kuchukiza mno. Baadaye alihamishiwa kwenye ngome iliyokuwa ng'ambo ya mto Rhine na pale akatunzwa kama mfungwa. Muda si mrefu Papa naye alitiwa kwenye gereza hilo hilo. [18] Alikuwa ameonekana kuwa na hatia ya makosa mabaya sana, kando ya mauaji, kuuza vitu vilivyowekwa wakfu na uzinzi, "dhambi ambazo hazikustahili kutajwa." Hatimaye alinyang'anywa ile taji. Mapapa waliopingana pia waliondoshwa madarakani, na Papa mpya akachaguliwa.

Ingawa Papa mwenyewe alikuwa na hatia ya uhalifu mkubwa zaidi ya ule wa Huss kuwashtaki mapadre, bado baraza lile lile ambalo lilimuondoa Papa liliendelea na kummaliza Mwanamatengenezo. Kufungwa kwa Huss kuliamsha ghadhabu kubwa sana Bohemia. Mfalme, kwa kutotaka kukiuka hati ya usalama, alipinga mashitaka kufanyika dhidi yake. Lakini maadui wa Mwanamatengenezo walileta hoja za kuthibitisha kwamba "sharti imani isitunzwe na wazushi, wala watu wanaoshukiwa kuwa na uzushi, ingawa wamepewa hati za usalama toka kwa watawala na wafalme." [19]

Kudhoofishwa na ugonjwa-unyevunyevu uliokuwa kwenye gereza la ardhini ulileta homa ambayo ilikaribia kumaliza maisha yake-Hatimaye Huss aliletwa mbele ya baraza. Akiwa na mzigo wa minyororo iliyomfunga, alisimama mbele ya mfalme, ambaye nia yake njema ilikuwa imetumika katika kumlinda. Bila kutetereka alisimamia ukweli na kuonesha upinzani mzito dhidi ya upotovu wa mamlaka ya Kanisa la Roma. Alipohitajika kuchagua kati ya kukana mafundisho yake au kuuawa, alikubali kifo cha ufia dini.

Neema ya Mungu ilimdumisha. Katika majuma ya kuteseka kabla ya kauli yake ya mwisho, amani ya mbinguni iliujaza moyo wake.

[69] "Ninaandika barua hii," alimwambia rafiki yake, "nikiwa gerezani kwangu, na mikono yangu ikiwa imefungwa, nikitegemea hukumu yangu ya kifo kesho.... Wakati ambapo, nikisaidiwa na Yesu Kristo, tutakutana tena kwenye amani iliyo tamu ya maisha yajayo, utajifunza jinsi ambavyo Mungu mwenye rehema amejione-

[18] *Ibid*, p. 247.

[19] Jacques Lenfant, *History of the Council of Constance*, vol. 1, p 516.

sha kwangu mimi, jinsi ambavyo amenisaidia wakati wa maonjo na majaribu yangu." [20]

### Ushindi Waonekana Mapema

Ndani ya gereza lake shimoni, aliuona mbeleni ushindi wa imani ya kweli. Katika njozi zake alimuona Papa na maaskofu wakifutilia mbali picha za Kristo alizokuwa amezichora kwenye kuta za kanisa dogo pale Prague. "Njozi ilimnyima raha : lakini siku iliyofuata aliona wachoraji wengi wakishughulika katika kurejesha picha hizi kwa wingi zaidi na katika rangi zilizong'aa zaidi...Wachoraji, ...wakiwa wamezingirwa na umati mkubwa, walisema kwa uchungu, 'Sasa acha Mapapa na maaskofu waje; hawataweza kuzifuta zaidi!'" Mwanamatengenezo akasema, "Sura ya Kristo haitafutwa kamwe. Wametamani kuiharibu, lakini itachorwa upya kwenye mioyo yote kupitia kwa wahubiri wazuri kuliko mimi." [21]

Kwa mara ya mwisho, Huss aliletwa mbele ya baraza, kusanyiko kubwa la watu wenye akili-wafalme, watoto wa kifalme, wasaidizi wa mfalme, makadinali, maaskofu, mapadre, na umati mkubwa wa watu.

Alipoulizwa atoe uamuzi wake wa mwisho, Huss alitamka kuwa asingekana msimamo wake. Huku akimkazia macho mfalme ambaye neno lake zito lilikuwa limekiukwa bila aibu, alisema, "Niliazimu, kwa kupenda kwangu mwenyewe, kusimama mbele ya baraza hili, nikiwa katika ulinzi wa umma na nia njema ya mfalme aliyeko hapa." [22] Msisimko wa hisia kali ulionekana usoni mwa Sigismund wakati macho ya wote yalipomwelekea.

Hukumu ilipotangazwa, utaratibu dhalili ulianza. Kwa mara [70]
nyingine akaitwa kufuta kauli yake, Huss akajibu, akigeukia watu: "Niitazame mbingu nikiwa na uso gani? Nitazameje ule umati wa watu ambao kwao nimehubiri Injili iliyo safi? La; ninaheshimu wokovu wao kuliko mwili huu dhaifu, ambao sasa unaelekezwa kwa mauti." Mavazi ya upadre yaliondolewa moja baada ya jingine, kila askofu akitamka Iaana alipokuwa akifanya sehemu yake ya sherehe hii. Hatimaye, "walimwekea kichwani kofia ya kiaskofu ya karatasi

[20]Bonnechose, vol 2, p. 67
[21]D'Aubigne, bk. l,ch. 6.
[22]Bonnechose, vol 2, p. 84.

iliyoundwa mfano wa piramidi, ambayo ilikuwa imechorwa picha za kutisha za maShetani, na kuandikwa maneno yaliyoonekana vizuri mbele ya kofla 'Mzushi Mkuu' . Huss akasema, 'Kwa furaha sana, nitaivaa hii taji ya aibu kwa ajili yako, Ee Yesu, ambaye kwa ajili yangu uliivaa taji ya miiba.' " [23]

## Huss Afa kwa Kuchomwa Moto

Aliongozwa sasa kutoka pale alipokuwa. Msafara mkubwa ulifuata. Wakati kila kitu kilipokuwa tayari kwa ajili ya moto kuwashwa, mfia dini huyu alishawishiwa kujiokoa mwenyewe kwa kukana makosa yake. "Makosa gani," alihoji Huss, "nikane? Ninajua sina hatia ya hata moja. Ninamuita Mungu kushuhudia kwamba yote niliyoandika na kuhubiri yamekusudiwa kuokoa roho toka dhambini na upotevuni; kwa hiyo, kwa furaha sana nitathibitisha kwa damu yangu ukweli huo ambao nimeuandika na kuuhubiri." [24]

Wakati miali ya moto ilipowaka kumzunguka, alianza kuimba, "Yesu, wewe Mwana wa Daudi, unirehemu mimi," na aliendelea hivyo hadi sauti yake iliponyamazishwa milele. Mkereketwa wa mamlaka ya Papa, akielezea ufia dini wa Huss na Jerome, ambaye alikufa muda mfupi tu baadaye, alisema: "Walijiandaa kwa ajili ya moto kana kwamba walikuwa wakienda kwenye sherehe ya harusi. Hawakutoa kilio chochote cha maumivu. Wakati miali ilipopanda, walianza kuimba nyimbo; na ilikuwa shida kwa ukali wa moto kukomesha kuimba kwao." [25]

[71] Baada ya mwili wa Huss kuteketezwa na moto, majivu yake yalikusanywa na kutupwa kwenye mto Rhine, na hapo yakapelekwa na maji hadi baharini na kuwa mbegu iliyosambazwa kwenye nchi zote za dunia. Katika nchi ambazo hazikufahamika bado, ingezaa matunda kwa wingi kwa njia ya shuhuda za ukweli. Sauti katika ukumbi wa baraza la Constance iliamsha miangwi ambayo imekuwa ikisikika katika kame zote zilizofuata. Mfano wake ungewatia moyo watu wengi kuweza kusimama imara wanapokabili mateso na mauti. Kuuawa kwake kulidhihirisha kwa ulimwengu ukatili wa kilaghai

[23] Wylie, bk. 3, ch. 7.
[24] *Ibid.*
[25] *Ibid.*

wa Kanisa la Roma. Maadui wa ukweli walikuwa wakiiendeleza kazi ambayo walifikiri waniuangamiza!

Bado damu ya shahidi mwingine ilikuwa lazima ishuhudie ukweli. Jerome alikuwa amemtia moyo Huss kuwa na ujasiri na uthabiti, akimwahidi kwamba kama angeingia kwenye hatari, angemkia pale ili kumsaidia. Aliposikia juu ya kufungwa kwa Mwanamatengenezo, mwanafunzi huyu mwaminifu alijiandaa kukamilisha ahadi yake. Bila ya hati ya usalama alielekea Constance. Alipofika, alishawishika kuwa alikuwa amejiweka hatarini mwenyewe bila kuweza kufanya lolote kwa ajili ya Huss. Alianza kukimbia lakini alikamatwa na kuletwa akiwa amefungwa kwenye minyororo. Aliposimama kwa mara ya kwanza mbele za baraza, alipojaribu kujibu alikutana na kelele, "Achomwe naye!" [26] Alitupwa kwenye gereza ardhini ambapo alilishwa mkate na maji. Ukatili wa gerezani ulipelekea kuugua kwake hadi kutishia uhai wake; na maadui zake, wakihofu kwamba angewatoroka, wali

## Jerome Ajisalimisha kvva Baraza

Kukiukwa kwa hati ya usalama ya Huss kulikuwa kumeibua dhomba ya ghadhabu. Baraza lilikusudia, badala ya kumchoma Jerome, limlazimishe afute kauli zake. Alipewa nafasi ya kuchagua kati ya kukana mafundisho yake au kufa kwa kuchomwa moto. Huku akiwa amedhoofishwa na ugonjwa, taabu za gerezani na mateso na fadhaa na mashaka, kutenganishwa na marafiki na kuumizwa na kifo cha Huss, ustahimilivu wa Jerome ulikwisha. Alikiri mwenyewe kufuata imani ya Kanisa la Roma na akakubali kauli ya baraza ya kumshutumu Wycliffe na Huss, isipokuwa, "ukweli mtakatifu" [27] walioufundisha.

Lakini katika upweke gerezani mwake aliona dhahiri kile ali- [72]
chokuwa amekifanya. Alifikiri juu ya ujasiri na uaminifu wa Huss kisha akatafakari juu ya jinsi yeye mwenyewe alivyokana ukweli. Alifikiri juu ya Bwana wa mbinguni ambaye kwa ajili yake alivumilia msalaba. Kabla hajarudi nyuma alikuwa amepata amani kati ya mateso katika uhakika wa upendeleo wa Mungu, lakini sasa, majuto na wasiwasi vilitesa roho yake. Alijua kuwa alitakiwa kufuta kauli

[26] Bonnechose, vol. 2, p. 168.
[27] *Ibid.*, ch. 19

nyingine kabla ya kupatana kikamilifu na Roma. Njia aliyokuwa akiingia ingeishia tu katika uasi kamili.

### Jerome Apata Toba na Ujasiri Mpya

Mara baada ya hapo alileletwa tena mbele ya baraza. Kujisalimisha kwake hakukuwaridhisha waamuzi. Ni kwa kuikana imani kikamilifu peke yake ambako kungeokoa uhai wake. Lakini alikuwa ameazimu kuitetea imani yake na kumfuata hadi kwenye moto ndugu yake aliyeifia dini.

Aliikataa ile kauli yake ya kwanza ya kuacha mafundisho na, kama mtu anayekufa, alihitaji kwa heshima nafasi ya kuwasilisha utetezi wake. Maaskofu walisisitiza kwamba ilimpasa tu akubali au akatae madai yaliyoletwa dhidi yake. Jerome alipinga dhuluma hiyo ya kikatili. "Mmenifungia siku mia tatu na arobaini ndani ya gereza la kutisha," alisema; "kisha mnanileta hapa mbele zenu, tena mkisikiliza adui zangu walio wanadamu tu, mnakataa kunisikiliza...Angalieni msitende dhambi dhidi ya haki. Mimi nilivyo, ni mwanadamu dhaifu; uhai wangu hauna umuhimu sana; na ninapowasihi msitoe hukumu isivyo haki, ninazungumza zaidi kuhusu ninyi kuliko mimi." [28]

Hatimaye, ombi lake lilikubaliwa. Mbele ya waamuzi wake, Jerome alipiga magoti na kuomba ili Roho wa Mungu atawale mawazo yake, ili kile alichotakiwa kunena kisiwe kinyume na ukweli kwa namna yoyote au kisichofaa kwa Bwana wake. Kwake yeye, ahadi hii ilitimia siku ile,

[73] "Lakini hapo watakapowapeleka, msifikiri-fikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakayosema. Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu." Mt. 10:19,20.

Kwa mwaka mzima Jerome alikuwa amekaa ndani ya gereza lililo ardhini asiweze kusoma wala kuona. Licha ya hivyo, hoja zake ziliwasilishwa kwa uwazi na kwa nguvu kana kwamba alikuwa na nafasi ya kujifunza bila usumbufu. Aliwaelekeza wasikilizaji wake kwa orodha ndefu ya watakatifu waliohukumiwa na waamuzi ambao hawakufuata haki. Karibu kila kizazi wale waliotafuta namna ya kuwainua watu wa wakati wao walitupiliwa nje. Kristo mwenyewe

[28] *Ibid.*, pp 146, 147.

alihukumiwa kama mhalifu kwenye mahakama ambayo haikuwa na haki.

Sasa Jerome alitangaza toba yake na kushuhudia juu ya kutokuwa na hatia na utakatifu wa mfia dini Huss. "Nilimjua tangu utoto wake," alisema. "Alikuwa mtu mzuri sana, mwenye haki na mtakatifu; alihukumiwa, bila kujali kutokuwa na hatia kwake...Nipo tayari kufa. Sitarudi nyuma ninapokuwa mbele ya mateso ambayo yameandaliwa na adui zangu na mashahidi wa uongo kwa ajili yangu, hawa ambao siku moja watawajibika kutoa taarifa ya ulaghai wao mbele za Mungu mkuu, ambaye hakuna awezaye kumdanganya."

Jerome aliendelea: "Katika dhambi zote ambazo nimewahi kutenda tangu ujana wangu, hakuna hata moja iliyo na uzito mkubwa mawazoni mwangu, na kunisababishia majuto makali, kama ile niliyotenda mahali hapa pa kufisha, wakati nilipokubali hukumu ile dhalimu iliyotolewa dhidi ya Wycliffe, na dhidi ya mfia dini mtakatifu, John Huss, bwana wangu na rafiki yangu. Ndiyo! Ninaikiri kutoka moyoni mwangu, na ninatamka nikiwa nimechukizwa kwamba nilinywea bila heshima, wakati ambapo kwa sababu ya hofu ya kifo, nilishutumu mafundisho yao. Kwa hiyo ninasihi... Mungu Mwenyezi akubali kusamehe dhambi zangu, na hususan hii, ambayo ni mbaya kuliko zote."

Akielekeza kwa waamuzi, alisema kwa uthabiti, "Uliwahukumu Wycliffe na John Huss...Mambo ambayo wameyasimamia, ambayo hayafai kupingwa, ninayafikiria na ninatamka, kuwa ninayapenda." Maneno yake yalikatishwa. Maaskofu huku wakitetemeka kwa hasira, walipiga kelele: "Je, kuna hitaji gani la uthibitisho zaidi? Tunashuhudia hapa kwa macho yetu mzushi mwenye ukaidi kuliko wote!"

Bila kutishwa na dhoruba, Jerome alisema kwa sauti: "Nini! Je, [74]
mnadhani ninaogopa kufa? Mmeniweka kwa mwaka mzima kwenye gereza la kutisha sana, zaidi ya mauti yenyewe.. .Siwezi kujizuia kueleza mshangao wangu kutokana na ukatili mkubwa kiasi hiki kwa Mkristo." [29]

[29]Bonnechose, vol. 2, pp. 151,153.

## Kuamriwa Kwenda Gerezani na Kufa

Kwa mara nyingine dhoruba ya hasira ilifumuka, na Jerome alipelekwa haraka gerezani. Hata hivyo wapo ambao kwao maneno yake yalikuwa yameweka mguso wa ndani sana na walitamani kuokoa maisha yake. Alitembelewa na waheshimiwa na wakamsihi ajisalimishe kwa baraza. Ahadi za kupendeza zilitajwa kwake kama zawadi.

"Nihakikishieni kutoka kwenye Maandiko Matakatifu kama nimekosea," alisema, "nami nitakana mafundisho haya."

"Maandiko Matakatifu!" mmoja wa waliomjaribu alisema kwa sauti, "inapasa tufanye kila kitu kulingana na hayo? Ni nani awezaye kuyaelewa basi hadi kanisa limeyafasiri?"

Jerome akamjibu: "Je, mapokeo ya wanadamu ni ya thamani katika imani kuliko Injili ya Mwokozi wetu?"

"Mzushi!" ndilo lililokuwa jibu la mmoja wao, "Ninajuta kwa kubembelezana nawe kwa muda mrefu kiasi hiki. Ninaona umetiwa moyo na mwovu." [30]

Baada ya muda mfupi, alipelekwa hadi mahali pale pale ambapo Huss alitoa uhai wake. Alikwenda akiimba njiani, uso wake uking'azwa kwa furaha na amani. Kwake yeye mauti imepoteza utisho wake. Wakati mnyongaji alipokuwa tayari kuuwasha moto, alipokaribia nyuma yake, mfia dini alisema kwa sauti, "Weka moto usoni mwangu. Ningekuwa na hofu, nisingekuwa hapa."

Maneno yake ya mwisho yalikuwa sala: "Bwana, Baba Mwenyezi, nihurumie, unisamehe dhambi zangu; kwani wewe unajua kuwa daima nimeupenda ukweli wako." [31] Majivu ya mfia dini yalikusanywa, na kama yalivyokuwa yale ya Huss, yalitupwa kwenye mto Rhine. Hivyo ndivyo walivyokufa wajumbe wa Mungu waaminifu walioibeba nuru.

[75] Kuuawa kwa Huss kulikuwa kumeibua moto wa ghadhabu na utisho katika Bohemia. Taifa zima lilikuwa limemtangaza kuwa mwalimu mwaminifu wa ukweli. Baraza likashitakiwa kwa kuua. Mafundisho yake yakaweka mvuto mkubwa kuliko wakati uliopita, na wengi wakaongozwa kukubali imani ya matengenezo. Papa

[30] Wylie, bk. 3, ch. 10.

[31] Bonnechose, vol. 2, p. 168.

na mfalme waliungana ili kulizima vuguvugu hili, na majeshi ya Sigismund yakamwagwa Bohemia.

Lakini mkombozi aliinuliwa. Ziska, mmoja kati ya majenerali waliokuwa na uwezo sana wa wakati wake, alikuwa ndiye kiongozi watu wa Bohemia. Akitegemea msaada wa Mungu, watu wale waliweza kupambana dhidi ya jeshi lililokuwa na nguvu sana kuliko yote ambayo yangewakabili. Kwa kurudia rudia, mfalme aliivamia Bohemia, na akaishia kurudishwa nyuma. Wafuasi wa Huss waliinuliwa juu ya hofu ya mauti, na hakuna ambacho kingewapinga. Shujaa Ziska alikufa, lakini mahali pake pakachukuliwa na Procopius, kwa namna fulani akiwa kiongozi mwenye uwezo zaidi.

Papa akatangaza mashambulio dhidi ya wafuasi wa Huss. Nguvu kubwa kuliko kawaida ilipelekwa kwa haraka Bohemia, na bado walishindwa vibaya. Shambulio lingine lilitangazwa. Katika nchi zote zilizokuwa kwenye mamlaka ya Papa kule Ulaya; watu, fedha na silaha za vita vilikusanywa. Umati wa watu ulijiunga na bendera ya Papa.

Nguvu kubwa sana ya kijeshi iliingia Bohemia. Watu walikusanyika ili kuwarudisha nyuma. Majeshi mawili yalikaribiana hadi ikawa ni mto tu ulioyatenganisha. "Washambuliaji walikuwa na jeshi kubwa na bora zaidi, lakini badala ya kuvuka mto, ili kukamilisha pambano dhidi ya wafuasi wa Huss, ambao walikuwa wamekuja mwendo wote huo ili kupambana nao, walisimama kimya wakiwaangalia wale mashujaa." [32]

Ghafla, jambo kubwa la kutisha lililiangukia jeshi. Bila hata ya pigo moja, jeshi lile kubwa lilivunjika na kutawanyika kana kwamba lilitawanywa na nguvu isiyoonekana. Jeshi la wafuasi [76]
wa Huss liliwakimbiza hawa waliokuwa wakitoroka, na vitu vingi vilivyotekwa vikakamatwa na washindi. Kwa hiyo vita, badala ya kuwafanya Wabohemia kuwa fukara, viliwatajirisha.

Miaka michache baadaye, chini ya Papa mpya, shambulio lingine liliandaliwa. Jeshi kubwa likaingia Bohemia. Majeshi ya wafuasi wa Huss yalirudi nyuma mbele yao, hivyo, wavamizi wakaingia ndani zaidi katika nchi, jambo lililowafanya wafikiri wamekwisha kushinda.

[32] Wylie, bk 3, ch. 17.

Hatimaye, jeshi la Procopius lilisonga mbele ili kupambana nao. Sauti ya jeshi lililokaribia iliposikika, hata kabla wafuasi wa Huss hawajaonekana, hofu iliwajaza wavamizi tena. Wana wa kifalme, majenerali, na askari wa kawaida, huku wakizitupa silaha zao, walikimbia na kutawanyika pande zote. Ushindi ulikuwa kamili, na kwa mara nyingine tena nyara nyingi sana zikaingia mikononi mwa washindi.

Kwa namna hiyo, kwa mara ya pili jeshi ia watu wa vita, waliofundishwa kwa ajili ya mapambano, walikimbia bila ya kupigwa mbele za walinzi wa taifa dogo dhaifu. Wavamizi walipigwa kwa utisho wa yeye aliye na nguvu isiyo ya kibinadamu. Yeye aliyewakimbiza majeshi ya Wamidiani mbele za Gideoni na watu wake mia tatu, alikuwa amenyoosha tena mkono wake. Angalia Amu. 7:19-25; Zab.53:5.

## Kusalitiwa na Diplomasia

Hatimaye viongozi katika mamlaka ya Papa walibadilisha mbinu na kutumia njia za kidiplomasia. Mwafaka ukafikiwa ambao uliwasaliti watu wa Bohemia wakaingia katika mamlaka ya Kanisa la Roma. Watu wa Bohemia waliweka mambo manne bayana kama masharti ya kupatana na Kanisa la Roma:

(1) Uhuru katika kuhubiri Biblia

(2) Haki kwa ajili ya kanisa zima kushiriki mkate na divai kwenye meza ya Bwana na matumizi ya lugha ya asili katika ibada kuu;

(3) Kuondolewa kwa viongozi wa kanisa kutoka katika ofisi zote na mamlaka za kiulimwengu; na

(4) Katika mazingira ya uhalifu, mamlaka ya kisheria ya mahakama za jamii yawe juu ya wachungaji na walei pia. Mamlaka ya pPapa ilikubali kuwa mambo hayo manne yakubaliwe, "lakini haki ya kuyaeleza iwe kwenye baraza-kwa maneno mengine, kwa Papa na kwa mfalme." [33]

[77] Kanisa la Roma lilifanikiwa kwa njia ya unafiki na udanganyifu katika kile lilichoshindwa kukipata kwa njia ya vita. Kwa kuweka tafsiri zake yenyewe kwenye maandishi ya wafuasi wa Huss, kama

[33] *Ibid*.y ch. 18.

ilivyofanya kwenye Biblia, ingefanikiwa kupotosha maana ili kupelekana na makusudi yake.

Kundi kubwa Bohemia, lilipoona kuwa uhuru wao umesalitiwa, halikukubaliana na mkataba. Mafarakano yakaanza, yaliyosababisha ugomvi kati yao wenyewe. Muungwana Procopius alishindwa, na uhuru wa Bohemia ukaisha.

Kwa mara nyingine, majeshi ya kigeni yalivamia Bohemia, na wale waliobaki wakiwa waaminifu kwa Injili walitoswa kwenye mateso ya umwagaji damu. Pamoja na hayo, uthabiti wao haukutingishika. Huku wakiwa wamelazimika kukimbilia mapangoni, waliendelea kukusanyika kwa ajili ya kusoma Neno la Mungu na kuungana katika kumw abudu yeye. Kwa njia ya wajumbe waliotumwa kwa siri kwenda nchi mbalimbali walifahamu kuwa "kati ya milima ya Alps kulikuwa na kanisa la kale, ambalo limejengwa katika misingi ya Maandiko, na kupinga upotovu wa Roma wa kuabudu miungu." [34] Kwa furaha kuu, mawasiliano na Wakristo Wawaldensia yalianzishwa.

Wakiwa thabiti katika Injili, watu wa Bohemia walisubiri katika usiku wa mateso yao, katika wakati wa giza nene wakiendelea kukaza macho yao yaone upeo wake kama watu wanaoingoja asubuhi.

[34] *Ibid.*, ch. 19

[78]

# Sura Ya 7 - Luther, Mwanamume Kwa Wakati Wake

Mtu wa kwanza miongoni mwa wale walioitwa kuliongoza kanisa litoke kwenye giza la utawala wa Papa liingie kwenye nuru safi ya imani alikuwa Martin Luther. Hakuwa na hofu na chochote isipokuwa kicho kwa Mungu. Hakutambua msingi mwingine wa imani isipokuwa Maandiko Matakatifu. Luther alikuwa ni mwanamume wa enzi zake.

Luther alitumia miaka yake ya awali katika nyumba duni ya mkulima wa Kijerumani. Baba yake alikuwa amedhamiria Luther awe mwanasheria, lakini Mungu alikuwa amekusudia kumfanya mjenzi wa hekalu lililokuwa linainuka taratibu kwa kame nyingi. Taabu, upweke, na adhabu kali ilikuwa ni shule iliyotumiwa na Mungu kumwandaa Luther kwa ajili ya Utume maishani mwake.

Baba yake Luther alikuwa mtu mwenye akili ya utendaji. Hisia zake bora zilimwongoza kuutilia mashaka mfumo wa maisha ya kitawa. Hakufurahishwa na Luther ambaye, bila idhini yake alikuwa ameingia katika nyumba ya watawa. Ilipita miaka miwili kabla baba hajafanya mapatano na kijana wake, na baada ya hapo nia yake haikubadilika.

Wazazi wa Luther walijitahidi kumfundisha mtoto wao katika kumjua Mungu. Jitihada zao zilikuwa za dhati na za kudumu kuwaandaa watoto wao kwa maisha yenye manufaa. Wakati fulani walifanya kwa ukali sana, lakini Mwanamatengenezo huyu alipata mafundisho zaidi katika adhabu zao kuliko shutuma.

Shuleni, Luther alikuwa anatendewa kwa ukali na hata kwa ukatili. Wakati mwingi aliteseka kwa njaa. Mawazo ya dini yaliyojengwa kwenye huzuni na mapokeo potuvu yaliyokuwepo nyakati hizo yalimjaza kwa hofu. Angeweza kulala usiku akiwa na moyo wa huzuni, na hofu ya kudumu alipomwazia Mungu kuwa ni katili na dhalimu, badala ya Baba mwema wa mbinguni.

Alipoingia katika Chuo Kikuu cha Erfurt, matarajio yake yaling'aa zaidi kuliko ilivyokuwa kwenye miaka ya awali. Wazazi

wake, kwa kujibana na kazi nyingi waliweza kumtimizia mahitaji yote yaliyokuwa yanatakiwa. Na marafiki waliokuwa waangalifu [79] kwake walipunguza madhara ya huzuni katika mafunzo yake ya awali. Kwa njia ya mivuto inayofaa, akili yake ilikua kwa haraka. Kutumika kwake bila kuchoka, mapema, kulimweka nafasi ya juu miongoni mwa rafiki zake.

Luther hakuacha kuianza siku kwa sala, moyo wake ulidumu katika maombi kwa ajili ya uongozi wa Mungu. Mara nyingi alisema, "Kuomba vema ni nusu ya kujifunza vizuri" [35]

Siku moja aligundua Biblia kwenye maktaba ya Chuo Kikuu, kitabu ambacho hakuwahi kukiona. Aliwahi kusikia sehemu tu za Injili na Nyaraka, ambazo alidhani kuwa ndiyo Biblia nzima. Sasa, kwa mara ya kwanza, aliliangalia Neno zima la Mungu. Kwa kicho na mshangao alizifungua kurasa takatifu na kuyasoma mwenyewe maneno ya uzima, akipumzika na kuonesha mshangao, "Oo kwamba Mungu angenipa kitabu kama hiki kwa ajili yangu!" [36] Malaika walikuwa kando yake. Miali ya nuru kutoka mbinguni ilifunua hazina za ukweli kwenye ufahamu wake. Hatia ya kina juu ya hali yake kama mwenye dhambi ilimshika kuliko wakati mwingine kabla.

### Kuitafuta Amani

Shauku ya kutafuta amani kati yake na Mungu ilikuwa inamwongoza kujitoa mwenyewe kuishi maisha ya kitawa. Hapa alikuwa anatakiwa kufanya kazi duni za kuchosha na kuombaomba nyumba kwa nyumba. Kwa ustahimilivu alivumilia hali hiyo duni, akiamini kuwa ilikuwa ni lazima kufanya hivyo kwa sababu ya dhambi zake.

Alikuwa anajinyima usingizi na kuwa na chuki hata wakati wa milo yake iliyokuwa haitoshi, ili afurahie kujifunza Neno la Mungu. Aliiona Biblia imefungwa kwa minyororo kwenye ukuta wa nyumba ya watawa, na hili alilisema mara kwa mara.

Alikuwa anaishi maisha magumu sana, akijitahidi kwa kufunga, kukosa usingizi, na kujitesa ili kudhibiti uovu wake. Baadaye alisema, "Ikiwa mtawa ataingia mbinguni kwa njia ya kazi zake [80] za kitawa, kwa hakika ningestahili nafasi hiyo...kama ningeendelea

[35] D'Aubigne, bk. 2, ch. 2.

[36] *Ibid*

kwa muda mrefu zaidi, ningeweza kuudhalilisha mwili wangu hadi mauti.” [37] Pamoja na jitihada hizo zote, roho yake iliyokuwa imeelemewa haikupata ahueni. Hatimaye alifika kwenye ukingo wa kukata tamaa.

Ilipoonekana kwamba kila kitu kilikuwa kimepotea, Mungu akamwinua rafiki kwa ajili yake. Staupitz alilifungua Neno la Mungu kwenye akili ya Luther na kumtaka asiiangalie nafsi bali amwangalie Yesu. “Badala ya kujitesa mwenyewe kwa ajili ya dhambi zako, jitupe kwenye mikono ya Mwokozi. Mwamini, iamini haki iliyo katika maisha yake, katika upatanisho wa kifo chake...Mwana wa Mungu...alifanyika mwanadamu ili akupatie uhakika wa kibali cha Mungu...mpende ambaye alikupenda kwanza.” [38] Maneno yake yalileta mvuto wa kina ndani ya moyo wa Luther. Amani ikaja ndani ya nafsi iliyokuwa inataabika.

Baada ya kuwekewa mikono ya upadre, Luther aliitwa kuwa mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Wittenberg. Alianza kutoa mihadhara juu ya Zaburi, Injili, na Nyaraka kwenye makundi ya wasikilizaji wenye furaha. Staupitz, mkubwa wake, alimtaka apande mimbarani kuhubiri. Lakini Luther alikuwa anajihisi kutostahili kuzungumza na watu kwa niaba ya Kristo. Ilikuwa baada ya masumbuko ya muda mrefu na rafiki zake wakimsihi, ndipo alipokubali. Alikuwa na nguvu katika Maandiko, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake. Usahihi na uwezo aliotumia kuuwasilisha ukweli, vilishawishi ufahamu wao na hamasa yake iliigusa mioyo yao.

Akiwa bado mwana wa kweli wa Kanisa la Papa, Luther hakuwa na wazo kwamba angekuwa mtu tofauti. Alipoongozwa kwenda Roma, aliishika njia kwa safari ya miguu, alikuwa analala kwenye nyumba za watawa njiani. Alistaajabia uzuri na anasa alizozishuhudia. Watawa walikuwa wanaishi katika nyuumba nzuri za fahari, walikuwa wanavaa mavazi ya thamani kubwa, walikuwa wanafanya karamu zao kwenye meza za gharama kuu. Moyo wa Luther ulianza kupata mashaka.

[81] Hatimaye kwa mbali aliuona ule mji wa vilima saba. Alianguka kifudifudi hadi chini ya nchi, akistaajabu na kusema: “Roma Mtakatifu, Ninakusalimu!” [39] Aliyatembelea makanisa, akazisik-

[37]Ibid., ch. 3.
[38]Ibid., ch. 4.
[39] Ibid., bk. 2, ch.6.

iliza hadithi za kuvutia zilizorudiwa mara kwa mara na mapadre na watawa, na akatimiza zile ibada zilizokuwa zinatakiwa. Kila mahali, matukio yalimfanya kushangaa-uovu miongoni mwa mapadre, na utani usio na maana kutoka kwa maaskofu. Alitishwa na machafu hata kwenye ibada. Alikutana na ufujaji, mauaji. "Hakuna awezaye kufikiria," aliandika, "ni dhambi na matendo maovu ya namna gani yanayotendeka Roma...wamezoea kusema kuwa, 'kama kuna jehanamu, basi Roma imejengwa juu yake.'[40]

### Ukweli Kwenye Ngazi ya Pilato

Ahadi ya kibali cha msamaha wa dhambi ilikuwa imetolewa na Papa kwa wote ambao wangepanda kwa magoti yao "Ngazi ya Pilato" ambayo inasemekana kuwa ililetwa kwa muujiza kutoka Yerusalemu hadi Roma. Siku moja Luther alikuwa akipanda ngazi hizi wakati sauti kama ya radi iliposikika kana kwamba inasema: "Mwenye haki ataishi kwa imani." Warumi 1:17. Alisimama ghafla kwa miguu yake kwa aibu na hofii. Tangu wakati huo aliuona kwa usahihi zaidi uongo juu ya kuzitumainia kazi za mwanadamu kuupata wokovu. Aliugeuza uso wake kutoka Roma. Tangu wakati huo utengano uliendelea kukua hadi pale alipovunja uhusiano wote aliokuwa nao na kanisa la Papa.

Baada ya kurejea kutoka Roma, Luther alipata shahada ya uzamivu katika teolojia. Sasa alikuwa huru kujikita kwenye Maandiko aliyokuwa anayapenda. Aliapa kwa dhati kuwa angelihubiri Neno la Mungu kwa ujasiri, na siyo mafu"ndisho ya Mapapa. Hakuwa tu mtawa wa kawaida, bali mjumbe wa Biblia mwenye mamlaka aliyeitwa kama mchungaji kulilisha kundi la Mungu lililokuwa na njaa na kiu ya ukweli. Alitamka kwa ujasiri kwamba Wakristo hawakupaswa kuyapokea mafundisho mengine zaidi ya yale yatokayo kwenye mamlaka ya Maandiko Matakatifu.

Makundi ya watu wenye shauku waliyaelewa maneno yake. [82]
Habari za furaha juu ya upendo wa Mwokozi, uhakika wa msamaha na amani kupitia damu yake ya upatanisho zilileta furaha mioyoni mwao. Pale Wittenberg taa iliwashwa ambayo mionzi ya nuru yake ingeendelea kuongeza mng'ao wake hadi mwisho wa wakati.

[40]Ibid.

Lakini kuna ukinzani kati ya ukweli na uongo. Mwokozi wetu alitamka mwenyewe kuwa: "Sikuja kuleta amani, bali upanga." Mathayo 10:34. Miaka michache baada ya kuanza kwa Matengenezo, Luther alisema: "Mungu...ananisukuma kwenda mbele...ninatamani kuishi kwa utulivu; lakini nimetupwa katikati ya misukosuko na mapinduzi" [41]

### Mauzo ya Vyeti vya Msamaha wa Dhambi

Kanisa la Roma lilikuwa linaichuuza neema ya Mungu. Kwa kigezo cha kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa la Mtakatifu Petro la Roma, mamlaka ya Papa ilikuwa inatoza na kuviuza vibali vya msamaha wa dhambi. Hekalu kwa ajili ya kumwabudu Mungu, lilijengwa kwa mapato ya udhalimu. Lilikuwa ni jambo hili lililowaamsha maadui wa uPapa waliofanikiwa na lililoongoza kwenye mapambano yaliyoitikisa enzi ya Papa na taji tatu juu ya kichwa chake.

Afisa aliyeteuliwa kuuza vibali vya msamaha wa dhambi huko Ujerumani alikuwa anaitwa Tetzel. Ingawa alikuwa amethibitika juu ya uovu dhidi ya jamii na sheria ya Mungu; lakini aliajiriwa kuendeleza miradi yenye kumletea Papa fedha kutoka Ujerumani. Aliurudia-rudia uongo uliokuwa unang'aa na hadithi za kuvutia ili kuwadanganya watu wajinga na wenye mashaka. Endapo wangekuwa na Neno la Mungu, hawangedanganyika, lakini Biblia ilikuwa imezuiliwa wasiipate. [42]

[83] Alipokuwa anaingia kwenye mji fulani, Tetzel alitanguliwa na mjumbe aliyekuwa anatangaza kuwa: "Neema ya Mungu na ya baba mtakatifu, ipo malangoni mwenu." [43] Watu walikuwa wanampokea mwigizaji huyu mwenye kukufuru; kana kwamba alikuwa Mungu mwenyewe. Tetzel, alipopanda mimbarani ndani ya kanisa, alikuwa anakisifia kibali cha msamaha wa dhambi kama ndiyo karama ya Mungu yenye thamani zaidi kuliko nyingine zote. Alitangaza kwamba tokana na ubora wa vyeti vyake vya msamaha; dhambi zote ambazo mnunuzi alikuwa anatamani kuzitenda baa-

[41] Ibid., bk. 5, ch. 2.

[42] See John C. L. Giesler, A Compendium of Ecclesiastical History, per. 4, sec. 1, Par. 5.

[43] D'Aubigne, bk. 3, ch. 1.

daye, zingesamehewa na ” hata asingelazimika kufanya toba.” [44] Aliwahakikishia wasikilizaji wake kuwa vyeti vyake vilikuwa na uwezo wa kumwokoa mtu aliyekufa; wakati ule-ule pesa inapogonga sakafu ya kasha la fedha, ile roho ambayo kwayo fedha hizo zilikuwa zimelipwa, ingeokoka kutoka toharani na kwenda mbinguni. [45]

Dhahabu na fedha vilitiririka na kuingia ndani ya hazina ya Tetzel. Wokovu uliokuwa unanunuliwa kwa pesa ulikuwa unapatikana kwa urahisi zaidi ya ule uliokuwa unahitaji toba, imani, na jitihada za dhati kupingana na kuishinda dhambi. (Angalia Kiambatisho)

Luther alikuwa amejawa na hofu. Wengi miongoni mwa kusanyiko lake, walikuwa wamenunua vyeti vya msamaha. Mara walianza kuja kwa Mchungaji wao, wakiungama dhambi na kutarajia kupata tamko rasmi kuwa wamesamehewa, siyo kwa sababu walikuwa na toba na walikuwa wanataka kufanya matengenezo, bali kwa misingi ya vyeti vya msamaha. Luther aliwakatalia na kuwaonya kuwa wasingefanya toba na matengenezo, wangeangamia pamoja na dhambi zao. Walimfuata Tetzel wakimlalamikia kuwa aliyekuwa anatakiwa kuwasamehe dhambi alikuwa amevikataa vyeti vyake, na baadhi walidai kwa ujasiri kuwa fedha zao zirejeshwe. Akiwa amejawa na hasira, mtawa huyo, alitamka laana za ajabu, akasababisha mtafaruku katika viwanja vya hadhara na alitangaza kuwa, “Alikuwa amepokea agizo kutoka kwa Papa kuwachoma moto waasi wote waliotarajia kupinga vyeti vyake vitakatifu sana vya msamaha” [46]

## Kazi ya Luther Vaanza [84]

Sauti ya Luther ilisikika kutoka mimbarani ikiwa na onyo thabiti. Aliweka wazi mbele ya watu tabia ya hatia ya dhambi na alifundisha kuwa haiwezekani mwanadamu kupunguza hatia au kuepuka adhabu kwa matendo yake. Hakuna chochote kinachoweza kumwokoa mwenye dhambi isipokuwa toba kwa Mungu na imani kwa Kristo. Neema ya Kristo hainunuliwi; ni karama ya bure. Aliwashauri watu wasinunue vyeti vya msamaha, bali wamtafute kwa imani Mwokozi aliYesulubiwa. Aliwasimulia maumivu yake aliyokuwa ameyapitia

[44] Ibid

[45] See K. R. Hagenbach, History of the Reformation, vol. 1, p. 96.

[46] D’Aubigne, bk. 3, ch. 4.

na kuwahakikishia wasikilizaji wake kuwa kwa kumwamini Kristo alikuwa amepata amani na furaha.

Kadiri Tetzel alivyoendelea kutoa maagizo yake yasiyomheshimu Mungu na wanadamu, Luther aliamua kuleta upinzani wenye nguvu zaidi. Kanisa la Wittenberg lilikuwa linamiliki vitu vya kumbukumbu ambavyo katika baadhi ya siku takatifu vilioneshwa kwa watu. Msamaha kamili wa dhambi ulitolewa kwa wote waliofika kanisani na kufanya maungamo. Moja kati ya matukio muhimu sana, siku kuu ya Watakatifu Wote, ilikuwa inakaribia. Luther, akiungana na makundi ya watu ambao tayari walikuwa wakienda kanisani, alibandika kwenye mlango maoni tisini na matano (95) dhidi ya fundisho la vyeti vya msamaha.

Maoni yake yalileta mvuto mahali pote. Yalisomwa na kurudiwa kila upande. Kulitokea msisimko mkubwa katika mji mzima. Kwa Maandiko haya, ilioneshwa kwamba uwezo wa kutoa msamaha wa dhambi na kuondoa adhabu yake haukuwahi kutolewa kwa Papa au mwanadamu yeyote. Ilioneshwa kwa usahihi kuwa neema ya Mungu inatolewa bure kwa wote wanaoitafuta kwa toba na imani.

Maandiko ya Luther yalisambaa katika nchi yote ya Ujerumani na ndani ya majuma machache yalikuwa yanasikika katika Ulaya
[85] nzima. Washiriki wengi waaminifu wa Kanisa la Roma walikuwa wanayasoma maoni hayo kwa furaha, wakiitambua ndani yake sauti ya Mungu. Walihisi kuwa Bwana alikuwa ameweka mkono wake ili kulituliza wimbi la uovu lililoumuka kutoka Roma. Wakuu na mahakimu walifurahi mioyoni mwao kwani mamlaka yenye kiburi, iliyokuwa imekataa maoni katika maamuzi yake, ingedhibitiwa.

Walipoona kuwa mapato yao yalikuwa yanahatarishwa, mapadre werevu walighadhabika. Sasa Mwanamatengenezo huyu alikuwa anakabiliwa na washitaki wakali. Luther alijibu, "Ni nani asiyejua kuwa ni mara chache mtu huleta wazo jipya pasipo... kushitakiwa kwa kuchochea mafarakano?... Ni kwa nini Kristo na wafia-dini wote waliuawa? Kwa sababu... waliendeleza mambo mapya pasipo kunyenyekea na kupata mashauri ya mitazamo ya kale." [47]

Mbinu walizotumia maadui wa Luther, upotoshaji wa makusudi yake, na chuki waliyotumia kuelezea tabia yake, vilimjia kama mafuriko. Alipata ujasiri kuwa viongozi wangeungana naye kwa

[47] Ibid., ch. 6.

furaha kwenye matengenezo. Kwa subira aliiona siku yenye nuru ikipambazuka kwa ajili ya kanisa.

Lakini badala ya kutiwa moyo alipokea shutuma. Viongozi wengi wa kanisa na serikali mara moja waliona kuwa kuzikubali hizi kweli, ingekuwa ni kushusha mamlaka ya Kanisa la Roma, kufunga maelfu ya mito iliyokuwa inatiririka kuelekea kwenye hazina, na hivyo kukatisha anasa za viongozi wa utawala wa Papa. Kuwafundisha watu wamtazame Kristo pekee kwa ajili ya wokovu ingekuwa ni kuipindua enzi ya Mapapa na hatimaye kuyaangamiza mamlaka yao wenyewe. Kwa hiyo walijipanga wenyewe kinyume na Kristo na ukweli kwa kumpinga mtu aliyemtuma kuwapa nuru.

Luther alipojitazama mwenyewe alitetemeka - mtu mmoja anapingana na mamlaka zenye nguvu za dunia. Anaandika "Mimi nilikuwa nani kuupinga utukufu wa Papa, ambaye mbele zake...wafalme wa dunia na ulimwengu wote unatetemeka?... Hakuna mmoja awezaye kujua moyo wangu ulivyoteseka katika miaka hii miwili ya kwanza na ni katika huzuni kiasi gani, naweza [86]
kusema ni kukosa tumaini kwa namna gani, nilikuwa nimezama." [48] Lakini msaada wa wanadamu uliposhindwa, alimtazama Mungu peke yake. Angeweza kujiegesha kwa usalama kwenye ule mkono wenye nguvu.

Luther alimwandikia rafiki yake kuwa: "Jukumu lako ni kuanza kwa sala...usitumaini chochote kutokana na matendo yako, kutokana na ufahamu wako: mtumaini Mungu pekee, na katika mvuto wa Roho wake." [49] Hapa lipo somo la muhimu kwa wale wanaohisi kuwa Mungu aliwaita ili waupeleke kwa wengine ukweli muhimu wa wakati huu. Katika mapambano dhidi ya nguvu za uovu kunahitajika kitu fulani zaidi ya akili na hekima ya kibinadamu.

## Luther Alikata Rufaa kwenye Biblia Pekee

Wakati maadui walipotegemea mila na desturi, Luther alikutana nao akiwa na Biblia pekee, hoja ambazo hawakuweza kujibu. Kutoka katika hotuba na maandishi ya Luther ilikuwa inatoka mionzi ya nuru iliyowaamsha na kuwaangazia maelfu. Neno la Mungu lilikuwa kama upanga ukatao kuwili, likikata ndani ya mioyo ya watu. Ma-

[48] Ibid.

[49] Ibid., ch. 7.

cho ya watu ambayo kwa muda mrefu yalielekezwa kwenye ibada za wanadamu na wapatanishi wa kidunia, sasa, kwa imani, yalikuwa yakimgeukia Kristo na Yeye aliYesulubiwa.

Shauku hii iliyosambaa kote iliamsha hofu za mamlaka ya Papa. Luther alipokea hati ya kuitwa Roma. Rafiki zake waliijua wazi hatari iliyomkabili katika ule mji uliokuwa umeharibika, ambao tayari ulikuwa umelewa kwa damu ya wafia-dini wa Yesu. Waliomba kwamba afanyiwe mahojiano yake huko Ujerumani.

Hilo lilifanyika, na balozi wa Papa aliteuliwa ili kulisikiliza shauri hilo. Katika maelekezo yaliyotolewa kwa balozi huyo, ilitamkwa kuwa Luther, tayari alikuwa ametangazwa kuwa ni mwasi. Balozi alipaswa tu "kutoa hukumu na kuitekeleza bila kuchelewa." Balozi alipewa mamlaka ya "kumpiga marufuku katika kila sehemu
[87] ya Ujerumani; kuwakataza, kuwalaani, na kuwatenga wale wote waliokuwa wamefungamana naye," kuwatenga wote, wenye vyeo vyovyote kanisani au serikalini, isipokuwa mfalme, ambaye atapuuzia kumkamata Luther na wafuasi wake na kuwapeleka Roma wakaadhibiwe. [50]

Hakuna hata dalili ya kanuni za Kikristo au hata haki ya msingi zilizoonekana kwenye waraka huo. Luther hakupata fursa ya kujieleza au kuutetea msimamo wake; na bado alitangazwa kuwa ni mwasi na siku ile ile alisumbuliwa, akashitakiwa, akahukumiwa na kushutumiwa.

Luther alipohitaji ushauri wa rafiki wa kweli, Mungu alimtuma Melanchthon kwenda Wittenberg. Maamuzi ya hekima aliyokuwa nayo Melanchthon, yakijumuishwa na usafi na msimamo mzuri wa tabia, vilistaajabiwa mahali pote. Mara, akawa ni rafiki aliyetumainiwa zaidi na Luther-upole wake, tahadhari, na umakini vilikuwa msaada, na kumpa Luther nguvu na ujasiri.

Mji wa Augsburg ulitengwa kuwa eneo la kufanyia mashauri hayo na Mwanamatengenezo alisaflri kwa miguu. Vitisho vilitolewa kwamba angeuawa njiani, na rafiki zake walimwomba asijihatarishe. Lakini mzigo wake ulikuwa, "Mimi ni kama Yeremia, mtu wa migongano, na mashindano; lakini kadiri wanavyoongeza vitisho vyao, ndivyo furaha yangu inavyozidi...Tayari wameiharibu heshima yangu na sifa yangu...lakini roho yangu hawawezi kuiondoa. Yeyote

[50] Ibid., bk. 4, ch. 2.

mwenye shauku ya kulitangaza Neno la Mungu ulimwenguni, ni lazima atarajie kifo kila wakati.” [51]

Habari za kuwasili kwa Luther katika mji la Augsburg zilimfurahisha sana balozi wa Papa. Mwasi mwenye usumbufu aliyekuwa amevuta usikivu wa ulimwengu, sasa alionekana yupo chini ya mamlaka ya Kanisa la Roma; hangeweza kuponyoka. Balozi wa Papa alipanga kumlazimisha Luther ayakanushe mafundisho yake, au akishindwa kufanya hilo, kumsafirisha hadi Roma ili akayashiriki yale yaliyowapata Huss na Jarome. Kwa hiyo kwa njia ya mawakala wake alijitahidi kushawishi Luther asipewe ulinzi, akijiamini mwenyewe kwa rehema yake. Hilo Mwanamatengenezo alikataa kulifanya. Baada ya kupewa waraka wenye ahadi ya ulinzi kutoka kwa mfalme, alikwenda kukutana na balozi wa Papa.

Kwa ajili ya kufuata sera zao, watawala Kanisa la Roma, waliamua kumshinda Luther kwa mwonekano wa kiungwana. Balozi wa Papa alijifanya rafiki mkubwa wa Luther, lakini alikuwa anamhitaji ajisalimishe kikamilifu kwa kanisa na kukikubali kila kipengele pasipo hoja ama swali. Katika jibu lake, Luther, alieleza anavyoliheshimu kanisa, shauku yake ya kujua ukweli, utayari wake kuzijibu hoja zote juu ya kile alichokuwa amefundisha, na kuyasalimisha mafundisho yake kwenye vyuo vikuu maarufu ili yachunguzwe. Lakini alikataa matakwa ya yule Kadinali kumtaka ayafute maoni yake pasipo kuthibitishiwa makosa yake. [88]

Jibu pekee lilikuwa, “Futa, futa!” Mwanamatengenezo alionesha kwamba msimamo wake ulijengwa juu ya Maandiko. Hangeweza kukanusha ukweli. Balozi wa Papa hakuweza kujibu hoja za Luther, alimshambulia kwa dhoruba ya shutuma, kebehi, sifa za uongo, nukuu kutoka kwenye mapokeo, na misemo ya mababa, akamnyima Mwanamatengenezo fursa ya kuzungumza. Hatimaye Luther alipewa ruhusa, japo kwa kinyongo, kutoa jibu lake kwa njia ya maandishi.

Alimwandikia rafiki yake akisema, “Kitu kilichoandikwa kinaweza kupelekwa kwa wengine ili wakitolee uamuzi; pili, kuna uwezekano mkubwa kwa mtu mmoja kufanya kazi akiongozwa na hofu, kama siyo upande wa dhamiri, ya mtu mwenye majivuno na

[51] Ibid., ch. 4.

mdhalimu anayeropoka, ambaye, vinginevyo, anaweza kushinda kwa lugha yake ya kulazimisha.” [52]

Kwenye mahojiano yake yaliyofuata, Luther, alileta ufafanuzi wa maoni yake kwa usahihi, habari nyingi katika maelezo mafupi, na yenye nguvu, yakijengwa juu ya Maandiko Matakatifu. Baada ya kuyasoma yale maandishi kwa sauti, alimpa yule Kadinali, ambaye aliyatupa pembeni bila kujali, akisema kuwa ni lundo la maneno yasiyo na maana na nukuu zilizowekwa mahali pasipozofaa. Sasa Luther alikutana na balozi wa Papa mwenye kiburi kwenye uwanja wake-na kuzipindua kabisa dhana zake.

[89] Balozi alishindwa kujidhibiti na kwa ghadhabu alipiga kelele akisema, “Futa! vinginevyo nitakupeleka Roma.” Na hatimaye alitamka kwa sauti ya kiburi na hasira kwamba, “Futa, ama usirudi tena.” [53]

Mwanamatengenezo pamoja na rafiki zake waliondoka haraka, kwa namna hiyo alitangaza wazi kuwa hakutegemea kamwe kufuta maoni yake. Hii ilikuwa kinyume na makusudio ya Kadinali. Sasa, akiwa ameachwa yeye na waliokuwa wanamwunga mkono, akamtazama mmoja baada ya mwingine akiwa amekata tamaa baada ya kushindwa kwa mbinu zake kinyume na matarajio.

Kusanyiko kubwa lililokuwepo lilipata fursa ya kuwalinganisha hawa watu wawili na kuamua wenyewe juu ya roho walioionesha, na pia uwezo na ukweli wa misimamo yao. Mwanamatengenezo, ni wa kawaida, mnyenyekevu, jasiri, akiwa na ukweli upande wake; mwakilishi wa Papa, anajiona wa muhimu, mwenye kiburi, asiye na mantiki, asiye na hoja hata moja kutoka kwenye Maandiko, lakini kwa hasira alikuwa akipaza sauti yake, “Futa, ama upelekwe Roma.”

## Kutoroka Augsburg

Marafiki wa Luther walipendekeza kwamba kwa sababu hapakuwa na umuhimu kwake kubaki pale; angepaswa kurejea Wittenberg bila kuchelewa, na pia tahadhari kubwa zichukuliwe. Naye aliufuata mpango huo, akaondoka kwa farasi huko Augsburg kabla ya mapambazuko, akiongozana na mlinzi aliyetolewa na hakimu. Kwa siri alipenya kwenye mitaa ya mji wenye giza. Adui, wakiwa

[52]Martyn, The Life and Times of Luther, pp. 271, 272.
[53]D’Aubigne, London ed., bk. 4, ch. 8.

makini na katili, walikuwa wanapanga maangamizi yake. Huo ulikuwa ni wakati wa dukuduku na maombi ya dhati. Akalifikia lango dogo kwenye ukuta wa mji. Lilifunguliwa kwa ajili yake, na akapita akiwa na mlinzi wake. Kabla balozi wa Papa hajagundua kuwa Luther ameondoka, alikuwa ameflka mbali kusikoweza kufikiwa na watesi wake.

Balozi alipopata taarifa kuwa Luther ametoroka, alishindwa [90] kabisa kwa mshangao na hasira. Alitarajia kupata heshima kubwa sana kwa ujasiri wake katika kumshughulikia huyu mtaabishaji wa kanisa. Katika barua aliyoandika kwa Frederick, mjumbe wa baraza la uchaguzi la Saksoni, balozi alimkosoa Luther vikali, akamtaka Frederick ampeleke Roma au yeye apigwe marufuku huko Saksoni.

Mjumbe wa baraza la uchaguzi, alifahamu kidogo tu juu ya mafundisho yaliyofanyiwa marekebisho, lakini alivutwa sana na nguvu na usahihi wa maneno ya Luther. Frederick aliazimu kumlinda Luther hadi itakapothibitika kuwa alikuwa na makosa. Katika jibu lake kwa balozi wa Papa Frederick, aliandika: "Kwa sababu Daktari Luther alikuja mbele zako pale Augsburg, ilikupasa uridhike. Hatukutegemea kwamba ungejitahidi kumfanya afute mafundisho yake bila kumwonesha makosa yake. Hakuna mtu miongoni mwa wasomi ndani ya nchi yetu aliyenipa taarifa kuwa mafundisho ya Martin hayamheshimu Mungu, yanampinga Kristo, au ni ya uasi." [54] Mjumbe wa baraza Ia kura alitambua kuwa matengenezo yalihitajika. Kwa siri, alifurahi kwamba hisia za mvuto mzuri zilianza kujitokeza kanisani.

Ni mwaka mmoja pekee ulikuwa umepita tangu Mwanamatengenezo alipobandika Maandiko yake kwenye mlango wa kanisa; lakini maandishi yake yalikuwa yamewasha shauku mpya juu ya Maandiko Matakatifu kila mahali. Wanafunzi walimiminika kwenye Chuo kikuu, siyo kutoka sehemu zote za Ujerumani pekee, lakini kutoka nchi nyingine. Vijana walipouona mji la Wittenberg kwa mara ya kwanza "waliinua mikono yao mbinguni, na kumsifu Mungu kwa kusababisha nuru kutoka mbinguni kuangaza kote kupitia mji huu." [55]

[54] D'Aubigne, bk. 4, ch. 10.

[55] Ib d.

Hadi hapo Luther alikuwa amegeuka kwa sehemu kutoka kwenye makosa ya Kanisa la Roma. Lakini, aliandika, "Ninazisoma amri za Mapapa, na...sifahamu endapo Papa ndiye mpinga Kristo mwenyewe, au mtume wake, kwa hiyo Kristo amepotoshwa na kusulubishwa ndani yao. [56]

[91] Kanisa la Roma zaidi na zaidi lilikasirishwa na mashambulizi ya Luther. Wapinzani wenye msimamo mkali, hata madaktari kwenye vyuo vikuu vya Wakatoliki, walitangaza kuwa yeye atakayemwua mtawa (Luther) atakuwa hana dhambi. Lakini Mungu alikuwa mlinzi wake. Mafundisho yake yalikuwa yanasikika kila mahali- "katika nyumba za watu na nyumba za watawa...katika majumba ya waheshimiwa, katika vyuo vikuu, na katika makao ya wafalme." [57]

Wakati huu Luther aligundua kuwa ukweli mkuu wa kuhesabiwa haki kwa imani ulikuwa unashikwa na Mwanamatengenezo wa Bohemia, Huss. "Sisi wote" alisema Luther, "Paulo, Augustino, na mimi mwenyewe, tulikuwa wafuasi wa Huss bila kufahamu!" [58]

Hivyo Luther aliandika kuhusu vyuo vikuu: "Nina hofu kubwa kwamba vyuo vikuu vitathibitika kuwa malango makuu ya kuzimu, isipokuwa kama watafanya bidii kuyafafanua Maandiko Matakatifu, na kuyaandika ndani ya mioyo ya vijana...kila taasisi ambayo ndani yake watu hawajajazwa na Neno la Mungu daima lazima itaharibika." [59]

Mwito huu ulisambazwa katika Ujerumani yote. Taifa zima lilitikiswa. Wapinzani wa Luther walimtaka Papa achukue hatua za uamuzi dhidi yake. Ilitolewa amri kwamba mafundisho yake yashutumiwe haraka. Mwanamatengenezo na wafuasi wake, kama hawangefuta mafundisho yao, wote wangetengwa.

## Zahama ya Kutisha

Hiyo ilikuwa ni Zahama ya kutisha kwa Matengenezo. Luther hakuwa kipofu kwa ajili ya dhoruba iliyokuwa karibu kufumuka, lakini alimtumaini Kristo awe msaada na ngao yake. "Kile kinachokaribia kutokea sikijui, na wala sijishughulishi kukijua...Jani

[56] Ibid., bk. 5, ch. 1

[57] Ibid., bk. 6, ch. 2.

[58] Wylic, bk. 6, ch. 1.

[59] D'Aubigne, bk. 6, ch. 3.

halitaanguka bila mapenzi ya Baba. Ni kwa kiasi gani basi anatujali sisi! Ni kitu rahisi kufa kwa ajili ya Neno, maana Neno aliyefanyika mwili Yeye mwenyewe alikufa” [60]

Amri ya Papa ilipomfikia Luther, alisema, “Ninaidharau na [92]
kuishambulia, kuwa ina kufuru, ni ya uongo...Ni Kristo mwenyewe aliyeshutumiwa ndani yake. Tayari ninahisi uhuru mkubwa moyoni mwangu; maana hatimaye ninafahamu kwamba Papa ni mpinga Kristo, na kwamba kiti chake ni kile cha Shetani mwenyewe.” [61]

Siyo kwamba mamlaka ya Kanisa la Roma ilikuwa bure. Watu dhaifu na waliokuwa wanashika mapokeo potovu, walitetemeka kwa ajili ya amri ya Papa, na wengi walihisi kuwa uhai ni bora sana na haungepaswa kuhatarishwa. Je, kazi ya Mwanamatengenezo ilikaribia kufungwa?

Luther bado hakuogopa. Kwa nguvu ya ajabu aliitupilia mbali hukumu Kanisa la Roma. Mbele ya umati mkubwa wa raia wa ngazi zote, Luther aliichoma moto amri ya Papa. Alisema, “Pambano zito ndiyo limeanza. Kabla ya hapo nilikuwa tu nacheza na Papa. Niliianza kazi hii kwa jina la Mungu; na itamalizika bila mimi, na kwa nguvu zake...Ni nani ajuaye kwamba Mungu hajanichagua na kuniita mimi, na kama hawapaswi kuliogopa hilo, kwa kunidharau mimi, wanamdharau Mungu mwenyewe?...

Mungu hajawahi kumchagua kuhani mkuu au mtu mwenye cheo kikubwa kuwa nabii; bali huwachagua watu duni na wanaodharauliwa, mara moja alimchagua Amosi mchungaji. Katika kila kizazi, watakatifu waliwakemea wakuu, wafalme, wana wa wafalme, makuhani, na watu wenye hekima, wakihatarisha maisha yao... Sisemi kuwa mimi ni nabii; bali nasema kuwa inawapasa kuwa na hofu kidogo kwa sababu niko pekee yangu na wao wako wengi. Nina uhakika na hili, kwamba Neno la Mungu liko upande wangu, na kwamba haliko kwao.” [62]

Uamuzi wa mwisho wa Luther kujitenga na kanisa uliambatana [93]
na pambano la kutisha ndani ya nafsi yake: “Oo ni maumivu kiasi gani yaliyonipata, ingawa nilikuwa na Maandiko upande wangu, kuhalalisha mwenyewe kwamba inanipasa kuthubutu kuwa na msimamo wa peke yangu dhidi ya Papa, na kumtaja kuwa ni mpinga

[60] D’Aubigne, 3’1 London ed., Walther, 1840, bk. 6, ch. 9.
[61] Ibid.
[62] Ibid.,ch. 10.

Kristo! Ni mara ngapi sikujiuliza kwa uchungu lile swali, ambalo mara nyingi sana, lilikuwa midomoni mwa watawala wa Kanisa la Roma kwamba: 'Je, peke yako u mwenye hekima? Je, inawezekana kuwa kila mmoja amekosea? Itakuwaje, ikiwa baada ya yote, itaonekana kuwa ni wewe mwenye makosa na unawahusisha wengi katika makosa, ambao hatimaye watapotea milele?' Ndivyo nilivyopigana mwenyewe pamoja na Shetani, hadi Kristo, kwa njia ya Neno lake lisilokosea, alipouimarisha moyo wangu dhidi ya mashaka haya." [63]

Amri mpya ikatolewa, ikitangaza hatua ya mwisho ya kutengwa kwa Mwanamatengenezo kutoka kwenye Kanisa la Roma, likimshutumu kuwa amelaaniwa mbinguni, na kwamba wote ambao wangeyapokea mafundisho yake wangehusika katika hukumu hiyo.

Upinzani ni fungu la wote ambao Mungu huwatuma kuupeleka ukweli hasa ule unaofaa kwa wakati wao. Kulikuwa na ukweli wa leo katika siku za Luther; kuna ukweli wa leo kwa ajili ya kanisa leo. Lakini ukweli haupendwi sana na wengi leo kuliko ilivyokuwa kwa watawala wa kanisa la Papa, waliompinga Luther. Wale wanaouleta ukweli wa wakati huu haiwapasi kutarajia kuwa watapokelewa kwa upendeleo mkubwa kuliko ilivyokuwa kwa wanamatengenezo wa awali. Pambano kuu baina ya ukweli na uongo, baina ya Kristo na Shetani, litazidi wakati historia ya ulimwengu inapoelekea kufungwa. Angalia Yohana 15:19, 20; Luka 6:2.

[63] Martyn, pp. 372, 373.

## Sura Ya 8 - Mtetezi Wa Ukweli [94]

Charles wa V, alipanda kwenye kiti cha ufalme wa Ujerumani. Mjumbe wa baraza la uchaguzi wa huko Saksoni ambaye kwa kiasi kikubwa alimsaidia sana Charles kuupata Ufalme wake; alimsihi kutomchukulia hatua yoyote Luther hadi atakapompa nafasi ya kusikiliza maelezo yake. FCwahiyo mfalme alitahayari na kupata mfadhaiko mkubwa. Wafuasi wa Kanisa la Roma wasingeridhika na jambo lolote zaidi ya kifo cha Luther. Mjumbe wa baraza la uchaguzi alikuwa ametangaza kuwa "Daktari Luther alipaswa kupewa ulinzi kwa ajili ya usalama wake ili aweze kusimama mbele ya mahakama ya wasomi, wacha Mungu, na majaji wasio na upendeleo" [64]

Mkutano ulifanyika katika mji wa Worms. Kwa mara ya kwanza wakuu wa Ujerumani walikuwa wanakutana na mtawala wao kijana kwenye kusanyiko. Watu wenye vyeo kanisani na serikalini na mabalozi wa nchi za kigeni wote walikusanyika katika mji wa Worms. Lakini jambo lililochochea mvuto mkubwa ni Mwanamatengenezo. Mfalme Charles alimwagiza Mjumbe wa baraza la uchaguzi kumleta Luther pamoja naye, alimhakikishia usalama na kuahidi kuwepo kwa majadiliano huru katika mambo yanayobishaniwa. Luther alimwandikia Mjumbe wa baraza la kura kwamba, "Kama mfalme ananiita, sina mashaka kuwa huo ni mwito wa Mungu mwenyewe. Kama wanatamani kutumia nguvu dhidi yangu,...ninaliweka jambo hili katika mikono ya Mungu...Endapo hataniokoa, maisha yangu yana umuhimu kidogo tu...Unaweza kutarajia kila kitu kutoka kwangu isipokuwa kukimbia na kubadili msimamo. Kukimbia sitaweza, na sitarudi nyuma." [65]

Kwa kadiri habari zilivyosambaa kwamba Luther angesimama mbele ya mkutano huo wa kimataifa, msisimko mkubwa ulichochewa. Aleander, balozi mdogo wa Papa alishtushwa na kughadhibishwa. Kuhoji kwenye shauri ambalo Papa alikwisha kulitolea

[64] D'Aubigne, bk. 6, ch. 11.

[65] Ibid., bk. 7, ch. 1.

[95] tamko la hukumu ingekuwa ni kuidharau mamlaka ya baba mtakatifu. Zaidi ya hayo, hoja za mtu huyu zingeweza kuwageuza wengi wa wakuu hao wamwache Papa. Alimlalamikia Charles dhidi ya kusimamishwa kwa Luther huko Worms na alimshawishi mfalme kusalimu amri.

Aleander hakuridhika na ushindi na akafanya bidii kuhakikisha kuwa Luther anahukumiwa. Alimtuhumu Mwanamatengenezo huyo kwa "uchochezi, uasi, utovu wa kicho, na mwenye kukufuru." Lakini ukali wake ulifunua ni roho gani aliyekuwa anamchochea. "Alikuwa amesukumwa na hali ya chuki na kisasi,“ [66] hayo yalikuwa ndiyo maoni ya jumla. Aleander alitoa hoja kwa shauku maradufu kuwa mfalme ayatendee kazi maagizo ya Papa. Baada ya kushindwa na ung'ng'anizi wa balozi huyo wa Papa, alimruhusu kulipeleka shauri lakini mbele ya mkutano. Kwa sababu ya mashaka wale waliompendelea Mwanamatengenezo walikuwa wanaingojea hotuba ya Aleander. Mjumbe wa baraza la uchaguzi wa Saksoni hakuwepo, lakini baadhi ya washauri wake waliiandika hotuba ya balozi huyo wa Papa.

### Luther Ashitakiwa kwa Uasi wa Kidini

Aleander akitumia ujuzi na lugha ya ushawishi alijiweka katika nafasi ya kumpindua Luther kama adui wa kanisa na wa serikali. Alisema, "Katika makosa ya Luther kuna mambo ya kutosha" kumfanya achomwe sawa na "mamia ya maelfu ya waasi."

"Wafuasi wote hawa wa Luther ni nini? Ni kundi la walimu wenye dharau, mapadre wasio na maadili, watawa wa kiume waliopotoka, wanasheria wajinga, na wakuu walioporomoka kimaadili... Wakatoliki ni bora kiasi gani katika idadi, uwezo na nguvu, ukiwalinganisha na hawa wafuasi wa Luther! Amri ya pamoja kutoka kwenye mkutano huu maarufu itawaelimisha watu wa kawaida, itawaonya wajinga, wanaoyumbayumba kufanya maamuzi, na itatoa nguvu kwa wadhaifu." [67]

Hoja za namna hii bado hutolewa dhidi ya wote wanaothubutu kuyaleta mafundisho ya Neno la Mungu kwa uwazi. "Hawa wahubiri
[96] wa mafundisho mapya ni akina nani? Hawana elimu, ni wachache

[66] Ibid.
[67] Ibid., ch. 3.

kwa idadi, na wanatoka kwenye daraja la maskini. Na bado wanadai kuwa wanao ukweli, na kwamba ndio walioteuliwa na Mungu. Ni wajinga na wamedanganyika. Ni ubora wa juu jinsi gani unaodhihirishwa na kanisa letu kwa idadi ya watu na mvuto!" Hoja hizi haziondoi tena mashaka sasa kuliko ilivyokuwa nyakati za wanamatengenezo.

Luther hakuwepo ili kuushinda utetezi wa utawala wa Papa kwa ukweli wa Neno la Mungu ulio wazi na wenye kushawishi. Kulikuwepo na mwelekeo wa jumla siyo tu wa kumhukumu Luther na mafundisho aliyofundisha, bali kama ingewezekana kuung'oa uasi. Yale yote ambayo Kanisa la Roma lingeweza kuyasema kwa ajili ya uthibitisho wake yalikuwa yamesemwa. Tangu wakati huo tofauti kati ya ukweli na uongo ilikuwa inaonekana dhahiri kwa kadiri pambano lilivyokuwa wazi.

Sasa Bwana alimsukuma mmoja wa wajumbe wa mkutano kufafanua undani wa madhara ya udhalimu wa utawala wa Papa. George, Mtawala wa jimbo la Saksoni, alisimama mbele ya lile kusanyiko la kifalme akachambua kwa usahihi wa ajabu udanganyifu na machukizo ya utawala wa Papa:

"Vilio vya dhuluma vinasikika kwenye Kanisa la Roma. Aibu yote imewekwa kando, na lengo lao pekee ni...pesa, pesa, pesa,...kiasi kwamba wahubiri waliokuwa wanatakiwa kufundisha ukweli, hawatamki chochote isipokuwa uongo, na siyo tu wanavumiliwa, bali pia wanatuzwa, kwa sababu, kwa kadiri uongo unavyokuwa mkubwa ndiyo faida inavyozidi kuwa kubwa kwao. Kutoka kwenye chemchemi hii mbovu ndipo yanapotoka maji haya machafu. Uuaji na ulafi wa mali vinashikamana... Ni huzuni, kashfa iliyosababishwa na makasisi inazitupa roho nyingi maskini kwenye hukumu ya milele. Matengenezo ya jumla ni lazima yafanyike." [68] Ukweli kuwa mzungumzaji alikuwa adui mkubwa wa Mwanamatengenezo, ulisababisha mvuto mkubwa kwa maneno yake.

Malaika wa Mungu waliliangazia nuru giza la uongo na kuifunua mioyo kwenye ukweli. Uwezo wa Mungu wa ukweli uliwadhibiti hata maadui wa matengenezo na ulitayarisha njia kwa ajili ya kazi kubwa iliyokuwa karibu kufanyika. Sauti ya Aliye mkuu kuliko Luther ilikuwa imesikika katika kusanyiko lile.

[68] Ibid., ch. 4.

[97] Iliteuliwa kamati ya kuandaa orodha ya dhuluma za utawala wa Papa ambazo zilikuwa mzigo mzito kwa watu wa Ujerumani. Orodha hiyo iliwasilishwa kwa mfalme, ikiwa na madai ya kumtaka achukue hatua za kuziondoa dhuluma hizo. Walalamikaji walisema, "Ni jukumu letu kuzuia uangamivu na kuvunjiwa heshima watu wetu. Kwa sababu hiyo kwa unyenyekevu mkuu na kwa umuhimu mkubwa tunakutaka uamuru matengenezo ya jumla, na kuhakikisha yanakamilika." [69]

### Luther Aitwa Shaurini

Sasa baraza lilihitaji uwepo wa Mwanamatengenezo. Hatimaye mfalme aliridhika, na Luther aliitwa. Hati ya kuitwa kwenye shauri ilitolewa pamoja na hati ya hakikisho la usalama wake. Hati hizi zilipelekwa huko Wittenberg kupitia kwa Mjumbe aliyepewa jukumu la kumpeleka Luther kwenye mji wa Worms.

Marafiki wa Luther walizijua chuki zisizo na sababu na uadui dhidi yake, na hivyo walipata hofu kuwa uhakikisho wa usalama wake haungeheshimiwa. Yeye alijibu: "Kristo atanipatia Roho wake ili niwashinde hawa watumishi wa upotovu. Ninawadharau wakati wa uhai wangu; nitapata ushindi dhidi yao kwa njia ya kifo changu. Wapo Worms wakishughulika kwa bidii juu ya kunilazimisha nikanushe; na hivi ndivyo nitakavyokanusha: Hapo kabla nilisema kuwa Papa ni wakili Wakristo; na sasa ninatangaza kuwa yeye ni adui wa Bwana na ni mtume wa Ibilisi." [70]

Zaidi ya mjumbe wa kifalme, marafiki watatu waliazimu kumsindikiza Luther. Moyo wa Melanchthon ulifiimwa kwenye moyo wa Luther, na alitamani kumfuata. Lakini, hakupata kibali. Mwanamatengenezo alisema: "Endapo sitarejea, na maadui zangu wakiniua, endelea kufundisha, na usimame imara katika kweli. Fanya kazi kwa niaba yangu...kama ukiwa hai wewe, kifo changu hakitakuwa na madhara makubwa. [71]

[98] Mioyo ya watu ililemewa na ubashiri wa kuhuzunisha. Walijua kuwa Maandiko ya Luther yalishutumiwa huko Worms. Mjumbe, alihofia usalama wa Luther kwenye baraza na alimwuliza ikiwa

[69] Ibid.
[70] Ibid., ch. 6.
[71] Ibid., ch. 7.

angeendelea na safari. Alijibu kuwa: "Ingawa ninapigwa marufuku katika kila mji, nitaendelea." [72]

Katika mji wa Erfurt, Luther alipitia mitaa ambayo mara nyingi alikuwa anaikatisha, alitembelea chumba chake kwenye nyumba ya watawa. Alifikiria juu ya masumbufu aliyoyapata alipokuwa anapatiwa nuru ambayo sasa ilikuwa inafurika katika Ujerumani yote. Aliombwa ahubiri. Jambo hilo hakuruhusiwa kufanya, lakini mjumbe alimpa ruhusa, na mtawa ambaye wakati fulani aliwekwa kuwa mfanyakazi wa kazi ngumu kwenye nyumba hiyo, sasa aliingia kwenye mimbara.

Watu walimsikiliza kwa umakini mkubwa. Mkate wa uzima ulimegwa kwa ile mioyo yenye njaa. Kristo aliinuliwa mbele yao kupita Papa, mabalozi, watawala na wafalme. Luther hakuongea chochote juu ya hali yake ya hatari kubwa. Alikuwa ameuficha ubinafsi wake katika Kristo. Alijificha nyuma ya Mtu wa Kalwari, akitafuta tu kumwasilisha Yesu kama Mkombozi wa mwenye dhambi.

### Ujasiri wa Mfia-dini

Kwa kadiri Mwanamatengenezo alivyoendelea, umati wa watu wenye shauku walimzunguka, na sauti zenye urafiki zilimwonya juu ya utawala wa Kanisa la Roma. Baadhi walisema, "Watakuchoma moto, na kuteketeza mwili wako kuwa majivu kama walivyomfanyia John Huss." Luther aliwajibu kuwa, "Hata kama watawasha moto njia nzima kutoka Worms hadi Wittenberg,...kwa jina la Bwana nitatembea kwenye njia hiyo; nitasimama mbele yao,...nikimkiri Bwana Yesu." [73]

Kukaribia kufika kwa Luther huko Worms kulisababisha ghasia [99]
kubwa. Marafiki zake walikuwa wanahofia usalama wake; maadui zake walihofu juu ya kusudi lao. Akichochewa na watawala wa Kanisa la Roma, alitakiwa aende kwenye nyumba ya mtu mmoja mwema na mwenye hadhi ya juu, ambako, mambo yote magumu yangetatuliwa kirafiki. Marafiki walielezea hatari zilizokuwa zinamkabili. Luther bila kutetemeka alitamka kuwa: "Hata kama mji

[72] Ibid.

[73] Ibid.

wa Worms utakuwa na maShetani wengi kama vigae vya paa la nyumba, bado nitauingia” [74]

Alipowasili katika mji wa Worms, kundi kubwa la watu lilikuwa limejaa langoni ili kumpokea. Kulikuwa na msisimko wa hali ya juu. Alipokuwa akitelemka kutoka kwenye gari lake la farasi alisema, “Mungu atakuwa mlinzi wangu.” Kuwasili kwake kuliwajaza fadhaa viongozi wa Kanisa la Roma. Mfalme aliwaita washauri wake. Aliwauliza ni njia gani wangeitumia. Kiongozi mmoja shupavu wa Kanisa la Roma alitamka kuwa: “Tumejadiliana kwa muda mrefu juu ya jambo hili. Hebu wewe mfalme mtukufu mfutilie mbali mtu huyu mara moja. Je, Sigismund hakuamuru John Huss achomwe moto? Hatufungwi na kanuni kumpa au kutimiza hakikisho la usalama wa mtu mwasi.” “Hapana” mfalme alisema, “Ni lazima tuitimize ahadi yetu.” [75] Iliamriwa kuwa Mwanamatengenezo apate nafasi ya kusikilizwa.

Watu wote wa mji ule walikuwa na shauku ya kumwona mtu huyu asiye na kifani. Luther alikuwa amechoka kwa safari, alihitaji pumziko na utulivu. Lakini alipata saa chache tu za kupumzika pale, watu wenye vyeo, waheshimiwa, mapadre, na raia walipokusanyika kumzunguka. Miongoni mwao ni waheshimiwa ambao kwa ujasiri walimtaka mfalme afanye matengenezo juu ya shutuma zilizolihusu kanisa. Marafiki na maadui walikuja kumwangalia mtawa huyu asiye na hofu. Mwonekano wake ulikuwa thabiti na wa kijasiri. Uso wake mwembamba, uliokuwa unaonekana, kunyong’onyea ulivaa mwonekano wa upole na furaha. Maneno yake ya dhati yalisababisha nguvu ambayo hata adui zake hawakuweza kuihimili kikamilifu. Wengine walishawishika kuwa alikuwa na nguvu ya Mungu iliyokuwa inamwongoza; wengine, kama Mafarisayo walivyomwambia Kristo, walitamka kuwa, “Ana pepo.” Yohana 10:20.

[100] Katika siku iliyofuata afisa mmoja wa serikali aliteuliwa kumwongoza Luther kwenye ukumbi ili akasikilizwe. Kila mahali palikuwa pamejaa watazamaji wenye shauku ya kumwona mtawa aliyethubutu kumpinga Papa. Jemadari mmoja mzee, aliyewahi kushinda vita vingi, alimwambia kwa upole, “Maskini mtawa,

[74] Ibid.

[75] Ibid., ch. 8.

sasa unakwenda kuonesha msimamo bora kuliko mimi au uliowahi kuoneshwa na makapteni wowote kwenye mapambano yetu yenye umwagaji damu. Lakini ikiwa kusudi lako ni la haki,...songa mbele katika jina la Mungu, na usiogope chochote. Mungu hatakuacha.” [76]

### Luther Asimama Mbele ya Baraza

Mfalme alikaa kwenye kiti chake. Alikuwa amezungukwa na watu mashuhuri zaidi katika ufalme wake. “Mwonekano huu kwa peke yake ulikuwa alama ya ushindi dhidi ya utawala wa Papa. Papa alikuwa tayari amemhukumu Luther, na sasa alikuwa anasimama mbele ya mahakama ambayo, kwa kitendo hicho, ilijiweka yenyewe juu ya Papa. Papa alikuwa amempiga marufuku, akamtenga kutoka kwenye jamii nzima ya wanadamu; na bado aliitwa kwa lugha yenye staha, na akapokelewa mbele ya kusanyiko adhimu zaidi duniani...Roma ilikuwa tayari inashuka kutoka kwenye enzi yake, na ilikuwa ni sauti ya huyu mtawa iliyosababisha fedheha hii.” [77]

Mwanamatengenezo huyo aliyezaliwa kwenye familia duni alionekana kutishika na kutahayari. Wakuu kadhaa walimsogelea, na mmoja wao akamnong’oneza kuwa asiwaogope “wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho.” Mwingine akasema: “Nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu, kuwa ushuhuda kwao na kwa mataifa. Lakini hapo watakapowapeleka, msifikiri-fikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakayosema.” Angalia Mathayo 10:28, 18, 19.

Kukawa na ukimya mkuu kwenye kusanyiko la umati wa watu. [101]
Ndipo yule afisa wa serikali akasimama, akiyaonesha Maandiko ya Luther na kumtaka Mwanamatengenezo huyo ajibu maswali mawili- ikiwa aliyatambua kuwa ni yake, na endapo alikuwa amefikiria kukanusha maoni yaliyomo ndani ya Maandiko yale. Vilipokwisha kusomwa vichwa vya vitabu, Luther alijibu swali la kwanza kwamba alivitambua kuwa ni vyake. “Kuhusu swali la pili,” akasema, “Nitatenda bila busara ikiwa nitajibu bila kutafakari. Ninaweza nikatoa uthibitisho kidogo kuliko hali inavyohitaji, ama zaidi ya vile ukweli unavyotaka. Kwa sababu hii ninakusihi mfalme mtukufu, kwa un-

[76] Ibid.
[77] Ibid.

yenyekevu wote, nipatie muda, ili niweze kujibu pasipo kulikosea Neno la Mungu.” [78]

Luther alilishawishi kusanyiko kuwa katika kutenda jambo lile hakuongozwa na hisia au mihemuko ya ghafla. Utulivu na kujiamini kwa namna ile, ambako hakukutarajiwa ndani ya mtu imara asiyebadili msimamo; ulimwezesha baadaye kujibu kwa busara na heshima iliyowashangaza adui zake na ikawa onyo kwa ufidhuli wao.

Siku iliyofuata, Luther alipaswa kutoa jibu lake la kwanza. Kwa muda mfupi moyo wake ulishuka. Adui zake walielekea kupata ushindi. Mawingu yalimzunguka na yalionekana kumtenga na Mungu. Akiwa na huzuni kuu rohoni, alimwaga vilio vya moyo uliopondeka na kuraruka, ambayo hakuna awezaye kuvifahamu isipokuwa Mungu. “Oo Mungu mkuu na wa milele,” alimsihi, “Ikiwa ni lazima niweke tumaini langu katika uwezo wa ulimwengu huu tu, kila kitu kimekwisha...Saa yangu ya mwisho imekuja, hukumu yangu tayari imetolewa...Oo Mungu, unisaidie dhidi ya hekima ya ulimwengu...Kazi ni yako...na ni kazi ya haki na ya milele. Oo Bwana, unisaidie! Mungu uliye mwaminifu na ambaye si kigeugeu, siliweki tumaini langu juu ya mwanadamu yeyote...Umenichagua kwa ajili ya kazi hii...Simama upande wangu, kwa ajili ya Mwanao mpendwa Yesu Kristo, ambaye ndiye mlinzi wangu, ngao yangu, na ngome yangu . [79]

Jambo lililomtia hofu kubwa halikuwa kuogopa taabu yake binafsi, mateso, ama kifo. Alikuwa anahisi kuwa upungufu na udhaifu
[102] wake ungeweza kudhoofisha kusudio la ukweli. Alishindana na Mungu si kwa ajili ya usalama wake mwenyewe, bali kwa ajili ya ushindi wa Injili. Katika udhaifu wake usio na msaada kabisa, alishikilia imani yake kwa Kristo, Mwokozi mwenye nguvu. Asingetokea akiwa pekee yake mbele ya baraza. Amani ilirejea moyoni mwake, na alifurahi kwa sababu aliruhusiwa kuliinua Neno la Mungu mbele ya watawala wa mataifa.

Luther alitafakari juu ya jibu lake, alizichunguza aya ndani ya maandishi yake, na kutoa ndani ya Maandiko Matakatifu ushahidi unaofaa kutetea msimamo wake. Kisha, aliuweka mkono wake

[78] Ibid.

[79] Ibid.

wa kushoto juu ya Kitabu Kitakatifu, akauinua mkono wake wa kuume mbinguni na kuapa "kudumu akiwa mwaminifu katika Injili, na kuikiri imani yake kwa uhuru, hata kama ushuhuda wake ungegharimu maisha yake." [80]

### Luther Mbele ya Mkutano kwa Mara Nyingine

Alipokaribishwa kwa mara nyingine ndani ya mkutano, alikuwa mtulivu na mwenye amani, lakini pia shujaa na mwenye heshima, kama shahidi wa Mungu miongoni mwa watu wakuu wa dunia. Yule afisa wa serikali sasa alikuwa anahitaji kupata uamuzi wa Luther. Je, alikuwa ameamua kukanusha? Luther alitoa jibu lake kwa sauti ya unyenyekevu, bila vurugu wala hofu. Mwonekano wake ulikuwa wa kutojiamini na wenye heshima; lakini alionesha ujasiri na furaha ambavyo viliwashangaza mkutano ule.

Alianza kwa kusema: "Mtukufu mfalme mkuu, wana adhimu wa wafalme, mabwana wenye hisani; ninasimama mbele yenu siku ya leo, ili kutimiza agizo lililotolewa kwangu jana. Ikiwa, kwa ujinga, nitakosea matumizi na taratibu za mahakama ninawasihi mnisamehe; maana sikulelewa kwenye nyumba za wafalme, bali kwenye nyumba za upweke za watawa." [81]

Kisha akasema kuwa ndani ya baadhi ya kazi zake zilizochapishwa juu ya imani na matendo; hata maadui zake walisema kuwa zinafaa. Kuzikanusha ingekuwa ni kuushutumu ukweli ambao watu wote wanaukiri. Daraja la pili lilijumuisha maandishi yaliyou- [103]
funua upotovu na dhuluma za utawala wa Papa. Kuyatangua hayo kungeimarisha udhalimu wa Kanisa la Roma na kufungua mlango mpana kwa kufuru kubwa. Katika daraja la tatu aliwashambulia watu binafsi walioyatetea maovu. Kuhusiana na hayo alikiri kwa uhuru kuwa alikuwa mkali kuliko ilivyotakiwa. Lakini vitabu hivi pia hangevitangua, kwani maadui wa ukweli wangechukua fursa hiyo kuwalaani watu wa Mungu kwa ukatili mkubwa zaidi.

Aliendelea kusema, "Nitajitetea mwenyewe kama Kristo alivyofanya: 'Ikiwa nimeongea uovu, uletwe ushahidi juu ya uovu'..Kwa rehema ya Mungu, ninakusihi sana wewe, mfalme mtukufu sana, na ninyi wana adhimu wa wafalme, na wanadamu wote wa kila hadhi,

[80] Ibid.
[81] Ibid.

kuthibitishiwa kutoka kwenye Maandiko ya manabii na mitume kwamba nimekosea. Mara tu nitakaposhawishika juu ya hili, nitakanusha kila kosa,.na kuwa wa kwanza kuvichukua vitabu vyangu na kuvitupa motoni...

"Badala ya kutishwa, ninafurahia kuona kuwa Injili, sasa inasababisha taabu na mafarakano, kama ilivyokuwa katika nyakati zilizopita. Hii ndiyo tabia, hii ndiyo hatima ya Neno la Mungu. 'Sikuja kuleta amani duniani, bali upanga,' alisema Yesu Kristo... Jihadharini, isije ikawa kwa kudhani mnazuia mafarakano, kumbe mnalitesa Neno Takatifu la Mungu, na kujiletea wenyewe gharika ya kutisha ya hatari zisizoondoka, za maafa ya wakati wa sasa, na ukiwa wa milele." [82]

Luther alizungumza kwa Kijerumani; na sasa alitakiwa kuyarudia maneno yale yale kwa Kilatini. Kwa mara nyingine tena aliitoa hotuba yake kwa ufasaha kama aliyoitoa kwanza. Ni majaliwa ya Mungu yaliyoliongoza hili. Wakuu wengi walikuwa wamepofushwa na uongo na mapokeo potuvu kiasi kwamba mwanzoni hawakuona nguvu ya hoja za Luther, lakini marudio yaliwawezesha kutambua kwa uwazi hoja alizozileta.

Wale ambao kwa kiburi waliyafumba macho yao wasipate nuru, walikasirishwa kutokana na uwezo uliokuwa kwenye maneno ya Luther. Msemaji wa lile baraza akasema kwa hasira: "Hujajibu swali uliloulizwa...unapaswa kutoa jibu lililo wazi na kwa ufupi...Je, utakanusha au hutakanusha?"

[104] Mwanamatengenezo akajibu: "Kwa vile wewe uliye mtakatifu sana na wakuu wenye nguvu wanataka kutoka kwangu jibu sahihi, rahisi, na fupi; nitawapa, nalo ni hili: "Siwezi kuisalimisha imani yangu kwa Papa au kwenye mabaraza, maana ni wazi kama mchana kwamba mara nyingi wamekosea na kujichanganya wenyewe. Kwa hiyo, nisiposhawishika kwa ushuhuda wa Maandiko,...*Siwezi na sitaweza kukanusha*, maana si salama kwa Mkristo kusema kinyume ma dhamiri yake. Huu ndio msimamao wangu, siwezi kufanya kitu kingine; Mungu anisaidie. Amina." [83]

Hivi ndivyo alivyosimama huyu mtu mwenye haki. Ukuu na usafi wa tabia yake, amani na furaha yake ya moyo, vilionekana

[82]Ibid
[83]Ibid

kwa wote alipokuwa akishuhudia ukuu wa ile imani iushindayo ulimwengu.

Katika jibu lake la kwanza Luther alizungumza akiwa na mwonekano wa heshima na kujisalimisha. Watawala wa Kanisa la Roma walichukulia kuwa ombi la muda wa ziada lilikuwa ni utangulizi wa kuyakanusha maoni yake. Mfalme Charles mwenyewe, alilitazama kwa dharau kidogo umbile la mtawa lililochakaa, akiwa kwenye mavazi yake ya kawaida, na usahili wa hotuba yake, alitamka kuwa: "Mtawa huyu kwangu mimi siyo mwasi." Ujasiri na uimara ambao sasa aliuonesha, uwezo wake wa kujenga hoja, ulisababisha watu wote kupigwa na butwaa. Mfalme, akiwa amevutwa na kustaajabu, alitamka kwa mshangao: "Huyu mtawa anazungumza kwa moyo wa ushujaa na ujasiri usiotikisika."

Wafuasi wa Kanisa la Roma walikuwa wamedanganywa. Walitaka kudumisha mamlaka yao kwa njia ya vitisho, hoja ya Kanisa la Roma isiyoshindwa, si kwa njia ya kuuliza kwenye Maandiko matakatifu bali, Msemaji wa baraza alisema: "Ikiwa hukanushi, mfalme na serikali ya ufalme wataamua ni hatua gani waichukue dhidi ya mwasi mwenye tabia isiyobadilika." Luther alijibu kwa utulivu: "Mungu awe msaada wangu, maana siwezi kukanusha chochote." [84]

Alikuwa ameelekezwa kufuta msimamo wake wakati wakuu [105]
walipokuwa wakinajadiliana. Tendo la Luther kukataa kujisalimisha lingeweza kuathiri historia ya kanisa kwa vizazi vingi. Iliamuliwa kuwa apewe nafasi nyingine zaidi ya kukanusha. Swali liliulizwa tena, endapo angeyafuta mafundisho yake? "Sina jibu lingine?" alisema, "zaidi ya lile ambalo tayari nimelitoa."

Viongozi wa utawala wa Papa walihuzunika kwani mamlaka yao ingepuuzwa na mtawa huyu duni. Luther alikuwa amezungumza kwa wote kwa heshima ya Kikristo na utulivu, maneno yake yalikuwa huru dhidi ya msisimko na upotovu. Hakujiona yeye bali alihisi tu kuwa alikuwa mbele ya Yule mwenye ukuu usio na kikomo anayewazidi Mapapa, wafalme, na watawala. Roho wa Mungu alikuwepo, akigusa mioyo ya wakuu na ufalme.

Baadhi ya wakuu kwa ushupavu walitambua ujasiri wa msimamo wa Luther. Kundi jingine kwa wakati huo halikuweza kueleza msi-

[84] Ibid

mamo wao, lakini wakati wa baadaye, wakawa waungaji mkono wasio na hofu wa Matengenezo.

Frederick, mjumbe wa baraza la uchaguzi, aliisikiliza hotuba ya Luther kwa hisia ya kina. Kwa furaha na fahari alishuhudia ujasiri wa Daktari yule na kujiamini kwake, na akaazimu kusimama imara katika kumlinda. Aliona kuwa hekima ya Mapapa, wafalme, na maaskofu iligeuzwa kuwa ubatili kwa uwezo wa ukweli.

Balozi wa Papa alipotambua athari ya hotuba iliyotolewa na Luther, aliazimia kutumia kila njia iliyokuwa ndani ya uwezo wake kuhakikisha Mwanamatengezo huyu anaangushwa. Alitumia ujuzi wa kidiplomasia na lugha yenye ushawishi kumwonesha mfalme kijana, hatari ya kuutoa kafara urafiki na msaada wa Kanisa la Roma kwa ajili ya suala la huyu mtawa asiye na maana.

Siku iliyofuata baada ya jibu la Luther, Charles alilitangazia baraza juu ya uamuzi wake wa kuidumisha na kuilinda dini ya Ukatoliki. Hatua kali zingetakiwa kutumika dhidi ya Luther pamoja na mafundisho yake ya uasi aliyoyatoa: "Nitautoa kafara ufalme wangu, hazina zangu, marafiki zangu, mwili wangu, damu yangu, roho yangu, na uhai wangu...nita...nitafungua kesi dhidi yake na
[106] dhidi ya wafuasi wake kwamba ni waasi wasiojali mamlaka, kwa kuwatenga, kwa kuwapiga marufuku, na kwa kila njia itakayopanga kwa umakini kuwaangamiza." [85] Hata hivyo, mfalme alitangaza kuwa hakikisho la usalama wa Luther lilikuwa ni lazima lizingatiwe. Ilikuwa ni lazima aruhusiwe kufika nyumbani kwake kwa usalama.

### Ulinzi wa Luther Hatarini

Wawakilishi wa Papa kwa mara nyingine walihitaji kuwa ulinzi wa Luther uondolewe. "Mto Rhine ni lazima uyapokee majivu yake, kama ulivyoyapokea yale ya John Huss kame moja iliyopita." [86] Lakini wakuu wa Ujerumani, pamoja na kuwa waliapa kuwa maadui wa Luther, walipingana na uvunjwaji wa makubaliano hayo mbele ya umma. Walionesha maafa yaliyofuatia kifo cha John Huss. Hawakuthubutu kuruhusu maovu hayo yajirudie huko Ujerumani.

Akitoa jibu juu ya pendekezo la msingi, Charles alisema: "Ingawa heshima na imani ni lazima vipigwe marufuku kwa

[85] Ibid.
[86] Ibid.

ulimwengu wote, ni lazima vipate kimbilio kwenye mioyo ya wafalme." [87] Maadui wa Luther, ambao ni wa utawala wa Papa, walimtaka awashughulikie wanamatengenezo kama vile Sigismund alivyomshughulikia John Huss. Akiwa na kumbukumbu za hali ilivyokuwa wakati Huss, mbele ya kusanyiko la hadhara, alipoonesha minyororo yake na kumkumbusha mfalme juu ya imani yake iliyokuwa taabuni, Charles V alitamka kuwa, "Sitapenda kufedheheka kama Sigismund." [88]

Lakini bado kwa makusudi Charles aliupuuza ukweli uliokuwa unafundishwa na Luther. Hakuweza kuiacha njia ya desturi ili kutembea kwenye njia za ukweli na haki. Kwa sababu baba zake walikuwa wamefanya hivyo, na yeye alipaswa kuutetea utawala wa Papa. Kwa hiyo alikataa kuikubali nuru mbele ya kile alichokuwa amekipokea kutoka kwa baba zake.

Wengi siku hizi wanazing'ang'ania desturi za baba zao. [107]
Bwana anapoileta nuru ya ziada wanakataa kuipokea kwa sababu haikupokelewa na baba zao. Hatutakubaliwa na Mungu kwa kuwaangalia baba zetu ili kuamua juu ya wajibu wetu badala ya kulichunguza Neno la Kweli sisi wenyewe. Tunawajibika kwa nuru ya ziada ambayo sasa inatuangazia kutoka kwenye Neno la Mungu.

Uwezo wa Mungu ulizungumza kwa mfalme na wakuu wa Ujerumani kupitia kwa Luther. Roho wake aliwasihi kwa mara ya mwisho ndani ya kusanyiko lile. Kama ilivyokuwa kwa Pilato, kame nyingi zilizokuwa zimepita, ndivyo ilivyokuwa kwa Charles V, aliikubali fahari ya kiulimwengu, akaamua kuiacha nuru ya ukweli.

Mipango dhidi ya Luther ilikuwa imesambaa kwa upana, na kusababisha msisimko katika mji wote. Marafiki wengi, wakifahamu ukatili na udanganyifu wa Kanisa la Roma, waliazimia kuwa Mwanamatengenezo hakupaswa kutolewa kafara. Mamia ya waheshimiwa waliahidi kumlinda. Katika malango ya nyumba, mabango yalibandikwa, baadhi yakimshutumu na mengine yakimuunga mkono Luther. Juu ya mlango mmoja yalibandikwa maandishi haya, "Ole wako, nchi, akiwa mfalme wako ni kijana." Mhubiri 10:16. Shauku ya wengi kumpendelea Luther ilimshawishi mfalme na

[87]Ibid.

[88]Lenfant, vol. 1, p. 422.

baraza kwamba jambo lolote lisilokuwa la haki ambalo angeoneshwa Luther lingehatarisha amani ya ufalme na nguvu za enzi yake.

### Jitihada za Mapatano na Kanisa la Roma

Frederick wa Saxony alizificha kwa uangalifu hisia zake halisi juu ya Mwanamatengenezo. Wakati huo huo alimchunga kwa uangalifu na bila kuchoka, akiziangalia nyendo zake na za maadui zake. Lakini watu wengi hawakujaribu kuzificha hisia zao juu ya huruma yao kwa Luther. Spalatin aliandika kuwa: Chumba kidogo cha Daktari, hakikuwatosha wageni wote waliomtembelea.” [89] Hata wale ambao hawakuyaamini mafundisho yake hawakuweza kujizuia, bali waliustajabia uadilifu uliomwongoza kwenye kifo cha kishujaa kuliko kupingana na dhamiri yake.

[108] Jitihada za dhati zilifanyika ili kupata ridhaa ya Luther kufanya mapatano na Kanisa la Roma. Wakuu na waheshimiwa walimwambia kuwa iwapo alikuwa ameliwekea kanisa na mabaraza hukumu yake mwenyewe, atafukuzwa katika Himaya na hatakuwa na ulinzi wowote. Kwa mara nyingine aliamriwa kujisalimisha kwenye uamuzi wa mfalme. Ndipo hangekuwa na chochote cha kuogopa. Alijibu, “Ninaridhika kwa moyo wangu wote, kwamba mfalme, wakuu, na hata Mkristo wa ngazi ya chini, anapaswa kuichunguza na kuihukumu kazi yangu; lakini kwa sharti moja, kwamba watalitumia Neno la Mungu kuwa kipimo chao. Wanadamu hawana lolote la kufanya ila kulitii.”

Katika mwito mwingine alisema: “Ninaridhika kuondolewa ulinzi wangu. Ninayaweka maisha yangu na nafsi yangu mikononi mwa mfalme, lakini sitalisalimisha Neno la Mungu-kamwe!” [90] Alitoa tamko juu ya uhiari wake wa kujisalimisha kwenye baraza kuu, lakini kwa sharti kuwa baraza lingetakiwa kufanya uamuzi kwa mujibu wa Maandiko. “Juu ya kile kinacholihusu Neno la Mungu na imani, kila Mkristo ni mwamuzi mzuri kama alivyo Papa, ingawa anaungwa mkono na mamilioni ya mabaraza.” [91] Mwishowe, marafiki na maadui walishawishika kwamba jitihada zaidi za kupatana zingekuwa bure.

[89] Martyn, vol. 1, p. 402.
[90] D’Aubigne, vol. 7, ch. 10.
[91] Martyn, vol. 1, p. 410

Endapo Mwanamatengenezo angekubaliana nao kwa kipengele kimoja, Shetani na majeshi yake wangepata ushindi. Lakini uimara wake usioyumbishwa, ilikuwa ndiyo njia ya kulikomboa kanisa. Mvuto wa mtu huyu mmoja aliyethubutu kufikiri na kutenda yeye mwenyewe, ulileta athari kwa kanisa na kwa ulimwengu, siyo tu wa wakati wake, bali kwa vizazi vyote vijavyo.

Kwa haraka Luther aliamriwa na mfalme kurudi nyumbani. Taarifa hiyo ingefuatana kwa haraka na hukumu yake. Mawingu ya kutisha yalikuwa juu ya njia yake, lakini alipokuwa akiondoka katika mji wa Worms, moyo wake ulijazwa furaha na sifa.

Baada ya kuondoka kwake, akiwa na shauku kuwa uthabiti wake [109]
usipotoshwe na kuleta uasi, Luther alimwandikia mfalme kuwa: "Nipo tayari kukutii wewe mtukufu kwa moyo wote, katika heshima na katika kudharauliwa, katika uzima au katika mauti, na bila kuliondoa Neno la Mungu, ambalo kwalo watu wanaishi...yanapohusika mambo ya milele, ni mapenzi ya Mungu kwamba mwanadamu asijisalimishe kwa mwanadamu. Maana kujitoa huko katika mambo ya kiroho ni ibada halisi, na inapaswa kutolewa kwa Mwumbaji peke yake." [92]

Akiwa safarini kutoka Worms wakuu wa makanisa walimkaribisha mtawa aliyetengwa, na viongozi wa umma walimheshimu mtu ambaye mfalme alikuwa amemkataa. Alitakiwa kuhubiri, na bila kujali marufuku ya kifalme, alipanda tena kwenye mimbara. Alisema, "Sikuahidi kulifunga minyororo Neno la Mungu na sitafanya hivyo." [93]

Haikuchukua muda mrefu tangu Luther alipoondoka Worms wakati utawala wa Papa ulipomwamuru mfalme kutoa amri dhidi yake. Luther alikuwa ameshutumiwa kuwa ni, "Shetani mwenyewe katika umbile la mwanadamu akijivalia joho la utawa." [94] Mara baada ya hati yake ya ulinzi ikiisha muda wake; watu wote wangekatazwa kumkaribisha, kumpa chakula au kinywaji, kwa maneno au matcndo au kushirikiana naye. Alitakiwa afikishwe mbele ya wenye mamlaka, wafuasi wake pia walipaswa kutupwa gerezani, na mali zao kutaifishwa. Maandiko yake yalipaswa kuangamizwa, na mwisho wale wote ambao wangethubutu kutenda kinyume na

[92] D'Aubigne, bk. 7, ch. 11.
[93] Martyn, vol. 1, p. 420
[94] D'Aubigne, bk. 7, ch. 11.

amri hii wangejumuishwa kwenye hukumu hiyo. Mjumbe wa baraza la uchaguzi wa Saksoni na wakuu waliokuwa na urafiki na Luther, waliondoka Worms baada ya kuondoka kwake, na amri ya mfalme ilipata idhini ya baraza. Watawala wa Kanisa la Roma walifurahi. Walichukulia kuwa suala la Matengenezo lilikuwa limefungwa.

[110]

## Mungu Amtumia Frederick wa Saxony

Mwenendo wa Luther ulifuatiliwa kwa jicho la uangalifu mkubwa, mtu mkweli na mwenye cheo kikubwa aliazimia kumwokoa. Mungu alimpatia Frederick wa Saksoni mpango wa kumlinda Mwanamatengenezo huyu. Katika safari yake kuelekea nyumbani Luther alitenganishwa na wahudumu wake na kwa haraka alipitishwa katika njia ya msituni na kupelekwa kwenye ngome iliyokuwa kule Wartburg, ngome iliyokuwa mahali pweke mlimani. Kufichwa kwake kulifanyika kwa siri sana kiasi kwamba hata Frederick mwenyewe hakuelewa namna alivyokuwa amepelekwa huko. Kutojua kwake huku kulikuwa kumepangwa ili asitoe siri. Alipojiridhisha ya kuwa Mwanamatengenezo huyo alikuwa salama, alitulia.

Majira ya kuchipua, majira ya joto, na mavuno yalipita na kipindi cha baridi kikaja na Luther alibakia kuwa mfungwa. Aleander na wafuasi wake walishangilia kwa furaha. Nuru ya Injili ilionekana kwamba ingezimwa. Lakini nuru ya Mwanamatengenezo huyu ilipaswa kuendelea kuangaza kwa miali yenye mng'ao mkubwa.

## Usalama Kule Wartburg

Hali ya usalama ilikuwa njema kule Wartburg, Luther alifurahia kuwa huru mbali na msuguano mkali na vurugu za mapambano. Akiwa amezoea maisha ya shughuli nyingi na mabishano makali, angeweza kuvumilia kwa shida sana kukaa bila shughuli yoyote. Katika siku hizo za upweke hali ya Kanisa ilikuja mbele yake. Aliingiwa na hofia kuwa angeonekana kuwa ni mwoga kwa kujitoa katika shindano. Alijilaumu mwenyewe kwa uvivu na kujishughulisha na mambo kupita kiasi.

Hata hivyo, wakati huohuo alikuwa akifanya mambo mengi kuliko anavyoweza mtu mmoja kutenda. Kalamu yake haikukoma

kuandika. Adui zake walistaajabu na kuchanganyikiwa kwa uthibitisho dhahiri kuwa alikuwa bado akifanya kazi. Vijitabu vingi alivyoviandika vilitawanywa katika Ujerumani yote. Pia alitafsiri Agano Jipya katika lugha ya Kijerumani. Kwa karibu mwaka mzima aliendelea kuihubiri Injili kutoka katika Patmo yake ya mlima wa majabali na kukemea makosa ya wakati huo.

Mungu alikuwa amemwondoa mtumishi wake kutoka katika [111]
maisha ya hadhara. Katika maisha ya upweke na mashaka na kukimbilia mlimani, Luther alikuwa ameondolewa katika kupata misaada na kusifiwa na wanadamu. Na kwa namna hiyo alikuwa amenusuriwa dhidi ya kiburi na kujiamini ambako mara nyingi husababishwa na mafanikio.

Wakati watu wanapofurahia uhuru unaoletwa kwao kwa njia ya ukweli, Shetani hutafuta kupindisha fikra na upendo wao kutoka kwa Mungu na kuuhamishia kwa mawakala wa kibinadamu, kumpatia heshima mtumishi na kumpuuza Yeye anayeongoza matukio ya ulinzi na utunzaji. Mara nyingi, viongozi wa kidini wanapotukuzwa, huongozwa katika kujitumainia wenyewe. Watu huelekezwa kuwatazama wao kama mwongozo wao badala ya Neno la Mungu. Mungu atayalinda Matengenezo kutoka katika hatari hii. Macho ya wanadamu yalikuwa yameelekezwa kwa Luther kama mfasili wa ukweli; aliondolewa ili macho yote yaweze kuelekezwa kwa Mwumbaji wa milele wa ukweli.

[112] # Sura Ya 9 - Nuru Yaamshwa Nchini Uswisi

Majuma machache baada ya Luther kuzaliwa kwenye kibanda cha mchimba madini kule Saksoni, Ulric Zwingli naye alizaliwa katika kijumba kidogo cha mchunga ng'ombe katikati ya milima ya Alps. Akiwa amelelewa katika mandhari ya hali ya asili na ya kuvutia, akili yake ilikuwa imevutiwa mapema na ukuu wa Mungu. Kando ya bibi yake alisikiliza visa vichache vya thamani vya Biblia alivyovikusanya huku na huko kutoka kwa watu mashuhuri na mapokeo ya kanisa.

Alipokuwa na umri wa miaka kumi na mitatu alikwenda Bem, mji uliokuwa na wasomi wengi na wenye kuheshimika nchini Uswisi. Hata hivyo, ilizuka hatari mahali hapa. Juhudi za makusudi zilifanywa na watawa kumshawishi ajiunge na nyumba nao. Na kwa uwezo wa Mungu baba yake alipata habari za mipango hiyo ya watawa. Aligundua kuwa ufanisi wa maisha yajayo ya mtoto wake ulikuwa hatarini, kwa hiyo alimwamuru arudi nyumbani.

Agizo lilitekelezwa, lakini kijana hakuridhika kuishi kwa muda mrefu kwenye bonde alikozaliwa, baada ya muda mfupi alirudi masomoni, huku kwa vipindi fulani akienda na wenzake kule Basel. Hapa ndipo Zwingli aliposikia kwa mara ya kwanza neema ya bure kwenye Injili ya Mungu. Alipokuwa akijifunza Kiyunani na Kiebrania hukoWittembach aliongozwa kwenye Maandiko Matakatifu, na hivyo ndivyo miali ya nuru ya mbinguni ilivyoingia katika mioyo ya wanafunzi aliokuwa anawafundisha. Alidai kuwa kifo cha Kristo ni fidia pekee kwa mwenye dhambi. Kwa Zwingli, maneno haya yalikuwa mwali wa kwanza wa nuru iliyotangulia mapambazuko.

Muda mfupi baadaye, Zwingli aliitwa kutoka Basel kwenda kwenye kazi yake ya kudumu. Kazi yake ya kwanza ilikuwa katika parokia iliyokuwa kwenye eneo la milima mirefu. Akiwa amewekwa wakfu kama kasisi, "alijitoa kwa moyo wake wote kuutafuta ukweli wa Mungu." [95]

[113] Kwa kadri alivyoyachunguza Maandiko, ndivyo ilivyodhihirika

[95] Wylie, bk. 8, ch.5.

kwa usahihi tofauti kati ya ukweli na uasi wa Kanisa la Roma. Alijisalimisha kwenye Biblia kama Neno la Mungu, linalojitosheleza peke yake, na kanuni isiyokosea. Aliona kuwa Biblia ni lazima ijifafanue yenyewe. Alitafuta kila msaada kupata uelewa sahihi na maana yake, na alikaribisha msaada wa Roho Mtakatifu. "Nilianza kumwomba Mungu anipatie nuru yake," baadaye aliandika, "na kwangu, Maandiko yakaanza kueleweka kwa urahisi." [96]

Mafundisho ya imani aliyokuwa akiyafundisha Zwingli hayakutoka kwa Luther. Yalikuwa ni mafundisho ya Kristo. Mwanamatengenezo huyu wa Uswisi alisema, "Ikiwa Luther anamhubiri Kristo anafanya kile ambacho mimi pia ninafanya....Hakuna neno lolote nililoliandika kwenda kwake, wala neno aliloliandika yeye kuja kwangu. Lakini kwa nini?...Ili ionekane namna Roho wa Mungu anavyofanya kazi, kwa kuwa sisi sote, bila kuwa tumekutana kwa vyovyote vile, tunafundisha maagizo ya Kristo kwa namna moja." [97] Mwaka 1516 Zwingli alialikwa kuhubiri kwenye nyumba ya watawa kule Einsiedeln. Kama Mwanamatengenezo, angeleta mvuto ambao ungeonekana hadi ng'ambo ya mipaka ya nchi yake aliyozaliwa huko Alps.

Kati ya vivutio vikubwa vilivyokuwa kule Einsiedeln, ilikuwa ni sanamu ya Bikira, iliyosemekana kuwa na nguvu za kutenda miujiza. Juu ya lango la kuingilia kwenye nyumba ya watawa yalikuwepo maandishi yaliyosema, "Ondoleo la dhambi zote linaweza kupatikana hapa." [98] Makundi ya watu yalikuja kwenye hekalu la Bikira kutoka sehemu zote za Uswisi, na hata wengine walitokea Ufaransa na Ujerumani. Zwingli alitumia fursa hiyo kutangaza uhuru kupitia Injili kwa watumwa hawa wa imani za mapokeo potovu.

Alisema, "Msidhani kuwa Mungu yumo ndani ya hekalu hili kuliko sehemu nyingine alizoziumba...Je, kazi zisizo na faida, safari ndefu za kwenda kuhiji, sadaka, sanamu, kumwomba msaada Bikira au watakatifu kunaweza kuwapatia neema ya Mungu?...itamfaa nini [114]
mtu kanzu inayong'aa, kichwa chenye upara, vazi refu na pana linalofunika mwili wote, ama makubadhi yaliyopambwa kwa dhahabu?" Alisema, "Ni Kristo, aliyetolewa msalabani mara moja,

[96] Ibid., bk. 8, ch. 6.

[97] D'Aubigne, bk. 8, ch. 9.

[98] Ibid., 8, ch. 5.

ni kafara na mhanga, ambaye alitosha kuziondoa dhambi zote za waaminio milele zote.” [99]

Kwa wengi ilikuwa ni masikitiko makubwa kuambiwa kwamba safari yao yenye kuchosha ilikuwa bure. Msamaha unaotolewa bure kwa njia ya Kristo hawakuufahamu. Walikuwa wameridhika na namna Kanisa la Roma lilivyowafundisha. Ilikuwa ni rahisi kutumainia wokovu wao kutoka kwa makasisi na Papa kuliko kutafuta usafi wa moyo.

Lakini kundi jingine lilipokea kwa furaha habari za wokovu kwa njia ya Kristo, na kwa imani waliipokea damu ya Mwokozi kwa ajili ya upatanisho. Hawa walirudi nyumbani kuwafunulia wengine nuru ya thamani waliyokuwa wameipokea. Hivyo ndivyo ukweli ulivyosambazwa kutoka mji mmoja kwenda mji mwingine na idadi ya mahujaji kwenda kwenye hekalu la Bikira ilipungua sana. Kulikuwa na kushuka chini kwa sadaka kwa kiwango kikubwa, na kusababisha kushuka kwa mshahara wa Zwingli uliopatikana kutoka kwenye sadaka hizo. Jambo hili lilimfurahisha sana Zwingli kuona nguvu za mapokeo potuvu zikivunjika. Ukweli uliendelea kukita mizizi katika mioyo ya watu.

### Zwingli Aitwa Kwenda Zurich

Baada ya miaka mitatu Zwingli aliitwa kwenda kuhubiri kwenye kanisa kuu la jimbo kule Zurich, mji muhimu katika shirikisho la Uswisi. Mvuto ambao ungewekwa hapa ungekuwa na mguso. Maaskofu walitangulia kumwelekeza wajibu wake:

“Utafanya kila jitihada kukusanya mapato ya baraza hili bila kuacha chochote kilicho kidogo...Ukusanye kwa juhudi mapato yanayotokana na wagonjwa, makundi ya watu, na kutoka kwa kila maagizo ya kanisa kwa ujumla. Kwa ajili ya kutoa sakramenti, kuhu-
[115] biri na kulitunza kundi...unaweza kumtumia mtu mwingine, na hasa kuhubiri.” [100] Zwingli alisikiliza kwa makini agizo hili na kujibu, “Kwa muda mrefu sana maisha ya Kristo yalikuwa yamefichwa kwa watu. Nitahubiri Injili yote ya Mtakatifu Mathayo...Ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu na sifa kwa Mwanawe, kwa wokovu halisi wa

[99] Ibid.

[100] Ibid., bk. 8, ch. 6.

roho za watu, na kuwajenga katika imani ya kweli, ili niiweke wakfu huduma yangu."

Watu walifurika kwa idadi kubwa kumsikiliza. Alianza huduma yake kwa kuzifungua Injili, huku akifafanua juu ya maisha, mafundisho, na kifo cha Kristo. "Ni shauku yangu kuwaongoza ninyi kwa Kristo,- kwenda kwa Kristo, chimbuko la kweli la wokovu." Watu maarufu katika nchi, wanazuoni, wasanii, na wakulima, waliyasikiliza maneno yake. Bila hofu yoyote, alikemea uovu na ufisadi wa wakati huo. Wengi walirudi nyumbani kutoka katika kanisa lile kuu wakimtukuza Mungu. "Mtu huyu," watu walisemezana, "ni mhubiri wa ukweli. Atakuwa Musa wetu kutuongoza kutoka katika giza hili la Misri." [101]

Baada ya muda fulani upinzani uliinuka. Watawa walianza kumshambulia vikali Zwingli kwa dhihaka na vicheko vya dharau, na wengine wakamtendea jeuri na vitisho. Lakini Zwingli aliyavumilia yote.

Mungu anapokusudia kuzivunja pingu za ujinga na mapokeo potovu, Shetani hufanya kazi kwa nguvu kubwa kuwafunika wanadamu kwa giza na kuikaza minyororo yao kwa uthabiti zaidi. Kwa nguvu mpya, Kanisa la Roma liliendelea kufungua masoko yake katika himaya yote ya Ukristo, likitoa msamaha wa dhambi kwa pesa. Kila dhambi ilikuwa na bei yake, na watu walipewa leseni za kufanya kila aina ya udhalimu ili mradi tu hazina ya kanisa ilikuwa imejaa vyema. Kwa jinsi hiyo vuguvugu hizi mbili zilisonga mbele- Kanisa la Roma likiruhusu dhambi na kuifanya kitega uchumi chake na Wanamatengenezo wakiishutumu dhambi na kuwaelekeza watu kwa Kristo kama kitulizo na mkombozi wao.

## Kuuzwa kwa Hati za Msamaha Nchini Uswisi [116]

Nchini Ujerumani, mauzo ya hati za msamaha wa dhambi yaliendeshwa na mtu mwovu kupindukia aliyekuwa anaitwa Tetzel. Na nchini Uswisi biashara hii ilikuwa ikisimamiwa na mtawa wa Kiitaliano aliyekuwa anaitwa Samson. Samson tayari alikuwa amekusanya kiasi kikubwa cha pesa na kuzijaza katika hazina ya utawala wa Papa kutoka nchini Ujerumani na Uswisi. Na kwa wakati huu alikwenda huku na huko nchini Uswisi akiwapora wakulima maskini

[101] Ibid.

mapato yao kidogo na kuwatoza matajiri vitu vya thamani. Mara moja Mwanamatengenezo huyo alijitosa kumpinga. Zwingli alifanikiwa sana kufunua unafiki wa mtawa huyu kiasi cha kumlazimisha kuondoka kwenda sehemu nyingine. Kule Zurich, Zwingli alihubiri kwa nguvu sana dhidi ya wachuuzi wa hati za msamaha wa dhambi, na Samson alipokwcnda mahali pale, alikutana na muuzaji wa vyeti kutoka katika baraza kukiwa na dalili kwamba alikuwa akitarajiwa kupita pale. Kwa werevu aliruhusiwa kuingia pale, lakini aliondoshwa bila kuuza cheti hata kimoja cha msamaha na baada ya muda mfupi aliondoka nchini Uswisi.

Mnamo mwaka 1519 tauni ama Janga Kuu la kifo liliikumba Uswisi. Wengi waliongozwa kujisikia jinsi zisivyofaa na zisivyokuwa na thamani yoyote hati za msamaha ya dhambi walizokuwa wamezinunua. Walitamani sana kupata msingi wa hakika wa imani yao. Kule Zurich, Zwingli aliugua sana, na taarifa zilienea kila sehemu ya kuwa alikuwa amekufa. Na katika saa hiyo ya kujaribiwa, aliuangalia kwa imani msalaba wa Kalivari, akitumainia upatanisho unaotosha kabisa dhidi wa dhambi. Aliponusurika kufa, alihubiri Injili kwa hamasa kubwa kuliko hapo kabla. Watu walikuwa wametoka kuwahudumia wagonjwa na wale waliokuwa wanakufa, na walijisikia hitaji la Injili kuliko ilivyokuwa hapo kabla.

Zwingli alikuwa ameelewa dhahiri ukweli wa Injili maana yeye mwenyewe alikuwa amepitia kikamilifu zaidi uwezo ya Injili wa kufanywa upya. Alisema, "Kristo amenunua kwa ajili yetu ukombozi usiokoma kamwe... Shauku yake kuu ni...kafara ya milele inayoleta uponyaji wenye matokeo yanayotakiwa na yasiyokoma, ambayo huridhisha haki ya Mungu milele kwa niaba ya wote wanaoitegemea kwa uthabiti na imani isiyoyumba... Popote palipo na imani kwa Mungu, shauku huja ya kusihi na kuwahimiza watu kutenda matendo mema." [102]

[117] Hatua kwa hatua, matengenezo yalikua kule Zurich. Kwa mshtuko wa hofu waliinuka kuleta upinzani mkubwa. Mashambulizi ya mara kwa mara yalifanywa dhidi ya Zwingli. Mwalimu wa uzushi ni sharti anyamazishwe. Askofu wa Constance aliwatuma wasaidizi wake watatu kwenda kwenye Baraza la Zurich, akimshitaki Zwingli kwa kuhatarisha amani na utaratibu katika jamii. Alisihi kuwa,

[102] Ibid., 8, ch. 9.

ikiwa mamlaka ya kanisa ingewekwa kando; vurugu ingetokea kila mahali.

Baraza lilikataa kumchukulia hatua Zwingli, kwa hiyo Kanisa la Roma likaanza kujiandaa kwa ajili ya mashambulizi mapya. Mwanamatengenezo huyu aliitikia kwa kusema: "Hebu na waje maana ninawaogopa kama vile jabali linaloning'inia linavyoyaogopa maji yanayoupiga msingi wake." [103] Juhudi za makasisi kutaka kuiangusha kazi ya Wanamatengenezo viliifanya iendelee kusonga mbele. Ukweli ulikuwa unaendelea kuenea. Nchini Ujerumani wafuasi wake waliokuwa wamekatishwa tamaa na kutoweka kwa Luther, walitiwa moyo tena walipoona maendeleo ya Injili nchini Uswisi. Matengenezo yalipokita mizizi kule Zurich matunda yake yalionekana kwa ukamilifu kwa kukomeshwa kwa uovu na kukuzwa kwa mfumo wa maisha yenye utaratibu.

### Mabishano Na Watawala wa Kanisa la Roma

Kwa kuona mafanikio kidogo yaliyopatikana kwa mateso ya kujaribu kukandamiza kazi ya Luther nchini Ujerumani, Watawala wa Kanisa la Roma waliamua kufanya mashindano ya maneno na Zwingli.Wangejihakikishia ushindi si tu kwa kuchagua sehemu ya kufanyia bali pia waamuzi na watu watakaoshiriki katika pambano hilo. Na ikiwa wangemtia Zwingli mikononi mwao, wangemlinda sana asije akawatoroka. Hata hivyo kusudi hili lilifanywa kwa kificho na uangalifu mkubwa.

Mabishano yalipangwa kufanyika kule Baden. Kwa kushuku [118]
makusudio ya watawala wa kanisa la Papa na likiwa limetahadharishwa na moto ulikuwa ukiwashwa kuwateketeza watu waliokuwa wakiikiri Injili kwenye majimbo yaliyokuwa chini yao; Baraza la Zurich lilimkataza mchungaji wao kujiingiza katika hatari hiyo. Kwenda Baden mahali ambapo damu ya wafiadini kwa ajili ya ukweli ilimwagwa, ilikuwa hakika ni kukiendea kifo. Waliochaguliwa kuwawakilisha Wanamatengenezo walikuwa ni Oecolampadius na Haller; wakati Dk. Eck akisaidiwa na kundi la madaktari wasomi na maaskofu, ndiye aliyekuwa mtetezi wa Kanisa la Roma.

Makarani wote walikuwa wamechaguliwa na watawala wa kanisa la Papa, na watu wengine hawakuruhusiwa kuandika cho-

[103] Wylie, bk. 8, ch. 11

chote, vinginevyo wangekabiliwa na kifo. Hata hivyo mwanafunzi fulani aliyekuwa akihudhuria kwenye mipango hiyo aliandika kila kilichokuwa kinajadiliwa kila siku. Karatasi hizi zilichukuliwa na wanafunzi na kupelekwa pamoja na barua zilizopelekwa kwa Oecolampadius na Zwingli kila siku kule Zurich. Mwanamatengenezo huyo alijibu na kutoa ushauri. Ili kuepuka macho ya walinzi wa malango ya mji, wajumbe hawa walikuja na vikapu vya kuku vichwani mwao na waliruhusiwa kupita bila kipingamizi.

Myconius alisema, "Zwingli amefanya kazi sana kuliko ambavyo angefanya kwa kujadiliana na mtu ana kwa ana katikati ya maadui zake, kwa tafakari zake, akipitisha nyakati za usiku bila kulala, na ushauri ule aliokuwa anaupeleka Baden." [104]

Wawakilishi wa Kanisa la Roma walikuja Baden wakiwa wamevalia mavazi yao ya fahari na vito vilivyokuwa vinang'aa. Walisafm kianasa, meza zao zilijaa vyakula vya gharama kubwa na mvinyo waliokuwa wakinywa ulikuwa wa viwango vya juu kabisa. Kulionekana tofauti kubwa kati yao na Wanamatengenezo ambao walikuwa wakitumia walivyokuwa navyo kwa uangalifu huku wakitumia muda mfupi katika meza ya chakula. Mwenye nyumba aliyokuwa anakaa Oecolampadius alitumia muda wake kufuatilia alichokuwa anafanya mpangaji wake na kugundua kuwa, mara nyingi alimkuta anasoma au anaomba, na kutoa taarifa ya kwamba alikuwa kwa kiasi fulani "Mcha Mungu sana."

[119] Kwenye mkutano ule, "Eck alisimama kwenye mimbari kwa majivuno makubwa akiwa amevalia mavazi ya fahari yaliyopambwa; wakati Oecolampadius aliyeonekana mnyenyekevu, aliyekuwa amevaa mavazi ya kawaida, alilazimishwa kuketi mbele ya mpinzani wake kwenye kiti kilichokuwa kimetengenezwa vibaya." Sauti kubwa na yenye kuunguruma ya Eck na moyo wa kujiamini aliokuwa nao havikumbabaisha. Yule ambaye angeitetea imani yake angepewa donge nono. Wakati alipotindikiwa na hoja za maana, Eck aligeukia matusi na kulaani.

Mwonekano wa Oecolampadius usioonesha majivuno na kujitumainia nafsi ulikuwa umenywea kwenye mabishano hayo. Japokuwa alionekana mpole na mwenye heshima, alithibitisha uwezo wake bila wasiwasi wala woga wowote. Kwa uthabiti, Mwanamaten-

[104] D'Aubigne, bk. 11, ch. 13.

genezo huyu aling'ang'ania kwenye Maandiko. Alisema, "Desturi hazina nguvu katika Uswisi yetu, vinginevyo ziwepo kwa mujibu wa katiba; na katika masuala ya imani, Biblia ndiyo katiba yetu." [105]

Utulivu aliokuwa nao Mwanamatengenezo huyu na jinsi alivyotoa hoja kwa ufasaha, alivyozitoa kwa upole na bila majivuno, aliwagusa watu kiasi cha kuyaona maneno ya Eck yasiyohakikishwa na yaliyokuwa yametolewa kwa majivuno kuwa karaha tupu.

Kwa siku kumi na nane mjadala uliendelea. Wawakilishi wa kanisa la Papa walidai kuwa walikuwa wameshinda. Wengi wa wabunge walisimama upande wa Kanisa la Roma, na baraza lote lilitamka ya kwamba Wanamatengenezo walikuwa wameshindwa vibaya na kutangaza ya kuwa wao pamoja na Zwingli walikuwa wametengwa kutoka katika kanisa. Hata hivyo majadiliano hayo yalisababisha mchocheo thabiti kwa Uprotestanti. Muda mfupi baadaye miji muhimu ya Bem na Basel ilitangaza kujiunga kwenye Matengenezo.

[105] Ibid.

[120] # Sura Ya 10 - MAENDELEO NCHINI UJERUMANI

Kutoweka kwa Luther kwa njia zisizoeleweka, kulichochea hofu na mshangao mkubwa kote nchini Ujerumani. Uvumi mbaya ulisambazwa na wengi waliamini kuwa alikuwa ameuawa. Kulikuwa na maombolezo makubwa, wengi walinuia kwa kiapo cha pekee kulipiza kisasi kwa kifo chake.

Ingawa mwanzoni walishangilia sana uvumi wa kifo chake, maadui wa Luther waliingiwa na hofu kwamba alikuwa mateka. Mmoja wao alisema, "Njia pekee iliyobakia kwa ajili ya kupona kwetu ni kuwasha myenge, na kumsaka Luther popote alipo duniani, na kumrejesha katika taifa linalomhitaji." [106] Habari ya kwamba alikuwa salama ingawaje alikuwa mfungwa ziliwafanya watu watulie, wakati huo huo Maandiko yake yakisomwa kwa shauku kubwa kuliko hapo kabla. Wengi walijiunga katika njia ya shujaa huyu aliyekuwa akililinda Neno la Mungu.

Mbegu alizokuwa amezipanda Luther zilichipuka kila mahali. Kutokuwepo kwake kulikamilisha kazi ambayo angekuwepo asingeweza kuifanya. Kwa kuwa kiongozi wao mkubwa alikuwa ameondolewa, watenda kazi wengine walisonga mbele ili kazi iliyokuwa imeanza vizuri isikwamishwe.

Shetani alianza kuwapotosha na kutaka kuwaangamiza watu kwa kuwashawishi kuamini maneno yasiyo kweli kwa kuwapatia kitu bandia mahali pa kazi ya kweli. Kama kulivyokuwa na makristo wa uongo kame ya kwanza, walitokea pia makristo wa uongo kwenye kame ya kumi na sita.

Watu wachache walijidhania kupokea ufunuo maalum kutoka mbinguni na kudai kuwa walikuwa wametumwa na Mungu kuendeleza Matengenezo, ambayo walidai, yalikuwa yameanzishwa kwa uhafifu na Luther. Lakini kwa kweli walikuwa wakiiharibu kazi
[121] aliyokuwa ameifanya. Waliikataa kanuni ya Matengenezo-kwamba Neno la Mungu lilikuwa linajitosheleza kabisa kama kanuni ya

[106] D'Aubigne, bk. 9, ch. 1.

imani na matendo. Mwongozo usiokosea waliubadili kwa viwango vyao vya hisia na maono yasiyoaminika.

Wengine waligeuka kwa urahisi na kujiunga na watu hawa wenye itikadi kali ya kidini. Shughuli za mashabiki zilileta msisimko mkubwa. Luther alikuwa amewaamsha watu kuona hitaji la matengenezo, na kwa wakati huu watu waliokuwa waaminifu walipotoshwa na hawa "manabii wapya wa kujifanya." Viongozi wa kundi hili walikwenda Wittemberg na kupeleka madai yao kwa Melanchthon: "Tumetumwa na Mungu kuwafundisha watu. Tumefanya mazungumzo ya karibu sana na Bwana; tunafahamu kile kitakachotokea; kwa kifupi, sisi ni mitume na manabii, na tuna maombi yetu kwa Dk. Luther."

Wanamatengenezo walichanganyikiwa. Melanchthon alisema, " Kuna roho asiye wa kawaida ndani ya watu hawa; lakini ni roho gani huyo?...Kwa upande mmoja, tunapaswa kuwa waangalifu tusije tukamzimisha Roho wa Mungu, na kwa upande mwingine tusije tukapotoshwa na roho wa Shetani." [107]

## Tunda la Mafundisho Mapya Ladhihirika

Watu waliongozwa kuipuuza Biblia au kuitupilia mbali kabisa. Wanafunzi walipiga teke vizuizi vyote, wakaachana na masomo yao na kuondoka katika Chuo Kikuu. Watu waliodhania kuwa walikuwa na uwezo wa kufanya uamsho na kuongoza jukumu la Matengenezo walifanikiwa tu kuyapeleka kwenye ukingo wa uharibifu. Watawala wa Kanisa la Roma walifanikiwa tena kumdisha matumaini yao na walishangilia kwa furaha huku wakitamka: "Bado pambano moja la mwisho, na yote yatakuwa ya kwetu."

Aliposikia kile kilichotokea akiwa Wartburg, Luther alisema kwa mguso: "Siku zote nategemea Shetani kutuletea pigo hili." [108] Alitambua tabia halisi ya "manabii hao wa kujifanya." Upinzani wa Papa na mfalme kwa wakati huu ulisababisha mkanganyiko [122]
mkubwa. Kutoka kwa marafiki waliokuwa wamekiri Matengenezo, waliibuka maadui wabaya sana waliokuwa wanachochea machafuko na kuleta mtafaruku.

[107] 107 Ibid. bk. 9, ch. 7.

[108] Ibid.

Luther alikuwa ameongozwa na Roho wa Mungu na alikuwa ametumiwa kuliko uwezo wake ulivyokuwa. Lakini mara kwa mara alitetemeka kwa matokeo ya kazi yake: "Kama ningetambua ya kwamba mafundisho yangu yalikuwa yamemjeruhi mtu mmoja, mtu mmoja tu; hata kama fundisho hilo lilikuwa duni na lisiloeleweka kiasi gani-jambo ambalo haliwezekani kwa sababu ni Injili yenyewe-ingekuwa heri nife mara kumi kuliko kuifuta kauli hiyo." [109] Jiji la Wittenberg lenyewe lilikuwa limeangukia mikononi mwa watu wenye itikadi kali ya kidini na vitendo vya kihalifu vilivyokithiri. Katika nchi yote ya Ujerumani, adui wote waliona kuwa Luther alihusika kwa vitendo hivyo. Kwa uchungu wa moyo Luther aliuliza, "Je, huo ndiyo unaweza kuwa mwisho wa kazi hii kubwa ya Matengenezo?" Alipokuwa akijibidisha kumwomba Mungu amani ilijaa na kufurika moyoni mwake. Alisema, "Kazi hii si yangu bali ni Yako." Aliazimia kurudi Wittenberg.

Alikuwa chini ya marufuku ya himaya ya Kanisa la Roma. Adui zake walikuwa na uhuru wa kuamua kuutoa uhai wake, marafiki walikuwa wamezuiwa kumpatia hifadhi. Lakini aliona kazi ya Injili ilikuwa hatarini, na kwa jina la Bwana aliondoka pasipo hofu yoyote kwenda vitani kwa ajili ya ukweli. Katika waraka aliomwandikia mbunge, Luther alisema, "Ninakwenda Wittenberg chini ya ulinzi wa juu kuliko ule wa wakuu na wabunge. Sihitaji kuomba msaada wako mheshimiwa, na sihitaji kabisa ulinzi wako, ingependeza zaidi kama mimi ningekulinda wewe."

Hakuna upanga wowote unaoweza kuendeleza kazi hii. Mungu pekee ndiye atakayefanya mambo yote." Katika waraka wake wa pili Luther aliongeza maneno haya: "Niko tayari kukukasirisha mheshimiwa na kuchukiwa na ulimwengu wote. Je, watu wa Wittenberg siyo kondoo wangu? Je, hainipasi, ikilazimu; kujitoa kufa kwa ajili yao?" [110]

## [123] Nguvu ya Neno

Mapema sana ilisikika katika mji wote wa Wittenberg kuwa Luther alikuwa amerudi na angehubiri. Kanisa lilijaa watu. Kwa busara ya hali ya juu na upole alifundisha na kukemea: "Misa ni

[109] Ibid.

[110] Ibid. bk. 9, ch. 8.

jambo baya; Mungu hapendi jambo hilo; inabidi lipigwe marufuku...Lakini mtu yeyote asiachishwe jambo hilo kwa nguvu...Neno la Mungu ni lazima lifanye kazi, sio sisi...Tuna haki ya kusema: hatuna haki ya kutenda. Kazi yetu ni kuhubiri; mambo mengine ni ya Mungu. Kama ningewashurutisha watu ningepata faida gani? Mungu ndiye agusaye moyo, na moyo unapokuwa umekamatwa; kila kitu huwa kimepatikana...

"Nitahubiri, nitazungumza, na nitaandika, lakini sitamlazimisha mtu yeyote, kwa sababu imani ni tendo la hiari...ninasimama kinyume na Papa, misamaha ya dhambi ya kununua, na utawala wa Papa na wafuasi wao, lakini pasipo kutumia nguvu wala ghasia. Ninaliweka mbele Neno la Mungu; Nilikuwa nahubiri na kuandika hayo yote ndiyo niliyokuwa nayafanya. Na bado nilipokuwa usingizini, neno nililokuwa nimelihubiri liliuangusha utawala wa Papa, hata hivyo si mwana mfalme wala mfalme aliyepata madhara makubwa. Mimi sikufanya chochote, Neno pekee ndilo lililofanya mambo yote." [111] Neno la Mungu lilivunja laana ya msisimko wa itikadi kali. Injili iliwarejesha katika njia ya ukweli watu waliokuwa wamepotoshwa.

Miaka kadhaa baadaye, itikadi kali ziliibuka zikiwa na athari za kutisha zaidi. Luther alisema, "Kwa watu hao Maandiko Matakatifu yalikuwa kama barua iliyokufa na wote walianza kupiga kelele, "roho! roho!" Lakini ninakuhakikishia sitakwenda kule roho wao anakowapeleka." [112]

Thomas Munzer, ni mtu aliyekuwa na bidii sana kati ya watu waliokuwa na itikadi kali. Alikuwa ni mtu mwenye uwezo mkubwa, lakini alikuwa hajajifunza dini ya kweli. "Alikuwa na shauku ya kufanya matengenezo ulimwenguni, lakini kama walivyo watu wengi wenye ari hiyo, alisahau kuwa inalazimika matengenezo yaanze na [124]
yeye mwenyewe." [113] Hakuwa tayari kushika nafasi ya pili baada ya kwa Luther. Alidai mwenyewe kuwa alikuwa ameagizwa na Mungu kuanzisha matengenezo ya kweli: "Mwenye roho huyu ana imani ya kweli, hata kama kamwe hatayaona Maandiko katika maisha yake." [114] Walimu wasiofaa walijitoa wenyewe kuongozwa

[111] Ibid.

[112] Ibid. bk. 10, ch. 8.

[113] Ibid. bk. 9, ch. 8.

[114] Ibid. bk. 10, ch. 10.

na maono, wakilichukua kila wazo na msukumo kama sauti ya Mungu. Wengine walidiriki hata kuchoma Biblia zao. Maelfu waliyapokea mafundisho ya Munzer. Mapema alitangaza ya kuwa kuwatii wakuu ilikuwa ni kujaribu kumtumikia Mungu na Shetani.

Mafundisho haya ya kimapinduzi ya Munzer yaliwaongoza watu kuasi kila mamlaka. Mandhari za kutisha na machafuko zilifuata, na maeneo mbalimbali nchini Ujerumani yaligubikwa na mauaji na umwagikaji wa damu.

### Masumbuko Makali Moyoni Sasa Vamshinikiza Luther

Wafuasi wakuu wa utawala wa Papa walidai kwamba uhalifu huo ulikuwa ni matunda ya mafundisho ya Luther. Shitaka hili lingemsababishia Mwanamatengenezo huzuni kuu ili kusudi la ukweli lifedheheshwa kwa kuwekwa kundi moja na uovu wa wenye itikadi kali. Kwa upande mwingine viongozi wa uasi walimchukia Luther. Si tu kwamba alikanusha madai yao ya kuvuviwa na Mungu lakini alisema kuwa walikuwa wameasi mamlaka ya serikali. Nao walimjibu kwa kisasi wakimshtumu kama mdanganyifu mkubwa.

Wafuasi wa Kanisa la Roma walitegemea kuporomoka kwa Matengenezo. Walimlaumu Luther hata kwa makosa aliyokuwa anajaribu kwa bidii kuyasahihisha. Upande wa wenye itikadi kali, walidai kwa udanganyifu kuwa hawakutendewa haki, walipata watu wa kuwaonea huruma na wakachukuliwa kama wafia dini. Hivyo ndivyo walivyotendewa wale waliokuwa wanapinga Matengenezo, walihurumiwa na kupongezwa. Hii ilikuwa ni kazi ya roho ileile ya uasi ambayo ilidhihirishwa kwanza kule mbinguni.

[125] Bila kukoma, Shetani anatafuta kuwadanganya wanadamu na kuwaongoza kuiita dhambi kuwa ni haki na haki kuiita dhambi. Utakatifu wa kughushi, utakaso wa uongo, bado vinaendelea kuonesha hadharani roho ileile kama ilivyokuwa siku za Luther, vikiivuta mioyo ya watu kutoka kwenye Maandiko Matakatifu na kuwaongoza wanadamu kufuata hisia na maono kuliko sheria ya Mungu.

Bila kuogopa, Luther aliilinda Injili kutokana na mashambulizi. Kwa kutumia Neno la Mungu alipambana na mamlaka iliyokuwa imetwaliwa na Papa, na wakati huo akisimama thabiti kama jabali dhidi ya wenye itikadi kali waliotaka kuungana na Wanamatengenezo.

Kila kimoja cha vikundi hivi vya upinzani kiliyaweka kando Maandiko Matakatifu, huku vikitukuza hekima ya kibinadamu kama chanzo cha ukweli. Imani katika mantiki huifanya akili kuwa sanamu na kulifanya hili kuwa kigezo cha dini. Dai la Kanisa la Roma kwamba wana uvuvio unaoanzia kwa mitume, huwapa fursa za kufanya ubadhirifu na ufisadi uliofichwa chini ya vazi la agizo la kitume. Uvuvio uliodaiwa kumshukia Munzer ulianza kutoka katika fikra na mawazo yasiyo na maana. Ukristo wa kweli hulipokea Neno la Mungu kama kipimo kuthibitisha uvuvio wa aina zote.

Aliporudi kutoka Wartburg, Luther alimalizia kutafsiri Agano Jipya, na baada ya muda mfupi baadaye, Injili ilitolewa kwa Wajerumani kwa lugha yao. Toleo hili liliwafurahisha sana waliokuwa wanapenda ukweli.

Makasisi waliingiwa na hofu walipotambua ya kwamba watu wa kawaida wangekuwa na uwezo wa kujadiliana nao Neno la Mungu na hivyo ujinga wao ungewekwa wazi. Kanisa la Roma lilitoa agizo kwa mamlaka yake kuzuia usambazaji wa Maandiko. Lakini kwa kadri Kanisa la Roma lilivyojaribu kupiga marufuku Biblia, ndivyo lilivyozidisha shauku ya watu kutaka kuelewa mafundisho yake. Wale walioweza kusoma walitembea nayo wala hawakuridhika mpaka hapo walipokuwa wamekariri sehemu kubwa ya Maandiko. Mara moja Luther alianza kutafsiri Agano la Kale.

Maandiko ya Luther yalipokelewa kwa namna moja mijini na [126]
katika vitongoji. "Kile walichokuwa wameandika Luther na wenzake, wengine walikisambaza. Baada ya kujithibitishia wenyewe uharamu wa wajibu waliokuwa wamepewa, ingawaje walikuwa hawalijui Neno la Mungu, ...watawa walikuwa wanaviuza vitabu vya Luther na wenzake. Kwa muda mfupi Ujerumani ikajaa Walnjilisti wa vitabu waliokuwa jasiri." [115]

## Kujifunza Biblia Kila Mahali

Wakati wa usiku walimu wa shule za vijijini waliyasomea kwa sauti makundi madogo ya watu waliokuwa wamekusanyika kwenye sebule za kuotea moto. Kwa kila jitihada baadhi ya watu; walisadikishwa ukweli. "Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga." Zaburi 119:130.

[115]Ibid. bk. 9, ch. 11.

Wafuasi wa Kanisa la Papa waliokuwa wamewaachia makasisi na watawa jukumu la kujifunza Maandiko; sasa waliwaita ili wayakanushe mafundisho mapya. Lakini, kwasababu ya kutojua kwao Maandiko, makasisi na watawa walishindwa kabisa. Mwandishi mmoja Mkatoliki alisema, "Kwa majonzi makubwa, Luther amewashawishi wafuasi wake kutoamini hekima yoyote isipokuwa Maandiko Matakatifu." [116] Makundi ya watu yalikusanyika kusikia ukweli uliokuwa ukitolewa na watu waliokuwa na elimu ndogo. Ujinga wenye kuaibisha wa wakuu ulidhihirika kwa hoja zao kujibiwa na mafundisho sahili kutoka katika Neno la Mungu. Wafanyakazi, askari, wanawake na hata watoto walikuwa na uelewa mpana wa Maandiko kuliko makasisi na madaktari waliofuzu.

Vijana wenye nia kuu walijitoa kujifunza, wakiyachunguza Maandiko na kujizoeza juu ya kazi za kale zilizoandikwa kwa ustadi. Wakiwa na akili zinazofanya kazi vizuri na bila mioyo ya hofu, vijana hawa walipata elimu ambayo kwa kipindi kirefu mtu yeyote asingeweza kushindana nayo. Katika mafundisho mapya, watu walikuwa wamepata mambo yaliyokidhi mahitaji ya mioyo yao, na waliwapa kisogo wale ambao, kwa muda mrefu, waliwalisha makapi yasiyofaa ya sherehe za mapokeo potovu na desturi za kibinadamu.

[127] Mateso yalipochochewa dhidi ya walimu wa ukweli, waliyakumbuka maneno ya Kristo: "Lakini watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine," Mathayo 10:23. Wakimbizi wangeweza kupata hifadhi na kukaribishwa na watu wakarimu, na kwa hiyo wangemhubiri Kristo pengine kanisani ama katika nyumba za watu binafsi au mahali pa wazi. Ukweli uliendelea kusambaa bila kipingamizi chochote.

Viongozi wa kanisa na serikali, bila mafanikio, waliwafunga gerezani, mateso, moto na upanga. Maelfu ya waumini walitia muhuri imani zao kwa damu yao, na bado mateso yalisaidia tu kueneza ukweli. Itikadi kali ambazo Shetani alijaribu kuungana nazo; zilileta matokeo dhahiri ya tofauti iliyokuwepo kati ya kazi ya Shetani na kazi ya Mungu.

[116] Ibid.

## Sura Ya 11 - Upinzani Wa Wakuu [128]

Mojawapo ya shuhuda zenye kuvutia zilizowahi kutolewa kwa ajili ya Matengenezo; ni upinzani walioutoa wakuu wa waliokuwa Wakristo nchini Ujerumani kwenye mkutano mkuu wa dini uliofanyika Spires mnamo mwaka 1529. Ujasiri na uimara wa watu hao wa Mungu, ulivipatia vizazi vilivyofuata-uhuru wa dhamiri, na kulipatia kanisa la Wanamatengenezo jina-Uprotestanti.

Uwezo wa Mungu ulikuwa umezuia nguvu zilizokuwa zinapinga ukweli. Charles V alikuwa amekamia kuponda ponda Matengenezo, lakini mara alipokuwa akinyanyua mkono wake kufanya hivyo, Mungu alikuwa akimlazimisha kuligeuzia pigo lake upande mwingine. Mara kwa mara katika wakati wa hatari, majeshi ya Waturuki yalionekana mpakani, au mfalme wa Ufaransa, ama Papa mwenyewe, alifanya vita naye. Katikati ya machafuko na ghasia za mataifa, Matengenezo yaliendelea kuimarika na kupanuka.

Hata hivyo mwishowe, watawala wa ngazi za juu wa mamlaka ya Papa walifanya makubaliano na Wanamatengenezo. Mfalme aliitisha Mkutano Mkuu wa kidini kule Spires mnamo mwaka 1529 kwa kusudi la kuuangamiza "uasi wa kidini". Endapo njia za amani zingeshindwa, Charles alikuwa amejiandaa kutumia upanga.

Kule Spires, wafuasi wa Kanisa la Papa walionesha waziwazi chuki yao dhidi ya Wanamatengenezo. Melanchthon alisema: "Sisi ni watu tunaochukiwa mno na tunaonekana kuwa takataka za ulimwengu; lakini Kristo atawaangalia watu wake walio maskini na kuwatunza." [117] Watu wa Spires walikuwa na kiu ya Neno la Mungu, bila kujali marufuku iliyokuwepo, maelfu walimiminika kwenye huduma zilizokuwa zikiendeshwa katika kanisa la mbunge wa Saksoni. Jambo hili liliiharakisha hali ya hatari. Taratibu juu ya uvumilivu wa kidini zilikuwa zimewekwa kisheria, na mataifa ya Kilnjili yaliamua kupinga kuingiliwa kwa haki zao. Luther hakuruhusiwa kuwepo kule Spires, lakini nafasi yake ilikuwa imejazwa [129]
na watendakazi wenzake pamoja na wakuu ambao Mungu alikuwa

[117] D'Aubigne, bk. 13, ch. 5.

amewasimamisha ili kulinda kusudio Lake. Kifo kilikuwa kimemwondoa Frederick wa Saxony, lakini mrithi wake aliyekuwa anaitwa John alikuwa ameyakaribisha Matengenezo kwa moyo wa furaha na kwa ujasiri mkubwa.

Mapadre waliyataka mataifa yaliyokuwa yameyapokea Matengenezo kujisalimisha kwenye sheria za Kanisa la Roma. Kwa upande wao, Wanamatengenezo hawakuridhia kuwa Kanisa la Roma, liyatawale tena mataifa yaliyokuwa yamepokea Neno la Mungu.

Hatimaye ilipendekezwa kuwa kwenye maeneo ambayo Matengenezo yalikuwa hayajaanzishwa, Sheria ya Worms ingeendelea kutumika; na ya kwamba "endapo watu hawangekubaliana na sheria hiyo pasipo hatari za kutokea uasi, wasifanye mageuzi hata kidogo, ... wasipinge kuadhimishwa kwa misa, wasimruhusu Mkatoliki kuwa Mlutheri " Uamuzi uliofanywa na mkutano huo, uliwaridhisha sana mapadre na maaskofu.

Endapo amri hii ingetekelezwa, "Matengenezo yasingeenea... na wala yasingeweza kujengwa kwenye misingi imara... ambamo tayari yalikuwa." [118] Uhuru ungepigwa marufuku. Kubadili dini kusingeruhusiwa. Matumaini ya ulimwengu yalionekana kutaka kuzimwa.

Upande wa Waprotestanti walitazamana kwa hofu wasijue la kufanya. "Nini kifanyike?" "Je, viongozi wa Matengenezo wajisalimishe na kukubaliana na agizo hilo?"...Wakuu wa Walutheri walikuwa wamehakikishiwa uhuru kwa shughuli za dini yao. Upendeleo wa aina hiyo hiyo ulikuwa umetolewa kwa watu wao, ambao kabla ya kupitishwa kwa uamuzi huo, walikuwa wamepokea ujumbe wa Matengenezo. "Je, jambo hili si la kuridhisha?"...

"Kwa furaha waliangalia kanuni iliyotumika kufikia mpango huu na walitenda kwa imani. Je, kanuni hiyo ilikuwa ni ipi? Ilikuwa ni haki ya Kanisa la Roma kushurutisha dhamiri na kuzuia
[130] maswali. Lakini je, haikuwa haki yao na watu wao waliokuwa Waprotestanti kuufurahia uhuru wa kidini? Ndiyo, ulikuwa upendeleo kama ilivyokuwa imesisitizwa katika mapatano, lakini si kama haki...Kukubaliwa kwa mapendekezo ya mapatano hayo ilikuwa ni kukiri ukweli kwa shingo upande ya kuwa uhuru wa dini ulikuwa un-

[118] Ibid.

apaswa kuishia tu kwa Wanamatengenezo wa Saxony; lakini kwenye maeneo mengine yote ya Himaya ya Kikristo; kuuliza maswali kwa uhuru na kukiri imani ya Wanamatengenezo yalikuwa ni makosa ya jinai ambayo adhabu yake ilikuwa kutupwa kwenye gereza la chini ya ardhi ama kufungwa kwenye nguzo na kuchomwa moto. Je, wangeridhia kuwa uhuru wa dini uwe wa sehemu fulani tu?...Je, Wanamatengenezo wangekiri kwamba watu hawa hawakuwa na hatia ya damu za watu mamia kwa maelfu, ambao kwa kutaka kufikia makubliano haya walilazimika kutoa uhai wao katika nchi zilizokuwa chini ya mamlaka ya Papa?" [119]

Viongozi hao walisema "Tulikatae agizo hili, katika masuala ya dhamiri uwingi hauna nguvu." Kulinda uhuru wa dhamiri ni wajibu wa serikali, na huu ni mpaka wa mamlaka yake katika masuala ya dini.

Wakatoliki walikuwa wamedhamiria kukomesha kile walichokiita "ukaidi wa makusudi." Wawakilishi wa miji iliyokuwa huru walitakiwa kutangaza ikiwa wangekubaliana na masharti yaliyokuwa yamependekezwa. Bila mafanikio waliomba jambo hili licheleweshwe. Karibu nusu nzima walikuwa upande wa Wanamatengenezo, wakifahamu kwamba msimamo wao huo ulikuwa unawaandaa kwa ajili ya mateso na shutuma za siku za usoni. Mmoja wao alisema, "Tunalazimika kulikana Neno la Mungu, ama- tuchomwe moto." [120]

## Msimamo Adilifu wa Wakuu

Ferdinand, aliyekuwa mwakilishi wa mfalme mkuu, alijaribu kutumia ustadi wa ushawishi. "Aliwasihi wakuu walipokee agizo, akiwathibitishia kuwa mfalme mkuu angewafurahia sana." Lakini watu hawa walimjibu kwa utulivu wakisema: "Tutamtii mfalme mkuu kwa kila jambo litakalochangia kudumisha amani na heshima kwa Mungu."

Hatimaye mwakilishi wa mfalme alitangaza ya kuwa, "njia moja [131]
tu ilikuwa imebakia kwao; kujisalimisha kwa uamuzi wa wengi." Na aliRomaliza kusema maneno hayo aliondoka bila kuwapatia Wanamatengenezo nafasi ya kujibu. "Walituma wawakilishi ili

[119] Wylie, bk. 9, ch. 15.

[120] D'Aubigne, bk. 13, ch. 5.

kumsihi mfalme arudi." Naye aliwajibu, "Ni jambo lililokwisha kuamuliwa, kutii ndiyo jambo pekee lililobakia." [121]

Upande wa mfalme ulikuwa ukijidanganya kwamba kusudio la mfalme na Papa lilikuwa thabiti na lile la Wanamatengenezo dhaifu. Iwapo Wanamatcngenezo wangetegemea msaada wa kibinadamu pekee; wasingekuwa na nguvu zozote kama wafuasi wa Kanisa la Papa walivyodhani. Lakini walikata rufaa "kutoka katika taarifa za Mkutano wa Kidini kwenda kwa Neno la Mungu, na kutoka kwa Charles mfalme kwenda kwa Yesu Kristo, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana."

Ferdinand alipokataa kuangalia kwa makini msimamo wa dhamiri zao, wakuu waliamua kumpuuza, na kupeleka hoja yao mbele ya baraza la taifa bila kuchelewa. Tamko zito lilipitishwa na kupelekwa kwenye mkutano mkuu.

"Kwa hati hii tunapinga... kwa niaba yetu na watu wetu, hatuko tayari kuridhia wala kuwa waaminifu kwa namna yoyote ile katika agizo lililopendekezwa, kwa kitu chochote kilicho kinyume na Mungu, na kwa Neno lake Takatifu, na kwa dhamiri zetu sahihi, kwa ajili ya wokovu wetu...Kwa sababu hii tunaikataa nira iliyolazimishwa kwetu.

... Wakati huohuo tunategcmea kuwa, mheshimiwa mfalme atatutendea sisi kama Mkristo anayempenda Mungu kuliko kitu chochote; na sisi wenyewe tunatangaza kwamba tuko tayari kumwonesha yeye, na ninyi watawala wetu wenye neema, upendo na utii wote mambo ambayo ni haki na wajibu wetu halali." [122]

Walio wengi walijawa na mshangao na hofu kwa ujasiri wa wapinzani. Mgawanyiko, machafuko, na umwagikaji wa damu vilionekana kutoepukika. Wakiwa wameutegemea mkono wa Mungu, Wanamatengenezo "walikuwa wamejawa na ujasiri na uthabiti."

[132] "Kanuni zilizotumika ndani ya upinzani huu mkuu ndizo zilizojenga tabia ya UprotestantL.Uprotestanti unaiweka nguvu ya dhamiri juu ya hakimu, na mamlaka ya Neno la Mungu juu ya kanisa linaloonekana...Wanasema pamoja na mitume na manabii kuwa, 'imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu.' Mbele ya taji ya kifalme ya Charles V, wanaiinua juu taji ya Yesu Kristo." [123]

[121] Ibid.

[122] Ibid. bk. 13, ch. 6.

[123] Ibid.

Upinzani uliofanywa kule Spires ulikuwa ni ushahidi mzito dhidi ya kutovumiliana kidini na utetezi wa haki ya watu wote kumwabudu Mungu kulingana na dhamiri zao wenyewe.

Uzoefu huu wa Wanamatengenezo waadilifu ni fundisho kwa vizazi vyote vitakavyofuata. Bado Shetani anapingana na Maandiko Matakatifu kufanywa mwongozo wa maisha. Katika zama zetu kuna haja ya kurudi kwenye kanuni kuu ya Uprotesanti- yaani Biblia, na Biblia pekee kama kanuni ya imani na wajibu. Shetani bado anafanya kazi kuangamiza uhuru wa dini. Nguvu ya mpinga Kristo ambayo wapinzani wa Spires waliikataa sasa inatafuta kurudisha upya mamlaka yake iliyopoteza.

### Mkutano wa Augsburg

Mfalme Ferdinand alikuwa amekataa kuwasikiliza Wakuu wa Kiprotestanti; lakini kwa kutaka kutuliza mafarakano yaliyokuwa yanavuruga ufalme wake, katika mwaka uliofuata baada ya Upinzani wa Spires, Charles V aliitisha mkutano wa kidini kule Augsburg. Alitangaza nia yake ya kuongoza kikao hicho mwenyewe. Viongozi wa Waprotestanti walialikwa kuhudhuria.

Madiwani walimsihi mbunge wa Saxony asiende kwenye mkutano huo: "Je, siyo kujihatarisha kwenda na kujifungia ndani ya kuta za mji na adui yako mwenye nguvu?" Lakini wengine kwa uadilifu walisema, "Hebu wakuu na wawe na ujasiri na Mungu kwa kuwatumia atainusuru kazi yake." Luther alisema, "Mungu ni mwaminifu, hatatuacha." [124]

Mbunge alianza safari kuelekea Augsburg. Wengi walikwenda [133]
huko na wenye nyuso zilizokuwa na huzuni na mioyo iliyokuwa na wasiwasi. Lakini Luther aliyekuwa amefuatana nao hadi Coburg, aliwatia shime imani yao kwa kuimba wimbo uliokuwa umetungwa kwenye safari hiyo, "Ngome Madhubuti ni Mungu Wetu." Wengi wa waliokuwa na mioyo mizito walichangamshwa kwa sauti tamu iliyokuwa inatia moyo.

Wakuu waliokuwa wamefanya matengenezo walikuwa wamedhamiria kutoa tamko la maoni yao, likiwa na ushahidi kutoka katika Maandiko na kuyatoa katika baraza hilo. Jukumu la kuandaa tamko hilo liliwekwa mikononi mwa Luther, Melanchthon, na washirika

[124] Ibid. bk. 14, ch. 2.

wao. Ungamo hili lilikubaliwa na Waprotestanti na walikusanyika na kuambatanisha majina yao katika waraka huo.

Wanamatengenezo walikuwa makini kuhakikisha kuwa kusudio lao halichanganywi na masuala ya kisiasa. Wakuu hao Wakristo walipoendelea kuweka sahihi zao kwenye Ungamo hilo, Melanchthon aliingilia kati na kusema, "Wanaotakiwa kupendekeza mambo haya ni wanateolojia na wachungaji na mambo mengine tuziachie mamlaka za wenye nguvu wa dunia hii." "La hasha!" mimi mniondoe humo. Nimedhamiria kwa ushupavu kufanya kile kilicho sahihi, pasipo kujisumbua mwenyewe juu ya taji yangu. Ninataka sana kumkiri Bwana. Kofia yangu ya ubunge na joho langu la ngozi si vya thamani kwangu kama msalaba wa Yesu Kristo." Alijibu John wa Saxony. Alipokuwa anachukua Kalamu, mmoja kati ya wakuu hao alisema, "Niko tayari ...kuachana na mali na maisha yangu endapo heshima ya Bwana wangu Yesu Kristo itanitaka kufanya hivyo." "Nitakuwa tayari kuwaacha watu wangu, vyeo na heshima zangu hata kuiacha nchi ya baba zangu na fimbo mkononi," na akaendelea kusema, "kuliko kuyapokea mafundisho mengine yoyote kuliko yale yaliyo katika Ungamo." [125]

Wakati uliokuwa umepangwa ulifika. Charles V akiwa amezungukwa na wabunge na wakuu alitoa nafasi kwa kuzungumza Wanamatengenezo Waprotestanti. Kwenye mkutano huo wa mwezi Agosti ukweli wa Injili uliwekwa wazi na makosa ya utawala wa Papa yalibainishwa. Siku hiyo ilitangazwa kuwa ni siku kuu kubwa kabisa ya Matengenezo, na moja ya siku tukufu sana katika historia ya Ukristo na wanadamu." [126]

[134] Mtawa wa Wittenberg alisimama mwenyewe kule Worms. Na mahali pake kwa sasa walikuwa wamesimama watu wakuu na wenye uwezo mkubwa kabisa katika himaya hiyo. "Nimefurahi kupita kawaida ya kwamba nimeendelea kuwa hai mpaka wakati huu muda ambao Kristo ametukuzwa na watu maarufu na wenye uwezo mkubwa, waliokiri imani katikati ya upinzani, na kwenye mkutano uliotukuka sana."

Lile ambalo mfalme alizuia lisihubiriwe kutoka katika mimbari lilitangazwa kutoka ikulu; kile ambacho wengi walikiona kuwa

[125]Ibid. bk. 14, ch. 6.
[126]Ibid. bk. 14, ch. 7.

hakikuwa kinafaa hata watumishi kukisikiliza; kilisikilizwa kwa mshangao na mabwana na wakuu wa ufalme. Wana wa wafalme na taji zao, walikuwa ndio wahubiri, na hotuba ilikuwa ni ukweli wa Mungu wa kifalme." [127] Tangu nyakati za mitume kamwe haijafanyika kazi kubwa ama kikiri imani kulikokuwa kunavutia zaidi."

Moja ya kanuni aliyoishikilia Luther kwa uthabiti na kuiendeleza ni kutotumia nguvu ya dola kusaidia kazi ya Matengenezo. Alifurahi kwa sababu Injili ilipopokelewa na wakuu katika ufalme; walipopendekeza kuunganisha nguvu kwa ajili ya ulinzi yeye alitangaza ya kuwa, "mafundisho ya Injili yatalindwa na Mungu peke yake... Kwa mtazamo wake, tahadhari zote za kisiasa zilizokuwa zimependekezwa zilikuwa zimesababishwa na hofu isiyo ya lazima na mashaka yanayotokana na dhambi." [128]

Baadaye alipokuwa anazungumzia muunganiko wa wakuu waliokuwa wamefanya matengenezo baada ya kufikiri kwa kina, Luther alisema ya kwamba, "silaha pekee katika vita hivi inabidi uwe "upanga wa Roho." Alimwandikia mbunge wa Saksoni: "Kwa dhamiri zetu, sisi hatutaweza kuuidhinisha ushirikiano uliopendekezwa. Msalaba Wakristo ni lazima ubebwe. Mheshimiwa usiwe na hofu. Tutatenda mambo makubwa zaidi kwa maombi yetu kuliko kile watakachofanya maadui zetu wote kwa majivuno yao." [129]

Kutoka mahali pa siri pa sala ilitokea nguvu ile iliyoutikisa [135]
ulimwengu wakati wa Matengenezo. Kule Augsburg, Luther, "hakupitisha siku bila kutoa wakfu angalau saa tatu kwa ajili ya maombi." Kwenye mahali pa siri chumbani kwake, alikuwa anasikika akiumimina moyo wake kwa Mungu kwa maneno yaliyojaa "ibada, kicho na tumaini." Alimwandikia Melanchthon akisema, "endapo jambo hili si la haki, achana nalo, na ikiwa kusudio hilo ni jema, kwa nini tushindwe kutimiza ahadi zake Yeye aliyetuagiza tulale bila hofu?" [130] Wanamatengenezo Waprotestanti walikuwa wamejenga juu ya Kristo. Milango ya kuzimu isingewashinda!

[127] Ibid.
[128] D'Aubigne, London ed., bk. 10, ch. 14.
[129] Ibid. bk. 14, ch. 1.
[130] Ibid. bk. 14, ch. 6.

[136] # Sura Ya 12 - Pambazuko Nchini Ufaransa

Upinzani kule Spires na Ungamo la Imani pale Augsburg vilifuatiwa na miaka ya giza na mapambano. Hatima ya Uprotestanti ilionekana kwenda kwenye uangamivu kwa sababu ulikuwa umedhoofishwa na mgawanyiko.

Lakini katika wakati ule ambapo mfalme alionekana kuwa mshindi dhahiri, hapo ndipo alipozidiwa nguvu. Hatimaye alilazimika kukubali kuvumilia mafundisho ambayo lengo lake kuu maishani lilikuwa ni kuyaangamiza. Aliyaona majeshi yake yakiangamia vitani, hazina yake ilikaukiwa, na falme nyingi zilizokuwa chini yake zilikuwa zinatishia kuasi, na kila mahali imani aliyokuwa akitaka kuikomesha ilikuwa inaendelea kupanuka. Charles V alikuwa akipigana na Mungu Mwenyezi. Mungu alikuwa amesema, "Iwe nuru," lakini mfalme alikuwa amekusudia giza lisivujwe. Huku akiwa amechoshwa sana na vita vya muda mrefu, aling'atuka toka kwenye kiti chake cha enzi na kwenda kujificha kwenye makazi ya watawa.

Wakati majimbo mengi kule Uswisi yalikuwa yamepokea imani ya matengenezo, wengine waling'ang'ania kanuni za imani za Kanisa la Roma. Mateso yalichochea vita vya wenyewe kwa wenyewe. Zwingli na wengine wengi waliokuwa wamejiunga kwenye matengenezo walianguka kwenye uwanja wa damu kule Cappel. Kanisa la Roma lilipata ushindi na katika maeneo mengi lilionekana kuyakomboa majimbo yote lililokuwa limeyapoteza. Lakini Mungu alikuwa hajasahau kazi yake ama watu wake. Kwenye maeneo mengine alinyanyua watendakazi kuendeleza matengenezo.

Nchini Ufaransa, mtu aliyekuwa wa kwanza kuipata nuru alikuwa ni profesa kwenye chuo kikuu cha Paris, aliyekuwa anaitwa Lefevre. Katika utafiti wake kwenye Maandiko ya kale, usikivu wake ulielekezwa kwenye Biblia, na alianzisha somo la Biblia miongoni mwa wanafunzi wake. Alikuwa amejitolea kuandaa historia ya watakatifu na wafia dini kama ilivyotolewa katika masimulizi ya kanisa na alikuwa ameifanya kwa sehemu kubwa, na katika muda

huo, alianza kufikiria kupata msaada kutoka kwenye Biblia, hivyo alianza kujifunza Biblia. Hapa alikutana na watakatifu si kama vile [137] wanavyoelezewa kwenye orodha ya Kanisa la Roma. Huku akiwa ameudhika kwa hilo, aliachana na jukumu alilokuwa amejitwisha na kujitoa kujifunza Neno la Mungu.

Mnamo mwaka 1512, kabla ya Luther au Zwingli kuanza kazi ya matengenezo, Lefevre aliandika, "Mungu hutupatia kwa njia ya imani ile haki ambayo kwa neema peke yake huwa tunahesabiwa haki hata uzima wa milele." [131] Na wakati alipokuwa anafundisha kwamba utukufu wa wokovu ni mali ya Mungu peke yake, pia alitangaza ya kuwa jukumu la kutii ni la mwanadamu.

Baadhi ya wanafunzi wa Lefevre walikuwa wakiyasikiliza kwa makini maneno yake na muda mrefu baada ya sauti ya mwalimu wao kunyamazishwa, wao waliendelea kuutangaza ukweli. Hivyo ndivyo alivyokuwa William Farel. Mwana wa wazazi waliokuwa wacha Mungu na mfuasi mwaminifu wa Kanisa la Roma, alikuwa anakasirika sana na kuwa na ari ya kuwaangamiza wale ambao wangediriki kulipinga kanisa. Baadaye alikuja kusema, "Ningesaga meno yangu mithili ya mbwa mwitu mwenye hasira, nilipomsikia mtu yeyote akizungumza maneno kinyume na Papa." Lakini kuwatukuza watakatifu, kuabudu kwenye madhabahu, na kuyapamba kwa tunu mahekalu matakatifu, hakukuleta amani moyoni. Kujisikia hatia ya dhambi kuliendelea kumsonga, hata matendo yote ya kitubio hayakuweza kuiondoa hali ya hatia. Aliyasikiliza maneno ya Lefevre. "Wokovu ni kwa neema." "Ni msalaba Wakristo peke yake uwezao kufungua malango ya mbinguni na kuyafunga malango ya kuzimu." [132]

Kwa uongofu kama ule wa Paulo, Farel aligeuka kutoka kwenye utumwa wa mapokeo na kwenda katika uhuru wa wana wa Mungu. "Badala ya moyo wa uuaji wa mbwa mwitu mkali," alirejea toka huko na anasema akiwa "mtulivu na mnyenyekevu na asiyedhuru kama mwanakondoo, baada ya moyo wake wote kuondolewa kwa Papa na kuutoa kwa Yesu Kristo." [133]

Lefevre alikuwa akisambaza nuru kwa wanafunzi, Farel alikuwa [138] anaendelea mbele kuutangaza ukweli mbele ya watu. Mtu mwenye

[131] Wylie, bk. 13, ch. 1.
[132] Ibid. bk. 13, ch. 2.
[133] D'Aubigne, bk. 12, ch. 3.

cheo kanisani, askofu wa Meaux, mapema aliungana nao. Walimu wengine walijiunga katika kuitangaza Injili, na ilipata wafuasi toka kwenye familia za wasanii na wakulima mpaka katika ikulu ya mfalme. Dada yake Francis wa Kwanza aliipokea imani ya matengenezo. Wakiwa na matumaini makubwa, Wanamatengenezo waliutazamia wakati ambao Ufaransa ingetekwa kwa Injili.

## Agano Jipya kwa Lugha ya Kifaransa

Lakini wasingeweza kuyafikia matumaini yao. Majaribu na mateso vilikuwa vikiwangojea mitume wa Yesu. Hata hivyo wakati wa amani ulikuja, ili waweze kupata nguvu za kukabiliana na kimbunga kilichokuwa mbele yao, na Matengenezo yalisonga mbele haraka. Lefevre alichukua jukumu la kutafsiri Agano Jipya; ni wakati huo Luther alipotua, kutoka mitamboni, Biblia ya Kijerumani kule Wittenberg, Agano Jipya kwa lugha ya Kifaransa lilichapwa pale Meaux. Baada ya muda mfupi, wakulima wa Meaux walikuwa na Maandiko Matakatifu mikononi mwao. Wafanyakazi kwenye mashamba, na mafundi kwenye karakana zao, walijipa moyo katika kazi zao ngumu za kila siku kwa kuzungumzia ukweli wa thamani wa Biblia. Ijapo walikuwa ni watu wa daraja la chini sana, wasio na elimu na wakulima wadogo wadogo wafanyao kazi zao kwa bidii, uwezo wa neema ya Mungu wa kubadilisha na kuinua juu ulionekana katika maisha yao.

Nuru iliyokuwa imewashwa Meaux ilitupa miali yake mbali. Idadi ya waongofu ilikuwa inaongezeka kila siku. Kwa kipindi fulani hasira isiyo na mipaka ya watawala ilizuiliwa na mfalme, lakini hatimaye utawala wa Papa ulishinda. Mti wa kuchomea watu ulisimamishwa tena. Wengi walishuhudia ukweli ndani ya miali ya moto.

Katika kumbi za majumba ya kifahari na ikulu kulikuwa na wana na mabinti wa kifalme waliouthamini ukweli kuliko utajiri, cheo, ama hata maisha yenyewe. Louis de Berquin, alikuwa amezaliwa kwenye nyumba ya kiungwana, alijitoa kujifunza, huku akiwa amelelewa vizuri na mwenendo safi, mtu asiye na lawama yoyote kimaadili "aliamua kuupamba uaminifu wake wote kwa kuupokea Ulutheri kwa chuki ya pekee." Kwa nguvu za Mungu aliongozwa

kusoma Biblia, na alichokikuta kule "si mafundisho ya Kanisa la Roma bali mafundisho ya Luther." Alijitoa kwa ajili ya Injili.

Wafuasi wa Kanisa Katoliki nchini Ufaransa walimtupa gerezani [139] kama "mwasi", lakini mfalme alimwachia huru. Kwa miaka mingi, Francis alikuwa anatanga tanga kati ya Roma na Matengenezo. Berquin alifungwa mara tatu na mamlaka za utawala wa Papa, na kuachiwa huru na mfalme aliyekuwa amekataa kumtoa mhanga kwa sababu ya chuki za watawala. Kwa kurudia rudia, Berquin alikuwa ameonywa kuhusu hatari iliyokuwa inamkabili nchini Ufaransa na walimsihi afuate nyayo za wale waliokuwa wamepata hifadhi na kuwa wakimbizi kwa hiari yao.

## Ujasiri wa Berquin

Ari ya Berquin ilikuwa inaendelea kuwa thabiti. Alidhamiria kuchukua hatua za ushupavu zaidi. Hatasimama tu kutetea ukweli, atakuwa anashambulia upotovu. Wapinzani wake wenye nguvu walikuwa ni watawa wasomi wa idara ya teolojia katika Chuo Kikuu cha Paris, moja ya mamlaka ya juu sana ya kidini katika taifa. Kutoka kwenye maandishi ya madaktari hawa, Berquin alipata mapendekezo kumi na mawili aliyoyatangaza hadharani kuwa "yalikuwa yanapingana na Biblia," na alimwomba mfalme awe mwamuzi kwenye ubishani huo.

Kwa furaha na kutaka kunyenyekesha kujikweza kwa watawa hawa, aliwaalika wafuasi wa Kanisa la Roma kukitetea kile wanachokiamini kupitia Biblia. Silaha hii ingewafaa kidogo sana; mateso na nguzo ya kuchomea watu moto vilikuwa ni silaha walizofahamu vizuri namna ya kuzitumia. Walijikuta karibu na kutumbukia kwenye shimo walilotaka kumtupia Berquin. Walitafuta namna ya kutoroka.

"Ni wakati ule sanamu ya bikira iliyokuwa katika moja ya kona za mtaa mmoja ilipoharibiwa." Makundi ya watu yalimiminika kwenda kwenye eneo hilo kwa hasira na maombolezo. Mfalme aliguswa sana na jambo hilo. "Haya ni matunda ya mafundisho ya Berquin," walilalamika watawa. Kila kitu kinaelekea kupinduliwa kwa njama za hawa Walutheri -dini, sheria, na ufalme wenyewe." [134]

Mfalme aliondoka Paris, na watawa waliachwa huru kutenda [140]

[134] Ibid.

wapendavyo. Berquin alishtakiwa na kuhukumiwa kifo, na ili Francis asiingilie kumwokoa, hukumu ilitekelezwa siku hiyo hiyo iliyokuwa imepitishwa. Mchana, mkutano mkubwa ulikusanyika kushuhudia tukio hilo, na wengi waliliangalia tukio hili kwa mshangao mkubwa kwa kuwa mhanga wa tukio hili alikuwa amechaguliwa toka kati ya watu bora na jasiri kabisa miongoni mwa familia za watu waungwana nchini Ufaransa. Mshangao, uchungu, kubeza, na chuki zilionekana kwenye nyuso zilizokuwa na simanzi kwa watu waliokuwa wanaongezeka, na juu ya uso wa mtu mmoja peke yake hakukuwa na dalili yoyote ya majonzi. Mfia dini huyo alikuwa anahisi uwepo wa Bwana wake.

Uso wa Berquin ulikuwa unang'aa kwa nuru ya mbinguni. Alikuwa amevaa "vazi lenye manyoya, jaketi la kubana la hariri, kitambaa chenye urembo na vazi la kubana la rangi ya njano lililofunika toka miguuni." [135] Alikuwa tayari kushuhudia imani yake mbele ya Mfalme wa wafalme na haikupaswa kuwepo dalili yoyote ya maombolezo kama kisingizio kwa furaha yake.

Kadri msafara ulivyokwenda taratibu kupitia mitaa iliyokuwa imejaa watu, watu walishangazwa na mwonekano wa ushindi mkubwa na wenye furaha aliokuwa nao. Walisema, "Anafanana na mtu yule anayekaa hekaluni, ambaye hutafakari kuhusu mambo matakatifu."

## Berquin Achomwa Moto

Kwenye nguzo ile Berquin alijitahidi kuwahutubia watu kwa maneno machache, lakini watawa walianza kupiga kelele huku askari wakigonganisha silaha zao na makelele yao yaliifunika sauti ya mfia dini. Hivyo mnamo mwaka 1529 mamlaka ya juu zaidi ya kanisa katika utamaduni wa Kifaransa, iliweka mbele ya umati wa watu waliokuwepo mwaka 1793 "kielelezo cha msingi cha kukabwa kwenye jukwaa la kunyongea maneno matakatifu ya yule anayekufa" [136] Berquin alinyongwa na mwili wake kuteketezwa kwa moto.

[141] Walimu wa imani ya matengenezo waliondoka na kwenda kwenye maeneo mengine. Lefevre alikwenda Ujerumani. Farel

[135] D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, bk 2, ch. 16.

[136] Wylie, bk. 13, ch. 9.

alirudi kusambaza nuru kwenye eneo alilokulia na mji wa kwao kule mashariki mwa Ufaransa. Ukweli aliokuwa anafundisha ulipata wasikilizaji. Alifukuzwa kutoka katika mji huo muda mfupi baadaye. Alikuwa anapita huku na huko katika vijiji akifundisha kwa siri kwenye makazi ya watu na kwenye maeneo ya maficho, akijihifadhi kwenye misitu na mapangoni kwenye sehemu alizokuwa akienda mara kwa mara alipokuwa mvulana.

Kama ilivyokuwa nyakati za mitume, mateso "yalikuwa yanasaidia tu kusambaza Injili." Wafilipi 1:12. Walipofukuzwa kutoka Paris na Meaux, "...wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno." Matendo 8:4. Hivyo ndivyo nuru ilivyokuwa inapenya kwenye majimbo mbalimbali nchini Ufaransa.

### Kuitwa kwa Calvin

Kwenye moja ya shule za mji wa Paris, kulikuwa na kijana mmoja mwangalifu, mkimya na mwadilifu katika maisha yake, aliyekuwa na juhudi kwenye mambo ya kiakili na moyo wa kujitoa katika mambo ya dini. Kipaji alichokuwa nacho na jinsi alivyokuwa anakitumia vilimfanya awe fahari ya chuo chake, na John Calvin alikuwa anatazamiwa kwa matumaini kuwa mmoja wa watetezi wenye nguvu kabisa wa kanisa.

Lakini nuru ya Mungu ilipenya kuta za usomi na mapokeo potuvu ambazo zilikuwa zimemfunga. Binamu yake na Calvin aliyekuwa anaitwa Olivetan alikuwa amejiunga na Wanamatengenezo. Ndugu hawa walikuwa wanazungumzia mambo yaliyokuwa yanauvuruga Ukristo. "Kuna dini mbili tu duniani," alisema Olivetan Mprotestanti. "Ile iliyoanzishwa na watu...ambamo watu wanajitumikia wenyewe kwa sherehe na matendo mema; nyingine ni dini iliyofunuliwa katika Biblia, inayomfundisha mwanadamu kutafuta wokovu bure kutoka kwenye neema ya Mungu peke yake."

"Sitapokea lolote kati ya mafundisho yako mapya, unafikiri kuwa mimi nimeishi kwenye makosa siku zangu zote?" [137] Akiwa peke yake chumbani Calvin alikuwa anayafikiria maneno ya bi- [142]
namu yake. Aliona kwamba hakuwa na mtetezi mbele za Mungu mtakatifu na mwenye haki. Matendo mema, kawaida na desturi za kanisa vyote havikuwa na uwezo wa kufanya upatanisho kwa ajili

[137] Ibid. bk. 13, ch. 7.

ya dhambi. Kukiri imani ya kanisa, kitubio havikuwa na uwezo wa kumpatanisha mtu na Mungu.

### Kushuhudia Mtu Akichomwa Moto

Siku moja alipokuwa ametembelea viwanja vya umma, Calvin alishuhudia "mwasi" mmoja akichomwa moto. Katikati ya mateso na kifo kiie cha kutisha chini ya laana ya kuogofya ya kanisa, mfia dini yule alidhihirisha imani na ujasiri aliokuwa nao. Yule kijana mwanafunzi aliona ukinzani kati ujasiri wa mfiadini na hali yake ya kuishi gizani na kukata tamaa. Alikuwa anafahamu ya kuwa "waasi" walikuwa wamejenga imani yao juu ya Biblia. Alidhamiria kuisoma ili agundue siri ya furaha yao.

Ndani ya Biblia alikutana na Kristo. "Ooh Baba" alilalama, "Kafara yake imetuliza ghadhabu yako; damu yake imeondoa uchafu wangu; msalaba wake umechukua laana yangu; kifo chake kimefanya upatanisho kwa ajili yangu...Umeugusa moyo wangu ili niyaone mambo mengine kuwa ni machukizo isipokuwa matendo ya Yesu." [138]

Aliamua kuyatoa maisha yake kwa ajili ya Injili. Lakini, yeye kwa asili alikuwa mwoga na alitaka sana kwanza kujitoa kwa masomo. Hata hivyo, juhudi walizozifanya marafiki zake kumsihi, hatimaye zilimfanya kuridhia kuwa mhubiri. Maneno yake yalikuwa kama umande unaoshuka kuiburudisha dunia. Kwa wakati huu alikuwa kwenye mji wa jimbo lililokuwa chini ya uangalizi wa binti mfalme aliyekuwa anaitwa Margaret, huyu akiwa anaipenda Injili, aliwawekea ulinzi waliokuwa wahubiri wa Injili. Calvin alianza kazi yake katika nyumba za watu. Wale waliokuwa wameusikia ujumbe waliwaambia wengine habari njema. Alisonga mbele huku akiweka msingi wa makanisa ambayo yangekuja kuzalisha mashahidi wa ukweli wasioogopa.

[143] Paris ingepokea mwaliko mwingine wa kuipokea Injili. Mwito wa Lefevre na Farel ulikuwa umekataliwa, lakini ujumbe ungesikika tena kwa madaraja yote ya watu katika mji huo mkuu. Mfalme alikuwa hajajiunga kwa ukamilifu na Kanisa la Roma dhidi ya Matengenezo. Margaret aliamua ya kwamba imani ya matengenezo ihubiriwe kwenye mji wa Paris. Alimwamuru mchungaji wa

[138] Martyn, vol. 3, ch. 13.

Kiprotestanti kuhubiri kwenye makanisa. Ijapo jambo hili lilikuwa limekatazwa na wakuu wa utawala wa Papa, binti mfalme alifungua wazi milango ya ikulu. Ilitangazwa ya kuwa kila siku kutakuwepo na mahubiri, watu walialikwa kuhudhuria. Maelfu walikuwa wanakusanyika kila siku.

Mfalme aliamuru kwamba mawili kati ya makanisa ya mji wa Paris yafunguliwe. Kamwe ilikuwa haijawahi kutokea mji ule kuguswa hivyo kwa Neno la Mungu. Kiasi, usafi wa moyo, utaratibu, na kufanya kazi kwa bidii vilikuwa vinachukua nafasi ya ulevi, uasherati, machafuko, na uvivu. Watu wengi waliipokea Injili, na wengi zaidi waliikataa. Wafuasi wa Kanisa la Roma walifanikiwa kuendelea kutawala. Makanisa yalifungwa tena, na nguzo ya kuchomea watu moto ilirudishwa tena mahali pake.

Calvin alikuwa bado mjini Paris. Mwishowe watawala walinuia kumkamata ili akateketezwe kwenye moto. Hakuwa anafikiria juu ya hatari iliyokuwa inamjilia wakati marafiki zake walipokuja kwa haraka chumbani mwake na habari ya kuwa wakuu walikuwa njiani kuja kumkamata. Na papo hapo watu walibisha hodi kwa nguvu kwenye lango la kuingilia. Hakukuwa na muda wa kupoteza. Marafiki waliwacheleweshа wale wakuu mlangoni, wakati wengine walimsaidia Mwanamatengenezo huyo kutokea dirishani, na aliharakisha kuelekea kwenye kijumba kidogo cha mfanyakazi mmoja aliyekuwa anapenda matengenezo. Alivaa mavazi ya mwenyeji wake ili kujificha asijulikane, akachukua jembe na kuliweka begani na kuanza safari yake. Alisafiri kuelekea upande wa kusini na kupata tena hifadhi kwenye milki ya Margaret.

Calvin asingekaa bila kazi kwa muda mrefu. Mara tu dhoruba ilipopungua, alitafuta eneo jipya la kazi kule Poitiers, mahali ambapo mawazo mapya yalikuwa yamepokelewa. Watu wa daraja zote waliisikiliza Injili kwa furaha. Kwa kadiri idadi ya wasikilizaji ilivyozidi kuongezeka, ilifikiriwa kwamba ilikuwa salama zaidi kuwa wanakutana nje ya mji. Pango lililokuwa limezungukwa [144]
kwa miti na majabali lilikuwa mahali kamili pa faragha na lilichaguliwa kuwa sehemu ya kukutania. Katika eneo hili lililokuwa limejitenga, Biblia ilikuwa inasomwa na kufafanuliwa. Hapa ndipo meza ya Bwana ilipoadhimishwa kwa mara ya kwanza na Waprotestanti nchini Ufaransa. Kutoka kwenye kanisa hili dogo walnjilisti waaminifu kadhaa walitumwa kupeleka Injili.

Kwa mara nyingine Calvin alirudi Paris, na kukuta karibu milango yote ya kazi imefungwa. Hatimaye aliamua kuondoka kwenda Ujerumani. Muda mfupi tu baada ya kuondoka kwake nchini Ufaransa, ghadhabu kali iliwakumba Waprotestanti. Wanamatengenezo wa Ufaransa waliamua kuupiga pigo mwenendo wa kishirikina wa Kanisa la Roma ambalo lingelishtua taifa lote. Kwa usiku mmoja, mabango yaliyokuwa yanashambulia misa yalibandikwa katika nchi yote ya Ufaransa. Vuguvugu hili lenye ari kubwa ambalo lilikuwa linaeleweka vibaya liliwafanya wafuasi wa Kanisa la Roma watoe sababu za kuhalalisha kuwaangamiza "waasi" kama wachochezi hatari dhidi ya ufalme na amani ya taifa.

Moja ya mabango hayo lilibandikwa kwenye mlango wa chumba cha mfalme. Kitendo cha ujasiri usiokuwa kifani wa kuingiza matamko ya kushtusha mbele ya mfalme kulichochea ghadhabu yake. Hasira yake ilitamkwa kwenye maneno haya ya kutisha: "Na wakamatwe pasipo kujali hali zao wote wanaoshukiwa kuwa waasi wamfuatao Luther. Wote nitawaangamiza." [139] Mfalme alikuwa amedhamiria kujiweka kikamilifu katika upande wa Kanisa la Roma.

## Enzi ya Hofu Kuu

Maskini wafuasi wa imani ya Wanamatengenezo waliokuwa wamezoea kuwakusanya waumini kwenye maeneo yao ya kukutania ya siri walikamatwa. Kwa tishio la kuua palepale kwenye nguzo ya kuchomea watu moto, mfalme aliagizwa kufanya kazi kama balozi wa Papa katika kila nyumba ya Mprotestanti pale mjini. Hofu ya moto ilitawala, mfalme alikuwa ameridhia kuwasaliti ndugu zake. Mpelelezi wa mfalme aliyekuwa anaitwa Morin, akifuatana na msal-
[145] iti, kimya kimya na polepole alikuwa anapita kwenye mitaa ya mji. Alipofika mbele ya nyumba ya Mlutheri, msaliti alikuwa anaonesha ishara, bila kutamka neno lolote. Msafara ulisimama, waliingia kwenye nyumba na watu wa familia ile wakiburutwa na kufungwa minyororo na msafara huu wa kutisha uliendelea mbele kuwasaka wahanga wengine wapya. "Morin aliufanya mji utetemeke...ilikuwa ni enzi ya hofu kuu." [140]

[139] D'Aubigne, bk. 2, ch. 30.

[140] Ibid. bk. 4, ch. 10.

Wahanga waliuawa kwa mateso makali, ilikuwa imeagizwa ya kwamba moto upunguzwe kuwaka kwake ili kurefusha muda wa maumivu yao. Wao walikufa kama washindi, uvumilivu na uaminifu wao haukutikiswa, amani yao ilikuwa angavu. Watesi wao walihisi kuzidiwa nguvu. "Paris yote iliwezeshwa kuona aina gani ya watu dhana mpya inaweza kuwatengeneza. Hakukuwa na mimbari kama rundo la kuni za kuchomea wafia dini. Furaha iliyotulia iliangaza kwenye nyuso za watu hawa walipokuwa wakipita... kwenda mahali pa kuuawa kwao...walikuwa wanasihi kwa sauti isiyoweza kupingwa kwa niaba ya Injili." [141]

Waprotestanti walishtakiwa kwa kupanga kuwaua Wakatoliki kinyama, kuipindua serikali na kumwua mfalme. Hakukuwa na chembe yoyote ya ushahidi uliotolewa kuthibitisha tuhuma hizo. Lakini, bado ukatili waliokuwa wanatendewa Waprotestanti wasio na hatia, vilikuwa vinaendelea kurundikana na kuongeza uzito wa adhabu, na kame zitakazofuata zingeleta maangamizi waliyokuwa wameyatabiri, juu ya mfalme, serikali na watu wake. Maangamizi hayo yaliletwa na makafiri na wafuasi wenyewe wa Ukatoliki. Kukandamizwa kwa Uprotestanti kungeiletea Ufaransa maafa haya makubwa.

Wasiwasi, kutoaminiana, na hofu vilikuwa vimeenea kwenye daraja zote za jamii. Mamia walikimbia kutoka Paris, wakimbizi walioondoka nchi ya kwao kwa matashi yao wenyewe, kwa sehemu kubwa wakitoa tangazo la kwanza kwamba walikuwa wanapendelea imani ya matengenezo. Wafuasi wa Kanisa Katoliki walikuwa wanawaangalia watu hawa kwa mshangao mkubwa kwa dhana kwamba walikuwa "waasi" ambao hawakuwashuku na ya kuwa walikuwa wanavumiliwa miongoni mwao.

## Uchapishaji Wapigwa Marufuku [146]

Francis I alikuwa akifurahia kuwakusanya kwenye baraza lake wasomi kutoka katika kila nchi. Lakini akiwa amepata msukumo wa kutokomeza "uasi wa kidini", kiongozi huyu wa wasomi alitoa agizo la kupiga marufuku uchapishaji katika nchi yote ya Ufaransa! Francis I anatoa mmoja kati ya mifano mingi katika historia ikionesha

[141] Wylie, bk.l3,ch. 20.

ya kwamba ustaarabu wa kisomi siyo kinga dhidi ya kutovumiliana kiimani na mateso.

Makasisi walidai kuwa tusi lililotolewa dhidi ya Mbingu kwa kulaani misa lisafishwe kwa damu. Januari 2, 1535 ilipangwa kwa ibada hiyo ya kuogofya. Mbele ya kila mlango ulikuwa umewashwa mwenge kwa heshima ya "sakramenti takatifu." Kabla ya mapambazuko msafara ulikuwa umejipanga kwenye ikulu ya mfalme.

"Mkate wa Ekaristi Takatifu ulikuwa umebebwa na askofu wa Paris, aliyekuwa amefunikwa kwa kivuli cha nguo cha kupendeza sana...Baada ya Ekaristi Takatifu alifuata mfalme...Francis I, katika siku hiyo hakuwa amevaa taji yake, ama vazi lolote la kitaifa." [142] Katika kila madhabahu alikuwa anainama kwa unyenyekevu, siyo kwa sababu ya maovu yaliyokuwa yameuchafua moyo wake, au ile damu isiyo na hatia iliyokuwa imenajisi mikono yake, lakini ati kwa sababu ya "dhambi ya kufisha" ya watu wake waliokuwa wamediriki kulaani misa.

Kwenye ukumbi mkubwa wa ikulu ya mfalme, mfalme alikuja na maneno yenye kugusa sana, akilaani kwa uchungu "maovu, makufuru, siku ya huzuni na fedheha zilizokuwa zimelipata taifa." Na alimwomba kila raia aliyekuwa mwaminifu kusaidia kuangamiza kabisa tauni ya "uasi wa kidini" iliyokuwa imetishia kuiharibu Ufaransa. Machozi yalikuwa yamesonga matamshi yake. Na mkutano wote ukalia, kwa nia moja wakitamka "Tutaishi na kufa kwa ajili ya dini Katoliki!" [143]

[147] "Neema iletayo wokovu" imefunuliwa, lakini Ufaransa iliyokuwa imemulikwa na mng'ao wake, wao wakaigeuzia upande mwingine,wakichagua giza badala ya nuru. Walikuwa wameuita ubaya wema na wema ubaya, mpaka walipokuwa wahanga wa kujidanganya kwa hiari yao wenyewe. Nuru iliyokuwa iwaokoe kutoka katika udanganyifu, kutoka katika kutoinajisi mioyo yao kwa hatia ya damu, kwa hiari yao walikuwa wameikataa.

Maandamano yalipangwa tena. "Kwa mbali kidogo majukwaa ya kuchomea watu yalikuwa yamesimamishwa na juu yake Wakristo fulani wa Kiprotestanti walitakiwa wachomwe moto wakiwa hai, na ilikuwa imepangwa ya kwamba kuni ziwashwe mara mfalme

[142] Wylie, bk. 13, ch. 20.

[143] D'Aubigne, bk. 4, ch. 12.

atakapokuwa amekaribia, na msafara ulipaswa kusimama kushuhudia adhabu hiyo.” [144] Kwa upande wao wahanga wa tukio hili walikuwa watulivu bila kuonesha wasiwasi wowote. Walipotakiwa kuikana imani yao, mmoja wao alijibu, “Ninaamini tu kile manabii na mitume walikuwa wanakihubiri, na kile ambacho watakatifu wote walikuwa wanakiamini. Imani yangu inatumaini katika Mungu kupingana na nguvu zote za kuzimu.” [145]

Walipofika ikulu, kutano lile la watu lilitawanyika, na mfalme na maaskofu walikwenda kupumzika, wakipongezana ya kwamba kazi ingeendelea mpaka hapo “uasi wa kidini” utakapokuwa umetokomezwa kabisa.

Injili ya amani ambayo Wafaransa walikuwa wameikataa, kwa hakika ingedhibitiwa kabisa, na matokeo ya kufanya hivyo yangekuwa ya kuogofya sana. Maandamano mengine yalipita kwenye mitaa ya Paris mnamo Januari 21, 1793. “Kwa mara nyingine, mfalme alikuwa mhusika mkuu; tena kulikuwa na ghasia na makelele, tena kilisikika kilio cha wahanga wengine zaidi, tena kulikuwa na majukwaa meusi ya kuchomea watu; tena mandhari ya siku ile ilimalizika kwa mauaji ya kutisha mno, Louis XVI alikuwa anapambana sambamba na walinzi wake wa gereza na wanyongaji wake, mmoja mmoja aliburutwa mbele kwenye kipande cha gogo, na pale walishikiliwa kwa nguvu zote hadi shoka liliposhushwa shingoni na kichwa kilichokuwa kimetenganishwa na kiwiliwili [148]
kiliendelea kuruka ruka juu ya jukwaa.” [146] Karibu na eneo hilo watu wapatao 2800 waliangamia kwa kukatwa vichwa vyao kwenye mashine ya kukatia vichwa vya wahalifu.

Matengenezo yalikuwa yameupatia ulimwengu Biblia iliyokuwa imefunguliwa. Upendo wa milele uliwafunulia wanadamu kanuni za mbinguni. Wafaransa walipokataa karama ya mbingu, walikuwa wamepanda mbegu ya uharibifu. Kwa sababu kila matokeo yana chanzo chake, utendaji wa kanuni hii isiyoepukika ulipelekea kwenye Mapinduzi na enzi ya hofli kuu.

Farel mtu jasiri na mwenye juhudi alilazimika kuikimbia nchi aliyozaliwa na kwenda Uswisi. Hata hivyo aliendeleza bidii na mvuto wake kwenye matengenezo nchini kwao Ufaransa. Akisaid-

[144] Wylie,bk. 13, ch. 21.

[145] D’Aubigne, bk. 4, ch. 12.

[146] Wylie, bk. 13, ch. 21.

iana na wakimbizi wengine, Maandiko ya Wanamatengenezo wa Ujerumani yalitafsiriwa katika lugha ya Kifaransa, pamoja na Biblia ya Kifaransa vilichapishwa kwa wingi. Vitabu hivi viliuzwa kwenye maeneo mbalimbali na kwa wingi na walnjilisti wa vitabu kule Ufaransa.

Farel alianza kazi yake kule nchini Uswisi kwa kujifanya mwalimu wa shule, huku kwa uangalifu mkubwa akifundisha ukweli wa Biblia. Wengine waliamini lakini makasisi walijitokeza na kuizuia kazi hiyo, watu waliokuwa na imani za kishirikina waliinuka na kuipinga kazi hiyo. "Hiyo haiwezi kuwa Injili ya Kristo," makasisi walisisitiza, "tunaona kuhubiriwa kwake hakuleti amani, ila vita." [147]

Alikwenda kutoka kijiji hadi kijiji, akivumilia njaa, baridi, na uchovu na kila mahali alikuwa anakabiliwa na hatari kubwa kwa uhai wake. Alikuwa anahubiri sokoni, makanisani na wakati mwingine kwenye mimbari za makanisa ya makao makuu ya dayosisi. Zaidi ya mara moja alipigwa karibu kufa. Bado alikuwa anasonga mbele. Alikuwa anafika miji iliyokuwa ngome ya uPapa mmoja baada ya mwingine akiyafungua malango yake kwa Injili.

[149] Farel alikuwa na shauku ya kuanzisha kipimo cha Uprotestanti kule Geneva. Endapo mji huu ungeongolewa, ungekuwa kitovu cha Matengenezo nchini Ufaransa, Uswisi, na Italia. Mingi ya miji na vitongoji vilivyokuwa vinauzunguka mji huu vilikuwa vimepokea Injili.

Aliingia Geneva akiwa na rafiki mmoja. Lakini aliruhusiwa kuhubiri hotuba mbili tu. Makasisi walimwita mbele ya baraza la kanisa, ambalo wao walikuja wakiwa na silaha zilizokuwa zimefichwa ndani ya mavazi yao, huku wamekamia kumuua. Genge la watu wenye hasira lilikuwa limekusanyika kuhakikisha kifo chake iwapo angeponyoka kutoka katika baraza. Hata hivyo, mahakimu na wanajeshi wenye silaha waliokuwepo hapo, waliokoa maisha yake. Alfajiri na mapema siku ilyofuata alisafirishwa kupitia ziwani kwenda mahali pa usalama. Hivyo ndivyo jitihada zake za kwanza za kuihubiri Injili Geneva zilipoishia.

Kwa ajili ya jaribio lililofuata chombo kingine duni kikichaguliwa- kijana mdogo mwenye mwonekano wa unyenyekevu kiasi

[147] Ibid. bk. 14, ch. 3.

kwamba hakuthaminiwa hata na marafiki waliokiri matengenezo. Lakini, mtu wa aina hiyo angefanya nini endapo Farel alikuwa amekataliwa? "Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu" 1 Kor. 1:27.

### Froment Mwalimu wa Shule

Froment alianza kazi yake kama mwalimu. Ukweli aliokuwa amewafundisha watoto shuleni walikuwa wanausimulia nyumbani. Muda si mrefu wazazi walikuja kusikiliza mafundisho ya Biblia. Agano Jipya na vitini vilikuwa vinagawiwa bure. Baada ya muda, mtendakazi huyu pia alilazimishwa kukimbia, lakini ukweli aliokuwa anafundisha ulibakia kwenye vichwa vya watu. Matengenezo yalikuwa yameanzishwa. Wahubiri walirudi na hatimaye ibada ya Kiprotestanti ilianzishwa mjini Geneva.

Mji ulikuwa umetangazwa kuwa na imani ya Matengenezo mara Calvin alipoyaingia malango yake. Alikuwa njiani kuelekea Bascl alipolazimishwa kupitia njia ya mzunguko iliyokuwa inapitia Geneva.

Katika ziara yake hii, Farel alikuwa ameuona mkono wa Mungu. Ingawaje Geneva walikuwa wameipokea imani ya matengenezo, bado kazi ya kuwaongoa watu ni lazima ifanyike moyoni kwa uwezo [150]
wa Roho Mtakatifu, na wala si kwa maagizo ya mabaraza. Ijapo watu wa Geneva walikuwa wamejitenga na mamlaka ya Roma, hawakuwa tayari kuachana na maovu yaliyokuwa yameshamiri chini ya utawala wake.

Kwa jina la Mungu, Farel alimwapisha kwa dhati mwlnjilisti kijana kubaki na kufanya kazi hapo. Calvin alikuwa amerudi nyuma kwa hadhari. Alikuwa ameogopa kukutana na watu jasiri na wapenda machafuko wa Geneva. Alikuwa na hamu ya kupata mahali palipotulia kwa ajili ya kujifunza zaidi, na kutoka mahali pale, kwa njia ya machapisho, ayaelekeze na kuyaimarisha makanisa. Lakini hakudiriki kukataa. Ilikuwa imeonekana kwake "ya kuwa mkono wa Mungu ulikuwa umenyooshwa kutoka mbinguni na kumkamata, na kumzuia asitoke mahali ambapo alikuwa tayari kuondoka." [148]

[148] D'Aubigne, bk. 9, ch. 17.

## Ngurumo ya Apizo la Kanisa

Apizo la utawala wa Papa lilinguruma dhidi ya Geneva. Ni kwa namna gani mji huu mdogo ungeweza kustahimili utawala huu msonge wenye nguvu uliokuwa umewalazimisha wafalme na wafalme wakuu kusalimu amri?

Ushindi wa kwanza wa Wanamatengenezo ulikuwa umepita, Roma iliyakusanya majeshi yake upya ili kufanya maangamizi. Chama cha watu katili mno, na waliokuwa na tabia mbaya sana cha Majesuti kilianzishwa, chama hiki kilikuwa na nguvu kuliko vyama vingine vyote vilivyokuwa vinatetea utawala wa Papa. Wakiwa hawana chembe yoyote ya huruma, na dhamiri zao zikiwa zimetiwa ganzi kabisa, hawakuwa wanajua kanuni yoyote, wala uhusiano na mtu yeyote isipokuwa ule wa chama chao. (Angalia Kiambatisho)

Injili ya Kristo ilikuwa imewawezesha wafuasi wake kuvumilia mateso, ama kutotishwa na baridi, njaa, kazi za sulubu, na ufukara,
[151] kutetea ukweli mbele ya mateso makali, kuwekwa kwenye magereza chini ya ardhi, au nguzo ya kuchomea watu moto. Ujesuti ulikuwa umewafundisha wafuasi wake kufanya mambo pasipo kutumia akili na kuwawezesha wao pia kuvumilia hatari kama hizo na kuipinga nguvu ya ukweli kwa silaha zote za udanganyifu. Hakuna uhalifu wowote mkubwa walioshindwa kuutenda, ama udanganyifu mbaya sana kuufanya, au kushindwa kujibadilisha sura ili kutimiza kusudi lao. Walikuwa wamejifunza hivyo kwa nia ya kuuangusha Uprotestanti na kuanzisha upya ubora wa utawala wa Papa.

Walijivika mavazi ya utakatifu, walikuwa wanatembelea magereza na mahospitali, wakiwahudumia wagonjwa na maskini, huku wakilichukua jina takatifu la Yesu, walikwenda huku na huko wakitenda mema. Lakini chini ya mwonekano huu wa nje usio na hatia walikuwa wameficha uhalifu na makusudi ya kutisha.

Ilikuwa ni kanuni ya msingi ya chama hiki kwamba matokeo ya mwisho wa jambo ndiyo yaliyohalalisha njia iliyotumika. Udanganyifu, wizi, kusema uongo baada ya kiapo cha kusema ukweli, mauaji ya watu maarufu, vilikuwa vinapongezwa kama vilikuwa vimefanywa kwa manufaa ya kanisa. Kwa kujigeuza umbo ili kudanganya, Majesuti walijipenyeza kwenye maofisi ya serikali, wakipanda vyeo mpaka kuwa washauri wa wafalme na kuzitengeneza walivyotaka sera za mataifa. Walikuwa watumishi ili

kuwapeleleza wakuu wao. Walianzisha vyuo kwa ajili ya wakuu na waungwana, na pia walianzisha shule kwa ajili ya watu wa kawaida. Watoto wa Waprotestanti walivutwa kutunza kanuni za kidini za Kanisa la Papa. Kwa hiyo ule uhuru wa mtu kufanya anavyotaka uliopatikana kwa taabu na kumwaga damu ulisalitiwa na watoto wao. Popote Majesuti walipokwenda walifanya uamsho wa utawala wa Papa.

Ili kuwapatia mamlaka makubwa, tangazo la Papa lilitolewa kuanzisha upya Mahakama ya Kanisa Katoliki. Mahakama hii ya kuogofya ilianzishwa na watawala wa Kanisa Katoliki, na mateso ya kutisha yasiyoweza kuvumiliwa mchana yalikuwa yanarudiwa kwenye magereza ya siri chini ya ardhi. Katika nchi nyingi maelfu kwa maelfu ya watu wema na wenye vipawa vya pekee sana wa mataifa, watu wenye akili na elimu kupindukia, waliuawa ama kulazimishwa kukimbilia katika nchi nyingine. **(Angalia Kiambatisho)**

### Ushindi kwa Wanamatengenezo [152]

Hizo ndizo njia Kanisa la Roma lilizitumia ili kuzima nuru ya Matengenezo na kurejesha ujinga na imani za kishirikina za Zama za Giza. Chini ya baraka za Mungu na utendaji kazi wa watu waadilifu aliowainua kuwa warithi wa Luther, Uprotestanti haukuangushwa. Haukupaswa kupata nguvu kutoka katika mikono ya wakuu. Mataifa madogo na dhaifu kabisa yaligeuka kuwa ngome imara. Ilikuwa ni mji mdogo wa Geneva; ilikuwa ni Uholanzi iliyokuwa inapigana na utawala wa kimabavu wa Hispania, nchi ya Sweden iliyo na baridi kali na isiyo na chochote, ndizo zilizoshinda kwa ajili ya Matengenezo.

Kwa karibu miaka thelathini, Calvin alikuwa akitenda kazi pale Geneva ili kuendeleza Matengenezo katika Ulaya yote. Si kwamba mwelekeo wake haukuwa na dosari ama mafundisho yake hayakuwa na makosa. Lakini alikuwa ni msaada katika kuusambaza ukweli uliokuwa na umuhimu wa pekee, kufanya Uprotestanti uendelee kuwepo kukabiliana na mawimbi ya kasi ya kurejea kwa utawala wa Papa, na kukuza usafi na usahili katika maisha.

Kutokea Geneva, machapisho na walimu walikwenda kusambaza mafundisho ya matengenezo. Kutoka hapa waliokuwa wanateswa kwenye nchi zote walipata maelekezo na kutiwa moyo. Mji wa

Calvin ulikuwa kimbilio la usalama kwa Wanamatengenezo wote waliokuwa wanawindwa kwenye eneo lote la Ulaya ya Magharibi. Walikuwa wanakaribishwa na kuhudumiwa vizuri, walipopata makazi hapa waliubariki mji ulio wa asili kwa ujuzi, elimu, na kwa kicho chao kwa Mungu. Mwanamatengenezo shujaa wa Scotland aliyekuwa anaitwa John Knox, Waprotestanti wengi walioitwa Puritans wa Uingereza, Waprotestanti wa Uholanzi na Hispania, na Waprotestanti wa Ufaransa waliokuwa wanaitwa Hugenots, waliuchukua mwenge wa ukweli kutoka Geneva na kwenda kuuangaza kwenye giza lililokuwa kwenye nchi walizokuwa wamezaliwa.

# Sura Ya 13 - Uholanzi Na Scandinavia [153]

Kule Uholanzi udikteta wa uPapa ulipata upinzani mapema. Miaka mia saba kabla ya Luther, maaskofu wawili bila woga wowote walionesha kutokuwa na imani na Papa wa Roma. Maaskofu hawa walikuwa wametumwa kama mabalozi kwenda Roma na huko walijifunza tabia halisi ya "utawala wa Papa": "Umejiingiza mwenyewe kwenye hekalu la Mungu; badala ya kuwa mchungaji, umekuwa mbwa mwitu kwa kondoo.... Ulitakiwa kuwa mtumishi wa watumishi, kama unavyojiita mwenyewe, lakini wewe unajaribu kujifanya bwana wa mabwana...Unayafanya maagizo ya Mungu kudharauliwa." [149]

Kame kwa kame wengine waliinuka kutoa mwangwi wa upinzani huu. Biblia ya lugha ya Waldensia ilitafsiriwa aya kwa aya kwenda katika lugha ya Kidachi. Walitangaza "kwamba kulikuwa na faida kubwa ndani yake; hakukuwa na masihara, hadithi za kubuni, wala vitu visivyo na thamani wala udanganyifu, isipokuwa maneno ya kweli." [150] Hivyo ndivyo walivyoandika marafiki wa imani ya kale, katika kame ya ishirini.

Mateso yaliyofanywa na Kanisa la Roma yalianza; hata hivyo waumini walikuwa wanazidi kuongezeka, wakisema kuwa Biblia ni mamlaka pekee isiyokosea kidini na kwamba "hakuna mtu atakayelazimishwa kuamini isipokuwa kuongolewa kwa njia ya mahubiri." [151]

Mafundisho ya Luther yalipata watu waaminifu na wenye bidii katika kuihubiri Injili nchini Uholanzi. Menno Simons alipata elimu yake kama muumini wa Kanisa Katoliki na aliwekwa wakfu kama padre, hakufahamu lolote kuhusu Biblia na alikuwa ameogopa kuisoma kwa sababu ya hofu ya kuwa mwasi. Alifanya ubadhirifu kutaka kuinyamazisha sauti ya dhamiri yake, lakini bila mafanikio. [154]

[149] Gerald Brandt, History of the Reformation in and About the Low Countries, bk. 1, p. 6.

[150] Ibid., p. 14.

[151] Martyn, vol. 2, p. 87.

Baada ya kitambo, aliongozwa kujifunza Agano Jipya; na hili pamoja na Maandiko ya Luther vilimfanya apokee imani ya matengenezo.

Kitambo kidogo alishuhudia kuuawa kwa mtu aliyekuwa amebatizwa mara nyingine. Hili lilimwongoza kujifunza Biblia kuhusiana na ubatizo wa watoto wadogo. Alijifunza kwamba toba na imani ni masharti ya ubatizo.

Menno alijiondoa katika Kanisa Katoliki la Roma na kuyatoa maisha yake kufundisha ukweli aliokuwa ameupokea. Kote Ujerumani na Uholanzi kundi la waumini wenye itikadi kali lilikuwa limechipuka, wakivuruga utaratibu na uzuri wa maisha na kuendelea mbele kufanya maasi. Kwa juhudi thabiti Menno aliyapinga mafundisho yao ambayo hayakuwa sahihi na njama za kinyama za watu hao. Kwa miaka ishirini na mitano alikuwa akienda huku na huko katika Uholanzi yote na katika sehemu ya kaskazini mwa Ujerumani akiweka juhudi zenye mvuto uliokuwa unasambaa, akiishi maisha yaliyo kielelezo kulingana na mafundisho aliyokuwa anayatoa. Alikuwa mwaminifu, mnyenyekevu, mwungwana, mkweli, na mwenye bidii. Watu wengi waliongolewa kwa jitihada zake.

Nchini Ujerumani Charles V alikuwa amepiga marufuku Matengenezo, lakini wana mfalme walikuwa wamesimama kinyume na udikteta wake. Nchini Uholanzi uwezo wake ulikuwa mkubwa. Amri za mateso zilikuwa zinafuatana kwa haraka haraka. Kusoma Biblia, kuisikiliza ikisomwa au kuhubiri, kumwomba Mungu kwa siri, kuachana na kusujudia sanamu, kuimba Zaburi yalikuwa ni makosa ya kuhukumiwa adhabu ya kifo. Maelfu waliangamia mikononi mwa Charles na Philip II.

Wakati fulani familia nzima ililetwa mbele ya waendesha mashtaka, wakishtakiwa kwa kutoshiriki misa na kufanya ibada zao nyumbani. Kijana mdogo kuliko wote kwenye familia ile alijibu: "Huwa tunapiga magoti na kumwomba Mungu atie nuru kwenye akili zetu na atusamehe dhambi zetu, huwa tunamwombea mfalme wetu, ili ufalme wake upate kustawi na maisha yake yawe yenye furaha; tunawaombea mahakimu wetu ili Mungu awatunze." Baba wa familia ile na kijana wake mmoja walihukumiwa kufa kwa kuchoma moto kwenye nguzo. [152]

[152] Wylie, bk. 18, ch. 6.

Siyo wanaume peke yao lakini wanawake na wanawali walionesha ujasiri usioyumba. “Wake walikuwa wanasimama kando ya nguzo za kuchomea moto waume zao, na wakati mume alipokuwa anauvumilia moto, alikuwa ananong’oneza maneno ya kutia moyo ama kuimba Zaburi kupunguza majonzi yake.” Wanawali walikuwa wanalala kwenye makaburi yao wakiwa hai kana kwamba walikuwa wanaingia vyumbani mwao kulala wakati wa usiku, ama kwenda kwenye majukwaa ya moto ya kuchomea watu na mavazi yao yaliyo mazuri sana ka na kwamba walikuwa wanakwenda kwenye arusi zao.” [153] [155]

Mateso yalikuwa yanaongeza idadi ya mashahidi wa ukweli. Mwaka baada ya mwaka mfalme alikuwa anaendeleza kazi yake ya ukatili, lakini bila mafanikio. Hatimaye William wa Orange aliruhusu uhuru wa kumwabudu Mungu huko Uholanzi.

## Matengenezo Nchini Denmark

Katika nchi za upande wa Kaskazini Injili iliingia kwa amani. Walipokuwa wanarudi nyumbani kutoka chuoni, wanafunzi wa Wittemberg walikuja nchini Skandinavia na imani ya matengenezo. Maandiko ya Luther yalikuwa yanasambaza nuru pia. Watu shupavu wa upande wa kaskazini waliachana na ufisadi na imani za kishirikina za Kanisa la Roma na kuukaribisha ukweli wa Biblia utoao uzima.

“Mwanamatengenezo wa Denmark” aliyekuwa anaitwa Tausen, akiwa bado mvulana, alionesha uhodari mkubwa kiakili kwa kujiunga kwenye makazi ya watawa. Mtihani ulidhihirisha kwamba alikuwa na karama zilizo matumaini mema katika utumishi wa kanisa. Kijana huyo aliruhusiwa kuchagua Chuo cha kujiunga nacho kilichoko Ujerumani au Uholanzi, lakini kwa sharti moja: hakutakiwa kwenda Wittemberg kwenye uwezekano wa hatari ya uasi. Ndivyo watawa walivyosema.

Tausen alikwenda Cologne, mji ulio moja ya ngome za Kanisa [156]
la Roma. Kukaa hapa kwa muda mfupi alikuwa amechafuliwa moyo. Na kwa wakati huohuo alisoma Maandiko ya Luther kwa furaha na alikuwa na shauku kubwa kupata mafundisho binafsi ya

[153] Ibid.

Mwanamatengenezo huyu. Kwa kufanya hivyo alikuwa anahatarisha msaada kutoka kwa wakuu wake. Baada ya muda mfupi sana alifanya maamuzi na kuwa mwanafunzi wa Wittemberg.

Aliporudi kwao Denmark hakuifunua siri yake, lakini alidiriki kuwaongoza marafiki zake kwenye imani safi. Alikuwa anaifungua Biblia na kuwafundisha habari za Kristo tumaini la pekee la wokovu kwa mwenye dhambi. Mkuu wa nyumba ya watawa alighadhabika maana alikuwa ameweka tumaini kwake kwamba atakuwa mtetezi wa Kanisa la Roma. Mara moja aliondolewa katika nyumba yake ya kitawa na kuwekwa kizuizini chumbani kwake.

Kutoka katika vizuizi vya chumba chake Tausen alikuwa anawasiliana na rafiki zake kuhusu elimu ya ukweli. Endapo mapadre hawa wa Denmark wangekuwa na uelewa wa mpango wa kanisa wa kushughulikia "uasi wa kidini", sauti ya Tausen isingesikika tena, kwa hiyo badala ya kumfungia katika magereza ya chini ya ardhi, walimfukuza toka katika makao ya watawa.

Amri ya mfalme iliyokuwa imetolewa muda mfupi uliokuwa umepita, ilitoa ulinzi kwa walimu waliokuwa wanafundisha mafundisho mapya. Makanisa yalikuwa yanamkaribisha, na watu walikuwa wanafurika kuja kumsikiliza. Agano Jipya kwa lugha ya watu wa Denmark lilikuwa linasambazwa kwenye maeneo mengi. Juhudi za kutaka kuiangusha kazi hiyo zilisaidia tu kuieneza, na kwa muda mfupi Denmark ilitangaza kuipokea imani ya matengenezo.

## Maendeleo Nchini Sweden

Kule Sweden pia, vijana kutoka Wittemberg walikwenda na maji ya uzima kwa watu wa nchi yao. Viongozi wawili wa Matengenezo wa Sweden, Olaf na Laurentius Petri, walikuwa wamejifunza chini ya Luther na Melanchthon. Kama alivyokuwa Mwanamatengenezo mkuu, Olaf alikuwa akiwagusa watu kwa ustadi wake wa kuzungumza, wakati Laurentius, kama alivyokuwa Melanchthon,
[157] alikuwa ni mtu mtulivu na mwangalifu sana. Wote walikuwa thabiti na wasioogopa. Mapadre wa Kanisa Katoliki waliwachochea watu waliokuwa hawajui chochote na wenye imani za kishirikina. Mara kadhaa Olaf Petri aliponea chupuchupu kuuawa. Hata hivyo Wanamatengenezo hawa walikuwa wanalindwa na mfalme ambaye alikuwa amedhamiria imani ya matengenezo iendelee na alikuwa

amewakaribisha wasaidizi hawa wenye uwezo kwenye pambano dhidi ya Kanisa la Roma.

Mbele ya mfalme na viongozi mbalimbali wa nchi ya Sweden, kwa uwezo mkubwa Olaf Petri aliitetea imani ya matengenezo. Alisema kwamba mafundisho ya mababu yapokelewe tu iwapo yatakubaliana na Maandiko; na kwamba mafundisho ya misingi ya imani yametolewa kwenye Biblia kwa njia dhahiri, ili watu wote waelewe. Shindano hili linatumika kutuonesha kuwa "watu waliokuwa wa kawaida ndiyo waliokuwa wameunda jeshi la Wanamatengenezo. Hawakuwa watu wasiojua kusoma na kuandika, ama wafuasi wa vikundi mbalimbali vya kidini au wabishani wenye makelele-hawakuwa watu wa aina hiyo. Walikuwa watu waliosoma Neno la Mungu na kujua vyema kuzitumia silaha walizokuwa wamepewa na Biblia. Walikuwa wasomi na wanateolojia, watu waliokuwa wameutawala mfumo wote wa ukweli wa Injili, ambao walishinda kwa urahisi dhidi ya wapotoshaji wa mafundisho na wakuu wa Kanisa la Roma." [154]

Mfalme wa Sweden aliipokea imani ya Kiprotestanti, na bunge la nchi hiyo liliunga mkono hoja hiyo. Kwa kibali cha mfalme ndugu hao wawili waliitafsiri Biblia yote. Ilikuwa imeamriwa kwenye mkutano wa kidini kuwa katika ufalme wote wachungaji wafundishe Maandiko na watoto wafundishwe kusoma Biblia shuleni.

Kukombolewa kwa taifa hili kutoka kwenye ukandamizaji wa [158] Kanisa la Roma, kulilifanya kufikia ukuu na uthabiti ambao ulikuwa haujafikiwa hapo kabla. Kame moja baadaye, taifa hili lililokuwa dhaifu-taifa pekee katika Ulaya yote liliisaidia Ujerumani kujikomboa toka kwenye pambano la kuogofya la Vita vya Miaka Thelathini. Ulaya ya Kaskazini yote ilikuwa inaonekana kumdishwa tena kwenye utawala wa kidikteta wa Kanisa la Roma. Majeshi ya Sweden yaliiwezesha Ujerumani kupata ushindi wa kuvumiliwa kwa Waprotestanti na kurejesha uhuru wa dhamiri katika nchi zilizokuwa zimepokea imani ya Matengenezo.

[154] bid., bk. 10, ch. 4.

[159] # Sura Ya 14 - Maendeleo Ya Ukweli Uingereza

W akati Luther anaifungua Biblia iliyokuwa imefungwa kwa watu wa Ujerumani, Tyndale alikuwa anahimizwa na Roho wa Mungu kufanya yayo hayo nchini Uingereza. Biblia ya Wycliffe ilikuwa imetafsiriwa kutoka kwenye Maandiko ya Kilatini, yaliyokuwa na makosa mengi. Gharama za nakala za miswada ilikuwa kubwa mno kiasi cha kufanya usambazaji wake kuwa mdogo.

Mnamo mwaka 1516, Agano Jipya lilichapishwa kwa mara ya kwanza katika lugha yake ya asili, yaani Kigiriki. Makosa mengi ya nakala zilizokuwa zimepita yalisahihishwa, na Maandiko yalikuwa yanaeleweka vizuri na kwa uwazi zaidi. Hili liliwaongoza wengi wa wanazuoni kuelewa vizuri elimu ya ukweli na kutoa msukumo mpya kwa kazi ya matengenezo. Kwa kiasi kikubwa, watu wa kawaida walikuwa wamezuiwa kulipata Neno la Mungu. Tyndale alikuwa amalizie kazi ya Wycliffe kwa kuwapatia watu wake Biblia.

Bila hofu yoyote alihubiri kile alichokuwa anakiamini. Tyndale alilijibu dai la Kanisa Katoliki kwamba lilikuwa limetoa Biblia na kuwa kanisa peke yake ndilo lililokuwa linaweza kifafanua Biblia kwa kusema: "Si kweli kwamba ninyi ndiyo mliotupatia Maandiko; ninyi ndiyo mliokuwa mmeyaficha Maandiko kwa ajili yetu; ninyi ndiyo mnaowachoma moto wale wanaoyafundisha, na kama mngeweza, mngekuwa mmeyachoma Maandiko." [155]

Mahubiri ya Tyndale yaliamsha hamasa kubwa. Lakini mapadre walikuwa wanajaribu kuiharibu kazi yake. "Nini kifanyike?" kwa mshangao alitamka. "Siwezi kuwa kila mahali, Oh! Endapo Wakristo wangekuwa na Maandiko Matakatifu kwa lugha zao, wao wenyewe wangewakabili wapotoshaji hawa. Bila Biblia haitawezekana kuwaimarisha watu wa kawaida kwenye ukweli." [156]

[160] Kusudio jipya liliingia moyoni mwake. "Injili haiwezi kunena kwa lugha ya Kiingereza miongoni mwetu? Inalipasa kanisa kuwa

[155] D'Aubigne, History of the Reformation of the Sixteenth Century, bk. 18, ch.4.
[156] Ibid.

na nuru kidogo wakati mchana kuliko wakati wa mapambazuko?... Ni lazima Wakristo walisome Agano Jipya kwa lugha ya kwanza." [157] Ni kwa njia ya Biblia peke yake watu watauelewa ukweli.

Mkatoliki msomi aliyekuwa akibishana naye alitamka kwa mshangao, "Tulikuwa watu bora bila sheria za Mungu kuliko bila kuwa na sheria za Papa." Tyndale alimjibu, "Ninamdharau Papa na sheria zake zote; na endapo Mungu atatunza maisha yangu, kabla ya miaka mingi nitamfanya mvulana anayelima kwa kutumia plau kujua zaidi Maandiko kuliko ninyi." [158]

## Tyndale Atafsiri Agano Jipya kwa Kiingereza

Mateso yalimlazimisha Tyndale kukimbia nyumbani na kwenda London alikofanya kazi bila kubughudhiwa kwa kipindi fulani. ICwa mara nyingine tena wafuasi wa Kanisa la Roma walimlazimisha kukimbia. Ilikuwa inaonekana kwamba Uingereza yote ilikuwa haihitaji kumpokea. Kule Ujerumani alianza kuchapa Agano Jipya kwa lugha ya Kiingereza. Alipokatazwa kuchapa katika mji mmoja alikwenda kwenye mji mwingine. Hatimaye alifika mji wa Worms, mahali ambapo miaka michache kabla yake, Luther alikuwa ameitetea Injili mbele ya baraza la kidini. Kwenye mji huo marafiki wa imani ya Matengenezo walikuwa wengi. Hapa kwa kipindi kifupi nakala elfu tatu za Agano Jipya zilikamilika, na toleo lingine lilifuata.

Neno la Mungu lilisafirishwa kwa siri kwenda London na kusambazwa katika nchi nzima. Wafuasi wa Kanisa la Roma walijaribu kuukandamiza ukweli bila ya mafanikio. Askofu wa Durham alinunua nakala zote za Biblia toka kwa mwuza vitabu kwa nia ya kwenda kuziharibu, akidhania kwamba jambo hilo lingekwamisha kazi. Pesa hiyo iliyokuwa imetolewa ilinunua mali ghafi kwa toleo jipya na bora zaidi. Baadaye Tyndale alipokuwa amefungwa, aliahidiwa kuachiliwa huru kwa sharti moja, ataje majina ya waliokuwa wamemsaidia kugharimia uchapaji wa Biblia.

Alijibu kuwa askofu wa Durham alikuwa amechangia pesa [161]
nyingi kuliko mtu mwingine yoyote kwa kununua Biblia zilizokuwa zimebaki kwa bei kubwa.

[157] Ibid.

[158] Anderson, Annals of the English Bible (rev.edition, 1862), p. 19.

Hatimaye Tyndale aliishuhudia imani yake kwa kifo cha mfia dini; lakini silaha alizokuwa ameziandaa ziliwasaidia askari wengine kupigana vita kwa kame nyingi, mpaka katika wakati wetu.

Kutoka katika mimbari, Latimer aliendelea kusema kwamba, Biblia inapaswa isomwe na watu kwa lugha yao. “Hebu tusiiache njia, lakini turuhusu Neno la Mungu lituongoze: wala tusienende... kama mababu zetu, wala tusiache kutafuta kujua walichokuwa wanafanya, lakini pia kile walichokuwa wanatakiwa kufanya.” [159]

Viongozi wa imani ya Matengenezo nchini Uingereza, Bames na Frith, Ridley na Cranmer walikuwa wasomi walioheshimika sana kwa juhudi zao ama kicho chao kwa Mungu kwenye jamii ya waumini wa Kanisa la Roma. Upinzani wao kwa utawala wa Papa yalikuwa ni matokeo ya ufahamu wao kuhusu makosa ya “Mamlaka ya Papa.”

## Maandiko Matakatifu-Mamlaka Isiyokosea

Kanuni kuu iliyokuwa inadumishwa na Wanamatengenezo hawa ilikuwa ni ileile iliyokuwa inashikiliwa na Wawaldensia, Wycliffe, Huss, Luther, Zwingli, na wale waliokuwa nao-“Maandiko Matakatifu-Mamlaka isiyokosea.” Kwa mafundisho yake, walipima mafundisho na madai yote. Imani katika Neno la Mungu iliwastahimilisha watu hawa watakatifu walipotoa uhai wao kwa kuchomwa moto. “Jipeni moyo,” alisema Latimer kwa mfia dini mwenzake wakati moto ulipokuwa unakaribia kuwanyamazisha, kwa neema ya Mungu, “katika siku kama hii, tutawasha mshumaa kama huu nchini Uingereza, na ninaamini hautazimishwa.” [160]

Kwa mamia ya miaka baada ya kanisa la Uingereza kusalimu amri kwa Kanisa la Roma, makanisa ya Scotland yalidumisha
[162] uhuru wao.Hata hivyo kwenye kame ya kumi na mbili utawala wa Papa ulikuwa umeimarishwa na katika kila nchi giza kuu la kiroho lilikuwa limetanda. Bado miali ya nuru ilikuwa inakuja kulipenya giza hilo. Wakitokea Uingereza wakiwa na Biblia na mafundisho ya John Wycliffe, wafuasi wa Wycliffe walikuwa wamefanya mambo makubwa ya kutunza maarifa ya ukweli wa Injili. Kuanza kwa Matengenezo kulifuatana na Maandiko ya Luther na

[159] Hugh Latimer, “First Sermon Preached Before King Edward VI.”

[160] Works of Hugh Latimer, vol. I, p. xiii.

Agano Jipya kwa lugha ya Kiingereza lililokuwa limetafsiriwa na Tyndale. Wajumbe hawa wa kimya walikwenda huku na huko milimani na mabondeni wakiwasha upya mwenge wa ukweli uliokuwa umekaribia kuzimika na kuharibu kazi ya ukandamizaji iliyokuwa imefanywa kwa kame nne.

Walipoishtukia hatari hiyo, viongozi wa Kanisa Katoliki waliwapeleka kwenye nguzo ya kuchomea moto baadhi ya watu waadilifu kabisa wa wana wa Sotland. Mashahidi hawa waliokuwa wanakufa katika nchi yote walikuwa wanaisisimua mioyo ya watu kwa kusudi lao lisilokoma la kuvitupilia mbali vifungo vya Kanisa la Roma.

## John Knox

Hamilton na Wishart, na wafuasi wao wengi na wanyenyekevu, walitoa maisha yao kuchomwa moto. Kutoka katika rundo la majivu ya kuni zilizomteketeza Wishart kwa moto, alitokea mtu mmoja ambaye asingenyamazishwa na miali ya moto, mtu mmoja aliyekuwa anaongozwa na Mungu angekuja kuukomesha utawala wa Papa nchini Scotland.

Alipoachana na mapokeo ya kanisa John Knox aligeukia kujilisha ukweli wa Neno la Mungu. Mafundisho ya Wishart yalithibitisha azma yake ya kulitelekeza Kanisa la Roma na kujiunga na Wanamatengenezo waliokuwa wanateswa.

Marafiki zake walikuwa wanamsihi kuhubiri lakini yeye alikuwa amenywea kwa sababu ya uzito wa wajibu huo. Baada ya siku zilizokuwa na mgongano wa kuhuzunisha katika nafsi yake, alikubali. Mara alipokubali alisonga mbele kwa ujasiri na bila woga wowote. Mwanamatengenezo huyu mwaminifu alikuwa haogopi uso wa mwanadamu. Alipokutana uso kwa uso na malkia wa Scotland, John Knox hakuwa mtu wa kurubuniwa kwa miPapaso ya mahaba wala hakuwa mtu wa kutetemeka kwa vitisho. Malkia alidai kuwa Knox, [163]
alikuwa amewafundisha watu kuipokea dini iliyokuwa imepigwa marufuku na serikali, na kwa hivyo alikuwa amelivunja agizo la Mungu linalowataka raia kuwatii wakuu wao. Kwa uthabiti alijibu, “Endapo wazao wote wa Ibrahimu wangekuwa wafuasi wa dini ya Farao, watu ambao walikuwa kwa muda mrefu chini ya utawala wao, ninakuuliza mheshimiwa, ni dini ya aina gani ingekuwepo duniani?

Au endapo watu wote waliokuwepo wakati wa mitume wangekuwa wafuasi wa wafalme wa Rumi, ni dini aina gani ingekuwepo juu ya uso wa dunia?"

Mariamu alimwuliza mwanamatengenezo: "Nyie wanamatengenezo mnayafasili Maandiko Matakatifu kwa namna nyingine, na kanisa Kikatoliki nao wanayafasili kwa njia nyingine, nani nimwamini kati yenu, na ni nani atakuwa mwamuzi kwa hilo?"

"Inakulazimu umwamini Mungu, hilo limenenwa waziwazi katika neno lake," alijibu Mwanamatengenezo huyo. "Neno la Mungu ni rahisi na linajifafanua lenyewe; iwapo itatokea kwa sehemu fulani fumbo au kutoeleweka, Roho Mtakatifu, ambaye hajipingi mwenyewe, hulifafanua kinagaubaga neno hilo katika sehemu nyingine za Maandiko." [161]

Kwa ujasiri mkubwa Mwanamatengenezo huyu asiyeogopa chochote, kwenye hatari kubwa iliyokuwa inamkabili, alisonga mbele na kusudi lake hadi kuhakikisha Scotland imekombolewa kutoka katika utawala wa Papa.

Huko Uingereza kuanzishwa kwa Uprotestanti kama dini ya taifa kulikuwa kumefifia, lakini jambo hilo halikuyamaliza kabisa mateso. Nyingi kati ya desturi za Kanisa la Roma walibaki nazo. Utawala wa Papa ulikuwa umekataliwa lakini mahali pake mfalme alitawazwa kuwa kiongozi wa kanisa. Walikuwa wameucha sana usafi wa Injili. Uhuru wa dini ulikuwa bado haujaeleweka sawasawa. Ijapo unyama uliokuwa unatumiwa na Kanisa la Roma waliuacha na kwa nadra vitendo hivyo vilikuwa vinafanywa na watawala wa Kiprotestanti, bado haki ya kila mtu kumwabudu Mungu kulingana na dhamiri yake haikutambuliwa. Waliokuwa wanajaribu kumwabudu Mungu kwa namna tofauti waliendelea kuteswa kwa mamia ya miaka.

[164]

## Maelfu ya Wachungaji Watimuliwa

Katika kame ya kumi na saba maelfu ya wachungaji walifukuzwa na watu walizuiliwa kuhudhuria kwenye mikutano ya kidini ambayo haikuwa imeidhinishwa na kanisa. Kwenye maficho yaliyokuwa yamesitirika msituni, wana wa Mungu waliokuwa wanateswa walikuwa wanakusanyika kuimimina mioyo yao kwa sala na sifa kwa Mungu. Wengi walikuwa wanateseka kwa sababu ya imani yao.

[161] David Laing, the Collected Works of John Knox, vol. 2, pp. 281, 284.

Magereza yalikuwa yamejaa watu na familia zilikuwa zimesambaratika. Na mateso yasingenyamazisha ushuhuda wao. Wengi walifukuzwa kupitia baharini na kwenda Amerika na kule waliweka misingi ya uhum wa kiraia na kidini.

Kwenye gereza la chini ya ardhi lililokuwa limejaa wahalifu, John Bunyan alikuwa anadokeza mbingu ilivyo na hapa ndipo alipoandika mashairi yake ya ajabu juu ya safari ya mahujaji kutoka kwenye nchi ya uharibifu kwenda katika mji wa mbinguni. *Safariya Mahujaji na Neema Tele kwa Mwenye Dhambi Mkuu* ni mashairi ambayo yamewaongoza watu wengi kwenda katika njia ya uzima.

Katika wakati wa giza la kiroho Whitefield na jamaa ya Wesley walionekana kuwa wachukua nuru wa Mungu. Kadri kanisa lilivyokuwa linazidi kuimarika, ndivyo watu walivyokuwa wanateleza kwenda katika hali ambayo ingekuwa vigumu sana kuwatofautisha na watu wasiomcha Mungu. Watu wa daraja la juu walikuwa wanadhihaki utauwa; na watu wa daraja la chini walikuwa wameachwa waishi katika uovu. Kanisa halikuwa na ujasiri au imani kuwasaidia waliokuwa wameanguka kutoka kwenye njia ya kweli.

## Kuhesabiwa Haki kwa Njia ya Imani

Fundisho kuu lililokuwa linafundishwa kwa uwazi zaidi na Luther la kuhesabiwa haki kwa njia ya imani, lilikuwa linaelekea kusahaulika kabisa; kanuni ya Kanisa la Roma la kutumainia matendo mema ili kuokolewa lilikuwa limechukua nafasi yake. Whitefield na wafuasi wa Wesley walikuwa waaminifu kutafuta kukubaliwa na Mungu. Hili walivyokuwa wamefundishwa, lilikuwa linapatikana kwa matendo mema na maagizo ya kidini.

Wakati Charles Wesley alipokuwa ameugua kiasi cha kuona [165]
kuwa kifo kilikuwa kinakaribia aliulizwa alipokuwa ameweka tumaini la uzima wa milele. Alijibu: "Nimetumia juhudi zangu wote kumtumikia Mungu." Rafiki yake alionekana kutoridhishwa na jibu hili. Wesley alitafakari: "NiniL.Je, atazipora jitihada zangu? Sina kingine cha kutumainia." [162] Hilo lilikuwa giza lililokuwa limetanda katika kanisa, likiwageuza watu kutoka katika tumaini lao la pekee la wokovu-damu ya Mwokozi aliYesulubishwa.

[162] John Whitehead, Life of the Rev. Charles Wesley, p. 102.

Wesley na washirika wake walikuwa wameongozwa kuona kwamba sheria za Mungu huwa zinasambaa kwenye mawazo, maneno na matendo. Kwa juhudi na bidii kwenye maombi zina uwezo wa kushinda uovu wa moyo. Walikuwa wanaishi maisha ya kujikana nafsi na ya kujidhili, wakitunza kwa usahihi sana kila kipengele walichokuwa wanadhani kingewasaidia kupata utakatifu na kukubalika mbele za Mungu. Lakini jitihada zao zilikuwa bure kuwapatia uhuru kutoka kwenye laana ya dhambi ama kuzivunja nguvu zake.

Moto wa ukweli wa mbinguni, ambao tayari ulikuwa umezimika katika madhabahu za Uprotestanti, ulipasa kuwashwa upya kutoka kwenye mwenge wa kale wa Wakristo wa Bohemia. Baadhi ya wakimbizi hawa walipata hifadhi kule Saksoni, waliiendeleza imani ya kale. Wesley alipata nuru yake kutoka kwa Wakristo hawa.

John na Charles walitumwa kupeleka habari njema kule Amerika. Kwenye meli waliyokuwa wanasafiri nayo, lilikuwemo kundi la Wamoravia. Mawimbi makali yaliwasumbua, na John akiwa uso kwa uso na mauti, alijisikia kutokuwa na uhakika wa amani yake na Mungu. Wajerumani walidhihirisha utulivu na tumaini lililomshangaza sana. "Muda mrefu kabla nilikuwa nimeona umakini mkubwa katika mwenendo wao....Ilikuwa ni fursa ya kujaribiwa kwao kama walikuwa wamekombolewa kutoka kwenye roho ya hofu, kiburi, hasira na kisasi. Katikati ya wimbo walipokuwa wameanza huduma yao ya ibada, bahari
[166] ilichafuka na kulivunjavunja tanga na kuifunika kabisa meli na kumwaga maji yake katikati ya sitaha kana kwamba bahari tayari ilikuwa imetumeza. Sauti za kutisha za mayowe zilianza kusikika miongoni mwa Waingereza. Kwa utulivu kabisa Wajerumani walikuwa wanaendelea kuimba. Baadaye nilimuuliza mmoja wao, 'Hamkuwa mmeogopa?' Naye alinijibu, 'Tunamshukuru Mungu maana hatukuwa tumeogopa.' Nami nilimwuliza tena, 'Lakini wanawake na watoto wenu nao hawakuwa wameogopa?' Naye akajibu kwa upole, 'Hapana, wanawake na watoto wetu hawaogopi kufa.' " [163]

[163] Ibid., p. 10.

### Moyo wa Wesley Wapata Joto kwa Njia ya Ajabu

Aliporudi Uingereza, Wesley alifikia mahali pa kuielewa imani ya Biblia kwa ufasaha zaidi chini ya usimamizi wa Wamoravia. Kwenye mkutano wa jumuia ya Wamoravia mjini London tamko la Luther lilisomwa. Alipokuwa anasikiliza, imani iliamshwa ndani ya moyo wa Wesley. Anasema "Nilijisikia moyo wangu ukipata joto kwa njia ya ajabu, nilijisikia kumtumainia Yesu, Yesu peke yake, kwa wokovu na nilipewa uthibitisho, kwamba ameziondoa dhambi zangu, hata mimi mwenyewe, na ameniokoa toka kwenye sheria ya dhambi na mauti." [164]

Na sasa alitambua kuwa ile neema aliyokuwa anaitaabikia kuipata kwa maombi, na kwa kufiinga, na kwa kujitesa ilikuwa inatolewa bure, "bila pesa na bila kima chochote." Moyo wake ulijaa hamasa na shauku ya kuisambaza kila mahali Injili tukufu ya Mungu na neema yake inayopatikana bure. "Ninauangalia ulimwengu wote kama parokia yangu," alisema; "katika sehemu yoyote nitakayokuwa, naona kuwa ni vema, ni haki, na ni wajibu wangu, kuwatangazia wale wote walio tayari kusikia habari njema za wokovu." [165]

Aliendelea na maisha yake ya utii na kujikana nafsi, kwa wakati huu yakiwa si msingi, lakini kama matokeo ya imani, si mzizi, lakini tunda la maisha matakatifu. Neema ya Mungu katika Kristo itadhihirishwa kwa utii. Wesley alikuwa ameyatoa maisha yake [167]
kuhubiri ukweli mkuu aliokuwa ameupokea-kuhesabiwa haki kwa njia ya imani kwa upatanisho wa damu ya Kristo, na moyo kufanywa upya kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, na kuzaa matunda maishani yanayopatana na kielelezo cha maisha ya Kristo.

Whitefield na wafuasi wa Wesley walikuwa wanaitwa kwa kebehi "Wamethodisti" na wanafunzi wenzao wasiokuwa wacha Mungu-jina linalochukuliwa kuwa ni la heshima kubwa katika siku zetu. Roho Mtakatifu alikuwa anawahimiza kumhubiri Kristo, Yeye aliYesulubishwa. Maelfu waliongolewa. Lilikuwa ni jambo la lazima kuwapatia kondoo hawa wa Mungu ulinzi dhidi ya mbwa mwitu wakali. Wesley hakuwa na wazo la kuanzisha dhehebu jingine jipya,

[164] Ibid., p. 52.
[165] Ibid., 74.

lakini aliwaweka pamoja watu hawa kwa kile kilichokuwa kinaitwa Muunganiko wa Wamethodisti.

Upinzani waliokuwa wanaupata wahubiri hawa kutoka kwenye kanisa lililokuwepo ulikuwa wa kisirisiri na wenye majaribu mengi-lakini bado ukweli uliweza kuingia katika milango ambayo vinginevyo ingebaki imefungwa. Baadhi ya wachungaji waliamka toka kwenye usingizi wao wa kimaadili na kuwa wahubiri hodari katika parokia zao.

Zama za Wesley watu waliokuwa na karama mbalimbali hawakuyafanya mafundisho yao kuwa na ulinganifu. Tofauti zilizokuwepo kati ya Whitefield na wafuasi wa Wesley vilitishia kuleta mfakarano mkubwa, lakini kwa kadri walivyojifunza unyenyekevu katika shule ya Kristo, kustahimiliana na kupendana kuliieta mapatano kwa pande hizi mbili. Hawakuwa na muda wa mafarakano wakati kila mahali makosa na uovu vilikuwa vinaendelea kutapakaa.

### Wesley Anusurika Kifo

Watu waliokuwa na mvuto walitumia uwezo dhidi yao. Wachungaji wengi walikuwa wamewachukia na milango ya makanisa ilikuwa imefungwa dhidi ya imani safi. Katika mimbari zao, wachungaji waliwakana hadharani wakionesha dalili za udhalimu na uovu. Mara kwa mara Wesley alinusurika kuuawa kwa mwujiza wa neema ya Mungu. Ilipoonekana hapakuwa na namna ya kuokoka, malaika katika umbo la binadamu alisimama upande wake na kundi la wahalifu walikuwa wanaanguka na mtumishi Wakristo alikuwa anapita kwa usalama kutoka katika hatari hiyo.

[168] Kuokolewa kwake kutoka katika moja ya matukio haya, Wesley alisema: ‘ingawaje wengi walikuwa wanajaribu kwa bidii kukamata ukosi wa mavazi yangu ili kuniangusha chini, hawakufaulu kabisa: ni mmoja tu aliwahi kukamata kwa nguvu upindo wa kizibao changu, ambacho upesi kilibakia mkononi mwake, na mwingine alipokamata upindo katika mfuko ninaohifadhia fedha, nilichoropoka mfuko ukawa umetatuka tu kidogo....Mtu mwenye nguvu aliyekuwa nyuma yangu, alijaribu mara kadhaa kunipiga kwa fimbo kubwa ya mwaloni; ambayo iwapo ingenipata kisogoni kwangu ningekufa. Kila wakati pigo lake liligeuziwa upande

mwingine, sikuelewa ilikuwa inatokeaje, kwa sababu sikuweza kujisogeza upande wa kuume ama wa kushoto.” [166]

Wamethodisti wa kipindi hicho walikuwa wanavumilia dhihaka na mateso, na mara nyingi walikuwa wanavumilia vurugu pia. Mara nyingine, mathalani; matangazo yaliwekwa katika mbao za matangazo za umma yakiwaita kwa pamoja wale wote waliokuwa wanahitaji kwenda kuvunja kwenye madirisha ya Wamethodisti na kuwaibia kukusanyika mahali na kwa muda fulani. Mateso yaliyokuwa yanaendeshwa kwa mpangilio yalikuwa yanafanywa dhidi ya watu ambao kosa lao peke yake lilikuwa kuwageuza wenye dhambi kuelekea njia ya utakatifii.

Kumomonyoka kwa hali ya kiroho nchini Uingereza muda mfupi kabla ya wakati wa Wesley kwa kiasi kikubwa yalikuwa ni matokeo ya fundisho kuWakristo alikuwa ameifuta kabisa sheria ya maadili na kwamba Wakristo hawalazimiki tena kuitunza. Wengine walikuwa wanadai kuwa halikuwa jambo la lazima kwa wachungaji kuwashawishi watu kutii maagizo ya sheria hiyo, kwa kuwa wale waliokuwa wamechaguliwa na Mungu kuokolewa “watakuwa wanaongozwa na kicho na wema wao kwa Mungu” na wale waliokuwa wamepangiwa kuangamia milele “hawakuwa na uwezo wa kuitii sheria ya Mungu.”

Wengine walikuwa wanadai kuwa “wateule hawawezi kuanguka na kuiacha neema ama kupoteza kukubaliwa kwao na Mungu,” na hata kufikia hitimisho lenye kuchafua moyo sana kwamba “matendo [169]
wanayotenda waovu kwa kweli siyo maovu kiasi hicho... kwa sababu hakutakuwa na wasaa wa kuungama dhambi zao ama kuziacha kwa kutubu” [167] Kwa hiyo, walikuwa wanadai kwamba, “hata kwa dhambi zenye kuaibisha mno” zilizokuwa zinajulikana pote kuwa ni uvunjifu mkubwa wa sheria ya Mungu haikuwa dhambi mbele za Mungu” kama zingekuwa zimetendwa na mteule. “Hawawezi kufanya lolote linalomchukiza Mungu ama lolote linalokatazwa na sheria.”

Mafundisho haya mabovu na ya kuogofya kimsingi yanafanana na yaliyotangulia yenye kufundisha kuwa hakuna sheria ya Mungu isiyoweza kubadilishwa kama kiwango cha haki na kwamba maadili yanadhihirishwa na jamii yenyewe na kila mara yalikuwa yanabadi-

[166] John Wesley, Wrks, vol. 3, pp.297, 298.

[167] McClintock & Strong, Cyclopedia, art. “Antinomians.”

lika. Dhana hizi zote huwa zinaongozwa na yule aliyekuwa miongoni mwa wakazi wa mbinguni wasio na dhambi aliyeanzisha kazi ya kuvunja vizuizi vya haki vya sheria ya Mungu.

Fundisho la maagizo ya Mungu, yasiyobadilika yanayotengeneza tabia za wanadamu, limewaongoza wengi kuikataa sheria ya Mungu. Na kwa uthabiti Wesley alikuwa analipinga fundisho hili lililopelekea baadhi ya Wakristo kudhani kuwa neema ya Mungu inawapa watu uhuru wa kutozishika sheria za maadili. "Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa." "...Mungu Mwokozi wetu...ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli. Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, MwanadamUkristo Yesu; ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote." "Kristo "nuru halisi,...amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu." Tito 2:11; lTim. 2:3-6; Yn. 1:9. Watu hujikosesha wenyewe wokovu kwa sababu ya kukataa kwa hiari yao karama ya uzima.

## Kuilinda Sheria ya Mungu

Katika kujibu dai kuwa wakati Kristo alipokufa Amri Kumi za Mungu zilitanguliwa pamoja na sheria za kawaida za matendo ya dini, Wesley alisema, "Hakuiondoa sheria ya maadili iliyomo katika
[170] Amri Kumi iliyokuwa inashikwa na manabii. Hii ni sheria ambayo kamwe haiwezi kutanguliwa, 'inasimama thabiti kama shahidi mwaminifu kule mbinguni.' "

Wesley alitangaza pia mapatano yaliyopo kati ya sheria ya Mungu na Injili. "Kwa upande mmoja sheria huendelea kutengeneza njia na kutuelekeza kwenye lnjili; na kwa upande wa pili habari njema huendelea kutuongoza kwa usahihi kuitimiza sheria. Mathalani sheria hututaka kumpenda Mungu, na majirani zetu; kuwa wapole, wanyenyekevu na watakatifu. Tunajisikia kwamba hatuna uwezo kuyatimiza haya;...lakini ahadi ya Mungu hutupatia upendo huo, na kutufanya kuwa wanyenyekevu, wapole na watakatifu: tunaing'ang'ania Injili na hizi habari njema...'haki ya sheria inatimizwa ndani yetu,' kwa njia ya imani iliyo katika Kristo Yesu....

"Walio wakuu miongoni mwa maadui wa Injili ya Kristo," asema Wesley, "ni wale wafundishao watu kuvunja, siyo amri moja tu, kati

ya zile zilizo ndogo au zilizo kubwa, bali amri zote kwa mpigo. Wao humheshimu Mungu kama alivyofanya Yuda aliposema, ‘Salamu Rabi akambusu’.... Kuzungumzia damu yake, na kumvua taji yake; kuhafifisha sehemu yo yote ya sheria yake, kwa kisingizio cha kueneza Injili yake ni sawa na kumsaliti kwa busu.” [168]

### Upatanifu wa Sheria na Injili

Kwa wale waliokuwa wanadai kwamba “kuhubiriwa kwa Injili lilikuwa jibu la matakwa yote ya sheria,” Wesley alijibu: “Haijibu matarajio ya kwanza ya sheria, yanayoitwa, kuwathibitishia wanadamu kwa habari ya dhambi, na kuwaamsha wale wanaolala kwenye kingo za kuzimu...kwa hiyo ni jambo la kipumbavu kuwapatia daktari watu wenye afya njema, na hata wale wanaodhania kuwa ni wazima. Jambo la kwanza unatakiwa kuwathibitishia kuwa ni wagonjwa; vinginevyo hawatakushukuru kwa jitihada zako. Ni jambo la kipuuzi pia kumtoa Kristo kwa watu ambao mioyo yao ni mizima wala haijavunjika vunjika.” [169]

Kama alivyokuwa Bwana wake alipokuwa anahubiri Injili ya [171]
neema ya Mungu, Wesley “aliitukuza sheria na kuiadhimisha.” Isaya 42:21. Matokeo aliyoruhusiwa kuyaona yeye mwenyewe yalikuwa ni ya kupendeza sana. Wakati wa kuhitimisha huduma yake iliyozidi nusu kame, wafuasi wake walikuwa wamefikia idadi ya watu zaidi ya nusu milioni. Lakini kundi kubwa la watu lililonyanyuliwa kutoka kwenye hali duni ya maisha ya dhambi kwenda katika maisha safi na ya hali ya juu kutokana na juhudi zake kamwe halitajulikana mpaka familia yote ya waliokombolewa watakapokusanyika kwenye ufalme wa Mungu. Maisha yake yanatupatia fundisho la kima kisichopimika cha thamani ya maisha ya kila Mkristo.

Imani aliyokuwa nayo, kutochoka kwenye juhudi zake, kujitoa mhanga kwake, na utauwa wa mtumishi huyu Wakristo ungeweza kuakisiwa kwenye makanisa ya leo!

[168] Wesley, Sermons 25.
[169] Wesley, Sermons 35.

[172] 

# Sura Ya 15 - Enzi Ya Hofu Kuu Ufaransa: Chimbuko Lake Halisi

Baadhi ya nchi zilikaribisha imani ya Matengenezo kama mjumbe wa Mbinguni. Katika nchi nyingine nuru ya ujuzi wa Biblia kwa ujumla ilikuwa kana kwamba imewekwa kando. Kwenye nchi moja ukweli na udanganyifu vilishindana kwa kame nyingi. Hatimaye ukweli wa mbinguni ulitupwa nje. Roho wa Mungu aliondolewa kutoka kwa watu waliokuwa wameidharau karama ya neema ya Mungu. Ulimwengu wote ulishuhudia tunda la kuikataa nuru kwa makusudi.

Vita dhidi ya Biblia nchini Ufaransa viliishia kwenye Mapinduzi, matokeo halali ya ukandamizaji wa Maandiko Matakatifu uliokuwa unafanywa na Kanisa la Roma.(Angalia Kiambatisho.) Jambo hili lilitoa kielelezo kikubwa cha matokeo ya mafundisho ya Kanisa la Roma kuliko vyote vilivyowahi kushuhudiwa.

Mwandishi wa Ufunuo anaonesha matokeo ya kuogofya ya utawala wa "mtu wa dhambi" yaliyokuwa yanarundikana huko Ufaransa: "...Nao wataukanyaga mji mtakatifu miezi arobaini na miwili. Nami nitawamhusu mashahidi wangu wawili, nao watatoa unabii siku elfu na mia mbili na sitini, hali wamevikwa magunia. ...Hata watakapoumaliza ushuhuda wao, yule mnyama atokaye katika kuzimu atafanya vita nao, naye atawashinda na kuwaua. Na mizoga yao itakuwa katika njia ya mji ule mkuu, uitwao kwa jinsi ya roho Sodoma, na Misri, tena ni hapo Bwana wao aliposulubiwa.... Nao wakaao juu ya nchi watafurahi juu yao na kushangilia. Nao watapelekeana zawadi wao kwa wao, kwa kuwa manabii hao wawili waliwatesa wao wakaao juu ya nchi. Na baada ya siku hizo tatu u nusu, roho ya uhai itokayo kwa Mungu ikawaingia, wakasimama ju ya miguu yao; na hofu kuu ikawaangukia watu waliowatazama." Ufunuo 11:2-11.

"Miezi arobaini na miwili" na "siku elfu moja mia mbili na sitini" ni kitu kile kile, wakati ambao Kanisa la Kristo lingepata mateso kutokana na ukandamizaji wa Kanisa la Roma. Miaka 1260

ilianza mnamo mwaka 538 na kuishia mwaka 1798 B.K.(Tazama Kiambatisho.) Wakati huo jeshi la Ufaransa lilimtia nguvuni Papa, na alifia uhamishoni. Tangu wakati huo utawala wa Papa haujapata mamlaka uliokuwa nayo hapo kabla.

Mateso kwa Kanisa hayakuendelea kwa miaka yote 1260. Re- [173]
hema ya Mungu ilipunguza muda huo wa mateso makali kwa watu wake yaliyokuwa yanachochewa na imani ya Matengenezo.

"Mashahidi wawili" wanawakilisha Maandiko Matakatifu yaani Agano la Kale na Agano Jipya, ushahidi muhimu wa chimbuko na umilele wa sheria ya Mungu, na mpango wa wokovu.

"...Nao watatoa unabii siku elfu na mia mbili na sitini, hali wamevikwa magunia." Biblia ilipopigwa marufuku, na shuhuda zake kupotoshwa, wakati wale waliodiriki kuzitangaza kweli zake waliposalitiwa, kuteswa na kuuawa kwa sababu ya imani yao ama kulazimishwa kukimbia- "mashahidi" waaminifu walikuwa wanatoa unabii wakiwa "wamevaa nguo za magunia." Kwenye nyakati za giza kuu wanadamu waliokuwa waaminifu walipewa mamlaka na busara kuutangaza ukweli wa Mungu. **(AngaIia Kiambatisho.)**

"Na mtu akitaka kuwadhuru, moto hutoka kwenye vinywa vyao na kuwala adui zao." Ufunuo 11:5. Watu hawawezi kukanyaga Neno la Mungu bila kuadhibiwa!

"Hata watakapoumaliza ushuhuda wao." Walipokaribia kumaliza kazi yao katika mazingira magumu, watashambuliwa na "yule mnyama atokaye katika kuzimu." Hapa inafunuliwa upya mamlaka ya kishetani.

Imekuwa ni sera ya Kanisa la Roma, kudai kuwa linaiheshimu Biblia, kwa kuifungia katika lugha isiyofahamika, na kuificha watu wasiisome. Chini ya utawala wake mashahidi walikuwa wanatoa unabii "hali wamevikwa magunia." Lakini "mnyama atokaye kuzimu." angekiri waziwazi kupiga vita Neno la Mungu.

"Mji mkuu" ambamo mashahidi waliuawa kwenye mitaa yake na mizoga yao kutupwa humo ni Misri ya "kiroho." Mataifa yote katika historia ya Biblia, ni Misri peke yake waliokataa kwa ujasiri mkubwa uwepo wa Mungu na walikuwa wanapinga maagizo Yake. Hakuna mfalme aliyediriki kufanya uasi kwa kiburi dhidi ya Mbingu
kama alivyofanya Farao mfalme wa Misri: "...Mimi simjui BWANA, [174]
wala sitawapa Israeli ruhusa waende zao."Kutoka 5:2. Huu ni ukana-

mungu; na taifa linalowakilishwa na Misri litatoa sauti ya kumkataa Mungu na kudhihirisha roho ya ujeuri.

"Mji mkuu" pia unalinganishwa "kiroho" na Sodoma. Ufisadi wa Sodoma ulidhihirishwa hasa katika uasherati. Dhambi hii pia ingeandamana na taifa ambalo lingetimiza andiko hili.

Kulingana na andiko hili la nabii, muda mfupi kabla ya mwaka 1798 mamlaka fulani zenye tabia ya kishetani zingeinuka kuipiga vita Biblia. Na kwenye nchi ambayo ushuhuda wa "mashahidi wawili" wa Mungu utanyamazishwa hivyo utabainishwa ukanamungu wa Kifarao na ufuska wa Sodoma.

### Utimilifu wa Kuvutia wa Unabii

Unabii huu ulitimia kwa namna ya ajabu katika historia ya Ufaransa wakati wa Mapinduzi ya Ufaransa, mnamo mwaka 1793. "Ufaransa inasimama kuwa nchi pekee katika historia ya dunia kutangaza kupitia Bunge lake kwamba hakuna Mungu, ambalo liliwafanya wakazi wote wanawake kwa wanaume wa mji mkuu na wengine wengi kutoka sehemu mbalimbali nchini humo, kwa kulipokea tangazo hilo kwa kucheza na kuimba kwa furaha." [170]

Ufaransa ilionesha tabia zilizokuwa zinadhihirishwa Sodoma. Mwanahistoria anatambulisha ukanamungu na ufuska wa Ufaransa kwa maneno haya: "Jambo lililokuwa limefungamana kwa karibu zaidi na sheria hizi zilizokuwa zinaathiri dini, lilikuwa ni lile lililodhalilisha uhusiano wa ndoa-uhusiano mtakatifu mwanadamu anaoweza kuufanya, na uthabiti wake ambao huchangia kwa kiasi kikubwa sana kuimarisha jamii-na kuifanya mkataba wa muda mfupi, watu wowote wawili kuuingia na kuachana kimchezo mchezo...Mwigizaji maarufu wa vichekesho, Sophie Amoult; aliielezea ndoa ya aina hiyo kuwa ni 'sakramenti ya uzinifu." [171]

[175]

### Ladui Dhidi ya Kristo

"Hapo Bwana wetu aliposulubiwa." Jambo hili pia lilitimia nchini Ufaransa. Hakuna nchi ambayo ukweli ulikumbana na upinzani mbaya sana kama hii. Mateso waliyokuwa wanafanyiwa

[170] Blackwood Magazine, November, 1870..

[171] Sir Walter Scott, Life of Napoleon, Vol. 1, ch. 17.

waliopokea Injili nchini Ufaransa yalikuwa yanamsulubisha Yesu kupitia wafuasi wake.

Kame baada ya kame damu ya watakatifu ilikuwa inamwagika. Wakati watu wa kule Waldensia walipoyatoa maisha kwenye milima ya Piedmont "kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu," ushuhuda kama wao ulikuwa unafanywa na watu walioitwa Albigenses wa Ufaransa. Wafuasi wa imani ya Matengenezo waliuawa baada ya mateso ya kuogofya. Wafalme, wakuu na mabinti zao, wanawali mahiri walikuwa wanajifurahisha kwa maumivu makali ya wafia dini Wakristo. Mashujaa wa jamii ya Huguenots walimwaga damu yao walipokuwa wanapambana, na walikuwa wanawindwa kama wanyama pori.

Wazao wachache wa Wakristo wa zamani waliokuwa wamebaki nchini Ufaransa kwenye kame ya kumi na nane, ambao walikuwa wamejificha milimani kusini mwa nchi hiyo, walikuwa wameihifadhi imani ya mababu zao. Walilazimishwa kwenda utumwani kwa vyombo vya baharini maisha yao yote. Watu waliofundishwa vizuri na wenye akili wa Ufaransa walikuwa katika mateso ya kutisha katikati ya wanyang'anyi na wauaji. Wengine waliuawa bila humma walipokuwa wanapiga magoti katika sala. Nchi yao ilikuwa imeharibiwa na upanga, shoka, moto, "ilikuwa imegeuzwa kuwa nyika kubwa yenye huzuni.

"Mauji haya ya kikatili yalifanyika...si katika zama za giza, lakini katika utawala wenye mafanikio wa Louis XIV. Kwa wakati huu sayansi ilikuzwa, elimu ilistawi, wakuu wa mahakama na ikulu walikuwa ni wasomi na wenye uwezo, na kwa kiasi kikubwa waliathiri neema ya unyenyekevu na upendo." [172]

## Uovu wa Kutisha zaidi [176]

Jambo la kuogofya kati ya matendo ya kishetani ya kame za kutisha yalikuwa ni mauaji ya halaiki ya St. Bartholomew. Mfalme wa Ufaransa aliombwa kibali na mapadre na maaskofu. Kengele iliyongongwa usiku wa manane ilikuwa ni ishara ya mauaji. Wakiwa wamelala kwenye nyumba zao, wakitumaini kuwa mfalme wao atawastahi, Waprotestanti kwa maelfu walikokotwa toka huko na kwenda kuuawa.

[172] Wylie, bk. 22, ch. 7.

Kwa muda wa siku saba mauaji yalikuwa yanaendelea mjini Paris. Kwa agizo la mfalme mauaji haya yalisambaa kwenda kwenye miji mingine walikokuwa Waprotestanti. Wakuu kwa wakulima, wazee kwa vijana, akinamama kwa watoto, waliuawa kwa pamoja. Waungwana wapatao 70,000 wa nchi yote ya Ufaransa waliangamia.

“Habari za mauaji hayo zilipofika Roma, mapadre walifurahia sana. Kardinali wa Lorraine alimzawadia mtu aliyepeleka ujumbe huo kwa taji elfu moja; Padre wa Kanisa Kuu la St. Angelo alibubujikwa na salamu za furaha; kengele ziligongwa kutoka katika kila mnara wa kengele wa kanisa; myoto mikubwa ya kusherehekea iligeuza usiku kuwa mchana; na Gregory XIII, alikuwa anawahudumia makardinali na wakuu wangine wa kanisa, walitembea katika msafara mrefu kwenye kanisa la St. Louis, mahali ambapo kardinali wa Lorraine aliimba wimbo unaosema Te *Deum*...Sahani ya chuma ilipigwa kwa ajili ya kukumbuka mauaji hayo...Padre wa Kifaransa ...aliizungumzia siku hiyo kama siku yenye furaha tele na kuridhisha, wakati baba mtakatifu alipozipokea habari hizo alikwenda kwa umakini kumshukuru Mungu na Mtakatifu Louis.” [173]

Roho aliyeongoza mauaji ya halaiki ya St. Bartholomew ndiye aliyeongoza matukio ya Mapinduzi. Yesu Kristo alitangazwa laghai na sauti ya makafiri wa Ufaransa ilikuwa “Mponde Fidhuli,” kwa maana ya Kristo. Makufum na uovu vilikuwa vinakwenda bega kwa bega. Katika yote haya, Shetani ndiye aliyepewa heshima na utii, wakati Kristo katika tabia yake ya ukweli, usafi wa moyo, na upendo usiokuwa na ubinafsi, “alisulubiwa.”

[177] “Mnyama atokaye kuzimu atafanya vita nao na atawashinda na kuwaua.” Ufunuo 11:7. Utawala usiomjua Mungu uliokuwa unatawala Ufaransa wakati wa Mapinduzi na Utawala wa Kidhalimu ulikuwa unafanya vita dhidi ya Mungu na Neno lake. Ibada ya Mungu ilipigwa marufuku na Bunge. Biblia zilikusanywa na kuchomwa moto hadharani. Taasisi za Biblia zilipigwa marufuku. Siku ya pumziko ya kila juma iliwekwa kando, na badala yake kila siku ya kumi ilitengwa kwa ajili ya sherehe na anasa. Ubatizo na Meza ya Bwana vilipigwa marufuku. Matangazo yaliyokuwa yamewekwa makaburini yalisema kuwa kifo ni usingizi wa milele.

[173]Henry White, The Massacre of St. Bartholomew, ch. 14, par.34.

Ibada zote za kidini zilipigwa marufuku, isipokuwa ile ya "uhuru wa watu kujiamulia mambo yao" na ya nchi. Askofu wa kikatiba wa mji wa Paris aliletwa mbele kutangaza kwenye Mkutano Mkuu kwamba ile dini aliyokuwa anaifundisha kwa miaka mingi ilikuwa ni sehemu ya maarifa ya mapadre, ambayo hayakuwa na msingi wowote kwenye historia au kwenye ukweli mtakatifu. Kwa maneno makini na ya wazi alikana uwepo wa Mungu ambaye kwa huyo aliwekwa wakfu kuhudumu ibada yake.

"Nao wakaao juu ya nchi wafurahi juu yao na kushangilia. Nao watapelekeana zawadi wao kwa wao, kwa maana manabii hao wawili waliwatesa wao wakaao juu ya nchi." Ufunuo 11:10. Makafiri wa Ufaransa walinyamazisha sauti ya mashahidi wawili wa Mungu wanaoonya. Neno la Mungu lilikuwa limekufa na kulala kwenye mitaa yake. Na waliokuwa wanaichukia sheria ya Mungu walikuwa wanashangilia. Wanadamu walimdharau Mfalme wa mbinguni waziwazi.

## Ushupavu katika Kumtukana Mungu

Mmoja wa mapadre wa shirika jipya alisema, "Kama wewe Mungu upo, jilipizie kisasi kwa sababu jina lako linatukanwa. Ninakudharau! Unabaki kimya; Huthubutu kuzituma ngurumo zako. Ni nani baada ya jambo hili atakayeamini kwamba Upo?" [174] Maneno haya yanaakisi kiasi gani yale madai ya Farao! kwamba: "BWANA ni nani hata niweze kuitii sauti yake?"

Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu; Na Bwana [178]
anasema "...Maana upumbavu wao utakuwa dhahiri kwa watu wote." Zaburi 14:1, 2; 2 Timotheo 3:9. Baada ya Ufaransa kukataa ibada ya Mungu aliye hai, nchi hiyo iliporomoka kuelekea kwenye ibada ya sanamu iliyokuwa duni sana kwa kuanza kumwabudu mungu mke wa Hekima (Goddess of Reason)- mwanamke mzinzi. Jambo hili lilifanyika kwenye Bunge la nchi hiyo! "Mojawapo ya sherehe za kiwendawazimu za wakati huu inayosimama bila mshindani kwa upumbavu unaojumuisha uovu.

Milango ya ukumbi wa mikutano ilifunguliwa... Wajumbe wa baraza la mji waliingia kwa maandamano mazito, wakiimba

[174] Lacretelle, History, vol. 11, p. 309: in Sir Archibald Alison, History of Europe, vol. 1, ch. 10.

wimbo wa sifa kwa sababu ya uhuru wa kujiamulia mambo, walikuwa wanasindikiza kitu cha kuabudiwa katika siku za usoni, sanamu ya mwanamke iliyokuwa imefunikwa, waliyokuwa wanaiita mungu mke wa hekima. Ilipoletwa ndani ya ukumbi ilifunuliwa kwa mwonekano wa kuvutia na kuwekwa upande wa kuume wa mwenyekiti na alitambuliwa kuwa ni msichana achezaye muziki kwenye ukumbi wa maonesho."

### Mungu Mke wa Hekima

"Kusimikwa kwa mungu mke wa hekima kulikuwa kunarudiwa rudiwa na kufuatishwa katika taifa zima, na kwenye maeneo ambayo wenyeji wake walikuwa wanatamani kwenda pamoja na Mapinduzi." [175]

Alipoletwa kwenye mkutano, msemaji aliushika mkono wake na kuugeukia mkutano na kusema: "'Ninyi watu, acheni kutetemeka mbele ya ngurumo zisizokuwa na nguvu za Mungu ambaye kwa hofu yenu mnadhani kuwa yupo. Tangu sasa na kuendelea, msimtambue Mungu ye yote isipokuwa mungu mke wa hekima. Ninawapatieni sanamu yake nzuri na safi isiyolinganishwa na chochote, na endapo mtalazimika kuwa na sanamu nyingine, toeni kafara kwenye sanamu hii peke yake....

Baada ya kukumbatiwa na mwenyekiti mungu mke alipakizwa kwenye gari la fahari na kupelekwa kwenye kanisa la dayosisi kule Notre Dame, na kuchukua nafasi ya Mungu. Na hapo mungu huyu aliwekwa juu ya mimbari iliyokuwa imeinuliwa sana na watu wote waliokuwa pale wakamwabudu." [176]

[179] Utawala wa Papa ulianzisha kazi ambayo ukanamungu ulikuwa unaikamilisha, na kuiharakisha nchi ya Ufaransa kuelekea kwenye maangamizi. Wakirejea vitisho vya Mapinduzi, waandishi wanasema, mambo haya yaliyokithiri yalikuwa yanatakiwa kubebeshwa kwenye kiti cha enzi cha kanisa.(Angalia Kiambatisho) Na kwa hali halisi ni sharti lawama juu ya jambo hili ziende kwa kanisa.

Utawala wa Papa ulikuwa umesumisha vichwa vya wafalme dhidi ya imani ya Matengenezo Nguvu za Roma zilikuwa zimeweka

[175] Scott, vol. 1, ch. 17.

[176] M. A. Thiers, History of the French Revolution, vol. 2, pp. 370, 371.

msukumo wa ukatili na ukandamizaji uliokuwa unatoka katika kiti cha enzi.

Popote Injili ilipopokelewa, mioyo ya watu ilizinduliwa. Wakaanza kuitupilia mbali minyororo iliyokuwa imewafunga kwenye utumwa wa ujinga na imani za kishirikina. Wafalme waliishuhudia na kutetemeka kwa sababu ya utawala wao wa kidhalimu. Utawala wa Papa ulifanya haraka kuchochea hofu yenye wivu ya wafalme hawa.

Mnamo mwaka 1525 Papa alisema maneno yafuatayo kwa mtawala wa Ufaransa: "Wazimu huu [yaani Uprotestanti] hautachanganya na kuharibu tu mambo ya dini bali mamlaka zote, tabia njema, sheria na mpangilio wa maisha ya watu."

Balozi wa Papa alimwonya mfalme kwa maneno haya: "Waprotestanti watavuruga utaratibu wote wa kiraia na ule wa kidini....Kiti cha enzi cha mfalme kiko hatarini kama vile mimbari ilivyo hatarini." [177] Kanisa la Roma lilifanikiwa kulipanga taifa la Ufaransa tayari kupiga vita imani ya Matengenezo.

Mafundisho ya Biblia yangejenga ndani ya mioyo ya watu kanuni za haki, kuwa na kiasi, ukweli, mambo ambayo ni mhimili wa ustawi wa taifa. "Haki huinua taifa." Na kwa namna hiyo "kiti cha enzi huthibitishwa." Mithali 14:34; Isaya 16:12 (Soma Isaya [180]
32:17.) Anayetii sheria ya Mungu pia ataheshimu na kutii sheria za nchi. Ufaransa ilipiga marufuku Biblia. Watu waaminifu na wenye nguvu kiakili na kimaadili, waliokuwa na imani kuvumilia mateso kwa sababu ya ukweli walipata taabu kubwa, baharini waliangamia kwenye nguzo ya kuchomea moto "waasi" ama waliachwa kuoza katika magereza yaliyokuwa chini ya ardhi. Maelfu walikimbilia mahali pa usalama miaka 250 baada ya imani ya Matengenezo kuanza.

"Kwa nadra kulikuwa na kizazi cha Wafaransa kwenye kipindi hiki kirefu ambacho hakikushuhudia wafuasi wa Injili wakikimbia mateso makali, wakichukua pamoja nao ujuzi, ustadi, uchapa kazi, mfumo wa maisha, ambapo kama kanuni ilivyo, walikuwa wamefanikiwa sana, hivyo kuzinufaisha nchi zilizokuwa zimewapatia hifadhi.... Endapo watu wote waliokuwa wamefukuzwa wangebaki

[177] D'Aubigne, History of the Reformatio in Europe in the Time of Calvin, bk. 13, ch.20.

nchini Ufaransa ...taifa hili lingekuwaje...taifa kubwa, lenye ustawi, na nchi yenye kuvutia- ingekuwa kielelezo kwa mataifa mengine!

Lakini ufinyu wa kuelewa na kutochukuliana na watu wenye mtazamo tofauti uliwafukuza kutoka kwenye ardhi yake kila mwalimu mwadilifu, kila mtetezi wa mfumo safi wa maisha, na kila mlinzi wa kiti cha enzi cha ufalme wa nchi hiyo...Hatimaye uangamivu wa taifa ulitimia." [178] Matokeo yake yalikuwa ni Mapinduzi ya kuogofya.

## Kile Ambacho Kingetokea

"Kukimbia kwa jamii ya Hugenots kulisababisha kudhoofika kwa Ufaransa katika hali zote. Miji ya viwanda iliyokuwa kwenye hatua za ustawi ilianguka na kuchakaa.... Inakisiwa kwamba mwanzoni mwa siku za Mapinduzi, kulikuwa na ombaomba wapatao mia mbili elfu katika mji wa Paris waliokuwa wanaomba msaada kutoka mikononi mwa mfalme. Kwenye taifa hili lililokuwa linaendelea kudhoofika ni Majesuti peke yao ndio waliokuwa wamestawi." [179]

[181] Injili ingeleta suluhisho kwa matatizo yaliyokuwa yanaisumbua Ufaransa na kuwatatiza viongozi wake wa kidini, mfalme, na wabunge, ambayo hatimaye yalilitumbukiza taifa hili kwenye uharibifu. Chini ya uongozi wa Kanisa la Roma watu walikuwa wamepoteza mafundisho ya Mwokozi ya kujikana nafsi na upendo usio na ubinafsi kwa kuwatendea mema watu wengine. Matajiri hawakukemewa kwa kuwagandamiza maskini wala maskini hawakuwa na msaada katika hali yao duni. Ubinafsi wa wenye mali na wenye nguvu ulikuwa umezidisha unyanyasaji. Kwa kame nyingi, matajiri walikuwa wanawakosea maskini na maskini waliwachukia matajiri.

Katika majimbo mengi wafanyakazi walikuwa wanategemea huruma za wenye mali na walilazimishwa kutekeleza matakwa makubwa kupita kiasi. Watu wa daraja la kati na la chini walikuwa wanatozwa kodi kubwa na mamlaka za serikali na mapadre. "Wakulima na wakulima wadogo walikuwa wanakufa bila bwana huyu mdhalimu kujali... Maisha ya wafanyakazi mashambani yalikuwa yenye kazi zisizokoma, na taabu isiyo na kupumzika; malalamiko yao ... yalipuuzwa na walikuwa wanatendewa jeuri....

[178] Wylie, bk. 13,ch.20.
[179] Ibid.

Majaji walikuwa wanapokea rushwa waziwazi...Chini ya nusu ya kodi iliyokuwa inatozwa ilifika katika hazina ya mfalme au hazina ya askofu; sehemu iliyobaki ilikuwa inatumiwa vibaya na kutapanywa kwenye mambo ya anasa. Watu waliowafukarisha wenzao kiasi hicho walikuwa wamesamehewa kulipa kodi na walikuwa wameruhusiwa kisheria au na desturi pia kuwekwa katika vyeo vyote vilivyokuwepo serikalini.... Kwa kutimiza tamaa zao mamilioni walizamishwa kwenye maisha duni na yasiyokuwa na matumaini. **(Angalia Kiambatisho.)**

Kwa zaidi ya nusu kame kabla ya Mapinduzi ya Ufaransa, nchi hiyo ilikuwa chini ya utawala wa Louis XV, mfalme huyu alijulikana kwa uzembe, kutokuwa makini, na uasherati. Na huku hazina ya nchi ikiwa imefilisika na watu wamekasirishwa vilivyo, halikuhitajika jicho na nabii kuona matokeo ya kutisha yaliyokuwa mbele. Hitaji la marekebisho lilikuwa linasisitizwa bila mafanikio. Maangamizi yaliyokuwa yanaikabili Ufaransa yalionekana katika jibu la ubinafsi na lenye fumbo la mfalme, "Baada yangu ni mafuriko!"

Kanisa la Roma lilikuwa limewafundisha wafalme na watawala [182]
kuwafanya watu kuwa watumwa, likikusudia kuwafunga pingu mioyoni mwao viongozi na watu wa kawaida. Mambo mengi ya kutisha kuliko maumivu ya kimwili yaliyosababishwa na sera za Kanisa la Roma ilikuwa ni mmomonyoko mkubwa wa maadili. Wakiwa wamenyimwa Biblia na kuachwa kuishi maisha ya ubinafsi, watu walikuwa wamegubikwa na ujinga na kuzama kwenye maovu, na hawakuwa wanafaa kutawala nafsi zao.

### Kuvuna Katika Damu

Badala ya kuwashikilia watu katika utii pasipo kujua juu ya mafundisho yake, kazi ya Kanisa la Roma iliwafanya watu hao kuwa makafiri na waasi. Walikuwa wameudharau utawala wa Papa na kuuita ujanja wa mapadre. Walikuwa wanamfahamu mungu mmoja tu, yaani mungu wa Roma. Walikuwa wanaitazama tamaa na ukatili wa Kanisa la Roma kama tunda la Biblia, na hivyo hawakuwa wanavihitaji vyote viwili.

Kanisa la Roma lilimwakilisha Mungu vibaya, kwa hiyo watu walitupilia mbali Neno la Mungu na Mwandishi wake. Kinyume

chake, Voltaire na washirika wake waliliweka kando Neno la Mungu na kuanza kusambaza ukanamungu. Kanisa la Roma lilikuwa linawakanyaga chini watu kwa kisigino cha chuma; sasa watu walitupilia mbali vizuizi vyote. Kwa hasira waliukataa ukweli na uongo pamoja.

Mwanzoni mwa Mapinduzi ya Ufaransa, kwa kibali cha mfalme, watu walikuwa wamepewa nafasi nyingi za uwakilishi kuliko idadi ya watawala na mapadre kwa pamoja. Na kwa namna hiyo, tayari madaraka yalikuwa mikononi mwa walio wengi; na hawakutaka kuyatumia kwa busara na nidhamu. Watu waliokuwa wamekasirishwa waliamua kulipa kisasi. Wenye kudhulumiwa walikuwa wamejifunza somo kutoka kwenye utawala wa kidiktcta na waligeuka kuwa wagandamizaji wa wale waliokuwa wanawadhulumu hapo kabla.

Ufaransa ilivuna katika damu kwa kukubali kulitii Kanisa la Roma. Mahali ambapo Ufaransa ilikuwa imesimamisha nguzo ya kwanza ya kuchomea "waasi wa kidini" chini ya utawala wa Kanisa la Roma mwanzoni mwa imani ya Matengenezo, hapo ndipo wanamapinduzi walipoweka mashine ya kukatia watu vichwa vyao. Mahali pale wafia dini wa kwanza wa imani ya Kiprotestanti walipochomwa moto kwenye karne ya kumi na sita, wahanga wa
[183] kwanza walikatwa vichwa katika karne ya kumi na nane. Wakati vizuizi vilivyo katika sheria ya Mungu vilipowekwa kando, taifa lilisombwa na uasi na machafuko. Vita dhidi ya Biblia inasimama katika historia ya dunia kama Utawala wa Udhalimu. Yule aliyepata ushindi siku ya kwanza, alihukumiwa siku ya pili.

Mfalme, mapadre, na watawala walilazimika kutii udhalimu mkubwa uliokuwa unafanywa na watu waliokuwa wamegeuka kuwa wendawazimu. Wale waliokuwa wanatangaza kifo cha mfalme walimfuata mapema kwenye jukwaa la kunyongea. Mauaji ya kikatili yalitangazwa kwa wale wote waliokuwa wanachukia Mapinduzi. Ufaransa ikawa uwanja mkubwa wa makundi ya watu yaliyokuwa yanashindana, yakisukasukwa huku na huko kwa hasira kali. "Mjini Paris machafuko yalifuata machafuko mengine, na raia walikuwa wamegawanyika katika makundi ya fujo, yaliyokuwa hayakusidii kufanya jambo lolote la maana isipokuwa kuangamiza... Nchi ilikuwa karibu kufilisika, majeshi yalikuwa yanazozana kwa ajili ya kupunjwa malipo yao, wakazi wa Paris walikuwa wanakufa njaa, mikoa ilikuwa imeharibiwa vibaya na wanyang'anyi na ustaarabu ulikuwa

karibu kutoweka kwa sababu ya machafuko na watu kujifanyia mambo walivyokuwa wanataka."

Pia watu walikuwa wamejifunza ukatili na mateso ambayo Kanisa la Roma lilikuwa linayafundisha kwa bidii. Wakati huu haukuwa kwa wafuasi wa Yesu kubumtwa kupelekwa kwenye mti wa kuchomea watu moto. Miaka mingi ilikuwa imepita tangu walipoangamia ama kulazimika kukimbilia uhamishoni. "Majukwaa ya kunyongea watu yalikuwa mekundu kwa damu ya mapadre. Vyombo vya baharini na magereza yaliyokuwa hapo mwanzo yamejaa wanamatengenezo Wahuguenot, sasa yalikuwa yamejaa watesi wao. "Akiwa amefungwa kwenye benchi na kusumbuka kwa kazi ngumu na ya muda mrefu, padre wa Kanisa Katoliki la Roma alipitia maumivu yote yaliyokuwa yanaendeshwa na kanisa lao bila kizuizi chochote kwa waasi wa mafundisho yake. **(Angalia Kiambatisho.)**

"Zikaja siku ambazo wapelelezi walikuwa wanavizia kila sehemu; wakati mashine ya kukata vichwa vya watu ilipokuwa inafanya kazi nzito na kwa muda mrefu kila asubuhi; wakati magereza yalipokuwa yamejazwa kama meli ya kubebea watumwa, wakati mitaro ya maji ilipojazwa kwa mapovu ya damu kuelekea mto [184]
Seine....Misururu mirefu ya mateka waliuawa kwa risasi zilizokuwa zinafyatuliwa toka kwenye mzinga. Matundu makubwa yalitobolewa chini ya meli zilizojaza watu. Mamia ya wavulana na wasichana wa umri wa miaka kumi na saba waliuawa na serikali hiyo dhalimu. Watoto waliopokonywa kutoka matitini kwa mama zao waliuawa kwa kuchomwa mikuki na wanachama wa Jacobin, moja ya vyama waasisi wa Mapinduzi ya Ufaransa." **(Angalia Kiambatisho.)**

Mambo haya yote ndiyo aliyokuwa anayataka Shetani. Sera zake ni udanganyifu na kusudi lake ni kuwadhalilisha wanadamu, kuharibu kazi ya Mungu ndani yao, kuumbua kusudi la upendo wa Mungu na hivyo kuihuzunisha mbingu. Na kwa kutumia stadi zake za udanganyifu, huwaongoza wanadamu kumtupia Mungu lawama, kana kwamba mateso haya yote yalikuwa ni matokeo ya mpango wa uumbaji wa Mungu. Watu walipogundua udanganyifu wa Kanisa la Roma, aliwachochea kuichukulia dini kuwa ni ulaghai na Biblia kama hekaya za kubuni.

## Kosa Baya

Kosa kubwa lililosababisha mabaya haya kwa Ufaransa ilikuwa ni kupuuza ukweli huu mkuu: kwamba uhuru wa kweli uko kwenye uzingatiaji wa makatazo yaliyobainishwa katika sheria ya Mungu. “Laiti ungasikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji, na haki yako kama mawimbi ya bahari.” Isaya 48:18. Wale ambao hawatajifunza kutoka katika Kitabu cha Mungu wanapaswa kukisoma kupitia histona.

Shetani alipolitumia Kanisa la Roma kuwapotosha watu wasitii, kazi yake ilikuwa inafanywa kwa hila. Kutokana na utendaji wa Roho wa Mungu makusudio ya Shetani yalizuiliwa yasikomae na kuzaa matunda. Watu hawakufuatilia matokeo ya tendo na kugundua chanzo cha masumbuko yao. Lakini wakati wa Mapinduzi Baraza la Taifa liliiweka kando sheria ya Mungu. Na kwenye Enzi ya Hofu kuu iliyofuata, athari za tendo na matokeo zingeonekana kwa watu wote.

Kuvunjwa kwa sheria njema na ya haki ya Mungu kungeleta uharibifiu. Roho wa Mungu azuiaye na kudhibiti nguvu za ukatili wa Shetani, kwa kiwango kikubwa alikuwa ameondolewa, na yule
[185] anayependelea kuona wanadamu wakiwa kwenye hali mbaya aliachwa kutenda kazi. Waliokuwa wamechagua uasi waliachwa kuvuna matunda yake. Nchi ilikuwa imejaa uhalifu. Kutoka kwenye mikoa iliyoharibiwa na miji iliyokuwa imeangamia kilio cha kuogofya kilisikika kwa maumivu na uchungu mkuu. Ufaransa ilikuwa imetikiswa kwa mfano wa tetemeko la nchi. Dini, sheria, utaratibu wa kijamii, familia, taifa na kanisa - vyote vilikuwa vimeangushwa na mikono ya udhalimu iliyokuwa imeinuliwa kinyume cha sheria ya Mungu.

Mashahidi waaminifu wa Mungu walikuwa wamechinjwa na utawala wa “mnyama atokaye katika kuzimu,” wasingeendelea kunyamaza kwa muda mrefu. “Na baada ya siku hizo tatu u nusu, roho ya uhai itokayo kwa Mungu ikawaingia, wakasimama juu ya miguu yao; na hofu kuu ikawaangukia watu waliowatazama.” Ufunuo 11:11. Mwaka 1793 amri zilitolewa kutoka katika Bunge la Ufaransa kupiga marufuku Biblia. Miaka mitatu na nusu baadaye, azimio la kutangua maagizo hayo lilikubaliwa na baraza hilohilo.

Wanadamu walikuwa wamegundua umuhimu wa imani kwa Mungu na Neno lake kama msingi wa utu wema na uadilifu.

Kuhusiana na "mashahidi wawili"[Agano la Kale na Jipya] nabii anaendelea kusema: "Wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni ikiwaambia, Pandeni hata huku. Wakapanda mbinguni katika wingu, adui zao wakiwatazama." Ufunuo 11:12. "Mashahidi wawili wa Mungu" wametukuzwa sana kuliko ilivyokuwa hapo awali. Mwaka 1804 Shirika la Biblia la Uingereza na Nchi za Nje lilianzishwa, likifuatiwa na mashirika mengine ya aina hiyo barani Ulaya. Mwaka 1816 shirika la Biblia la Amerika lilianzishwa. Tangu wakati huo Biblia imetafsiriwa katika mamia ya lugha. (Angalia Kiambatisho.)

Kabla ya mwaka 1792 kazi ya utume katika nchi za nje ilikuwa imepewa uzito kidogo. Lakini kuelekea mwisho wa kame ya kumi na nane mabadiliko makubwa yalitokea. Watu hawakuridhika na falsafa ya mantiki na walitambua umuhimu wa ufunuo wa Mungu na dini ya vitendo. Kuanzia wakati huu vituo vya kimisionari nchi za nje vilifikia ukuaji ambao haukuwepo hapo kabla.(Angalia Kiambatisho).

Maendeleo katika taaluma ya uchapishaaji yameleta msukumo katika usambazaji wa Biblia. Kusambaratika kwa hisia za kale, ubaguzi wa utaifa, na kupotea kwa nguvu za utawala wa Papa wa [186]
Roma; kumefungua njia kwa ajili ya Neno la Mungu. Kwa sasa Biblia imepelekwa kila mahali duniani.

Mkanamungu Voltaire alisema: "Nimechoshwa na watu wanaorudia rudia kusema, watu kumi na wawili walianzisha dini ya Kikristo. Nataka kuwathibitishia kwamba mtu mmoja anatosha kuiangusha." Mamilioni wamejiunga kuipiga vita Biblia. Lakini haiwezekani kuiharibu. Pale palipokuwa na Biblia mia moja wakati wa Voltaire, leo hii kuna nakala laki moja za Kitabu cha Mungu. Kwa kauli ya Mwanamatengenezo wa awali, "Biblia ni chuma anachopondea mhunzi ambacho kimechakaza nyundo nyingi."

Chochote kilichojengwa juu ya mamlaka ya mwanadamu kitaangushwa, na kile kilichojengwa juu ya mwamba wa Neno la Mungu, kitasimama milele.

[187] # Sura Ya 16 - Kuutafuta Uhuru Katika Ulimwengu Mpya

Mamlaka na kanuni za imani ya Kanisa la Roma ziliachwa na Kanisa la Uingereza. Lakini taratibu nyingi za ibada hazikuachwa. Ilidaiwa kuwa mambo ambayo hayajakatazwa ndani ya Maandiko hayana asili ya uovu. Kuyashika kulielekea kupunguza umbali uliotenganisha kati ya makanisa ya matengenczo na Kanisa la Roma. Pia ilidaiwa kwamba yangewahamasisha wauamini wa Kanisa la Roma kuikubali imani ya Waprotestanti.

Kundi lingine halikufuata dhana hiyo. Wao waliona kuwa desturi hizo ni ishara za utumwa wa kule walikokuwa wamekombolewa. Walitoa sababu kuwa Mungu, ndani ya Neno lake ameweka taratibu zinazoongoza ibada yake, na kwamba wanadamu hawana uhuru wa kuziongea ama kuzipunguza. Kanisa la Roma lilianza kwa kuamuru mambo ambayo Mungu hakuyakataza, likamalizia kwa kukataza yale ambayo kwa wazi aliyaamuru.

Watu wengi waliziona desturi za Kanisa la Uingereza kama makumbusho ya ibada ya sanamu, na hawakujiunga katika ibada zake. Lakini kanisa likisaidiwa na mamlaka ya serikali halikuruhusu maoni tofauti. Mikusanyiko ya ibada isiyo na kibali ilipigwa marufuku kwa adhabu ya kifungo, kuhamishwa, au kifo. Watu walioitwa Puritans waliwindwa, waliteswa, na kufungwa gerezani; hawakuweza kugundua ahadi ya siku zilizo bora. Baadhi yao walipoamua kutafuta hifadhi huko Uholanzi, walisalitiwa na kutiwa mikononi mwa adui zao. Uvumilivu wa kudumu hatimaye ulishinda, na walipata hifadhi kwenye fukwe nzuri.

Walikuwa wameacha nyumba zao na njia za kupatia mahitaji yao. Walikuwa wageni kwenye nchi ya ugeni wakalazimika kuishia kwenye kazi za kubahatisha ili kupata riziki zao. Lakini hawakupoteza muda kwa uvivu na manung'uniko. Walimshukuru Mungu kwa ajili ya baraka alizowapa na wakapata furaha kwenye ushirika wa kiroho usio na usumbufu.

## Mungu Alidhibiti Matukio [188]

Mkono wa Mungu ulipoonekana kana kwamba unawaelekeza ng'ambo ya bahari katika nchi ambayo wangeanzisha taifa ambalo wangeacha urithi wa uhuru wa dini kwa watoto wao; walisonga mbele wakiwa katika uongozi wa Mungu. Mateso na kufukuzwa kulifungua njia kuelekea kwenye uhuru.

Mara ya kwanza walipolazimishwa kujitenga na Kanisa la Uingereza, watu walioitwa *Puritans* walijiunga wenyewe kwa agano kama watu wa Mungu walio huru "kutembea pamoja katika njia zake zote wanazozijua au watakazozijua" [180] Hapa ndipo ilipokuwa kanuni ya muhimu ya Uprotestanti. Wakiwa na lengo hili Mahujaji waliondoka kutoka Uholanzi ili watafute makao kwenye Ulimwengu Mpya. John Robinson, mchungaji wao, katika hotuba yake ya kuwaaga aliwaambia: Nawapa wajibu mbele za Mungu na malaika zake wenye baraka kunifuata mimi si zaidi ya vile nilivyomfuata Kristo. Kama Mungu atawafunulia kitu chochote, kwa kutumia chombo chake chochote, mwe tayari kupokea kama mlivyokuwa tayari kuupokea ukweli wa huduma yangu; maana nina hakika Bwana anao ukweli na nuru ambayo hajaitoa bado kutoka kwenye Neno lake takatifu." [181]

"Kwa upande wangu, siwezi kuisikitikia kwa ukamilifu hali ya makanisa yaliyofanya matengenezo, ni nani...kwa wakati huu, ambao hawatakwenda mbali zaidi kuliko kuwa watumishi wa matengenezo. Walutheri hawawezi kuvutwa na kwenda mbali ya kile alichokiona Luther;...na wafuasi wa Calvin, unaona, wanasimama imara pale walipochwa na yule mtu wa pekee wa Mungu, ambaye naye hakuona vitu vyote...Ingawa kwa wakati wao walikuwa ni nuru iliyokuwa inawaka na kung'aa, lakini hawakupenya kwenye mawaidha yote ya Mungu, lakini kama wangekuwa hai, wangekuwa tayari tena kuipokea nuru zaidi kama ile waliyoipokea awali." [182]

"Ikumbukeni ahadi na agano kati yenu na Mungu na ninyi kwa ninyi, kuupokea ukweli na nuru yoyote atakayoifunua kwenu kutoka kwenye Neno lililoandikwa; lakini juu ya hayo, iweni waangalifu, ninawasihi, ni kitu gani mnakipokea kama ukweli, na kukilin- [189]

[180] J. Brown, The Pilgrim Fathers, p. 74.

[181] Martyn, vol. 5, p. 70.

[182] D. Neal, History of Puritans, vol. 1, 269.

ganisha na kukipima kwa Maandiko mengine ya ukweli kabla ya kukikubali; maana haiwezekani ulimwengu wa Kikristo uchelewe kutoka kwenye giza hili nene la mpinga Kristo, na ule ufahamu mkamilifu utatokea mara.” [183]

Shauku ya uhuru wa dhamiri iliwatia moyo Mahujaji kuivuka bahari, kuuvumilia ugumu wa jangwani, na kuuweka msingi wa taifa kubwa. Lakini Mahujaji hawakufahamu bado kanuni ya uhuru wa kidini. Uhuru walioupata kwa kujitoa mhanga sana, hawakuwa tayari kuutoa kwa wengine. Fundisho linalosema kwamba Mungu amelipatia kanisa haki ya kudhibiti dhamiri, kubaini, na kuadhibu uasi, ni moja kati ya yale makosa ya utawala wa Papa yenye mizizi ya kina. Wanamatengenezo, hawakuachwa huru kabisa, bila ile roho ya Kanisa la Roma ya kutovumiliana. Giza nene ambalo kwalo Kanisa la Roma lilikuwa limeufunika ulimwengu wa Ukristo, lilikuwa halijatawanyika kikamilifu.

## Roger Williams

Kama ilivyokuwa kwa Mahujaji, Roger Williams alikuja kwenye Ulimwengu Mpya ili kufurahia uhuru wa kidini. Lakini, yeye, kinyume na wao, alikuwa ameona kile ambacho wachache sana walikuwa wamekiona-kwamba uhuru ni haki ya wote isiyoweza kuondolewa. Alikuwa mtafutaji wa dhati wa ukweli. Williams “alikuwa mtu wa kwanza katika ulimwengu wa Ukristo wa kisasa kuanzisha serikali ya kiraia yenye msingi wa fundisho la uhuru wa dhamiri.” [184] “Umma au mahakimu wanaweza kuamua,” alisema, “iliyo haki kutoka mwanadamu hadi mwanadamu; lakini wanapojaribu kuamuru wajibu wa mwanadamu kwa Mungu, wametoka nje ya mstari, na hakutakuwa na usalama; maana ni wazi kuwa kama hakimu angekuwa na uwezo, leo angeweza kuamuru aina moja ya maoni au imani na kesho aina nyingine; kama ilivyofanywa na wafalme na malkia mbalimbali huko Uigereza na Mapapa na mabaraza mbalimbali ndani ya Kanisa la Roma.” [185]

[190] Mahudhurio kanisani yalikuwa yanalazimishwa kwa adhabu ya faini au kifungo. “Kuwalazimisha wanadamu waungane na wale

[183] Martyn, vol. 5, pp. 70, 71.
[184] Bancroft, pt. 1, ch.15, par. 16.
[185] Martyn, vol. 5, p. 340.

wenye imani tofauti nao, Williams alichukulia kuwa ni ukiukaji wa wazi wa haki za asili; kuwakokota wasio na dini na wasio hiari hadi kwenye ibada ya hadhara, ilionekana tu kama kushurutisha unafiki... 'Hakuna mtu apaswaye kulazimishwa kuabudu au kuendesha ibada kinyume na matakwa yake'" [186]

Roger Williams aliheshimiwa, lakini hitaji lake la uhuru wa kidini halikuweza kuvumiliwa. Ili kujiepusha asikamatwe alilazimika kutoroka katikati ya baridi na dhoruba za msimu wa baridi hadi kwenye msitu usiofikika.

Anasema, "Kwa majuma kumi na manne, nilikuwa nimetupwa pekee yangu kwenye kipindi kichungu, bila kujua mkate ama kitanda vilimaanisha nini." Lakini "Kunguru walinilisha jangwani" na mti wenye uwazi mara zote ulitumika kama nyumba. [187] Aliendelea na ukimbizi wake wenye uchungu kupitia kwenye barafu na msitu usio na njia hadi alipopata kimbilio kwenye kabila moja la Kihindi ambalo lilimwamini na kumpenda.

Aliweka msingi wa taifa la kwanza la kisasa ambalo lilitambua "kuwa kila mtu anatakiwa awe na uhuru wa kumwabudu Mungu kulingana na nuru ya dhamiri yake." [188] Taifa lake dogo la Rhode Island, liliendelea kukua na kustawi hadi misingi ya kanuni zake-uhuru wa kiraia na wa kidini-zilipokuwamisingi ya Jamhuri ya Marekani.

## Hati ya Uhuru [191]

Tamko la uhuru wa Marekani linasema kuwa: "Tunaaminikuwa ukweli huu ni bayana; kwamba watu wote wameumbwa sawa; kwamba wamepewa na Mwumbaji wao haki kadhaa zisizoweza kuondolewa; kwamba miongoni mwa hizo ni uhai, uhuru, na kutafuta furaha." Katiba inatoa uhakikisho wa heshima ya dhamiri: "Bunge halitatunga sheria yoyote inayohusu kuanzisha dini, au kupiga marufuku uhuru wa kufanya hivyo."

Walioiunda Katiba waliitambua kanuni ya milele kuwa uhusiano wa mwanadamu na Mungu, uko juu ya sheria zilizotungwa

[186] Bancroft, pt. 1, ch. 15, par. 2.
[187] Martyn, vol. 5, pp. 349, 350.
[188] Ibid., vol. 5, p. 354.

na wanadamu, na haki yake ya dhamiri haiondosheki...Ni kanuni anayozaliwa nayo ambayo hakuna kinachoweza kuing'oa." [189]

Habari zilisambaa katika Ulaya yote kuhusu nchi ambayo kila mtu anaweza kufurahia matunda ya kazi yake na kuiridhisha dhamiri yake. Maelfu walifurika katika fukwe za Ulimwengu Mpya. Ndani ya miaka ishirini baada ya nanga ya kwanza kutiwa pale Plymouth (1620), maelfu wa Mahujaji walikuwa wamefanya makazi katika New England. "Hawakuomba chochote kutoka ardhini isipokuwa mapato ya haki ya kazi yao...Kwa ustahimilivu waliuvumilia upweke wa nyikani, wakiumwagilia mti wa uhuru kwa machozi yao, na kwa jasho la nyuso zao, hadi ulipokita mzizi chini ya nchi."

## Kinga ya Uhakika kwa Ukuu wa Taifa

Kanuni za Biblia zilifundishwa nyumbani, shuleni, na kanisani; matunda yake yalidhihirika katika mafanikio, akili, usafi, na kiasi. Kwa miaka mingi mtu asingeweza kumwona "mlevi, ama kusikia jina la Mungu linatajwa bure, au kukutana na ombaomba." [190]

[192] Kanuni za Biblia ni kinga ya uhakika kwa ukuu wa taifa. Makoloni dhaifu yalikua na kuwa nchi zenye nguvu, na ulimwengu uliweka alama ya ustawi wa "kanisa bila Papa, na nchi pasipo mfalme" Lakini idadi iliongezeka ya watu waliovutwa kwenda Marekani wakisukumwa na malengo tofauti na yale ya Mahujaji. Idadi ya wale waliokuwa wanatafuta faida za kidunia tu iliongezeka.

Wakoloni wa awali waliruhusu washiriki wa kanisa pekee kupiga kura au kupewa uongozi serikalini. Kipimo hiki kilikubalika ili kutunza usafi wa taifa; matokeo yake yalikuwa ni uharibifu kwa kanisa. Wengi walijiunga na kanisa bila badiliko la moyo. Hata ndani ya huduma walikuwemo wasiojua uwezo wa Roho Mtakatifu unaomfanya mtu kuwa mpya. Tangu wakati wa Kostantino hadi sasa, kujaribu kulijenga kanisa kwa msaada wa serikali, yaweza kuonekana kuwa ulimwengu unavutwa karibu na kanisa, lakini uhalisia ni kwamba kanisa linavutwa karibu na ulimwengu.

Makanisa ya Kiprotestanti ya Marekani na yale ya Ulaya, yalishindwa kusukuma mbele njia ya matengenezo. Walio wengi, kama vile Wayahudi wakati Wakristo au waumini wa Kanisa la

[189] Congressional Documents (U. S. A), serial No. 200, Document No. 271.

[190] Bancroft, pt. 1, ch. 19, par. 25.

Papa wakati wa Luther, waliridhika kuamini kile ambacho baba zao waliamini. Makosa na mapokeo potovu vilitunzwa. Matengenezo yalikufa polepole, hadi ilipoonekana kuwa kunahitaji kubwa la matengenezo ndani ya makanisa ya Waprotestanti kama ilivyokuwa kwa Kanisa la Roma wakati wa Luther. Kulikuwa na tabia ile ile ya kuheshimu maoni ya watu na kulibadilisha Neno la Mungu na mahali pake kuweka nadharia za wanadamu. Watu waliacha kuyachunguza Maandiko na hivyo wakaendelea kushika mafundisho yasiyo na msingi kwenye Biblia. Majivuno na ubadhirifu viliendelezwa ndani ya umbo la dini, na makanisa yakaharibika. Desturi ambazo baadaye zingewaharibu mamilioni; zilikuwa zinakita mizizi chini. Kanisa lilikuwa linaziinua desturi hizi badala kushindania "imani waliyopewa watakatifu mara moja." Hivi ndivyo zilivyohafifishwa kanuni ambazo Wanamatengenezo walizitesekea sana.

[193] 

# Sura Ya 17 - Ahadi Za Ujio Wakristo

Ahadi ya kuja kwa Kristo mara ya pili kukamilisha kazi kubwa ya ukombozi ni wazo kuu la Maandiko Matakatifu. Tangu Bustani ya Edeni, wana wa imani wamekuwa wakingojea kuja kwake Yeye Aliyeahidiwa kuwarejeshea Paradiso iliyokuwa imepotea.

Henoko mtu wa saba kutoka kwa kwao waliokuwa wanaishi Edeni, ambaye alitembea na Mungu kwa kame tatu anasema, "Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote." Katika usiku wa maumivu makali Ayubu alipaza sauti yake na kusema, "Lakini mimi najua ya kuwa Mteteaji wangu yu hai, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi:...Lakini, pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mungu; Nami nitamwona mimi nafsi yangu, na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine." Ayubu 19:25-27. Washairi na manabii wa Biblia wameelezea sana habari za kuja kwa Kristo kwa maneno yenye kuvutia sana. "Mbingu na zifurahi na nchi ishangilie, ...mbele za Bwana: kwa maana anakuja, Kwa maana anakuja ili aihukumu nchi: Atauhukumu ulimwengu kwa haki." Zaburi 96:11-13.

Isaya anasema: Na katika siku hiyo watasema, Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie; Huyu ndiye Bwana tuliyemngoja, Na tushangilie na kuufurahia wokovu wake." Isaya 25:9.

Kipindi kile Mwokozi alipokaribia kutenganishwa na wafuasi wake, aliwafariji kwa huzuni waliyokuwa nayo kwa kuwathibitishia kwamba atakuja tena: "Msifadhaike mioyoni mwenu; ...maana naenda

kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda...nitakuja tena niwakaribishe kwangu." "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake; na mataifa yote watakusanyika mbele zake" Yn. 14:2, 3; 25:31,32.

Malaika walimdia kuwaambia wanafunzi juu ya ahadi ya kumdi kwake: "Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu

mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni." Mdo. 1:11. Na Paulo anashuhudia: "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti [194] ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu" 1 Wathesalonoke 4:16. Nabii wa Patmo anasema: "Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona" Ufu. 1: 7.

Kanuni ya muda mrefu ya uovu itakomeshwa: "Ufalme wa dunia" umekwisha kuwa "ufalme wa Bwana wetu na Wakristo wake, naye atamiliki hata milele na milele." Ufu. 11:5. "Bwana MUNGU atakavyootesha haki na sifa mbele ya mataifa yote." Isaya 61:11.

Ufalme wa amani wa Masihi utaanzishwa: "Maana Bwana amefariji Sayuni; amepafariji mahali pake palipokuwa ukiwa; amefanya jangwa lake kuwa kama bustani ya Edeni, na nyika yake kama bustani ya Bwana." Isaya 51:3.

Kuja kwa Bwana limekuwa ni tumaini la wafuasi wake wa kweli kwa vizazi vyote. Katikati ya maumivu na mateso, "mafunuo ya Mungu mkuu na Mwokozi wetu" limekuwa ni "tumaini lenye baraka" Tito 2:13. Paulo alikuwa analenga tukio la ufufuo utakaoambatana na kuja kwa Mwokozi, wakati wale waliokufa katika Kristo watafufuka, wataungana na walio hai na kisha kunyakuliwa ili wakutane na Bwana hewami. "Kwa hiyo," alisema, "farijianeni kwa maneno hayo" 1 Wathesalonoke 4:17.

Katika kisiwa cha Patmo Mwanafunzi mpendwa alisikia ahadi kwamba, "Naam; naja upesi." Na mwitikio wake unawakilisha ombi la kanisa, "na uje, Bwana Yesu." Ufunuo 22:20.

Kutoka kwenye gereza la chini ya ardhi, kwenye mti na mbele ya jukwaa la kuchomea watu moto, mahali ambapo watakatifu na wafiadini waliushuhudia ukweli, yalitoka maneno ya imani na tumaini lao kwa kame nyingi. Mmoja kati ya Wakristo hawa alisema, "Wakiwa na uhakika juu ya kufufuka kwake, na kisha ufufuo wao wenyewe Yeye atakapokuja, kwa ajili ya hili; walikidharau kifo, na walionekana kuwa wako juu ya kifo." [191]

Watu waliokuwa wanaitwa Waldensia waliidumisha imani hiyo [195] hiyo. Wycliffe, Luther, Calvin, Knox, Ridley, na Baxter walitazamia kwa imani kuja kwa Bwana. Hilo pia lilikuwa ni tumaini la kanisa

[191] Daniel T. Taylor, The Reign of Christ on Earth: or, The Voice of the Church in All Ages, p. 33.

la mitume, tumaini la "kanisa la jangwani", na lile la Wanamatengenezo.

Unabii hautabiri tu namna na kusudi la kuja kwa Kristo, lakini unaonesha ishara zitakazowajulisha watu kwamba ile siku imekaribia. "kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota" Luka 21:25. "jua litatiwa giza, na mwezi hatautoa mwanga wake. na nyota za mbinguni zitakuwa zinaanguka, na nguvu zilizo mbinguni zitatikisika. Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nyingi na utukufu." Marko 13:24-26. Hivi ndivyo Yohana wa Ufunuo alivyoielezea ishara ya kwanza kati zile zitakazotangulia kuja kwake mara ya pili: "palikuwa na tetemeko kuu la nchi; jua likawa jeusi kama gunia la singa, mwezi wote ukawa kama damu."

## Tetemeko Lililotikisa Dunia

Kama utimilifu wa unabii huu, mwaka 1755, kulitokea tetemeko la kutisha zaidi kuwahi kuwekwa kwenye kumbukumbu. Linajulikana kama tetemeko la Lisbon, lilienea katika mabara ya Ulaya, Afrika, na Marekani. Tetemeko hilo lilitokea huko Greenland, visiwa vya West Indies, Madeira, Norway na Sweden, Uingereza na Ireland, na lilienea kwenye maili za mraba zisizopungua milioni 4. Katika Afrika nguvu yake ilikuwa sawa na ile iliyokuwa Ulaya. Sehemu kubwa ya nchi ya Algiers iliharibiwa. Wimbi la bahari lililochukua eneo kubwa liligharikisha pwani ya Hispania na Afrika na kuimeza miji.

Baadhi ya ile milima mikubwa ya Ureno, ilitikiswa kwa nguvu, kana kwamba ni kutoka kwenye misingi yake: na baadhi ya milima vilele vyake vilifunuka, kugawanyika na kuvunja vunjwa kwa namna ya ajabu, vifusi vyake vikubwa vilitupwa kwenye mabonde yaliyokuwa jirani. Inasemekana kuwa miali ya moto ilitokea katika milima hii.

Katika mji wa Lisbon, "Ngurumo ya radi ilisikika kutoka chini ya ardhi, na ghafla baadaye, mshindo mkuu uliitupa chini sehemu kubwa ya mji ule. Ndani ya dakika kama sita, watu wapatao elfu sitini walikuwa wameangamia. Bahari Kwanza bahari ilikupwa

na kuacha nchi kavu; baadaye lilikuja wimbi lenye kimo cha futi hamsini au zaidi ya kimo chake cha kawaida.” [192]

“Tetemeko lilitokea mwisho wa juma, watu wakiwa wamejaa kwenye makanisa na nyumba za watawa, ni wachache sana kati yao walisalimika” [193] “Hofu iliyowakumba watu ilikuwa haielezeki. Hakuna mtu aliyelia; ilikuwa ni zaidi ya machozi. Walikimbia huku na huko, wakiwa wamefadhaika kwa hofu na mshangao, wakipigapiga nyuso na vifua vyao nakulia ‘dunia imefika mwisho!’ Akina mama waliwasahau watoto wao, walizunguka wakikimbia wakiwa na misalaba yenye sanamu ya Yesu aliYesulubiwa. Kwa bahati mbaya wengi walikimbilia makanisani kwa ajili ya usalama; Sakramenti ilioneshwa lakini haikusaida, watu hawa maskini walikumbatia madhabahu; sanamu, mapadre, na watu walifunikwa katika maangamizi hayo ya jumla.” [196]

## Mwezi Na Jua Vyatiwa Giza

Miaka ishirini na mitano baadaye, ilionekana ishara nyingine iliyotajwa kwenye unabii-kutiwa giza kwa jua na mwezi. Wakati wa utimilifu wake ulikuwa umetajwa kwa usahihi katika mazungumzo ya Mwokozi akiwa na wanafiinzi wake kwenye mlima wa Mizeituni “Lakini siku zile, baada ya dhiki hiyo, jua litatiwa giza, na mwezi hatautoa mwanga wake.” Marko 13:24. Siku au miaka 1260 zilifikia mwisho wake mwaka 1798. Robo ya kame kabla, mateso yalikuwa yamekoma kabisa. Kufuatia mateso haya, jua lingetiwa giza. Siku ya tarehe 19 Mei 1780 unabii huu ulitimia.

Shahidi aliyeshuhudia kule Massachusetts analilielezea tukio kama ifuatavyo: “Wingu zito jeusi lilitanda katika anga lote isipokuwa ukingo mwembamba kwenye upeo wa macho, na kulikuwa na giza kama lile la saa 3 usiku wa majira ya joto . . .

“Woga, wasiwasi, na hofu iliamza kuingia katika akili za watu. Wanawake walisimama mlangoni wakiangilia nje kwenye sura ya nchi iliyofunikwa na giza; watu walirejea kutoka kwenye sehemu zao za kazi mashambani. Seremala aliacha vifaa vyake, Mfua chuma [197] aliiacha karakana, Mfanyabiashara aliacha meza yake. Watoto wa shule waliruhusiwa kutawanyika kwenda nyumbani, nao kwa

[192] Sir Charles Lyell, Principles of Geology, p. 495.

[193] Encyclopedia Americana, art. “Lisbon” (ed. 1831).

hofu walikimbia kwenda nyumbani. Wasafiri walijihifadhi kwenye nyumba za mashambani zilizokuwa karibu. "Ni nini kinachokuja?" kila mtu alikuwa anauliza. Ilionekana kana kwamba kimbunga kilikuwa kinakaribia kupita kwa kasi katika ardhi, au kana kwamba ilikuwa ni siku ya kuangamia kila kitu.

"Mishumaa ilitumika; na moto mkali uliwaka ukiwa na mwangaza mkubwa kama ule wa jioni isiyo na mbalamwezi katika kipindi cha kuputika. . . .Kuku walirudi kwenye mabanda yao na kulala, ngombe walirudi kwenye mabanda yao na kulala, vyura walitoa sauti zao, Ndege waliimba nyimbo zao za jioni, Popo walirukaruka. Lakini wanadamu walijua kwamba usiku haujafika. .

"Mikusanyiko ya watu katika sehemu . . . .nyingi ilikutana. Mafungu kwa ajili ya mahubiri ambayo yalikuwa hayajaandaliwa vizuri yalikuwa ni yale yale ya siku zote yaliokuwa yanaonesha kwamba giza liko kwenye unabii wa Biblia . . .Giza lilikuwa zito zaidi muda mfupi baada ya saa tano kamili." [194]

"Katika sehemu kubwa ya nchi, giza lilikuwa zito mno wakati mchana, kiasi kwamba watu hawakuweza kujua muda kwa kuangalia saa za mkononi au saa za ukutani wala hawakuweza kula au kufanya kazi zao za nyumbani, bila mwanga wa mshumaa." [195]

## Mwezi Kama Damu

"Giza la mchana lilikuwa sio la kawaida lenye kutisha kuliko lile la usiku. Ingawa mwezi ulikuwa mpevu, hakuna kitu kilichokuwa kinaonekana isipokuwa kwa msaada wa kutumia mwanga, ambao wakati unaonekana kutoka kwenye nyumba za jirani na sehemu nyingine kutoka umbali mfupi ilionekana kama giza la Misri
[198] lililoonekana kutopitisha miali ya mwanga." [196] "Kama kila kitu cha angani kinachotoa mwanga katika ulimwengu kingefunikwa na vivuli visivyo pitisha mwanga au kuondolewa, giza lisingekuwa

[194] The Essex Antiquarian, April 1899, vol. 3, no. 4, pp. 53, 54.

[195] William Gordon, Hisory of the Rise, Progress and Establishment of the Independence of the U.S.A., vol. 3, p. 57.

[196] Isaiah Thomas, Massachusetts Spy; or, American Oracle of Liberty, vol.10, no. 472, (May 25, 1780).

zito sana” [197] Baada ya usiku wa manane giza lilitoweka, na mwezi ulipoonekana kwa mara ya kwanza, ulikuwa na rangi ya damu.

Tarehe 19 Mei 1780 inakumbukwa katika historia kama “siku ya giza.” Tangu enzi za Musa hakuna giza zito, lililofunika sehemu kubwa ya nchi, na lililochukua muda mrefu lililowahi kuwekwa kwenye kumbukumbu. Maelezo yaliyotolewa na mashahidi walioona kwa macho ni mwangwi wa maneno yaliyoandikwa na Yoeli miaka 2500 iliyopita. “Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja hiyo siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo.” Yoeli 2:31.

“Basi mambo hayo yaanzapo kutokea,” Kristo alisema, “changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia.” Akawaonesha mtini wanafunzi wake, “Wakati iishapo kuchipuka, mwaona na kutambua wenyewe ya kwamba majira ya mavuno yamekaribia. Nanyi kadhalika, mwonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu.” Luka 21:28, 30,31.

Lakini kanisani upendo kwa Kristo na imani katika ujio wake imepungua. Watu wanaokiri ni wa Mungu walipofushwa wasiyaelewe maelekezo ya Mwokozi kuhusu ishara ya kuja kwake. Fundisho la kuja kwa Yesu mara ya pili limepuuzwa, hadi kwa kiasi kikubwa lilipokuwa limepuuzwa na kuachwa hasa Marekani. Jitihada kubwa katika utafutaji wa pesa, kukimbilia umaarufu na madaraka kuliwafanya watu kuifikiria kwamba siku hiyo ya kutisha iko wakati ujao, utaratibu wa sasa wa mambo utakapokuwa umepita.

Mwokozi aliwatahadharisha mapema hali ya wale watakaorudi [199]
nyuma katika imani kabla ya kuja kwa Yesu mara ya pili. Kwa wale watakaokuwa hai wakati huo, ujumbe Wakristo ni: “Basi, jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafula, kama mtego unasavyo; “Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu.” Luka 21:34, 36.

[197]Letter b Dr. Samuel Tenney, of Exter, New Hampshire, December 1785, in Massachussetts Historical Society Collections, 1792, (1st series, vol. 1, p. 97).

Ilikuwa ni jambo la muhimu kwamba wanadamu waamshwe ili wajiandae kwa ajili ya matukio ya kutisha ya kufungwa kwa mlango wa rehema.

Siku ya Bwana ni kuu, yenye kitisho sana; naye ni nani awezaye kuistahimili? Ni nani atakayesimama atakapoonekana yeye ambaye "uliye na macho safi hata usiweze kuangalia uovu." Na asiyeweza "kuangalia uovu?" "Nami nitaadhibu ulimwengu kwa sababu ya ubaya wake, na wenye dhambi kwa sababu ya hatia yao; nami nitaikomesha fahari yao wenye kiburi; nami nitayaangusha chini majivuno yao walio wakali." "Fedha yao wala dhahabu yao havitaweza kuwaokoa" "Na huko utajiri wao utakuwa mateka, na nyumba zao zitakuwa ukiwa" Yoeli 2:11; Habakuki 1:13; Isaya 13:11; Sefania 1:18,13.

## Mmwito wa Kuamka

Katika kuitazamia siku ya Bwana Neno la Mungu linawaita watu wake kuutafuta uso wake kwa toba: Kwa maana siku ya Bwana inakuja. Kwa sababu inakaribia; Takaseni saumu, kusanyeni kusanyiko kuu; Kusanyeni watu, litakaseni kusanyiko, Kusanyeni wazee, kusanyeni watoto, Na hao wanyonyao maziwa: . . . "Hao makuhani, wahudumu wa Bwana, na walie kati ya patakatifu na madhabahu" "nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea; rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu, mkamrudie Bwana, Mungu wenu; kwa maana yeye ndiye mwenye neema, amejaa huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema, naye hughairi mabaya." Yoeli 2:1, 15-17, 12, 13.

Ilikuwa inatakiwa ifanyike Kazi kubwa ya Matengenezo ili kuwaandaa watu kusimama katika siku ya BWANA. Kwa rehema yake Mungu alikuwa anataka kutuma ujumbe... kuwaamsha watu wake wanaomkiri na kuwaongoza kujiandaa kwa ajili ya ujio wa BWANA.

[200] Onyo hili linaonekana katika Ufunuo 14. Hapa kuna ujumbe wenye sehemu tatu unaowakilishwa ukitangazwa na malaika wa mbinguni na muda mfupi baadaye kufuatiwa na kuja kwa Mwana wa Adamu kuvuna "mavuno ya dunia." Nabii alimwona malaika... "akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri

hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:6,7.

Ujumbe huu ni sehemu ya "Injili ya milele." Kazi ya kuhubiri wamekabidhiwa wanadamu. Malaika watakatifu wanaelekeza, lakini kazi ya kuhubiri Injili inafanywa na watumishi Wakristo duniani. Watu waaminifu, ambao ni watiifu kwa uongozi wa Roho Mtakatifu wanaihesabu Injili kuwa ni, "bora kuliko biashara ya fedha, Na faida yake ni nyingi kuliko dhahabu safi." "Siri ya Bwana iko kwao wamchao, Naye atawajulisha agano lake." Mithali 3:14; Zaburi 25:14.

## Ujumbe Watolewa na Watu Duni

Kama wanateolojia wangekuwa walinzi waaminifu, wenye bidii na kwa maombi wakiyachunguza Maandiko Matakatifu, wangekuwa wameutambua wakati. Unabii ungewafunulia matukio ambayo yamekaribia kutimia. Lakini ujumbe ulihubiriwa na watu wanyenyekevu,. Wale wanaopuuzia kuutafuta ukweli ikiwa wanaweza kuupata wameachwa gizani. Lakini Mwokozi anasema, "yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima." Yohana 8:12. Kwa mtu huyo baadhi ya nyota zenye mng'ao wa mbinguni zitatumwa kumwongoza katika nuru yote.

Wakati Kristo alipokuja mara ya kwanza makuhani na waandishi wa Mji Mtakatifu wangezielewa "dalili za nyakati" na kutangaza ujio wa yeye aliyeahidiwa. Mika alieleza siku yake ya kuzaliwa. Danieli alieleza habari za kuja kwake mara ya kwanza. Mika 5:2, Danieli 9:25. Viongozi wa Wayahudi hawakuwa na kisingizio chochote iwapo walikuwa hawajui. Kutokujua kwao ilikuwa ni matokeo ya dhambi na kiburi cha kutojali.

Kwa ufahamu mkubwa wazee wa Israeli wangepaswa kujifunza [201]
mahali, wakati, mazingira, ya tukio kubwa la historia ya ulimwengu kuja kwa Mwana wa Mungu. Watu walitakiwa wawe wanakesha ili waweze kumkaribisha Mkombozi wa ulimwengu. Lakini kule Bethlehemu wasafiri wawili walikuwa wamechoka kutoka Nazareti walipita katika njia ndefu ya mtaani iliyo nyembamba ya kuelekea upande wa mashariki kabisa mwa mji, wakitafuta ma-

hali pa kulala usiku bila mafanikio. Hakuna mlango uliofunguliwa ili kuwakaribisha. Katika banda bovu lililokuwa limeandaliwa kwa ajili ya ng'ombe hatimaye walipata mahali pa kimbilio la kujihifadhi, na hapo Mwokozi wa ulimwengu alizaliwa

Malaika walipewa jukumu la kupeleka habari za furaha kwa wale waliokuwa wamejiandaa kuzipokea na ambao kwa furaha wangezieneza habari hizo. Kristo alinyenyekea akabeba asili ya mwanadamu, akabeba huzuni ili kuitoa nafsi yake kafara kwa ajili dhambi. Lakini malaika walitamani hata katika hali yake ya kudhalilishwa, Mwana wa Aliye juu angeonekana mbele za wanadamu akiwa na heshima na utukufu unaolingana na tabia yake. Je, watu wakuu wa dunia wangekusanyika katika mji mkuu wa Israeli kumpokea anapokuja. Je, malaika wangeandamana naye kwa kundi kubwa lililotarajiwa?

Malaika alitembelea dunia kuwaona wale waliokuwa wamejiandaa kumkaribisha Yesu. Hakuisikia sauti ya kusifu kwamba wakati wa kuja kwa Mwokozi ulikuwa karibu. Malaika alizungukazunguka huku na huko juu ya mji mteule na hekalu ambamo uwepo wa Mungu ulidhihirika kwa vizazi vingi, hata hapo kulikuwa na kutojali kwa namna ileile. Makuhani walitoa kafara zenye unajisi kwa majivuno na kiburi. Mafarisayo, kwa sauti za kupayuka walikuwa wakiwahutubia watu na kutoa maombi ya kujisifu kwenye njiapanda za mitaa. Wafalme, wanafalsafa, walimu wa sheria, wote hawakuujali ukweli wa kustaajabisha kwamba Mwokozi wa wanadamu alikuwa karibu kuonekana.

Kwa mshangao mjumbe wa mbinguni alitaka kurudi mbinguni akiwa na habari za kuaibisha, alipogundua kundi la wachungaji waliokuwa wakilinda mifugo yao. Kadiri walipoitazama kwa
[202] mshangao mbingu iliyokuwa imejaa nyota nyingi, waliuelewa unabii wa Masihi ajaye na walikuwa na hamu ya ujio wa Mkombozi wa ulimwengu. Hapa kulikuwa na kundi ambalo lilikuwa limeandaliwa kuupokea ujumbe wa mbinguni. Ghafla utukufu wa mbinguni ulitawala eneo lote, kundi la malaika wasioweza kuhesabika lilionekana; na kana kwamba haikutosha kwa mjumbe mmoja kuleta furaha iliyokuwa kuu sana kutoka mbinguni, sauti nyingi zilisikika katika wimbo ambao mataifa yote ya waliokombolewa wataimba siku moja: "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." Luka 2:14.

Ni somo zuri sana la kisa hiki cha ajabu cha Bethlehemu! Jinsi kinavyokemea kutokuamini kwetu, kiburi na hali ya kuridhika tuliyonayo. Jinsi kisa hiki kinavyotutahadharisha kuwa waangalifu, ili sisi pia tusije tukashindwa kuzitambua ishara za nyakati na kwa hiyo tukashindwa kuijua siku ya kujiliwa kwetu.

Sio tu miongoni mwa wachungaji wanyenyekevu ambapo malaika waliwakuta watu wanaosubiria ujio wa Masihi. Kwa watu wa mataifa pia walikuwepo watu waliokuwa wanatazamia ujio wa Masihi-watu matajiri na wenye hekima-wanafalsafa kutoka Mashariki. Katika Maandiko ya Kiebrania watu hawa walikuwa wanajifunza habari za nyota itakayoinuka katika Yakobo. Kwa shauku kubwa waliusubiria ujio wake Yeye ambaye hatakuwa tu "faraja ya Israeli" bali "Nuru ya kuwaangazia mataifa" na kuwa wokovu hata mwisho wa dunia." Luka 2:25, 32; Matendo 13:47. Nyota ya mbinguni iliyotumwa iliwaongoza wageni kutoka mataifa ya mbali hadi kwenye sehemu aliyozaliwa mfalme wa dunia.

Ni kwa "Wale wamtazamiao kwa wokovu" ndio ambao Kristo "atatokea mara ya pili, pasipo dhambi" Waebrania 9: 28. Kama habari za kuzaliwa kwa Mwokozi, ujumbe wa kuja kwa Kristo haukukabidhiwa kwa viongozi wa kidini. Waliikataa nuru kutoka mbinguni; kwa hiyo wao hawakuwemo katika idadi aliyoeleza mtume Paulo: "Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi.

Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi sio wa usiku, wala wa giza." 1 Wathesalonike 5: 4, 5.

Iliwapasa walinzi kwenye kuta za Sayuni kuwa wa kwanza kuzipata habari za ujio wa Mwokozi, iliwapasa wawe wa kwanza kutangaza kwamba yuko karibu. Lakini walikuwa wamekaa tu pasipo jitihada yoyote wakati watu wakiwa wamelala katika dhambi zao. Yesu aliliona kanisa lake, kama mtini usiozaa uliofunikwa na majani yadanganyayo wakati haukuwa na matunda. Roho ya unyenyekevu wa kweli, toba na imani vilikosekana. Kulikuwa na kiburi, dini ya matendo, ubinafsi, ukandamizaji. Kanisa lililorudi nyuma lilifumbia macho ishara za nyakati. Walimwacha Mungu na kujitenga na upendo wake. Kadiri walivyopuuzia kuishi sawasawa na maagizo, ahadi yake haikutimizwa kwao. [203]

Wengi miongoni mwa wale waliodai kuwa wafuasi Wakristo walikataa kuipokea nuru kutoka mbinguni. Kama walivyokuwa

Wayahudi wa zamani, hawakuujua wakati wa kujiliwa kwao. Bwana aliwapita wao na akawafunulia ukweli wake watu ambao kama walivyokuwa wafugaji wa Bethlehemu na mamajusi wa Mashariki, walizingatia ukweli wote waliokuwa wameupokea.

## Sura Ya 18 - Nuru Mpya Katika Ulimwengu Mpya [204]

Mkulima mnyofu na mwaminifu ambaye alikusudia kuujua ukweli alikuwa ni mtu aliyechaguliwa na Mungu kuongoza utangazaji wa kurudi kwa Yesu mara ya pili. Kama wanamatengenezo wengine wengi, William Miller alipambana na umaskini na alijifunza somo la kujinyima na kujikana nafsi

Hata katika wakati wa utoto wake alionesha ushahidi usio wa kawaida wa akili yenye uwezo katika utendaji. Alipokuwa mtu mzima akili yake ilikuwa na uwezo na maendeleo na alikuwa na hamu kubwa ya kujua maarifa. Kupenda kwake kujifunza na tabia ya kuwa mwangalifu katika kufikiri na kupima mambo kulimfanya awe na uamuzi sahihi na mtazamo sahihi. Alikuwa mwenye tabia nzuri kiroho na sifa njema kwa watu. Alipata sifa katika ofisi za kiraia na kijeshi. Utajiri na heshima vilionekana kuwa tayari kwa ajili yake..

Wakati wa utoto wake, alikuwa na uelekeo wa kuvutiwa na mambo ya dini. Hata hivyo mwanzoni mwa utu uzima aliingizwa kwenye chama cha deists (Yaani wanaoamini kuwepo Mungu mwumbaji lakini asiyejishughulisha na viumbe wake), watu ambao mvuto wao ulikuwa mkubwa maana wengi wao walikuwa raia wema wenye ubinadamu na wakarimu.. Wakiwa wanaishi kwenye taasisi za Kikristo, kwa kiasi fulani tabia zao zilikuwa zimeathiriwa na mazingira yao. Sifa njema zilizowajengea heshima, zilitokana na Biblia na lakini vipawa hivyo vizuri, vilipotoshwa na kuwa na ushwishi uliokuwa kinyume na Neno la Mungu. Miller aliongozwa kufuata mitazamo yao.

Fasili za Maandiko za wakati huo zilileta ugumu ambao kwake ulioelekea kutoondosheka: akiweka kando Biblia, bado imani yake mpya, , haikuleta kitu chochote bora, na alibaki katika hali ya kutoridhika. Lakini Miller alipokuwa na umri wa miaka 34, Roho Mtakatifu aliushawishi moyo wake juu ya hali yake ya dhambi. Hakuwa na uhakika wa furaha baada ya kifo. Mustakabali ulikuwa

giza na wakuhuzunisha. Akirejea katka hisia alizokuwa nazo kipindi hiki, alisema:

[205] "Mbingu zilikuwa kama shaba juu ya kichwa changu na dunia kama chuma miguuni pangu...Kwa Kadiri nilivyofikiri zaidi, ndivyo uamuzi wangu ulivyozidi kukosa umakini. Nilijaribu kuacha kufikiri, lakini sikuweza kuyadhibiti mawazo yangu. Kwa hakika nilihuzunika, lakini sikuelewa chanzo chake. Nilinung'unika na kulalamika lakini, sikujua ni kwa nani nilifanya hivyo. Nilijua kuwa kulikuwa na kosa, lakini sikujua ni kwa namna gani ama ni wapi kwa kuupata ukweli."

## Miller Apata Rafiki

"Ghafla" alisema, "tabia ya Mwokozi kwa dhahiri ilitia mvuto akilini mwangu". Ilionekana kuwa yupo Aliye bora na mwenye huruma kiasi cha yeye mwenyewe kulipia kosa la dhambi zetu na hivyo kutuokoa katika mateso na adhabu ya dhambi ... lakini swali liliibuka, inawezekanaje kuthibitika kwamba huyo yupo? Niligundua kuwa bila Biblia nisingeweza kupata ushahidi wa uwepo wa Mwokozi kama huyo, au ushahidi wa hali ya baadaye.

"Niliona kuwa Biblia ilikuwa inamdhihirishaMwokozi yule yule nilikuwa ninamhitaji; nilishangaa kuwa kitabu kisichovuviwa kingewezaje kuelezea kanuni zinazokidhi kikamilifu kwa kiasi hicho endana mahitaji ya ulimwengu ulioanguka. Ilinibidi kukubali kwamba Maandiko lazima uwe ni ufunuo kutoka kwa Mungu. Maandiko yakawa ndiyo furaha yangu; nilimpata rafiki Yesu. Mwokozi, kwangu akawa mkuu miongoni mwa elfu kumi; na Maandiko ambayo mwanzo yalikuwa giza na yenye kukinzana, sasa yakawa taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu .. Nilimpata Bwana Mungu kuwa mwamba katikati ya bahari ya maisha. Biblia ikawa kitabu changu kikuu cha mafunzo, na ninaweza kusema , nilichuguza kwa furaha kuu... nilistaajabu kwa nini nilikuwa sijauiona uzuri na utukufu wake hapo kabla, nikashangaa kuwa ningewezaje kuikataa nilipoteza hamu yote ya vitabu vingine na nilielekeza moyo wangu kupata hekima kwa Mungu" [198]

[206] Miller alikiri imani yake hadharani. Lakini wenzi wake wasioamini walitanguliza hoja zote ambazo yeye mwenyewe mara

[198] S. Bliss, Memories of William Miller, pp. 65-67

kwa mara alizipinga kwa kutumia Maandiko. Aliionesha mantiki ya kuwa kama Biblia ni ufunuo kutoka kwa Mungu, ni lazima ikubaliane yenyewe. Aliazimu kujifunza Maandiko na kupata uhakika endapo kila ukinzani uliokuwa dhahiri ungeweza kupatanishwa.

Bila kutumia vitabu vya ufafanuzi wa Biblia alilinganisha andiko na andiko kwa msaada wa maelezo ya pembeni na itifaki. Alianza na kitabu cha Mwanzo akasoma mstari mmoja baada ya mwingine, alipogundua kitu chochote chenye ugumu,ilikuwa ni desturi yake kukilinganisha na kila fungu lingine lililoelekea kurejeza kwenye mada inayohusika. Kila neno lilipewa uzito wake ndani ya fungu. Kwa hiyo wakati wowote alipokutana na aya ngumu kueleweka alitafuta maelezo kwenye sehemu nyingine za Maandiko. Alijifunza kwa maombi ya dhati ili apate ufahamu kutoka mbinguni, na akaupata uzoefu wa ukweli wa maneno ya mtunga zaburi kuwa: "Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga." Zaburi 119:130.

Alijifunza vitabu vya Danieli na Ufunuo kwa shauku kubwa na akagundua kuwa vielelezo vya vingeweza kueleweka. Aliona kuwa vielelezo vyote, sitiari, tashbihi, nk., vilikuwa vimeelezewa pale pale au vimefafanuliwa kwenye Maandiko mengine na vingeweza kueleweka neno kwa neno. Kiungo kimoja baada ya kingine katika mnyororo wa ukweli kilifanya jitihada yake kuwa na faida. Hatua kwa hatua alizifuatilia njia kuu za unabii. Malaika wa mbinguni waliongoza fikra zake.

Miller aliridhika kuwa mtazamo wa wengi kwamba kutakuwa na milenia ya muda mfupi kabla ya mwisho wa dunia haujengwi katika Neno la Mungu. Fundisho hili, linaloelekeza kwenye miaka elfu moja ya amani kabla ya kuja kwa Bwana, ni kinyume na mafundisho ya Kristo na mitume wake, ambao walitamka kwamba sharti ngano na magugu vikue pamoja hadi wakati wa mavuno, mwisho wa dunia, na kwamba "watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu."2Timotheo 3:13.

## Kuja Kwa Kristo Katika Mwili [207]

Fundisho la uongofu wa ulimwengu na utawala wa kiroho Wakristo halikushilikiwa na kanisa la mitume. Kwa ujumla ha-

likukubaliwa na Wakristo mpaka mwanzoni mwa kame ya kumi na nane. Lilifundisha watu kuutarajia ujio wa Bwana miaka mingi baadaye na liliwazuia wasiziangalie dalili zinazotangaza ukaribu wa marejeo yake. Liliwafanya wengi wadharau maandalizi ya kukutana na Bwana wao.

Miller aligundua kuwa kuja kwa Kristo ni halisi na atakuja katika mwili kama ilivyofundishwa wazi katika Maandiko. "Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu." "Nao watamwona Mwana wa Mungu akishuka pamoja na mawingu ya mbinguni kwa nguvu na utukufu mwingi." "Kama umeme utokavyo mashariki na kumulika hata magharibi; hivyo ndivyo atakavyokuja Mwana wa Adamu." "Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wake pamoja na malaika zake." Naye atatuma malaika zake pamoja na sauti ya tarumbeta nao watawakusanya watakatifu wake." 1 Wathesalonike.4:16,17; Mathayo 24:30,27; 25:31; 24:31.

Wakati wa kuja kwake, wenye haki waliokufa watafufuliwa na wenye haki walio hai watabadilishwa. "Hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa.". "Waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza: kisha sisi tulio hai tuliosalia tutanyakuliwa pamoja mawinguni, ili tumlaki Bwana hewani: hivyo tutakuwa na Bwana milele" 1 Wakorintho 15:51-53; 1 Wathesalonike 4:16-17.

Mwanadamu katika hali yake ya sasa, anafikwa na mauti, ni wa kuharibika; lakini ufalme wa Mungu hautakuwa wa kuharibika. Hivyo mwanadamu katika hali yake ya sasa, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu. Yesu atakapokuja, atawatunukia watu wake hali ya kutokufa, na kuwakaribisha waurithi ufalme ambao hata sasa wao ni warithi peke.

[208]

## Maandiko na Matukio ya Miaka

Maandiko haya na mengine yalimthibitishia Miller kwa uwazi kuwa utawala wa amani kwa ulimwengu mzima na kusimamishwa kwa ufalme wa Mungu duniani kutakuwa baada ya kuja kwa Yesu

mara ya pili. Zaidi ya hayo aliona kuwa hali ya ulimwengu ililingana na maelezo ya unabii wa siku za mwisho. Alilazimika kufikia hitimisho kuwa muda ambao dunia ilipewa katika hali yake ya sasa ulikuwa karibu kutimia.

"Ushahidi mwingine ambao ulikuwa na mguso hai katika moyo wangu" Miller alisema, "ni mtiririko wa matukio katika Maandiko Niligundua kuwa matukio yaliyotabiriwa ambayo yalitimizwa wakati uliopita, mara zote yaliyotokea ndani ya wakati uliowekwa matukio kwanza yalikuwa ni jambo la unabii tu, yalitimizwa kulingana na utabiri wake." [199]

Alipogundua kuwa mtiririko wa vipindi vya matukio unafika hadi wakati wa kuja kwa Yesu mara ya pili, alihesabu kuwa "muda uliotengwa kabla" ambao Mungu aliwafunulia watumishi wake. "Mambo yale yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele". Bwana alitamka kwamba, hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake." Kum. 29:29; Amo. 3:7. Wanafunzi wa Neno la Mungu wanaweza kutazamia kukutana na matukio makubwa katika historia ya mwanadamu yakioneshwa katika Maandiko.

"Nilikuwa nimekubali kabisa" alisema Miller, kuwa kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho; kwa kuwa liliandikwa na watu walioongozwa na Roho Mtakatifu, na liliandikwa kwa mafundisho ili sisi kupitia subira na faraja ya Maandiko tupate tumaini Nilijisikia kuwa katika kujitahidi kufahamu kile Mungu alichokifunua kwetu kwa neema yake, sikuwa na haki kuruka vipindi vya unabii." [200]

Unabii ulioonekana kufunua vizuri zaidi ujio Wakristo mara ya [209]
pili ni ule wa Daniel 8:14 "Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifii patakapotakaswa." Akiacha Maandiko yajitafsiri yenyewe, Miller alijifunza kuwa siku katika lugha ya mafumbo ya unabii huwakilisha mwaka mmoja. (Angalia Kiambatisho) Aliona kuwa siku za kiunabii 2300, au miaka halisi, ungeenda mbali zaidi ya kipindi cha kufungwa kwa mfumo wa dini wa Kiyahudi, kwa hiyo haikumaanishawa patakatifu pa mfumo huo.

[199] *Ibid.*, pp. 74,75.
[200] Ibid.

Miller aliukubali mtazamo wa jumla kuwa katika zama za Ukristo dunia ndipo "patakatifu" na kwa hiyo akaelewa kuwa kutakaswa kwa patakatifu kulikotabiriwa katika Daniel 8:14 kuliwakilisha utakaso wa dunia kwa moto wakati wa kuja kwake Kristo. Kama muda sahihi wa kuanza kwa siku 2300, ungefahamika, alihitimisha kuwa muda wa kurudi kwa Yesu mara ya pili ungekuwa umefunuliwa.

### Kugundua Ratiba ya Unabii

Miller aliendelea kuuchunguza unabii, alikesha wakati wa usiku na mchana akijifunza unabii ulioonekana kuwa na umuhimu wa ajabu. Katika sura ya 8 ya Danieli hakupata dokezo la mahali zilipoanza kuhesabiwa siku 2300; malaika Gabriel, ambaye ijapokuwa aliamriwa kumsaidia Danieli kuelewa maono alimpa maelezo ya juu juu tu. Kwa kadiri mateso ya kuogofya ambayo yangelipata kanisa yalivyofunuliwa kwa nabii, hakuweza kuvumilia zaidi. Danieli "alizimia na akawa mgonjwa kwa siku kadhaa." Naliyastaajabia yale maono lakini hakuna aliyefahamu." Alisema. Danieli 8:27.

Bado Mungu alimwagiza mjumbe wake kuwa, "mfahamishe mtu huyu maono haya." Kwa utii, malaika alirudi tena kwa Danieli, akisema; "nimetokea sasa ili nikupe akili upate kufahamu basi itafakari habari hii na kuyafahamu maono haya." Jambo moja la muhimu katika sura ya 8 liliachwa bila maelezo ambalo ni siku 2300; kwa hiyo malaika, alianza tena maelezo akikazia hasa juu ya wakati: "Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako na juu ya mji wako mtakatifu Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma sabini na katika majuma sitini na mawili kutajengwa tena pamoja na njia
[210] kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu. Na baada ya majuma sitini na mawili, masihi atakataliwa mbali atakuwa hana kitu; Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu." Daniel 8:16-9:22, 23, 24-27.

Malaika alitumwa kwa Danieli kuelezea sehemu ambayo alikuwa hajaielewa -"Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na

mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa.” Maneno ya kwanza ya malaika ni, “Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako na juu ya mji wako mtakatifu” Neno “kuamriwa” kiuhalisia linamaanisha “kuamriwa.” Majuma sabini, miaka 490 ingekatwa kwa ajili ya wayahudi.

### Vipindi Viwili vya Wakati Vyaanza Pamoja

Lakini ni kutoka katika kitu gani vipindi hivi vilikatwa? Kwa sababu siku 2300 ndio kipindi pekee kilichotajwa katika sura ya 8, majuma sabini yatakuwa ni sehemu ya siku 2300. Vipindi viwili lazima vianze pamoja , majuma sabini kuanzia tarehe ya ” amri iliyotolewa” kuujenga upya Yerusalemu. Endapo tarehe ya amri hii ingeonekana, mahali pa kuanzia kwa siku 2300 pangekuwa ni hakika.

Tamko linapatikana katika sura ya saba ya kitabu cha Ezra,, likitolewa na mfalme Artashasta wa Uajemi mwaka 457 B.C. Wafalme watatu katika kuanzisha na kukamilisha amri, walizifanya ukamilifu uliohitajika na unabii kuwa ndio mwanzo wa siku 2300. Ukichukua miaka 457 BC wakati tamko lilipotolewa , kama tarehe ya “amri” kila maelekezo ya majuma sabini yalionekana kukamilika. **(Angalia Kiambatisho)**

“Tangu amri ya kuujenga upya na kuutengeneza Yerusalemu mpaka masihi aliye mkuu kutakuwa na majuma saba, na majuma sitini na tisa au miaka 483. Amri ya Artashasta ilikuwa ni katika majira ya kupukutisha majani 457 B.C Kuanzia tarehe hii miaka 483 inakwenda mpaka wakati wa kupukutisha majani AD 27 wakati ambao unabii ulitimizwa katika wakati wa kupukutisha majani A.D 7 Yesu Kristo alibatizwa na Yohana na kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu Baaada ya ubatizo wake alikwenda Galilaya “akihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu , akisema ,wakati umetimia.” Marko .1: 41: 15.

### Injili Iliyotolevva Kvva Ulimwengu [211]

“Naye atafanya na kulithibisha agano kwa wengi kwa muda wa juma moja” Miaka saba ya mwisho ilitolewa kwa ajili ya Wayahudi. Wakati huu, kuanzia A.D. 27 mpaka A.D. 34, Kristo na wanafunzi

wake walitangaza Injili ya mwaliko hasa kwa Wayahudi. Maelekezo ya Kristo yalikuwa "Msiende kwa mataifa na wala miji ya wasamaria msiingie, lakini nendeni kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli, Mt 10: 56.

"Katikati ya juma ataikomesha sadaka na dhabihu" Katika A.D. 31, miaka mitatu na nusu baada ya ubatizo wake, Bwana wetu alisulubiwa. Katika kafara kuu iliyotolewa Kalvari, kielelezo kilikutana na kile kilicho halisi. Saadaka zote za kuteketeza na dhabihu za kila siku zilikoma.

Miaka 490 waliyopewa Wayahudi iliishia A.D 34, Wakati huo , kwa kitendo cha Baraza ya Kiyahudi la Sanhedrini taifa lilitia muhuri wa kuikataa Injili kwa kumwua Stefano na kuwatesa Wafuasi Wakristo. Kisha ujumbe wa wokovu ukatolewa kwa ulimwengu. Wanafunzi wakisukumwa na mateso walikimbia kutoka Yerusalemu " Wakihubiri Injili kila mahali" Matendo ya Mitume 8:4.

### Hitimisho la Kushtusha

Pale mwanzoni Miller hakuwa na tumaini la kufikia hitimisho alilofikia sasa. Yeye mwenyewe hakuamini kwa urahisi matokeo ya uchunguzi wake.. Lakini ushahidi wa Maandiko ulikuwa wazi kiasi cha kushindwa kuuweka kando.

Mnamo 1818 alisadiki kwa dhati kuwa baada ya miaka ishirini na tano Yesu angerudi kuokoa watu wake, "sihitaji kueleza," alisema Miller, "juu ya furaha iliyoujaza moyo wangu kwa taraja yenye furaha, wala shauku niliyo nayo kutaka kushiriki furaha ya waliokombolewa ...Oo ni kwa mng'ao na utukufu kiasi gani ukweli ulionekana!..."Swali lilimjia kwa nguvu kubwa kuhusiana na jukumu langu kwa ulimwengu, kwa mtazamo wa ushahidi uliougusa
[212] moyo wangu" [201] Alihitajika tu kuhisi kuwa ulikuwa ni wajibu wake kuwapatia wengine nuru aliyoipokea. Aliutazamia upinzani kutoka kwa kwa wale wasiomcha Mungu, lakini alikuwa na ujasiri kuwa Wakristo wangelifurahia tumaini la kukutana na Mwokozi . Alisita kulitoa taraja la ukombozi wenye utukufu, ulio karibu sana kutimizwa, asije akakosea na kuwapotosha wengine. Hivyo aliongozwa kupitia upya na kuufikiria kwa uangalifu kila ugumu

[201] Ibid., pp. 76, 77, 81.

ulioonekana katika akili yake. Miaka mitano aliitumia kupata usahihi wa msimamo wake.

### "Nenda Kauambie Ulimwengu"

"Wakati nikiwa kwenye shughuli zangu," alisema, "iliendelea kusikika katika masikio yangu, 'Nenda uuambie ulimwengu juu ya hatari inayoukabili.' Aya hii iliindelea kunijia: 'Nimwambiapo mtu mbaya, Ewe mtu mbaya, hakika utakufa, nawe husemi neno la kumwonya mtu huyo aiache njia yake, mtu mbaya huyo atakufa katika uovu wake, lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Walakini ukimwonya mtu mbaya kwa sababu ya njia yake, kusudi aiache; wala yeye asiiache; atakufa huyo katika uovu wake, lakini wewe utajiokoa roho yako.' Ezekieli 33:8, 9. Nilijihisi kuwa endapo waovu wataonywa kikamilifu; wengi wao watatubu; na kama hawataonywa, damu yao itatakiwa mkononi mwangu." [202] Maneno hayo yalikuwa yanajirudia rudia katika akili yake. "Nenda kauambie ulimwengu; damu yao nitaitaka mikononi mwako." Alisubiri kwa miaka tisa, jukumu hilo likimsumbua rohoni, hadi mwaka 1831 alipotangaza hadharani sababu za imani yake.

Wakati huo alikuwa na miaka hamsini, akiwa hana uzoefu wa kuhubiri hadharani, ila jitihada zake zilibarikiwa. Hotuba yake ya kwanza ilifuatiwa na uamsho mkuu wa kiroho. Familia nzima kumi na tatu, kasoro watu wawili tu, ziliongolewa. Aliombwa kwenda kuhubiri mahali pengine, na karibu kila mahali wadhambi waliongolewa. Wakristo waliamshwa na kujiweka wakfu kwa Mungu. Wenye mizaha na wasioamini Mungu wakaupokea ukweli wa Biblia. Hotuba zake za Neno la Mungu ziliamsha ari ya kiroho katika jamii na kupunguza kasi ya ukengeufu na anasa katika kizazi hicho.

Katika sehemu nyingi makanisa ya Kiprotestanti ya madhehebu [213]
karibu zote yalifungua milango yao kumruhusu ahutubie, na mialiko hiyo mara nyingi ilitoka kwa wachungaji wa makanisa hayo. Ilikuwa ni kanuni yake kutohutubia mahali ambapo hakupewa mwaliko, hata hivyo alijikuta hawezi kuhudumia hata nusu ya mialiko aliyokuwa anapewa. Wengi walishawishika juu ya uhakika na ukaribu wa kuja kwa Kristo na hitaji lao la kujiandaa.

[202] Ezekiel 33:8, 9; Bliss, p. 92

Katika baadhi ya miji mikubwa, wauza pombe walibadili maduka kuwa vyumba vya mikutano; sehemu za kamari zilifungwa; makafiri na mafisadi walibadilika. Mikutano ya maombi ilianzishwa na madhehebu mbalimbali iliyofanyika karibu kila saa, wafanya biashara wakikusanyika wakati wa adhuhuri kwa ajili ya sala na sifa. Hakukuwa na burudani za kifujaji. Kazi yake, kama ilivyokuwa kazi ya wana-matengenezo wa awali, ilikuwa na mwelekeo wa kushawishi ufahamu na kuamsha dhamiri kuliko kusisimua hisia tu.

Mwaka 1833 William Miller alipewa hati ya kuhubiri kutoka Kanisa la Kibaptisti. Idadi kubwa ya wachungaji wa madhehebu yake waliridhika na kazi yake; aliendelea na kazi yake kwa idhini yao. Alisafiri na kuhubiri bila kukoma; japo alikuwa hana kipato cha kutosha kukidhi gharama za safari kufika maeneo yote aliyoalikwa. Hivyo juhudi zake za hadhara ziliathiri sana mali zake.

## "Nyota Zitaanguka"

Mwaka 1833 ishara ya mwisho kati ya zile zizokuwa zimeahidiwa na Mwokozi kama dalili za kuja kwake itokea: "Nyota zitaanguka kutoka mbinguni." Naye Yohana katika Ufunuo anasema: "Na nyota zikaanguka juu ya nchi kama vile mtini upukutishavyo mapooza yake, utikiswapo na upepo mwingi" (Mathayo 24:29; Ufunuo 6:13). Unabii huu ulitimia kwa namna ya ajabu kwa anguko kuu la vimondo Novemba 13, 1833, onesho la ajabu la kuanguka kwa nyota lililochukua muda mrefu kabisa kuliko yote yaliyowahi kuandikwa katika kumbukumbu. "Hakujawahi kunyesha mvua kubwa kama ile ya vimondo vilivyoanguka chini; mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini, hali ilikuwa ile ile. Kwa kifupi, anga lote lilikuwa katika hekaheka. ... Tangu saa nane usiku mpaka kulipopambazuka kabisa, anga lilikuwa safi bila mawingu, onesho la vitu vinavyong'ara lilidumu katika anga lote." [203]

[214] "Ilionekana kana kwamba nyota zote mbinguni zimekutana katika upeo wa anga, na zilikuwa zinafyatuka kwa pamoja kwa kasi ya radi, zikielekea kila upande lakini zilikuwa haziishi—maelfu yali-

[203] R. M. Devens, American Progress: or, The Great Events of the Greatest Century, ch. 28, pars. 1-5.

fuata upesi katika njia ya maelfu kana kwamba zilikuwa zimeumbwa kwa ajili ya tukio hilo." [204]

"Taswira sahihi zaidi ya mtini unaopukutisha mapooza yake unapotikiswa na upepo mkali, ambayo ilikuwa haiwezekani kuitazama." [205]

Katika jarida la Biashara la New York la Novemba 14, 1833 kulitokea makala ndefu kuhusu hali hiyo: "Hakuna mwanafalsafa au mwanazuoni aliyewahi kusimulia au kuandika juu ya tukio kama lile la jana asubuhi. Nabii mmoja alilitabiri kwa usahihi karne kumi na nane zilizopita. kama tutakuwa na tatizo kuelewa kwamba kuanguka kwa nyota inamaanisha nyota zinazoanguka; maana pekee ambapo inawezekana kwa jambo hili kuwa kweli kama lilivyokuwa limeandikwa."

Kwa njia hiyo ilidhihirishwa dalili ya mwisho katika dalili za kuja kwake ambazo Yesu aliwaambia wanafunzi wake: "Nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, milangoni." (Mathayo24:33). Wengi walioshuhudia kuanguka kwa zile nyota, waliona jambo hilo kama tangazo la hukumu illiyokuwa inakuja.

Mwaka 1840 utimilifu mwingine wa unabii ulivuta usikivu mkuu wa watu. Miaka miwili kabla ya hapo, Josiah Litch aliandika ufafanuzi wa Ufunuo 9, ikitabiri kuanguka Himaya ya Ottoman mwaka 1840, mnamo mwezi wa nane." Siku chache tu kabla ya ku- [215]
timia kwa unabii huo aliandika: "Itakoma Agosti 11, 1840, ambapo himaya ya Ottoman huko Constantinople inatarajiwa kuvunjika."[206]

## Utabiri Watimia

Katika muda uliokuwa umetajwa, Uturuki ilikubali kuwa chini ya ulinzi wa majeshi ya umoja ya Ulaya, hivyo kujiweka yenyewe chini ya mataifa ya Kikristo. Tukio hilo lilitimiza unabii huo kwa usahihi. Watu wengi waliziamini njia za kufasili zilizokuwa zinatumiwa na Miller na wenzi wake. Wasomi na wakuu waliungana na Miller katika kuhubiri na kuchapisha maoni yake. Tangu mwaka 1840 hadi 1844 kazi ilipanuka kwa kasi.

[204] F. Reed, Christian Advocate and Joumal, Dec. 13, 1833.

[205] "The Old Countryman," Portland (Maine) Evening Advertiser, Nov. 26, 1833.

[206] Josiah Litch, Signs of the Times, August 1, 1840.V

William Miller alikuwa na uwezo mkubwa kiakili, na aliongezea hekima za mbinguni kwa kuwa na uhusiano na Chanzo cha Hekima. Aliheshimiwa po pote ambapo unyofu na ubora wa maadili ulikuwa unathaminiwa. Akiwa na unyenyekevu wa Kikristo, alikuwa msikivu na rafiki wa wote, akiwa tayari kuwasikiliza wengine na kupima hoja zao. Alizipima nadharia zote kwa Neno la Mungu, na busara zake na ujuzi wake wa Maandiko vilimwezesha kupinga uongo.

Lakini, kama ilivyokuwa kwa wanamatengenezo wa mwanzo, ukweli aliokuwa anaufundisha haukupokelewa na walimu mashuhuri wa kidini. Kwa vile walimu hao wa kidini hawakuweza kudumisha nafasi yao kwa Maandiko, waligeukia mafundisho ya wanadamu, desturi za Mababa. Lakini Neno la Mungu lilikuwa ushuhuda pekee uliokuwa unakubalika na wahubiri wa ukweli wa kuja kwa Yesu. Kejeli na dhihaka zilitumiwa na wapinzani ili kuwaharibia sifa wale waliokuwa wanafurahia kurudi kwa Bwana wao na walikuwa wakijitahidi kuishi maisha matakatifu na kuwaandaa wengine kwa ajili ya ujio wake. Ilifanywa ionekane kuwa ni dhambi kuchunguza unabii wa kurudi kwa Kristo na wa mwisho wa dunia. Hivyo huduma iliyopendwa na wengi ilihafifisha imani katika Neno la Mungu. Mafundisho yao yaliwafanya watu kuwa waovu, na wengi walihalalisha kuenenda kwa kuzifuata tamaa za watu waovu. Halafu waasisi wa uovu huo, walipeleka lawama zote kwa Waadventista.

[216] Huku akijaza wasikilizaji makini katika majumba, jina la Miller lilitajwa mara chache katika vyombo vya habari vya kidini isipokuwa kwa kubezwa au shutuma. Waovu, wakiwa wamehamasishwa na walimu wa kidini, waligeukia kejeli za kukufuru(p. 210) dhidi yake pamoja na kazi yake. Mzee huyu mwenye mvi aliyekuwa ameacha makazi yake mazuri na kusafiri kwa gharama zake mwenyewe kwa ajili ya kuupelekea ulimwengu onyo la hukumu iliyokuwa inakaribia, alishutumiwa kwamba alikuwa na itikati kali.

## Shauku na Kutokuamini

Shauku ilizidi kuongezeka. Kutoka makumi na mamia, makanisa yaliongezeka hadi kuwa na maelfu ya washiriki. Lakini baada ya muda, upinzani ulijitokeza dhidi ya waongofu hawa, na makanisa yakaanza kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wale waliokuwa

wakipokea maoni ya Miller. Jambo hili lilihitaji kujibiwa na Miller kwa maandishi: "Kama tumekosea, tafadhali mtuoneshe tulipokosea. Tuonesheni kosa letu kutoka kwenye Neno la Mungu; tumebezwa kiasi cha kutosha; kejeli haziwezi kutushawishi kuwa tumekosea; Neno la Mungu tu ndilo liwezalo kubadili maoni yetu. Uamuzi wetu umefanyika kwa umakini na maombi, kama tulivyouona ushahidi katika Maandiko." [207]

Wakati uovu wa watu waliokuwa wanaishi kabla ya Gharika ulipomfanya Mungu alete gharika duniani, kwanza aliwajulisha azma yake. Kwa miaka 120 lilitangazwa onyo kwa ajilinya kutubu. Walimbeza mjumbe wa Mungu. Ikiwa ujumbe wa Nuhu ulikuwa sahihi, ni kwa nini ulimwengu wote usiuone na kuuamini? Madai ya mtu mmoja dhidi ya hekima ya maelfu! Hawakutaka kuliamini lile onyo wala kutafuta hifadhi katika safina.

Wafanya dhihaka walionesha mfuatano wa majira usiobadilika, anga la samawi ambalo lilikuwa halijawahi kudondosha mvua. Kwa dharau, mhubiri wa haki walimwita mwendawazimu mwenye shauku. Waliendelea na njia zao mbaya kwa jeuri zaidi kuliko mwanzo. Lakini hukumu za Mungu zilimwagwa juu ya walioikataa rehema katika wakati uliokuwa umepangwa.

## Wabishi na Wasioamini [217]

Kristo alisema kuwa kama ilivyokuwa kwa watu wa siku za Nuhu, hawakutambua, "hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu" (Mathayo 24:39). Wakati wanadai kuwa watu wa Mungu wanajiunga na ulimwengu; wakati anasa za ulimwengu zinakuwa anasa za kanisa, wakati wote wakitarajia miaka mingi ya ustawi kiulimwengu—ndipo matumaini yao ya bandia yatakapokoma ghafla kama radi inavyopiga. Kama vile Mungu alivyomtuma mtumishi wake kuuonya ulimwengu kuhusu Gharika iliyokuwa inakuja, ndivyo alivyotuma wajumbe wake wateule kuutangaza ukaribu wa hukumu ya mwisho. Kama vile watu wa kizazi cha Nuhu walivyocheka wakibeza utabiri wa mhubiri huyo wa haki, ndivyo wengi wa wale waliokuwa wanaodai kuwa watu wa Mungu wakati wa Miller walivyokejeli maneno hayo ya onyo.

[207] BIiss, pp. 250, 252.

Hakuwezi kuwa na ushahidi wa uhakika zaidi kuwa makanisa yalikuwa yamemwacha Mungu kuliko chuki iliyochochewa na ujumbe huu uliotoka mbinguni.

Wale waliolikubali fundisho la ujio wa Yesu waliona kuwa wakati wa kufanya uamuzi ulikuwa umefika. Mbingu iliwakaribia na wakajiona kuwa na hatia mbele za Mungu." [208] Wakristo walifanywa waone kuwa muda ulikuwa mfupi, na mambo waliyokuwa wanapaswa kuyafanya kwa ajili ya wanadamu wenzao yalipaswa kufanyika haraka. Umilele ulionekana ukifunguka mbele zao. Roho wa Mungu alitia nguvu kusihi kwao wakiwaandaa watu kwa ajili ya siku ya Mungu. Maisha yao ya kila siku yalikuwa kemeo kwa washiriki wa kanisa waliokuwa hawajajiweka wakfu. Hawa hawakutaka kubughudhiwa katika starehe zao, kutafuta pesa, na kutafuta heshima ya kidunia. Hatimaye kukawa na upinzani dhidi ya imani juu ya ujio.

Wapinzani walijaribu kukatisha tamaa ya uchunguzi wa unabii kwa kufundisha kuwa unabii ulikuwa utiwa muhuri. Kwa hiyo, Waprotenstanti walifuata nyayo za Wakatoliki. Makanisa ya Kiprotestanti yalidai kwamba, sehemu muhimu ya Neno, se-
[218] hemu inayohusu hasa wakati wetu, ilikuwa haieleweki. Wachungaji walidai kuwa vitabu Danieli na Ufunuo vilikuwa mafumbo yasizoeleweka.

Lakini Kristo aliwaelekeza wanafunzi wake kwenye maneno ya nabii Danieli, "Asomaye na afahamu" (Mathayo 24:15). Kitabu cha Ufunuo kinapaswa kueleweka. "Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwapo upesi .... Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu." Ufunuo 1:1-3.

"Heri asomaye"—wapo ambao hawatasoma; "na wale wasikiao"—wapo wasiotaka kusikia cho chote kuhusu unabii; "na kuyashika yaliyoandikwa humo"—wapo wengi wanaokataa kuyashika maagizo yaliyotolewa katika kitabu cha Ufunuo; kati yao hakuna aliye na haki ya kudai baraka zilizoahidiwa.

Mwanadamu anawezaje kuthubutu kufundisha kuwa kitabu cha Ufunuo hakiwezi kueleweka na wanadamu? Ni siri iliyofunuliwa,

[208] Ibid.,p. 146.

yaani kitabu kilichofunguliwa. Kitabu cha Ufunuo kinaelekeza akili kwenye kitabu cha Danieli. Vyote viwili vintotoa maelezo muhimu juu ya matukio yanayoambatana na kufungwa kwa historia ya ulimwengu.

Yohana aliziona hatari, migongano, na ukombozi wa mwisho wa watu wa Mungu. Aliuandika ujumbe wa mwisho utakaokomaza mavuno ya nchi, ama kwa ajili ya ghala la mbinguni ama kwa ajili ya moto wa maangamizi, ili wale wanaouacha ukosefu waelezwe juu ya hatari na migongano iliyo mbele yao.

Ni kwa nini basi kuna ujinga ulitapakaa pote kuhusu sehemu hii muhimu ya Maandiko Matakatifu? Ni matokeo ya juhudi za makusudi za mkuu wa giza kuficha jambo ambalo litafichua uongo wake. Kwa sababu hiyo, Kristo ambaye ndiye afunuaye, akiiona kabla vita dhidi ya Ufunuo, aliahidi baraka kwa wote watakaosoma, watakaosikia, na kuushika unabii huu.

[219] # Sura Ya 19 - Kwa Nini Matumaini Yalivunjika?

Tangu kizazi hata kizazi,kazi ya Mungu, huonesha mfanano wa ajabu m katika kila matengenezo makubwa au harakati za kidini. Kanuni za Mungu za kushughulika na wanadamu ni zile zile siku zote. Harakati muhimu za sasa zinafanana na zile zilizopita na mambo yaliyolipata kanisa katika zama zilizopita yana mafundisho kwa ajili ya wakati wetu.

Kwa njia ya Roho wake Mtakatifu Mungu kwa huwaongoza watumishi wake wa duniani kwa namna ya pekee, kuendeleza kazi ya wokovu. Wanadamu ni vyombo katika mkono wa Mungu. Kila mmoja amepewa kiasi cha nuru inayotosha kufanya kazi aliyopewa. Lakini hakuna mwanadamu aliyewahi kuyaelewa kikamilifu makusudi ya Mungu katika kazi iliyopo kwa wakati wake. Wanadamu huwa hawauelewi kwa upana wote ujumbe wanaoutangaza kwa jina lake. Hata manabii hawakuwa wanaelewa kikamilifu ufunuo waliokuwa wamepewa. Maana yake ilitarajiwa kufunuliwa kutoka kizazi hadi kizazi.

Petro asema: Katika habari za wokovu huo "manabii walitafutatafuta na kuchunguza chunguza, ambao walitabiri habari za neema itakayowafikia ninyi. Wakatafuta ni wakati upi, na wakati wa namna gani ulioonywa na Roho Wakristo aliyekuwa ndani yao, ambaye alitangulia kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo. Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yetu walihudumu katika mambo hayo." (I Pet. 1:10-12). Ni somo muhimu jinsi gani kwa watu wa Mungu katika Zama za Ukristo! Watakatifu hao wa Mungu, "walitafuta na kuchunguza kwa makini" kuhusu ufunuo uliokuwa umetolewa kwa ajili ya vizazi vilivyokuwa havijazaliwa bado. Hili ni kemeo kubwa kiasi gani kwa hali ya kutokujali na kupenda dunia, kuridhika na kutamka kuwa unabii hauwezi kueleweka.

Siyo mara chache akili za watumishi imara wa Mungu hupofushwa na mapokeo na mafundisho ya uongo kiasi kwamba wanaweza kuelewa kwa sehemu tu mambo yanayofunuliwa katika

Neno lake. Hata Mwokozi alipokuwa nao, wanafunzi Wakristo walikuwa na dhana iliyopendelewa na wengi ya kuwa Masihi ni mfalme wa kidunia ambaye angeikweza Israeli na kuwa dola ya ulimwengu. Hawakuwa wanaelewa maneno yake yaliyokuwa yanatabiri juu ya mateso na kifo chake.

### "Wakati Umetimia" [220]

Kristo aliwatuma wakiwa na ujumbe: "Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili." Marko 1:15. Ujumbe huo ulikuwa unatokana na unabii wa Danieli 9. "Majuma sitini na tisa" yalikuwa yaishie kwa "Masihi mkuu," nao wanafunzi kwa shauku kuu walikuwa wanatazamia kuanzishwa kwa ufalme wa Masihi huko Yerusalemu, ili atawale ulimwengu mzima.

Walihubiri ujumbe uliokabidhiwa kwao, ingawa hawakuelewa maana yake. Wakati ujumbe wao ulikuwa unatokana na Danieli 9:25, hawakuona katika aya inayofuata kuwa Masihi angekatiliwa mbali. Mioyo yao ilikuwa ikifikiria utukufu wa enzi ya kidunia; jambo hilo lilipofusha ufahamu wao. Katika muda ule ule waliokuwa wanatarajia kumwona Bwana wao akikalia kiti cha enzi cha Daudi, walimwona akikamatwa, na kupigwa, na kudhihakiwa, na kuhukumiwa kifo cha msalaba. Mioyo ya wale wanafunzi iliumia sana kwa fadhaa na uchungu mkubwa!

Kristo alikuwa katika wakati ule uliokuwa umetabiriwa. Maandiko yalikuwa yametimia katika kila kipengele. Neno na Roho wa Mungu walikuwa wanashuhudia kazi ya kimbingu ya Mwana wake. Lakini akili za wanafunzi zilikuwa zimegubikwa na mashaka. Ikiwa kweli Yesu alikuwa Masihi, wangetumbukiaje kwenye huzuni na kuvunjika kwa matumaini yao? Hili ndilo swali lililokuwa linawasumbua nafsi wakati walipokuwa wamekata tamaa siku ile ya Sabato iliyokuwa katikati ya kifo na kufufiika kwake.

Hata hivyo walikuwa hawajaachwa. "Nikaapo gizani, BWANA atakuwa nuru yangu... Atanileta nje kwenye nuru, nami nitaiona haki yake." "Nuru huwazukia wenye adili gizani." "Nitafanya giza kuwa nuru mbele yao; na mahali palipopotoka kuwa pamenyoka. Haya nitayatenda, wala sitawaacha." Mika 7:8,9; Zaburi 112:4; Isaya 42:16.

Tangazo lililofanywa na wanafunzi lilikuwa sahihi, "Wakati [221]

umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia." Mwisho wa ule muda wa majuma sitini na tisa wa Danieli 9, ungeishia kwa Masihi, yaani "Mtiwa Mafuta"—Kristo alitiwa mafuta na Roho Mtakatifu baada ya kubatizwa na Yohana. "Ufalme wa Mungu" haukuwa wa ulimwengu huu, kama walivyokuwa wamefundishwa kuamini. Wala haukuwa ule ufalme ujao usiokuwa na mwisho, ambapo "wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii." (Danieli 7:27).

Usemi huu "ufalme wa Mungu" unamaanisha ufalme wa neema na ufalme wa utukufu. Mtume Paulo anasema: "Basi na tukikaribie *kiti cha neema* kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji." Waebrania 4:16. Kuwepo kwa kiti cha enzi kunamaanisha kuwepo kwa ufalme. Kristo anatumia usemi huu "ufalme wa mbinguni" kuelezea kazi ya neema katika mioyo ya watu. Hivyo kiti cha utukufu kinawakilisha ufalme wa utukufu. Mathayo 25:31, 32. Ufalme huu ni wa baadaye. Hautasimamishwa hadi hapo Kristo atakapokuja mara ya pili.

Wakati Kristo alipoutoa uhai wake na kupaza sauti, "Imekwisha," ahadi ya wokovu, iliyokuwa imetolewa kwa wale wanandoa wawili wenye dhambi katika bustani ya Edeni, ilithibitishwa. Ufalme wa neema, ambao ulikuwa upo kwa ahadi ya Mungu, sasa ulisimamishwa.

Kwa hiyo, kifo cha Kristo—tukio ambalo wanafunzi waliona kama uangamivu wa tumaini lao—ndicho kiichofanya tumaini hili liwe la uhakika milele. Japo liliwavunja moyo kabisa, lilikuwa uthibitisho kuwa kuamini kwao kulikuwa sahihi. Tukio ambalo liliwavunja moyo lilikuwa linafungua mlango wa matumaini kwa waaminifu wote wa Mungu katika vizazi vyote.

Dhahabu safi ya upendo wa wanafunzi kwa Yesu ilikuwa imechanganyika na hali duni za nia zenye ubinafsi. Dira yao ilikuwa ni kiti cha enzi, taji, na utukufu. Kiburi cha moyo, tamaa ya fahari za kidunia, iliwafanya wasizingatie maneno ya Mwokozi yaliyokuwa yanaonesha ufalme wake ulivyo, yakielekeza kwenye mauti yake. Makosa hayo yalisababisha majaribu ambayo yaliruhusiwa kwa ajili ya kuwarudi. Injili tukufu ya Bwana aliyefufuka ilikuwa ikabidhiwe kwa wanafunzi hao. Tukio lililoonekana kuwa la uchungu sana liliruhusiwa ili kuwaandaa kwa ajili ya kazi hiyo.

[222] Baada ya kufufuka kwake, Yesu aliwatokea wanafunzi wake katika njia ya kwenda Emau, "akawaeieza katika Maandiko yote

mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe." Lengo lake lilikuwa kukuza imani yao juu ya "lile neno la unabii lililo imara zaidi" (Luka 24:27; 2 Petro 1:19), si kwa ushuhuda tu, bali kwa unabii wa Agano la Kale. Na kama hatua ya kwanza kabisa ya kuwapatia maarifa hayo, Yesu aliwaelekeza wanafunzi wake katika vitabu vya "Musa na manabii wote" wa Maandiko ya Agano la Kale.

### Kukata Tamaa Hadi Uhakika

Wanafunzi walikuwa wamemwona "Yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati na manabii," (Yohana 1:45) kwa ukamilifu zaidi kuliko pale mwanzo. Mashaka, na kukata tamaa, vilitoa nafasi kwa matumaini, na imani safi. Walikuwa wamepita katika majaribu makali kuliko yote waliyokuwa wanaweza kuyapitia, na walikuwa wameona jinsi neno la Mungu lilivyotimizwa kwa ushindi. Baada ya hapo hakuna jambo ambalo lingeweza kutishia imani yao? Katika huzuni kuu waliyokuwa nayo, walipata "faraja iliyo imara," yaani, tumaini lilikuwa kama "nanga ya roho yenye salama, yenye nguvu." Waebrania 6:18,19.

Bwana asema: "Watu wangu hawatatahayari kamwe." "Kilio huja usiku, lakini asubuhi huwa furaha." Yoeli 2:26; Zaburi 30:5. Siku ya kufufuka kwake, wanafunzi hawa walikutana na Mwokozi, na mioyo yao iliwaka ndani yao kadiri walivyokuwa wakisikiliza maneno yake. Kabla ya kupaa kwake, Yesu aliwaagiza, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe," kisha akasisitiza, "Tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote." Marko 16:15; Mathayo 28:20. Katika siku ya Pentekoste Mfariji aliyekuwa ameahidiwa alishuka, na mioyo ya waumini iliburudika kwa kutambua uwepo wa Bwana wao aliyekuwa amepaa.

### Ujumbe wa Wanafunzi Ukilinganishwa na Ujumbe wa Mwaka 1844

Uzoefu walioupitia mitume kwenye ujio wa kwanza Wakristo ulipata kifani chake katika uzoefu wa wale walioutangaza ujio wake wa pili. Kama wanafunzi walivyohubiri wakisema, "Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia," ndivyo Miller na wenzi wake walivyotangaza kwamba kipindi cha mwisho cha unabii wa [223]

Biblia kilikuwa kinakaribia kwisha, kwamba hukumu ya Mungu karibu, na kwamba ufalme wa milele ulikuwa unakaribia kuanza. Hotuba za wanafunzi kuhusu wakati zilikuwa zimejengwa katika majuma sabini ya Danieli 9. Ujumbe uliokuwa unatolewa na Miller pamoja na wanzi wake ulikuwa unatangaza mwisho wa siku 2300 za Danieli 8:14, ambazo ndani yake kuna yale majuma sabini. Mahubiri ya wanafunzi na akina Miller yalikuwa yanategemea kutimia kwa sehemu tofauti za unabii mmoja.

Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa kwanza, William Miller na wenzake hawakuuelewa kikamilifu ujumbe waliokuwa wanautoa. Makosa yaliyokuwa kanisani kwa muda mrefu yalizuia fasiri sahihi ya jambo muhimu katika unabii huo. Kwa hiyo, japo walikuwa wanatangaza ujumbe ambao Mungu alikuwa ameukabidhi kwao, lakini kutokana na fasili mbaya, waliishia kuvunjika moyo.

Miller alichukua msimamo wa wengi kwamba dunia ndiyo "patakatifu" na akaamini kuwa "kutakaswa kwa patakatifu" kulikuwa kunawakilisha kutakaswa kwa dunia kwa moto wakati wa kuja kwa Bwana. Kwa hiyo alihitimisha kuwa mwisho wa zile siku 2300, ulikuwa unaonesha wakati wa ujio wa pili.

Kutakaswa kwa patakatifu ilikuwa huduma ya mwisho iliyokuwa inafanywa na kuhani mkuu katika mzunguko wa kila mwaka. Ilikuwa sehemu ya mwisho ya upatanisho—kuhamisha na kuondoa dhambi katika Israeli. Ilikuwa inawakilisha kazi ya mwisho ya Kuhani wetu Mkuu huko mbinguni ya kuhamisha na kuondoa dhambi za watu wake zinazoandikwa katika vitabu vya mbinguni. Huduma hii inahusisha uchunguzi, yaani kuhukumu, nayo nafainyika kabla ya kurudi kwa Kristo akiwa katika mawingu, kwani atakapokuja kila kesi itakuwa imekwisha kuamuliwa. Yesu anasema: "Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo." Ufunuo 22:12. Kazi hii ya hukumu ndiyo inayotangazwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14:7: "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja."

[224] Wale waliokuwa wanautangaza ujumbe huu walikuwa wanatoa ujumbe sahihi kwa wakati sahihi. Kama wanafunzi walivyokosea kuhusu ufalme uliokuwa usimamishwe mwishoni mwa yale "majuma sabini," Waadventista nao walikosea juu ya tukio ambalo lingetokea mwishoni mwa zile "siku 2300." Katika matukio yote, makosa

yaliyokuwa yamezoeleka na wengi yalipofusha akili zisiuone ukweli. Wote walitimiza mapenzi ya Mungu katika kuuhubiri ujumbe aliokuwa anataka utolewe, na wote walivunjika moyo kutokana na kuuelewa vibaya ujumbe wao.

Lakini Mungu alitimiza makusudi yake kwa kuruhusu onyo juu ya hukumu litolewe kama lilivyokuwa. Katika majaliwa yake, ujumbe huo ulikuwa wa kulipima na kulitakasa kanisa. Je, upendo wao ulikuwa umeelekezwa katika dunia hii au kwa Kristo na mbinguni? Je, walikuwa tayari kuachana na matamanio yao ya kidunia na kuukaribisha ujio wa Bwana wao?

Kuvunjika kwa matumaini yao kulikusudiwa pia kupima mioyo ya wale waliokuwa wanadai kuwa wamepokea onyo hilo. Je, wangeiacha imani yao upesi na kuacha kuliamini Neno la Mungu wanapokutana na dhihaka ya ulimwengu na jaribu la kuchelewa na kuvunjika moyo? Je, wangeuacha ukweli uliothibitishwa na ushuhuda wa wazi wa Neno lake kwa sababu hawakuelewa upesi jinsi Mungu alivyokuwa anafanya kazi?

Jaribio hili lingewaonesha hatari za kuchukua fasili za watu badala ya kuiacha Biblia ijifasili yenyewe. Wana wa imani wangepaswa kuisoma Biblia kwa makini, kuchunguza kwa undani misingi ya imani yao, na kukataa kila kitu ambacho hakikujengwa katika Maandiko, hata kama kinakubalika na wengi katika ulimwengu wa Kikristo.

Jambo ambalo lilikuwa giza wakati wa kupimwa baadaye lingewekwa wazi. Pamoja na majaribu waliyoyapata kutokana na kukosea kwao, wangejifunza kupitia uzoefu wenye baraka kwamba Bwana ni "mwingi wa fadhili na kweli, kwao walishikao agano lake na shuhuda zake." Zaburi 25:10.

Unabii mrefu kuliko wote katika Biblia upo katika Danieli 8, ukifuatiwa na maelelezo zaidi katika Danieli 9. Unabii huu unaonesha wakati wa kusulibiwa kwa Kristo na mwanzo wa hukumu ya upelelezi kule mbinguni. Angalia Ukurasa 203-206

[225] # Sura Ya 20 - Kuupenda Ujio Wakristo

[226]

Uamsho mkuu wa kidinr umetabiriwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14. Malaika anaonekana akiruka "katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa." Akisema kwa sauti kuu, "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:6, 7.

Malaika anawakilisha umakini wa kazi inayopaswa kufanywa na ujumbe huo na nguvu na utukufu ambao utaambatana nayo. Kuruka kwa malaika "katikati ya mbingu," ile "sauti kuu," na kueneza kwa "kila taifa na kabila na lugha na jamaa" ni ushahidi wa kuenea kwa harakati hizo ulimwenguni kote kwa kasi. Jambo hii litakapotokea, litakuwa linatangaza mwanzo wa hukumu.

Ujumbe huu ni sehemu ya Injili ambayo ingeweza kuhubiriwa katika siku za mwisho tu, kwani wakati huo saa ya hukumu itakuwa imekuja kweli. Danieli aliagizwa kuifunga na kuitia muhuri "hatawakati wa mwisho,"(Danieli 12:4.) sehemu ya unabii wake iliyokuwa inahusu siku za mwisho. Mpaka hapo ujumbe unaohusu hukumu usingeweza kuhubiriwa, kulingana na kutimia kwa unabii huu.

Paulo alilionya kanisa lisitarajie kurudi kwa Kristo katika siku zake. Hatuwezi kutarajia ujio wa Bwana wetu kabla ya "ukengeufu" na utawala wa muda mrefu wa yule "mtu wa kuasi." Tazama 2 Wathesalonike 2:3. Huyo "mtu wa kuasi"—ambaye pia ni "siri ya kuasi," "mwana wa uharibifu," na "yule asi,"—anawakilisha utawala wa Papa, ambao ungedumisha mamlaka yake kwa miaka 1260. Kipindi hicho kilikwisha mwaka 1798. Ujio Wakristo usingeweza kutokea kabla ya wakati huo. Tahadhari ya Paulo inajumuisha kipindi chote cha Ukristo hadi mwaka 1798. Baada ya ujumbe huo, ujio Wakristo ndipo utahubiriwa.

Ujumbe wa namna hiyo haujawahi kuhubiriwa huko nyuma. Kama tulivyoona, Paulo hakuuhubiri, alionesha kuwa kuja kwa

Kristo lilikuwa suala la baadaye sana. Wana matengenezo hawakuhubiri ujumbe huo. Martin Luther aliiweka hukumu kama miaka 300 hivi kutoka wakati wake. Lakini tangu mwaka 1798 kitabu cha Danieli kimefunuliwa, na wengi wamehubiri ujumbe wa hukumu iliyokaribia. [227]

## Katika Nchi Mbalimbali kwa Wakati Mmoja

Kama yalivyokuwa matengenezo ya kame ya kumi na sita, harakati za Waadventista zilitokea katika nchi mbalimbali kwa wakati mmoja. Watu wenye imani walisoma unabii na wakaona ushahidi unaoonesha kuwa mwisho ulikuwa karibu. Kwa kusoma Biblia tu, makundi mbalimbali ya Wakristo, waliamini kuwa ujio wa Mwokozi ulikuwa umekaribia.

Miaka mitatu baada ya Miller kufanya ufafanuzi wake wa unabii, Dr Joseph Wolff, "mmisionari kwa ulimwengu," alianza kutangaza ujio wa Bwana uliokuwa karibu. Akiwa amezaliwa Ujerumani na wazazi wa Kiebrania, tangu alipokuwa kijana, alikuwa ameuamini ukweli wa dini ya Kikristo. Alikuwa msikilizaji mzuri wa maongezi katika nyumba ya baba yake wakati Waebrania waaminifu walipokusanyika kuelezea matumaini ya watu wao, utukufu wa Masihi aliyekuwa anakuja, na kurejeshwa kwa taifa la Israeli. Wakati mmoja, aliposikia Yesu wa Nazareti akitajwa, yule kijana alitakakujua, Yeye alikuwa nani. Jibu lilikuwa, "Myahudi mwenye vipaji vingi, ila kwa kuwa alijifanya Masihi, mahakama ya Kiyahudi ilimhukumu kifo."

Akazidi kuuliza swali jingine, "Ni kwa nini Yerusalemu imeharibiwa, na kwa nini tuko uhamishoni?" "Ahaa!" baba yake alijibu, "Kwa sababu Wayahudi waliwaua manabii." Wazo likamjia pale pale: "huenda Yesu alikuwa nabii pia, na Wayahudi walimwua wakati hakuwa na hatia." Ingawa alikuwa anakatazwa kuingia katika Kanisa la Wakristo, kijana huyu wa Kiyahudi alikuwa anakaa nje kusikiliza mahubiri. Alipokuwa na miaka saba tu, alikuwa anajivuna mbele ya jirani yao Mkristo juu ya ushindi ujao wa Israeli siku Masihi atakapokuja. Yule mzee alijibu kwa upole: "Kijana wangu mpendwa, ngoja nikwambie Masihi halisi alikuwa nani: Alikuwa Yesu wa Nazareti. ... ambaye babu zenu walimsulibisha. ... Nenda

nyumbani ukasome Isaya 53, nawe utaamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu." [209]

[228] Alikwenda nyumbani na kusoma Maandiko. Yalikuwa yametimia kikamilifu kabisa ndani ya Yesu wa Nazareti. Je, maneno ya yule Mkristo yalikuwa sahihi? Yule kijana alimwomba baba yake ufafanuzi wa ule unabii lakini alikutana na kimya kikali kiasi kwamba kijana hakuthubutu kuzungumzia tena jambo hilo.

Akiwa na miaka kumi na moja tu, alikwenda ulimwenguni kutafuta elimu, kuchagua dini yake, na kazi yake katika maisha. Akiwa peke yake na bila pesa, ilimpasa kujitegemea. Alisoma kwa bidii, akijikimu kwa kufundisha Kiebrania. Aliongozwa kupokea imani ya Kanisa la Roma, naye akaenda kusoma katika Chuo cha Propaganda cha Roma. Hapa alikemea waziwazi maovu ya Kanisa na akataka kuwe na matengenezo. Baada ya Muda alifukuzwa. Ilikuwa wazi kuwa asingeweza kujisalimisha chini ya utumwa wa Kanisa la Roma. Alitangazwa kuwa jeuri na akaachwa aende ko kote alikokuwa anataka. Alikwenda Uingereza na kujiunga na Kanisa la Uingereza. Baada ya miaka miwili ya masomo, mwaka 1821 alianza kufuatilia lengo lake. Wolff aligundua kuwa unabii unadhihirisha ujio Wakristo kwa uweza na utukufu. Wakati akitaka kuwaelekeza watu wake kwa Yesu wa Nazareti kama Masihi aliyekuwa ameahidiwa, kuwaonesha ujio wake wa kwanza kama dhabihu ya dhambi, alikuwa akiwafundisha pia kuhusu ujio wake wa pili.

Wolff aliamini kuwa ujio wa Bwana ulikuwa karibu. Fasili yake ya vipindi vya unabii iliuweka katika miaka ya karibu na kipindi kilichokuwa kimetajwa na Miller. "Je, Bwana wetu hakutupatia ishara za nyakati, ili tuweze kujua angalau kukaribia kwa ujio wake, kama mtu anavyojua kuwa majira ya joto yamekaribia kwa mtini kuchipua? Mambo ya kutosha yatajulikana kwa njia ya ishara za nyakati, kutufanya tujiandae kwa ajili ya ujio wake kama Nuhu alivyoandaa safina." [210]

[209] Travels and Adventures of the Rev. Joseph Wolff, vol. 1, pp. 6, 7.
[210] Joseph Wolff, Researches and Missionary Labors, pp. 404, 405.

## Tofauti na Fasili za Wengi

Wolff aliandika hivi juu ya mfumo wa kufasili Maandiko uliokuwa unatumiwa na wengi, "Sehemu kubwa ya Kanisa la Kikristo imechepuka kutoka katika maana sahili ya Biblia, na ...kudhani wanaposoma *Wayahudi* ni lazima waelewe *Watu wa Mataifa*; na wanaposoma

*Yerusalemu*, ni lazima waelewe kanisa; na kama ikisemwa [229]
dunia, inamaanisha anga; na kuja kwa Bwana, ni lazima waelewe *maendeleo ya vyama vya kimisionari*; na kwenda katika mlima wa nyumba ya Bwana, inamaanisha *mkutano wa Wamethodisti mashuhuri*. " [211]

Tangu mwaka 1821 hadi 1845, Wolff alisafiri kule Misri, Ethiopia, Palestina, Shamu, Uajemi, Bokhara, India, na Marekani.

## Uwezo Ndani ya Kitabu

Dk. Wolff alitembelea nchi nyingi za watu wakatili kabisa bila ulinzi wo wote; akistahimili matatizo na kuzungukwa na hatari nyingi. Alikosa chakula, akauzwa kama mtumwa, akahukumiwa kifo mara tatu, akazingirwa na wanyang'anyi, na wakati mwingine alinusurika kufa kwa sababu ya kiu. Wakati fulani alivuliwa na kuachwa atembee kwa miguu mamia ya kilometa katika milima, wakati theluji ikipiga uso wake na miguu yake iliyokuwa peku ikifa ganzi kwa sababu ya ardhi iliyokuwa imeganda.

Alipoonywa asisafiri bila ulinzi katika ya makabila katili, alisema kuwa amepewa silaha—"maombi, ari kwa ajili ya Kristo, na imani kubwa kuhusu aliye msaada wake." "Pia nimepewa upendo kwa ajili ya Mungu na jirani yangu katika moyo wangu, na Biblia iko mkononi mwangu." "Nilikuwa naona kuwa nguvu yangu ilikuwa katika Kitabu, na kwamba uwezo wake ungenihifadhi." [212]

Alisonga mbele hadi ujumbe ulipoenea katika sehemu kubwa ya ulimwengu uliokuwa na wakazi. Alieneza neno la Mungu katika Iugha mbali mbali kwa Wayahudi, Waturuki, Waparsi, Wahindu na mataifa mengine pamoja na jamii zingine, na kila mahali alitangaza kukaribia kwa ujio wa Masihi.

[211] Joumal of the Rcv. Joseph Wolff, p. 96.
[212] W. H. D. Adams, In Perils Oft, pp. 192, 201.

Kule Bokhara alikuta fundisho la kuja kwa Bwana hivi karibuni likishikiliwa na watu waliotawanyika. Anasema, Waarabu wa Yemeni, "wana kitabu kiitwacho *Seera* kinachozungumzia kuja
[230] kwa Kristo na utawala wake wa utukufu; na wanatarajia matukio makubwa katika mwaka 1840." "Niliwakuta wana wa Israeli, wa kabila la Dani, ... pamoja na Warekabi... wanaotarajia kuja upesi kwa Masihi akiwa katika mawingu ya mbinguni." [213]

Imani kama hiyo ilikutwa na mmisionari mwingine huko Tatar. Kuhani wa Tatar aliuliza Yesu atarudi lini. Mmisionari huyo aliposema hajui lo lote, yule kuhani alishangazwa na ujinga huo kwa mwalimu huyu wa Biblia, naye akamwelezea imani aliyokuwa nayo, iliyokuwa inatokana na unabii, kwamba Kristo angekuja manamo mwaka 1844.

## Ujumbe wa Ujio Kule Uingereza

Ujumbe wa ujio ulishaanza kuhubiriwa kule Uingereza tangu mwaka 1826. Kwa sehemu kubwa muda halisi wa ujio huo ulikuwa hautajwi, ila ukweli wa kuja upesi kwa Kristo katika uweza na utukufu ulitangazwa kila mahali. Mwandishi mmoja wa Kiingereza alieleza kuwa wachungaji wapatao 700 wa Kanisa la Uingereza walikuwa wanaihubiri "Injili hii ya ufalme."

Ujumbe uliokuwa unaelekeza mwaka 1844 kama wakati wa kuja kwa Bwana ulihubiriwa pia huko Uingereza, Scotland na Wales. Machapisho kutoka Marekani yaliyokuwa yanahusu kuja kwa Yesu yalisambazwa kila mahali. Mwaka 1842 Robert Winter, Mwingereza aliyekuwa amepata imani ya ujio wa Yesu kule Marekani, alirejea nchini kwake kutangaza kurudi kwa Bwana. Wengi walijiunga naye katika kazi hiyo katika sehemu mbalimbali za Uingereza.

Huko Amerika ya Kusini, Lacunza ambaye ni Mhispania na Mjesuti, aliupokea ukweli wa ujio wa Yesu uliokuwa umekaribia. Ili aepuke karipio kutoka Kanisa la Roma, alichapisha kitabu chake kwa jina la bandia la Rabbi Bin Ezra, akijifanya Myahudi aliyeongoka. Mwaka 1825 kitabu chake kilitafsiriwa katika lugha ya Kiingereza. Kilisaidia kuimarisha mwamko ambao tayari ulishajionesha huko Uingereza.

[213] Joumal of the Rev. Joseph Wolff, pp. 377, 389.

## Ufunuo Wadhihirika kwa Bengel [231]

Katika Ujerumani fundisho hili lilikuwa limefundishwa na Bengel, mchungaji wa Kilutheri na mwanazuoni wa Biblia. Wakati akiandaa mahubiri yake kutoka Ufunuo 21, nuru ya ujio Wakristo ilikuja katika akili zake. Unabii wa Ufunuo ulidhihirika katika akili zake. Kwa kuwa alijawa na fikra juu ya umuhimu na utukufu wa matukio yaliyoelezewa na nabii aliyeandika kitabu cha Ufunuo, alilazimika kuliacha jambo hilo kwa muda. Alipokuwa madhabahuni lilimjia tena kwa udhahiri. Tangu wakati huo aliazimu kusoma unabii na muda si mrefu aliamini kuwa ujio wa Yesu ulikuwa umekaribia. Tarehe aliyoiweka ya ujio wa pili ilikuwa ndani ya miaka michache kutoka ile iliyowekwa na Miller.

Maandishi ya Bengel yalienea katika jimbo lake la Wiirtemberg na sehemu nyingine za Ujerumani. Ujumbe wa kurudi kwa Kristo ulisikika Ujerumani wakati ule ule ulipokuwa unavuta usikivu wa wengi katika nchi nyingine.

Kule Geneva, Gaussen alihubiri ujio Wakristo. Alipojiunga na kazi ya uchungaji alikuwa na mwelekeo wa mashaka. Katika ujana wake alikuwa anatamani kujifunza unabii. Baada ya kusoma kitabu cha Rollin kiitwacho "Ancient History," akili yake ilivutiwa na sura ya pili ya kitabu cha Danieli. Alishangazwa sana na usahihi ambao unabii huo ulikuwa umetimia. Hapa kulikuwa na ushahidi wa uvuvio wa Maandiko. Hakuridhika na maelezo ya udhuru na katika kusoma Biblia alielekezwa kwenye imani chanya

Aliamini kuwa ujio Wakristo ulikuwa karibu. Kwa kuwa alivutiwa na umuhimu wa ukweli, alitamani kuuflkisha kwa watu. Lakini imani ya wengi kwamba unabii wa Danieli hauwezi kueleweka ilikuwa kikwazo kikubwa. Hatimaye aliazimu—kama alivyofanya Farel kabla yake katika kueneza Injili kule Geneva—kuanza na watoto, ambao alitarajia wangewavuta wazazi. Alisema, "Nikakusanya hadhira ya watoto... kundi linapokuwa kubwa, inapoonekana kwamba wanasikiliza, wanapendezwa, wanavutiwa, kwamba wanaelewa na kuielezea mada husika, bila shaka nitakuwa na kundi lingine muda si mrefu, na kwa upande wao, watu wazima [232] wataona kuwa kuna haja ya kukaa na kujifunza. Jambo hilo likifanyika lengo litakuwa limetimia. [214]

[214] L. Gaussen, Daniel the Prophet, vol. 2, dibaji.

Alipokuwa anahutubia watoto, watu wazima walikuja kusikiliza. Njia zote katika kanisa lake zilijaa wasikilizaji, watu wenye vyeo na wasomi, wageni na watu wa mataifa mengine waliokuwa wanatembelea Geneva. Kwa njia hiyo ujumbe ulikwenda sehemu zingine.

Kwa kuwa alitiwa moyo, Gaussen alichapisha masomo yake akitumaini kuinua usomaji wa vitabu vya unabii. Baadaye alikuwa mwalimu katika chuo cha teolojia, na Jumapili aliendelea na kazi yake ya ukatekista, akiwahutubia watoto na kuwafundisha Maandiko. Kutoka katika kiti chake cha uprofesa, hadi katika kiwanda cha kuchapa vitabu na kufundisha watoto, kwa miaka mingi alichangia sana katika kuwafanya watu wengi wasome unabii uliokuwa unaonesha kuwa ujio wa Bwana ulikuwa umekaribia.

### Wahubiri Watoto wa Scandinavia

Kule Scandinavia ujumbe wa kurudi kwa Kristo ulihubiriwa pia. Wengi walichochewa kuungama na kuziacha dhambi zao na kutafuta msamaha katika jina la Kristo. Lakini wachungaji wa kanisa la taifa walizipinga harakati hizo, na baadhi ya watu waliokuwa wanahubiri ujumbe huo walitupwa gerezani. Katika sehemu nyingi ambapo wahubiri wa ujio wa Bwana ulioukuwa umekaribia walinyamazishwa, Mungu alipendezwa kupeleka ujumbe huo kwa kutumia watoto. Kwa kuwa walikuwa chini ya umri wa kushtakiwa, serikali haikuweza kuwazuia na waliruhusiwa kunena bila kusumbuliwa.

Katika makazi duni ya wafanyakazi, watu walikusanyika kusikiliza maonyo. Baadhi ya hao watoto waliohubiri walikuwa si zaidi ya miaka sita au minane; na wakati maisha yao yalishuhudia kuwa walikuwa wanampenda Mwokozi wao, na kwa kawaida walionesha akili nauwezo usio wa kawaida kwa watoto wa umri huo. Hata hivyo, walipokuwa wamesimama mbele ya watu, waliwezeshwa na uwezo uliokuwa zaidi ya vipaji vyao vya asili. Sauti zao na jinsi ya uzungumzaji vilibadilika, na walitoa onyo juu ya hukumu kwa uwezo mkubwa, "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja."

[233] Watu walipokea ujumbe huo kwa kutetemeka. Roho wa Mungu aliongea na mioyo ya watu. Wengi waliongozwa kuyatafuta Maandiko, wapenda anasa na waasheratiwalibadili mienendo yao,

na kazi kubwa ya matengenezo ilifanyika kiasi kwamba hatamakasisi wa kanisa la nchi hiyo walilazimika kukiri kwamba mkono wa Mungu ulikuwa unaongoza harakati hizo.

Ulikuwa ni mpango wa Mungu kwamba habari njema za kurudi kwa Kristo zihubiriwe kule Scandinavia, hivyo akaweka Roho wake ndani ya watoto ili kazi hiyo ipate kutimizwa. Wakati Yesu alipokuwa anaingia Yerusalemu, watu waliokuwa wakimshangilia, walilazimika kutulia walipolikaribia lango la mji, kwa sababu waliwaogopa makuhani na wakuu. Lakini watoto waliokuwa kwenye nyua za hekalu waliendeleza nyimbo hizo wakisema, "Hosana, Mwana wa Daudi!" Mathayo 21:8-16. Kama Mungu alivyofanya makuu kwa kutumia watoto wakati wa ujio wa kwanza Wakristo, vivyo hivyo alifanya makuu kwa kutumia watoto kwa kuwakabidhi ujumbe wa ujio Wakristo.

## Ujumbe Waenea

Marekani ilikuwa kitovu cha harakati za ujio. Machapisho ya Miller na wenzi wake yalisambazwa hadi nchi za mbali, kila mahali palipokuwa na wamisionari ulimwenguni. Ujumbe wa Injili ya milele ulienea hadi mbali na kila mahali ukisema: "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja."

Unabii uliokuwa unaonekana kuwa unatabiri kurudi kwa Kristo katika majira ya kuchipua ya mwaka 1844 ulikubalika na watu wengi. Wengi walisadiki kuwa hoja za vipindi vya unabii zilikuwa sahihi, nao waliacha kiburi cha kung'ang'ania maoni yao, walipokea ukweli kwa furaha. Baadhi ya wachungaji waliacha mishahara yao namakanisa yao wakaungana kutangaza ujio Wakristo. Hata hivyo ni wachungaji wachache tu walioupokea ujumbe huu; hivyo kwa sehemu kubwa ulikabidhiwa kwa walei wanyenyekevu. Wakulima waliyaacha mashamba yao; mafundi waliziacha karakana zao;wafanyabiashara waliachana na bidhaa zao; watu wenye taaluma waliachana na nyadhifa zao. Walikabiliana kwa hiari na hali ngumu, kukosa mahitaji na mateso ili wawaite watu kuja kwenye toba na wokovu. Ujumbe wa ujio ulipokelewa na maelfu ya watu.

[234] **Maandiko Sahili Valeta Imani**

Kama vile alivyofanya Yohana Mbatizaji, wahubiri hao waliweka shoka katika shina la mti na kuwahimiza wote "kuzaa matunda yapasayo toba." Kinyume na hotuba za amani na usalama zilizokuwa zinasikika katika madhabahu maarufu, ushuhuda sahili wa Maandiko ulileta imani ambayo haikuwa rahisi kupingika. Wengi walimtafuta Bwana kwa toba. Mapenzi yaliyokuwa yamezama katika vitu vya duniani sasa yalielekezwa mbinguni. Wakiwa na mioyo iliyolainika na kunyenyekea waliungana kupaza sauti; "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja."

Wenye dhambi waliuliza huku wakilia: "Yanipasa nifanye nini ili nipate kuokoka?" Wale ambao hawakuwa waaminifu walikuwa wanahaha kutaka kufidia. Wote waliokuwa na amani katika Kristo walitamani kuona wengine wakifaidi baraka hizo. Mioyo ya wazazi iliwaelekea watoto wao, na mioyo ya watoto iliewaelekea wazazi wao. Malaki 4:5,6. Vikwazo vya kiburi na kusitasita viliondoka. Maungamo ya dhati yalifanyika. Kila mahali kulikuwa na mioyo inayomsihi Mungu. Wengi walikuwa wanakesha katika maombi wakitaka uhakika kama dhambi zao zimesamehewa, au kuombea ndugu na majirani zao waongoke.

Watu wa madaraja yote, matajiri kwa maskini, wakuu na wanyonge, walikuwa na shauku ya kulisikia fundisho la ujio Wakristo. Roho wa Mungu aliupatia nguvu ukweli wake. Uwepo wa malaika watakatifu ulihisiwa katika mikusanyiko hiyo ya watu, na walioamini walikuwa wanaongezeka kila siku. Makundi makubwa ya watu yalisikiliza maneno hayo muhimu kwa utulivu. Mbingu na dunia zilikuwa kana kwamba zimekaribiana. Watu walikwenda nyumbani kwao wakiwa na vinywa vilivyojaa sifa, na sauti ya furaha ilijaa katika hewa tulivu ya usiku. Hakuna hata mmoja aliyehudhuria mikutano hiyo ambaye angesahau matukio hayo makuu yaliyokuwa yanavutia.

[235] **Ujumbe Wapingwa**

Kutangazwa kwa tarehe maalum ya kurudi kwa Kristo kulisababisha upinzani mkubwa kutoka kwa watu wengi wa matabaka yote; tangu mchungaji aliyekuwa madhabahuni hadi mwenye

dhambi aliyekubuhu. Wengi walisema kuwa walikuwa hawapingi fundishao la ujio Wakristo; walichokuwa wanapinga ni ile tarehe maalumu. Lakini jicho la Mungu lionalo kila mahali lilikuwa linasoma mioyo yao. Walikuwa hawataki kusikia kuWakristo alikuwa anakuja kuuhukumu ulimwengu kwa haki. Matendo yao yasingestahimili uchunguzi wa Mungu asomaye mioyo, na hivyo walikuwa wanaogopa kukutana na Mungu wao. Kama ilivyokuwa kwa Wayahudi wakati wa ujio wa kwanza Wakristo, hawakuwa tayari kumkaribisha Yesu. Pamoja na kukataa kusikiliza hoja za wazi kutoka katika Biblia, walikuwa wanawadhihaki wale waliokuwa wanamtafuta Bwana. Shetani alimdhihaki Yesu kwamba watu wake walikuwa wanampenda kidogo sana kiasi kwamba walikuwa hawatamani kuonekana kwake.

"Hakuna aijuaye siku wala saa" ndiyo hoja iliyokuwa inatolewa na wapinzani wa imani ya ujio.Maandiko yanasema, "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake." Mathayo 24:36Maelezo ya wazi ya aya hii yalikuwa yanatolewa na wale waliokuwa wanamtafuta Bwana, na matumizi mabaya ya aya hiyo kwa upande wa wapinzani wao yalidhihirishwa.

Kauli moja ya Mwokozi haiwezi kutumika kuhafifisha nyingine. Japo hakuna mtu aijuaye siku wala saa ya kuja kwake, inatupasa kujua inapokaribia. Kukataa au kupuuzia kujua ujio wake unapokaribia ni hatari kwetu kama ilivyokuwa kutokujua kuwa Gharika ilikuwa imekaribia katika siku za Nuhu. Kristo alisema, "Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi,wala hutaijua saa nitakayokuja kwako." Ufunuo. 3:3.

Paulo anawazungumzia wale waliolisikia onyo la Mwokozi: "Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana." 1 Thesalonike 5:2-5.

Lakini wale waliokuwa wanatafuta udhuru wa kuukataa ukweli, [236]
waliziba masikio yao wasisikie maelezo haya, na maneno "Hakuna mtu aijuaye siku wala saa" yakaendelea kutamkwa na wenye kudhihaki na hata na wale waliokuwa wakidai kuwa watumishi Wakristo. Watu walipokuwa wanauliza njia ya wokovu, walimu wa dini walisimama katikati yao na ukweli kwa kulifasili vibaya Neno la Mungu.

Kwa kawaida wale waliokuwa watauwa zaidi katika makanisa walikuwa wa kwanza kuupokea ujumbe. Kila mahali ambapo watu walikuwa hawadhibitiwi na wachungaji, po pote walipokuwa wanaweza kulichunguza Neno la Mungu wao wenyewe, fundisho la ujio lilikuwa linahitaji kulinganishwa na Maandiko tu, ili kuthibitisha mamlaka yake kutoka kwa Mungu.

Wengi walipotezwa na waume zao, wake zao, wazazi wao, au watoto wao, na wakafanywa waamini kuwa ni dhambi hata kusikiliza "uzushi" kama ule uliokuwa unafundishwa na Waadventista. Malaika waliagizwa kuwalinda sana watu hawa, kwani nuru nyingine ilikuwa haijawaangazia kutoka kiti cha enzi cha Mungu.

Wale waliokuwa wameupokea ujumbe waliungojea ujio wa Mwokozi wao. Muda waliokuwa wanatarajia kukutana naye ulikuwa karibu. Waliikaribia saa hiyo kwa umakini mtulivu. Hakuna aliyepitia hali hiyo anayeweza kuusahau muda huo mzuri wa kungojea. Kwa majuma kadhaa kabla ya siku hiyo, shughuli za kidunia ziliwekwa kando. Waumini waaminifu waliipeleleza mioyo yao kana kwamba katika saa chache wasingeyaona tena mambo ya ulimwengu. Hawakuwa wanaandaa "mavazi ya kupaa nayo," bali wote waliona hitaji la ushahidi wa ndani kwamba walikuwa tayari kukutana na Mwokozi. Mavazi meupe kwao ulikuwa usafi wa moyo—tabia zilizosafishwa kwa damu ya Kristo iletayo upatanisho. Kujipeleleza ndani ya moyo kunapaswa kuwepo miongoni mwa watu wa Mungu hata sasa.

Mungu alikuwa amekusudia kuwapima watu wake. Mkono wake ulificha kosa lililokuwa katika upigaji hesabu wa vipindi vya unabii. Muda waliokuwa wanautarajia [yaani, kwamba Kristo angekuja katika majira ya kuchipua ya mwaka 1844] ulipita, naye Kristo hakutokea. Wale waliokuwa wanamngojea Bwana wao walivunjika moyo kwa uchungu mkubwa. Hata hivyo Mungu alikuwa
[237] anaijaribu mioyo ya wale waliokuwa wanadai kuwa walikuwa wanangojea kuonekana kwake. Wengi walikuwa wamechochewa na hofu. Watu walisema kuwa hwakuwahi kuamini kuWakristo angekuja. Walikuwa miongoni mwa watu wa kwanza kudhihaki huzuni ya wale waumini wa kweli. Lakini Yesu pamoja na jeshi iote la mbinguni alikuwa anawaangalia kwa upendo na huruma wale waaminifu waliokuwa wamevunjika moyo. Kama pazia linalotenganisha ulimwengu usioonekana na ule unaoonekana lingeondolewa,

malaika wangeonekana wakiwakaribia watu hawa wenye saburi na kuwakinga na kejeli za Shetani.

[238]

# Sura Ya 21 - Kuvuna Upepo

William Miller na wenzi wake walikuwa wanataka kuwaonesha wale waliokuwa wanadai kuwa watu wa dini, tumaini la kweli la kanisa na hitaji lao la kuwa na UKristo wa kina zaidi. "Hawakutaka kuwaingiza watu katika kundi lililojitenga na makanisa yao. Walikuwa wanafanya kazi katika makundi na madhehebu yote." Miller alisema, "Nilikuwa nimekusudia kuwanufaisha wote. Nikidhani kwamba Wakristo wote wangefurahia tumaini la kuja kwa Yesu, na wale ambao hawakuyaona mambo kama nilivyokuwa nayaona wasingepunguza upendo wao kwa wale waliolipokea fundisho hili, sikuwa nafikiria kwamba kungekuwa na haja ya kuwa na mikutano ya pembeni.... Sehemu kubwa ya wale walioamini kutokana na mahubiri yangu walijiunga na makanisa yaliyokuwapo wakati huo." [215]

Lakini kwa kuwa viongozi wa dini walikuwa wameamua kulipinga fundisho la Ujio, waliwakatalia washiriki wao kuhudhuria mahubiri ya Ujio wa pili au hata kuzungumzia tumaini lao katika kanisa. Wale waumini walikuwa wanayapenda makanisa yao. Lakini walipoona kuwa haki yao ya kuchunguza unabii inazuiliwa, waliona kwamba utii kwa Mungu ulikuwa unawakataza kusalimu amri. Hivyo waliona uhalali wa kujitenga. Katika majira ya joto ya mwaka 1844, takriban watu 1000 walijitenga na na makanisa yao.

Katika makanisa mengi, kwa miaka mingi kulikuwa na ongezeko la kukubaliana taratibu na desturi za ulimwengu na kuzorota kwa maisha ya kiroho. Lakini mwaka huo, kulikuwa na ushahidi wa kuzorota katika makanisa karibu yote nchini. Ukweli huo ulielezwa katika vyombo vya habari na katika madhabahu.

Bw. Barnes, aliyekuwa mwandishi wa kitabu cha ufafanuzi na mchungaji wa moja ya makanisa makubwa ya Filadelphia, "alisema kwamba ... sasa hivi hakuna uamsho, hakuna wanaoongoka, hakuna ukuaji katika neema miongoni mwa wanaodai kuwa waumini, na wengi hawaji kujifunza kwake ili wazungumzie wokovu wa roho

[215] Bliss, p. 328.

zao. ... Kuna ongezeko la kupenda ulimwengu. Hivyo ndivyo ilivyo kwa madhehebu zote. [216]

Mwezi wa Februari wa mwaka huo, Profesa Finney wa Chuo Kikuu cha Oberlin alisema: "Kwa ujumla, makanisa ya Kiprotestanti nchini mwetu, ama yamekuwa baridi au yamekuwa na chuki dhidi ya kila aina ya matengenezo ya uadilifu katika kizazi hiki. Ubaridi wa kiroho umeenea kote na umezama kwa kina mno; vyombo vya habari vya nchi yetu vinashuhudia.... Kwa sehemu kubwa washiriki wanazidi kuwa wapenzi wa mitindo, wanaungana na watu wasiomcha Mungu katika tafrija za anasa, katika dansi, katika karamu, na kadhalika.... Makanisa kwa ujumla yanazidi kuzorota. Yametanga mbali sana na Bwana naye amejitenga nao. [239]

## Wanadamu Waikataa Nuru

Giza la kiroho halisababishwi na Mungu kuondoa neema yake, bali linasababishwa na wanadamu kuikataa nuru. Kutokana na kupenda ulimwengu na kumsahau Mungu, Wayahudi hawakujua cho chote juu ya Ujio wa Masihi. Kwa sababu ya kutokuamini, walimkataa Mkombozi. Mungu hakuliondoa taifa la Wayahudi katika baraka za wokovu. Wale walioukataa ukweli walikuwa "watiao giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza." Isaya 5:20.

Baada ya kuikataa Injili Wayahudi waliendelea kudumisha taratibu zao za zamani za kidini, huku wakikiri kuwa uwepo wa Mungu haukuwa pamoja nao. Unabii wa Danieli ulitabiri kwa usahihi wakati wa kuja kwa Masihi na ulitabiri kifo chake moja kwa moja. Hivyo walipinga usomaji wa kitabu hicho, na hatimaye maarabi walitoa laanakwa wote ambao wangejaribu kufanya mahesabu ya wakati. Kwa upofu na roho isiyotaka toba watu wa Israeli waliendelea kutokujali fursa za neema ya wokovu kwa kamenyingi, bila kujali baraka za Injili, hali ambayo ni onyo la kutisha juu ya hatari ya kukataa nuru itokayo mbinguni.

Mtu anayetweza ushawishi juu ya wajibu kwa kuwa unaingiliana na matamanio yake atapoteza uwezo wake wa kutofautisha ukweli na uongo. Roho hutengwa na Mungu.Pale ukweli wa Mungu unapokataliwa kwa fedheha, kanisa litakuwa gizani, imani na upendo [240]

[216] Congregational Joumal, May 23, 1844.

hupoa, na mivutano hutokea. Washiriki wa kanisa huvutiwa na mambo ya dunia, na wenye dhambi huthibitika katika ukaidi wao.

### Ujumbe wa Malaika wa Kwanza

Ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14 ulikuwa umekusudiwa kuwatenga watu wanaokiri kuwa wa Mungu na mivuto mibaya. Katika ujumbe huu, Mungu alituma onyo kwa kanisa, ambalo, kama lingepokelewa, lingerekebisha uovu uliokuwa unawatenga na Mungu. Kama wangeupokea ujumbe huo, wakinyenyekeza mioyo yao, na kutaka kujiandaa kusimama mbele zake, Roho wa Mungu angedhihirishwa. Kwa mara nyingine kanisa lingekuwa na umojaimani, na upendo uliokuwepo zama za mitume, wakati waumini "walikuwa na moyo mmoja na roho moja," na ambapo Bwana alilizidisha "kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." Matendo 4:32; 2:47.

Kama watu wa Mungu wangeipokea nuru kutoka katika Neno lake, wangekuwa na umoja ambao mtume Paulo anauelezea, yaani "umoja wa Roho katika kifungo cha amani." Anasema, "mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la mwito wenu; Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja." Waefeso 4:3-5.

Wale walioupokea ujumbe wa kurudi kwa Kristo walitokea kwenye madhehebu mbalimbali, nao tufauti zao za kimadhehebu zilitupiliwa mbali. Itikadi zilizokuwa zinapingana zilivunjwa vunjwa na kuwa kama atomu. Dhana potovu juu ya Ujio wa pili zilisahihishwa. Mabishano ya kiitikadi za kila dini iliyeyushiwa mbali. Mitazamo potovu kuhusu kurudi kwa Kristo ilisahihishwa. Makosa yalirekebishwa na mioyo iliungana katika ushirika mwanana. Upendo ulishika hatamu. Fundisho hili lingefanya hivyo kwa wote kama wote wangelipokea.

Wachungaji, ambao walipasa kuwa wa kwanza kuzitambua dalili za kuja kwa Yesu kama walinzi, walikuwa wameshindwa kujifunza ukweli kutoka kwa manabii au katika ishara za nyakati. Upendo kwa Mungu na imani kwa Neno lake vilikuwa vimepoa, na fundisho la
[241] Ujio Wakristo lilichochea tu kutokuamini kwao. Kama ilivyokuwa kwa ushuhuda wa zamani, Nenola Mungu lilikutana na swali: "Ni nani katika wakuu amwaminiye, au katika Mafarisayo?" Yohana

7:48. Wengi walikatisha tamaa usomaji wa unabii, wakifundisha kwamba vitabu vya unabii vilikuwa vimefungwa, tena havikupasa kueleweka. Walio wengi, wakiwaamini wachungaji wao, walikataa kuusikiliza ujumbe huo; na wengine, japo walikuw wameshawishiwa na ukweli, walikataa kuukiri wazi wasije "wakaondolewa kutoka katika sinagogi." Yohana 9:22. Ujumbe ambao Mungu aliutuma ili kulipima Kanisa ulidhihirisha jinsi idadi ya waliokuwa wameweka mapenzi yao kwa ulimwengu badala ya Mungu, ilivyokuwa kubwa.

Kulikataa onyo la malaika wa kwanza ilikuwa sababu ya hali mbaya ya kupenda dunia, kuasi, na kufa kiroho iliyokuwa katika makanisa mwaka 1844.

### Ujumbe wa Malaika wa Pili

Katika Ufunuo 14 ujumbe wa malaika wa kwanza unafuatiwa na malaika wa pili, anayesema "Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanyweshamataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Ufunuo 14:8. "Babeli" inamaanisha machafuko. Katika Maandiko inawakilisha mifumo mbalimbali ya diniza uongo au zilizoasi. Katika Ufunuo 17, Babeli inaelezewa kama mwanamke— kielelezo kitumikacho katika Biblia kuwakilisha kanisa, mwanamke safi huwakilisha kanisa safi; mwanamke fuska huwakilisha kanisa lililoasi.

Katika Biblia, uhusiano kati ya Kristo na kanisa lake unawakilishwa na ndoa. Bwana anasema: "Nami nitakuposa uwe wangu kwa milele; naam, nitakuposa kwa haki, na kwa hukumu, na kwa ufadhili, na kwa rehema." "Rudini, enyi watoto wenye kuasi, asema Bwana; maana mimi ni mume wenu." Naye Paulo asema: "Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi." Hosea 2:19; Yeremia 3:14; 2 Wakorintho 11:2.

### Uzinzi wa Kiroho

Ukosefu wa uaminifu wa kanisa kwa Kristo kwa kuruhusu mambo ya kidunia yautawale moyo unafananishwa na kuvunja kiapo cha ndoa. Dhambi ya Israeli katika kumwacha Bwana imeelezewa [242]
kwa kielelezo kifuatacho: "Hakika kama vile mke amwachavyo

mumewe kwa hiana, ndivyo mlivyonitenda mimi kwa hiana, Ee nyumba ya Israeli, asema Bwana.” Mmekuwa kama “mke wa mtu, aziniye! Akaribishaye wageni badala ya mumewe!” Yeremia 3:20; Ezekieli 16:32.

Mtume Yakobo anasema: “Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu.” Yakobo 4:4.

Mwanamke huyu (Babeli) alikuwa “amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake. Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, Babeli mkuu, mama wa makahaba na machukizo ya nchi.” Babeli ni “mji ule mkubwa, wenyeufalme juu ya wafalme wa nchi.” Ufunuo 17:4-6, 18.

Mamlaka ambayo kwa kame nyingi ilikuwa inadhibiti wafalme katika nchi za Kikristo ni ile ya Kanisa la Roma. Rangi ya zambarau, na nyekundu, na dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, vinaonesha utukufu ambao mamlaka ya Kanisa la Roma ilikuwa imejivika. Hakuna mamlaka nyingine inayoweza kuelezewa kwa usahihi kama mwanamke ambaye “amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu” (Ufunuo 17:6) kama kanisa ambalo liliwatesa wafuasi Wakristo kikatili.

Babeli pia inatuhumiwa kwa kuwa na uhusiano batili na “wafalme wa dunia.” Kanisa la Kiyahudi lilipomwacha Bwana na kushikamana na wapagani, lilikuwa kahaba, na lile la Roma lilipotumia nguvu za kudunia linastahili hukumu hiyo hiyo.

“Babeli ni “mama wa makahaba.” Mabinti zake ni makanisa yanayoshikilia mafundisho yake na kufuata mfano wake wa kutelekeza ukweli ili yashikamane na ulimwengu. Ujumbe unaotangaza kuanguka kwa Babeli unahusu taasisi za kidini ambazo zilikuwa safi hapo mwanzo na sasa zimeasi. Kwa kuwa ujumbe unafuata baada ya ule ujumbe wa onyo la hukumu, basi unapasa
[243] kutolewa katika siku za mwisho. Hivyo hauwezi kulihusu Kanisa la Roma peke yake, kwani kanisa hilo limekuwepo katika hali ya kuanguka kwa kame nyingi.

Isitoshe, watu wa Mungu wanaitwa watoke Babeli. Kulingana na andiko hili, wengi wa watu wa Mungu bado wako ndani ya Babeli.

Sehemu kubwa na wafuasi Wakristo wanapatikana katika taasisi zipi za kidini sasa hivi? Ni katika makanisa yanayokiri imani ya Kiprotestanti. Yalipoanzishwa makanisa haya yalikuwa na msimamo safi wa kutetea ukweli, na baraka za Mungu ziliambatana nayo. Ila yalianguka kwa tamaa ile ile iliyowaangusha Israeli—kuiga desturi na kufanya urafiki na wasiomcha Mungu.

### Kuungana na Ulimwengu

Makanisa mengi ya Kiprotestanti yamefuata nyayo za Kanisa la Roma kwa kushikamana na "wafalme wa dunia"—yaani, makanisa ya kitaifa, kwa kushikamana na serikali za kidunia; na madhehebu mengine, kwa kutaka kupendwa na ulimwenguni. Neno "Babeli" (au, machafuko) linaweza kuwakilisha taasisi hizi zinazodai kuwa zinatoa mafundisho katika Biblia, lakini zimegawanyika katika madhehebu nyingi zenye mafundisho yanayopingana.

Kitabu kimoja cha Kikatoliki kinasema kwamba "kama Kanisa la Roma lina hatia ya ibada ya sanamu kwa sababu ya watakatifu; binti yake Kanisa la Uingereza, ana hatia hiyo hiyo kwani ana makanisa kumi yaliyopewa heshima ya Mariamu kwa kila kanisa moja lililopewa heshima ya Kristo." [217]

Naye Dk. Hopkins anasema: "Hakuna sababu ya kudhania kuwa tabia na desturi za upinga Kristo zinahusu kanisa ambalo leo linaitwa Kanisa la Roma. Makanisa ya Kiprotestanti yana upinga Kristo mwingi, na bado hayajabadilika ipasavyo ... kutoka katika ufisadi na uovu." [218]

Kuhusu Kanisa la Presbyterian kujitenga na Kanisa la Roma, Dk. Guthrie aliandika: "Miaka mia tatu iliyopita, kanisa letu, likiwa na Biblia iliyo wazi katika nembo yake, na mwito usemao "Yachunguzeni Maandiko" katika bango lake, lilitoka katika malango ya Roma." Kisha aliuliza swali muhimu: "Je walitoka Babeli wakiwa safi?" [219] [244]

[217] Richard Challoner, The Catholic Christian Instructed, Preface, pp. 21, 22.
[218] Samuel Hopkins, "A Treatise on the Millennium," Works, vol. 2, p. 328.
[219] Thomas Gruthrie, The Gospel in Ezekiel, p. 237.

## Hatua za Kwanza za Kuiacha Injili

Kanisa lilianzaje kuuacha usahihi wa Injili? Kwa kukubaliana na upagani, ili Ukristo ukubalike na wapagani. "Kuelekea sehemu ya mwisho ya kame ya pili makanisa mengi yalichukua sura mpya. ... Wale wanafunzi wazee walipokuwa wanalala makaburini, watoto wao pamoja na waumini wapya...walikuja na kubadili kusudi la Injili" "Wimbi la wapagani liliingia kanisani, likiwa na utamaduni, desturi na saanamu zao. [220] Dini ya Kikristo ikapata kibali na kuungwa mkono na watawala wa dunia. Ilipokelewa nusunusu na wengi. Lakini wengi "waliendelea kuwa wapagani kwa ndani, huku wakiabudu miungu yao kwa siri." [221]

Je, mchakato wa aina hiyo hiyo haujajirudia karibu katika kila kanisa linalojiita la Kiprotestanti? Waasisi wenye moyo halisi wa matengenezo wanapokufa, watoto wao "hubadili kusudi". Kwa kuwa walikataa kupokea nuru yo yote zaidi ya ile waliyokuwa nayo baba zao, watoto wa wana-matengenezo waliuacha mfano wao wa kujikana nafsi na kuukataa ulimwengu.

Ni ajabu kwamba makanisa yetu maarufu yamekiacha kiwango cha Biblia! Akizungumzia pesa, John Wesley alisema: "Msipoteze sehemu yo yote ya talanta hii yenye thamani, kwa ajili ya mavazi aghali yasiyo ya lazima, au mapambo yasiyohitajika. Msipoteze sehemu yake katika kupamba nyumba kifahari; katika samani aghali; katika picha, au nakshi za dhahabu. Kadiri unavyoendelea kuvaa 'nguo za rangi ya zambarau, na kitani safi, na kula siku zote kwa anasa,' bila shaka wengi watasifia uzuri wa mwonekano wako, wema na ukarimu wako. Lakini ni bora uridhike na heshima itokayo kwa Mungu." [222]

[245] Watawala, wanasiasa, wanasheria, madaktari, wafanya biashara, hujiunga na kanisa kama njia ya kuendeleza maslahi yao ya kidunia. Taasisi za kidini, zikitiwa nguvu na wapenda anasa hawa waliobatizwa, hujitahidi kutafuta umaarufu zaidi. Makanisa makubwa ya kifahari hujengwa. Mshahara mkubwa hulipwa kwa mchungaji mwenye kipawa kwa ajili ya kuburudisha watu. Hotuba zake lazima

[220] Robert Robinson. Ecclesiastical Researches (ed. 1792), ch. 6, par. 17, p. 51..

[221] Gavazzi, Lectures (ed. 1854), p. 278.

[222] Wesley Works, Sermon 50, "The LJse of Money

ziwe laini, za kupendeza katika masikio ya kisasa. Kwa njia hiyo dhambi zinazopendwa na wengi hufichwa katika utauwa wa bandia.

Mwandishi mmoja katika gazeti la *New York Independent* alisema hivi juu ya Umethodisti: "Tofauti kati ya watauwa na wasiokuwa na dini inatoweka taratibu na kuwa kama uvuli, na watu wenye ari wa pande zote wanajitahidi kuifuta tofauti iliyopo katika aina ya matendo na burudani zao."

Katika wimbi hili la kutafuta anasa, kujikana nafsi kwa ajili ya Kristo kumekaribia kutoweka kabisa. "Kama pesa zinatakiwa sasa, ... watu wasiombwe kutoa. Labda uwe na maonesho ya biashara, maonesho ya picha, mahakama ya bandia, chakula cha kijadi au adimu, au chakula cho chote—kitu cho chote kinachoburudisha watu."

Robert Atkins anaonesha taswira ya kuanguka kiroho huko Uingereza: "Uasi, uasi, uasi, umeandikwa mbele kabisa ya kila kanisa; na kama wangejua, kama wangeweza kuhisi, kungekuwa na tumaini, lakini sasa, wanasema, "mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu." [223]

Dhambi kubwa ambayo Babeli inatuhumiwa ni kuwanywesha "mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Kikombe hiki kinawakilisha mafundisho potovu ambayo imeyapokea kutokana na urafiki wake na dunia. Nayo kwa upande wake imekuwa na ushawishi kwa ulimwengu kwa kufundisha mafundisho yanayopingana na maelezo ya wazi ya Biblia.

Kama ulimwengu huu ungekuwa haujalewa mvinyo wa Babeli, wengi wangeamini na kuongolewa na ukweli dhahiri wa Neno la Mungu. Lakini imani ya dini inaonekana kuwa imechafuliwa na [246]
kukanganyika kiasi kwamba watu hawajui waamini nini. Dhambi ya ulimwengu kukosa toba imekaa mlangoni mwa Kanisa.

Ujumbe wa malaika wa pili haukutimia kikamilifu mwaka 1844. Wakati huo makanisa yalianguka kimaadili kwa kuikataa nuru ya ujumbe wa Ujio, lakini anguko hilo halikuwa kamilifu. Kadiri wanavyoendelea kuukataa ukweli maalum wa wakati huu wamekuwa wakianguka zaidi na zaidi. Hata hivyo bado haiwezi kusemwa kuwa "umeanguka Babeli, ... maana umewanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Makanisa ya

[223] Second Advent Library, tract No. 39.

Kiprotestanti yanajumuishwa katika tangazo hilo la malaika wa pili. Lakini kazi ya uasi haijafikia kilele chake.

Kabla ya kuja kwa Bwana, Shetani atafanya kazi "kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu;" na wote ambao "hawakukubali kuipenda ile kweli, ili wapate kuokolewa," wataachwa wapokee "nguvu ya upotevu, wauamini uongo." 2 Wathesalonike 2:9-11. Kuanguka kwa Babeli kutakamilika pale muungano wa kanisa na ulimwengu utakapokuwa umekamilika. Badiliko hili ni la hatua kwa hatua na utimilifu wa Ufunuo 14:8 uko katika siku za usoni.

Pamoja na giza la kiroho lililo katika makanisa yanayounda Babeli, watu wengi walio wafuasi wa kweli Wakristo bado wako katika ushirika wa makanisa hayo. Wengi hawajauona ukweli maalumu wa wakati huu. Si wachache wanaotamani nuru zaidi. Wanatafuta bila mafanikio sura ya Kristo katika makanisa waliyojiunga nayo.

Ufunuo 18 inatuelekeza katika wakati ambao watu wa Mungu walioko Babeli watatakiwa kujitenga na Babeli. Ujumbe huu, ambao ni wa mwisho kutolewa kwa ulimwengu, utakamilisha kazi yake. Nuru ya ukweli itawaangazia wote ambao mioyo yao iko tayari kuipokea, na watoto wote wa Bwana walio Babeli watautii mwito huo: "Tokeni kwake, enyi watu wangu." Ufunuo 18:4.

# Sura Ya 22 - Unabii Watimia [247]

Wakati wa kwanza ambao Bwana alikuwa anatarajiwa kuja ulipopita—majira ya kuchipusha ya mwaka 1844—wale waliokuwa wametarajia kuonekana kwake walikuwa katika mashaka na wasiwasi. Wengi waliendelea kuyachunguza Maandiko, wakiupima upya ushuhuda wa imani yao. Ule unabii, uliokuwa wa wazi na usio na mashaka, ulikuwa unaonesha kwamba Ujio Wakristo ulikuwa umekaribia. Baraka za Bwana katika uongofu na uamsho miongoni mwa Wakristo ulikuwa umedhihirisha kuwa ule ujumbe ulikuwa umetoka mbinguni. Pamoja na unabii ambao walikuwa wameuchukulia kuwa ulikuwa unahusu wakati wa Ujio wa pili, kulikuwa na maelekezo yaliyokuwa yanawahimiza kungoja kwa subira wakiamini kwamba mambo ambayo yalikuwa giza katika ufahamu wao kwa sasa yangewekwa wazi. Kati ya unabii huo ulikuwapo ule wa Habakuki 2:1-4. Hata hivyo hakuna aliyegundua kuwa katika unabii huo kulikuwa na uchelewaji dhahiri—wakati wa kukawia. Baada ya kuvunjika moyo, andiko hili lilionekana kuwa na maana kubwa: "Njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia... Mwenye haki ataishi kwa imani yake."

Unabii wa Ezekieli pia ulikuwa faraja kwa wale waumini: "Basi uwaambie, Bwana MUNGU asema hivi; ... Siku hizo ni karibu, na utimilizo wa maono yote. ... Maana mimi ni Bwana; mimi nitanena, na neno lile nitakalolinena litatimizwa; wala halitakawilishwa tena." "Neno nitakalolinena litatimizwa, asema Bwana MUNGU." Ezekieli 12:23-25, 28.

Wale waliokuwa wakisubiri walifurahi. Yeye anayeujua mwisho tangu mwanzo alikuwa amewapatia tumaini. Bila sehemu za Maandiko kama hizo, imani yao ingetoweka.

Ule mfano wa wanawali kumi wa Mathayo 25 pia unaonesha mambo yaliyowapata waliokuwa wanaamini juu ya Ujio. Katika mfano huo, linadhihirishwa kanisa la siku za mwisho. Mambo yaliy-

owapata yanaelezewa kwa matukio ya arusi ya watu wa Mashariki ya Kati.

[248] "Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi, waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi. Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara. Wale waliokuwa wapumbavu waiizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao; bali wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane, pakawa na kelele, Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki." Mathayo 25:1-6.

Ujio Wakristo, kama ulivyotangazwa na ujumbe wa malaika wa kwanza, ulieleweka kuwa ulikuwa unawakilishwa na Ujio wa bwana arusi. Matengenezo yaliyoenea kila mahali kutokana na tangazo la kuja kwa Kristo ambako kulikuwa kumekaribia, yalikuwa sawa na kutoka kwa wale wanawali. Katika mfano huu, wote walikuwa wamechukua taa zao, yaani Biblia, na walikuwa wamekwenda "kumlaki bwana arusi." Lakini wale wapumbavu hawakutwaa "mafuta pamoja nao," wale wenye busara "walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao." Wale wenye busara walikuwa wamesoma Maandiko na kuujua ukweli na walikuwa wameguswa wao wenyewe, yaani walikuwa na imani ambayo isingeweza kushindwa kwa sababu ya kuvunjika kwa matumaini na kuchelewa. Wengine walikuwa wanasukumwa na msisimko, uliotokana na hofu iliyosababishwa na ule ujumbe. Lakini walikuwa wanategemea imani ya ndugu zao, wakiwa wameridhika na mwanga hafifu wa mihemko, bila kuwa na ufahamu kamili wa ukweli au kazi halisi ya neema ndani ya moyo. Hawa walikuwa wamekwenda kumlaki bwana arusi wakitarajia tuzo ya haraka lakini hawakuwa tayari kukutana na ucheleweshaji na kuvunjika kwa matumaini. Imani yao ilizimia.

"Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia, wakalala usingizi." Kukawia kwa bwana arusi kunawakilisha kupita kwa ule muda, kuvunjika kwa matumaini na kile kilichoonekana kama uchelewaji. Wale ambao imani yao ilikuwa imejengwa katika ujuzi binafsi wa Biblia walikuwa na mwamba chini ya miguu yao ambao mawimbi y kuvunjika kwa matumaini yasingeweza kuuhamisha. "wote wakasinzia, wakalala usingizi," kundi moja likiwa limeiacha imani, na lingine likingoja kwa subira hadi nuru kubwa zaidi itakapotolewa.

Wale waliokuwa na imani ya juu juu wasingeweza tena kutegemea imani ya ndugu zao. Kila mtu alitakiwa kusimama au kuanguka mwenyewe.

## Itikadi Kali Zajitokeza [249]

Katika kipindi hicho, itikadi kali zilianza kuonekana. Baadhi walionesha itikadi kali. Mawazo yao yenye itikadi kali yalilipingwa vikali ya sehemu kubwa ya wale waliokuwa wakiamini juu ya Ujio, lakini yalisababisha fedheha kwa kazi ya kueneza ukweli.

Shetani alikuwa anapoteza watu wake, na ili aifedheheshe kazi ya Mungu, alitaka kuwadanganya baadhi ya wale waliokuwa wanakiri imani na kuwafanya wawe na msimamo uliopitiliza. Wakati huo mawakala wake walikuwa tayari kuchukua kila kosa, kila tendo lisilofaa, na kulitia chumvi ili kuwafanya wale waliokuwa wakiamini juu ya Ujio waonekane kama kero. Kadiri alivyowafanya wengi wakiri imani yao katika Ujio wa pili huku akitawala mioyo yao, ndivyo alivopata nafasi nzuri zaidi ya kufanikiwa.

Shetani ni "mshitaki wa ndugu zetu." Ufunuo 12:10. Roho yake huwashawishi watu kutafuta kasoro za watu wa Mungu, na kuzifanya zionekane, wakati matendo yao mema yakiachwa bila kutajwa.

Katika historia yote ya Kanisa hakuna matengenezo yaliyofanyika bila kukutana na vikwazo vikali. Kila mahali ambapo Paulo alianzisha kanisa, baadhi ya wale waliokiri kuipokea imani waliingiza mafundisho potovu. Luther pia alikutana na adha kutoka kwa watu wenye itikadi kali waliokuwa wanadai Mungu alikuwa amenena moja kwa moja kupitia kwao, ambao waliyafanya mawazo yao kuwa bora kuliko Maandiko. Wengi walidanganywa na hao walimu wapya wa uongo, na kujiunga na Sheatani katika kubomoa yale ambayo Mungu alikuwa amemvuvia Luther kuyajenga. Wafuasi wa Wesley walikutana na hila za Shetani za kuwasukumia katika itikadi kali wale wasio na ulingano na utakaso.

William Miller hakuendekeza itikadi kali. "Yule mwovu" alisema Miller, "ana uwezo mkubwa juu ya akili za wengine wakati huu." "Mara nyingi nimekuwa nikipata ushahidi wa utauwa wa kina

kutoka katika jicho lenye shauku, shavu lenye machozi na sauti inayokwama, kuliko katika kelele zote za Ukristo.” [224]

[250] Matengenezo yalilaumiwa na maadui wake kwa uovu wa itikadi kali uliokuwa juu ya wale waliokuwa wanajitahidi sana kuyapinga. Njia hiyo hiyo ilitumiwa na wale waliokuwa wakipinga harakati za Ujio. Kana kwamba kutia chumvi makosa ya wale wenye itikadi kali hakutoshi, walieneza habari ambazo hazikuwa na ukweli hata kidogo. Amani yao ilikerwa na tangazo la kukaribia kwa Yesu. Walikuwa wanahofia kwamba ingeweza kuwa kweli, lakini pia walikuwa wanaombea isiwe kweli. Hii ilikuwa ndiyo siri ya vita yao dhidi ya wale waliokuwa wakiamini juu ya Ujio.

Kuhubiriwa kwa ujumbe wa malaika wa kwanza kulielekea kutokomeza itikadi kali moja kwa moja. Wale waliokuwa wanashiriki katika harakati hizi nyeti walikuwa na umoja; mioyo yao ilikuwa imejazwa upendo kati yao na upendo kwa Yesu, ambaye walikuwa wanatarajia kumwona muda si mrefu. Imani hiyo moja, tumaini hilo moja lenye baraka, lilithibitika kuwa ngao dhidi ya mashambulizi ya Shetani.

## Makosa Yarekebishwa

“Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usikuwa manane, pakawa na kelele, Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki.” (Mathayo25:5,6). Katika kiangazi cha mwaka 1844 ujumbe huu ulitangazwa kwa nguvu kama Maandiko yalivyokuwa yanasema.

Kilichosababisha harakati hizo ni ugunduzi kwamba amri ya Artashasta ya kuujenga upya Yerusalemu, ambayo ilikuwa inaonesha mwanzo wa zile siku 2300, ilitolewa katika majira ya kupukutisha ya mwaka 457 K.K., na siyo mwanzo wa mwaka, kama ilivyo kuwa ikiaminika. Ukihesabu kuanzia mwaka 457, miaka 2300 inaishia msimu wa kupukutisha wa mwaka 1844. Vielelezo vya Agano la Kale pia vilikuwa vinaonesha “kutakaswa kwa hekalu” lazima kufanyike katika majira ya kupukutisha.

Kuchinjwa kwa mwana kondoo wa Pasaka ilikuwa ishara ya kifo cha Kristo, jambo ambalo lilitimia si katika tukio tu, bali kwa wakati pia. Siku ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza wa Kiyahudi, si ku

[224] Bliss, pp. 236, 237.

ile ile na mwezi ule ule ambao mwana kondoo wa Pasaka alikuwa anachinjwa kwa kame nyingi, Kristo alianzisha siku kuu ambayo ingeadhimisha kifo chake Yeye mwenyewe kama “Mwana Kondoo wa Mungu.” Usiku huo huo alichukuliwa kwenda kusulibiwa na kuuawa.

Vivyo hivyo vielelezo vinavyo husu Ujio wa pili vinapaswa kutimia katika muda uliotabiriwa katika vielelezo. Kutakaswa kwa hekalu au Siku ya Upatanishao, kulikuwa kunaangukia katika siku ya kumi ya mwezi wa saba wa Kiyahudi ambapo kuhani mkuu, alikuwa anatoka na kuwabariki watu baada ya kufanya upatanisho kwa ajili ya Israeli wote na hivyo kuziondoa dhambi kutoka katika hekalu. Kwa hiyo iliaminiika kuWakristo angekuja kuitakasa dunia kwa kuiangamiza dhambi na waovu, na kuwabariki kwa kuwapa kutokufa watu wake waliokuwa wanamngojea. Siku ya kumi ya mwezi wa saba, Siku kuu ya Upatanisho, siku ya kutakaswa kwa hekalu, ambayo mwaka 1844 ilikuwa inaangukia tarehe 22 oktoba, ilichukuliwa kuwa siku ya kuja kwa Bwana. Siku 2300 zilikuwa zinaishia katika majira ya kupukutisha, hatima hiyo ilikuwa inaonekana kuwa haipingiki. [251]

### “Kelele ya Usiku wa Manane”

Hoja hizo zilikuwa na ushawishi mkubwa, na “kelele ya usiku wa manane” ilitangazwa na maelfu ya waumini. Harakati hizo zilienea kutoka mji hadi mji na kutoka kijiji hadi kijiji kama wimbi za bahari. Itikadi kali zilitoweka kama ukungu kabla ya kuchomoza kwa jua. Harakati hizo zilikuwa zinafanana na vile vipindi vya kumrudia Bwana miongoni mwa wana wa Israeli vilivyokuwa vinatokea baada ya maonyo ya watumishi wake. Hakukuwa na nderemo sana, bali kujipeleleza mioyo kwa kina, maungamo ya dhambi, na kuachana na ulimwengu. Kulikuwa na kujitoa kikamilifu kwa Mungu.

Katika harakati zote za kidini tangu wakati wa mitume, hakuna harakati zilizokuwa hazina dosari za wanadamu na hila za Shetani kama zile za majira ya kupukutisha ya mwaka 1844.

Baada ya mwito, “Haya, bwana arusi anakuja,” wote waliokuwa wakisubiri “wakaondoka ... wakazitengeneza taa zao”; walijifunza Neno la Mungu kwa shauku kubwa ambayo ilikuwa haijawahi kutokea. Hawakuwa wale wenye vipaji, bali wale wanyenyekevu na

watauwa, ndio waliokuwa wa kwanza kuutii mwito huo. Wakulima waliyaacha mazao yao mashambani, mafundi waliacha zana zao,
[252] wakatoka kwa furaha kwenda kutoa ujumbe wa onyo. Makanisa kwa ujumla yaliukataa ujumbe huo, na wengi walioupokea ujumbe huu walijitenga na makanisa hayo. Wasioamini ambao walikuwa wanakusanyika kwenye mikutano ya Waadventista waliihisi nguvu ya ushawishi iliyoambana na ujumbe huo: "Haya, bwana arusi anakuja!" Imani ilileta majibu kwa maombi. Roho wa neema aliwashukia kama manyunyu ya mvua kwenye ardhi kavu, wale waliokuwa wanatafuta ukweli kwa dhati. Wale waliokuwa wanatarajia kuonana uso kwa uso na Bwana wao karibuni, walikuwa na furaha. Roho Mtakatifu aliiyeyusha mioyo yao.

Wale waliokuwa wameupokea ule ujumbe walifika katika kipindi ambacho walikuwa wanategemea kukutana na Bwana wao. Waliomba pamoja. Mara nyingi walikuwa katika sehemu zisizokuwa na watu wengi ili waongee na Mungu, na sauti yao ya kuombea wengine ilipanda kwenda mbinguni kutoka katika mashamba. Uhakika wa kukubalika na Bwana ulikuwa wa lazima sana kwao kuliko chakula cha kila siku, na pale mashaka yalipoingia katika akili zao, hawakutulia mpaka walipoona ushahidi wa neema ya msamaha.

## Matumaini Yavunjika Tena

Lakini tena, muda uliotarajiwa ulipita, na Mwokozi wao hakutokea. Sasa walijisikia kama Mariamu alivyojisikia alipofika kwenye kaburi la Mwokozi na kukukuta liko tupu, ambaye alisema akilia: "wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka." Yohana 20:13.

Wasiwasi kwamba ujumbe huo ungeweza kuwa wa kweli, ulisaidia kuwafanya wasioamini wanyamaze. Lakini dalili za ghadhabu ya Mungu zilipokosekana, walizinduka kutoka katika wasiwasi wao na kuanza tena dhihaka na kejeli zao. Sehemu kubwa ya wale waliokuwa wamekiri kuamini waliikana imani. Wenye kudhihaki waliwapata walio dhaifu na waoga na kuwavutia upande wao, na hawa wote waliungana katika kutangaza kwamba dunia ingeweza kubakia hivyo kwa niaka elfu.

Wale waumini wanyofu walikuwa wameacha vyote kwa ajili ya Kristo, na kwa kuamini kwao, walikuwa wameshatoa onyo la mwisho kwa ulimwengu. Walikuwa wamemwomba Mungu kwa shauku kubwa, "Na uje Bwana Yesu." Lakini sasa kurudia tena [253] mahangaiko ya maisha na kustahimili kejeli za wenye kudhihaki, lilikuwa jaribu kubwa.

Wakati Yesu alipoingia Yerusalemu kama mshindi, wafuasi wake waliamini kuwa alikuwa anakaribia kuketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi na kuwakomboa Israeli kutoka kwa watesi wao. Wengi walitandika mavazi yao kama zulia katika njia yake au kutandaza matawi ya mitende kwa matumaini. Wanafunzi hao walikuwa wanatimiza makusudi ya Mungu, lakini walikuwa wanaelekea katika kuvunjika moyo sana. Siku chache baadaye walishuhudia Mwokozi wao akipiga kite wakati anakabiliana na mauti na wakamzika kaburini. Matumani yao juu ya Yesu yalikufa. Mpaka Bwana wao alipotoka kaburini ndipo walipoelewa kwamba yote yalikuwa yametabiriwa katika unabii.

### Ujumbe Uliotolewa kwa Wakati Mwafaka

Vivyo hivyo Miller na wenzake walitimiza unabii na kutoa ujumbe uliokuwa umetabiriwa kuwa ilipasa utolewe kwa ulimwengu. Wasingeweza kuutoa ujumbe huo kama wangekuwa wameuelewa kikamilifu unabii uliokuwa unatabiri kuvunjika kwa matumaini yao na kuwasilisha ujumbe mwingine uliopasa kuhubiriwa kwa mataifa yote kabla ya kuja kwa Bwana. Ujumbe wa malaika wa kwanza na ujumbe wa malaika wa pili ulitolewa kwa wakati sahihi na ulifanya kazi ambayo Mungu alikuwa amekusudia kuifanya kwa ujumbe huo.

Ulimwengu ulikuwa unatarajia kuwa kama Kristo asingerudi, imani ya Ujio ingeachwa. Lakini, pamoja na wengi kuiacha imani yao, kulikuwa na baadhi ambao walisimama imara. Matokeo ya harakati za Ujio, moyo wa kujipeleleza moyoni, wa kuikana dunia na matengenezo ya maisha, vilishuhudia kwamba jambo hili lilikuwa la Mungu. Hawakuthubutu kukanusha kwamba Roho Mtakatifu alikuwa amehusika katika mahubiri ya Ujio wa pili. Hawakuweza kugundua kosa lo lote katika vile vipindi vya unabii. Wapinzani wao walikuwa hawajafaulu kuupinga ufasiri wao. Hawakukubali kukana

msimamo uliokuwa umefikiwa kwa usomaji makini wa Maandiko ulioambatana na maombi ambao ulifanywa na watu waliokuwa wameangaziwa na Roho wa Mungu na mioyo iliyokuwa ikiwaka kwa nguvu yake ihuishayo, na ambayo ilisimama imara dhidi ya elimu na lugha ya ushawishi.

[254] Waadventista walikuwa wanaamini kuwa Mungu alikuwa amewaongoza kutoa onyo juu ya hukumu. Walikuwa wanasema, "Onyo hilo limeipima mioyo ya wale waliolisikia, ... ili wale watakaojipileleza mioyo yao, wajue wangekutwa wakiwa upande gani, kama Bwana angekuja—kama wangesema 'Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, ndiye tuliyemngoja atusaidie; huyu ndiye Bwana tuliyemngoja, na tushangilie na kuufurahia wokovu wake;' au wangeiambia miamba na milima iwaangukie ili iwasitiri mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi." (Isaya 25:9; Ufunuo 6:16). [225]

Hisia za wale wakuwa wanaendelea kuamini kuwa Mungu ameongoza zinaonekana katika maneno ya William Miller: "Tumaini langu la Ujio Wakristo ni imara kama lilivyokuwa siku zote. Nilichokifanya ni kile ambacho, niliona kuwa kilikuwa wajibu wangu kukifanya, baada ya kutafakari kwa makini." "Kwa mtazamo wa kibinadamu, mahubiri yaliyokuwa yanahusu huo wakati, yaliwafanya maelfu ya watu, kusoma Maandiko; na kwa njia hiyo, wameweza kupatanishwa na Mungu kwa kunyunyiziwa damu ya Kristo." [226]

### Imani Yadumishwa

Roho wa Mungu bado alikuwa na wale ambao hawakuikana kwa pupa imani waliyokuwa wameipokea na kuzipinga harakati za Ujio. "Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi y Mungu mpate ile ahadi. Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia. Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita- sita, rohoyangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu." Waebrania 10:35-39

[255] Mawaidha haya yametolewa kwa kanisa la siku za mwisho.

[225] The Advent Herald and Signs of the Times Reporter, vol. 8, no. 14 (Nov. 13, 1844).
[226] Bliss, pp. 256, 255, 277, 280, 281.

Inaonekana wazi kwamba Bwana angeonekana kana kwamba anakawia. Watu wanaoambiwa hapa walikuwa wamefanya mapenzi ya Mungu katika kufuata uongozi wa Roho na Neno lake; lakini walikuwa hawalielewi kusudi lake katika mambo yaliyokuwa yamewapata. Walijaribiwa kuwa na mashaka kama Bwana alikuwa anawaongoza kweli. Wakati huo maneno haya yalikuwa mwafaka: "Mwenye haki ataishi kwa imani." Wakiwa wamenyong'nyea kwa matumaini yaliyovunjika, wasingeweza kusimama isipokuwa kwa imani juu ya Mungu na Neno lake. Kuikana imani yao pamoja na nguvu ya Roho Mtakatifu iliyokuwa imeambatana na ujumbe huo ingekuwa ni kurudi katika uharibifu. Njia pekee iliyokuwa salama kwao ilikuwa kushikilia nuru ambayo walikuwa wameipokea kutoka kwa Mungu, kuendelea kuyachunguza Maandiko, na kungoja kwa subira kupokea nuru zaidi.

[256] 

# Sura Ya 23 - Fumbo Lililo Wazi La Patakatifu

Andiko lililokuwa msingi na nguzo ya imani ya Waadventista ni tangazo lisemalo, “Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa.” Danieli 8:14. Haya yalikuwa maneno ya kawaida kwa wote waliokuwa wanaamini kuwa Bwana alikuwa anakuja upesi. Lakini Bwana alikuwa hajatokea. Wale waumini walikuwa wanaamini kuwa Neno la Mungu lisingesema uongo; bila shaka ufasiri wao wa unabii ulikuwa na kasoro. Lakini kasoro ilikuwa wapi?

Mungu alikuwa wamewaongoza watu wake katika harakati kubwa za Ujio. Asingeruhusu ziishie katika giza na kuvunjika moyo, zikishutumiwa kuwa za uongo na zenye itikadi kali. Ingawa wengi waliachana na hesabu zao za vipindi vya uabii na kuzikana harakati hizo kwa sababu hiyo, wengine hawakuwa tayari kuzikana hoja za imani na matukio ambayo yalithibitishwa na Maandiko pamoja na Roho wa Mungu. Ulikuwa wajibu wao kushikilia ulweli uliokuwa umekwisha kupatikana. Waliyachunguza Maandiko kwa maombi ya dhati ili waone kosa lao. Walipoona kuwa hakukuwa na kosa katika hesabu zao za vipindi vya unabii, walianza kuchunguza kwa undani zaidi suala la patakatifu.

Waligundua kuwa hakukuwa na ushahidi wa Maandiko unaounga mkono dhana ya wengi kwamba dunia ndiyo patakatifu; bali walipata maelezo kamili ya patakatifu, palivyo, pako wapi na huduma zake; “Basi hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida za ibada, na patakatifu pake, pa kidunia. Maana hema ilitengenezwa, ile ya kwanza, mlimokuwa na kinara cha taa, na meza, na mikate ya Wonyesho; ndipo palipoitwa, patakatifu. Na nyuma ya pazia la pili, ile hema iitwayo patakatifu pa patakatifu, yenye chetezo cha dhahabu, na sanduku la agano lililofunikwa kwa dhahabu pande zote, mlimokuwa na kopo la dhahabu lenye ile mana, na ile fimbo ya Haruni iliyochipuka, na vile vibao vya agano; na juu yake makerubi ya utukufu, yakikitia kivuli kiti cha rehema; basi hatuna nafasi sasa ya kueleza habari za vitu hivi kimoja kimoja.” Waebrania 9:1-5.

Patakatifu palikuwa mahali palipojengwa na Musa kwa agizo la Mungu kama makazi ya Aliye Juu hapa duniani. Agizo alilopewa Musa lilikuwa "Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao" (Kutoka 25:8). Hema ile ilikuwa jengo lenye utukufu. Pamoja na ua wa nje, hema yenyewe ilikuwa na vyumba viwili vilivyokuwa vinaitwa patakatifu na patakatifu sana, vilivyokuwa vinatenganishwa na pazia. Pazia la aina hiyo hiyo lilikuwa linaziba mlango wa kuingilia katika chumba cha kwanza. [257]

### Patakatifu na Patakatifu Sana

Mle patakatifu mlikuwa na kinara cha taa upande wa kusini kikiwa na taa zake saba zilizokuwa zinatoa nuru usiku na mchana; upande wa kaskazini kulikuwa na meza ya mikate ya wonyesho. Mbele ya pazia lililokuwa linatenganisha patakatifu na patakatifu sana, kulikuwa na madhabahu ya dhahabu ya kufukizia uvumba, ambapo wingu la manukato lilikuwa linapanda pamoja na maombi ya wana wa Israeli kwenda mbele za Mungu kila siku.

Baada ya Waebrania kukaa katika nchi ya Kanaani, ile hema ilibadilishwa na kujengwa hekalu la Sulemani, ambalo, pamoja na kuwa jengo la kudumu, na kubwa zaidi, lilikuwa na uwiano ule ule na lilikuwa na samani zile zile. Patakatifu paliendelea kuwa hivyo mpaka palipoharibiwa na Warumi mwaka wa 70 B.K., isipokuwa wakati palipokuwa gofu wakati wa Danieli. Hapa ni patakatifu pekee duniani ambapo panazungumziwa na Biblia, patakatifu pa agano la kwanza. Lakini je, agano jipya halina patakatifu?

Walipokiangalia tena kitabu cha Waebrania, wale waliokuwa wanatafuta ukweli waligundua kwamba patakatifu pengine au patakatifu pa agano jipya palikuwa panagusiwa katika maneno yaliyokwisha kunukuliwa; "Basi hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida za ibada, na patakatifu pake, pa kidunia." (Ebr. 9:1).

Walipoangalia mwanzoni mwa sura ya nyuma yake, walisoma: "Tunaye kuhani mkuu wa namna hii,aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha ukuu mbinguni, mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu." Waebrania 8:1,2.

Hapa panaoneshwa patakatifu pa agano jipya. Patakatifu [258]
pa agano la kwanza palijengwa na Musa; patakatifu pa sasa

pamejengwa na Bwana. Katika patakatifu pa kwanza, walikuwa wanahudumu makuhani wa kidunia; katika patakatifu pa pili Kristo, Kuhani wetu Mkuu anahudumu akiwa mkono wa kulia wa Mungu. Patakatifu pa kwanza palikuwa duniani, na pa pili pako mbinguni.

Hema iliyojengwa na Musa ilijengwa kulingana na mfano. Bwana alielekeza: "Sawasawa na haya yote nikuonyeshayo, mfano wa maskani, na mfano wa vyombo vyake vyote, ndivyo mtakavyovifanya." "Nawe angalia ya kwamba uvifanye kama mfano wake, ulioonyeshwa mlimani." Hema ya kwanza ilikuwa "mfano wa wakati huu uliopo sasa; wakati huo sadaka na dhabihu zinatolewa," na patakatifu pake palikuwa "nakala za mambo yaliyo mbinguni." Makuhani walihudumu kama "mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni." " Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu." Kutoka 25:9, 40; Waebrania 9:9, 23; 8:5; 9:24.

Patakatifu pa mbinguni ni patakatifu chanzi na patakatifu palipojengwa na Musa palikuwa nakala yake. Utukufu wa ile hema ya duniani ulikuwa unaakisi utukufu wa lile hekalu la mbinguni ambapo Kristo anahudumu kwa ajili yetu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Ukweli muhimu juu ya patakatifu pa mbinguni na wokovu wa mwanadamu ulifundishwa kwa kutumia patakatifu pa duniani pamoja na huduma zake.

### Vile Vyumba Viwili

Vyumba viwili vya patakatifu pa mbinguni vinawakilishwa na vile vyumba viwili katika patakatifu pa duniani. Yohana alioneshwa hekalu la Mungu kule mbinguni. Aliona "taa saba za moto zikiwaka mbele ya kile kiti cha enzi." Aliona malaika "mwenye chetezo cha dhahabu, akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote juu ya madhabahu ya dhahabu, iliyo mbele ya kiti cha enzi." Ufunuo 4:5; 8:3. Hapa nabii huyu alikuwa anaona chumba cha kwanza cha patakatifu pa mbinguni; na hapo aliona "taa saba za moto" na "madhabahu ya dhahabu," vilivyokuwa vinawakilishwa na kinara cha taa cha dhahabu na madhabahu ya kufukizia uvumba katika patakatifu pa duniani.

[259] "Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa" tena, na

akatazama ndani ya pazia katika patakatifu sana. Hapo aliona "sanduku la agano" lililokuwa linawakilishwa na sanduku lililokuwa limetengenezwa na Musa kwa ajili ya kuwekea sheria ya Mungu. Ufunuo 11:19. Kwa hiyo wale waliokuwa wanachunguza suala hili walipata ushahidi wa kuwepo kwa patakatifu mbinguni. Yohana anashuhudia kuwa alipaona.

Katika lile hekalu la mbinguni, ndani ya patakatifu sana, kuna sheria ya Mungu. Sanduku linalohifandhi sheria hiyo limefunikwa kwa kiti cha rehema, ambacho Kristo anasimama mbele yake na kusihi kwa damu yake kwa niaba ya mwenye dhambi. Kwa njia hiyo, muungano wa haki na rehema vinawakilishwa katika mpango wa ukombozi, mwungano unaoifanya mbungu yote istaajabu. Hii ndiyo siri ya rehema ambayo malaika wanatamani kuitazama—kwamba Mungu anaweza kuwa mwenye haki na wakati huo huo akamhesabia haki mwenye dhambi atubuye, kwamba Kristo aliweza kuinama ili awainue wengi kutoka katika uharibifu na kuwavika mavazi safi ya haki yake mwenyewe.

Kazi ya Kristo kama mwombezi wa mwanadamu inaelezewa katika Zekaria: "Tazama, mtu huyu ndiye ambaye jina lake ni Chipukizi; naye atakua katika mahali pake, naye atalijenga hekalu la Bwana. Naam, yeye atalijenga hekalu la Bwana; naye atauchukua huo utukufu; ataketi akimiliki katika kiti chake cha enzi; na kutakuwa na kuhani katika kiti chake cha enzi; na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili." Zekaria 6:12,13.

"Naam, yeye atalijenga hekalu la Bwana." (Zekaria 6:12): Kwa njia ya dhabihu yake na upatanishi wake, Kristo ni msingi na mjenzi wa kanisa la Mungu, "jiwe kuu la pembeni ambalo katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana." Waefeso 2:20, 21.

"Naye atauchukua huo utukufu." (Zekaria 6:13): Wimbo wa waliokombolewa utakuwa: "Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake. . . utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina." Ufunuo 1:5,6.

"Ataketi akimiliki katika kiti chake cha enzi; na kutakuwa na [260]
kuhani katika kiti chake cha enzi" (Zekaria 6:13): Ufalme wa utukufu haujaanza bado. Kazi yake kama mwombezi itakapokoma ndipo Mungu atakapamkabidhi ufalme ambao "utakuwa hauna mwisho." Luka 1:33. Sasa hivi Kristo amekaa pamoja na Baba

katika kiti chake cha enzi kama kuhani. Katika kiti hicho cha enzi amekaa yeye "ayachukuaye masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu," ambaye "alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi," ili aweze "kuwasaidia wao wanaojaribiwa." Isaya 53:4; Waebrania 4:15; 2:18. Ile mikono yenye majeraha, ubavu uliochomwa, miguu iliyoumizwa, inasihi kwa ajili ya mwanadamu aliyeanguka ambaye ukombozi wake ulinunuliwa kwa gharama hiyo.

"Na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili." (Zekaria 6:13): Upendo wa Baba ni Chemchemi ya wokovu kwa jamii ya waliopotea. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Baba mwenyewe awapenda ninyi." Mungu "alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake." "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 16:27; 2 Wakorintho 5:19; Yohana 3:16.

## Fumbo la Patakatifu Lafumbuliwa

"Hema ya kweli" iliyo mbinguni ndiyo patakatifii pa agano jipya. Wakati Kristo alipokufa huduma kielelezo zilikoma. Kwa kuwa Danieli 8:14 ilitimia katika kipindi cha agano jipya, basi patakatifu panapozungumziwa hapa ni lazima pawe pa agano jipya. Kwa hiyo unabii unaosema "Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa," unahusu patakatifu pa mbinguni.

Lakini kutakaswa kwa patakatifu ni nini? Je, kunaweza kukawa na kitu cho chote cha kutakaswa mbinguni? Katika Waebrania 9 kutakaswa kwa patakatifu pa duniani na patakatifu pa mbinguni panaelezewa: "Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo. Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo, lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasaflshwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo" (Waebrania 9:22, 23), yaani damu ya Kristo iliyo na thamani.

## Kutakaswa kwa Patakatifu [261]

Utakasaji katika huduma halisi sharti ufanyike kwa damu ya Kristo. “na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo.” Kuondoa dhambi ndiyo kazi inayopasa kufanyika.

Lakini ingewezekana vipi kukawa na dhambi inayohusiana na hekalu la mbinguni? Jambo hili linaweza kueleweka kwa kuangalia ile huduma kielelezo, kwa kuwa makuhani wa duniani walihudumu kama “mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni.” Waebrania 8:5.

Huduma katika patakatifu pa duniani ilikuwa na sehemu mbili. Makuhani walikuwa wanahudumu kila siku katika chumba cha patakatifu, na mara moja kwa mwaka kuhani mkuu alikuwa anafanya kazi maalum ya upatanisho katika chumba cha patakatifu sana, kwa ajili ya kupatakasa patakatifu. Kila siku mwenye dhambi alikuwa analeta dhabihu yake na kuweka mikono yake juu ya kichwa cha mhanga huyo akiungama dhambi zake, kama kielelezo cha kuzihamisha kutoka kwake kwenda kwa ile dhabihu isiyo na hatia. Kisha yule mnyama alikuwa anauawa. “Kwa kuwa uhai wa mwili u katika hiyo damu.” Walawi 17:11. Sheria ya Mungu iliyokuwa imevunjwa ilikuwa inahitaji uhai wa mkosaji. Damu, inayowakilisha uhai wa mwenye dhambi ambaye hatia yake ilikuwa inachukuliwa na yule mhanga, ilikuwa inapelekwa na kuhani katika chumba cha patakatifu na kunyunyiziwa mbele ya pazia, ambalo nyuma yake kulikuwa sheria ambayo mwenye dhambi alikuwa ameivunja. Kwa utaratibu huu dhambi ile ilikuwa kana kwamba imehamishiwa patakatifu. Wakati mwingine ile damu ilikuwa haipekekwi katika chumba cha patakatifii, bali nyama ilikuwa inaliwa na kuhani. Utaratibu wote huu ulikuwa unawakilisha kuhamishwa kwa dhambi kutoka kwa mtu aliyetubu kwenda patakatifu.

Hiyo ndiyo kazi iliyokuwa inafanyika mwaka mzima. Dhambi za Israeli zilikuwa zinahamishiwa patakatifu kwa njia hiyo, na hivyo kazi maalum ya kuziondoa ilikuwa inahitajika.

## Siku kuu ya Upatanisho

Kuhani mkuu alikuwa anaingia patakatifu sana mara moja kwa mwaka, katika siku kuu ya upatanisho, kwa ajili ya kupatakasa patakatifu. Wana mbuzi wawili walikuwa wanaletwa na kupigiwa [262]

kura, "kura moja kwa ajili ya Bwana; na kura ya pili kwa ajili ya Azazeli." Walawi 16:8. Mbuzi wa BWANA alichinjwa kama sadaka ya dhambi za watu, na ilimpasa kuhani kuipeleka damu yake ndani ya pazia na kuinyunyizia mbele ya kiti cha rehema na pia kwenye madhabahu ya kufukizia uvumba iliyokuwa mbele ya pazia.

"Na Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai, na kuungama juu yake uovu wote wa wana wa Israeli, na makosa yao, naam, dhambi zao zote; naye ataziweka juu ya kichwa chake yule mbuzi, kisha atampeleka aende jangwani kwa mkono wa mtu aliye tayari. Na yule mbuzi atachukua juu yake uovu wao wote, mpaka nchi isiyo watu; naye atamwacha mbuzi jangwani." Walawi 16:21, 22. Mbuzi wa Azazeli hakuwa anarudi tena katika kambi ya Israeli.

Sherehe hiyo ilikusudiwa kuwafanya Waisraeli wahisi utakatifu wa Mungu na chuki yake dhidi ya dhambi. Kila mtu alikuwa anatakiwa kuitaabisha nafsi yake wakati kazi hii ya upatanisho inaendelea. Shughuli zote ziliwekwa kando, na ilikuwa inawapasa Israeli kuitumia siku hiyo kwa maombi, kufunga na kujihoji moyoni.

Mbadala alikubalika badala ya mdhambi, ila dhambi ilikuwa haifutwi na ile damu ya yule mhanga: ilikuwa inahamishiwa patakatifu. Kwa kutoa hiyo damu, mwenye dhambi alikuwa anakiri mamlaka ya sheria, alikuwa anaungama makosa yake, na alikuwa anaonesha imani yake kwa Mwokozi aliyekuwa anakuja; lakini alikuwa haondolewi kabisa hukumu ya sheria. Siku ya upatanisho kuhani mkuu, baada ya kuchukua dhabihu kutoka katika kusanyiko, alikuwa anaingia patakatifu sana. Alikuwa ananyunyizia damu ya dhabihu hiyo kwenye kiti cha rehema, juu ya sheria, ili kutimiza matakwa ya sheria hiyo. Kisha akiwa kama mwombezi, alikuwa anazichukua dhambi hizo mwilini mwake na kuzipeleka nje ya patakatifu. Akiweka mikono yake juu ya yule mbuzi wa Azazeli, alizihamisha dhambi hizo kwa kielelezo toka kwake kwenda kwa yule mbuzi. Yule mbuzi alikuwa anakwenda nazo mbali, na kwa njia hiyo zilikuwa zinachukuliwa kuwa zimeondolewa kutoka kwa watu.

[263]

## Jambo Halisi Mbinguni

Jambo lililokuwa linafanyika kama kielelezo katika huduma ya patakatifu pa duniani, linafanyika kikweli katika patakatifu pa

mbinguni. Baada ya kupaa kwake, Mwokozi wetu alianza kazi kama kuhani wetu mkuu: "Kwa sababUkristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu." Waebrania 9:24.

Huduma ya kuhani katika chumba cha kwanza, "ndani ya pazia" lililokuwa linatenganisha patakatifu na ua wa nje, inawakilisha kazi ambayo Kristo aliianza baada ya kupaa. Katika huduma ya kila siku kuhani alikuwa anawasilisha mbele ya Mungu damu ya ile sadaka ya dhambi, na pia uvumba ambao ulipanda pamoja na maombi ya Israeli. Ndivyo Kristo alivyosihi kwa damu yake mbele ya Baba kwa niaba ya wenye dhambi na kuwasilisha mbele yake, maombi ya wenye dhambi waliotubu pamoja na harufu nzuri ya haki yake. Hivyo ndivyo huduma ilivyokuwa katika chumba cha kwanza cha patakatifu pa mbinguni.

Huko ndiko imani ya wanafunzi wa Yesu ilikomfuata wakati amepaa. Hapo ndipo matumaini yao yalipokuwa, "matumaini ... tuliyo nayo kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia, alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu, amekuwa kuhani mkuu hata milele." "Kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele." Waebrania 6:18-19, 20; 9:12.

Kazi hii iliendelea katika chumba cha kwanza cha patakatifu kwa kame kumi nane. Damu ya Kristo ilileta msamaha na kukubalika mbele za Baba kwa niaba ya waumini waliotubu, lakini dhambi zao zilibaki katika vitabu vya kumbukumbu. Kama ilivyokuwa katika huduma kielelezo, kulikuwa na kazi ya upatanisho mwishoni mwa kila mwaka, vivyo hivyo kabla ya kazi ya Kristo kwa ajili ya wanadamu kukamilika, kuna kazi ya upatanisho kwa ajili ya kuondoa dhambi kutoka patakatifu. Kazi hii ilianza mwishoni mwa zile siku 2300. Wakati huo Kuhani Mkuu aliingia patakatifu sana kupatakasa patakatifu.

## Kazi ya Hukumu [264]

Katika agano jipya, dhambi za wale wanaotubu huwa zinawekwa juu ya Kristo kwa njia ya imani na kuhamishiwa patakatifu pa mbinguni. Na kama vile kutakaswa kwa patakatifu pa duniani kulivy-

ofanyika kwa kuziondoa dhambi ambazo zilikuwa zimepachafua, vivyo hivyo utakaso halisi wa patakatifu pa mbinguni unafanyika kwa kuziondoa au kuzifuta dhambi zilizoandikwa. Lakini kabla ya jambo hilo kufanyika ni lazima kuwa na ukaguzi wa vitabu vya kumbukumbu kuona ni nani anastahili kunufaika na upatanisho Wakristo kwa njia ya toba na imani kwake. Kwa hiyo kutakaswa kwa patakatifu kunaambatana na kazi ya upelelezi—kazi ya hukumu—kabla ya kuja kwa Kristo, kwani atakapokuja, ujira wake utakuwa pamoja naye kumlipa kila mtu sawasawa na matendo yake. Ufunuo 22:12.

Kwa hiyo wale walioifuata nuru ya neno la unabii waliona kwamba, badala ya kuja duniani mwishoni mwa zile siku 2300, mwaka 1844, Kristo aliingia patakatifu sana pa patakatifu pa mbinguni kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho kama maandalizi ya kuja kwake.

Kristo anapoondoa dhambi za watu wake kwa damu yake kutoka patakatifu pa mbinguni mwishoni mwa huduma yake, ataziweka juu ya Shetani, ambaye inampasa kupata ile adhabu ya mwisho. Mbuzi wa azazeli alikuwa anapelekwa katika nchi isiyokaliwa na watu, na hakurudi tena katika kusanyiko la Israeli. Hivyo ndivyo Shetani akakavyoondolewa katika uwepo wa Mungu na watu wake, na ataondoshwa kabisa wakati wa maangamizi ya mwisho ya dhambi na wenye dhambi na hatakuwapo tena.

# Sura Ya 24 - Yesu Anafanya Nini Sasa? [265]

Suala la patakatifu lilifumbua lile fumbo la kuvunjika kwa matumaini. Liliweka wazi mfumo mzima wa ukweli mwingi, uliokuwa unahusiana na kupatana, kuonesha kuwa mkono wa Mungu ulikuwa umeongoza zile harakati za Ujio. Wale waliokuwa wametazamia Ujio wa pili kwa imani walikuwa wanamtegemea atokee katika utukufu, lakini matumaini yao yalipovunjika, wakawa hawanwoni Yesu. Sasa walikuwa wakimtazama Kuhani wao Mkuu tena katika patakatifu sana, ambaye anakuja upesi kama mfalme na mkombozi. Nuru kutoka patakatifu iliangazia mambo yaliyopita, yaliyopo, na yajayo. Ingawa walikuwa hawakuuelewa ujumbe waliokuwa wanautoa, bado ujumbe huo ulikuwa wa kweli.

Kosa halikuwa katika kuhesabu vipindi vya unabii, lakini lilikuwa juu ya tukio ambalo lingetokea mwishoni mwa zile siku 2300. Hata hivyo yote yaliyokuwa yametabiriwa na unabii huo yalikuwa yametimia.

Kristo alikuwa amekuja, lakini si duniani, bali patakatifu sana pa hekalu la mbinguni: "Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye." Danieli 7:13.

Ujio huu ulitabiriwa na Malaki: "Angalieni, namtuma mjumbe wangu, naye ataitengeneza njia mbele yangu; naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafula; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema Bwana wa majeshi." Malaki 3:1. Ujio wa Bwana katika hekalu lake ulikuwa wa "ghafla" usiotarajiwa na watu wake. Walikuwa hawamtafuti hapo.

Watu hawakuwa tayari kukutana na Bwana wao. Bado kulikuwa na kazi ya maandalizi juu yao. Wanapomfuata Kuhani wao Mkuu katika huduma yake, kazi mpya zitafunuliwa. Ujumbe mwingine ulikuwa unapasa kutolewa kwa kanisa.

[266]

## Nani Atasimama?

Nabii Malaki anasema: "Lakini ni nani atakayestahimili siku ya kuja kwake? Au ni nani atakayesimama atakapoonekana yeye? Kwa maana yeye ni mfano wa moto wa mtu asafishaye fedha, ni mfano wa sabuni ya mtu afuaye nguo; naye ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa, naye atawatakasa wana wa Lawi, atawasafisha kama dhahabu na fedha; nao watamtolea Bwana dhabihu katika haki." Malaki 3:2, 3. Wale watakaokuwa wanaishi duniani wakati huduma ya Kristo ya maombezi itakapokoma, watasimama mbele za Mungu bila mwombezi. Itapasa mavazi yao yawe safi bila mawaa, tabia zao zitakuwa zimetakaswa dhidi ya dhambi kwa kunyunyiziwa damu. Kwa neema ya Mungu na juhudi zao za dhati itawapasa kuwa washindi katika vita dhidi ya uovu. Wakati hukumu ya upelelezi inaendelea huko mbinguni, kutakuwa na kazi maalum ya kuondoa dhambi miongoni mwa watu wa Mungu hapa duniani. Kazi hii inaelezewa katika ujumbe wa Ufunuo 14. Kazi hii itakapokamilika, wafuasi Wakristo watakuwa tayari kwa Ujio wake. Wakati huo kanisa ambalo Bwana atalipokea wakati wa kuja kwake litakuwa "kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali ... takatifu lisilo na mawaa." Waefeso 5:27.

## "Haya, Bwana Arusi"

Kuja kwa Kristo kwenye patakatifu sana kama Kuhani Mkuu kwa ajili ya kupatakasa patakatifu (Dan. 8:14), kuja kwa aliye mfano wa mwanadamu kwa Mzee wa Siku (Danieli 7:13), na kuja kwa Bwana katika hekalu lake (Malaki 3:11) ni tukio moja. Jambo hili linawakilishwa pia na kuja kwa bwana arusi kwenye arusi katika mfano wa wanawali kumi wa Mathayo 25.

Katika mfano huo, bwana arusi alipokuja, "wale waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa." Kuja huku kwa bwana arusi kulitokea kabla ya arusi. Arusi inawakilisha Kristo kupokea ufalme wake. Mji Mtakatifu, Yerusalemu Mpya, mji mkuu na kiwakilishi cha huo ufalme, unaitwa, "bibi arusi, mke wa Mwanakondoo." Malaika alimwambia Yohana: "Njoo huku, nami nitakuonyesha yule Bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo." "Akanichukua katika Roho", nabii Yohana anasema, "akanionye-

sha ule mji mtakatifii, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu.” Ufunuo 21:9, 10.

Bibi arusi anawakilisha ule Mji Mtakatifu, na wale wanawali [267]
waliokwenda kumlaki bwana arusi ni kielelezo cha kanisa. Katika Ufunuo watu wa Mungu wanaonekana kuwa wageni katika karamu ya arusi. Kama ni wageni, basi hawawezi kuwa bibi arusi. Kristo atapokea kutoka kwa Mzee wa Siku “mamlaka, na utukufu, na ufalme,” Yerusalemu mpya, makao makuu ya ufalme wake, ulioandaliwa, “kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.” Baada ya kuupokea ufalme, atakuja kama Mfalme wa Wafalme na Bwana wa mabwana kwa ajili ya ukombozi wa watu wake ambao watashiriki katika karamu ya arusi ya Mwana-kondoo. Danieli 7:14; Ufunuo 21:2.

### Kumngoja Bwana Wao

lle kelele, “Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki” iliwafanya maelfu watarajie Ujio wa Bwana mara moja. Bwana arusi alikuja katika wakati uliopangwa, si duniani, lakini kwa Mzee wa Siku kule mbinguni, kwenye arusi, kupokea ufalme wake. “Nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini.” Haikuwapasa kuwa hapo kwani walikuwa duniani. Inawapasa wafuasi Wakristo “kumngojea Bwana wao, atakaporudi kutoka arusini, ili atakapokuja na kubisha, wamfungulie mara.” Luka 12:36. Laini inawapasa kuielewa kazi yake na kumfuata kwa imani. Kwa maana hiyo wanasemekana kuwa wamekwenda kwenye arusi. Ila inawapasa kuielewa kazi yake na kumfuata kwa imani.

Katika mfano huo, wale waliokuwa na mafuta katika taa zao waliingia arusini. Wale ambao walingoja kwa uvumilivu, katika giza Ia majaribu makali, wakiichunguza Biblia kwa ajili ya nuru zaidi—hawa waliuona ukweli juu ya patakatifu pa mbinguni na badiliko la huduma ya Mwokozi. Walimfuata kwa imani katika kazi yake ya patakatifu kule juu. Na wale wote wanaoupokea ukweli huo, wakimfuata Kristo kwa imani akifanya kazi yake ya mwisho ya uombezi, wataingia katika arusi.

## Kazi ya Mwisho ya Patakatifu

Katika mfano wa Mathayo 22, hukumu ilifanyika kabla ya arusi. Kabla ya arusi mfalme alikuja kuona kama wageni wote wamevaa vazi la arusi, vazi lisilo na mawaa la tabia iliyooshwa katika damu ya Mwana Kondoo. Ufunuo 7:14. Wote walioonekana na vazi la arusi baada ya ukaguzi walikubaliwa na kuhesabiwa kuwa walikuwa wanastahili kushiriki katika

[268] ufalme wa Mungu na kuwa na sehemu katika kiti chake cha enzi. Kazi hii ya uchunguzi wa tabia ni hukumu ya upelelezi, kazi ya mwisho ya patakatifu pa mbinguni.

Mashauri ya wale ambao wamekuwa wakimkiri Yesu katika enzi zote yatakapokuwa yameamuliwa, muda wa matazamio utakwisha na mlango wa rehema utafungwa. Hivyo kwa sentensi moja fupi isemayo "Nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa," tunapelekwa katika wakati ambapo kazi kubwa ya wokovu wa mwanadamu itakamilika.

Wakati kuhani mkuu alipokuwa anaingia patakatifu sana siku ya upatanisho, huduma katika chumba cha kwanza ilikuwa inasimama. Kwa hiyo Kristo alipoingia patakatifu sana kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho, alikomesha huduma yake katika hema ya kwanza. Wakati huo huduma katika chumba cha pili ilianza. Kristo alikuwa amekamilisha sehemu moja tu ya kazi yake kama mwombezi, na kuingia katika sehemu nyingine ya kazi hiyo. Bado alikuwa anasihi mbele ya Baba kwa kwa niaba ya wenye dhambi kwa kutumia damu yake.

Wakati ni kweli kwamba mlango wa matumaini na rehema ambao wanadamu walipitia kwenda kwa Mungu kwa miaka 1800 ulikuwa umefungwa, mlango mwingine ulifunguliwa. Msamaha wa dhambi ulikuwa unatolewa kuwa njia ya uombezi Wakristo akiwa patakatifu sana. Bado kulikuwa na mlango "ulio wazi" wa kuingia patakatifu, ambapo Kristo alikuwa anahudumu kwa niaba ya mwenye dhambi Sasa palioenekana mahali pa kuyatumia maneno ya Kristo aliyoyasema katika Ufunuo, ambayo yalikuwa yemelenga wakati huu hasa: "Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye

... Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga." Ufunuo 3:7, 8.

Wale wanaomfuata Yesu katika kazi kubwa ya upatanisho hunufaika na uombezi wake, wakati wale wanaoikataa nuru hiyo hawanufaiki nayo. Wayahudi ambao walikataa kumwamini Yesu kama Mwokozi hawakuweza kupata msamaha kupitia kwake. Yesu alipoingia patakatifu pa mbinguni baada ya kupaa kwake na kuwamwagia wanafunzi wake baraka za uombezi wake, Wayahudi waliachwa katika giza nene wakiendelea kutoa dhabihu na sadaka [269] sisizo na maana. Mlango ambao mwanzoni watu walikuwa wanaingilia ulikuwa hauko wazi tena. Wayahudi walikuwa wamekataa kumtafuta katika njia pekee aliyokuwa anaweza kupatikana, yaani kwa njia ya patakatifu pa mbinguni.

Wayahudi ambao hawakuamini, ni kilelezo cha wale wasiojali na wasioamini miongoni mwa wale wanaojiita Wakristo ambao hawaielewi kazi ya Kuhani wetu Mkuu kwa kujitakia wenyewe. Katika ile huduma ya kilelezo, kuhani mkuu alipokuwa anaingia patakatifu sana, Israeli wote walikuwa wanatakiwa kukusanyika kupazunguka patakatifu na kunyenyekeza nafsi zao mbele za Mungu, ili wapate msamaha wa dhambi na ili wasikatiliwe mbali na kusanyiko. Ni muhimu zaidi katika siku hii halisi ya upatanisho, tuielewe kazi ya Kuhani wetu Mkuu na kuyajua majukumu anayotaka tuyatimize.

Katika siku za Nuhu, ujumbe ulitumwa kutoka mbinguni, na wokovu wao ulikuwa unategemea jinsi walivyouchukulia ujumbe huo. Mwanzo 6:6-9; Waebrania 11:7. Wakati wa Sodoma, watu wote waliteketezwa na moto uliokuwa umetoka mbinguni isipokuwa Lutu na binti zake wawili. Mwanzo 19. Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Kristo. Mwana wa Mungu aliwaambia Wayahudi wasioamini: "Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa." Mathayo 23:38. Ukizitazama siku za mwisho, uwezo huo huo usio na kikomo unasema juu ya wale ambao "hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo." 2 Wathesalonike 2:10, 11. Wanapoyakataa mafundisho ya Neno lake, Mungu humwondoa Roho wake na kuwaacha katika udanganyifu ambao wanaupenda. Lakini Kristo bado anaomba kwa ajili ya mwanadamu, na nuru itatolewa kwa wale wanaoitafuta.

Kupita kwa wakati mwaka 1844 kulifuatiwa na jaribu kubwa kwa wale waliokuwa na imani ya Ujio. Nafuu yao pekee ilikuwa ile nuru iliyoelekeza akili zao katika patakatifu pa mbinguni. Walipokuwa wanangoja na kuomba, waliona kwamba Kuhani wao Mkuu alikuwa ameingia katika kazi nyingine ya huduma. Wakimfuata kwa imani, walioneshwa pia kazi ya mwisho ya kanisa. Waliuelewa zaidi ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili, na walikuwa tayari kupokea na kutoa onyo nyeti la malaika wa tatu wa Ufunuo 14 kwa ulimwengu.

## Sura Ya 25 - Sheria Ya Mungu Haibadiliki [270]

“Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na l\sanduku la agano lake likaonekana ndani ya hekalu lake.” Ufunuo 11:19. Sanduku la agano la Mungu liko patakatifu pa patakatifu, yaani chumba cha pili cha patakatifu. Katika huduma za hema ya duniani, ambazo zilikuwa “mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni” (Waebrania. 8:5), chumba hiki kilifunguliwa katika siku ya upatanisho tu kwa ajili ya kupatakasa patakatifu. Kwa hiyo maneno yanayosema kwamba hekalu la Mungu lilifunguliwa mbinguni na sanduku la agano lake likaonekana, yanaonesha kufunguliwa kwa patakatifu pa patakatifu pa mbinguni mwaka 1844 wakati Kristo anaingia humo kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho. Wale waliomfuata kwa imani Kuhani wao Mkuu alipokuwa anaingia patakatifu sana, waliliona sanduku la agano lake. Kadiri walivyokuwa wakilichunguza suala la patakatifu walilielewa badiliko la huduma ya Mwokozi, na waliona kwamba, sasa alikuwa anahudumu mbele ya sanduku la Mungu.

Sanduku lililokuwa katika hema ya duniani lilikuwa na mbao mbili za mawe ambazo zilikuwa zimeandikwa sheria ya Mungu. Hekalu la Mungu lilipofunguliwa kule mbinguni, sanduku la agano lake lilionekana. Sheria ya Mungu ilikuwa imehifadhiwa patakatifu sana kule mbinguni—sheria ambayo ilitamkwa na Mungu na kuandikwa kwa chanda chake katika mbao za mawe.

Wale waliolielewa jambo hilo waliiona nguvu ya maneno haya ya Mwokozi kuliko wakati mwingine wo wote ule: “Amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka hata yote yatimie.” (Mathayo 5:18). Sheria ya Mungu ambayo ni ufunuo wa mapenzi yake na hati ya tabia yake, itadumu milele.

Amri ya Sabato ipo katikati ya Amri Kumi. Roho wa Mungu aliwaonesha wanafunzi wa Neno lake kwamba walikuwa wameivunja amri hii bila kujua kwa kuipuuza siku ya Mwumbaji ya kupumzika. Walianza kuchunguza sababu za kuadhimisha siku ya kwanza ya

juma. Hawakupata ushahidi wo wote kwamba amri ya nne ilikuwa imefutwa au kwamba Sabato ilikuwa imebadilishwa. Walikuwa wanatafuta kwa dhati kujua na kuyafanya mapenzi ya Mungu; sasa walionesha utii wao kwa Mungu kwa kuishika Sabato yake takatifu.

[271] Juhudi zilizokuwa zinafanyika kuiangusha imani ya waumini Waadventista zilikuwa nyingi. Wote waliona kwamba, kuupokea ukweli juu ya patakatifu pa mbinguni kulikuwa kunajumuisha matakwa na sheria ya Mungu na Sabato ya amri ya nne. Hapa ndipo kulikuwa na siri ya upinzani wa makusudi dhidi ya ufafanuzi linganifu wa Maandiko yaliyokuwa yanaonesha huduma ya Kristo katika patakatifu pa mbinguni. Watu walikuwa wanatafuta kuufunga mlango ambao Mungu alikuwa ameufungua, na kuufiingua ule ambao alikuwa ameufunga. Lakini Kristo alikuwa ameufungua mlango wa huduma ya patakatifu sana. Amri ya nne ilikuwa katika sheria iliyokuwa imehifadhiwa humo.

Wale waliokuwa wameipokea nuru iliyokuwa inahusu uombezi Wakristo na sheria ya Mungu waliona kuwa huu ulikuwa ukweli wa Ufunuo 14, yaani onyo lenye sehemu tatu la kuwaandaa wakazi wa dunia kwa ajili ya Ujio wa Bwana. (Tazama kiambatisho) Tangazo lisemalo, "Saa ya hukumu yake imekuja" linatangaza ukweli ambao unapasa kuhubiriwa mpaka uombezi wa Mwokozi utakapokoma na yeye kurudi kuja kuwachukua watu wake awapeleke kwake. Hukumu ambayo ilianza mwaka 1844 itaelendelea mpaka mashauri ya watu wote, walio hai na waliokufa, yaaamuliwe; kwa hiyo itaendelea mpaka mwisho wa muda wa matazamio wa wanadamu. Ujumbe huu unawaagiza wanadamu kumcha "Mungu na kumtukuza," na kumsujudia "yeye aliyeziumba mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Matokeo ya kuupokea ujumbe huu yanaelezwa: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu." Ufunuo 14:7, 12.

IIi watu wawe tayari kwa ajili ya hukumu, inawapasa kuishika sheria ya Mungu, ambayo ni kipimo cha tabia na kigezo kitakachotumika katika hukumu. Paulo anasema "Kwa kuwa wote waliokosa ... wenye sheria, watahukumiwa kwa sheria." "Ni wale waitendao sheria watakaohesabiwa haki." Imani ni ya lazima katika kuishika sheria ya Mungu; kwani "pasipo imani haiwezekani kumpendeza

Mungu.” “Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi.” Warumi 2:12-16; Waebrania 11:6; Warumi 14:23.

Malaika wa kwanza aliwasihi watu kumcha “Mungu na kumtukuza,” na kumsujudia kama Mwumbaji wa mbingu na nchi. Inawapasa kuishika sheria ya Mungu ili waweze kufanya hivyo. bila utii, hakuna ibada inayoweza kumpendeza Mungu. “Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake.” 1 Yohana 5:3; soma Mithali 28:9. [272]

## Mmwito wa Kumsujudia Mwumbaji

Wajibu wa kumsujudia Mwumbaji unatokana na ukweli kwamba yeye ni Mwumbaji. “Njoni, tuabudu, tusujudu, Tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba.” Soma pia Zaburi 96:5; Zaburi 100:3, Isaya 40:25, 26; Isaya 45:18.

Katika Ufunuo 14 watu wanatakiwa kumsujudia Mwumbaji na kuzishika amri za Mungu. Moja kati ya amri hizi inamwelezea Mungu kuwa ni Mwumbaji: “Lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.” Kutoka 20:10, 11. Bwana anasema, Sabato ni “ishara ... mpate kujua ya kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu.” Ezekieli 20:20.

Kama Sabato ingeshikwa ulimwenguni kote, mwanadamu angeelekezwa kwa Mwumbaji kama mlengwa wa ibada. Kusingekuwa na mtu anayeabudu sanamu, asiyeamini kuwa hakuna Mungu, au mpagani. Kushika Sabato ni ishara ya utii kwake “aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.” Ujumbe unaoagiza wanadamu kumsujudia Mungu na kuzishika amri zake utawataka hasa kuishika amri ya nne.

Tofauti na wale wanaozishika amri za Mungu na imani ya Yesu, malaika wa tatu anaelezea kundi lingine: “Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa

katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu." Ufunuo 14:9, 10. Vinavyowakilishwa na mnyama, sanamu na alama ni vitu gani?

[273] Unabii ulio na vielelezo hivyo unaanzia katika Ufunuo 12. Joka aliyekuwa anataka kumwangamiza Kristo wakati wa kuzaliwa kwake anatajwa kuwa ni Shetani (Ufunuo 12:9); alimchochea Herode kumwua Mwokozi. Lakini wakala wa Shetani katika vita dhidi ya Kristo na watu wake katika kame za mwanzo ilikuwa dola ya Kirumi, ambako upagani ulikuwa ndiyo dini iliyo shamiri. Kwa hiyo, kwa maana nyingine joka ni kielelezo cha Rumi.

Katika Ufunuo 13 kuna mnyama mwingine, "mfano wa chui," ambaye joka alimpa "nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi." Kama vile Waprotestanti wengi wamekuwa wakiamini, kielelezo hiki kinawakilisha mamlaka ya Papa, ambayo ilipokea nguvu na kiti na mamlaka ambayo yalikuwa yanashikiliwa na dola ya Kirumi. Mnyama anayefanana na chui anazungumziwa hivi: "Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru ... Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa." Ufunuo 13:2, 5-7. Unabii huu unaofanana sana na maelezo ya pembe ndogo ya Danieli 7, bila shaka unaelezea mamlaka ya Papa.

"Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili."—ile miaka mitatu na nusu, au siku 1260 za Danieli 7—ambapo mamlaka ya Papa iliwakandamiza watu wa Mungu. Kipindi hiki kilianza mwaka 538 B. K. na kumalizika mwaka 1798. Wakati huo mamlaka ya Papa ilipata "jeraha la mauti," na utabiri usemao "Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa," (Ufunuo 13:10) ukawa umetimia.

### Kuinuka Kwa Mamlaka Nyingine

Hapa kinaanza kuelezewa kielelezo kingine: "Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo." (Ufunuo 13:11). Taifa hili halifanani na yale yaliyotajwa kwa vielelezo vilivyotangulia. Falme kubwa zilizokuwa zimetawala dunia zilikuwa zimeoneshwa kwa nabii Danieli kama wanyama wanaoua na kula wanyama

wengine, zilizoinuka wakati "pepo nne za mbinguni zilipovuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa." (Danieli 7:2). Katika Ufunuo 17:15 malaika mmoja alieleza kuwa maji yanawakilisha "jamaa [274] na makutano na mataifa na lugha." Upepo ni kielelezo cha ghasia. Pepo nne zinazovuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa zinawakilisha matukio ya kutisha ya kuangushana na mapinduzi ambayo falme ziliyatumia kujipatia mamlaka.

Lakini mnyama huyu mwenye pembe kama mwana kondoo alionekana "akipanda juu kutoka katika nchi." Badala ya kuangusha falme zingine ili kujiimarisha, taifa hilo ni lazima litokee katika eneo ambalo halikuwa na wakazi na ilipasa likue kwa amani. Taifa hilo ni lazima litafutwe katika bara la magharibi mwa dunia.

Ni taifa gani katika eneo jipya ambalo lilikuwa likiinuka kwa mamlaka mwaka 1798, likiwa na dalili za uwezo na kutambulika ulimwenguni? Ni taifa moja tu, tena moja tu, linalokidhi vigezo vya unabii huu-— Marekani. Karibu maneno yale yale ya mwandishi wa Maandiko yametumiwa bila kujua na mwanahistoria mmoja akielezea kuinuka kwa taifa hili. Mwandishi mmoja maarufu anazungumzia "*fumbo la kuinuka kwake kutoka mahali patupu*, " na kusema, "Tulimea na kuwa dola kama mbegu imeayo kimya." [227] Jarida moja la mwaka 1850 lilisema kuhusu "kuinuka" kwa Marekani na "katika ukimya wa dunia ikaongezeka katika nguvu na fahari" [228]

"Naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo." Pembe kama za Mwana-Kondoo zinaonesha ujana, kutokuwa na hatia, na upole. Miongoni mwa wahamiaji wa Kikristo waliokimbilia kwanza Marekani, kutokana na ukandamizaji wa wafalme na kukosa uvumilivu kwa makasisi, kulikuwa na wengi waliokuwa wameazimia kuanzisha uhuru wa kiraia na kidini. Tamko la Uhuru [la Marekani] linaelezea ukweli kwamba, "watu wote wameumbwa sawa" na kupewa haki isiyoweza kuondolewa ya kuishi, uhuru, na kutafiita fiiraha." Katiba [ya Marekani] inawahakikishia watu haki ya kujitawala, ikielekeza kuwa wawakilishi waliochaguliwa kwa kura za wengi watatunga na kusimamia sheria. Uhuru wa imani ya kidini pia ulitolewa. Mfumo wa jamhuri na Uprotestanti vikawa

[227] G. A. Townsend, *The New World Compared With the Old*, p. 462.
[228] *Dublin Nation.*

kanuni kuu za kitaifa, siri ya uwezo na mafanikio ya Marekani. Wengi wamekuwa wakitafuta kwenda huko, na Marekani imeinuka na kuwa miongoni mwa mataifa yenye nguvu kabisa duniani.

[275] Lakini lile taifa lenye pembe kama za mwanakondoo lilinena "kama joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona ... akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi." Ufunuo 13:11-14

Pembe kama za mwanakondoo na sauti ya joka vinaonesha ukinzani. Utabiri kwamba atanena "kama joka" na kutumia "nguvu zote za yule mnyama wa kwanza" unaonesha roho ya kutokuvumiliana na mateso ya yule joka na yule mnyama aliye mfano wa chui. Na ule usemi kwamba yule mnyama mwenye pembe mbili "aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza," unaonesha kwamba mamlaka ya taifa hili italazimisha utii kwa mamlaka ya Papa.

Kitendo kama hicho kitakuwa kinakinzana na mfiimo wake wa taasisi huru, Tamko la Uhuru na katiba. Katiba inasema, "Bunge halitatunga sheria inayopendelea taasisi ya kidini, au kuzuia uhuru kwa kidini," na kwamba "hakuna sharti la kidini litakalozingatiwa kama sifa ya kuchaguliwa kushika ofisi yo yote ya serikali iliyo nchini Marekani." Katika kielelezo hiki kumeoneshwa uvunjaji wa makusudi wa mihimili hii ya uhuru. Mnyama mwenye pembe kama za mwana kondoo— ambaye kwa maneno ni msafi, mpole na asiye na madhara—atanena kama joka.

"Akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama.," Hapa imewakilishwa aina ya serikali ambapo mamlaka ya kutunga sheria yamo mikononi mwa watu, ushahidi wa wazi kwamba Marekani ndiyo taifa linalozungumziwa hapa. Lakini, sanamu ya mnyama ni nini? Itaundwa vipi.

Kanisa la mwanzo lilipopotoka, lilitafuta msaada wa mamlaka za kidunia. Matokeo yake ni: mamlaka ya Papa, yaani kanisa lililokuwa linatawala serikali, na hasa katika kuwaadhibu "waasi." Ili Marekani iunde "sanamu ya mnyama," ni lazima mamlaka za kidini zidhibiti utawala wa kiraia kiasi kwamba serikali itatumiwa pia na kanisa kutimiza makusudi ya kanisa.

[276] Makanisa ya Kiprotestanti yaliyofuata nyayo za Kanisa la Roma

yameonesha shauku kama hiyo ya kudhibiti uhuru wa dhamiri. Mfano ni mateso ya muda mrefu yaliyofanywa na Kanisa la Uingereza dhidi ya watu waliojitenga. Katika kame ya kumi na sita na ya kumi na saba, wachungaji na watu waliokuwa hawakubaliani na kanisa walitozwa faini, walifungwa, waliteswa na kuuawa.

Uasi ulilifanya kanisa la awali kutafuta msaada wa serikali ya kiraia, na jambo hilo liliandaa njia kwa ajili ya mamlaka ya Papa—yaani mnyama. Paulo alisema: "Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi." 2 Wathesalonike 2:3.

Biblia inasema: "Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake; hao nao ujiepushe nao." 2 Timotheo 3:1-5. "Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya maShetani." 1 Timotheo 4:1.

Wote ambao "hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa," watapokea "nguvu ya upotevu, wauamini uongo." 2 Wathesalonike 2:10,11. Hali hii itakapofikiwa, athari zile zile zitafuata kama ilivyokuwa katika kame za mwanzo.

Tofauti kubwa ya imani katika makanisa ya Kiprotestanti inachukuliwa kama ushahidi kwamba hakutakuwa na mwafaka wa lazima. Lakini kwa miaka kadhaa kumekuwa na mwelekeo miongoni mwa makanisa ya Kiprotestanti wa kutaka mwungano. Ili kuwa na mwungano wa aina hiyo, mijadala ya mambo ambayo wote walikuwa hawakubaliani itabidi iwekwe kando. Katika juhudi za kufikia mwafaka kamili, itakuwa imebaki kidogo tu kugeukia matumizi ya nguvu.

Makanisa makubwa ya Marekani, yakiwa yameungana katika [277]
masuala ya mafundisho yanayoshikwa na wote, yatakapoishawishi serikali kulazimisha imani zao na kuunga mkono taasisi zao, Marekani ya Kiprotestanti itakuwa imeunda sanamu ya utawala wa

Kanisa la Roma, na taabu ya adhabu za kiserikali kwa wanaopinga itafuata bila shaka.

## Mnyama na Sanamu Yake

Yule mnyama mwenye pembe mbili "awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake." Ufunuo 13:16, 17. Malaika wa tatu anatoa onyo: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu."

"Mnyama" ambaye watu wanalazimishwa kumwabudu ni yule wa kwanza, au aliye mfano wa chui, yaani mnyama wa Ufunuo 13— mamlaka ya Papa. "Sanamu ya mnyama" inawakilisha ile aina ya uprotestanti ulioasi ambao utatokea makanisa ya Kiprotestanti yatakapotafuta msaada wa nguvu za dola kulazimisha kanuni zao. "Alama ya mnyama" bado inahitaji kufafanuliwa.

Wale wazishikao sheria ya Mungu wako kinyume na wale wanaomsujudia mnyama na sanamu yake na kupokea alama yake. Ushikaji wa sheria ya Mungu kwa upande mmoja na uvunjaji wa sheria hiyo kwa upande mwingine, utaweka tofauti kati ya wanaomsujudia Mungu na wale wanaomsujudia mnyama.

Sifa bainifu ya mnyama na sanamu yake ni uvunjaji wa amri za Mungu. Danieli anasema hivi juu ya pembe ndogo, yaani mamlaka ya Papa: "Naye ataazimu kubadili majira na sheria." Danieli 7:25. Paulo aliita mamlaka hiyo "mtu wa kuasi" (2 Wathesalonike 2:3), ambaye angejiinua nafsi yake juu ya Mungu. Mamlaka ya Papa
[278] ingeweza kujiinua nafsi yake juu ya Mungu kwa kubadili sheria ya Mungu tu. Kila atakayeishika sheria iliyobadilishwa hivyo huku akijua, atakuwa anatoa heshima kubwa mamlaka ya Papa, jambo ambalo ni ishara ya utii kwa Papa, badala ya Mungu.

Mamlaka ya Papa ilijaribu kubadili sheria ya Mungu. Amri ya nne imebadilishwa ili kuruhusu uadhimishaji wa siku ya kwanza badala ya Sabato ya siku ya saba. Badiliko la makusudi linaelezewa hapa: "Naye ataazimu kubadili majira na sheria." Badiliko la amri

ya nne linatimiza unabii huu kwa usahihi kabisa. Hapa, mamlaka ya Papa inajiweka juu ya Mungu waziwazi kabisa.

Wanaomwabudu Mungu watajulikana kwa namna wanavyoichukulia amri ya nne ambayo ni ishara ya uwezo wake wa kuumba. Wale wanaomwabudu mnyama watajulikana kwa juhudi zao za kuikanyaga kumbukumbu ya Mwumbaji na kutukuza jambo lililoanzishwa na Kanisa la Roma. Mamlaka ya Papa ilijigamba kwa mara ya kwanza kuhusu suala la Jumapili kuwa "siku ya Bwana." (Angalia kiambatisho.) Lakini Biblia inaeleza kuwa siku ya saba ndiyo siku ya Bwana. Kristo alisema: "Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato pia." Marko 2:28. Soma pia Isaya 58:13: Mathayo 5:17-19. Hoja inayotolewa kuWakristo alibadili Sabato inakanushwa na maneno yake mwenyewe.

### Ukimya Mkubwa wa Agano Jipya

Waprotestanti wanakiri kuwa kuna "ukimya mkubwa wa Agano Jipya kuhusu agizo la "Sabato" [Jumapili, yaani siku ya kwanza ya juma] au sheria zo zote kwa ajili ya kuiadhimisha." [229]

"Hadi wakati kifo cha Yesu, kulikuwa hakuna badiliko Io lote juu ya siku hiyo"; na "kulingana na kumbukumbu zilizoandikwa, mitume hawakuwahi ... kutoa agizo lo lote linalohusu kuiacha Sabato ya siku ya saba, na kuiadhimisha katika siku ya kwanza ya juma." [230]

Wakatoliki wanakiri kwamba badiliko la Sabato lilifanywa [279]
na kanisa lao, na wanasema kwamba Waprotestanti, wanaitambua mamlaka ya Kanisa Katoliki kwa kuiadhimisha siku hiyo. Wanasema hivi: "Wakati wa sheria ya zamani, Jumamosi ilikuwa siku iliyotakaswa; lakini Kanisa, kwa kuagizwa na Yesu Kristu, na kuelekezwa na Roho wa Mungu, limeweka Jumapili badala ya Jumamosi; kwa hiyo sasa tunaitakasa siku ya kwanza, na siyo siku ya saba. Jumapili inamaanisha siku ya Bwana, na sasa ni siku ya Bwana." [231]

Waandishi wa Kikatoliki hulielezea badiliko hilo kama ishara ya mamlaka ya Kanisa Katoliki, wakisema, "kitendo cha kuibadili

[229] .

[230] A. E. Waffle, *The Lord's Day* , pp. 186-188.

[231] *Catholic Catechism of Christian Religion.*

Sabato kwenda Jumapili, jambo ambalo Waprotestanti wanaliafiki; ... kwani kwa kushika Jumapili, wanakiri uwezo wa Kanisa kuweka sikukuu, na kuamuru zishikwe chini ya dhambi.” [232]

Sasa badiliko la Sabato ni nini? Kama siyo ishara au alama ya mamlaka ya Kanisa la Rumi—“alama ya mnyama?” Kanisa la Roma halijakanusha madai yake ya ukuu. Ulimwengu pamoja na makanisa ya Kiprotestanti wanapoafiki sabato iliyowekwa na kanisa hilo, huku wakiikataa Sabato ya Biblia, kimsingi wanakubaliana na madai hayo. Kwa kufanya hivyo wanaipuuza kanuni ambayo inawatofautisha na Kanisa la Roma— isemayo, “Biblia, Biblia pekee ndiyo dini ya Waprotestanti.” Kadiri harakati za kulazimisha ushikaji wa Jumapili zinavyozidi kukubalika, hatimaye zitauweka ulimwengu wote wa Kiprotestanti chini ya bendera ya Kanisa la Roma.

Wakatoliki wanadai kuwa “uadhimishaji wa Jumapili kwa upande wa Waprotestanti ni heshima kubwa wanayoitoa, kwa mamlaka ya kanisa [Katoliki], kinyume cha msimamo wao wenyewe.” [233]

Kulazimisha wajibu wa kidini kwa kutumia nguvu za dola kutaunda sanamu ya mnyama; hivyo kulazimisha ushikaji wa Jumapili nchini Marekani kutakuwa ni kulazimisha kumsujudia mnyama na sanamu yake.

[280] Wakristo wa vizazi vilivyopita walikuwa wanashika Jumapili wakidhani kuwa walikuwa wanashika Sabato ya Biblia, na hata sasa kuna Wakristo wa kweli katika kila kanisa wanaoamini kwa dhati kwamba Jumapili ni siku iliyochaguliwa na Mungu. Mungu anaukubali uaminifu na unyofu wao. Lakini ushikaji wa Jumapili utakapolazimishwa kisheria na ulimwengu utakapokuwa umepata nuru juu ya Sabato ya kweli, ye yote atakayeivunja amri ya Mungu na kutii sheria ya Kanisa la Roma, atakuwa ameiheshimu mamlaka ya Papa kuliko Mungu. Atakuwa anatoa heshima kwa Kanisa la Roma. Atakuwa anamsujudia mnyama na sanamu yake. Wakati huo watu watapokea alama ya utii kwa Kanisa la Roma—yaani “alama ya mnyama.” Haitakuwa hivyo mpaka suala hili liwekwe wazi mbele ya watu na wafike mahali pa kuchagua kati ya amri za Mungu na

[232] Henry Tuberville, *An Abridgement of the Christian Doctrine,* p. 58.
[233] Mgr. Segur, *Plain Talk About the Protestantism of Today*, p. 213.

amri za wanadamu, ndipo wale wanaoendelea katika uasi watapokea "alama ya mnyama."

### Onyo la Malaika wa Tatu

Onyo la kutisha kuliko yote yaliyowahi kutolewa kwa wanadamu lipo katika ujumbe wa malaika wa tatu. Haipasi watu waachwe gizani juu ya suala hili muhimu; onyo hili halina budi kutolewa kwa ulimwengu kabla ya mapigo ya hukumu Mungu, ili wanadamu wote wawe na fursa ya kuyaepuka. Malaika wa kwanza anatangazia "kila taifa na kabila na lugha na jamaa." (Ufunuo 14:6). Onyo la malaika wa tatu litaenea vivyo hivyo. Litatangazwa kwa sauti kuu na litavuta usikivu wa ulimwengu mzima.

Watu wote watagawanyika katika makundi mawili makubwa—wale wazishikao amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu, na wale wanaomsujudia mnyama na sanamu yake na kupokea alama yake. Kanisa na serikali vitaungana kuwalazimisha watu "wote" kupokea "alama ya manyama," lakini watu wa Mungu hawataipokea. Nabii Yohana aliwaona wale "wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kando-kando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu." Ufunuo

[281] # Sura Ya 26 - Watetezi Wa Ukweli

Matengenezo ya Sabato katika siku za mwisho yalitabiriwa katika kitabu cha Isaya: "Bwana asema hivi, Shikeni hukumu, mkatende haki; kwa maana wokovu wangu u karibu kuja, na haki yangu kufunuliwa. Heri afanyaye haya, na mwanadamu ayashikaye sana; azishikaye Sato asizivunje, auzuiaye mkono wake usifanye uovu wo wote...Na wageni, walioandamana na Bwana ili wamhudumu, na kulipenda jina la Bwana, kuwa watumishi wake; kila aishikaye Sabato asiivunje, na kulishika sana agano langu; Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala; makafara yao na dhabihu zao zitakubaliwa juu ya madhabahu zangu; kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote." Isaya 56:1, 2, 6,7.

Utendaji wa maneno haya upo katika zama za Ukristo kama inavyooneshwa kwenye muktadha (soma fungu la 8). Hapa umetabiriwa mkusanyiko wa mataifa kwa ajili ya Injili, wakati watumishi wa Mungu wanapohubiri habari ya furaha kwa kila taifa.

Bwana aliamuru, "...ukaitie muhuri sheria kati ya wanafunzi wangu." Muhuri wa Mungu unapatikana kwenye amri ya Nne. Amri hii pekee, kati ya kumi, huonesha jina na cheo cha Mtoa sheria. Wakati Sabato ilipobadilishwa na mamlaka ya Papa, muhuri ulitolewakutoka kwenye sheria. Wanafunzi wa Yesu wanaitwa kuurejesha muhuri kwa njia ya kuiinua Sabato kama kumbukumbu ya Mwumbaji na alama ya mamlaka yake.

Amri imetolewa: "Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu wangu kosa lao." Wale ambao Mungu anawaita, "Watu wangu" watashutumiwa kwa ajili ya dhambi zao, na daraja la watu wanaojidhania kuwa ni wenye haki katika kumtumikia Mungu. Karipio hili zito la Yule anayeichunguza mioyo ni uthibitisho kuwa wanaoyakanyaga maagizo ya Mungu. Isaya 58:1, 2.

[282] Kwa hiyo nabii anaionesha sheria iliyoachwa: "utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali

palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia. Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika Bwana." Isaya 58:12-14.

Mahali "palipobomoka" katika sheria ya Mungu ni badiliko la Sabato lililofanywa na mamlaka ya Kirumi. Lakini muda umefika wa kutengeneza mahali palipobomoka.

Sabato ilikuwa inashikwa na Adamu alipokuwa hana hatia pale Edeni; Adamu alikuwa anaishika baada ya anguko, akiwa ametubu baada ya kufukuzwa kutoka kwenye shamba lake. Ilikuwa inashikwa na wazee wote kuanzia Habili hadi Nuhu, hadi Ibrahimu, hadi Yakobo. Alipokuwa amewakomboa wana wa Israeli, Mungu aliitangaza sheria yake kwenye makutano.

## Sabato ya Kweli Imekuwa IkishikwaDaima

Tangu siku ile hadi sasa Sabato imekuwa ikishikwa. Ingawa yule "mtu wa kuasi" alifaulu kuikanyaga siku takatifu ya Mungu chini ya miguu yake, lakini katika sehemu za siri walikuwa wamejificha watu waaminifu waliokuwa wanaiheshimu. Tangu nyakati za matengenezo, baadhi katika kila kizazi wamedumisha utunzaji wake.

Ukweli huu kuhusiana na "lnjili ya milele" utalitofautisha kanisa la Kristo wakati wa atakapotokea. "Hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:12.

Wale walioipokea nuru juu ya Patakatifu na sheria ya Mungu walijazwa na furaha walipoona upatanifu katika ukweli. Walitamani ile nuru wapewe Wakristo wote. Lakini ukweli uliokuwa unahitilafiana na ulimwengu haukukubaliwa na wengi waliodai kumfuata Kristo.

Madai ya Sabato yalipokuwa yanatolewa, wengi walisema: "Wakati wote tumekuwa tunaishika Jumapili, baba zetu walikuwa wanaishika, na watu wengi wazuri kwa furaha walikufa wakiwa wanaishika. Kushika Sabato mpya kutatufanya tutengwe na ulimwengu. Ni kitu gani ambacho kikundi kidogo cha watu [283]

wanaoshika Sabato ya siku ya saba kitafanikisha dhidi ya ulimwengu wote unaotunza Jumapili? Kwa kutumia hoja zinazolingana na hii, ndivyo Wayahudi walivyohalalisha tendo la kumkataa Yesu. Vivyo hivyo wakati wa Luther, Wakatoliki walikuwa wanatoa sababu kuwa Wakristo wa kweli walikufa wakiwa katika imani ya Kikatoliki; kwa hiyo imani hiyo inatosha. Hoja kama hizi zilikuwa kikwazo kwa maendeleo ya imani.

Wengi walitoa hoja kwamba kushika Jumapili ilikuwa ni desturi ya kanisa kwa kame nyingi. Hoja kinyume na hiyo ilionesha kuwa Sabato na ushikaji wake ilikuwa ya kale zaidi, ikiwa na umri sawa na dunia na ilianzishwa na Mzee wa Siku.

Wakiwa hawana ushuhuda wa Biblia, wengi walitoa hoja kuwa, "Kwa nini watu wetu wakuu hawalielewi suala hili la Sabato? Ni wachache tu wanaoamini kama ninyi. Haiwezekani ninyi mwe sahihi na wasomi wote wawe wamekosea."

Ili kuzipinga hoja hizo ilikuwa ni lazima kutoa nukuu za Maandiko na kuyaelezea matendo ya Mungu kwa watu wake katika zama zote. Sababu inayomfanya Mungu mara nyingi asiwachague wasomi na kuwafanya viongozi wa matengenezo ni kuwa wanazitumainia kanuni zao za imani na mifumo ya kiteolojia, na kuona kuwa hawana hitaji la kufundishwa na Mungu. Watu wenye elimu kidogo ya shuleni wakati mwingine huitwa ili wautangaze ukweli, siyo kwa sababu hawana elimu, lakini kwa sababu wanajitambua kuwa hawajitoshelezi na wako tayari kufundishwa na Bwana. Unyenyekevu na utii wao unawafanya wafae.

Historia ya wana wa Israeli ni kielelezo kizuri cha uzoefu uliopita wa jamii ya Waadventista. Mungu aliwaongoza watu wake kwenye vuguvugu la Ujio, kama alivyowaongoza wana wa Israeli kutoka Misri. Endapo watu wote walioshughulika kwa umoja katika kazi ya mwaka 1844 wangeupokea ujumbe wa malaika yule wa tatu na kuutangaza kwa nguvu ya Roho Mtakatifu; miaka mingi iliyopita dunia ingekuwa imekwisha kuonywa na Kristo angekuwa amekuja kuwakomboa watu wake.

[284] **Siyo Mapenzi ya Mungu**

Haukuwa mpango wa Mungu kwamba Waisraeli wazunguke jangwani kwa miaka arobaini; alitamani kuwaongoza moja kwa

moja hadi Kanaani na kuwafanya taifa takatifu, watu wenye furaha. Lakini, "hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao." Waebrania 3:19. Kwa namna hiyo hiyo, hayakuwa mapenzi ya Mungu kwamba kuja kwa Kristo kuchelewe na watu wake wakae kwa miaka mingi katika ulimwengu huu wa dhambi na huzuni. Kutokuamini kuliwatenganisha na Mungu. Ni kwa sababu ya rehema kwa ulimwengu, Yesu anakawia kuja ili wenye dhambi wasikie onyo na kutafuta kimbilio kabla ya kumwagwa kwa ghadhabu ya Mungu.

Wakati huu, kama ilivyokuwa nyakati za zamani, kuuhubiri ukweli kutachochea upinzani. Wengi wakiwa na kijicho watashambulia tabia na nia za wale wanaosimama kuutetea ukweli usiopendwa. Eliya aliambiwa kuwa ni mtaabishaji wa Israeli, Yeremia aliitwa msaliti, na Paulo mwenye kulinajisi hekalu. Tangu siku zile hadi sasa, wale ambao ni waaminifu kwenye ukweli wamekuwa wakishutumiwa kuwa ni wachochezi, waasi, na wenye kuleta mafarakano.

Maungamo ya imani yaliyofanywa na watakatifu na wafla dini, vile vielelezo vya utakatifu na uadilifu usiobadilika, huamsha ujasiri kwa wale ambao sasa wanaitwa kusimama kama mashahidi wa Mungu. Kwa mtumishi wa Mungu kwa wakati huu amri inasema, "Piga kelele, usiache, paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao." "Nimekuweka kuwa mlinzi kwa nyumba ya Israeli; basi ulisikie neno hili kinywani mwangu, ukawape maonyo yangu." Isaya 58:1; Ezekieli 33:7.

Kipingamizi kikubwa cha ukweli kukubalika ni usumbufu na shutuma zinazoambatana nao. Hii ndiyo hoja pekee dhidi ya ukweli ambayo watetezi wake hawakuweza kuishinda. Lakini wafuasi wa kweli Wakristo hawasubiri hadi ukweli upendwe na watu wengi. Wanaukubali msalaba, pamoja na Paulo wakihesabu kuwa, "dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana"; pamoja yule wa zamani aliyekuwa, "akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri." 2 Wakorintho 4:17; Waebrania 11:26.

Inatupasakuuchagua ukweli kwa sababu ni ukweli na kumwachia [285]
Mungu matokeo yote. Watu wanaofuata kanuni, wenye imani, na wanaothubutu wana wajibu juu ya matengenezo katika ulimwengu.

Kupitia watu hawa kazi ya matengenezo kwa wakati huu ni lazima isukumwe mbele.

# Sura Ya 27 - Uamsho Wa Kisasa Umefanikiwa Kwa Kiasi Gani? [286]

Mahali popote lilipohubiriwa Neno la Mungu kwa uaminifu matokeo yaliyofuatia yalithibitisha kuwa chanzo chake ni Mungu. Wenye dhambi waliyaona matokeo yake haraka. Hatia kuu ilizishika akili na mioyo yao. Walikuwa na ufahamu wa haki ya Mungu, na walilia, "Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?" Warumi 7:24. Kadiri msalaba ulivyofunuliwa, waliona kuwa ni kafara ya Kristo pekee ambayo ingewapatanisha kutokana na uasi wao. Kupitia damu ya Yesu walipata, "kuziachilia katika ustahimili wa MUNGU dhambi zote zilizotangulia kufanywa." Warumi 3:25.

Watu hawa Waliamini na walibatizwa na wakasimama wakitembea kwenye upya wa uzima, kwa njia ya imani ya Mwana wa Mungu, kufuata nyayo zake, kuakisi tabia yake, na kujitakasa wenyewe kama na Yeye alivyo msafi. Mambo ambayo wakati fulani waliyachukia, sasa waliyapenda; na yale waliyoyapenda mwanzo, waliyachukia. Wenye majivuno wakawa wapole, wasiofaa na wenye kiburi wakawa makini na wasio na kimbelembele. Walevi wakawa watulivu, waasherati wakawa safi. Wakristo hawakutafuta, "kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi, bali... katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu." IPetro 3:3, 4.

Uamsho ulikuwa na kawaida ya kutoa mwito mzito kwa wenye dhambi. Matokeo yalionekana katika mioyo ambayo haikunywea katika kujikana nafsi bali walifurahi kwa sababu walionekana wanastahili kuteseka kwa ajili ya Kristo. Wanadamu waliyaona mabadiliko ndani ya wale waliolikiri jina la Yesu. Hayo ndiyo matokeo ambayo miaka ya zamani yaliambatana na uamsho wa kidini.

Lakini nafasi nyingi za uamsho siku hizi zinaonesha kinyume chake. Ni kweli kwamba wengi wanakiri kuongoka na kuna idadi kubwa ya watu wanaoongezeka makanisani. Pamoja na hayo matokeo, hayo si hakikisho kuwa kuna ukuaji katika maisha ya kiroho

unaoambatana na ongezeko. Nuru inayong'aa kwa muda ghafla inazimika.

[287] Uamsho unaopendwa mara nyingi huchochea msisimko na kuamsha tamaa ya kufahamu mambo mapya na yale yenye utata. Waongofu wanaopatikana kwa njia hii wanayo shauku kidogo ya kusikiliza ukweli wa Biblia. Wanavutwa na huduma ya kidini yenye kitu fulani kinachosisimua.

Kwa kila moyo ulioongoka kweli kweli, uhusiano wake na Mungu na mambo ya milele litakuwa ndilo somo kuu la maisha. Iko wapi ile roho ya kujitoa wakfu kwa Mungu katika makanisa maarufu ya siku hizi? Waongofu hawaachi majivuno na kuupenda ulimwengu. Hawako tayari tena kujikana nafsi na kumfuata Yesu aliye mpole na mnyenyekevu kama ilivyokuwa wakati wa kuongoka kwao. Utauwa umeondoka kwenye makanisa mengi.

Pamoja na kutetereka kwa imani kulikoenea, wako wafuasi wa kweli Wakristo kwenye makanisa haya. Kabla ya kujiliwa na hukumu ya mwisho ya Mungu, kutakuwa na uamsho wa utauwa wa zamani miongoni mwa watu wa Bwana ambao haujashuhudiwa tangu wakati wa mitume. Roho wa Mungu atamwagwa. Wengi watajitenga kutoka kwenye makanisa ambayo kuupenda ulimwengu kumechukua nafasi ya upendo wa Mungu na Neno lake. Wachungaji wengi na watu wataukubali kwa furaha ule ukweli unaowaandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Bwana.

Adui wa roho anatamani kuizuia kazi hii, na kabla ya wakati wa harakati hizi kufika, atajitahidi kuzizuia kwa kuleta uamsho bandia. Ndani ya yale makanisa ambayo ataweza kuyaweka chini ya udhibiti wake, atafanya ionekane kuwa baraka ya pekee ya Mungu imemwagwa. Watu wengi watashangilia na kusema, "Mungu anafanya kazi ya kushangaza," kumbe kazi ni ile ya roho mwingine. Kwa kutumia mfumo wa kidini, Shetani atajitahidi kuenezamvuto wake kwenye ulimwengu wa Kikristo. Kutakuwa na msisimko wa kihisia, kuchanganya ukweli na uongo, ambao utakuwa umeandaliwa vizuri ili kupotosha.

Hata hivyo katika nuru ya Neno la Mungu si vigumu kutambua asili ya harakati hizo. Wakati wowote watu watakapoupuuza ushuhuda wa Biblia, kugeukia mbali na ukweli huu ulio wazi, ukweli unaoupima moyo na unaowataka kujikana nafsi na kuukana ulimwengu; hapo tutakuwa na uhakika kwamba baraka ya Mungu

haijatolewa. Na kwa kanuni isemavyo, "Mtawatambua kwa matunda yao." (Mathayo 7:12) ni ushahidi kwamba harakati hizi siyo kazi ya Roho wa Mungu.

Ukweli wa Neno la Mungu ni ngao dhidi ya udanganyifu wa [288]
Shetani. Kuupuuzia ukweli huu umefungua mlango kwa maovu yaliyoenea sasa ulimwenguni. Kwa sehemu kubwa, umuhimu wa sheria ya Mungu hauonekani. Dhana potovu ya sheria ya Mungu imesababisha makosa kwenye uongofu na utakaso, ikishusha kiwango cha uchaji wa Mungu. Hapa ndipo inapopatikana siri ya ukosefu wa Roho wa Mungu kwenye uamsho wa siku zetu.

## Sheria ya Uhuru

Walimu wengi wa kidini wanadai kuwa kwa kifo chake, Yesu aliiondoa kabisa sheria. Baadhi wanaiwakilisha kama ni nira yenye maumivu makali na kinyume na "utumwa" wa sheria wanasisitiza "uhuru" upatikanao kwenye lnjili.

Lakini sivyo manabii na mitume walivyoichukulia sheria ya Mungu. Daudi anasema, "Nami nitakwenda panapo nafasi, Kwa kuwa nimejifunza mausia yako." Zaburi 119:45. Mtume Yakobo anarejea kwenye Amri Kumi za Mungu anaposema, "sheria kamilifu iliyo ya uhuru." Yakobo 1:25. Mwandishi wa kitabu cha Ufunuo anatamka baraka kwa wale wazifuao nguo zao, "wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima." Ufunuo 22:14.

Kungekuwa na uwezekano wa kuibadilisha sheria au kuiweka kando, Kristo hangekufa ili kumwokoa mwanadamu kutoka kwenye adhabu ya dhambi. Mwana wa Mungu alikuja, "kuitukuza sheria, na kuiadhimisha." Isaya 42:21. Anasema, "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati." "Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaoondoka" Kumhusu Yeye Mwenyewe anasema, "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu." Mathayo 5:17,18; Zaburi 40:8.

Sheria ya Mungu haibadiliki, ni ufunuo wa tabia ya mtunga sheria. Mungu ni upendo na sheria ni upendo. "Pendo ndilo utimilifu wa sheria." Mwandishi wa Zaburi anasema: "sheria yako ni kweli"; "Maana maagizo yako yote ni ya haki." Paulo anatamka kuwa, "torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema." Warumi [289]

13:10; Zaburi 119:142, 172; Warumi 7:12. Sheria ya namna hiyo yapaswa kuwa yenye uvumilivu kama alivyo mtunzi wake.

Ni kazi ya uongofu na utakaso kuwapatanisha wanadamu na Mungu kwa kuwaleta kwenye muafaka na kanuni za sheria yake. Hapo mwanzo mwanadamu alikuwa na mapatano kamili na sheria ya Mungu. Lakini dhambi ilimtenganisha kutoka kwa Muumba wake. Moyo wake ulikuwa unapingana na sheria ya Mungu. "ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii." Lakini, "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee" ili mwanadamu apatanishwe na Mungu, arejeshwe kwenye mapatano na Muumba wake. Badiliko hili ni kuzaliwa upya, ambalo bila hilo "hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Yohana 3:16, 3.

## Hatia ya Dhambi

Hatua ya kwanza ya upatanisho na Mungu ni kugundua hatia ya dhambi. "Dhambi ni uasi wa sheria" "kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria." lYohana3:4. Warumi 3:20. Ili kugundua hatia, mwenye dhambi ni lazima aijaribu tabia yake kwa kutumia kioo cha Mungu kinachoonesha ukamilifu wa tabia ya haki na kumwezesha kuyaona mapungufu yake mwenyewe.

Sheria humfunulia mwanadamu dhambi yake lakini haitoi suluhisho. Inatangaza kuwa mauti ni fungu la mwenye dhambi. Ni Injili ya Kristo pekee iwezayo kumweka huru dhidi ya hukumu au unajisi wa dhambi. Ni lazima afanye toba kwa Mungu, ambaye sheria yake imevunjwa, na amwamini Yesu ambaye ndiye kafara yake ya upatanisho. Ndipo atapata, "kuziachilia katika ustahimili wa MUNGU dhambi zote zilizotangulia kufanywa." Warumi 3:25. Na anakuwa mtoto wa Mungu.

Je, sasa yupo huru kuivunja sheria ya Mungu? Paulo anasema: "Basi, je! twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! Kinyume cha hayo twaithibitisha sheria." "Hasha! Sisi tulioifla dhambi tutaishije tena katika dhambi?" Yohana anatamka kwamba: "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito." Katika kuzaliwa upya, moyo unaletwa kwenye upatanifu na Mungu, kwenye muafaka na sheria yake. Badiliko
[290] hili likitokea ndani ya mwenye dhambi, anakuwa ametoka kwenye

mauti na kwenda kwenye uzima, kutoka kwenye dhambi na uasi kwenda kwenye utii na uaminifu. Maisha ya zamani yamekoma; maisha mapya ya upatanisho, imani,na upendo yameanza. Ndipo, "maagizo ya torati" yatatimizwa ndani yetu sisi, tunaoenenda sio kwa kuufuata mwili, bali roho. Lugha ya moyo itakuwa: "Sheria yako naipenda mno ajabu, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa." Warumi 3:31; Warumi 6:2; lYohana 5:3; Warumi 8:4; Zaburi 119:97.

Pasipo sheria wanadamu hawawezi kuwa na hatia ya kweli ya dhambi na hawatahitaji toba. Hawatambui hitaji lao la damu ya Kristo inayofanya upatanisho. Tumaini la wokovu limekubaliwa pasipo badiliko la dhati la moyo ama matengenezo ya maisha. Hivyo kuna uongofu wa juu juu na idadi ni kubwa, watu wengi wanaojiunga na kanisa ambao bado hawajajiunga na Kristo..

## Utakaso ni Nini?

Nadharia zenye makosa za utakaso zinatokana pia na kuiacha sheria ya Mungu. Nadharia hizi ambazo, zina mafundisho ya uongo na matokeo hatari ya utendaji wake, kwa ujumla ndizo zinazopendwa.

Paulo anatangaza: "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu." Biblia kwa uwazi inafundisha maana ya utakaso na namna ya kuupata. Mwokozi aliwaombea wanafunzi wake: "Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli." Na Paulo anafundisha kwamba wauamini wanatakiwa, "kutakaswa na Roho Mtakatifu." 1 Wathesalonike 4:3; Yohana 17:17; Warumi 15:16.

Kazi ya Roho Mtakatifu ni nini? Yesu aliwaambia wanafunzi wake: "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote." Yohana 16:13. Na mtunga Zaburi anasema: "sheria yako ndiyo kweli" Kwa sababu, "sheria ya Mungu ni takatifu na ya haki na njema" tabia itakayojengwa kwa njia ya utii wa sheria hiyo itakuwa takatifu. Kristo ni kielelezo kamili cha tabia hiyo. Anasema nimezishika "amri za Baba yangu" "Nafanya siku zote yale yampendezayo." Yohana 15:10; 8:29. Inawapasa wafuasi Wakristo wawe kama Yeye - kwa neema ya Mungu watengeneze tabia zinazopatana na kanuni za sheria yake takatifu. Huu ndio utakaso wa Biblia.

[291]

## Ni Kwa Njia ya Imani Pekee

Kazi hii inaweza kukamilishwa tu kwa njia ya imani katika Kristo, kwa uwezo wa Roho wa Mungu aliye ndani yetu. Mkristo atahisi misukumo ya kutenda dhambi, lakini atadumisha vita visivyokoma dhidi yake. Yupo mahali ambapo msaada Wakristo unahitajika. Udhaifu wa kibinadamu unaunganishwa na uwezo wa Mungu, na imani inatamka kwa mshangao kwamba: "Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo."l Wakorintho 15:57.

Kazi ya utakaso ni endelevu. Katika uongofu, mwenye dhambi anapata amani kati yake na Mungu, ndipo maisha ya Ukristo yanakuwa yameanza. Sasa anatakiwa auendee "utimilifu" kukua "hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu Wakristo" "nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mmwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu." Waebrania 6:1; Waefeso 4:13; Wafilipi 3:14.

Wale wanaopitia uzoefu wa utakaso wataonesha unyenyekevu. Wanaona kutostahili kwao wakijilinganisha na ukamilifu wa Yeye asiye na ukomo. Nabii Danieli alikuwa kielelezo cha utakaso wa kweli. Badala ya kudai kwamba alikuwa safi na mtakatifu, huyo nabii aliyeheshimiwa, alijiweka kundi moja na Waebrania wenye dhambi pale alipomlilia Mungu kwa niaba ya watu wake. Danieli 9:15,18,20; 10:8, 11.

Kwa wale wanaotembea katika kivuli cha msalaba wa Kalvari, hapatakuwa na kujiinua nafsi, wala kudai kwa majivuno, kwamba wapo huru dhidi ya dhambi. Wanahisi kwamba ni dhambi yao iliyosababisha maumivu makali, yaliyouvunja moyo wa Mwana wa Mungu, na wazo hili litawaongoza katika kujishusha. Wale wanaoishi karibu na Yesu, wanatambua kwa uwazi kabisa udhaifu na hali ya dhambi ya mwanadamu, tumaini lao pekee ni kafara ya Mwokozi aliYesulibiwa akafufuka.

Utakaso unaopata umaarufu sasa katika ulimwengu wa kidini unabeba roho ya kujiinua nafsi na kuidharau sheria ya Mungu hata kuiona kama kitu kigeni ndani ya Biblia. Watetezi wake wanafundisha kuwa utakaso ni tukio au kazi ya mara moja, ambapo, kwa njia ya "imani pekee" wanapata utakatifu kamili. Wanasema kuwa
[292] "Amini tu" na " na baraka itakuwa yako" Anayepokea utakaso huo

haimpasi kuwa na juhudi za ziada. Sambamba na hilo wanaokataa mamlaka ya sheria ya Mungu, wakitoa hoja kwamba wako huru dhidi ya wajibu wa kutunza amri. Lakini je, inawezekana kuwa mtakatifu pasipo kufikia mapatano na kanuni zinazofunua tabia na mapenzi ya Mungu?

Ushuhuda wa Neno la Mungu uko kinyume na fundisho hili lenye mtego la imani bila matendo. Si imani inayotupatia kibali mbinguni pasipo kutimiza masharti ambayo kwayo rehema itatolewa. Ni jambo la kudhaniwa tu. (soma Yakobo 2:14-24).

Hebu pasiwepo watu watakaojidanganya kwamba wanaweza kuwa watakatifu wakiendelea kuvunja kwa makusudi moja ya matakwa ya Mungu. Dhambi inayofahamika hunyamazisha sauti ya Roho inayoshuhudia na huitenganisha nafsi na Mungu. Ingawa Injili na nyaraka za Yohana zimejikita kikamilifu kwenye mada ya upendo; hajasita kuifunua tabia halisi ya daraja la watu wanaodai kuwa wametakaswa huku wakiendelea kuishi maisha ya uasi dhidi ya sheria ya Mungu.

"Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli." 1Yohana 2:4, 5. Hapa kipo kipimo kwa kila mtu anayemkiri Yesu. Kama wanadamu watapunguza umuhimu na kuondoa uzito katika maagizo ya Mungu, ikiwa mtu ye yote atavunja, "amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo" (Mathayo 5:18, 19) tutaweza kujua kuwa madai yao hayana msingi.

Madai ya kutokuwa na dhambi ni uthibitisho kuwa yeye atoaye madai hayo yu mbali na utakatifu. Hana ufahamu wa kweli juu ya usafi usio na mwisho na utakatifu wa Mungu, na ubaya na uovu wa dhambi. Kadiri anavyokuwa mbali na Yesu, ndivyo anavyozidi kujiona mwenye haki machoni pake.

## Utakaso Unaotajwa Kwenye Biblia

Utakaso unapaswa kuwa kamili unaojumuisha roho, nafsi, na mwili. (Angalia, 1 Wathesalonike 5:23). Wakristo wanatakiwa kuitoa miili yao, "iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu" Warumi 12:1. Kila tendo linalodhoofisha nguvu za mwili au za akili linamwondolea mwanadamu sifa za kumhudumia Mwum- [293]

baji wake. Wale wanaompenda Mungu kwa moyo wote watadumu kujitahidi kuweka kila nguvu waliyonayo ipatane na sheria zinazowapa uwezo wa kufanya mapenzi yake. Hawatadhoofisha ama kuinajisi sadaka wanayoitoa kwa Baba yao wa mbinguni; kwa kuendekeza uchu na tamaa za mwili.

Kila tendo la kujifurahisha kwa dhambi huelekea kupumbaza na kufisha utambuzi wa kiakili na wa kiroho; moyo huvutiwa kidogo mno na Neno au Roho wa Mungu. "Na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu." 2 Wakorintho 7:1.

Ni wangapi wanaokiri kuwa Wakristo; ambao wanaushusha ubinadamu wao wenye mfano wa Mungu kwa ulafi, kwa kunywa pombe, na kwa anasa zisizoruhusiwa. Na mara nyingi kanisa linahamasisha uovu, ili kutunisha hazina yake ambayo upendo kwa Kristo ulio duni ndani yao umeshindwa kuijaza. Endapo Yesu angeingia kwenye makanisa ya leo na kuziangalia sikukuu zinazoendeshwa kama za kidini; je, hangewafukuza hao waharibifu wa vitu vitakatifu kama alivyowafanyia wavunja fedha hekaluni? "Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu." 1 Wakorintho 6:19, 20. Yule ambaye mwili wake ni hekalu la Roho hawezi kuwa mtumwa wa tabia zenye madhara. Uwezo wake wote unamilikiwa na Kristo. Mali yake ni ya Bwana. Atawezaje kutapanya mtaji alioaminiwa na Bwana?

Wale wanaokiri kuwa Wakristo kila mwaka hugharamia na kuzika pesa nyingi kuridhisha uchu kwa vitu vinavyodhuru. Mungu ameibiwa zaka na sadaka. Wao wanatumia, kwa ajili ya tamaa, zaidi ya vile ambavyo wangetoa kusaidia maskini au kusaidia kazi ya Injili. Matokeo ni uangamivu. Kama wote wanaomkiri Kristo wangekuwa wametakaswa kweli kweli, mali zao, zingepelekwa kwenye hazina ya Bwana, badala ya kutumika kwa vitu visivyo vya lazima vyenye kutosheleza uchu na mwisho vina madhara. Wakristo wangeweka kielelezo kwa kuwa na kiasi na kujitoa kafara nafsi zao. Ndipo watakuwa nuru ya Ulimwengu.

[294] "Tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima" (1 Yohana 2:16), huwatawala watu wengi. Lakini wafuasi Wakristo wana mwito mtakatifu. "Tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema

Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu” Kwa wale wanaoenenda sawa na masharti hayo, ahadi ya Mungu ni, “Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike” 2 Wakorintho 6:17, 18.

Kila hatua ya imani na utii inauleta moyo karibu na muunganiko na Yeye aliye nuru ya ulimwengu. Miali angavu ya Jua la Haki huwaangazia watumishi wa Mungu, wao wanapaswa kuakisi miali hiyo. Nyota zinatuambia kuwa kuna nuru mbinguni ambayo utukufu wake unazifanya zing’ae; vivyo hivyo Wakristo wanadhihirisha kuwa yuko Mungu kwenye kiti cha enzi, ambaye tabia yake inastahili kutukuzwa na kuigwa. Utakatifu wa tabia yake utadhihirika ndani ya mashahidi wake.

Kupitia sifa njema za Kristo tunayo njia ya kukifikia kiti cha enzi cha Uwezo usio na kikomo. “Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?” “Ombeni, nanyi mtapata”; furaha yenu iwe timilifu. Yesu anasema: “Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?” “Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.” ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu.” Warumi 8:32; Luka 11:13; Yohana 14:14; 16:24.

Ni fursa ya kila mmoja kuishi hivyo ili Mungu ampe kibali na ambariki. Siyo mapenzi ya Baba yetu wa mbinguni kwamba tutakuwa daima chini ya hukumu na giza. Hakuna ushahidi juu ya unyenyekevu wa kweli unaoonekana kwa mtu kutembea akiinamaisha kichwa na moyo uliojaa mawazo ya ubinafsi. Tunaweza kwenda kwa Yesu akatutakasa na kusimama mbele ya sheria bila aibu wala huzuni.

Kwa njia ya Yesu, wana wa Adamu walioanguka wanakuwa, “wana wa Mungu.” “Haoni haya kuwaita ndugu zake” Maisha ya Mkristo yapaswa kuwa yale ya imani, ushindi na furaha katika Mungu. “Furaha ya Bwana ni nguvu zenu.” “Furahini siku zote; ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.” Waebrania 2:11; Nehemia 8:10; 1 Wathesalonike 5:16-18.

Haya ndiyo matunda ya uongofu na utakaso unaofundishwa [295]
ndani ya Biblia; matunda haya yanashuhudiwa mara chache kwa

sababu, kanuni kuu za haki zilizowekwa zimeachwa bila kujali. Na ndiyo maana ule udhihirisho wa kina, wa kazi ya kudumu ya Roho Mtakatifu, ambao ulionekana kwenye uamsho wa zamani, upo kidogo sana.

Ni kwa kutazama ndipo tunapobadilika. Kwa kadiri yale maagizo matakatifu ambamo Mungu amewafunulia wanadamu ukamilifu na utakatifu wa tabia yake yanavyochwa; na akili za watu zikivutiwa na mafundisho ya watu na nadharia zao; kumekuwepo na upungufu katika uchaji wa Mungu ndani ya kanisa. Ni pale tu sheria ya Mungu itakaporejeshwa mahali pake sahihi; ndipo utakapokuwepo uamsho wa imani ya zamani na utauwa miongoni mwa watu wanaomkiri.

# Sura Ya 28 - Kukabiliana Na Kumbukumbu Ya Maisha Yetu [296]

"Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa." Danieli 7:9, 10.

Hivi ndivyo Danieli alivyopewa maono ya ile siku kuu wakati maisha ya wanadamu yatakapochunguzwa mbele ya hakimu wa dunia yote. Mzee wa Siku ni Mungu Baba. Yeye, aliye asili ya viumbe vyote, chemchemi ya sheria yote, ndiye atakayeongoza hukumu. Na malaika watakatifu watakuwa watumishi na mashahidi.

"Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele." Danieli 7:13, 14.

Kuja kwa Kristo kunakoelezewa hapa, siyo tukio la kuja kwake mara ya pili duniani. Anakuja kwa Mzee wa Siku mbinguni ili apokee ufalme atakaopewa mwishoni mwa kazi yake kama mpatanishi. Ni tukio hili, na siyo, kuja kwake duniani mara ya pili, ambalo lilikuwa linakwenda kutimia mwishoni mwa unabii wa siku 2300 hapo mwaka 1844. Kuhani wetu mkuu aliingia Patakatifu sana ili afanye sehemu ya mwisho ya huduma ya upatanisho kwa niaba ya wanadamu.

Katika huduma kielelezo(patakatifu pa duniani), ni wale tu ambao dhambi zao zilikuwa zimepelekwa kwenye hema ya kukutania, waliokuwa na sehemu katika Siku ya Upatanisho. Vivyo hivyo katika siku kuu ya upatanisho na hukumu ya upelelezi mashauri yanayotendewa kazi ni ya wale tu wanaodai kuwa watu wa Mungu.

Hukumu ya waovu ni kazi itakayofanyika baadaye. “Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu. 1 Petro 4:17.

[297] Vitabu vya kumbukumbu vilivyoko mbinguni ndivyo vitakavyotumika kufanya uamuzi. Kitabu cha uzima kina majina ya wale wote waliowahi kufanya kazi ya Mungu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake: “Furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni.” Paulo anawaambia Watendakazi wenzake, “majina yao yamo katika kitabu cha uzima.” Danieli anasema kuwa watu wa Mungu wataokolewa “kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.” Na Yohana wa Ufunuo anasema watakaoingia katika mji wa Mungu ni wale wenye majina, “Yaliyoandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo.” Luka 10:20; Wafilipi 4:3; Danieli 12:1; Ufunuo 21:27.

Kwenye “Kitabu cha kumbukumbu” yameandikwa matendo mema ya “Hao waliomcha Bwana, na kulitafakari jina lake.” Kila jaribu walilolipinga, kila uovu walioushinda, kila neno la huruma lililotolewa, kila tendo la kujitoa, kila uchungu uliovumiliwa kwa ajili ya Yesu vimeandikwa. “Umehesabu kutanga-tanga kwangu; Uyatie machozi yangu katika chupa yako; (Je! Hayamo katika kitabu chako?)” Malaki 3:16; Zaburi 56:8.

## Makusudi ya Siri

Kuna kumbukumbu pia kwa ajili ya dhambi za wanadamu. “Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya.” “Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.” “Kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.” Mambo ya siri yanaonekana kwenye kitabu, kwani Mungu “atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo” Mhubiri 12:14; Mathayo 12:36, 37; 1 Wakorintho 4:5. Mbele ya kila jina kwenye vitabu vya mbinguni limeandikwa kila neno lisilofaa, kila tendo la ubinafsi, kila wajibu usiotimizwa, na kila dhambi ya siri. Maonyo yaliyotumwa kutoka mbinguni au makaripio yaliyopuuzwa, wakati uliopotea, mvuto uliowekwa kwa mema au kwa mabaya pamoja na matokeo yake ya mwisho, yote yanaandikwa na malaika anayetunza kumbukumbu.

## Kipimo cha Hukumu [298]

Sheria ya Mungu ni kipimo katika hukumu. "Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni" "Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru." Mhubiri 12:13, 14; Yakobo 2:12.

"Lakini, wale wahesabiwao kuwa wamestahili" watakuwa na sehemu katika ufufuo wa wenye haki. Yesu anasema: "wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kule kufufuka katika wafu...ni wana wa Mungu, kwa vile walivyo wana wa ufufuo." "Wale waliofanya mema" watatoka kwanza "kwa ufufuo wa uzima" Luka 20:35, 36; Yohana 5:29. Wafu walio hai hawatafufuliwa mpaka baada ya hukumu watapohesabiwa wamestahili "kwa ufufuo wa uzima." Hivyo hawatakuwepo wakati kumbukumbu zao zitakapokuwa zinachunguzwa na mashauri yao kuamuliwa.

Yesu atatokea kama wakili wao, kusihi mbele za Mungu kwa niaba yao. "Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki" "Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu" "Kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee." lYohana 2:1; Waebrania 9:24; 7:25.

Vitabu vya kumbukumbu vitakapofimguliwa katika hukumu, maisha ya wote waliokuwa wanamwamini Yesu yataonekana mbele za Mungu. Wakili wetu ataleta mashauri ya kila kizazi kwa mfuatano, akianza na wale waliokuwa wa kwanza kuishi hapa duniani. Kila jina litatajwa na kila shauri litachunguzwa. Majina yatakubaliwa na mengine yatakataliwa. Wote watakaoonekana na dhambi kwenye vitabu vya kumbukumbu, ambazo hawakutubu na kusamehewa; majina yao yatafutwa kutoka kwenye kitabu cha uzima. Bwana alimwambia Musa: "Mtu ye yote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika kitabu changu." Kutoka 32:33.

Wale wote ambao wamefanya toba ya kweli na kwa imani [299]
wamedai damu ya Yesu kama kafara yao ya upatanisho wamepata msamaha na umeingizwa kwenye vitabu vya mbinguni. Kwa sababu wamekuwa washirika wa haki ya Kristo na tabia zao zinaonekana

kuwa zinapatana na sheria ya Bwana, dhambi zao zitafutwa, na watahesabiwa kuwa wamestahili uzima wa milele. Bwana anatangaza kuwa: "Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako." Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe...nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake." "Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni.'Tsaya 43:25; Ufunuo 3:5; Mathayo 10:32, 33.

Mpatanishi wa mbinguni anapeleka ombi kwamba wote walioshinda kwa imani katika damu yake, warejeshwe kwenye makazi yao ya Edeni na pia wavikwe taji ya kuwa warithi pamoja naye katika "Mamlaka ya kwanza." Mika 4:8. Kristo sasa anaomba kwamba ule mpango wa Mungu wa kumwumba mwanadamu uendelee kana kwamba mwanadamu alikuwa hakuanguka. Hawaombei watu wake msamaha na kuhesabiwa haki tu, bali pia wawe na sehemu katika utukufu wake na kiti cha enzi katika Ufalme wake.

Wakati Yesu anaendelea kusihi kwa ajili ya walengwa wa neema yake, Shetani anawashtaki mbele za Mungu. Ananyosha kidole chake kwenye kumbukumbu za maisha yao, upungufu wa kitabia, kutofanana na Kristo, kwenye dhambi zote alizowajaribu ili watende. Kwa ajili ya dhambi hizo, anadai kuwa hao ni watu wake.

Yesu hawaondolei dhambi zao tu, bali huonesha toba na imani yao. Anapowaombea msamaha, huinua mikono yake iliyojeruhiwa mbele za Baba, na kusema: Nimewaandika kwenye viganja vya mikono yangu. "Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau." Zaburi 51:17.

[300] **Bwana Anamkemea Shetani**

Na kwa yule mshitaki anasema: "Bwana na akukemee Ewe Shetani; naam, Bwana, aliyechagua Yerusalemu, na akukemee; je! hiki si kinga kilichotolewa motoni?" Zekaria 3:2. Kristo atawavisha wale waaminifu wake vazi la haki yake, ili awalete kwa Baba yake "Kanisa tukufu, lisilo na ila waia kunyanzi wala lo lote kama hayo." Waefeso 5:27.

Hivyo itakuwa imetimia kwa ukamilifu ile ahadi ya agano jipya: "Nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena." "Katika siku hizo na wakati huo, asema Bwana, uovu wa Israeli utatafutwa, wala uovu hapana; na dhambi za Yuda zitatafutwa, wala hazitaonekana" "Tena itakuwa ya kwamba yeye aliyebaki katika Sayuni, na yeye aliyeachwa ndani ya Yerusalemu, ataitwa mtakatifu; yaani, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa hao walio hai ndani ya Yerusalemu." Yeremia 31:34; 50:20; Isaya 4:3.

## Kuzifuta Dhambi

Kazi ya hukumu ya upepelezi na kuzifuta dhambi itakamilika kabla ya kuja kwa Bwana mara ya pili. Katika zile huduma kielelezo(patakatifu pa duniani), kuhani mkuu alikuwa anatoka nje ya hema ya kukutania na kulibariki kusanyiko. Vivyo hivyo Kristo, atakaRomaliza kazi yake kama mpatanishi, atatokea, "Pasipo dhambi, kwa wokovu." Waebrania 9:28.

Kuhani mkuu alipokuwa anaziondoa dhambi kutoka kwenye hema ya kukutania, aliziungama akiweka mikono yake juu ya kichwa cha mbuzi wa Azazeli. Kristo ataziweka dhambi hizi zote juu ya Shetani, ambaye ni mwanzilishi wa dhambi. Mbuzi wa Azazeli alipelekwa mbali "mpaka nchi isiyo watu." Mambo ya Walawi 16:22. Shetani, atafungwa kwa miaka elfu moja kwenye dunia iliyo ukiwa, akiwa amebeba hatia ya dhambi alizowashawishi watu kutenda, na mwishowe atateseka kwa adhabu ya moto utakaowateketeza waovu. Hivyo mpango wa wokovu utafikia utimilifu wake wakati dhambi itakapong'olewa.

## WakatiUIioamuIiwa

Katika muda uliopangwa-kumalizika kwa siku 2300 mwaka 1844, kazi ya upelelezi na kuzifuta dhambi ilianza. Dhambi zisizofanyiwa toba na kuachwa, hazitafutwa kwenye vitabu vya [301]
kumbukumbu. Malaika wa Mungu waliishuhudia kila dhambi na kuiandikisha. Dhambi inaweza kukataliwa, kufichwa ili baba, mama, mke, watoto, na washirika wengine wasijue; lakini imewekwa wazi mbinguni. Mungu hawezi kudaganywa na jinsi tunavyoonekano..

Hawezi kukosea. Wanadamu wanaweza kudanganywa na wale wenye mioyo miovu, lakini Mungu huyasoma maisha ya ndani.

Hili ni wazo nyeti sana! Mshindi mwenye nguvu hapa duniani, hana uwezo wa kuirudisha kumbukumbu yake ya siku moja. Matendo yetu, maneno yetu, na hata mambo ya siri, ingawa tumeyasahau, yatatushuhudia kutupatia haki ama kutuhukumu.

Katika hukumu matumizi ya kila talanta yatachunguzwa kwa makini. Ni kwa namna gani tumeutumia muda, kalamu zetu, sauti zetu, pesa zetu, na mvuto wetu? Ni kitu gani tumemfanyia Kristo kupitia kwa maskini, wanaoteseka, yatima, ama wajane? Tumeufanyia nini ukweli na nuru tuliyopewa. Ni ule upendo tu uliooneshwa kwa matendo utakaohesabiwa. Upendo pekee yake, kwa mtazamo wa mbinguni, hulifanya kila tendo kuwa la thamani.

## Ubinafsi Uliofichwa Wafunuliwa

Ubinafsi uliofichwa, unaonekana wazi ndani ya vitabu vya mbinguni. Ni mara nyingi kiasi gani wakati, wazo, na nguvu ambavyo ni mali ya Kristo alikuwa amepewa Shetani? Wafuasi wanaomkiri Kristo wametopea katika kutafuta mahitaji ya kidunia ama kufurahia anasa za dunia. Pesa , muda na nguvu hutumika kwaajili ya kujionesha na kujifurahisha nafsi; na muda mfupi hutengwa kwa ajili ya maombi, kuyachunguza Maandiko, na kuungama dhambi.

Shetani anabuni mipango isiyo na idadi ili aijaze kwenye akili zetu. Mdanganyifu mkuu anuchukia ukweli mkuu unaoifunua kafara ya upatanisho na Mpatanishi mwenye nguvu. Jambo kubwa kwake ni kuzichepua akili kutoka kwa Yesu.

Wale wanaotaka kushiriki matunda ya upatanisho wa Mwokozi yapasa wasiruhusu chochote kijiingize katika wajibu wao wa kukamilisha utakatifu katika kicho cha Mungu. Badala ya kutu-
[302] miwa kwa kujifurahisha ama kutafuta mapato, muda wa thamani ungetakiwa utolewe kwa ajili ya kujifunza kwa maombi Neno la Kweli.. Somo la Patakatifu na Hukumu ya Upelelezi ni lazima yaeleweke kwa uwazi. Ni hitaji la wote kufahamu nafasi na huduma ya Kuhani wao Mkuu. Vinginevyo haitawezekana kuwa na imani ambayo ni muhimu kwa wakati huu.

Patakatifu pa mbinguni ni kiini cha kazi ya Kristo kwa niaba ya wanadamu. Inamhusu kila mwanadamu anayeishi duniani. In-

aufunua mpango wa ukombozi, na kutuleta hadi kwenye kufungwa kwa shindano kati ya haki na dhambi.

## Maombezi ya Kristo

Huduma ya Kristo ya upatanisho kwa niaba ya mwanadamu katika hekalu la mbinguni; ni ya muhimu katika mpango wa ukombozi kama kilivyokuwa muhimu kifo chake msalabani. Kwa kifo chake, aliianza ile kazi ambayo alipaa kwenda kuikamilisha mbinguni. Kwa imani inatupasakuingia ndani ya pazia, "alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu" Waebrania 6:20. Pale, nuru kutoka msalabani imeakisiwa. Pale ndipo tunapopata utambuzi ulio wazi kuhusu siri za ukombozi.

"Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; Bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema." Mithali 28:13. Kama wale wanaotoa visingizio kwa ajili ya dhambi zao wangeona namna Shetani anavyomdhihaKikristo kwa sababu ya mwenendo wao; wangeungama dhambi zao na kuziondoakuzitupa mbali. Shetani anajitahidi kuidhibiti akili yote, na anajua kwamba kasoro zikiendekezwa, yeye atafanikiwa. Kwa hiyo anadumu kutafuta namna ya kuwadanganya wafuasi Wakristo kwa maneno ya hila na yenye kufisha ambayo ni vigumu kwao kuyashinda. Lakini Yesu alitangaza kwa wote ambao wangemfuata: "Neema yangu yakutosha" "Nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi." 2Wakorintho 12:9; Mathayo 11:30. Hebu wasiwepo watu wanaouona upungufu wao kuwa hautibiki. Mungu atawapa imani na neema ili waushinde.

Sasa tunaishi katika siku ile kuu ya upatanisho. Wakati kuhani [303]
alipokuwa anafanya upatanisho kwa Waisraeli, iliwapasa wote wazitaabishe nafsi zao kwa kutubu dhambi zao. Kwa namna ile ile, wale wote ambao wanataka majina yao yabaki kwenye kitabu cha uzima wanatakiwa wazitaabishe nafsi zao mbele za Mungu kwa toba ya kweli. Kunatakiwa kuwepo na uchunguzi wa kina wa moyo. Ile roho isiyokuwa na kusudi maalum, ambayo imeendekezwa na wengi haina budi kuwekwa mbali. Kuna vita vya dhati kwa wote wanaotaka kuishinda mielekeo yao inayopambana ili kuwashinda. Kila mmoja ni lazima akutwe bila "ila wala kunyanzi, wala lo lote kama hayo." Waefeso 5:27.

Katika wakati huu juu ya mengine yote, yapasa kila nafsi isikilize maagizo ya Mwokozi: "Kesheni, ombeni, kwa kuwa hamjui wakati ule utakapokuwapo." Marko 13:33.

## Hatima ya Wote Kuamuliwa

Wakati wa matazamio utamalizika muda mfupi kabla ya kutokea kwa Bwana katika mawingu ya mbinguni. Akiutazamia wakati huo, Yesu atatangaza: "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa. Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo."Ufunuo 22:11, 12.

Wanadamu watakuwa wakipanda na kujenga, wakila na kunywa, wote bila kujua kuwa uamuzi wa mwisho umekwisha kutolewa katika hekalu la mbinguni. Kabla ya gharika, baada ya Nuhu kuingia ndani ya safina, Mungu alimfungia ndani na waovu aliwafungia nje; lakini kwa siku saba watu walikuwa wanaendelea na maisha yao ya kupenda anasa na walikuwa wanadhihaki maonyo juu ya hukumu. Mwokozi anasema, "Ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." Saa ya kuweka hatima ya kila mwanadamu itakuja kimya kimya, bila kuonekana, kama mwivi wa usiku wa manane, "Kesheni basi... asije akawasili ghafula akawakuta mmelala" Mathayo 24:39; Marko 13:35, 36.

[304] Wale ambao baada ya kuchoshwa na kukesha, wanageukia kwenye vivutio vya ulimwengu, hali yao ni ya hatari. Wakati mfanyabiashara akiwa ametopea katika kufukuzia faida, wakati mpenda anasa akiwa anatafuta kujifurashisha, wakati binti mwanamitindo akiyapangaa mapambo yake-huenda ikawa katika saa ile, hakimu wa dunia yote atatoa tamko lisemalo: Umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka." Danieli 5:27.

# Sura Ya 29 - Kwa Nini Dhambi Iliruhusiwa? [305]

Wengi huiona kazi ya uovu pamoja na huzuni, na namna yake ya kutelekeza, na kuuliza ni kwa namna gani hili linaweza kuwepo chini ya enzi ya yule ambaye hana ukomo wa hekima, uwezo, na upendo. Wale wanaopendelea kuona mashaka huchukulia hicho kama kisingizio cha kuyakataa Maandiko Matakatifu. Mapokeo na tafsiri potovu vimetia giza fundisho la Biblia juu ya tabia ya Mungu, asili ya serikali yake, na kanuni anazotumia anaposhughulikiadhambi.

Haiwezekani kuelezea chanzo cha dhambi ili kutoa sababu ya kuwepo kwake. Lakini mengi yanaweza kufahamika juu ya chanzo na hatima ya tabia ya dhambi ili kubainisha kikamilifu haki na ukarimu wa Mungu. Mungu, kwa namna yoyote ile hahusiki na kuwepo kwa dhambi; hakukuwa na uondoaji kiholela wa neema ya Mungu, hakukuwa na upungufu katika serikali ya Mungu, uliotoa nafasi kwa uasi. Dhambi ni kitu kiiichojipenyeza ambacho uwepo wake hauna sababu inayoweza kutolewa. Kuitolea udhuru ni kuitetea. Endapo udhuru wake ungepatikana, ingekoma kuwa dhambi. Dhambi ni matokeo ya utendaji wa kanuni inayopingana na sheria ya upendo, ambayo ni msingi wa serikali ya Mungu.

Kabla ya kuingia kwa uovu kulikuwa na amani na furaha katika ulimwengu wote. Upendo kwa Mungu lilikuwa ndilo jambo kubwa kabisa, upendo kwa wengine haukuwa na upendeleo. Kristo Mwana pekee wa Mungu alikuwa mmoja na Baba, wa milele katika asili, katika tabia, na katika makusudi-nafsi pekee ambayo ingeingia katika mashauri yote na makusudi ya Mungu. "Katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni ...ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka." Wakolosai 1:16.

Sheria ya upendo ikiwa ndiyo msingi wa serikali ya Mungu, furaha ya viumbe vyote ilikuwa inategemea hiari yao juu ya kanuni zake za haki. Mungu hafurahishwi na utii wa kulazimishwa, na huwapatia wote uhuru wa dhamiri, ili wamtolee huduma ya hiari.

Lakini alikuwepo mmoja aliyechagua kuupotosha uhuru huo. [306]
Dhambi ilianzia kwake, yeye ambaye alimfuatia Kristo, kwa

kuheshimiwa sana na Mungu. Kabla ya anguko lake, Lusifa alishika nafasi ya kwanza kati ya makerubi wafunikao, mtakatifu, asiye na unajisi. "Bwana MUNGU asema hivi; Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri. Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako... Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako...Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako." "Kwa kuwa umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu." "Nawe ulisema... Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano...Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu." Ezekieli 28:12-17; 28:6; Isaya 14:13-14.

Akiitamani heshima ambayo Baba alikuwa anaitoa kwa Mwaawe, mkuu huyu wa malaika, aliutamani uwezo ambao ulikuwa ni haki ya Kristo pekee kuwa nao. Hali ya kutoelewana iliharibu amani ya mbinguni. Kujiinua nafsi kuliamsha dalili za uovu ndani ya mioyo ambayo kwayo utukufu wa Mungu ulikuwa jambo la kwanza. Mabaraza ya mbinguni yalihojiana na Lusifa. Mwana wa Mungu alimweleza juu ya uzuri na haki ya Mwumbaji na asili takatifu ya sheria yake. Kwa kuiacha, Lusifa alikuwa anamvunjia heshima Mwumbaji wake na kujiletea uangamivu wake mwenyewe. Lakini onyo hilo liliamsha upinzani. Lusifa aliruhusu wivu aliokuwa nao dhidi ya Yesu kushinda.

Majivuno yalikuza shauku ya kutaka mamlaka ya juu. Heshima za juu alizotunukiwa Lusifa hazikumsukuma kumshukuru Mwumbaji. Alikuwa anatamani kuwa sawa na Mungu. Na bado Mwana wa Mungu alikuwa ndiye Mwenye enzi aliyetambuliwa mbinguni, mwenye uwezo na mamlaka pamoja na Baba. Katika mabaraza yote ya Mungu, Kristo alikuwa mshiriki, lakini Lusifa hakuruhusiwa kuingia kwenye makusudi ya Mungu. "Kwa nini?" Aliuliza huyu malaika mwenye nguvu, "Kristo awe na mamlaka ya juu? Ni kwa nini ameheshimiwa hivyo kupita Lusifa?

## Kutoridhika Miongoni mwa Malaika [307]

Akiiacha nafasi yake mbele ya uwepo wa Mungu, Lusifa alisonga mbele katika kueneza kutokuridhika kwake miongoni mwa malaika. Kwa mafumbo yenye usiri, akilificha kusudi lake halisi chini ya mwonekano wa uchaji wa Mungu, alijitahidi kuchochea kutoridhika juu ya sheria zilizoongoza viumbe wa mbinguni, akitangaza kwamba zililazimisha vizuizi visivyo vya lazima. Kwa vile malaika ni watakatifu, alitoa hoja kwamba wangepaswa kufuata matakwa ya nia zao. Mungu hakumtendea haki kwa kumpa Kristo mamlaka kuu. Alidai kwamba hakuwa akitafuta kujiinua nafsi bali kuwahakikishia uhuru wakazi wote wa mbinguni, ili waweze kupata maisha bora zaidi.

Mungu alimvumilia Lusifa kwa muda mrefu. Pamoja na kutoa madai potovu mbele za malaika, Mungu hakumshusha daraja kutoka katika nafasi yake iliyokuwa juu. Mara kwa mara alipewa msamaha kwa sharti la toba na kujisalimisha. Juhudi hizo, ni upendo usio na mwisho pekee ambaoungeweza kuzibuni, ili kumshawishi atambue kosa lake. Hali ya kutoridhika haikuwahi kufahamika mbinguni kabla ya hapo. Lusifa mwenyewe mara ya kwanza hakuifahamu asili halisi ya hisia zake. Ilipothibitika kuwa kutondhika kwake hakukuwa na msingi, Lusifa alishawishika kwamba madai ya Mungu yalikuwa ya haki na kwamba alipaswa kukiri mbele za mbingu yote. Endapo angelifanya hili, huenda angejiokoa yeye mwenyewe na malaika wengi. Ikiwa angehiari kumrudia Mungu, akiwa ameridhika kujaza nafasi ambayo angepewa, angerejeshwa katika ofisi yake. Lakini majivuno yalimzuia asijisalimishe. Alikuwa kuwa hakuwa na haja natoba, na akajitoa kikamilifu katika pambano kuu dhidi ya Mwumbaji wake.

Nguvu zote za akili zake zenye ubunifu sasa zilielekezwa kwenye udanganyifu, ili apate kuungwa mkono na malaika. Shetani alikuwa analalamika kuwa alihukumiwa isivyo halali na kwamba uhuru wake ulizuiwa. Baada ya kuyapotosha maneno ya Kristo alileta uongo wa moja kwa moja, akimshitaki Mwana wa Mungu kwamba alikuwa amemdhalilisha mbele ya wakazi wa mbinguni.

Wote ambao hakuweza kuwachochea wawe upande wake aliwashtaki kuwa hawakuyajali matakwa ya viumbe wa mbingum. Aliishia kuipotosha tabia ya Mwumbaji. Ilikuwa ni sera yake

[308] kuwafadhaisha malaika kwa hoja ngumu juu ya makusudi ya Mungu. Kila kitu rahisi alikifunika kwenye usiri, na kwa kutumia upotoshaji wenye ustadi akazitia mashaka kauli za Mungu zilizo wazi kabisa. Nafasi yake ya juu aliyokuwa nayo ikatoa msukumo kwa malalamiko yake. Wengi waliungana naye katika uasi.

### Chuki Yakomaa na kuwa llasi Halisi

Mungu kwa hekima yake alimruhusu Shetani kuendelea na kazi yake, hadi ile roho ya chuki ilipopevuka na kuwa uasi. Ilikuwa ni lazima mipango yake ifunuliwe kwa ukamilifu, ili asili yake halisi ionekane kwa wote. Lusifa alipendwa sana na viumbe mbinguni, na mvuto wake juu yao ulikuwa mkubwa. Serikali ya Mungu haikujumuisha tu wakazi wa mbinguni, bali ulimwengu wote aliokuwa ameuumba; na Shetani alipanga kuwa endapo angewachukua malaika pamoja naye katika uasi, angeweza pia kuchukua ulimwengu wote. Akitumia hila na udanganyifu, uwezo wake wa kuhadaa ulikuwa mkubwa sana. Hata malaika waaminifu hawakuweza kuitambua tabia yake kwa ukamilifu ama kuona ni wapi kazi yake ilikuwa inaelekea.

Shetani alikuwa anaheshimiwa sana, na matendo yake yote yalikuwa yamesitiriwa kwa usiri, kiasi kwamba ilikuwa ni vigumu kuifunua asili ya kazi yake kwa malaika. Kabla ya haijafunuliwa kwa ukamilifu; dhambi haingeonekana kuwa kitu kibaya kama ilivyokuwa. Viumbe watakatifu, hawakuweza kutambua matokeo ya kuiweka kando sheria ya Mungu. Mwanzoni Shetani alidai kwamba alikuwa akikuza heshima ya Mungu na mema ya wakazi wote wa Mbinguni.

Katika kushughulikia dhambi, Mungu alikuwa anatumia haki na kweli pekee. Shetani alikuwa anatumia kile ambacho Mungu hangeweza kukitumia- ubembe na ulaghai. Tabia ya kweli ya mnyang'anyi ni lazima ifahamike kwa wote. Alitakiwa apate muda wa kujifunua mwenyewe kwa kazi zake mbovu.

Shetani alimlaumu Mungu kwa kukosekana kwa maelewano kulikosababishwa na mwelekeo wake kule mbinguni. Alitangaza kuwa uovu wote ni matokeo ya utawala wa Mungu. Na hivyo ilikuwa lazima aoneshe utendaji wa mabadiliko aliyoyapendekeza ndani
[309] ya sheria ya Mungu. Kazi yake ni lazima imhukumu mwenyewe.

Ulimwengu mzima ni lazima uone mdanganyifu akifunuliwa.

Hata wakati ilipoamuliwa kwamba hangeendelea kubakia mbinguni, Mungu hakumwangamiza Shetani. Utii wa viumbe wa Mungu ni uthibitisho wa haki yake. Kwa vile wakazi wa mbinguni na ulimwengu wote, hawakutayarishwa kufahamu matokeo ya dhambi, hawangeweza wakati ule, kuiona haki na rehema ya Mungu katika kumwangamiza Shetani. Endapo mara moja angefutwa asiwepo, wangekuwa wanamtumikia Mungu kwa hofu na siyo kwa upendo. Mvuto wa mdanganyifu ungekuwa haujaangamizwa kikamilifu, na wala roho ya uasi haingekuwa imeng'olewa. Kwa faida ya ulimwengu katika vizazi vyote ilikuwa ni lazima Shetani akuze kwa ukamilifu zaidi kanuni zake, ili madai yake dhidi ya serikali ya Mungu yapate kuonekana na viumbe vyote katika nuru halisi.

Uasi wa Shetani ulitakiwa kuwa ushuhuda kwa ulimwengu juu ya matokeo ya kutisha ya dhambi. Utawala wake ungeonesha matunda yatokanayo na kuiacha kando sheria ya Mungu. Historia ya jaribio hili la kutisha la uasi ingekuwa ni ulinzi endelevu kuwaokoa katika dhambi na adhabu yake.

Ilipotangazwa kwamba mnyang'anyi mkuu pamoja na wote waliomwunga mkono ni lazima wafukuzwe kutoka kwenye makao ya furaha, kiongozi wa uasi kwa ujasiri aliapa kuitweza sheria ya Mungu. Alizishutumu sheria za Mungu kwamba zinanyima uhuru na akatangaza kusudi lake la kuifuta sheria. Alisema kuwa yakiwa yameachwa huru dhidi ya kizuizi hiki; majeshi ya mbinguni yangeweza kuishi maisha yaliyotukuka zaidi.

### Kufukuzwa Kutoka Mbinguni

Shetani na jeshi lake walimtupia Kristo lawama za uasi wao; kwamba kama wasingeshutumiwa wasingeasi. Wakiwa na kiburi na ufidhuli na bado kwa kufuru wakidai hawana hatia na walikuwa wameonewa na utawala wa kidikteta; mwasi mkuu pamoja na waliomwunga mkono walifukuzwa kutoka mbinguni. (Angalia Ufunuo 12:7-9).

Roho ya Shetani bado inaongoza uasi duniani ndani ya wa- [310]
toto wa kuasi. Kama alivyofanya yeye wanawaahidi watu uhuru utakaopatikana kwa kuvunja sheria ya Mungu. Shutuma dhidi ya dhambi bado huamsha chuki. Shetani anawaongoza watu kujih-

esabia haki wenyewe na kutafuta kuungwa mkono na wengine katika dhambi zao. Badala ya kurekebisha makosa yao, wao huchochea chuki dhidi ya mtu anayeishutumu dhambi, kana kwamba ndiye aliyesababisha shida.

Kwa upotoshaji ule ule wa tabia ya Mungu alioufanya mbinguni na kusababisha Mungu aonekane kuwa mkali na dikteta; Shetani alisababisha mwanadamu kutenda dhambi. Alitangaza kuwa makatazo ya Mungu yasiyo ya haki yalimfanya mwanadamu aanguke, kama yalivyomwongoza yeye kwenye uasi.

Kwa kumfukuza Shetani kutoka mbinguni, Mungu aliitangaza haki na heshima yake. Lakini mwanadamu alipotenda dhambi, Mungu alitoa uthibitisho wa pendo lake kwa kumtoa Mwanawe afe kwa ajili ya wanadamu walioanguka. Katika upatanisho tabia ya Mungu imefunuliwa. Hoja yenye nguvu ya msalaba huonesha kwamba serikali ya Mungu kwa namna yoyote ile haikusababisha dhambi kuwepo. Wakati wa huduma ya Mwokozi duniani, mdanganyifu mkuu alifunuliwa. Kufuru za makusudi za kumtaka Yesu amwabudu, kwa nia mbaya akimwinda kila mahali, na kuisukuma mioyo ya makuhani na watu ili wakatae upendo wake na kulia, “Msulibishe! Msulibishe!”-haya yote yalichochea bumbuwazi na uchungu kwa ulimwengu. Mkuu wa giza alitumia ujanja na nguvu zake zote ili kumwangamiza Yesu. Shetani aliajiri watu kama mawakala wake kuyajaza uchungu na mateso maisha ya Mwokozi. Moto wa wivu na kijicho, chuki na kisasi uliripuka pale Kalvari dhidi ya Mwana wa Mungu.

Na sasa, hatia ya Shetani ilidhihirika bila udhuru. Alikuwa ameifunua tabia yake halisi. Madai yake ya uongo dhidi ya tabia ya Mungu yalionekana katika nuru yake halisi. Alimtuhumu Mungu kwa kuwa anajiinua mwenyewe anapotaka kupokea utii kutoka kwa viumbe wake na alitangaza kuwa wakati Mwumbaji alikuwa anawahimiza wengine kujikana nafsi, Yeye mwenyewe hakujikana nafsi wala kutoa kafara yoyote. Sasa ilikuwa inaonekana kwamba Mtawala wa ulimwengu alikuwa ameitoa kafara iliyo kuu ambayo upendo ungeweza kutoa, kwani, “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake “(2Wakonntho 5:19.) Kwa lengo la kuiangamiza dhambi Kristo alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti.

## Hoja kwa Ajili ya Kumsaidia Mwanadamu [311]

Mbingu yote iliona haki ya Mungu ikifunuliwa. Lusifa alikuwa amedai kwamba wanadamu wenye dhambi walikuwa mbali na wokovu. Lakini adhabu ya dhambi ilimwangukiwa yule aliye kuwa sawa na Mungu na mwanadamu alikuwa huru kuikubali haki ya Kristo na kwa toba na unyenyekevu kupata ushindi dhidi ya nguvu za Shetani.

Lakini haikuwa tu kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu hata Kristo akaja kufa duniani. Alikuja kuuonesha ulimwengu wote kuwa, Sheria ya Mungu haibadiliki. Kifo cha Kristo kinathibitisha kuwa haibadiliki na kinaonesha kwamba haki na rehema ni msingi wa serikali ya Mungu. Katika hukumu ya mwisho itaonekana kwamba hakuna kisingizio cha kuwepo kwa dhambi. Wakati hakimu wa dunia yote atakapomwuliza Shetani, "Kwa nini uliniasi?" mwanzilishi wa uovu hataweza kujitetea.

Katika kilio cha Mwokozi, "Imekwisha", kengele ya kifo cha Shetani iligongwa. Pambano kuu lilikuwa limeamuliwa, kung'olewa milele kwa uovu kulikuwa ni hakika. Wakati ambapo, "siku ile inakuja, inawaka kama tanuru... wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi." (Malaki 4:1).

Uovu hautaonekana tena. Sheria ya Mungu itaheshimiwa kama sheria ya uhuru. Uumbaji uliojaribiwa na kuthibitishwa hautageuka tena na kuacha utii kwake ambaye tabia yake imeonekana ni ya upendo na ana hekima isiyo na kikomo.

[312] ## Sura Ya 30 - Shetani Na Mwanadamu Vitani

"Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino." (Mwanzo 3:15) Uadui huu si wa asili. Mwanadamu alipoiasi sheria ya Mungu, asili yake ikawa uovu, ikipatana na Shetani. Malaika walioanguka na wanadamu waovu walifanya muungano wa uasi. Kama Mungu asingeingilia kati, Shetani na mwanadamu wangeungana wawe kinyume na mbingu, na familia yote ya wanadamu ingekuwa imeungana kwa ajili ya kumpinga Mungu.

Shetani aliposikia kuwa kungekuwa na uadui kati yake na mwanamke, na kati ya uzao wake na ule wa mwanamke, alijua kuwa kwa namna fulani mwanadamu angewezeshwa kumletea upinzani.

Kristo anapandikiza ndani ya mwanadamu uadui dhidi ya Shetani. Pasipo hii neema ibadilishayo na nguvu ifanyayo upya, mwanadamu angeendelea daima kuwa mtumwa, tayari kumtii Shetani. Lakini kanuni hii mpya inaleta mgongano ndani ya nafsi; nguvu aitoayo Kristo inamwezesha mwanadamu kumpinga mdhalimu. Kuichukia dhambi badala ya kuipenda kunaonesha kanuni kamili ya mbinguni.

Uhasama kati ya Shetani na Kristo ulionekana wazi zaidi katika namna ulimwengu ulivyompokea Yesu. Usafi na utakatifu Wakristo uliamsha chuki ya waovu dhidi yake. Hali yake ya kujikana nafsi ilikuwa ni shutuma ya kudumu kwa watu wenye kiburi na wapenda anasa. Shetani pamoja na watu waovu waliungana dhidi ya mtetezi wa ukweli. Uadui ule ule unaonekana dhidi ya wafuasi Wakristo. Yeyote alipingaye jaribu ataamsha ghadhabu ya Shetani. Kristo na Shetani hawawezi kupatana. "Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." (2Timotheo 3:12)

Mawakala wa Shetani wanatafuta kuwadanganya wafuasi Wakristo na kuwashawishi wasimtii. Wanapotosha Maandiko ili kufanikisha lengo lao. Yule roho aliyemuua Yesu anawasukuma

waovu kuwaangamiza wafuasi wake. Haya yote yalitabiriwa kabla katika ule unabii wakwanza usemao, “Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake”

Ni kwa nini Shetani hapati upinzani mkubwa? Kwa sababu [313] askari Wakristo wana muunganiko kidogo mno ulio halisi na Yesu. Kwao dhambi siyo kitu kibaya kama ilivyokuwa kwa Bwana wao. Hawana jitihada ya kuipinga. Wamepofushwa juu ya tabia ya mkuu wa giza. Watu wengi hawajui kuwa adui yao ni kamanda mkubwa apiganaye vita na Kristo. Hata wahubiri wa Injili wanadharau ushahidi wa kazi zake. Wanaonekana kuupuuzia uwepo wake.

### Adui Aliye Macho

Adui huyu aliye macho anajiingiza katika kila nyumba, kila mtaa, kwenye makanisa, kwenye mabaraza ya taifa, kwenye mahakama za haki, akitatanisha, akidanganya, akishawishi, kila mahali akiharibu nafsi na miili ya wanaume, wanawake, na watoto. Anasambaratisha familia, akipanda chuki, ugomvi, uchochezi, na mauaji. Na ulimwengu unaelekea kuchukulia kwamba Mungu ameyapanga mambo hayo na hayana budi kuwepo. Wale wote ambao ni wafuasi nusu-nusu Wakristo ni watumishi wa Shetani. Wakristo wanapochagua jamii ya waovu, wanajipeleka wenyewe kwenye majaribu. Shetani anajiflcha wasimwone na kuleta vivutio vinavyodanganya machoni pao.

Mapatano na desturi za kiulimwengu yanalibadilisha kanisa kuelekea kwenye ulimwengu na siyo ulimwengu kuelekea kwa Kristo. Kuzoeana na dhambi kutaifanya ionekane kuwa inatia kinyaa kidogo tu. Tunapokuwa kazini tunaletwa kwenye majaribu, tunaweza kuwa na hakika kuwa Mungu atatulinda; lakini endapo tutajiweka wenyewe chini ya majaribu tutanguka muda wowote.

Mara nyingi mjaribu hufanya kazi yake kwa mafanikio makubwa kupitia wale ambao hudhaniwa kidogo sana kuwa wapo chini ya udhibiti wake. Talanta na maarifa ni vipawa vya Mungu; lakini vinapoelekezwa mbali naye, vinageuka kuwa mtego.Wengi wa watu wenye akili na maarifa na wenye mvuto ni vyombo vilivyonolewa mikononi mwa Shetani.

Usisahau onyo lililovuviwa likitoa sauti tangu kame nyingi hadi [314] wakati wetu. “Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu

Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze." "Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani." 1 Petro 5:8; Waefeso 6:11. Adui yetu mkuu anajiandaa kwa ajili ya kampeni yake ya mwisho. Wale wote wanaomfuata Yesu watakuwa katika pambano dhidi ya adui huyu. Kwa kadiri Mkristo anavyoiga kielelezo cha mbinguni, ndivyo atakavyojiweka kuwa shabaha ya mashambulizi ya Shetani.

Shetani alimshambulia Yesu kwa ukali na majaribu ya werevu; lakini alishindwa katikakila pambano. Ushindi huo unatufanya sisi kushinda. Kristo atawapa uwezo wale wote wanaoutafuta. Hakuna mtu ambaye atashindwa na Shetani bila hiari yake. Mjaribu hana uwezo wa kuudhibiti utashi au kuilazimisha nafsi kutenda dhambi. Anaweza kusababisha dhiki lakini siyo unajisi. Yapasa ukweli kuwa Yesu alishinda uwavuvie wafuasi wake nguvu za kupigana vita dhidi ya dhambi na Shetani.

# Sura Ya 31 - Roho Za Uchafu



Malaika wa Mungu na roho wachafu wamefunuliwa kwa uwazi ndani ya Maandiko Matakatifu na haiwezekani kuwatenganishana historia ya wanadamu. Malaika watakatifu, wanao “hudumu wale watakaourithi wokovu” (Waebrania 1:14) wanadhaniwa na wengi kuwa ni roho za wafu. Lakini Maandiko yanatoa uthibitisho kuwa hawa siyo roho zilizotengana na miili ya waliokufa.

Kabla ya kuumbwa kwa mwanadamu, malaika walikuwepo tayari, kwani wakati misingi ya ulimwengu ilipowekwa, “...nyota za asubuhi ziliimba pamoja, Na wana wote wa Mungu walipiga kelele kwa furaha.” Baada ya anguko la mwanadamu, malaika walitumwa kwenda kuulinda mti wa uzima kabla mwanadamu hajafa. Malaika wana nguvu kuliko wanadamu kwa sababu, mwanadamu alifanywa ... ” mdogo punde kuliko Mungu.” Zaburi 8:5

Anasema nabii, “...nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi.” Mbele ya Mfalme wa wafalme wanasubiri- “Ninyi watumishi wake mfanyao mapenzi yake” “Mkiisikiliza sauti ya neno lake.” majeshi ya malaika elfu nyingi” Ufunuo 5:11; Zaburi 103:20,21; Waebrania 12:22. Kama wajumbe wa Mungu wanakwenda haraka, “kama kuonekana kwa kumulika kwa umeme.” Wanaruka haraka sana. Malaika aliyeonekana kwenye kaburi la Mwokozi, sura yake, “ilikuwa kama umeme”, ikasababisha walinzi kutetemeka kwa hofu na, “wakawa kama wafu.” Senakeribu alipomkufuru Mungu na kuwatishia Israeli, “malaika wa Bwana alitoka, akakiingia kituo cha Waashuri, akawapiga watu mia na themanini na tano elfu.” Ezekieli 1:14; Mathayo 28:3,4; 2 Wafalme 19:35.

Malaika hutumwa kwa ajili ya kuwarehemu watoto wa Mungu. Kwa Ibrahimu, walikwenda na ahadi ya baraka; Sodoma, kumwokoa Lutu kwenye maangamizi; kwa Eliya , aliyekuwa karibu kuangamia jangwani; kwa Elisha, wakiwa na magari ya farasi wa moto alipokuwa amezingirwa na adui zake; kwa Danieli, alipotupwa awe chakula cha simba; kwa Petro alipokabiliwa na kifo ndani ya

gereza la Herode; kwa wafungwa kule Filipi; kwa Paulo, katika usiku wa dhoruba baharini; kwenda kufungua moyo wa Komelio ili apokee Injili; kumtuma Petro akiwa na ujumbe wa wokovu kwa mgeni mmataifa-hivyo malaika watakatifu waliwatumikia watu wa Mungu.

[316]

## Malaika Walinzi

Malaika mlinzi amewekwa kwa kila mfuasi Wakristo. “Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa.” Akizungumza na wale wanaomwamini Mwokozi alisema: “malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni.” Zaburi 34:7; Mathayo 18:10. Watu wa Mungu wakiwa wamefunuliwa mbele ya uovu usiolala wa mkuu wa giza, wanahakikishiwa ulinzi usiokoma wa malaika. Uhakika huo unatolewa kwa sababu wapo mawakala wenye nguvu kwa ajili ya kukabiliana naomawakala wasio na idadi, waliodhamiria na wasiochoka.

Roho waovu, mwanzo waliumbwa bila dhambi, walikuwa na asili moja, uwezo, na utukufu kama viumbe watakatifu ambao sasa ni wajumbe wa Mungu. Lakini wakiwa wameanguka dhambini, walijiunga pamoja kwa ajili ya kumvunjia Mungu heshima na kuwaangamiza wanadamu.Waliungana na Shetani katika uasi, walishirikiana kupigana vita dhidi ya mamlaka ya Mungu.

Historia ya Agano la Kale inataja uwepo wao, lakini wakati Kristo alipokuwepo duniani, roho waovu walionesha uwezo wao kwa hali ya juu zaidi. Kristo alikuja kumkomboa mwanadamu, na Shetani aliazimia kuudhibiti ulimwengu. Alikuwa amefaulu kuanzisha ibada ya sanamu katika kila sehemu ya dunia isipokuwa Palestina. Yesu alikuja akiinyosha mikono yake ya upendo kwa nchi ambayo ilikuwa haijajitoa kikamilifu kwa mjaribu, akiwaalika wote wapate msamaha na amani ndani yake. Majeshi ya giza yalifahamu kwamba endapo utume Wakristo ungefanikiwa, utawala wao ungekwisha mapema.

Imeelezwa wazi katika Agano Jipya kwamba wanadamu wamekuwa wakipagawa na maShetani. Watu hao waliokuwa wakiteseka hawakuwa wakisumbuliwa na ugonjwa wa asili pekee; Kristo alitambua uwepo wa moja kwa moja wa mawakala wa roho waovu. Waliokuwa wamepagawa na pepo katika nchi ya Wagerasi, wa-

likuwa wagonjwa, wakifurukuta, wakitoa povu, wakipiga kelele za fujo, walikuwa wanajifanyia vumgu wao wenyewe na kuhatarisha [317] usalama wa wote ambao wangewasogelea. Miili yao iliyokuwa imelowa damu na akili zilizochanganyikiwa viliwakilisha kioja kilichokuwa kinamfurahisha mkuu wa giza. Mmoja wa maShetani aliyekuwa anawadhibiti waliokuwa wanateseka akanena kwa nguvu, “Jina langu ni Legioni: maana tuko wengi” Marko 5:9. Katika jeshi la Warumi legioni ilijumuisha watu kati ya 3,000 hadi 5,000. Kwa amri ya Yesu roho wachafu waliwatoka wale wahanga wao, wakiwaacha wakiwa wamepungua nguvu, wenye akili timamu, na waungwana. Lakini pepo waliwasomba kundi la nguruwe hadi baharini, na kwa wakazi wa nchi ya Wagerasi hasara waliyopata ilikuwa inazidi baraka Kristo alizokuwa amezitoa: Mungu mponyaji alikuwa ameamriwa kuondoka. Angalia Mathayo 8:22-34. Kwa kumtumpia Yesu lawama kwa hasara yao, Shetani aliamsha hofu za watu na kuwazuia kusikiliza maneno yake.

Kristo aliruhusu pepo wachafu kuwaangamiza wale nguruwe kama karipio kwa Wayahudi waliokuwa wanafuga wanyama najisi kwa ajili ya biashara. Kama Yesu asingewadhibiti, wale pepo wangewaangamiza si nguruwe pekee bali pia waangalizi na wamiliki wao.

Zaidi ya hayo,tukio hili liliruhusiwa ili wanafunzi wa Yesu washuhudie ukatili wa Shetani kwa wanadamu na kwa wanyama, ili wasidanganywe kwa mbinu zake. Yalikuwa ni mapenzi yake pia kuwa watu waweze kutazama nguvu yake ya kuvunja utumwa wa Shetani na kuwafungulia mateka wake. Ingawa Yesu mwenyewe aliondoka, yule mtu aliyekuwa ameokolewa kimuujiza alibaki ili atangaze rehema za mfadhili wao.

Matukio mengine yameandikwa: Binti wa mwanamke Msirofoinike, akiwa amehuzunika na kuchukizwa na Ibilisi, ambaye Yesu alimtoa kwa njia ya Neno lake. (Marko 7:26-30); kijana aliyekuwa amepagawa ambaye mara nyingi, “amemtupa katika moto, na katika maji, amwangamize” (Marko 9:17-27); aliyepagawa, ameteswa na roho wa ibilisi mchafu aliyevuruga utulivu wa Sabato kule Kapemaumu (Luka 4:33-36)-—wote waliponywa na Mwokozi. Karibu katika kila tukio, Kristo alikuwa anazungumzia pepo kama kiumbe chenye akili, akimwamum kutomtesa yule mtu tena. Waabuduo huko Kapemaumu, “Mshangao ukawashika wote, wakasemezana

wakisema, Ni neno gani hili, maana awaamum pepo wachafu kwa uwezo na nguvu, nao hutoka." Luka 4:36.

[318] Kwa malengo ya kupata nguvu za miujiza, Baadhi ya watu walikuwa wanakaribisha mivuto ya kishetani. Hiyo haikupingana na maShetani. Miongoni mwa watu wa kundi hili ni wale waliokuwa na roho wa uaguzi- Simon Magus, Elima mchawi, na kijakazi aliyewafuata Paulo na Sila kule Filipi, Angalia Matendo. 8:9, 18; 13:8; 16:16-18.

Hakuna watu walio katika hatari kubwa kama wale wanaokataa uwepo wa ibilisi na malaika zake. Wengi huzingatia rai zao huku wakijidhania kuwa wanafuata hekima yao wenyewe. Kwa kadiri tunavyokaribia kufungwa kwa wakati, Shetani anatumia nguvu kubwa zaidi kudanganya, anasambaza kila mahali imani kwamba yeye hayupo. Ni sera yake kujificha mwenyewe na utendaji kazi wake.

Mdanganyifu mkuu anaogopa kuwa tutazifahamu mbinu zake. lli kuificha tabia yake halisi anajifanya mwenyewe aonekane kama kitu cha kudhihakiwa au kutwezwa. Anafurahia anapochorwa na kuonekana kama mpumbavu, mwenye umbile baya, nusu mnyama na nusu mtu. Anafurahia kuona jina lake likitumiwa kwenye michezo na mizaha. Kwa sababu amejificha mwenyewe kwa ujuzi kamili, swali linaloulizwa mara nyingi: "Je, kiumbe wa aina hiyo yupo?" Shetani ana uwezo wa kudhibiti kwa upesi mioyo ya wale ambao hawafahamu juu ya mvuto wake. Neno la Mungu linafunua mbele zetu nguvu zake za siri,na hivyo kutuweka sisi katika hali ya kuwa macho.

Tunaweza kupata kimbilio na ukombozi katika nguvu kubwa ya Mwokozi wetu. Kwa uangalifu tunafunga milango yetu kwa komeo na kufuli ili kulinda mali zetu na maisha yetu dhidi ya watu waovu, ni mara chache tunafikiria juu ya malaika waovu ambao mashambulizi yao hatuna nguvu zetu wenyewe kujilinda nayo. Kama wakiruhusiwa wanaweza kuzivuruga akili zetu, kuiletea maumivu miili yetu, kuharibu mali zetu na maisha yetu. Lakini wale wanaomfuata Kristo wako salama chini ya uangalizi wake. Malaika wenye nguvu nyingi wanatumwa kuwalinda. Yule mwovu hawezi kupita ulinzi ambao Mungu ameuweka kwa watu wake.

## Sura Ya 32 - Namna Ya Kumshinda Shetani [319]

Pambano kuu kati ya Kristo na Shetani litakwisha muda si mrefu, yule mwovu anaongeza juhudi yake maradufu ili kuishinda kazi ya Kristo kwa niaba ya mwanadamu. Lengo analotaka kulitimiza ni kuwashikilia watu gizani na kuwafanya wasitubu hadi kazi ya Mwokozi ya maombezi imekwisha.

Kutojali kunapoenea kanisani, Shetani hasumbuliwi na jambo hilo. Lakini wakati nafsi za watu zinapojiuliza, "Nifanye nini ili niokolewe?" yupo uwanjani kwa ajili ya kulinganisha nguvu zake dhidi ya Kristo na kupinga mvuto wa Roho Mtakatifu.

Katika tukio moja ambapo malaika walijihudhurisha, Shetani pia alikuja kati yao, siyo kwa lengo la kumsujudia Mfalme wa milele, bali kuendeleza makusudi yake mabaya dhidi ya haki. Angalia Ayubu 1:6. Huwa anakuwepo pale wanadamu wanapokusanyika kufanya ibada, akifanya kazi kwa juhudi kudhibiti mioyo ya wale wanaoabudu. Anapomwona mjumbe wa Mungu akichunguza Maandiko, huliwekea alama somo litakalotolewa. Kisha hutumia ujanja na werevu wake ili kwamba ujumbe usiwafikie wale ambao anawadanganya kuhusiana na somo lile. Yule ambaye atalihitaji sana lile onyo atasukumwa kuwa na jambo fulani la kufanya ama kwa njia yoyote nyingine atazuiwa kusikiliza neno.

Shetani anahakikisha kuwa watumishi wa Bwana wamelemewa kwa sababu ya giza linalowagubika watu. Anasikia maombi yanayotolewa kwa ajili ya neema ya Mungu na uwezo wa kuvunja hali ya kutojali na uvivu. Kisha kwa juhudi mpya huwajaribu wanadamu kwa njia ya uchu wa chakula ama kwa kufurahisha tamaa zao binafsi, na hivyo kupumbaza ufahamu wao ili wasisikie yale mambo wanayohitaji zaidi kujifunza.

Shetani anajua kwamba wale wote wanaopuuzia maombi na Maandiko watashindwa kwa mashambulizi yake. Kwa hiyo anabuni kila mbinu iwezekanayo kuishughulisha akili. Mawakala wake wanatenda kazi kwa bidii wakati Mungu awapo kazini. Huwawasilisha wale watumishi waaminifu Wakristo na wale wanaojikana nafsi

[320] kana kwamba wamedanganyika ama ni wadanganyifu. Ni kazi yao kupotosha nia ya kila tendo jema, kusambaza visingizio na kuamsha mashaka ndani ya moyo ya wale wasio na uzoefu. Hata hivyo inaweza kuonekana kwa urahisi kwamba ni watoto wa nani, ni mfano wa nani wanaufuata, na ni kazi ya nani wanaifanya. "Mtawatambua kwa matunda yao." Mathayo 7:16; pia Angalia Ufunuo 12:10.

## Ukweli Unatakasa

Mdanganyifu mkuu ana mafundisho mengi aliyoyatayarisha yaliyo kinyume na ukweli kufaa vionjo mbalimbali vya wale ambao angeweza kuwaangamiza. Ni mpango wake kuleta ndani ya kanisa mambo ya unafiki na yasiyo na wongofu ambayo yatachochea mashaka na kutoamini. Wengi ambao hawana imani kwa Mungu wanazikubali baadhi ya kanuni za ukweli na kukubalika kama Wakristo, na hivyo kuwezeshwa kuingiza makosa kuwa sehemu ya mafundisho ya msingi. Shetani anajua kuwa ukweli ukipokelewa kwa upendo, utaitakasa nafsi. Kwa hiyo badala ya Injili, anaweka nadharia potovu na hadithi za kubuni. Tangu mwanzo, watumishi wa Mungu walipambana na walimu wa uongo, siyo tu kama watu waovu, bali kama wafundishaji wa uongo unaofisha nafsi. Eliya, Yeremia, na Paulo walisimama imara kuwapinga wale waliokuwa wakiwageuza watu kutoka kwenye Neno la Mungu. Uhuru ule unaoichukulia imani sahihi kuwa siyo kitu muhimu haukukubaliwa na watetezi watakatifu wa ukweli.

Fasili za Maandiko zenye mashaka na zenye mawazo yanayopendelewa pamoja na nadharia zinazokinzana katika ulimwengu wa Kikristo ni kazi ya adui yetu mkuu ili kuichanganya mioyo. Kutokubaliana pamoja na migawanyiko miongoni mwa makanisa kwa sehemu kubwa ni kwa sababu ya upotoshaji wa Maandiko ili kuunga mkono nadharia inayopendwa.

Ili kuyasimamisha mafundisho potovu, wengine huchukua aya za Maandiko zikiwa zimeondolewa kwenye muktadha wake, wananukuu sehemu ya aya ili ifae kuthibitishwa hoja zao wakati sehemu ya aya inayosalia huonesha maana iliyo kinyume chake. Kwa kutumia ujanja wa nyoka wanajikita wakiwa na maneno yasiyo na muunganiko yaliyotengenezwa ili yafae kwa ajili ya kuifaa tamaa ya mwili. Wengine huchukua michoro na vielezo na ku-

vipa tafsiri zinazoyafaa mawazo wanayoyapendelea, wakizingatia kidogo tu ushuhuda wa Maandiko kujitafsiri yenyewe, na kisha kuyaleta mashaka yao kama mafundisho ya Biblia.

## Biblia Nzivna ni Kiongozi [321]

Wakati ambapo kujifunza Maandiko kutafanywa bila roho ya maombi na inayokubali kufundishwa fungu lililo wazi sana litapotoshwa kutoka kwenye maana yake ya kweli.Biblia nzima ni lazima iletwe kwa watu kama inavyosomeka.

Mungu alilitoa neno la unabii lililo imara; malaika na hata Kristo mwenyewe alikuja kumfahamisha Danieli na Yohana mambo ambayo kwamba, "hayana budi kuwako upesi" Ufunuo 1:1. Mambo makubwa yanayohusu wokovu wetu hayakufunuliwa katika hali ya kutatanisha na kumpotosha mtu anayeutafuta ukweli kwa uaminifu. Neno la Mungu liko wazi kwa wote wanaojifunza kwa moyo wa maombi.

Kwa ajili ya kilio cha uhuru, watu wamepofushwa wasione mbinu za adui yao. Yeye amefanikiwa kuuweka ubahatishaji wa wanadamu mahali pa Biblia; sheria ya Mungu imewekwa kando ; na makanisa yako chini ya utumwa wa dhambi huku yakidai kuwa yako huru.

Mungu ameruhusu nuru kubwa katika ulimwengu kwa ajili ya uvumbuzi wa kisayansi. Lakini hata uwezo huo wa juu wa akili, kama hautaongozwa na Neno la Mungu, utatatizwa katika majaribio ya kuchunguza uhusiano wa sayansi na Ufunuo.

Mwanadamu anajua kwa sehemu, ufahamu wake siyo mkamilifu; Kwa hiyo wengi hawawezi kupatanisha mitazamo yao ya sayansi na Maandiko. Wengi wanazikubali nadharia tu kama kweli za kisayansi, na wanadhani kuwa Neno la Mungu linapaswa kuhakikiwa kwa, "...elimu iitwayo elimu kwa uongo" 1 Timotheo 6:20. Kwa sababu hawawezi kumwelezea Mwumbaji na kazi zake kwa kutumia sheria za asili; historia ya Biblia imechukuliwa kuwa haiaminiki. Wale wanaotilia mashaka Agano la Kale na Agano Jipya, wanapiga hatua nyingine mbele na kutilia mashaka uwepo wa Mungu. Kwa sababu wameacha nanga yao, wamebaki wakigonga mwamba wa kutoamini.

Ni kazi ya usanifu wa udanganyifu wa Shetani kuwafanya [322]

wanadamu waendelee kukisia maana ya mambo ambayo Mungu hakuyafunua. Lusifa hakuridhika kwa sababu siri zote za makusudi ya Mungu hakupewa yeye, na alipuuzia kile kilichokuwa kimefunuliwa. Na sasa anatafuta kuwajaza wanadamu roho ile ile na kuwaongoza wao pia kutozingatia amri za Mungu.

Kwa kadiri mafundisho yasiyokuwa ya kiroho na yenye msukumo kidogo wa kujikana nafsi yanavyozidi kutolewa, ndivyo yatakavyopendwa na kupokelewa kwa nguvu zaidi. Shetani yuko tayari kutimiza shauku ya moyo, na kushawishi hadi uongo utakapochukua nafasi ya ukweli. Hivyo ndivyo ilivyokua hadi utawala wa Papa ukapata nguvu juu ya mioyo ya wanadamu. Na kwa kuukataa ukweli kwa vile unahusisha msalaba; Waprotestanti wanaifuata njia ie ile. Wote wanaojifunza urahisi na sera, ili wasitofautiane na dunia; wataachwa kupokea, "uharibifu usiokawia" 2 Petro 2:1. Yule anayetishwa kwa udanganyifu mmoja ataupata mwingine mara moja, "Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu." 2 Wathesalonike 2:1,12.

## Makosa ya Hatari

Miongoni mwa mawakala wenye kufanikiwa sana wa yule mdanganyifu mkuu ni watendaji wa miujiza ya umizimu. Kwa kadiri wanadamu wanavyoukataa ukweli; wanakuwa mawindo ya udanganyifu.

Kosa lingine ni fundisho linalopinga Uungu Wakristo, ikidaiwa kuwa hakuwepo kabla ya kuja hapa duniani. Nadharia hii hukinzana na kauli za Mwokozi wetu kuhusu uhusiano wake na Baba na uwepo wake kabla ya kuja duniani. Huidhoofisha imani katika Biblia kama Ufunuo kutoka kwa Mungu. Kama wanadamu wakiukataa ushuhuda wa Maandiko juu ya Uungu Wakristo, ni bure kuhojiana nao; hakuna hoja, hata iwe nzuri kiasi gani, itakayowashawishi. Hakuna mtu anayelishikilia kosa hili anayeweza kuwa na utambuzi wa kweli Wakristo au juu ya mpango wa Mungu wa ukombozi wa mwanadamu.

[323] Kosa lingine ni imani kuwa Shetani sio kiumbe halisi mwenye nafsi, na kwamba jina hili linapotumika kwenye Maandiko linawakilisha tu mawazo na tamaa mbaya za wanadamu.

Fundisho linalosema kuwa kuja kwa Yesu mara ya pili ni kuja kwa kila mmoja anapokufa ni mbinu ya kuzipotosha akili juu ya kuja kwake na mawingu ya mbinguni. Shetani amekuwa akisema, "Tazama yumo nyumbani" (Angalia 24:23-26) na wengi wamepotea kwa kuukubali udanganyifu huu.

Halafu, wanasayansi wanadai kuwa hakuwezi kuwa na jibu halisi kwa maombi; hili litakuwa ni uvunjaji wa kanuni kwani miujiza ni nadharia tu. Wanasema, ulimwengu unaongozwa na sheria ambazo tayari zipo, na kuwa Mungu mwenyewe hafanyi jambo lolote kinyume na sheria hizo. Na hivyo husema kuwa Mungu anabanwa na sheria zake mwenyewe (kana kwamba sheria za Mungu zingeondoa uhuru wa Mungu). Mafundisho kama hayo yanapingana na ushuhuda wa Maandiko.

Je, miujiza haikutendwa na Kristo na mitume wake?. Mwokozi yule yule yuko tayari kuyasikiliza maombi ya imani kama alivyofanya alipokuwepo kimwili miongoni mwa wanadamu. Wanadamu wanashirikiana na Mungu. Ni sehemu ya mpango wa Mungu kutupatia tunachoomba kwa imani, ambacho hangetupatia kama tusingeomba.

### Mipaka ya Neno

Mafundisho ya uongo miongoni mwa makanisa yanaondoa mipaka iliyowekwa na Neno la Mungu. Wachache; hukoma kuendelea mbele kwa kukataa kanuni moja ya ukweli. Watu walio wengi huweka kando kanuni moja ya ukweli baada ya nyingine mwisho wanageuka kuwa makafiri.

Makosa yatokanayo na teolojia inayopendwa yamezifanya roho nyingi kuwa na nadharia ya kushuku. Ni vigumu kwake kuyakubali mafundisho yanayopingana na hisia za mtu juu ya haki, rehema, na ukarimu. Kwa sababu haya yanaletwa kama mafundisho ya Biblia, anakataa kuyapokea kama Neno la Mungu.

Neno la Mungu limcangaliwa kwa mashaka kwa sababu [324]
linaishutumu na kuihukumu dhambi. Wale ambao hawako tayari kulitii wanajitahidi kuyatupilia mbali mamlaka yake. Wengi wanaamua kutoamini ili kuhalalisha kuacha kutimiza wajibu wao. Wengine, kwa kupenda anasa, hawawezi kukamilisha jambo lolote

linalohitaji kujikana nafsi; wanapata sifa ya kuwa na hekima ya hali ya juu kwa kuikosoa Biblia.

Wengi wanahisi ni jambo bora kuwa upande wa kutoamini, mashaka, na ukafiri. Lakini nyuma ya mwonekano wa unyofu kutaonekana kujitumainia nafsi na majivuno. Wengi wanafurahia kutafuta kitu fulani ndani ya Maandiko kitakachoikanganya mioyo ya wengine. Baadhi huanza na kutetea uongo kwa sababu tu ya kupenda mabishano. Lakini baada ya kueleza waziwazi kutoamini kwao, huona kuwa ni vema wakiendeleza misimamo yao. Na hivyo wanajiunga na waovu.

## Ushahidi wa Kutosha

Katika Neno lake, Mungu ameweka ushahidi wa kutosha kuonesha kuwa limetoka kwake. Lakini akili zenye ukomo hazina uwezo wa kufahamu kikamilifu makusudi ya Yule Asiye na ukomo. "Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani!" Warumi 11:33. Tunaweza kutambua pendo lisilo na mipaka na rehema vikiwa vimeungana na uwezo usio na kikomo. Baba yetu wa mbinguni atatufunulia mambo mengi kwa ajili ya manufaa yetu; zaidi ya hayo tunapaswa kuamini Mkono wa Mwenyezi, Moyo uliojaa upcndo.

Mungu hataondoa visingizio vyote vinavyosabisha kutoamini. Wote wanaotafuta visingizio juu ya mashaka yao watavipata. Na wale wanaokataa kutii hadi kila kipingamizi kimeondolewa, hawataweza kuja kwenye nuru. Moyo ambao haujaongoka una uadui na Mungu. Lakini imani ni uvuvio wa Roho Mtakatifu na itastawi kwa kadiri inavyotunzwa. Hakuna awezaye kuwa na imani imara bila jitihada za makusudi. Ikiwa wanadamu watajiendekeza kuwa wakosoaji bila sababu; mashaka yatapata nguvu zaidi.

Lakini wale wanaoona shaka na kutoamini uhakika wa neema yake hawamheshimUkristo. Hao ni miti isiyozaa, inayouzuia
[325] mwanga wa jua usiifikie mimea mingine, idumae na kufa chini ya kivuli chenye baridi. Kazi za maisha ya watu hawa zitakuwa ushuhuda wa daima dhidi yao.

Ipo njia moja tu kwa wale wanaotafuta kwa uaminifu kuwa huru dhidi ya shaka. Badala ya kukitilia shaka wasichokielewa, hebu

waitii ile nuru ambayo tayari wanayo na wataipokea nuru kubwa zaidi.

Shetani anaweza kuleta uongo unaolingana kwa karibu sana na ukweli ili awadanganye wale wanaohiari kudanganyika, wanaotamani kuepuka kujitoa kwa ajili ya ukweli. Lakini hawezi kuidhibiti roho moja inayotamani kwa uaminifu, na kwa gharama yoyote, kufahamu ukweli. Kristo ndiye kweli, "Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu." "Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo." Yohana 1:9; 7:1

Bwana anaruhusu watu wake wapate majaribu makali, siyo kwa sababu anaifurahia dhiki yao, lakini kwa sababu ni ya lazima kwa ajili ya ushindi wao wa mwisho. Kwa ajili ya utukufu wake, hawezi kuwakinga na majaribu, kwani lengo la majaribu ni kuwatayarisha kwa ajili ya kuvipinga vivutio vyote vya uovu. Watu waovu na maShetani hawawezi kuuondoa uwepo wa Mungu kutoka kwa watu wake endapo wataungama na kuziweka mbali dhambi zao na kuzidai ahadi zake. Kila jaribu, la wazi ama la siri, linaweza kupingwa kwa mafanikio, "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi." Zekaria 4:6

"Naye ni nani atakayewadhuru, mkiwa wenye juhudi katika mema?" lPetro 3:13. Shetani anajua vizuri kuwa roho moja dhaifu inayomtii Kristo ina nguvu kupita majeshi ya giza. Kwa hiyo anatafuta kuwavuta askari wa msalaba mbali na ngome yao yenye nguvu, huku akiwavizia, tayari kwa kuwaangamiza wote wanaojihatarisha kwenye uwanja wake. Ni kwa kumtegemea Mungu pekee na kuzitii amri zake zote ndipo tutakuwa salama.

Hakuna mwanadamu aliye salama kwa siku moja ama kwa saa [326]
moja asipofanya maombi. Umwombe Bwana akupe hekima ya kulifahamu Neno Lake. Shetani ni stadi wa kunukuu Maandiko, huweka fasiri yake kwenye mafungu ambayo anataka kutufanya tujikwae. Inatupasakujifunza kwa unyenyekevu wa moyo. Wakati ambapo ni lazima tukeshe daima dhidi ya mbinu za Shetani, ni lazima pia tuombe kwa imani bila kukoma: "Na usitutie majaribuni." Mathayo 6:1.

## [327] Sura Ya 33 - Baada Ya Kifo Kinachotokea Nl Nini ?

Shetani, ambaye alichochea uasi mbinguni, alitamani kuwashawishi wakazi wa dunia katika vita vyake dhidi ya Mungu. Adamu na Hawa walikuwa na furaha kamilifu kwa kuitii sheria ya Mungu-ushuhuda wa daima dhidi ya madai aliyoyatoa Shetani mbinguni kwamba sheria ya Mungu ilikuwa ya ukandamizaji. Shetani alikuwa ameazimu kusababisha anguko lao, ili aimiliki dunia, na auanzishe ufalme wake hapa kinyume na Aliye juu.

Adamu na Hawa walikuwa wameonywa kuhusu adui huyu wa hatari, lakini alitenda kwa kificho, akilifunika kusudi lake. Akimtumia nyoka kuwa chombo chake, wakati huo akiwa kiumbe mwenye mwonekano wa kuvutia, alimwuliza Hawa: "Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?" Hawa alijihatarisha kwa kuzungumza naye na akawa mhanga wa hila zake: "Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya" Mwanzo 3:1-5.

Hawa akakubali kushindwa, na kwa mvuto wake Adamu akashawishika kuingia dhambini. Waliyakubali maneno ya nyoka; walimwonea shaka Mwumbaji wao na walifikiri kuwa alikuwa anauwekea mipaka uhuru wao.

Lakini kwa Adamu maneno; "kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.", yalikuwa yanamaanisha nini?. Je, angeingizwa kwenye maisha ya juu zaidi? Adamu hakuona kuwa hii ndiyo maana ya kauli ya Mungu. Mungu alitamka kuwa mwanadamu alilazimika kurudi mavumbini ikiwa ni adhabu ya dhambi zake: "...u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi." Mwanzo 3:19. Maneno ya Shetani, "...mtafumbuliwa macho", yalithibitika kuwa kweli kwa maana hii tu: macho yao yalifum-

buliwa ili watambue upuuzi wao. Waliyajua mabaya na wakalionja tunda chungu la uasi.

Mti wa uzima ulikuwa na uwezo wa kuudumisha uhai. Adamu [328] angeweza kuendelea kuwa na fursa ya uhuru wa kuufikia mti huu na kuwa hai milele, lakini alipotenda dhambi alizuiliwa mti wa uzima na kuwa mwenye kupatwa na mauti. Hali ya kutokufa iliondolewa kwa sababu ya uasi. Hakungekuwa na tumaini kwa jamii iliyoanguka, endapo Mungu, kwa njia ya kafara ya Mwanawe, asingeisogeze hali ya kutokufa karibu nao. Wakati dhambi iliwafikia, “watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi,” Kristo aliufunua “uzima na hali ya kutokufa, kwa njia ya Injili.” Ni kwa njia ya Kristo pekee hali ya kutokufa inaweza kupatikana. “Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima.” Warumi 5:12; 2Timotheo 1:10; Yohana 3:36.

## Udanganyifu Mkuu

Aliyeahidi uzima pasipo utii alikuwa ndiye mdanganyifu mkuu. Na tamko la nyoka pale Edeni kuwa, “Hakika hamtakufa.”- Ilikuwa ndiyo hotuba ya kwanza kuwahi kuhubiriwa juu ya hali ya kutokufa kwa roho. Lakini tamko hili, likiwa na msingi wake katika mamlaka ya Shetani pekee, linasikika kutoka majukwaani na kupokelewa haraka na wanadamu wengi kama walivyofanya wazazi wetu wa kwanza. Kauli ya Mungu, “Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa” (Ezekieli 18:20), imegeuzwa kumaanisha kuwa, Roho itendayo dhambi, haitakufa, bali itaishi milele. Endapo mwanadamu baada ya anguko, angepewa uhuru wa kula kutoka kwenye mti wa uzima, dhambi ingekuwa imepata hali ya kutokufa. Lakini hakuna hata mmoja kutoka kwenye familia ya Adamu aliyeruhusiwa kula tunda liletalo uzima. Kwa hiyo hakuna mdhambi mwenye hali ya kutokufa.

Baada ya anguko, Shetani aliwataka malaika zake kufundisha imani juu ya hali ya asili ya mwanadamu ya kutokufa. Baada ya kuwashawishi watu kuupokea upotovu huu; walitakiwa kuwaongoza kwenye hitimisho kuwa mwenye dhambi angeishi milele katika mateso. Sasa mkuu wa giza anamwelezea Mungu kuwa ni dikteta mwenye kulipa kisasi, akitangaza kuwa Mungu, huwatumbukiza ndani ya jahannamu wote wasiompendeza na kwamba wanapoun-

gua kwenye moto wa milele, Mwumbaji wao huwachungulia na kuridhika. Hivyo mdhalimu huyu mkuu, anamvisha mfadhili wa wanadamu tabia zake. Ukatili ni tabia ya kishetani. Mungu ni upendo. Shetani ni adui ambaye anawashawishi wanadamu kutenda dhambi na kisha akiweza, anawaangamiza. Ni Mgongano
[329] ulioje kati ya upendo, rehema, na haki; na fundisho linalodai kuwa waovu waliokufa wanateseka kwenye moto wa milele na kwamba kwa dhambi walizotenda katika maisha haya mafupi hapa duniani, wataendelea kuteseka kwa kadiri Mungu aishivyo!

Je, fundisho hili linapatikana wapi ndani ya Neno la Mungu? Je, hisia za ubinadamu wa kawaida zigeuke kuwa ukatili na ushenzi? Hasha, hilo siyo fundisho la kitabu cha Mungu. "Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi. Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa." Ezekieli 33:11

Je, Mungu anafurahia kuyaangalia mateso yasiyokoma? Je, anaburudishwana sauti za maumivu na vilio vya viumbe wanaoteseka ambao anawashikilia katika miali ya moto? Je, sauti hizi za kuchukiza zaweza kuwa wimbo katika sikio la Mungu mwenye upendo usio na mwisho? Oh! kufuru ya kutisha! Utukufu wa Mungu hauongezwi kwa kudumisha dhambi katika muda usio na mwisho.

## Fundisho Potovu la Mateso ya Milele

Uovu umeletwa na fundisho potovu la mateso ya milele. Dini ya Biblia, iliyojaa upendo na wema imetiwa giza kwa mapokeo potovu na kufunikwa na vitisho. Shetani ameipotosha tabia ya Mungu. Mwumbaji wetu mwenye rehema anaogopwa, anahofiwa, na hata kuchukiwa. Mitazamo ya Mungu anayeogofya iliyosambaa kote duniani kutokana na mafundisho ya kwenye mimbara; imewafanya watu wengi kuwa na mashaka na makafiri.

Mateso ya milele ni moja ya mafundisho ya uongo, mvinyo wa machukizo (Ufunuo 14:8; 17:2), ambao Babeli anayanywesha mataifa. Watumishi Wakristo waliukubali uasi huu kutoka Kanisa la Roma kama walivyokuwa wameipokea sabato ya uongo. Kama tukiliacha Neno la Mungu na kuyakubali mafundisho ya uongo kwa vile baba zetu waliyafundisha, tunaangukia kwenye hukumu

iliyotangazwa juu ya Babeli; tunakunywa mvinyo wa machukizo yake.

Kundi kubwa la watu wamevutwa kuelekea kwenye kosa lililo kinyume. Wanaona kuwa Maandiko yanamwakilisha Mungu kuwa ni mwenye upendo na huruma na hawaamini kuwa atawapeleka [330] viumbe wake kwenye moto wa milele. Wanashikilia fundisho kuwa roho kwa asili ina hali ya kutokufa; wanahitimisha kuwa wanadamu wote wataokolewa. Kwa hiyo mwenye dhambi anaweza kuishi kwa anasa za ubinafsi, akipuuza matakwa ya Mungu, na bado akapokelewa naye. Fundisho la aina hii, linalotambua rehema ya Mungu huku likipuuza haki yake; linafurahisha tamaa ya mwili.

## Wokovu wa Jumla Siyo Fundisho la Maandiko

Wanaoamini juu ya wokovu wa jumla wanayapotosha Maandiko. Wanaodai kuwa watumishi Wakristo wanautangaza uongo uliotamkwa na nyoka pale Edeni kwa kurudia-rudia, “Hamtakufa hakika.” “siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu.” Anatamka kuwa mdhambi atiaye aibu - muuaji, mwizi, -mzinzi - baada ya kifo wataingia kwenye furaha kamili ya hali ya kutokufa. Uongo unaopendelewa kabisa, ulifaa kuupendeza moyo wenye tamaa ya mwili.

Kama ingekuwa ni kweli kuwa katika saa ya mauti watu wote wanakwenda moja kwa moja mbinguni, huenda tungekitamani kifo badala ya uzima. Wengi wamekuwa wakiongozwa na fundisho hili kujiua. Baada ya kuchanganyikiwa na kuvunjika moyo, inaonekana kuwa ni rahisi kuukatisha uhai na kupaa hadi kwenye raha kamili ulimwengu wa milele.

Ndani ya Neno lake, Mungu ametoa ushahidi wazi kuwa atawaadhibu wavunjaji wa sheria yake. Je, Yeye ana rehema kubwa mno kiasi cha kushindwa kumtendea haki mwenye dhambi? Uangalie msalaba wa Kalvari. Kifo cha Mwana wa Mungu kinashuhudia kuwa, “mshahara wa dhambi ni mauti” (Warumi 6:23), ili kila uvunjaji wa sheria ya Mungu upate adhabu inayostahili. Kristo asiye na dhambi alikuwa dhambi kwa ajili ya mwanadamu. Aliibeba hatia ya dhambi na uso wa Baba yake ulikuwa umefichwa hadi moyo wake ulipovunjika na uhai wake kuangamizwa - haya yote ni kwa ajili ya kumwokoa mwenye dhambi. Na kila mwanadamu anayekataa

kuupokea upatanisho uliopatikana kwa gharama kubwa kiasi hiki, ni lazima abebe mwenyewe hatia na adhabu ya dhambi.

[331]

## Masharti Vamewekwa Bayana

“Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima, bure” Ahadi hii ni kwa wale tu wenye kiu. “Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu.” Ufunuo 21:6,7 Masharti yamebainishwa. Ili kupata urithi wa vitu vyote ni lazima tuishinde dhambi.

“Haitakuwa heri kwa mwovu” Mhubiri 8:13. Mwenye dhambi anajiwekea mwenyewe, “akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu; atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake, “dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu.” Warumi 2:5, 6, 9.

“Hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme Wakristo na Mungu.” “Heri wazifuao nguo zao, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake. Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya.” Waefeso 5:5; Ufunuo 22:14, 15

Mungu amewapa wanadamu tamko juu ya kanuni yake ya kushughulikia dhambi. “Na wote wasio haki atawaangamiza.” “Wakosaji wataangamizwa pamoja, Wasio haki mwisho wao wataharibiwa.” Zaburi 145:20; 37:38. Mamlaka ya serikali ya Mungu itakomesha uasi, lakini adhabu ya haki italingana na tabia ya Mungu, mwenye rehema na ukarimu.

Mungu hashurutishi dhamiri. Mungu hapendezwi na utii wa kitumwa. Anatamani kwamba viumbe walio kazi ya mikono yake wampende kwa sababu anastahili upendo. Anawataka wamtii Yeye kwa sababu wana akili ya kuitambua hekima yake, haki, na ukarimu wake.

Kanuni za serikali ya mbinguni zinapatana na agizo la Mwokozi, “Wapendeni adui zenu” Mathayo 5:44. Mungu huwatendea haki waovu kwa faida ya ulimwengu na hata kwa manufaa ya wale ambao hukumu yake inawaangukia. Anaweza kuwapa furaha akipenda. Anawazingira kwa thawabu za upendo wake na anawafuata akiwapa rehema; lakini wanalipuuza pendo lake, wakiibatilisha sheria

yake, na kuitupa rehema yake. Daima wakipokea vipawa vyake, hawamheshimu mtoaji. Mungu anauvumilia ukaidi wao kwa muda mrefu; lakini je, atawafunga pingu waasi hawa ili wawe upande wake na kuwalazimisha kutenda mapenzi yake? [332]

## Hawajajitayarisha Kuingia Mbinguni

Wale ambao wamemchagua Shetani kuwa kiongozi wao, hawajajitayarisha kuingia kwenye uwepo wa Mungu. Majivuno, udanganyifu, tamaa ya mwili, ukatili vimekazwa katika tabia zao. Je, wanaweza kuingia mbinguni na kuishi milele na wale ambao walivachukia duniani? Ukweli hautakubalika kwa mtu mwongo, upole hautakidhi haja ya kujitukuza nafsi; usafi haukubaliki kwa mtoa rushwa; upendo usiotaka faida haumvutii mbinafsi. Ni fursa gani ambayo mbingu zingetoa kwa wale ambao wametopea kwenye matakwa ya ubinafsi?

Je, wale ambao mioyo yao imejazwa na chuki kwa Mungu, na wanaochukizwa na ukweli na utakatifu, wataweza kuchangamana na umati wa mbinguni na kuimba pamoja nyimbo za sifa? Walipewa miaka ya matarajio lakini, hawakuzifunza akili zao kupenda usafi. Hawakujifunza lugha ya mbinguni. Na sasa wamechelewa.

Maisha ya uasi dhidi ya Mungu yamewakosesha kuingia mbinguni. Utakatifu na amani yake vitakuwa ni mateso kwao; utukufu wa Mungu utakuwa ni moto ulao. Watatamani kukimbia kutoka ile sehemu takatifu, na wataomba uharibifu uwafike, ili angalau wasiuone uso wa Yeye aliyekufa ili awakomboe. Hatima ya waovu inapangwa kutokana na uchaguzi wao. Kutokuwepo kwao mbinguni ni hiari yao, na ni haki na rehema kwa upande wa Mungu. Kama yalivyo maji ya mafuriko, moto wa siku ile kuu unatangaza hukumu ya Mungu kwamba waovu hawatapona. Mapenzi yao waliyatimiza katika uasi. Uhai utakapokuwa umekoma, wamechelewa, hawawezi kuyageuza mawazo yao kutoka kwenye uasi kwenda kwenye utii, kutoka kwenye chuki kwenda kwenye upendo.

## Mshahara wa Dhambi

"Mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" Wakati ambapo uzima

ni urithi wa wenye haki, mauti ni fungu la waovu. “Mauti ya pili” ni kinyume cha uzima wa milele. Warumi 6:23; Ufunuo 20:14.

[333] Kama matokeo ya dhambi ya Adamu, mauti imeifikia jamii yote ya wanadamu. Wote wanashushwa kaburini kwa namna ile ile. Na kwa kupitia mpango wa wokovu, wote watatolewa kutoka katika makaburi yao: kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia.”

“Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.” Lakini kuna tofauti baina ya makundi mawili yatakayofufuliwa: “...watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.”Matendo 24:15; 1 Wakorintho 15:22; Yohana 5:28, 29.

## Ufufuo wa Kwanza

Wale “wahesabiwao kuwa wamestahili” ufufuo wa uzima wana “Heri, na mtakatifu” “...juu ya hao mauti ya pili haina nguvu” Luka 20:35; Ufunuo 20:6. Lakini wale ambao hawatapokea msamaha kupitia toba na imani “mshahara wa dhambi” adhabu “kwa kadiri ya matendo yao” wataishia katika “mauti ya pili”

Kwa vile haitawezekana Mungu kumwokoa mwenye dhambi katika dhambi zake, atamnyang’anya uzima ambao uasi wake ulimwondoa kwa huo, atathibitika mwenyewe kuwa hakuustahili. “...bado kitambo kidogo asiye haki hatakuwapo, Utapaangalia mahali pake wala hatakuwapo.” “...nao watakuwa kana kwamba hawakuwa kamwe.” Zaburi 37:10; Obadia 16. Wanazama bila tumaini na kusahauliwa milele.

Hapo ndipo utakapofika mwisho wa dhambi. “Umemwaangamiza mdhalimu; Umelifuta jina lao milele na milele; Adui wamekoma na kuachwa ukiwa milele” Zaburi 9:5,6. Yohana, katika Ufunuo alisikia wimbo wa sifa wa watu wote ambao mpangilio wa sauti zake haujaharibiwa. Hakuna roho zilizopotea zitakazomkufuru Mungu zitakazokuwa zikitapatapa kwenye mateso yasiyokwisha. Hakuna viumbe wanyonge motoni ambao sauti za vilio vyao zitachangamana na nyimbo za waliookolewa.

[334] Juu ya uongo wa hali ya asili ya kutokufa kuna fundisho la hali ya kujitambua baada ya kufa. Kama ilivyo kwa somo la mateso

ya milele, liko kinyume na Maandiko, ufahamu, na hisia zetu za ubinadamu.

Kwa mujibu wa imani inayopendelewa na wengi, waliokombolewa walioko mbinguni wanajua kila kinachoendelea hapa duniani. Lakini inawezekanaje wafu wapate furaha wakijua taabu za walio hai, kuwaona wakivumilia huzuni, kuvunjika moyo, na maumivu makali ya maisha? Na inachukiza kiasi gani imani kwamba mara tu pumzi inapotoka katika mwili, roho ya yule aliyekufa inakwenda kwenye moto wa milele!

Maandiko yanasemaje? Mtu akifa hana ufahamu: "Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, Siku hiyo mawazo yake yapotea." "walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno Io lote... Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote lililofanyika chini ya jua." "Kwa kuwa kuzimu hakuwezi kukusifu; mauti haiwezi kukuadhimisha; Wale washukao shimoni hawawezi kuitarajia kweli yako. Aliye hai, naam, aliye hai, ndiye atakayekusifu, kama mimi leo" ˜ ..mautini hapana kumbukumbu lako; Katika kuzimu ni nani atakayekushukuru?" Zaburi 146:4; Mhubiri 9:5, 6; lsaya 38:18, 19; Zaburi 6:5.

Katika siku ya Pentekoste Petro alitamka kuwa Daudi "alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo." "Maana Daudi hakupanda mbinguni." Ukweli kwamba Daudi atasalia kaburini hadi siku ya ufufuo unathibitisha kuwa wenye haki hawaendi mbinguni baada ya kifo.

Paulo alisema: "Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu.

Na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea." lWakorintho 15:16-18. Ikiwa kwa miaka 4,000 wenye haki walikwenda moja kwa moja mbinguni baada ya kifo, Paulo angewezaje kusema ikiwa hakuna ufufuo, "...wao nao waliolala katika Kristo wamepotea."?

Alipokaribia kuwaacha wanafunzi wake, Yesu hakuwaambia kuwa bado kitambo wangeenda kwake: "...naenda kuwaandalia mahali." Alisema. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu." Yohana 14:2,3. Paulo anaongeza ku- [335]
tuambia, "Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja

na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele." Na anaongeza. "Basi, farijianeni kwa maneno hayo."l Wathesalonike 4:16-18. Bwana atakapokuja pingu za kaburi zitavunjika na "waliokufa katika Kristo" watafufuliwa ili waishi milele.

Watu wote watahukumiwa sawa sawa na mambo yaliyoandikwa katika vitabu na kupewa thawabu kama matendo yao yalivyokuwa. Hukumu hii haitafanyika siku ya kufa. "Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki" "Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote." Matendo 17:31; Yuda 14,15.

Lakini ikiwa wafu tayari wanafurahia mbinguni au wanateseka kwenye moto wa jahannamu, , hukumu ijayo ina kazi gani? Neno la Mungu linaweza kueleweka na watu wa kawaida. Lakini ni nini ambacho akili iliyo wazi itakiona, iwe hekima au haki katika nadharia iliyopo sasa? Je, wenye haki wataambiwa, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu,... ingia katika furaha ya Bwana wako," baada ya kuishi mbele ya uso wake kwa muda mrefu? Je, waovu wataitwa watoke kwenye mateso ili waipokee hukumu kutoka kwa hakimu, "Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele"? Mathayo 25:21, 41.

Nadharia ya hali ya kutokufa kwa roho ilikuwa moja ya mafundisho ya uongo ambayo Kanisa la Roma liliyaazima kutoka kwenye upagani. Luther aliliweka kundi moja na, "Kauli za uongo wa ajabu na wa kutisha ambazo zinaunda sehemu ya rundo la nyaraka za Mapapa wa Kanisa la Roma." [234] Biblia inafundisha kwamba wafu wanalala hadi siku ya ufufuo.

Pumziko lenye baraka kwa wenye haki waliochoka! Muda, hata kama utakuwa mrefu ama mfupi; ni kitambo tu kwao. Watalala;
[336] na wataamshwa kwa tarumbeta ya Mungu kwenye utukufu wa kutokufa. "...maana parapanda italia, na wafu watafufiiliwa, wasiwe na uharibifu,... Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile

[234] E. Petavel, *The Problem of Immortality*, p.255.

neno lililoandikwa, Mauti imemezwa kwa kushinda.” 1 Wakorintho 15:52-54.

Wataamshwa kutoka kwenye usingizi wao, wataanzia kufikiri pale walipoishia. Hisia za mwisho zilikuwa ni maumivu ya kifo; wazo la mwisho, kwamba walikuwa wanaangukia chini ya mamlaka ya mauti. Watakapoamka kutoka kaburini, wazo lao la kwanza la furaha litasikika katika kelele za ushindi: “Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?” lWakorintho 15:55.

[337] 

# Sura Ya 34 - Roho Nl Nani Katika Imani Ya Mizimu?

Fundisho la hali ya asili ya kutokufa,-awali liliazimwa kutoka kwenye falsafa ya wapagani na wakati wa giza kuu la uasi lilijumuishwa kwenye imani ya Ukristo, sasa limechukua nafasi ya ukweli kwamba, "...wafu hawajui neno lolote". Mhubiri 9:5. Watu wengi wanaamini kuwa roho za wafu ndizo, "...roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?" Waebrania 1:4.

Imani kwamba roho za wafu zinarudi kuwahudumia waliohai imefungua mlango kwa ajili ya imani ya kisasa ya mizimu. Ikiwa wafu wanapata fursa ya kuwa na maarifa yanayozidi yale waliyokuwa nayo wakiwa hai, kwa nini wasirudi duniani ili wawafundishe walio hai? Ikiwa roho za wafu huvinjari juu ya rafiki zao duniani, kwa nini zisiwasiliane nao? Ni kwa namna gani wale wanaoamini kuwa mwanadamu anajitambua baada ya kifo wanaikataa "nuru ya Mungu" iliyoletwa na roho wenye utukufu? Hii ni njia inayotiliwa maanani kuwa ni takatifu ambayo kwayo Shetani anafanya kazi. Malaika walioanguka wanaonekana kama wajumbe kutoka katika ulimwengu wa roho.

Mkuu wa uovu anao uwezo wa kuleta mbele ya wanadamu mwonekano wa rafiki zao waliokufa. Sura ya bandia itaonekana ni kamilifu, imetengenezwa kwa ubainifu wa ajabu. Wengi wanafarijika kwa uhakika kwamba wapendwa wao waliokufa wana fursa ya kuwa mbinguni. Pasipo hisia za hatari wanasikiliza, "roho zidanganyazo" lTimotheo 4:1

Wale waliokufa pasipo matayarisho wanadai kuwa wana furaha na wanashika nyadhifa za juu mbinguni. Hawa wageni wakujifanya kutoka kwenye ulimwengu wa roho wakati mwingine wanatoa maonyo ambayo yanathibitika kuwa ni sahihi. Kisha, kwa sababu wameaminika, wanaleta mafundisho yanayoshusha hadhi ya Maandiko. Ukweli kwamba wanatoa baadhi ya kauli za kweli na pengine kubashiri matukio ya siku za usoni unawafanya kuaminika,

na mafundisho yao potovu kukubalika. Sheria ya Mungu imewekwa kando, Roho wa neema amedhihakiwa. Hizo roho zinaukataa Uungu Wakristo na kumweka Mwumbaji daraja moja na wao. Wakati ni uk- [338] weli kwamba matokeo ya hila yamekuwa na ushawishi kana kwamba ni udhihirisho wa kweli, kumekuwa na maonesho wazi ya nguvu za miujiza, ambazo ni kazi za moja kwa moja za Shetani. Wengi wanaamini kuwa imani ya mizimu ni ulaghai tu wa wanadamu. Watakapokutana uso kwa uso na udhihirisho ambao watauona kama miujiza, watadanganyika na kuukubali kuwa ni uwezo mkuu ya Mungu.

Kwa msaada wa kishetani wachawi wa Farao waliiga kazi ya Mungu kwa udanganyifu. Angalia Kutoka 7:10-12. Paulo anashuhudia kuwa kuja kwa Bwana kutatanguliwa na "kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea" 2Wathesalonike 2:9,10. Na Yohana anatamka kuwa: "Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya" Ufunuo 13:13,14. Hapa si ulaghai tu wa wanadamu uliotabiriwa. Wanadamu wanadanganyika kwa miujiza ambayo mawakala wa Shetani wanatenda, na siyo ile wanayojifanya kuitenda.

### Ushawishi wa Shetani kwa Wasomi

Kwa wenye elimu na waungwana, mkuu wa giza anaipeleka imani ya mizimu kwa kutumia mbinu makini na za kitaalamu zaidi. Anapendelea ubunifu wenye mandhari za kupendeza na mwonekano wenye ushawishi wa upendo na ukarimu. Anawaongoza wanadamu kujivunia sana hekima yao kiasi kwamba ndani ya mioyo yao wanamdhihaki Yule wa milele.

Shetani anawalaghai wanadamu sasa kama alivyowalaghai Adamu na Hawa pale Edeni kwa kuchochea shauku ya kujiinua nafsi. "mtakuwa kama Mungu" anatangaza, "mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:5. Imani ya mizimu inafundisha "kuwa mwanadamu ni kiumbe anayekua...kuelekea kwenye Uungu." Na tena: "Hukumu itakuwa sahihi, kwa sababu ni hukumu ya nafsi...kiti cha enzi kipo

ndani yako" Na mwingine anatangaza kuwa: "Kiumbe yeyote ambaye ni mwenye haki na mkamilifu ni Kristo."

Shetani ameiweka asili ya dhambi ya mwanadamu mwenyewe kuwa ndiyo kanuni pekee ya uamuzi. Haya ni maendeleo ya kuelekea chini na siyo juu. Mwanadamu hataweza kwenda juu
[339] zaidi ya kiwango chake cha usafi na wema. Kama nafsi ndiyo kiwango chake cha juu kabisa, hataweza kufikia kiwango chochote cha juu zaidi. Neema ya Mungu pekee ina uwezo wa kumwinua mwanadamu. Akiachwa mwenyewe, mwelekeo wake lazima utakuwa ni wa kwenda chini.

### Ushawishi kwa Wanaopenda Anasa

Kwa wasiojizuia nafsi, wanaopenda anasa, wenye tamaa ya mwili, imani ya mizimu inaleta mitego isiyo na ustadi mkubwa. Katika hali zake za kawaida wanatafuta kile kinachopatana na mielekeo yao. Shetani anaziwekea alama dhambi ambazo kila mwanadamu huelekea kuzitenda na kisha anahakikisha kuwa fursa hazitakosekana ili kuyatukuza mazoea. Anawajaribu wanadamu kupitia kutokuwa na kiasi ili kudhoofisha uwezo wa kimwili, kiakili, na kimaadili. Anawaangamiza watu wengi kupitia uendekezaji wa tamaa, na kuukatili mwili. Ili kukamilisha kazi yake, roho wanatamka kuwa "elimu ya kweli inamweka mwanadamu juu ya sheria yote"; kwamba "chochote kilichopo, ni sahihi" kwamba "Mungu hahukumu"; na kwamba "dhambi zote...si hatia." Wakati watu wanapoamini kuwa tamaa ndiyo kanuni ya juu zaidi, kwamba uhuru ni kibali cha mtu kufanya kile atakacho, kwamba mwanadamu anawajibika kwake mwenyewe tu, ni nani atakayeshangaa kuona uovu unafurika kila mahali? Watu wengi kwa uchu wanakubali vishawishi vya tamaa. Shetani anawanasa kwenye wavu wake wengi wa wale wanaokiri kumfuata Kristo.

Lakini Mungu ametoa nuru ya kutosha kugundua mitego. Msingi halisi wa imani ya mizimu unapingana na Maandiko. Biblia inatamka kuwa wafu hawajui neno lolote, kwamba mawazo yao yametoweka; hawana sehemu katika furaha ama huzuni za walio hai.

Zaidi ya hayo, Mungu amekataza mawasiliano ya udanganyifu na roho zilizoanguka. Hizi "roho mashuhuri" kama walivyoitwa

hawa wageni kutoka ulimwengu mwingine, wametamkwa na Biblia kuwa ni "roho za maShetani." Angalia Hesabu 25:1-3; Zaburi 106:28; lWakorintho 10:20; Ufunuo 16:14. Ilikatazwa kuhusiana nao, adhabu ya kifo ilitolewa kwa wasiotii Walawi 19:31; 20:27. Lakini imani ya mizimu imeingia kwenye fani ya sayansi, imevamia makanisa, na inakubalika kwenye vyombo vya kutunga sheria, na hata ndani ya nyumba za wafalme. Udanganyifu huu mkubwa ni mbinu ya kuamsha kwa mbinu mapya za uchawi uliokuwa umeshutumiwa zamani.

Kwa kudai kuwa wanadamu waovu wapo mbinguni, Shetani [340] anauambia ulimwengu kuwa, "Haijalishi kama unamwamini au humwamini Mungu na Biblia, ishi upendavyo; mbinguni ni nyumba yako" Neno la Mungu linasema: "Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; watiao giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza" Isaya 5:20.

## Biblia Inawakilishwa Kama Riwaya

Mitume, wakiigizwa na roho zidanganyazo, wapo kwa ajili ya kuleta ukinzani dhidi ya yale waliyoandika walipokuwepo duniani. Shetani anaufanya ulimwengu uamini kuwa Biblia ni hadithi ya kubuni; kitabu chenye manufaa tangu mwanzo wa jamii ya wanadamu, lakini sasa kinaonekana kuwa hakifai kwa matumizi. Kitabu ambacho kitamhukumu yeye na wafuasi wake anakifanya kuwa duni, Mwokozi wa ulimwengu anamfanya kuwa si zaidi ya mwanadamu wa kawaida. Na wale wanaoamini juu ya udhihirisho wa roho, wanajaribu kufanya ionekane kuwa katika maisha ya Yesu, hakuna chochote ambacho ni muujiza. Wanatangaza kuwa miujiza yao inazidi sana kazi za Kristo.

Imani ya mizimu kwa sasa inachukua mtindo wa Ukristo. Lakini mafundisho yake hayawezi kukataliwa wala kufichwa. Katika sura yake ya sasa, ni udanganyifu hatari na wenye ustadi mkubwa. Imani hii inajidai sasa kumkubali Kristo na Biblia. Lakini Biblia inafasiliwa ili kuupendeza moyo ambao haujaongoka. Upendo unaelezwa sana kuwa ni tabia kuu ya Mungu, lakini umeshushwa hadhi na kuwa hisia dhaifu za moyo, na kufanya iwepo tofauti ndogo kati ya wema na uovu. Shutuma za Mungu juu ya dhambi, matakwa ya sheria yake takatifu, yamewekwa kando. Hadithi za

uongo zinawaongoza watu kuikataa Biblia kama msingi wa imani yao. Kristo kwa hakika anakanwa kama alivyokataliwa mwanzo, lakini udanganyifu haujagundulika.

Ni wachache wenye utambuzi halisi juu ya nguvu ya udanganyifu ya imani ya mizimu. Wengi wanashughulika nayo kwa manufaa ya udadisi tu. Wangejawa na hofu endapo wangefikiria juu ya wazo la kuwa wamepagawa na pepo. Lakini wanajihatarisha kwenye maeneo yaliyokatazwa, na mwangamizaji anaionesha uwezo wake juu
[341] yao kinyume na dhamiri zao. Hebu mara moja waelekeze akili zao upande wake, naye atawashikilia mateka. Hakuna kitakachowaokoa isipokuwa uwezo wa Mungu kwa kujibu maombi ya uaminifu.

Wale wote wanaolea dhambi zinazofahamika, wanakaribisha majaribu ya Shetani. Wanajitenga wenyewe kutoka kwa Mungu na kwenye ulinzi wa malaika zake. "Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong'ona; je! Haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? Je! Waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Isaya 8:19,20.

Kama wanadamu wangehiari kupokea ukweli juu ya asili ya mwanadamu na hali ya wafu, wangeweza kuona katika imani ya mizimu uwezo wa Shetani na miujiza ya uongo. Lakini wengi wanafumba macho wasione nuru, na Shetani husokota mitego yake kuwazunguka. "Kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa." Kwa hiyo, "Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo" 2Wathesalonike 2:10,11.

Wale wanaopinga imani ya mizimu wanamchokoza Shetani na malaika zake. Shetani hataachia uwanja hata inchi moja isipokuwa

kwakufukuzwa na wajumbe wa mbinguni. Anaweza kunukuu Maandiko na atapotosha mafundisho yake. Wale watakaosimama katika waakati huu wa hatari ni lazima waufahamu wenyewe ushuhuda wa Maandiko.

Hizo roho za maShetani zikichukua sura za ndugu au marafiki zitavuta huruma zetu na kutenda miujiza. Ni lazima tuwashinde kwa njia ya ukweli wa Biblia kwamba wafu hawajui neno lolote na wale wanaotokea ni roho za maShetani.

Wote ambao imani yao haijajengwa kwenye Neno la Mungu watadanganywa na kushindwa na Shetani. Shetani "hutenda kazi kwa udanganyifu wote wa udhalimu." na udanganyifli yake utaongezeka. Lakini wale wanaoitafuta kweli na kuitakasa mioyo yao kwa kutii watampata ndani yake Mungu wa kweli mlinzi wa hakika. Muda si mrefu, Mwokozi atamtuma kila malaika atoke mbinguni ili kuwalinda watu wake kama asivyoiacha nafsi moja inayomtumaini kushindwa na Shetani. Wale wanaojifariji wenyewe [342] kwa uhakika kwamba hakuna adhabu kwa mdhambi, anayeukataa ukweli ambao umewekwa na mbingu uwe ulinzi kwa ajili ya siku ya taabu, wataukubali uongo wa Shetani, udanganyifu wa kuigiza wa imani ya mizimu.

Wenye dhihaka wanakejeli tamko la Maandiko juu ya mpango wa wokovu na adhabu itakayowaangukia wanaoukataa ukweli. Wanazidhuru akili zilizo finyu sana, dhaifu, na zenye mapokeo potovu kuweza kutii matakwa ya sheria ya Mungu. Wamejitoa kikamilifu kwa mjaribu, wameungana naye kwa karibu na mioyoni wamejazwa roho yake, kiasi kwamba hawana nguvu ya kujinasua kwenye mtego wake.

Msingi wa kazi ya Shetani uliwekwa juu ya uthibitisho aliopewa Hawa pale Edeni: "Hamtakufa hakika." "Siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:4,5. Ubunifu wa hali ya juu wa udanganyifu wake ataufikia mwisho wa wakati uliosalia. Nabii anasema "Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura,... Hizo ndizo roho za maShetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi." Ufunuo 16:13, 14.

Isipokuwa wale wanaolindwa na uwezo wa Mungu kwa njia ya imani kwa Neno lake, ulimwengu wote utaingia kwenye udanganyifu wake. Watu wanakubali haraka kuliwazwa kwa usalama usio na uhakika, wataamshwa tu wakati Mungu atakapokuwa akimwaga ghadhabu yake.

[343] # Sura Ya 35 - Kutishiwa Kwa Uhuru Wa Dhamiri

Waprotestanti sasa, wanaujali Ukatoliki zaidi ya ilivyokuwa katika miaka iliyotangulia. Katika zile nchi ambazo Ukatoliki unachukua hatua za mapatano ili kupata ushawishi, kuna mtazamo unaopata nguvu kwamba, hatutofautiani sana kwenye mambo ya msingi kama ilivyokuwa inadhaniwa na kwamba maafikiano kidogo kwa upande wetu yatatuleta kwenye maelewano mazuri zaidi na Kanisa la Roma. Ulikuwepo wakati ambapo Waprotestanti waliwafundisha watoto wao kuwa kutafuta mapatano na Kanisa la Roma itakuwa ni kukosa uaminifu kwa Mungu. Lakini sasa tofauti ya mawazo yanayotolewa ni kubwa!

Watetezi wa utawala wa Papa wanatamka kuwa kanisa limekashifiwa, kwamba si halali kulihukumu kanisa la sasa kwa utawala wake wa kame za ujinga na giza. Wanautolea udhum ukatili wake wa kutisha kuwa ulikuwa ni ushenzi wa nyakati hizo.

Je, watu hawa wameyasahau madai yanayotolewa na utawala huu kwamba kanisa halikosei? Kanisa la Roma linadai kuwa, "Kanisa halikukosea; na wala, kulingana na Maandiko halitakosea" [235]

Kanisa la Papa halitayaacha madai yake ya kutokosea. Hebu vikwazo vinavyowekwa na serikali za mataifa viondolewe na Kanisa la Roma limdishwe kwenye utawala wake wa zamani, kutakuwa na uamsho wa udhalimu wake na mateso.

Ni kweli kwamba kuna Wakristo wazuri ndani ya ushirika wa Kanisa Katoliki la Roma. Maelfu ya watu katika kanisa lile wanamtumikia Mungu kwa uaminifu kulingana na num waliyonayo. Mungu anawaangalia kwa humma na upole watu hawa ambao, wameelimishwa katika imani yenye udanganyifu na isiyokidhi haja. Atawaletea num ya ukweli ili ipenye katika giza na wengi watajiunga na watu wa Mungu.

[344] Lakini Ukatoliki kama mfumo hauna upatanifu na Injili ya Kristo sasa zaidi ya ilivyokuwa katika kipindi chochote cha nyuma.

[235] ohn L. von Mosheim, *Institute of Ecclesiastical History*, book 3, century 11, part 2, chapter 2, section 9, note 17.

Kanisa la Roma linatumia kila mbinu kupata upya udhibiti wa dunia, kuyaanzisha tena mateso, na kuyaharibu yale yote ambayo Uprotestanti umeyafanya. Ukatoliki unapata nguvu kila upande. Angalia idadi ya makanisa yake inavyoongezeka. Tazama umaarufu wa vyuo na shule zake, Waprotestanti wakiwa wateja wao wakubwa. Angalia ukuaji wa kanuni za ibada huko Uingereza na dosari za mara kwa mara kwenye ngazi za uongozi za Wakatoliki.

## Maridhiano na Makubaliano

Waprotestanti wamekuwa wateja wa utawala wa utawala wa Papa; wamefanya maridhiano na makubaliano ambayo Wakatoliki wenyewe wanashangaa kuyaona. Wanadamu wanaifumbia macho tabia halisi ya Ukatoliki. Watu wanatakiwa kuzipinga hatua za huyu adui hatari kuelekea kwenye uhuru wa kiraia na uhuru wa kidini.

Wakati Ukatoliki umejengwa juu ya udanganyifu, haimaanishi kuwa ni mfumo duni usio na ustadi. Huduma ya ibada ya Kanisa la Roma ni ya kuvutia sana. Mwonekano wake wenye mapambo ya kufurahisha na ibada yenye kicho inawapumbaza watu na kunyamazisha uwezo wa kuangalia mantiki na dhamiri. Jicho linavutwa. Makanisa yanayovutia, maandamano ya ibada, mimbara za dhahabu, vihekalu vyenye nakshi za vito, picha zilizochorwa kwa ustadi na sanaa zenye ubora zinavutia kupenda uzuri. Muziki hauna mpinzani. Muziki mwanana unaopigwa kwa mpangilio mzuri na mchanganyiko wa mawimbi ya sauti nyingi zinazopaa kwenye mahekalu makubwa na mazuri, unachochea moyo kuwa na kicho na heshima kubwa.

Uzuri huu wa nje na sherehe haukidhi tamaa ya mtu mwenye kulemewa na dhambi. Dini ya Kristo haihitaji vivutio vya aina hiyo. Nuru ing'aayo kutoka kwenye msalaba inaonekana kuwa safi na iliyojaa upendo kiasi kwamba hakuna mapambo ya nje yawezayo kuongeza thamani yake ya kweli.

Fikra za juu za kazi za sanaa, ulaini halisi wa ladha, mara nyingi vimetumiwa na Shetani kuwaongoza wanadamu kuyasahau mahitaji ya muhimu ya moyo na kuishi kwa ajili ya ulimwengu huu pekee.

Fahari na taratibu za ibada za Kikatoliki zina nguvu ya kushawishi na kupumbaza, ambayo imewadanganya wengi. Wanaona kana kwamba Kanisa Katoliki ni lango la kuingilia mbinguni. Ni wale tu [345]

wanaokita miguu yao juu ya msingi wa ukweli, mioyo yao ikiwa imefanywa upya na Roho Mtakatifu, ambao hawataathiriwa na ushawishi wake. Mtindo wa maisha ya uadilifu bila nguvu zake ndiyo shauku ya watu wengi.

Dai la kanisa kuwa na haki ya kusamehe dhambi linamfanya Mkatoliki kuhisi kuwa anao uhuru wa kutenda dhambi, ibada ya kitubio pia huchangia kuhalalisha uovu. Yule anayempigia magoti mwanadamu mwenye dhambi na kufunua katika maungamo mawazo ya siri za moyo wake anaivunjia heshima nafsi yake. Kwa kuzifunua dhambi za maisha yake kwa padre-mkosaji mwenye kupatwa na mauti - kiwango cha tabia yake kinashushwa, na matokeo yake ananajisika. Wazo lake kuhusu Mungu linashuka hadhi na kumfananisha na ubinadamu ulioanguka, maana padre anasimama kama mwakilishi wa Mungu. Maungamo haya yanayoshusha hadhi kati ya mwanadamu na mwanadamu, ni chemchemi ya siri ambayo kwayo kiasi kikubwa cha uovu unaounajisi ulimwengu unabubujika. Lakini kwa yeye apendaye kuiendekeza nafsi, inapendeza zaidi kuungama kwa mwanadamu mwenzake mwenye kupatwa na mauti kuliko kufungua moyo wake kwa Mungu. Inakubalika zaidi kwa asili ya mwanadamu kutubu kuliko kuikana dhambi; ni rahisi kuudhalilisha mwili kwa nguo za magunia kuliko kuzisulubisha tamaa za mwili.

## Mlandano wa Kuvutia

Wakati ambapo kwenye ujio wa kwanza Wakristo Wayahudi, kwa siri, walikuwa wanaikanyaga sheria ya Mungu; kwa nje waliyashika matakwa yake kwa ushupavu, wakiijaza mahitaji yanayotaka umakini zaidi na kufanya utii kuwa mzigo mzito kuubeba. Kwa namna ile ile ambavyo Wayahudi walijidai kuiheshimu sheria; ndivyo Wakatoliki wanavyodai kuuheshimu msalaba.

Wanaweka misalaba juu ya makanisa, madhabahu, na mavazi yao. Kila mahali nembo ya msalaba, kwa nje, inapewa heshima na kuinuliwa. Lakini mafundisho ya Kristo yamezikwa chini ya mapokeo yasiyo na mantiki na misimamo mikali kwenye mambo madogo. Watu waaminifu wamewekwa katika hofu ya ghadhabu ya Mungu aliyekasirishwa, wakati ambapo watu wenye vyeo ndani ya kanisa wanaishi maisha ya anasa na kujifurahisha kwa tamaa.

[346] Ni jitihada za kudumu za Shetani kuipotosha tabia ya Mungu,

asili ya dhambi, na mambo ya kufa na kupona ndani ya pambano kuu. Udanganyifu wake unawapa wanadamu uhalali wa kutenda dhambi. Wakati huo huo yanawafanya watunze dhana za uwongo juu ya Mungu ili wamheshimu kwa hofu na chuki badala ya upendo. Kwa njia ya dhana zilizopotoshwa juu ya tabia za Mungu, mataifa ya kipagani yalikuwa yanaongozwa kuamini kuwa kafara za binadamu zilikuwa za lazima ili kupata kibali kutoka kwa miungu. Ukatili wa kutisha ulikuwa unafanyika isivyo halali chini ya mitindo kadhaa ya ibada ya sanamu.

### Muungano wa Upagani na Ukristo

Kitendo cha Kanisa Katoliki la Roma, kuunganisha upagani na Ukristo, na kama ulivyo upagani, kupotosha tabia ya Mungu; kimepelekea vitendo vya ukatili mkubwa. Vyombo vya mateso viliwalazimisha watu wakubali mafundisho yake. Watu wenye vyeo kanisani walijifunza kuvumbua njia za kusababisha mateso makali iwezekanavyo bila kuwaua wale waliokataa kuyakubali madai yake. Katika matukio mengi, mtu aliyekuwa anateseka alikikaribisha kifo kama pumziko tamu.

Kwa wafuasi wake waaminifu, Kanisa la Roma lilikuwa linatumia adhabu za mijeledi, kuwanyima chakula, na nyingine za kimwili. Ili kupata kibali cha mbinguni, wenye kutubu walifundishwa kujitenga na vifungo alivyoweka Mungu ili awabariki na kuwapa furaha kama wapitaji duniani. Uwanja wa kanisa umejaa mamilioni ya watu ambao katika maisha yao wanafanya jitihada zisizo na mafanikio, za kuzuia kila wazo na hisia ya huruma kwa viumbe wenzao kana kwamba mambo hayo yanamchukiza Mungu. Mungu hawabebeshi wanadamu mizigo hiyo mizito. Kristo hakuweka kielelezo kwa wanaume na wanawake kujifungia kwenye nyumba za watawa ili wastahili kuingia mbinguni. Hakufundisha kuwa upendo ni lazima unyamazishwe.

Papa anadai kuwa yeye ni wakili Wakristo. Lakini, je, kuna tukio lolote linaloonesha kuWakristo alikuwa anawafunga watu gerezani kwa kosa la kutomsheshimu kama mfalme wa mbinguni? Je, sauti yake ilisikika ikiwahukumu kifo wale waliokuwa wamemkataa?

Kanisa Katoliki linajionesha mbele ya ulimwengu kuwa linatenda haki, huku likiomba radhi na kuzifunika kumbukumbu za [347]

ukatili wake wa kutisha. Limejivika mavazi kama ya Kristo, lakini halijabadilika. Kila kanuni ya zamani ya utawala wa Papa ipo hadi leo. Mafundisho yaliyobuniwa zama za giza bado yanashikiliwa hadi leo. Utawala wa Papa ambao Waprotestanti wa leo wanauheshimu ni ule ule uliokuwa unatawala katika siku za Wanamatengenezo, wakati watu wa Mungu waliposimama ili kuufunua uovu wake wakihatarisha maisha yao.

Utawala wa Papa uko vile ulivyo sawa na unabii ulivyotamka, kwamba kungekuwa na uasi ambao ungekuja baadaye. 2Wathesalonike 2:3, 4. Chini ya mwonekano wa kinyonga unaobadilika, utawala wa Papa umeifunika sumu ya nyoka isiyobadilika. Je, nguvu hii, ambayo kumbukumbu yake kwa miaka elfu moja, imeandikwa kwa damu ya watakatifu; sasa ikubaliwe kama sehemu ya kanisa la Kristo?

### Badiliko Ndani ya Uprotestanti

Dai limetolewa katika nchi za Kiprotestanti kwamba Ukatoliki unatofautiana kidogo sana na Uprotestanti kuliko zamani. Kumekuwa na badiliko, lakini badiliko haliko ndani ya utawala wa Papa. Ukatoliki kwa kweli unafanana sana na Uprotestanti uliopo sasa kwa sababu Uprotestanti umeharibika kwa kiasi kikubwa tangu siku za Wanamatengenezo.

Makanisa ya Waprotestanti, yakitafuta kuungwa mkono na ulimwengu, yanaamini uovu wote kuwa ni wema na matokeo yake mwishoni yataamini wema wote kuwa ni uovu. Kwa sasa, kama ilivyokuwa zamani, yanaomba radhi kwa Kanisa la Roma kwa ajili ya mtazamo wao usiobadilika dhidi yake, wakiomba msamaha kwa kung'ang'ania mawazo yao kupita kiasi. Wengi wanatoa hoja kuwa giza la kiakili na kimaadili lililokuwepo zama za kati lilisaidia kuenea kwa mapokeo potovu na mateso ya Kanisa la Roma; na kwamba uwezo mkubwa wa kiakili wa wakati wa sasa na uhuru unaoongezeka katika mambo ya kidini unazuia kuinuka tena kwa hali ya kutovumiliana. Dhana kwamba hali kama hiyo ya mambo itakuwepo katika kizazi hiki chenye nuru limepuuzwa. Lakini ni lazima ikumbukwe kuwa kadiri nuru kubwa inavyotolewa, ndivyo giza linavyozidi kwa wale wanaoipotosha na kuikataa.

[348] Nyakati za giza la kiakili zilijenga mazingira mazuri kwa

mafanikio ya utawala wa Papa. Nyakati za nuru kubwa ni mazingira mazuri pia. Katika vizazi vilivyopita wakati watu walipokuwa hawana ufahamu wa ukweli, maelfu walinaswa, pasipo kuona nyavu zilizokuwa zimetegwa miguuni pao. Katika kizazi hiki wengi hawauoni wavu na wanauendea kwa haraka kama vipofu. Wakati wanadamu wanapoziinua nadharia zao kupita Neno la Mungu; maarifa yanaweza kuleta madhara makubwa kuliko ujinga. Hivyo sayansi ya uongo ya siku hizi itaonesha mafanikio kwa kuandaa njia ya kuukubali utawala wa Papa, kama ulivyofanya ukosefu wa maarifa katika zama za giza

## Kuishika Jumapili

Kuishika Jumapili ni desturi iliyoanzishwa na Kanisa la Roma, ambalo linadai kama ndiyo alama ya mamlaka yake. Roho ya utawala wa Papa - ya kuzikubali desturi za kidunia, kuzitukuza mila za wanadamu kupita amri za Mungu-inapenya ndani ya makanisa ya Kiprotestanti na kuwaongoza kwenye kazi ile ile ambayo utawala wa Papa uliifanya kabla yao; ya kuiinua Jumapili.

Sheria za kifalme, mabaraza makuu, na sheria za kanisa zikisaidiwa na nguvu ya serikali zilikuwa ni hatua zilizowezesha sherehe za kipagani kupata nafasi ya heshima kwenye ulimwengu wa Ukristo. Hatua ya kwanza ya kulazimishwa ushikajiji wa Jumapili kwa watu wote, ni sheria iliyowekwa na Kostantino. Ingawa kimsingi ni sheria ya kipagani, ilikuwa imelazimishwa na mfalme baada ya kuupokea Ukristo kwa jina tu.

Eusebio, askofu aliyetafuta kupendwa na wakuu, na ambaye alikuwa rafiki wa pekee wa Kostantino, alilieneza dai kuWakristo alihamisha Sabato kwenda Jumapili. Hakuna ushuhuda wa Maandiko unaotolewa kulihakikisha hilo. Eusebio mwenyewe pasipo kujua anakiri hilo si halali. "Mambo yote" anasema, jambo lolote lililokuwa ni wajibu kutendwa siku ya Sabato, tumelihamisha kwenda kwenye Siku ya Bwana" [236]
Utawala wa Papa ulipoanzishwa, Jumapili iliendelea kuinuliwa. [349]
Kwa muda fulani siku ya saba iliendelea kuchukuliwa kama ndiyo Sabato, lakini polepole badiliko lilifanyika. Baadaye Papa alitoa

[236] Robert Cox, *Sabhath Laws and Sabbath Duties*, p. 538

maelekezo kwamba paroko anapaswa kuwaonya wanaokiuka kutunza Jumapili wasije wakapata madhara makubwa wao na majirani zao.

Maagizo ya mabaraza yaliposhindwa, mamlaka za serikali ziliombwa kutoa sheria ambayo ingetia hofu ndani ya mioyo ya watu na kuwalazimisha kuacha kufanya kazi siku ya Jumapili. Katika mkutano wa majimbo (sinodi) uliofanyika Roma, uamuzi wote uliotangulia ulisisitizwa upya na kujumuishwa kwenye sheria za kanisa na kulazimishwa na mamlaka za umma. [237]

Hali ya kuutokuwepo kwa mamlaka ya Maandiko inayoagiza kushika Jumapili bado ilikuwa inaleta usumbufu. Watu walikuwa wanauliza juu ya haki ya walimu wao kuliweka kando tangazo, "Siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako." ili kuiheshimu siku ya jua. Ili kujaza nafasi ya kutokuwepo ushuhuda wa Biblia, kukawa na ulazima wa kuweka sababu zilizokuwa zinaonekana kufaa.

Mtetezi wa Jumapili mwenye bidii, ambaye mwishoni mwa kame ya kumi na mbili alitembelea makanisa ya Uingereza, alikataliwa na mashahidi waaminifu wa ukweli; na hivyo juhudi zake hazikuzaa matunda na akaondoka huko kwa muda. Aliporejea, alikuwa na gombo alilodai kuwa lilitoka kwa Mungu mwenyewe, ndani yake lilikuwa na amri iliyohitajika ya kushika Jumapili, ikiambatana na vitisho vikubwa kuwapa hofu ambao wangekataa kutii. Waraka huo wa thamani inasemekana ulianguka kutoka mbinguni na uliokotwa Yemsalemu juu ya madhabahu ya Mtakatifu Simeoni, huko Goligota. Lakini kwa hakika ikulu ya Papa huko Roma ilikuwa ndiyo chanzo chake. Udanganyifu na mambo ya kughushi katika vizazi vyote yamekuwa yakihalalishwa na utawala wa Papa. **(Angalia Kiambatisho)**

Lakini bila kujali jitihada zote za kuuimarisha utakatifu wa Jumapili, Wakatoliki wenyewe walikiri hadharani kuwa Sabato inayo mamlaka kutoka kwa Mungu. Katika kame ya kumi na sita
[350] baraza la kiPapa lilitangaza kuwa, "Hebu Wakristo wote wakumbuke kuwa Sabato ilitakaswa na Mungu, na imekuwa ikipokelewa na kutunzwa, siyo tu na Wayahudi, lakini na wote wengine waliokuwa wanajifanya kumwabudu Mungu; ingawa Wakristo waliibadili

[237] Heylyn, *History of the Sabbath*, pt. 2, ch. 5, sec. 7.

Sabato yao kwenda kwenye Siku ya Bwana." [238] Wale waliokuwa wanajaribu kuibadili sheria ya Mungu hawakuwa gizani juu ya tabia ya kazi yao.

Kielelezo cha kuvutia juu ya sera ya Kanisa la Roma kilitolewa wakati wa mateso ya muda mrefu yenye umwagaji damu dhidi ya Wawaldensia, baadhi yao wakiwa watunza Sabato. **(Angalia Kiambatisho)** Historia ya makanisa ya Ethiopia na Abyssinia ni ya muhimu. Katikati ya utusitusi wa Zama za Giza, Wakristo wa Afrika ya kati hawakujulikana na walikuwa wamesahauliwa na ulimwengu na kwa kame nyingi walifurahia uhuru wa Ukristo wao. Mwishowe Kanisa la Roma likagundua uwepo wao, na mfalme wa Abyssinia akadanganywa na kumtambua Papa kama wakili Wakristo. Sheria ilitangazwa ya kukataza utunzaji wa Sabato, ikiambatana na adhabu kali. [239] Lakini ghafla udhalimu wa Papa ukawa kama nira inayoumiza hata watu wa Abyssinia wakaazimu kuivunja. Wakatoliki walipigwa marufuku kwenye utawala wao na imani yao ya awali ikarejeshwa.

Wakati ambapo makanisa ya Afrika yalikuwa yanatunza Sabato na kuzitii amri za Mungu, hawakufanya kazi siku ya Jumapili kulingana na desturi za kanisa. Kanisa la Roma liliikanyaga sheria ya Mungu na kuiinua sheria yake, lakini makanisa ya Afrika, yakiwa yamefichwa kwa karibu miaka elfu moja, hayakushiriki uasi huu. Yalipowekwa chini ya Kanisa la Roma, yalilazimishwa kuiweka kando Sabato ya kweli na kuiinua ya uongo. Lakini mapema baada ya kupata uhuru wao walirudia kwenye utii wa amri ya nne. **(Angalia Kiambatisho)**

Kumbukumbu hizi zinafunua kwa uwazi uadui wa Kanisa la Roma dhidi ya Sabato na Watetezi wake. Neno la Mungu linatufundisha kuwa matukio haya yatajirudia wakati Ukatoliki utakapoungana na Uprotestanti kwa ajili ya kuiinua Jumapili.

### Mnyama Mwenye Pembe kama za Mwanakondoo [351]

Unabii wa Ufunuo 13 unatangaza kwamba mnyama mwenye pembe kama za Mwanakondoo "Aifanya dunia na wote wakaao

[238] Thomas Morer, *Discourse in Six Dialogues on the Name, Notion, and Observation of the Lord's Day*, pp. 281, 282.

[239] Michael Geddes, *Church History of Ethiopia*, pp. 311,312.

ndani yake" kuuabudu utawala wa Papa-ambao umewakilishwa na mnyama "mfano wa chui" Mnyama mwenye pembe mbili atawaambia "wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama." Zaidi ya hayo atawalazimisha wote "...wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa" watiwe chapa ya mnyama. Ufunuo 13:11-16. Marekani ndiyo mamlaka inayowakilishwa na mnyama mwenye pembe kama za Mwanakondoo. Unabii huu utatimizwa wakati Marekani itakapolazimisha kushika Jumapili, ambayo Roma inadai ni kuukiri ukuu wake.

"Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote, ikamstaajabia mnyama yule." Ufunuo 13:3. Jeraha la mauti linatuonesha kwenye anguko la utawala wa Papa mwaka 1798. Baada ya hayo anasema nabii, "jeraha lake la mauti likapona: Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule." Paulo anasema kuwa "mtu wa kuasi" atafanya kazi yake ya udanganyifu karibu na mwisho wa wakati. 2Wathesalonike 2:3-8. Na "watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima" Ufunuo 13:8. Katika ulimwengu wa zamani na wa sasa utawala wa Papa utapokea heshima inayotolewa kwa adhama ya Jumapili.

Tangu katikati ya kame ya kumi na tisa, wanafunzi wa unabii waliuleta ushuhuda huu katika ulimwengu. Na sasa tunaona kasi ya maendeleo katika kutimia kwa utabiri huu. Miongoni mwa walimu wa Kiprotestanti lipo dai lile lile la kuwepo mamlaka kutoka mbinguni juu ya kuishka Jumapili, na bado uthibitisho wa Maandiko unakosekana, kama ilivyo kwa viongozi wa utawala wa Papa. Madai kwamba hukumu za Mungu zitawakalia wanadamu kwa uvunjaji wa sabato ya jumapili yatarudiwa; na tayari hoja zimeanza kutolewa.

Kanisa la Roma lina werevu wa ajabu. Lina uwezo wa kufahamu kabla, nini kitatokea baadaye - kwamba makanisa ya Kiprotestanti yanalipatia heshima kuu kwa kuikubali sabato ya uongo na kwamba wanajiandaa kuilazimisha kwa njia ambayo lilikuwa linaitumia zamani. Litakuwa tayari kiasi gani kuwasaidia Waprotestanti katika kazi hii, si vigumu kubashiri!

[352] Kanisa Katoliki la Roma linaunda taasisi kubwa ambayo ipo chini ya udhibiti wa mamlaka ya Papa, wapo mamilioni ya waleta habari wake katika kila nchi wakifungwa kifungo cha utii kwa Papa, bila kujali wapo katika nchi au serikali gani. Ingawa wanaweza

kuapa kuwa waaminifu kwa nchi waliyomo, lakini nyuma yake wana kiapo cha utii kwa Roma.

Historia inao ushuhuda wa jitihada zisizokoma na zenye ustadi za kujipenyeza kwa Kanisa la Roma kwenye mambo ya mataifa, na likipata nafasi, litaitumia kufanikisha malengo yake hata kama ni kwa uangamivu wa watawala na watu. [240]

Kanisa la Roma linajivuna kuwa halibadiliki. Waporotestanti wanafahamu kidogo juu ya kile wanachofanya wanapopendekeza kupata msaada kutoka kwenye Kanisa la Roma katika kazi ya kuiinua Jumapili. Wakiwa wamejielekeza katika kusudi lao, Kanisa la Roma linalenga katika kuijenga upya mamlaka yake, kuurejesha ukuu wake uliopotea. Hebu kanuni iwekwe tena kuwa kanisa linaweza kudhibiti mamlaka ya serikali; kwamba taratibu za kanisa zilazimishwe na sheria za nchi; kwa ufupi, kwamba mamlaka ya kanisa na ya nchi yatawale dhamiri - ndipo Kanisa la Roma litakuwa limejihakikishia ushindi wake.

Ulimwengu wa Kiprotestanti utagundua makusudi ya Kanisa la Roma wakati utakapokuwa umechelewa kujinasua kwenye mtego. Kanisa la Roma kwa ukimya linakua kuelekea kwenye mamlaka. Mafundisho yake yana mvuto kwenye mabunge ya kutunga sheria, makanisani, na katika mioyo ya wanadamu. Linayaimarisha majeshi yake ili kuendeleza malengo yake muda utakapofika. Tamaa yake pekee ni kupata mazingira muafaka. Yeyote atakayeamini na kulitii Neno la Mungu ataambulia shutuma na mateso.

[240] John Dowling, *The History of Romanism*, bk. Ch. 6, sec. 55; and Mosheim, bk. 3' cent. 11, pt. 2, sec. 9, notel 7.

## [353] Sura Ya 36 - Pambano Linalokaribia

Tangu mwanzo wa pambano kuu mbinguni, limekuwa ni kusudi la Shetani kuipindua sheria ya Mungu. Iwe ni kwa kuitupilia mbali sheria yote ya Mungu, au kwa kupuuzia sehemu ya sheria hizo, matokeo yatakuwa yale yale. Yule ambaye atajikwaa, "katika neno moja" hudhihirisha kukosa juu ya sheria yote; mvuto na kielelezo chake viko upande wa uasi naye atakuwa "amekosa juu ya yote." Yakobo 2:10.

Shetani ameyapotosha mafundisho ya Biblia na makosa yameingizwa katika imani ya maelfu ya watu. Pambano kuu la mwisho kati ya ukweli na uongo linahusu sheria ya Mungu, kati ya Biblia na dini ya uongo na mapokeo. Biblia inaweza kufikiwa na wote, lakini ni wachache tu ambao wanaikubali kama mwongozo wa maisha. Ndani ya kanisa wengi wanakana nguzo za imani ya Kikristo. Uumbaji, anguko la mwanadamu, upatanisho, na sheria ya Mungu vimepuuzwa, iwe ni vyote au kwa sehemu. Maelfu ya watu wanaona kuwa kuiamini Biblia ni kuonesha udhaifu.

Ni rahisi sana kutengeneza sanamu ya nadharia za uongo kama ilivyo kutengeneza sanamu ya mbao au mawe. Kwa kumwasilisha Mungu visivyo, Shetani amewafanya watu wamfikirie Mungu kuwa ni mwenye tabia ya udanganyifu.. Sanamu ya falsafa imeinuliwa na kuwekwa mahali pa Mungu aliye hai kama alivyodhihirishwa katika Neno lake, katika Kristo na katika uumbaji. Mungu huyu wa wanafalsafa, washairi, wanasiasa, waandishi wa habari wengi wa vyuo vikuu vingi na hata baadhi ya taasisi za kiteolojia ni bora kidogo tu kuliko Baali, mungu-jua wa Wafoinike katika siku za Eliya.

Hakuna kosa linaloshambulia kwa nguvu mamlaka ya mbinguni, hakuna kosa lililo na madhara mabaya kuliko lile fundisho kwamba sheria ya Mungu si sharti tena. Hebu fikiria kama wahubiri maarufu wangefundisha waziwazi kwamba sheria zinazoiongoza nchi siyo za lazima, na kwamba zinazuia uhuru wa watu kwa hiyo hazipaswi

kuheshimiwa. Je, ni kwa muda gani watu hao wangevumiliwa kuendelea kuwepo mimbarani?

Ingekuwa ni sawa kwa mataifa kukomesha sheria zao kuliko [354]
Mtawala wa ulimwengu kuiondoa sheria yake. Jaribu la kuiondoa sheria ya Mungu liliwahi kufanyika Ufaransa wakati upagani ulipotawala. Ilidhihirishwa kuwa kutupilia mbali sheria ambazo Mungu ameziweka ni kuukubali utawala wa mfalme wa giza.

## Kuiweka Pembeni Sheria ya Mungu

Wale wanaowafundisha watu kuzichukulia juu juu sheria za Mungu wanapanda uasi ili wavune uasi. Hebu sheria yote ya Mungu itupiliwe mbali, na sheria ya mwanadamu itapuuzwa. Matokeo ya kupuuzia sheria za Mungu yatakuwa na madhara ambayo hayakutarajiwa. Mali za watu hazitakuwa salama, watu watachukua mali za majirani zao kwa nguvu na wenye nguvu ndio watakao kuwa matajiri. Hata maisha yenyewe hayataheshimiwa, kiapo cha ndoa hakitakuwa tena ngome ya kuilinda familia. Aliye na nguvu anaweza kumchukua mke wa jirani yake kwa nguvu. Amri ya tano na ya nne zitawekwa pembeni. Watoto hawatajizuia kuuondoa uhai wa wazazi wao ikiwa kwa kufanya hivyo watapata kutimiza shauku ya mioyo yao iliyopotoka. Ulimwengu uliostaarabika utageuka kuwa genge la vibaka na wauaji, furaha na amani vitatoweka duniani.

Tayari fundisho hili limefungulia mafuriko ya upotovu duniani. Rushwa na kukosa uadilifu vinafagia kama wimbi kubwa. Hata katika kaya za Wakristo kuna unafiki, talaka, kusaliti viapo vitakatifu na kuendekeza tamaa. Kanuni za kidini, msingi wa maisha ya jamii inaonekana ni jabali linaloyumbayumba tayari kuanguka. Wahalifu sugu mara nyingi wamekuwa wakipewa heshima kana- kwamba ni watu wa pekee wa kuonewa husuda. Umaarufu mkubwa umewekwa katika makosa yao. Vyombo vya habari vinawaongoza watu katika mambo mabaya, na kuwaongoza wengine katika udanganyifu, uporaji na mauaji. Kushawishi maovu, kutokuwa na kiasi na uasi wa kila namna kutainuka. Je, nini kifanyike ili kujiepusha na wimbi la uovu?

### Kutokuwa Na Kiasi KumewapumbazaWengi

Mahakama zimepotoka, watawala wanasukumwa na tamaa ya kulimbikiza mali na kupenda anasa. Kutokuwa na kiasi kumewapumbaza wengi kiasi kwamba Shetani amewatawala kabisa. Ma-
[355] hakimu wamepotoka, wanahongwa kwa rushwa na kudanganywa. Ulevi na fujo, kukosa uaminifu wa kila namna, kumeshamiri miongoni mwa wale wanaozisimamia sheria. Hivi sasa kwasababu Shetani hawezi tena kuudhibiti ulimwengu kwa kuyaficha Maandiko, anatumia njia nyingine kutimiza lengo hilo. Kuiharibu imani katika Biblia kunafanya kazi sawa na kuiharibu Biblia yenyewe.

Kama ilivyokuwa kwa vizazi vilivyopita, Shetani ametenda kazi kupitia makanisa kuendeleza mipango yake. Katika kuushambulia ukweli usiopendwa, wanazikubali fasili ambazo zinatawanya mbegu za mashaka. Wakiyang'ang'nia makosa ya mamlaka ya Papa ya hali ya kutokufa kwa nafsi na hali ya mwanadamu kuwa na ufahamu baada ya kufa wanakataa kinga yao ya pekee dhidi ya imani ya mizimu. Fundisho la mateso ya milele limewafanya wengi kutoiamini Biblia. Kadiri madai ya amri ya nne yanavyosisitizwa, inaonekana kuwa ushikaji wa Sabato ya siku ya saba unatolewa agizo; na kama njia pekee kwao kujiweka huru kutoka kwenye wajibu ambao hawako radhi kuutekeleza, walimu wanaopendwa wanaitupa mbali sheria ya Mungu pamoja na Sabato. Kadiri matengenezo kuhusu Sabato yanavyoendelea, kukataliwa kwa sheria ya Mungu ili kuepuka amri ya nne kutaenea karibu ulimwengu mzima. Viongozi wa kidini wataruhusu ukafiri, imani ya mizimu na dharau kwa sheria takatifu ya Mungu-wajibu wa kutisha kwaajili ya uovu uliopo kwenye ulimwengu wa Kikristo.

Na bado kundi hili hili la watu litadai kuwa ulazimishaji wa amri ya Jumapili utaboresha maadili ya jamii. Ni mojawapo ya hila za Shetani kuchanganya uongo na ukweli mwingi ili uonekane kuwa ni kitu cha kukubalika. Viongozi wa harakati za amri ya Jumapili wanaweza kutetea matengenezo ambayo watu wayanahitaji, kanuni zinazopatana na Biblia, lakini kwa kuwa pamoja na hayo kuna hitaji linalopingana na sheria ya Mungu, watumishi wake hawataungana nao. Hakuna kiwezacho kuhalalisha uwekaji kando wa sheria za Mungu kwa ajili ya kutimiza maagizo ya wanadamu.

Kwa kutumia makosa mawili makubwa, hali ya kutokufa kwa roho na utakatifu wa Jumapili, Shetani atawaweka watu chini ya udanganyifu wake. Wakati kosa la kwanza linaweka msingi wa imani ya mizimu, lile la pili linatengeneza kiungo cha wema wa Kanisa la Roma. Waprotestanti wa Marekani watakuwa mstari wa mbele kunyosha mikono yao ili kuvuka shimo kubwa na kuushika [356]
mkono wa imani ya mizimu; watalivuka lindi kuu na kupeana mikono na mamlaka ya Kanisa la Roma; na chini ya ushawishi wa huu muungano wenye sehemu tatu mashirika matatu nchi hii (Marekani) itafuata nyayo za Kanisa la Roma katika kukanyaga haki za dhamiri.

Imani ya mizimu inaponaigiza Ukristo wa wakati huu, inakuwa na uwezo mkubwa wa kudanganya. Ibilisi mwenyewe "ameongoka." Atatokeza kama malaika wa nuru. Kwa njia ya imani ya mizimu, miujiza mingi itatendeka, wagonjwa wataponywa, na maajabu mengi yasiyoweza kupingika yatatendeka.

Wafuasi wa Papa wanaojivunia miujiza kama ishara ya kanisa la kweli watadanganywa upesi na uwezo huu utendao miujiza, na Waprotestanti, wakiwa wameitupilia mbali ngao ya ukweli, watadanganywa pia. Wafuasi wa Papa, Waprotestanti, na watu wa dunia wote kwa pamoja wataona ndani ya harakati kuu kwa ajili ya kuuongoa ulimwengu.

Kwa njia ya imani ya mizimu, Shetani anaonekana kuwa ndiye mfadhili wa jamii ya wanadamu, akiponya magonjwa na kuleta mfumo mpya wa imani ya kidini, lakini wakati huo huo anawaongoza wengi kwenye uharibifu. Kutokuwa na kiasi kunazipindua akili; kunaendekeza tamaa ya mwili, migogoro, na umwagaji damu unafuatia. Vita vinachochea tamaa mbaya za nafsi na kuwafagilia mbali wahanga wake milele na kuwatumbukiza kwenye uovu na umwagaji wa damu. Ni kusudi la Shetani kuyachochea mataifa kwenda vitani kwani kwa njia hiyo anaweza atawapotosha watu ili wasifanye Maandalizi ya kusimama katika siku ya hukumu.

Shetani amejifunza siri za maumbile, na anatumia uwezo wake wote kudhibiti viumbe vya asili kwa kadiri Mungu anavyoruhusu. Ni Mungu anayewalinda viumbe wake dhidi ya mharabu. Hata hivyo, ulimwengu wa Kikristo umeonesha dharau kwa sheria yake ,na Bwana atafanya kile alichosema kuwa angekifanya - kuuondoa ulinzi wake kwa wale wanaoiasi sheria yake na kuwawalazimisha

wengine kufanya hivyo. Shetani ndiye anayewadhibiti wale wote ambao kwa namna ya pekee hawalindwi na Mungu. Atawapatia upendeleo na ustawi baadhi yao, na ataleta shida kwa wengine, na kuwaongoza watu kuamini kuwa ni Mungu anayewatesa.

[357] Huku akijitokeza kama tabibu mkuu awezaye kuyaponya maradhi yao yote, Shetani ataleta magonjwa na majanga hadi miji yenye watu wengi itakapoharibiwa na kuwa magofu. Katika ajali za baharini na za nchi kavu, katika majanga makubwa ya moto, katika vimbunga vikali, na mvua za mawe, tufani, mafuriko, mawimbi ya bahari na matetemeko ya ardhi kwa namna mbalimbali; Shetani anautumia uwezo wake. Anayafagilia mbali mavuno yaliyokwisha kukomaa, kisha njaa na mateso vinafuata. Anaichafua hewa kwa harufu ya kufisha na watu wengi wanakufa.

Kisha mwongo mkuu atashawishi watu kuelekeza mashtaka yao yote kwa wale ambao utii wao kwa shcria za Mungu ni shutuma ya daima kwa watenda dhambi. Itatamkwa kwamba watu wanamkosea Mungu kwa kuihalifu Jumapili, na kuwa dhambi hii imeleta maafa ambayo hayatakoma mpaka ushikaji wa Jumapili utakapolazimishwa. "Wale ambao wanaiharibu heshima ya Jumapili wanazuia urejeshwaji wa fadhila za mbinguni na ustawi." Kwa hiyo shutuma za zamani dhidi ya mtumishi wa Mungu zitajirudia. "Ikawa, Ahabu alipomwona Eliya,.. Ahabu akamwambia, Je! Ni wewe, Ewe mtaabishaji wa Israeli?" 1 Fal. 18:17,18.

Uwezo utendao miujiza utatumia mvuto wake dhidi ya wale wanaomtii Mungu kuliko wanadamu. "roho" watatamka kuwa Mungu amewatuma kuwashawishi wanaoipinga Jumapili juu ya kosa lao. Watalalamikia uovu mkubwa unaotendeka duniani na kuunga mkono shuhuda za walimu wa kidini kwamba uporomokaji wa maadili unasababishwa na kutoiheshimu Jumapili.

Chini ya utawala wa Kanisa la Roma, wale walioteseka kwa sababu ya Injili walishutumiwa kuwa ni watenda maovu wakishirikiana na Shetani. Hivyo ndivyo itakavyokuwa sasa. Shetani atawasababisha wale wanaozitii sheria za Mungu washitakiwe kuwa ndio watu wanaoleta hukumu duniani. Kwa kutumia vitisho anajitahidi kutawala dhamiri za watu, akishawishi mamlaka za kidini na serikali kulazimisha sheria za binadamu zinazopingana na sheria ya Mungu.

Wale wanaoiheshimu Sabato ya Biblia watashutumiwa kuwa ni adui wa sheria na utaratibu, kwamba wanavunja sheria za maadili, kusababisha vurugu na uharibifii, na kuleta hukumu ya Mungu duniani. Watashtakiwa kwa kuichukia serikali. Wachungaji wanaokana [358]
majukumu ya sheria ya mbingu watahubiri kutoka mimbarani jukumu la utii kwa mamlaka za kiraia. Katika kumbi za mabunge na katika mahakama za sheria, washika sheria watahukumiwa. Kauli zao zitapotoshwa; nia zao zitawasilishwa vibaya.

Maafisa wakuu kutoka serikali na kanisani wataungana kuwashawishi au kuwalazimisha watu wote waiheshimu Jumapili. Hata ndani ya Marekani iliyo huru watawala na wabunge watalikubali hitaj linalopendelewa la sheria inayoshinikiza ushikaji wa Jumapili. Uhuru wa dhamiri ambao umegharimu kafara kubwa sana hautaheshimiwa tena. Katika Mgogoro unaokuja hivi karibuni tutaona mifano ya maneno kama yale ya nabii yakiigizwa . . . "Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu." Ufu. 12:17

[359] ## Sura Ya 37 - Usalama Wetu Pekee

Watu wa Mungu wanaelekezwa kwenye Maandiko Matakatifu kama usalama wao wa pekee dhidi ya mvuto wa walimu wa uongo na roho za giza. Shetani anatumia kila hila kuwazuia watu wasipate maarifa ya Biblia, ambayo ina maelezo yaliyo wazi yanayofunua udanganyifu wake. Udanganyifu mkuu wa mwisho hivi punde utawekwa wazi mbele yetu. Mpinga Kristo atafanya miujiza yake ya kushangaza mbele ya macho yetu. Udanganyifu utafanana na ukweli kwa karibu sana kiasi kwamba haitawezekana kutofautisha isipokuwa kwa kutumia Maandiko.

Wale wanaojitahidi kuzishika sheria zote za Mungu, watapingwa na kubezwa. Ili kuvumilia majaribu, ni lazima wayaelewe mapenzi ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika neno lake. Ni wale tu watakao kuwa wamezijenga akili zao kwa kweli za Biblia ndio watakaosimama katika pambano kuu la mwisho.

Kabla ya kusulubishwa kwake, Mwokozi aliwaeleza wanafunzi wake kwamba angeuawa na kisha angefufuka. Lakini maneno hayo yaliondolewa akilini mwa wanafunzi. Jaribu lilipokuja, kifo cha Yesu kiliondoa kabisa matumaini yao kana kwamba alikua hajawaonya mapema. Hivyo katika unabii wakati ujeo umewekwa wazi mbele yetu kwa uwazi kama ulivyokuwa umewekwa wazi kwa wanafunzi na Kristo. Matukio yanayohusiana na kufungwa kwa mlango wa rehema na kazi ya maandalizi katika kipindi cha mateso yameelezwa wazi. Lakini watu wengi hawana uelewa wa kweli hizi muhimu, na wakati wa mateso utawakuta hawako tayari.

Mungu anapotoa maonyo, anamhitaji kila mtu aliyejaliwa akili auzingatie ujumbe. Hukumu ya kutisha dhidi ya ibada ya mnyama na sanamu yake (Ufunuo 14:9-11) yapasa iwaongoze wote wajifunze maana ya alama ya mnyama na jinsi ya kuepuka kuipokea. Lakini idadi kubwa ya watu hawapendi ukweli wa Biblia, kwa sababu unapingana na tamaa za moyo wenye dhambi. Shetani anawapa udanganyifu wanaoupenda.

Lakini Mungu anataka watu wadumishe Biblia na Biblia pekee, kama kipimo cha mafundisho yote na msingi wa matengenezo yote. Maoni wasomi, mambo yaliyofasiliwa kisayansi, maamuzi [360] ya mabaraza ya kidini, sauti ya walio wengi - hakuna moja kati ya haya linaloapasa kuchukuliw kuwa ushahidi au sababu ya kupinga andiko lolote. Yatupasa kudai kwa wazi andiko linalosema "Hivi ndivyo asemavyo Bwana". Shetani anawaelekeza watu wawaangalie wachungaji, kwa walimu wa teolojia kama miongozo yao, badala ya wao wenyewe kuyachunguza Maandiko. Kwa kuwadhibiti viongozi hawa anaweza kuwashawishi watu wengi.

Kristo alipokuja, watu wa kawaida walimsikiliza kwa furaha. Lakini wakuu wa ukuhani na watu wanaoongoza,walijifungia wenyewe kwenye maono yasiyo sahihi; wakiukataa ushahidi uliodhihirisha kuwa yeye ni masihi. "Imekuwaje" watu waliuliza, "kwamba watawala wetu na waandishi wasomi hawamwamini Yesu?" Walimu kama hao waliliongoza taifa la Kiyahudi kumkataa mwokozi wao.

### Kuinua Mamlaka Ya Binadamu

Kristo alikuwa na mtazamo wa kiunabii kuhusu kazi ya kuinua mamlaka ya kibinadamu itakayotawala dhamiri, ambayo imekuwa laana mbaya katika zama zote. Maonyo yake kuhusu kutowafuata viongozi vipofu yamewekwa kwenye kumbukumbu kuwa tahadhari kwa vizazi vijavyo.

Kanisa Katoliki linawapa viongozi wake haki ya kufasili Maandiko. Ijapokuwa matengenezo yaliruhusu Maandiko kwa watu wote, bado kanuni ile ile iliyotumiwa na Kanisa la Roma inawazuia watu wengi katika makanisa ya kiprotestanti kutojisomea Maandiko wao wenyewe. Wanafundishwa kuyapokea mafundisho yake kama yanavyofasiliwa na kanisa. Maelfu hawapati chochote, hawayafahamu Maandiko jambo ambalo ni kinyume na imani zao.

Wengi wako tayari kusalimisha mioyo yao kwa wachungaji. Pasipo kujua wanayaacha mafundisho ya Mwokozi. Lakini je wachungaji hawawezi kukosea? Tunawezaje kuamini mwongozo wao isipokuwa tumejifunza kutoka katika Neno la Mungu ya kuwa wao ni wabeba nuru? Upungufu wa ujasiri wa kimaadili unawafanya wengi kuwafuata wasomi na wanaishia kwenye makosa pasipo matumaini. Wanauona ukweli wa wakati huu ndani ya Biblia na

wanaona Roho Mtakatifu akiongoza ujumbe unaohubiriwa, lakini bado wanawaruhusu wachungaji kuwaondoa kutoka kwenye nuru.

[361] Shetani anawashikilia watu wengi kwa kuwaunganisha kwa kamba za urafiki na wale ambao ni maadui wa msalaba Wakristo. Muungano huu waweza kuwa wa wazazi, wa mtoto wa kike au kiume, wa ndoa au wa kijamii. Roho za watu katika hali ya kuhangaika hazina ujasiri wa kuyatii yale wanayoyaamini kuwa ni wajibu wao.

Wengi watasema haidhuru kile mtu anachokiamini, ikiwa maisha yake ni sahihi. Lakini maisha hujengwa na imani. Kama ukweli uko ndani ya uwezo wetu kuufikia na tukashindwa kuuzingatia tutakuwa tumeukataa tukichagua giza badala ya nuru.

Kutojua isiwe kisingizio cha kosa au dhambi, wakati kila fursa ipo ya kufahamu mapenzi ya Mungu. Mtu anayesafiri akifika sehemu ambapo kuna barabara kadhaa na kuna mabango yanayoonesha kila moja iendako, ikiwa atapuuzia yale mabango na kupita njia yoyote aonayo kuwa sahihi, anweza kufanya hivyo lakini atajikuta katika njia isiyo sahihi.

## Wajibu wa Kwanza wa Muhimu

Haitoshi kuwa na dhamiri njema, kufanya kile mtu anachokifikiri kuwa ndio sahihi au kile mchungaji anachomwambia kuwa ni sahihi. Yampasa ayachunguze Maandiko yeye mwenyewe. Anayo chati inayoonesha kila alama ya barabarani katika safari ya kuelekea mbinguni, na hatakiwi kubahatisha katika lolote.

Ni wajibu wa kwanza na wa muhimu wa kila kiumbe mwenye akili kujifunza kutoka katika Maandiko nini maana ya ukweli na kisha kutembea katika nuru na kuwatia moyo wengine kufuata mfano wake. Yatupasa tujihukumu sisi wenyewe kama ambavyo tutakavyojibu kwa ajili yetu mbele za Mungu.

Wasomi, wakijifanya wenye hekima kubwa wanafundisha kwamba Maandiko yana siri, na kwamba yana maana ya kiroho isiyoweza kueleweka kutokana na lugha inayotumika. Watu hawa ni walimu wa uongo. Lugha ya Biblia yapasa ifundishwe sawa-
[362] sawa na maana yake ya kawaida, isipokuwa pale ambapo mfano au vielelezo vimetumika. Kama watu wangeisoma Biblia jinsi ilivyo ingefanyika kazi ambayo ingewaleta kwa zizi la Kristo maelfu kwa maelfu ambao kwa sasa wanapotea katika ukosefu.

Maandiko ambayo wasomi wengi hawayaangalii kwa kina kana kwamba siyo ya muhimu yamejaa faraja kwa yule ambaye amejifunza katika shule ya Kristo. Uelewa wa ukweli wa Maandiko hautegemei sana uwezo wa akili katika kuyachunguza bali ni kuwa na kusudi moja, kuwa na shauku ya dhati ya kuipata haki.

### Matokeo ya Kupuuzia Maombi na Kujifunza Biblia

Kujifunza Biblia kusifanyike bila maombi. Roho mtakatifu pekee ndiye anayeweza kutufanya tuguswe na umuhimu wa mambo ambayo ni rahisi kuelewa au kutuepusha kushindana na mambo ambayo ni vigumu kuyaelewa. Malaika wa mbinguni wanauandaa moyo kulielewa Neno la Mungu. Tutavutwa na uzuri wake, tukionywa na kuimarishwa na ahadi zake. Mara nyingi majaribu yanaonekana kama yasiyopingika kwa sababu yule anayejaribiwa hawezi kuzikumbuka ahadi za Mungu na kukabiliana na Shetani kwa silaha ya Maandiko. Lakini malaika wanawazunguka wale ambao wako tayari kujifunza na wanawakumbusha ukweli unaohitajika.. . .

"Yeye atakufundisha mambo yote na kukukumbusha yale yote niliyokuambia'-Yn. 14:26. Lakini sharti mafundisho ya Kristo yawe yametunzwa mawazoni ili Roho wa Mungu aweze kutukumbusha wakati wa shida.

Mustakabali wa wakazi wa wanaoijaza dunia unakaribia kuamuliwa. Yampasa kila mfuasi Wakristo aombe kwa bidii: "Nifanye nini, Bwana?" Matendo 22:10.(Angalia pia Matendo 9:6.) Yatupasa tujitahidi sasa kuwa na uzoefu wa kina na ulio hai katika mambo ya Mungu. Hatuna muda wa kupoteza. Tupo katika uwanja wa Shetani. Msilale, askari wa Mungu.

Wengi wanajipongeza kwa kutofanya mambo mabaya. Haitoshi wao kuwa miti katika bustani ya Mungu. Wanapaswa kuzaa matunda. Katika vitabu vya mbinguni wameandikwa kama vikwazo ardhini. Na kwa wale ambao wameichezea rehema ya Mungu na kuitumia vibaya neema yake moyo wenye upendo wa kuvumilia bado unasihi.

Katika kipindi cha kiangazi kunakua hakuna tofauti iliyo wazi [363]
kati ya miti ambayo daima inakuwa na kijani kibichi na miti mingine, lakini kipindi cha upepo na baridi kinapokuja ile miti ya kijani kibichi haibadiliki wakati miti mingine inapukutisha. Hebu upinzani

uje, hebu ije hali ya kutovumiliana iliyo na msukosuko, hebu mateso yachochewe tena na wale walio na mashaka na wanaflki wataiacha imani. Lakini Mkristo wa kweli atasimama imara, imani yake ikiwa imara, tumaini lake liking'aa kuliko siku za mafanikio. "Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, Uenezao mizizi yake karibu na mto; Hautaona hofu wakati wa hari ujapo, Bali jani lake litakuwa bichi; wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda.Yeremia 17:8.

## Sura Ya 38 - Ujumbe Wa Mwisho Wa Mungu

[364]

U Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya maShetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza;. . . Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. "Ufunuo 18:1,2,4.

Tangazo lililotolewa na malaika wa pili wa ufunuo 14 (fungu la 8) litarudiwa na kutaja maovu ambayo yamekuwa yakiingia Babeli tangu ujumbe huo ilipotolewa mwanzoni.

Hali mbaya inaelezwa hapa. Kwa kila ukataaaji wa ukweli akili za watu zinatiwa giza, mioyo yao ikiwa migumu zaidi. Wataendelea kukanyaga moja ya kanuni za Amri Kumi mpaka kuflkia hatua ya kuwatesa wale wanaoiamini kanuni hiyo kuwa ni takatifu. Kristo anaonekana kwamba sio kitu kwa sababu ya kudharau Neno lake na watu wake.

Kudai kuwa na dini kutatumika kama pazia la kufunika maovu. Imani ya mizimu inafungua mlango kukaribisha mafundisho ya Shetani na kwa hiyo mvuto wa malaika waovu utaonekana makanisani. Babeli amejaza kipimo cha hatia yake, na uharibifu unakaribia kutokea.

Lakini Mungu bado anao watu katika Babeli na waaminifu hawa ni lazima waitwe ili "wasishiriki dhambi zake na kupokea mapigo yake." Malaika atashuka kutoka mbinguni akiiangazia dunia utukufu wake na kutangaza dhambi za Babeli. Mmwito utasikika, "tokeni kwake watu wangu" matangazo haya yana beba onyo la mwisho litakalotolewa kwa watu wa dunia.

Nguvu za dunia zikiungana katika vita dhidi ya amri za Mungu zitatangaza kwamba, "wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa" Ufunuo 13:16. Watazifuata tamaduni za kanisa kwa kuitunza sabato ya uongo. Wale wote

[365] watakaokataa hatimaye watatangaziwa kustahili amri ya kifo. Kwa upande mwingine sheria ya Mungu inayojumuisha siku ya Bwana ya kupumzika inatishia ghadhabu dhidi ya wale wote wanaoasi maagizo yake.

Kwa mambo ambayo yameelezwa bayana, yeyote atakayeikanyaga sheria ya Mungu na kuyatii maagizo ya wanadamu atapokea alama ya mnyama, ishara ya utii kwa mamlaka achaguayo kuitii badala ya Mungu. “Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake.” Ufiinuo 14:9,10

Hakuna hata mmoja atakayetaabika kwa ghadhabu ya Mungu mpaka pale ukweli utakapokuwa umeeleweka akilini mwake na dhamiri yake imeukataa. Wengi hawajapata fursa ya kusikiliza ujumbe wa pekee wa wakati huu. Yeye asomaye moyo wa kila mtu hatamwacha yeyote aliye na shauku ya ukweli adanganyike katika masuala ya pambano kuu. Kila mmoja atapkuwa na nuru ya kutosha ili afanye uamuzi wake kwa busara.

## Jaribio Kuu la Uaminifu

Sabato, jaribu kuu la uaminifu, ni ukweli ambao kwa nanma ya pekee unakanushwa. Wakati ushikaji wa sabato ya uongo utakuwa ndicho kiapo cha uaminifu kwa mamlaka inayopingana na Mungu; ushikaji wa Sabato ya kweli ni ushahidi wa utiifu kwa Muumbaji. Wakati ambapo kundi moja la watu linapokea alama ya mnyama lingine linapokea muhuri wa Mungu.

Utabiri anaonesha kwamba kutovumiliana katika mambo ya kidini kutatawala, kwamba kanisa na serikali vitawatesa wale wanaozishika amri za Mungu; umetamkwa kuwa hauna msingi na ni upuzi.. Lakini ushikajiwa Jumapili unavyoendelea kubishaniwa pote, tukio ambalo kwa muda mrefu limetiliwa shaka linaonekana kukaribia, ujumbe utakuwa na matokeo ambayo usingekuwa nayo hapo kabla.

Katika kila kizazi Mungu ametuma watumishi wake kukemea dhambi duniani na kanisani. Wanamatengenezo wengi walipokuwa
[366] wakianza kazi yao waliazimia kuwa na hadhari katika kushambulia

dhambi za kanisa na za taifa. Walitumaini kwamba kwa kuwa kielelezo cha maisha safi ya Ukristo watawaongoza watu wairejee Biblia. Lakini Roho wa Mungu alikuja juu yao; pasipo kuogopa matatizo hawakuacha kuhubiri mafundisho yaliyo wazi ya Biblia.

Kwa hiyo ujumbe utahubiriwa. Mungu atatenda kazi kwa kutumia vyombo duni ambavyo vimejiweka wakfu kwa ajili ya huduma yake. Watenda kazi watakamilishwa kwa kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu kuliko mafunzo ya taasisi za masomo. Watu watahamasika kwenda kazini wakiwa na ari takatifu wakitamka maneno ambayo Mungu amewapatia. Dhambi za Babeli zitawekwa wazi. Watu watachochewa. Maelfu hawajawahi kusikia maneno kama haya. Babeli ni kanisa lililoanguka kwa sababu ya dhambi zake, kwa sababu ya kuupuzia ukweli. Kama vile watu waendavyo kwa walimu wao wakiwa na swali kwamba "Je, mambo haya ndivyo yalivyo?" wachungaji watawajibu kwa kuwaeleza hadithi za uongo ili kuzinyamazisha roho zaozilizoamshwa. Lakini kwa sababu wengi wanadai andiko lililowazi kwamba "hivi ndivyo asemavyo Bwana," huduma inayopendwa itawachochea watu wengi wanaopenda dhambi kuwakosoa na kuwatesa wale wanaoihubiri Injili hiyo.

Viongozi wa dini wataweka jitihada zisizo za kawaida ili kuzuia ukweli, kupinga mjadala wa maswali haya muhimu. Kanisa litaomba msaada wa mkono wenye nguvu wa mamlaka za kiraia na katika kazi hii wafuasi wa Papa na Waprotestanti wataungana. Kadiri harakati za kulazimisha ibada ya Jumapili zinavyozidi kuwa imara, washika amri watatishiwa kwa kulipishwa faini na kufungwa magerezani. Baadhi wataahidiwa kupewa vyeo vya mvuto na zawadi nyingine ili wazikane imani zao. Lakini jibu lao litakuwa "tuoneshe kutoka kwenye Neno la Mungu kosa letu." Wale watakaoshtakiwa mahakamani kufanya udhihirisho wenye nguvu wa ukweli, na baadhi wanaowasikia wataongozwa kufanya uamuzi wao wa kuzishika amri zote za Mungu. Vinginevyo maelfu hawatajua chochote kuhusu ukweli huu.

Utii kwa Mungu utachukuliwa kuwa ni kuasi. Wazazi watakuwa wakali kwa watoto wanaoamini. Watoto hawatapewa urithi na watafukuzwa nyumbani. "Wale wote watakao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." . . 2 Timotheo 3; 12. Kadrii watetezi wa ukweli watakavyozidi kuikataa Jumapili, baadhi [367]

yao watatupwa magerezani, wengine kupelekwa uhamishoni, na wengine watatendewa kama watumwa. Kadiri Roho wa Mungu anavyoendelea kuondolewa kutoka kwa watu kutakuwa na mambo ya ajabu yatakayoendelea. Moyo wa mwanadamu naweza kuwa na ukatili sana ikiwa upendo na hofu ya Mungu vimeondolewa.

## Dhoruba Inakaribia

Kadiri dhoruba inavyokaribia, kundi kubwa ambalo limeikiri imani katika ujumbe wa malaika wa tatu lakini hawajatakaswa kwa njia ya utii wa Maandiko wataziacha nafasi zao na kujiunga na upinzani. Kwa kuungana na dunia wamekuja kuyaona mambo karibia kwa uelewa ule ule, na wanachagua upande unaopendwa na wengi. Watu ambao hapo mwanzo walifurahia katika ukweli wanatumia talanta zao na hotuba nzuri kuzipotosha roho. Wanakuwa maadui wakali wa ndugu zao wa zamani. Waasi hawa ni mawakala madhubuti wa Shetani katika kuwawakilisha vibaya na kuwashtaki washika Sabato na kuwafanya watawala wawachukie.

Watumishi wa Bwana wametoa onyo. Roho wa Bwana amewabidisha. . Hawajaangalia faida zao za kitambo au kufikiria kutunza heshima zao au maisha yao. Kazi inaonekana kubwa kuzidi uwezo wao wa kuikamilisha. Lakini pamoja na hayo hawawezi kurudi nyuma. Wakijisikia wasio kuwa na uwezo wa kufanya chochote, wanamkimbilia mwenye nguvu ili kupewa nguvu.

Vipindi tofauti katika historia vimetambulika kwa maendeleo ya ukweli fulani wa pekee, ulipokelewa ili kukidhi mahitaji ya watu wa Mungu kwa wakati huo. Kila ukweli mpya umefaulu kuushinda upinzani. Mabalozi Wakristo lazima watekeleze majukumu yao na wamwachie Mungu matokeo.

## Upinzani Kuinuka Katika Viwango vya Juu Zaidi

Kadiri upinzani unavyoinuka katika viwango vya juu vya ukali, watumishi wa Bwana watafathaishwa tena, kwa sababu itaonekana kwao kuwa wameleta zahama. Lakini dhamiri zao na Neno la Mungu vitawathibitishia kwamba msimamo wao ni sahihi. Imani na ujasiri wao vitainuka tayari kwa ajili ya wakati wa hatari, ushuhuda

wao ni "Kristo amezishinda nguvu za dunia, na je, tutaiogopaje dunia ambayo tayari imeshindwa?"

Hakuna mtu awezaye kumtumikia Mungu pasipo kusimama kinyume na upinzani wa majeshi ya giza. Malaika waovu watamshambulia, wakitambua kwamba mvuto wake unachukua mawindo kutoka mikononi mwao. Watu waovu watajitahidi kumtenganisha na Mungu kwa kumshawishi kwa majaribu makali. Ikiwa hawatafanikiwa kwa njia hizi nguvu itatumika kuilazimisha dhamiri. [368]

Lakini kadiri Yesu anavyoendelea kuwa mpatanishi wa mwanadamu katika patakatifu pa mbinguni, nguvu ya ushawishi ya Roho Mtakatifu inatenda kazi kwa watawala na watu. Wakati wengi wa watawala wetu ni mawakala hai wa Shetani, Mungu pia anao mawakala wake miongoni mwa watu wanaoongoza mataifa. Watu wachache watasimama kupinga wimbi lenye nguvu la uovu. Upinzani wa maadui wa kweli utadhibitiwa ili ujumbe wa malaika wa tatu ufanye kazi yake. Onyo la mwisho litavuta usikivu wa viongozi hawa, na baadhi wataupokea na kusimama na watu wa Mungu katika wakati wa taabu.

Mvua ya Masika na Kilio Kikuu

Malaika anayeungana na malaika wa tatu ataiangazia dunia yote kwa utukufu wake. Ujumbe wa malaika wa kwanza ulipelekwa katika kila kituo cha utume duniani, na katika baadhi ya nchi kulikuwa na mwitikio mkubwa wa kidini ulioshuhudiwa tangu wakati wa Matengenezo. Lakini matokeo haya yatapitwa na onyo la mwisho la malaika wa tatu.

Kazi itakuwa kama ile ya kipindi cha Pentekoste. "Mvua ya vuli" ilimwagwa katika kipindi cha ufunguzi wa Injili ili kuotesha mbegu ya thamani; kwa hiyo "mvua ya masika" itamwagwa wakati wa kufungwa kwa Injili ili kuivisha mavuno.. Hosea 6:3, Yoeli 2:23. Kazi kubwa ya Injili haitafungwa kukiwa na udhihirisho mdogo wa nguvu ya Mungu kuliko ilivyoshuhudiwa katika ufunguzi wake. Unabii uliotimia wakati wa mvua ya awaliwakati wa ufunguzi wa Injili utatimizwa tena katika mvua ya masika wakati wa kufungwa kwa Injili. hizi ndizo "nyakati za kuburudishwa" ambazo mtume Petro alizitazamia wakati aliposema "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifiitwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani." Matendo 3:19,20.

[369] Watumishi wa Mungu, nyuso zao ziking'aa kwa kujitoa wakfu, wataharakisha kutoka sehemu moja kwenda nyingine kuutangaza ujumbe wa mbinguni. Miujiza itatendeka,wagonjwa wataponywa. Shetani pia atatenda kazi kwa miujiza ya uongo hata kushusha moto kutoka mbinguni.-Ufunuo 13:13 kwa hiyo watu wa dunia watapaswa wawe na msimamo.

Ujumbe hautahubiriwa kwa msingi wa hoja ila kwa ushawishi wa kina wa Roho wa Mungu. Hoja zilikuwa zimetolewa, machapisho yaliwapa mvuto, lakini wengi hawakuuelewa ukweli. Sasa ukweli utaonekana jinsi ulivyo.. Mwunganiko wa familia, mahusiano ya kanisa hayana nguvu sasa kuwazuia watoto waaminifu wa Mungu. Pamoja na kwamba mawakala wameungana dhidi ya ukweli, idadi kubwa watafanya uamuzi wao kuwa upande wa Bwana.(Tense)

## Sura Ya 39 - Wakati Wa Taabu [370]

U Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile." Danieli 12:1.

Wakati ujumbe wa malaika wa tatu utakapofungwa, watu wa Mungu watakuwa wamekamilisha kazi yao. Watakuwa wamepokea "mvua ya masika" na wamejiandaa kwa ajili ya saa ya majaribu iliyo mbele yao. Jaribu la mwisho litakuwa limeletwa duniani na wote ambao wamethibitika kuwa waaminifu kwa sheria za mbingu watakuwa wamepokea "muhuri wa Mungu aliye hai." Kisha Yesu atakoma kufanya kazi yake ya upatanisho katika patakatifu pa mbinguni na kwa sauti kubwa atasema "imekwisha." "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa."- Ufunuo22:ll. Kristo atakuwa amefanya upatanisho kwa ajili ya watu wake na kufuta dhambi zao. "Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote," (Danieli 7:27) umekaribia kutolewa kwa warithi wa wokovu na Yesu atatawala kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Atakapoondoka katika patakatifu, giza litawafunika wakazi wa dunia. Wenye haki itawapasa waishi mbele za Mungu Mtakatifu pasipo mpatanishi. Kiizuizi kwa watu waovu sasa kitakuwa kimeondolewa na Shetani atakuwa na udhibiti kamili kwa wale ambao hawakutubu. Hatimaye Roho wa Mungu atakuwa ameondolewa. Shetani atawaingiza watu wa dunia kwenye taabu kuu ya mwisho. Malaika wa Mungu wataacha kuzuia pepo kali za tamaa za wanadamu. Dunia yote itaingizwa katika maangamizi mabaya kuliko yale yalioipata Yerusalemu ya zamani. Zipo nguvu ambao ziko tayari hivi sasa, zinazosubiri ruhusa ya Mungu, kueneza uharibifu kila mahali.

Wale wanaoiheshimu sheria ya Mungu watachukuliwa kuwa ndio wanaosababisha migogoro ya kutisha na umwagaji damu ulioenea duniani pamoja na huzuni.Uwezo ulio kwenye onyo la mwisho utawakasirisha waovu na Shetani ataweka roho ya chuki na mateso dhidi ya wale wote watakaokuwa wameupokea ujumbe.

[371] Uwepo wa Mungu ulipokuwa ametolewa kwa taifa la Wayahudi, makuhani na watu bado walijihesabu kwamba wao ni wateule wa Mungu. Huduma za hekaluni ziliendelea; kila siku baraka ya mbingu ilitolewa kwa watu ambao walikuwa na hatia ya damu ya Mwana wa Mungu. Kwa hiyo uamuzi usioweza kubadilika wa patakatifu utakapokuwa umetangazwa na hatima ya dunia itakapokuwa imekwisha kuamriwa milele, wakazi wa dunia hawatajua. Mitindo ya dini itaendelezwa na watu ambao Roho wa Mungu atakuwa ameondolewa kutoka kwao; ari ya Shetani ya kutaka mafanikio ya mbinu za uharibifu itafanana na ari kwa ajili ya Mungu.

### Wakati Wa Taabu Ya Yakobo.

Kadiri Sabato itakavyozidi kuwa mada kuu iletayo utata kwa jamii ya Wakristo, itaamriwa kwamba wale wachache wanaopingana kanisa na serikali hawapaswi kuvumiliwa, kwamba ni heri wao kuteseka kuliko taifa lote kuingia katika machafuko na vurugu. Hoja hiyo hiyo ilitolewa dhidi ya Kristo,"wala hamfikiri ya kwamba yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie taifa zima." Yohana 11:50. Hoja hii itaonekana kuwa ni hitimisho; hatimaye amri itatolewa dhidi ya wale wote wanaoiheshimu Sabato ya amri ya nne, kiwashutumu ni wakosaji na kuwapa watu uhuru baada ya muda fulani kuwaua. Ukatoliki wa ulimwengu wa zamani na Uprotestanti ulioasi katika ulimwengu wa kisasa utatekeleza jukumu lile lile. Kisha watu wa Mungu wataingizwa katika hayo matukio ya mateso ambayo yanajulikana kama "taabu ya Yakobo."-Yeremia 30:5-7.

Usiku wa uchungu kwa Yakobo, alipokesha katika maombi ili aokolewe na mikono ya Esau; (Mwanzo 32:24-30) unawakilisha uzoefu wa watu wa Mungu wakati wa taabu. Kwa sababu ya uongo aliousema ili apate baraka za baba yake zilizokuwa zimekusudiwa kwa ajili ya Esau, Yakobo alitoroka, ikiogopa vitisho vikali vya kaka yake. Baada ya kukaa miaka kama mkimbizi, alipanga kurudi nyum-

bani kwao. Alipofika mpakani alijawa na hofu kutokana na taarifa za kuja kwa Esau, ambaye bila shaka angelipiza kisasi. Tumaini pekee la Yakobo lilikuwa ni rehema za Mungu; ulinzi wake pekee ulipaswa kuwa ni maombi.

Akiwa yeye na Mungu, aliungama dhambi zake kwa unyenyekevu. Zahama ilikuwa imemfikia katika maisha yake. Aliendelea kuomba katika gizani. Ghafla mkono uliwekwa begani mwake. Alidhani adui alikuwa akiutafuta uhai wake. Kwa nguvu zote akiwa amekata tamaa alipambana na adui yake. Kulipoanza kupambazuka, malaika alitumia nguvu zisizokuwa za kawaida. Yakobo alionekana kuishiwa nguvu na akaanguka, akiomba na kulia, shingoni mwa mpinzani wake wa ajabu. Ndipo alitambua kuwa alikuwa akipambana na malaika wa agano. Kwa muda mrefu alikuwa amevumilia kuugua kwa nafsi kulikotokana na dhambi yake; sasa alipaswa kuwa na uhakika kuwa ilikuwa imesamehewa. Malaika akamwambia, "Niache, niende, maana kunapambazuka" lakini Yakobo akamwambia "sikuachi usiponibariki" Yakobo aliungama kutostahili kwake, akatumainia rehema za Mungu mwenye kushika agano. Kwa njia ya toba na kujisalimisha, huyu mdhambi apatikanaye na mauti alimshinda Mwenye enzi wa mbinguni. [372]

Shetani alikuwa amemshitaki Yakobo mbele za Mungu kwa sababu ya dhambi yake, akamshawishi Esau aende kupambana naye. Katika usiku wa mieleka wa mzee Yakobo, Shetani alikusudia kumkatisha tamaa na kuvunja tumaini lake kwa Mungu. Alikuwa amefikishwa karibu na hali ya kuvunjika moyo; lakini alikuwa amefanya toba ya dhati ya dhambi yake na kumng'ang'ania malaika akiomba kwa bidii na machozi hadi akashinda.

Namna Shetani alivyomshtaki Yakobo, ndivyo atakavyo yaleta mashtaka yake dhidi ya watu wa Mungu. Anazifahamu vizuri dhambi ambazo alizitumia kuwashawishi wazitende na anatangaza kwamba kwa kufuata haki, Bwana hawezi kuwasamehe dhambi zao bado amuangamize yeye pamoja na malaika zake. Anadai kuwa wakabidhiwe mikononi mwake ili waangamizwe.

Bwana atamruhusu ili awajaribu kwa kiwango cha juu. Ujasiri wao kwa Mungu, imani yao itajaribiwa vikali. Kadiri watakavyokumbuka maisha yao yaliyopita, matumaini yao yatazama, kwa sababu katika maisha yao yote wataweza kuona mema machache. Shetani atajitahidi kuwatishia ka dhana kwamba

hakuna matumaini katika mashtaka yao. Kwa njia hiyo atakusudia kuharibu imai yao na kwamba watashawishika kwa majaribu yake na kugeuka na kuuacha uaminifu wao kwa Mungu.

[373] **Mungu Analaumiwa Kwa Sababu ya Maumivu**

Lakini uchungu ambao watu wa Mungu wataupata hautakuwa hofu ya mateso. Watahofu kuwa kwa sababu ya makosa yao fulani, ahadi ya Mwokozi: "Mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi."- Ufunuo 3:10, haitatimia kwao.. Wakidhihirisha kutostahili kwao kwa sababu ya upungufu katika tabia zao, jina takatifu la Mungu litatukanwa.

Wataikumbuka toba ya zamani juu ya dhambi zao nyingi na wataomba ahadi ya mwokozi: "Au azishike nguvu zangu, Afanye amani nami; Naam, afanye amani nami." Isaya 27:5. Hata kama watasumbuliwa na mateso, msongo na huzuni; hawataacha kuomba. Watamshika Mungu kama Yakobo alivyomshika malaika, na lugha ya roho zao itakuwa "Sitakuachia uende, mpaka unibariki."

**Kufutwa kwa Dhambi**

Katika kipindi cha taabu, kama watu wa Mungu watakuwa na dhambi ambazo hawakutubu, ambazo zitatokea mbele yao wakati wakiwa katika ile hofu na uchungu; kwa hakika watashindwa. Kukata tamaa kutaondoa imani yao, na hawataweza kumsihi Mungu awaokoe. Lakini hawatakuwa na makosa yoyote yatakayohitaji kufunuliwa. Dhambi zao zitakuwa zimetangulia kwenye hukumu na kuondolewa, na hawataweza kuzikumbuka.

Katika kushughulika na Yakobo, Bwana ameonesha kwamba hawezi kuvumilia uovu. Wale wote wanaotoa udhuru au kuzificha dhambi zao na kuruhusu ziendelee kuwepo kwenye vitabu vya mbinguni bila kutubu na kusamehewa wanashindwa na Shetani. Kwa kadiri wanavyozidi kupanda vyeo, ndivyo adui yao anavyozidi kuwashinda. Wanaochelewa kufanya maandalizi hivi sasa hawatapata nafasi hiyo wakati wa taabu. Hali ya watu wote kama hao haina matumaini.

Historia ya Yakobo ni uhakika pia kwamba Mungu hatawatupa wale ambao baada ya kudanganyika dhambini, wameamua kurudi kwake kwa toba ya kweli. Mungu atatuma malaika kuwafariji wakati wa shida. Jicho la Bwana lipo juu ya watu wake. Miali ya moto wa tanuru inaonekana karibu itawaangamiza, lakini msafishaji atawatoa wakiwa kama dhahabu iliyojaribiwa motoni.

## Imani Inayostahimili [374]

Wakati wa mateso na maumivu makali ulio mbele yetu utahitaji imani inayoweza kustahimili uchovu, kuchelewa, na njaa, imani ambayo haitazimia hata kama itajaribiwa vikali. Ushindi wa Yakobo ni ushahidi wa nguvu ya maombi yasiyokoma. Wale wote watakaozishikilia ahadi za Mungu kama alivyofanya Yakobo, watashinda kama alivyoshinda. Kupigana mieleka na Mungu-ni wachache kiasi gani wale wanaojua maana yake! Wakati mawimbi ya mashaka yanapomwathiri muombaji, ni wachache sana wanaoshikilia kwa imani ahadi za Mungu.

Wale ambao wanaonesha imani kidogo sasa, wako katika hatari kuu ya kuangukia kwenye uwezo wa Shetani wa udanganyifu. Na hata kama watastahimili jaribio watatumbukizwa katika mateso mazito wakati wa taabu, hii ni kwa sababu hawakuifanya kuwa tabia yao kumtumainia Mungu. Yatupasa wakati huu tuthibitishe ahadi zake.

Mara nyingi taabu inakuwa kubwa wakati inapotarajiwa kuliko katika uhalisia, lakini hili sio kweli kuhusiana na Zahama iliyo mbele yetu. Maelezo yaliyo wazi kabisa hayawezi kufikia ukubwa wa majaribu. Wakati huo wa mateso kila nafsi lazima ijisimamie mbele za Mungu.

Wakati huu ambapo kuhani mkuu anafanya upatanisho kwa ajili yetu, yatupasa tujitahidi kuwa wakamilifu katika Kristo. Mwokozi wetu hakufikishwa hatua ya kuanguka katika jaribu hata kwa wazo moja. Shetani anatafuta mahali ndani ya moyo wa mwanadamu anapoweza kuweka makao, tamaa fulani mbaya inatunzwa, ambayo anaitumia majaribu yake yanapata uwezo wake. Lakini Kristo alisema kuhusu yeye mwenyewe: "Mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu." Yohana 14:30. Shetani hakukupata kasoro yoyote katika maisha ya Mwana wa Mungu ambayo ingemwezesha

kupata ushindi. Hakukuwa na dhambi katika maisha yake ambayo Shetani angeitumia kwa manufaa yake. Hii ndio hali wanayotakiwa kuwa nayo wale watakaoshinda katika wakati wa taabu.

[375] Ni katika maisha haya ndipo tunatakiwa kujitenga na dhambi, kwa njia ya imani katika damu ya upatanisho ya Kristo. Mwokozi wetu wa thamani, anatualika tujiunge naye, tuunganishe udhaifu wetu na nguvu zake, tuunganishe kutostahili kwetu na kufaa kwake. Ni jukumu letu kushirikiana na mbingu katika kazi ya kutengeneza tabia zetu ili zifikie mfano wa mbinguni.

Kazi ya Shetani ya udanganyifu na uharibifu itafikia katika kilele chake wakati wa taabu. Mionekano ya kutisha ya kiumbe asiye wa kawaida itafunuliwa angani, katika sura ya uwezo wa maShetani wa kutenda miujiza. Roho za maShetani zitaenda kwa "wafalme wa dunia" na duniani kote kuwashawishi ili waungane na Shetani katika jitihada zake za mwisho dhidi ya serikali ya mbinguni. Watu watainuka wakijifanya kuwa wao ni Kristo mwenyewe. Watafanya miujiza ya uponyaji na kukiri kwamba wana ufunuo kutoka mbinguni unaopingana na Maandiko.

Kama tendo la mwisho katika igizo kuu la udanganyifu, Shetani mwenyewe atamwigiza Kristo. Kanisa kwa muda mrefu limetazamia kuja kwa Mwokozi kama utimilifu wa matumaini yote. Sasa mdanganyifu mkuu atafanya ionekane kuWakristo amekuja. Shetani atajidhihirisha mwenyewe kama kiumbe mwenye nguvu aliye na nuru inayong'ara , akifanana na maelezo ya Mwana wa Mungu katika Ufunuo.(Ufunuo 1:13-15).

Utukufu utakaomzunguka Shetani haupitwi na kitu chochote ambacho macho ya mwanadamu yamewahi kukiona. Sauti kuu ya ushindi itasikika "Kristo amekuja!" Watu wataanguka kifudifudi mbele zake. Naye atainua mikono yake na kuwabariki. Sauti yake ni laini lakini tamu. Kwa kutumia sauti ya huruma ataeleza baadhi ya kweli zile zile za mbinguni ambazo Mwokozi alizitamka. Ataponya magonjwa, kisha kwa kujifanya ana tabia ya Kristo, atadai kwamba aliibadilisha Sabato kuwa Jumapili. Atasema kwamba wale wanaoishika siku ya saba takatifu wanalikufuru jina lake. Huu ni udanganyifu mkubwa unaoangusha. Wengi watausikiliza uchawi huu, wakisema, "Huu ni uweza wa Mungu, ule Mkuu." Matendo 8:10.

### Watu wa Mungu Hawatapotoshwa [376]

Lakini watu wa Mungu hawatapotoshwa. Mafundisho ya kristo huyu wa uongo hayapatani na Maandiko Matakatifu. Baraka zake zinatolewa kwa wale wanaomwabudu mnyama na sanamu yake, kundi lile lile ambalo Biblia inasema watakinywea kikombe cha ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa na maji.

Zaidi ya hayo, Shetani hataruhusiwa kufanya udanganyifu wa namna ujio Wakristo utakavyokuwa. Kristo amewaonya watu wake dhidi ya udanganyifu juu ya jambo hili. "Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.. .Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki. Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." Mathayo 24:24-27. Angalia pia Mathayo 25:31; Ufunuo 1:7; 1 Wathesalonike 4:16,17; Ujio huu, hakuna uwezekano wa kuupotosha. Utashuhudiwa na dunia yote.

Ni wanafunzi tu wenye bidii ya kujifunza Maandiko ambao wamepokea upendo wa kweli watakaosimama imara dhidi ya udanganyifu unaouteka ulimwengu. Kwa ushuhuda wa Biblia hawa watamtambua mdanganyifu katika hila zake. Je watu wa Mungu wameimarika vilivyo katika neno lake kiasi cha kutoshawishiwa na ushahidi wa akili zao? Je, katika zahama kama hii wataing'ang'ania Biblia, na Biblia pekee?

Kwa vile tamko litakalotolewa na viongozi mbalimbali wa ulimwengu wa Ukristo dhidi ya washika amri litapelekea kuondolewa kwa ulinzi wa serikali na kuwaacha mikononi mwa wale wanaotaka kuwaharibu; watu wa Mungu watakimbia kutoka kwenye miji na vijiji kujiunga pamoja kwenye makundi, wakiishi mahali palipo ukiwa na upweke kabisa.. Wengi watatafuta makao katika maeneo ya milimani, kama Wakristo wa mabonde ya Piedmont. (Angalia sura ya nne). Lakini watu wengi kutoka mataifa yote na madaraja mbalimbali, wa hali ya juu na ya chini, maskini na matajiri,, weupe na weusi, watatupwa katika utumwa usio wa haki na wa kikatili. Wapendwa wa Bwana watapitia katika siku za kuchosha wakifungwa magerezani, watahukumiwa kuchinjwa, wataachwa wafe gizani katika magereza ya ardhini.

[377] Je, Bwana atawasahau watu wake katika saa hii ya kujaribiwa? Je, aliwasahau watu wakewaaminifu Nuhu, Lutu, Yusufu, Eliya, Yeremia au Danieli? Japo adui awatupa gerezani, lakini kuta za gereza la ardhini, hataweza kukata mawasiliano kati ya roho zao na Kristo. Malaika watawaijia kwenye vyumba hivyo vyenye upweke. Gereza litakuwa kama ikulu, kuta zitaangaziwa nuru kama ilivyokuwa kwa Paulo na sila walipoimba usiku wa manane katika gereza kule Filipi.

Hukumu ya Mungu itawaangukia wale wanaotafuta kuwaangamiza watu wake. Kwa Mungu hukumu ni "tendo la ajabu." Isaya 28:21; Angalia pia Ezekieli 33:11. "Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe." Kutoka 34:6,7; Nahumu 1:3. Taifa ambalo amelivumilia na ambalo limekijaza kikombe cha uharibifu wake hatimaye litakunywa kikombe cha ghadhabu ya Mungu kisichochanganywa na rehema.

Kristo atakapoacha kufanya upatanisho katika patakatifu pa mbinguni, ghadhabu isiyochanganywa na maji dhidi ya wale wanaomwabudu mnyama itamwagwa. Mapigo kule Misri yalifanana na hukumu zile zilizokuwa za kutisha ambazo ndizo zitakazoupata ulimwengu kabla ya ukombozi wa mwisho wa watu wa Mungu. Mwandishi wa Ufunuo anasema: "Pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake." Bahari, "ikawa damu kama damu ya mfu ... mito na chemchemi za maji; zikawa damu." na malaika akasema, "Wewe u mwenye haki, uliyeko na uliyekuwako, Mtakatifu, kwa kuwa umehukumu hivi; Kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na ya manabii, nawe umewapa damu wainywe; nao wamestahili." Ufunuo 16:2-6. Kwa kuwahukumu watu wa Mungu adhabu ya kifo, hakika wamepokea hatia ya damu yao kana kwamba ilimwagwa kwa mikono yao. Kristo alisema juu ya hatia ya Wayahudi wa wakati wake ya umwagaji damu ya watakatifu tokea zamani za Habili (Mathayo 23:34-36), kwa kuwa wao pia walikuwa na roho ile ile kama wale wauaji wa manabii.

Katika pigo lililofuata, jua linapewa uwezo, "ili kuwaunguza wanadamu kwa moto." Ufunuo 16:8,9. Nabii anaeleza

kuhusu wakati huu wa kutisha, “Maana mavuno ya mashamba yamepotea...Naam, miti yote ya mashamba imekauka; maana furaha imekauka katika wanadamu...Jinsi wanyama wanavyougua! Makundi ya ng’ombe yamefadhaika, kwa sababu hawana malisho. ..Kwa maana vijito vya maji vimekauka, na moto umeyateketeza malisho ya nyikani.” Yoeli 1:11, 12, 18-20. [378]

Mapigo haya hayatapiga sehemu zote za dunia, lakini yatakuwa mapigo yanayotisha kuliko yote yaliyopata kutokea. Hukumu zote zitakazo tokea kabla ya mlango wa rehema kufungwa zitakuwa zimechanganywa na rehema. Damu ya Kristo inamlinda mwenye dhambi toka kwenye hatia kamili; lakini wakati wa hukumu ya mwisho utakapowadia, ghadhabu haitachanganyika na rehema. Wengi wataitamani rehema ya Mungu ambayo walikuwa wakiidharau.

Watu wa Mungu hawataachwa waangamie japokuwa wanateseka na kutaabika kwa sababu ya mambo mema. Malaika watawahudumia kwa mahitaji yao, . atapewa chakula chake; maji yake hayatakoma.” mimi, Bwana, nitawasikia, mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha.”Isaya 33:16; 41:17.

Lakini katika macho ya kibinadamu itaonekana kuwa watu wa Mungu watakuwa radhi kutia muhuri ushuhuda wa maisha yao kwa damu yao, kama walivyofanya wafia dini waliowatangulia. Utakuwa wakati wa uchungu wa kutisha. Waovu watawadhihaki kwa kusema, “Iko wapi sasa imani yenu? “Ikiwa kweli ninyi ni watu wa Mungu, kwa nini hajawakomboa kutoka mikononi mwetu?” Lakini watu watakaokuwa na subira watakumbuka jinsi Yesu alivyokuwa akifa pale msalabani. Kama Yakobo, wote watakuwa wakimng’ang’ania Mungu.

### Makundi ya Malaika Wanalinda

Malaika wamewekwa katika vituo kuwalinda wale ambao wamelitunza neno la subira la Kristo. Watakuwa wameshuhudia matatizo na kuwasikia wakitoa maombi yao. Watasubiri kauli ya Kamanda wao ya kuwadaka kutoka kwenye hatari yao. Lakini itawabidi wasubiri kwa kitambo kidogo. Watu wa Mungu sharti wakinywee kikombe na wabatizwe kwa ule ubatizo. Mathayo 20:20-

23. Lakini kwa sababu ya wateule muda wa mateso utafupishwa. Mwisho utafika haraka kuliko matarajio ya watu.

[379] Japokuwa tamko kuu litakuwa limekwisha weka muda maalum ambapo washika sheria watauawa, adui zao katika baadhi ya matukio watawashambulia kuondoa uhai wao. Lakini hakuna atakayeweza kuwapita walinzi watakaokuwa wameizingira kila nafsi yenye uaminifu. Wengine katika jitihada zao za kutoroka mijini watateswa, lakini mapanga yatakayoinuliwa dhidi yao yatavunjika kama mabua. Wengine watalindwa na malaika watakaoonekana kama watu ya vita.

Katika vipindi vyote vya historia malaika wametekeleza majukumu muhimu katika mambo ya wanadamu. Wameukubali ukarimu waliotendwa katika nyumba za watu, wamekuwa viongozi kwa wasafiri wa usiku, wamefungua milango ya magereza na kuwaweka huru watumishi wa Bwana. Waliliondoa jiwe kwenye kaburi la Mwokozi.

Malaika huenda kwenye makusanyiko ya watu waovu, kama walivyoenda sodoma kujua ikiwa wamevuka ukomo wa uvumilivu wa Mungu. Kwa ajili ya watumishi wachache wanaomtumikia Mungu kwa uhalisi, anazuia majanga na kudumisha amani kwa watu wengi. Wenye dhambi wanafahamu kidogo sana kwamba inawapasa kushukuru kwa sababu ya maisha yao ambayo yanalindwa kwa sababu ya waaminifu wachache ambao wao wanafuraia kuwatesa.

Mara kwa mara katika mabaraza ya dunia hii, malaika wamekuwa wasemaji. Masikio ya kibinadamu yamesikiliza maombi yao, midomo ya kibinadamu imedhihaki mashauri yao. Wajumbe hawa wa mbinguni wamedhihirisha uwezo mkubwa na kuwasaidia wale wanaoteseka kuliko walinzi walio bora sana wa kibinadamu. Wameyashinda na kuuzuia maovu ambayo yangesababisha mateso makubwa kwa watu wa Mungu.

Kwa hamu kubwa, watu wa Mungu wanasubiria dalili ya mfalme wao ajaye. Kadiri watu wanaoishandana na Mungu wananavyoendelea kusihi mbele zake. mbingu zitang’aa kwa mapambazuko ya milele. Kama ilivyo sauti tamu ya nyimbo za malaika, ndivyo yatakavyokuwa maneno yatakayoingia katika sikio: “msaada unakuja.” Sauti ya Kristo itatoka kwenye malango yaliyo wazi: “Tazama, niko pamoja nanyi. Msiogope. Nimepigana vita kwa niaba yenu, na kwa jina langu ninyi ni zaidi ya washindi.”

Mwokozi mpendwa atatuma msaada wakati tutakapouhitaji. [380] Wakati wa taabu utakuwa ni wakati wa mateso ya kutisha kwa watu wa Mungu, lakini kila muumini wa kweli ataona kwa imani upinde wa ahadi za Mungu ukimzunguka. "Nao waliokombolewa na Bwana watarejea, Watafika Sayuni, wakiimba; furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; watapata shangwe na furaha; huzuni na kuugua zitakimbia." Isaya 51:11.

Kama damu ya mashahidi Wakristo ingemwagwa wakati huu, uaminifu wao usingekuwa ushuhuda wa kuwashawishi wengine kuhusu ukweli, kwa sababu moyo mkaidi unakuwa umeyakataa mawimbi ya rehema mpaka yamekoma kuja. Ikiwa wenye haki sasa wangeanguka mateka kwa maadui zao, huo ungekuwa ushindi wa mfalme wa giza. Kristo amesema: "Njoni, watu wangu, ingia wewe ndani ya vyumba vyako, ukafunge mlango nyuma yako ujifiche kitambo kidogo, mpaka ghadhabu hii itakapopita. Kwa maana, tazama, Bwana anakuja kutoka mahali pake, ili kuwaadhibu wakaao duniani, kwa sababu ya uovu wao." Isaya 26:20, 21

Kwa wale ambao watakuwa wamesubiri kwa uvumilivu ujio wa Bwana na wale ambao majina yao yameandikwa kwenye kitabu cha uzima, ukombozi wao utakuwa wenye utukufu.

## [381] Sura Ya 40 - Watu Wa Mungu Wakombolewa

Wakati ulinzi wa sheria za wanadamu utakapoondolewa kutoka kwa W wale ambao wanaiheshimu sheria ya Mungu, sambamba na hilo, katika nchi tofauti kutakuwa na harakati za kutaka kuwaangamiza. Kadiri wakati utakaotajwa kwenye sheria utakapokaribia, watu watapanga njama ili kufanya shambulio kubwa katika usiku mmoja litakalo nyamazisha upinzani na shutuma.

Watu wa Mungu baadhi yao wakiwa magerezani, misituni, na katika milima-wataomba ulinzi wa Mungu. Watu wenye silaha wakichochewa na malaika waovu watajiandaa kwa kazi ya mauaji. Sasa mnamo saa ya mwisho wa mateso, Mungu ataingilia kati: "Mtakuwa na wimbo kama vile wakati wa usiku, ishikwapo sikukuu takatifu, mtakuwa na furaha ya moyo kama vile mtu aendapo na filimbi katika mlima wa Bwana, aliye Mwamba wa Israeli. Naye Bwana atawasikizisha watu sauti yake ya utukufu, naye atawaonyesha jinsi mkono wake ushukavyo, na ghadhabu ya hasira yake, na mwako wa moto ulao, pamoja na dhoruba, na tufani, na mvua ya mawe ya barafu." Isaya 30:29,30.

Makundi ya watu waovu yamekaribia kukimbilia mawindo yao, wakati giza nene, kuliko usiku, litakapoijilia nchi. Kisha upinde wa mvua utakuwa angani na utaonekana ukilizunguka kila kundi la wanaoomba. Makutano ya watu waliokasirika watakamatwa. Kusudi la ghadhabu yao limesahaulika. Wanashangaa ishara ya agano la Mungu na wanatamani kujificha mbali na mng'aro wake.

Watu wa Mungu watasikia sauti, ikisema, "tazama juu," Kama Stefano, watatazama juu na kuuona utukufu wa Mungu na Yesu akisimama upande wa mkono wa kuume wa Mungu. (Angalia Matendo 7:55,56.) Watatambua alama za kudhalilishwa kwake, na kulisikia ombi, "Baba, hao ulionipa nataka wawe pamoja nami po pote nilipo, wapate na kuutazama utukufu wangu ulionipa."Yohana 17:24. Sauti itasikika ikisema, "Wamekuja, watakatifu, pasipo maumivu, pasipo kunajisiwa! Wamelishika neno la subira yangu." Usiku wa manane Mungu atadhihirisha uwezo wake kwa ukombozi kwa watu

wake. Jua litatokeza likiwaka kwa nguvu zake. Kisha ishara na maajabu yatafuata. Kwa hofu kuu waovu wataangalia matukio, wakati [382] huo wenye haki wakiangalia alama za ukombozi wao. Katikati ya mbingu zenye ghadhabu, angani kutatokea wingu lenye utukufii usioelezeka ambapo itasikika sauti ya Mungu, kama sauti ya maji mengi, ikisema, "Imekwisha!" Ufunuo 16:17.

Sauti hiyo itazitikisa mbingu na nchi. Kutakuwa na tetemeko kubwa, "ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi hapakuwa namna ile, jinsi lilivyokuwa kubwa tetemeko hilo." Ufunuo 16:18. Mawe yaliyopasuliwa yatasambaa kila mahali. Bahari itachochewa na kughadhibika. Utasikika mvumo wa sauti ya kimbunga kama sauti ya maShetani. Uso wa dunia utapasukapasuka. Misingi yake itaonekana kutengeneza ufa.. Bandari ambazo zimegeuka na kuwa kama Sodoma kwa uovu zitamezwa na maji yenye hasira. "Babeli mkuu" ukakumbukwa mbele za Mungu, "kupewa kikombe cha mvinyo ya ghadhabu ya hasira yake." Ufunuo 16:19. Mvua kuu ya mawe itafanya kazi yake ya uharibifu. Miji yenye kiburi itaangushwa chini. Majumba ya kifahari ambamo watu walitumia kwa anasa utajiri wao yatabomoka mbele ya macho yao. Kuta za gereza zitabomoka vipande vipande na watu wa Mungu watawekwa huru.

Makaburi yatafunguka, na "wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele." "na hao waliomchoma." Wale waliombeza Kristo alipokuwa katika maumivu ya kufa, na wapinzani wakorofi wa ukweli watafufuliwa ili kuiona heshima watakayopewa waaminifu. Danieli 12:2; Ufunuo 1:7.

Radi kali zitaifunika dunia kwa miali ya moto. Zaidi ya ngurumo, sauti, za kushangaza na kutisha zitatangaza maangamizo ya waovu. Wale waliokuwa na majivuno na wasiokuwa watii, waliokuwa wakali kwa watu wa Mungu woanashika amri, sasa watatetemeka kwa hofu. Mapepo yatatetemeka wakati watu watakuwa wakiomba rehema.

### Siku ya Bwana

Nabii Isaya alisema: "Siku hiyo kila mtu atazitupilia mbali sanamu zake za fedha, na sanamu zake za dhahabu, walizojifanyia ili kuziabudu, kwa fuko na popo; ili aingie ndani ya pango za majabali,

na ndani ya tundu za miamba iliyopasuka, mbele za utisho wa Bwana na utukufu wa enzi yake, atakapoondoka ili aitetemeshe mno dunia.” Isaya 2:20,21.

[383] Wale waliotoa vyote kwa ajili ya Kristo sasa watakuwa salama. Mbele za ulimwengu na mbele za kifo watakuwa wamedhihirisha uaminifu wao kwake aliyewafia. Nyuso zao ambazo muda mfupi kabla zilikuwa zimepauka na zisizopendeza, sasa zitang’aa kwa mshangao. Watapaza sauti katika wimbo wa ushindi: “Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari“Maji yake yajapovuma na kuumuka, Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake.” Zaburi 46:1-3.

Wakati maneno haya ya watakatifu yatakapokuwa yanapaa kwa Mungu, utukufu wa jiji la mbinguni utashuka kutoka kwenye malango yaliyo wazi. Kisha hapo utatokeza kutoka angani mkono ambao umebeba mbao mbili za mawe. Ile sheria takatifu, iliyotangazwa kutoka Sinai, sasa itafunuliwa kuwa kanuni ya hukumu. Maneno yatakuwa wazi kabisa kiasi cha watu wote kuweza kuyasoma. Kumbukumbu zitahuishwa. Giza la imani potovu na uasi litaondolewa katika kila moyo.

Haiwezekani kuelezea utisho na kukatishwa tamaa kwa wale walioikanyaga sheria ya Mungu. Ili kuifurahisha Dunia, waliweka sheria za Mungu pembeni na kuwafudisha watu uasi. Sasa watahukumiwa na sheria ileile walioidharau. Watajiona kuwa hawana udhuru. Adui wa sheria ya Mungu watapata ufahamu mpya kuhusu kweli na wajibu. Sasa wakiwa wamechelewa ndipo wataona kwamba Sabato ni muhuri wa Mungu aliye hai. Wakiwa wamechelewa watauona msingi wa mchanga ambao walikuwa wakijenga juu yake. Wamekuwa wakipigana dhidi ya Mungu. Walimu wa dini walikuwa wakiwaongoza watu Jehannamu huku wakidai kuwaongoza kwenda Paradiso. Ni kubwa kiasi gani jukumu la watu wanaofanya kazi katika ofisi takatifu, Ni ya kutisha jinsi gani matokeo yao ya kutokuwa waaminifu .!

## Kutokea kwa Mfalme wa Wafalme

Sauti ya Bwana itasikika ikitangaza siku na saa ya kuja kwa Yesu. Israeli wa Mungu watasimama wakisikiliza, sura zao zikiangaziwa

utukufu wake. Punde litaonekana upande wa mashariki wingu dogo jeusi. Ni wingu litakalomzunguka Mwokozi. Kwa ukimya mkuu [384] watu wa Mungu watalikazia macho kadiri litakavyokaribia, hadi litakapokuwa wingu kubwa jeupe, sehemu yake ya chini kutakuwa na utukufu kama wa moto ulao, na juu yake upinde wa agano. Sasa siyo "Mtu wa huzuni," Yesu atakuwa akija kama mshindi mkuu. Malaika watakatifu kundi kubwa lisilohesabika watakuwa pamoja naye, "kumi elfu mara kumi elfu na maelfu kwa maelfu." Kila jicho litamwona Mfalme wa uhai. Taji ya utukufu itatulia kichwani mwake. Sura yake itang'aa kuliko jua la mchana. "Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NABWANA WA MABWANA." Ufunuo 19:16.

"Mfalme wa wafalme atashuka na wingu, lililozungushiwa moto unaowaka. Dunia itatetemeka mbele yake: "Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza, Moto utakula mbele zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote. Ataziita mbingu zilizo juu, Na nchi pia awahukumu watu wake." Zaburi 50:3,4.

"Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?" Ufunuo 6:15-17.

Vicheko vya dhihaka vitakuwa zimekoma, midomo ya uongo itanyamazishwa. Hakuna kitakachosikika isipokuwa sauti ya maombi na sauti ya kulia. Waovu wanaomba wazikwe chini ya miamba kuliko kukutana na uso wa yule waliyemdhihaki. Sauti hiyo inayopita kwenye sikio la wafu, wanaijua. Ni mara ngapi sauti hii laini uiliwaita ili watubu? Ni mara ngapi kulisikika kusihi kwake rafiki, ndugu, Mwokozi. Sauti hiyo itaamsha kumbukumbu za maonyo yaliyopuuzwa na mialiko iliyokataliwa.

Wapo wale waliomdhihaKikristo wakati wa mateso yake. Alisema: "Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni." Mathayo 26:64. Sasa watamwona katika utukufu wake; na tena watamwona akiwa ameketi katika mkono wa kuume wa mamlaka. Pale atakuwepo Herode mwenye kiburi aliyezomea akiwa na cheo chake [385]

cha ufalme. Watakuwepo hapa watu ambao walimvisha kichwani taji ya miiba na mkononi mwake wakampa fimbo ya kifalme - wale waliosujudu mbele yake kwa dhihaka ya kukufuru, wale waliomtemea mate mfalme wa uzima. Watataka kukimbia mbele zake. Wale walioipigilia misumari kwenye mikono na miguu yake wataziangalia alama kwa hofu na majuto.

Kwa uwazi wa kutisha makuhani na watawala watakumbuka matukio ya Kalvari, jinsi walivyokuwa wakitikisa vichwa katika mizaha ya kishetani, wakapaza sauti na kusema, "Aliokoa wengine; hawezi kujiokoa mwenyewe." Mathayo 27:42. Huku wakipaza sauti kwa nguvu kuliko ile waliyoitoa ikasikika Yerusalemu yote wakisema, "asulibiwe, asulibiwe! Sasa watatoa kilio cha kukata tamaa, "Ni Mwana wa Mungu!" Watatafuta kukimbia kutoka mbele ya Mfalme wa wafalme.

Katika maisha ya wale wote wanaoukataa ukweli kuna wakati ambapo dhamiri huamka, wakati ambapo nafsi inasumbuka kwa majuto ya bure. Lakini haya ni kidogo kuliko majuto ya siku ile? Katikati ya hofu yao kuu watasikia sauti za watakatifu zikisema: "Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie." Isaya 25:9.

Sauti ya Mwana wa Mungu itawaita watakatifu waliolala. Duniani kote wafu wataisikia sauti hiyo, na wale watakaoisikia wataishi, jeshi kubwa kutoka kila taifa, kabila, lugha na jamaa. Watatoka katika nyumba ya gereza la kifo, wakiwa wamevikwa utukufu wa kutokufa., wakilia: "Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?" 1 Wakorintho 15:55.

Wote watatoka makaburini wakiwa na kimo kilekile walichokuwa nacho wakati wanazikwa makaburini. Lakini wote watainuka wakiwa na upya wa uzima na nguvu za ujana wa milele Kristo alikuja kurejesha kile kilichopotea. Ataibadilisha miili yetu yenye dhambi na kuiumba iwe kama mwili wake wa utukufu. Miili yetu ya kufa na kuharibika ambayo hapo awali ilichafuliwa na dhambi, itakuwa haina dosari, mizuri na isiyopatwa na mauti. Dosari na ulemavu vitaachwa kaburini. Waliokombolewa "Watakua" (Malaki 4:2) kufikia kimo kamili cha mwanadamu akiwa katika utukufu wake wa mwanzo, dalili za mwisho za laana ya dhambi zitakuwa zimeondolewa. Waaminifu Wakristo katika akili na roho na mwili wataakisi sura ya Bwana wao.

Wenye haki walio hai watakuwa wamebadilishwa “Kwa dakika moja, kufumba na kufumbua.” Kwa sauti ya Mungu watabadilishwa kuwa na hali ya kutokufa pamoja na watakatifu waliofufuliwa watachukuliwa ili kukutatana na Mwokozi wao angani. Malaika “watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu.” Mathayo 24:31. Watoto wadogo watabebwa na kukabidhiwa kwa mikono ya mama zao. Marafiki ambao kwa muda mrefu walikuwa wametenganishwa na kifo sasa wataungana tena, kamwe hawatatengana, na kwa nyimbo za furaha watapaa pamoja kwenda katika mji wa [386]

**Katika Mji Mtakatifu.**

Kutoka katika jeshi la waliokombolewa, lisilo na idadi; kila jicho litaelekezwa kwa Yesu Kila jicho litauangalia utukufu wake yeye ambaye, “uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu ye yote, na umbo lake zaidi ya wanadamu.” Isaya 52:14. Juu ya vichwa vya washindi Yesu ataweka taji za utukufii. Kwa kila mmoja kutakuwa na taji iliyo na “jina jipya” (Ufunuo 2:17) na maneno, “Mtakatifu kwa Bwana.” Katika kila mkono kutakuwa na mtende wa mshindi na kinubi king’aacho. Kisha malaika kiongozi anapopiga noti, kila mkono unavuta uzi kwa mguso wenye ujuzi katika fahari na sauti tamu yenye mvuto. Kila sauti inainuliwa kwa sifa za shukrani: “Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina.” Ufunuo 1:5,6.

Mbele ya mkutano mkubwa uliokombolewa kwa kafara kutakuwa na Mji Mtakatifu. Yesu atafungua malango, na mataifa ambao waliishika kweli wataingia ndani. Kisha sauti yake itasikika, “Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu.” Mathayo 25:34. Kristo atawasilisha kwa Baba yake wale aliowanunua kwa damu yake, Akisema: “mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu.” “mimi naliwalinda kwa jina Iako ulilonipa” Waebrania 2:13;Yohana 17:12. Aha! Itakuwa ni saa ya ajabu ya kunyakuliwa wakati Baba wa milele, atakapowaangalia waliokombolewa kwa kafara ya Yesu, akiiona sura yake, madhara ya dhambi yakiwa yameondolewa, na kwa

mara nyingine tena mwanadamu akiwa katika hali ya kupatanana Mungu.

[387] Furaha ya Mwokozi ni kuziona katika ufalme wa utukufu, roho ambazo zitakuwa zimekombolewa kutokana na matokeo ya uchungu na kudhalilishwa kwake. Waliokombolewa watashiriki furaha yake; watawaona wale waliokombolewa kwa maombi, kazi na kafara yao ya upendo. Mioyo yao itajazwa na furaha watakapoona mmoja amempata mwingine, na wale wengine kupata wengine zaidi.

## Kukutana kwa Adamu Wawili

Waliokombolewa watakapokuwa wakikaribishwa katika mji wa Mungu, hapo itasikika kelele ya ushindi. Adamu wawili karibia wanakutana. Mwana wa Mungu atampokea baba wa jamii yetu-ambaye alimuumba, aliyetenda dhambi, na kwa sababu ya dhambi yake alama za kusulubishwa ziko kwenye mwili wa Mwokozi. Adamu atakapokuwa akiziangalia alama za misumari, kwa unyenyekevu ataanguka miguuni pa Mwokozi. Mwokozi atamwinua na kumkaribisha aiangalie bustani ya Edeni ambayo aliondolewa kutoka kwayo muda mrefu.

Maisha ya Adamu yalikuwa yamejaa huzuni. Kila jani lililoanguka, kila mnyama wa kafara, kila doa katika maisha safi ya mwanadamu ulikuwa ni ukumbusho wa dhambi yake. Alikuwa na uchungu na majuto ya kutisha alipokutana na shutuma alizotupiwa yeye kama aliyesababisha dhambi. Kwa uaminifu alitubu dhambi yake, na alikufa katika tumaini la ufufuo. Sasa kupitia katika upatanisho, Adamu atakuwa amerejeshwa.

Atasafirishwa kwa furaha, ataiona miti ambayo hapo awali ilikuwa furaha yake, ambayo matunda yake yeye mwenyewe aliyachuma katika siku zile ambazo alikuwa hana hatia. Ataiona miti ambayo aliihudumia kwa mikono yake, maua yale yale aliyokuwa akipenda kuyatunza. Kwa hakika hii ni Edeni iliyorejeshwa!

Mwokozi atampeleka kwenye mti wa uzima na kumsihi ale. Atayaona makutano ya familia yake wakiwa wamekombolewa. Kisha atatupa taji yake miguuni pa Yesu na kumkumbatia Mwokozi. Atashika kinubi na anga la mbinguni litakuwa na mwangi wa wimbo wa ushindi: “Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa.” Ufunuo 5:12. Familia ya Adamu watatupa taji zao miguuni pa Yesu watakaposu-

judu kumtukuza. Malaika walilia Adamu alipoanguka na walifurahi Yesu alipolifungua kaburi kwa wote watakaoliamini Jina lake. Sasa wataiangalia kazi ya ukombozi ikiwa imekamilishwa na kuunganisha sauti zao katika kusifu.

Kwenye "bahari ya kioo iliyochangamana na moto," watakusanyika wale "wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake." Mia moja arobaini na nne elfu waliokombolewa kati ya watu na wanaimba "wimbo mpya" wimbo wa Musa na Mwana- Kondoo. Ufunuo 15:2,3. Si wengine isipokuwa wale mia moja arobaini na nne elfu ndio watakaoweza kujifunza wimbo ule, kwa sababu ni wimbo wa uzoefu ambao hamna kundi lingine wamewahi kuupitia. "Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako." Hawa baada ya kubadilishwa kutoka miongoni mwa walio hai, ni "malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo." Ufunuo 14:4,5. Walipitia katika kipindi cha mateso ambacho kamwe hakijawahi kuwapo tangu taifa lilipoanza kuwepo, walivumilia uchungu wa wakati wa taabu ya Yakobo, walisimama bila kuwa na mpatanishi katika kipindi cha mwisho cha hukumu ya Mungu. "nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo." "Na katika vinywa vyao haukuonekana uongo. Maana hawana mawaa" mbele za Mungu. "Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao." Ufunuo 7:14; 14:5; 7:16,17. [388]

### Waliokombolewa Wakiwa Kwenye Utukufu

Katika zama zote wateule wa Bwana wamekuwa wakitembea katika njia nyembamba. Walitakaswa katika tanuru la mateso. Kwa ajili ya Yesu walivumilia kuchukiwa, kusingiziwa, kujikana nafsi, na kukatishwa tamaa. Walijifunza ubaya wa dhambi, nguvu yake, hatia yake, huzuni yake, wanaiangalia kwa chuki. Kutambua jinsi kafara ya milele ilivyotolewa ili kuondoa tatizo la dhambi kunawafanya wajishushe na kunaijaza mioyo yao shukrani. Wanapenda zaidi kwa sababu wamesamehewa dhambi nyingi zaidi. Angalia Luka 7:47.

Washirika wa mateso ya Kristo, wanastahili kuwa washirika wa utukufii.

[389] Warithi wa Mungu watatokea katika upenu, vibanda vibovu, magereza ya chini ya ardhi, majukwaa ya kunyongea wahalifu, milimani, katika majangwa, mapango. "Walikuwa maskini, walinyanyaswa, waliteswa." Mamilioni walikwenda kaburini kwa kusingiziwa mabaya kwa sababu walikataa kukubaliana na Shetani. Lakini sasa hawateswi tena, kutawanywa na kukandamizwa. Kutoka sasa watasimama wakiwa wamevikwa mavazi mazuri kupita mavazi ambayo matajiri walioheshimika duniani waliwahi kuvaa, wakiwa wamevikwa taji zenye utukufu kupita zile taji walizovishwa viongozi wa mataifa ya dunia. Mfalme wa utukufu atakuwa amefuta machozi kwenye nyuso zote. Wataimba wimbo wa sifa ulio mtamu na wenye mpangilio mzuri. Wimbo utaongezeka na kujaza makao ya mbinguni. "Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo." Kisha wote wataitikia, "Amina; Baraka na utukufu na hekima na shukrani na heshima na uweza na nguvu zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina." Ufunuo 7:10,12.

Katika maisha haya tunaweza tu kuanza kuelewa mada kuu ya wokovu. Kwa uelewa wetu ulio na ukomo tunaweza kutafakari kwa umakini kuhusu aibu na utukufu, maisha na kifo, haki na rehema vilivyokutana msalabani; na bado hata kwa kutumia nguvu zetu zote za kiakili tunashindwa kuelewa umuhimu wake kikamilifu. Urefu na upana, kina na kimo cha upendo wa ukombozi vinaeleweka kidogo sana. Mpango wa ukombozi hautaeleweka kwa ukamilifu, hadi pale wale waliokombolewa watakapoona mambo jinsi yalivyo, na kuyajua mambo jinsi yanavyojulikana; lakini katika zama za milele ukweli mpya utaendelea kufunuliwa kwenye mioyo ya wale watakaokuwa wakishangaa kufurahi. Japo maumivu na uchungu na majaribu ya dunia yatakuwa yamekwisha na chimbuko lake kuondolewa, watu wa Mungu daima watakuwa na maarifa ya ufahamu wa pekee kukumbuka kile ukombozi wao ulichogharimu.

Msalaba utakuwa wimbo wa waliokombolewa milele zote. Katika Kristo aliyetukuzwa watamwona Kristo aliYesulubishwa. Kamwe haitasahaulika kuwa Mwenye enzi wa mbinguni alijishusha ili amwinue mwanadamu aliyeanguka, kwamba alibeba hatia na aibu ya dhambi na kufichwa kwa uso wa Baba yake hadi taabu za dunia iliyokuwa imepotea zilipouvunja moyo

wake na kuyaangamiza maisha yake. Muumbaji wa ulimwengu wote aliuweka pembeni utukufu wake kwa sababu alimpenda mwanadamu-jambo hili daima litachochea mshangao wa ulimwengu wote. Mataifa ya waliokombolewa watakapomtazama Mwokozi na kutambua kwamba ufalme wake hauna mwisho, wataanza kuimba [390]
“Anastahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa na ametukomboa kutuleta kwa Mungu kwa damu yake ya thamani!”

Mwujiza wa msalaba utaielezea miujiza yote. Itadhihirika kwamba yeye aliye na hekima isiyo na ukomo hangepanga mpango mwingine wa kutukomboa isipokuwa kafara ya Mwana wake. Fidia kwa ajili ya kafara itakuwa ni furaha ya kuijaza dunia na viumbe waliokombolewa, watakatifu, wenye furaha, na wasioweza kupatwa na mauti. Hiyo ndiyo thamani ya nafsi ambayo Baba anaridhishwa iliyolipwa. Na Kristo mwenyewe, atakapoyatazama matunda ya kafara yake kuu, ataridhika.

## [391] Sura Ya 41 - Dunia Ikiwa Magofu

Wakati sauti ya Mungu itakapowarudisha watu wake waliotekwa, kutakuwa na utambuzi wa kuogofya kwa wale waliopoteza yote katika pambano kuu la maisha. Wakiwa wamepotoshwa na udanganyifu wa Shetani, matajiri walijisifia wenyewe juu ya ubora waliokuwa nao dhidi ya wasiokuwa na kitu. Walipuuzia kuwapa chakula wenye njaa, kuwavisha waliokuwa uchi, kutenda haki, na kupenda rehema. Sasa watakuwa wamenyang'anywa vyote vilivyowafanya kuwa wakuu na kuachwa katika umaskini. Kwa hofu watashuhudia kuangamizwa kwa sanamu zao. Waliuza roho zao kwa anasa za dunia na hawakujitajirisha kwa Mungu. Maisha yao yameshindwa, anasa zao zimegeuka kuwa uchungu. Mafanikio ya maisha yote yamefagiliwa mbali kwa muda mfupi. Matajiri wataombelezea uharibifu wa majumba yao, na kutawanywa kwa dhahabu na fedha zao, na hofu kwamba wao pia wataangamia pamoja na sanamu zao. Waovu wataomboleza kwamba hayo ndiyo matokeo, lakini hawatatubu kwa ajili ya uovu wao.

Mchungaji aliyeutoa kafara ukweli ili apate kupendwa na watu sasa atautambua ushawishi wa mafundisho yake. Kila mstari ulioandikwa, kila neno lilitamkwa lililowafanya watu kubaki kwenye udanganyifu lilikuwa likitawanya mbegu; na sasa atayaona mavuno. Asema Bwana: "Ole wao wachungaji, wanaoharibu kondoo za malisho yangu na kuwatawanya!...Tazama, nitawapatiliza uovu wa matendo yenu." "Kwa kuwa ninyi mmemhuzunisha moyo mwenye haki kwa uongo, ambaye mimi sikumhuzunisha; na kuitia nguvu mikono ya mtu mbaya, hata asigeuke, na kuiacha njia yake mbaya, na kuhifadhika." Yeremia 23:1,2; Ezekieli 13:22.

Wachungaji na watu wataona kuwa wameasi dhidi ya Mwanzilishi wa sheria zote za haki. Kuweka kando sheria za Mungu kulitoa fursa ya kuibuka kwa vyanzo vingi vya uovu, hadi dunia ikawa shimo moja kubwa la uovu. Hakuna lugha itakayoweza kueleza shauku watakayoihisi wasiowaaminifu kwa ajili ya kile walichokipoteza milele-Uzima wa milele.

Watu watalaumiana wao kwa wao kwa kuongozwa katika uharibifu, lakini wote wataungana katika kurundika shutuma zao chungu kwa wachungaji wasiokuwa waaminifu waliotabiri "maneno laini," (Isaya 30:10), waliwaongoza wasikilizaji wao kuifanya tupu sheria ya Mungu na kuwatesa wale walioishika. "Tumepotea" watalia, "na ninyi ndio sababu" Mikono ambayo wakati fulani iliwavika taji heshima itainuka ili kuwaangamiza.. Kila mahali kutakuwa fujo na umwagaji wa damu. [392]

Mwana wa Mungu na wajumbe wa mbinguni wamekuwa katika mapambano dhidi ya yule mwovu ili kuwaonya, kuwaangazia, na kuwaokoa watoto wa wanadamu. Sasa wote wamefanya uamuzi; waovu wameungana kikamilifu na Shetani katika vita yake dhidi ya Mungu. Pambano halipo kwa Shetani peke yake bali pia kwa wanadamu "Maana Bwana ana mashindano na mataifa." Yeremia 25:31.

## Malaika wa Mauti.

Sasa malaika wa mauti atatokea, aliyewakilishwa kwenye njozi ya Ezekieli kama watu wenye silaha za kuua, ambao kwao amri amri itatolewa: "Waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana, na watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu ye yote mwenye hiyo alama; tena anzeni katika patakatifu pangu." "Basi, wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba." Ezekieli 9:6.

Walinzi wasio wakweli ndiyo watakaoanza kuangungamia. "Bwana anakuja kutoka mahali pake, ili kuwaadhibu wakaao duniani: ardhi nayo itafunua damu yake, wala haitawafunika tena watu wake waliouawa." "Mashaka makubwa yatokayo kwa Bwana yatakuwa kati yao; na kila mmoja wao atakamata mkono wa jirani yake, na mkono wake utainuliwa ili kushindana na mkono wa jirani yake." Isaya 26:21; Zekaria 14:13.

Katika hali ya mabishano makali ya hisia zao na kwa kumwagwa kwa ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa makuhani, watawala na watu waovu watangamia "Na waliouawa na Bwana siku ile watakuwapo, toka upande mmoja wa dunia hata upande wa pili." Yeremia 25:33.

Wakati wa kuja kwa Kristo waovu wataangamizwa kwa mng'ao wa utukufu wake. Kristo atawapeleka watu wake kwenye mji

wa Mungu, na dunia itakuwa tupu bila wakazi wake. “Tazama, [393] Bwana ameifanya dunia kuwa tupu, aifanya ukiwa, aipindua, na kuwatawanya wakaao ndani yake....Dunia hii itafanywa tupu kabisa, na kuharibiwa kabisa; maana Bwana amenena neno hilo...kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele.Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia: ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketea.” Isaya 24:1,3,5,6.

Dunia itaonekana kama jangwa lililo ukiwa. Miji itaharibiwa kwa tetemeko la ardhi, miti itang’olewa, miamba iliyopasuka kutoka kwenye dunia itasambaa juu ya uso wake. Mabonde makubwa yatakuwa alama za mahali ilipokuwa milima iliyong’oka kutoka kwenye misingi yao.

## Kifungo Cha Shetani

Tukio linalotokea sasa lilitabiriwa katika huduma yenye taadhima ya Siku ya Upatanisho. Wakati dhambi za Israeli zilipokuwa zimekwisha kuondolewa kutoka katika hema kwa njia ya damu ya kafara ya dhambi, mbuzi wa Azazeli aliletwa akiwa hai mbele za Bwana. Kuhani mkuu aliungama juu yake “uovu wote wa wana wa Israeli, . . . akiziweka “juu ya kichwa chake yule mbuzi” Mambo ya Walawi 16:21. Kwa namna hiyo hiyo wakati kazi ya upatanisho katika hekalu la mbinguni itakapokamilika, ndipo, katika mbele za Mungu na malaika wa mbinguni na jeshi la waliokombolewa, dhambi za watu wa Mungu zitawekwa juu ya Shetani; atahukumiwa kuwa na hatia ya uovu wote aliosababisha wakautenda. Kama vile mbuzi wa Azazeli alivyopelekwa katika nchi isiyokaliwa na watu, ndivyo Shetani atakavyondolewa hadi kwenye dunia iliyo ukiwa.

Baada ya kuelezea matukio ya kuja kwa Bwana, mwandishi wa Ufunuo anaendelea: “Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu, na mnyororo mkubwa mkononi mwake. Akamshika yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu; akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache.” Ufunuo 20:1-3.

"Kuzimu" kunawakilisha dunia ikiwa katika hali ya giza na kuchanganyikiwa. Akiitazamia siku ile kuu ya Bwana Yeremia anasema: "Naliiangalia nchi, na tazama, ilikuwa ukiwa, haina watu; [394]
naliziangalia mbingu, nazo zilikuwa hazina nuru. Naliiangalia milima, na tazama, ilitetemeka, na milima yote ilisogea huko na huko. Nikaangalia, na tazama, hapakuwa na mtu hata mmoja, na ndege wote wa angani wamekwenda zao. Nikaangalia, na tazama, shamba lililozaa sana limekuwa ukiwa, na miji yake yote ilikuwa imebomoka." Yeremia 4:23- 26.

Hapo patakuwa makao ya Shetani na malaika zake waovu kwa miaka 1,000. Akiwa amezuiliwa duniani, hataweza kuufikia ulimwengu mwingine kuwajaribu na kuwasumbua wale ambao hawajaanguka. Kwa maana hiyo "amefungwa." Hakuna atakayesalia ambaye kwake Shetani ataonesha uwezo wake. Atakuwa ameondolewa kutoka katika kazi ya udanganyifu na maangamizi ambayo ilikuwa furaha yake pekee.

Isaya, akiutazama wakati wa Shetani kutupwa chini, alisema kwa mshangao: "Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifaLNawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu. Lakini utashushwa mpaka kuzimu; Mpaka pande za mwisho za shimo. Wao wakuonao watakukazia macho, Watakuangalia sana, wakisema, Je! Huyu ndiye aliyeitetemesha dunia, Huyu ndiye aliyetikisa falme; Aliyeufanya ulimwengu ukiwa, akaipindua miji yake; *Asiyewafungua wafungwa wake waende kwao?*' Isaya 14:12-17.

Kwa miaka 6000 gereza la Shetani liliwapokea watu wa Mungu, lakini Kristo atavivunja vifungo vyake na kuwaweka wafungwa huru. Yeye peke yake na akiwa na malaika zake waovu atapata madhara ya dhambi: "Wafalme wote wa mataifa wamezikwa wote kwa heshima, Kila mmoja ndani ya nyumba yake mwenyewe (kaburi). Bali wewe umetupwa mbali na kaburi lako, Kama chipukizi lililochukiza kabisa; Hutaungamanishwa pamoja nao katika mazishi, Kwa maana umeiharibu nchi yako, umewaua watu wako."Isaya 14:18-20.

Kwa miaka 1,000, Shetani atayaona matokeo ya uasi wake dhidi ya sheria ya Mungu. Mateso yake yatakuwa makali. Sasa atakuwa ameachwa ili atafakari juu ya kazi aliyoifanya tangu alipoasi na kuisubiri hatima yake ya kutisha wakati atakapolazimika kuadhibiwa.

[395] Wakati wa miaka 1,000 kati ya ufufuo wa kwanza na wa pili, hukumu ya waovu itafanyika. Paulo analionesha hili kuwa ni tukio litakalofuatia ujio wa pili. lWakorintho 4:5. Wenye haki watatawala kama wafalme na makuhani. Yohana anasema: "Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; . . . Watakuwa makuhani wa Mungu na Wakristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu." Ufunuo 20:4-6.

Wakati huo "watakatifu watauhukumu ulimwengu" lWakorintho 6:2. Kwa kuungana na Kristo watawahukumu waovu, wakiliamua kila shauri sawasawa na matendo yaliyofanyika katika mwili. Kisha kiwango ambacho waovu wanapaswa kuteseka kitapimwa, sawasawa na matendo yao na kuandikwa mbele ya majina yao katika kitabu cha mauti.

Shetani na malaika waovu watahukumiwa na Kristo na watu wake. Paulo anasema: "Au hamjui ya kwamba watakatifu watauhukumu ulimwengu?" lWakorintho 6:3. Yuda anasema: "Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu." Yuda 6.

Mwisho wa miaka 1,000 ufufuo wa pili utafanyika. Kisha waovu watafufuliwa kutoka katika wafu na kuja mbele za Mungu ili kufanyiwa "hukumu iliyoandikwa." Zaburi 149:9. Kwa hiyo mwandishi wa ufunuo anasema: "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu." Ufunuo 20:5. Na Isaya, kuhusu waovu anasema: "nao watakusanywa pamoja kama vile wakusanywavyo wafungwa katika shimo nao watafungwa katika gereza; na *baada ya muda wa siku nyingi watajiliwa*." Isaya 24:22.

# Sura Ya 42 - Amani Ya Milele: Pambano Lafika Mwisho [396]

Mwisho wa miaka 1,000 Kristo atarudi duniani akisindikizwa na waliokombolewa na jeshi la malaika. Atawaamuru waovu walikufa kufufuka ili wapokee hukumu yao. Watafufuka, watakuwa hawahesabiki kama mchanga wa bahari, wakiwa na dalili za ugonjwa na mauti. Tofauti iliyoje baina ya wale waliofufuliwa kwenye ufufuo wa kwanza!

Kila jicho litakuwa limegeuka kuutazama utukufu wa Mwana wa Mungu. Kwa sauti moja jeshi la waovu litasema: "Amebarikiwa yeye ajaye kwa jina la Bwana" Mathayo 23:39. Si upendo utakaosababisha tamko hili. Nguvu ya ukweli italazimisha maneno kutoka kwenye midomo isiyoradhi kutamka. Kama ilivyokuwa wakati walipolala katika makaburi yao, waovu watafufuka wakiwa na uadui ule ule kwa Kristo, wakiwa na roho ile ile ya uasi. Hawatapata kipindi kingine cha rehema ili kurekebisha maisha yao yaliyopita.

Nabii anasema: "Miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, . . . nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake."Zekaria 14:4. Yerusalemu Mpya utakaposhuka kutoka mbinguni, utakaa juu ya mahali palipotayarisha, na Kristo na watu wake na malaika wataingia kwenye mji mtakatifu.

Akiwa amekatiliwa mbali na kazi zake za udanganyifu, mkuu wa uovu atakuwa na huzuni na kuvunjika matumaini, lakini waovu waliokufa watakapofufuliwa na atakapouona mkutano mkubwa ukiwa upande wake, matumaini yake yatakuwa hai. Hakusudii kushindwa katika pambano kuu. Atawapanga waliopotea chini ya bendera yake. Kwa kumkataa Kristo waliukubali utawala wa mwasi, walikuwa tayari kutimiza amri zake. Akiwa bado na hila zake za awali, atakataa kukiri kuwa yeye ni Shetani. Atadai kuwa yeye ndiye mmiliki halali wa dunia ambaye urithi wake ulinyanganywa pasipo uhalali. Atajionesha mwenyewe kuwa ni mkombozi, akiwahakikishia wale aliowadanganya kuwa ni uwezo wake uliowafufua kutoka makaburini mwao. Shetani atawafanya walio dhaifu kuwa na nguvu,

na atawavuvia wote kwa uwezo wake kuwaongoza kuutwaa mji wa Mungu. Anawaonesha mamilioni wasiohesabika waliofufuliwa kutoka katika wafu, na atatamka kuwa yeye kama kiongozi wao anaweza kutawala katika enzi na ufalme wake.

[397] Kwenye mkutano huu mkubwa kutakuwa na jamii ya watu walioishi muda mrefu waliokuwepo kabla ya gharika, watu wa kimo kirefu na uwezo mkubwa wa akili; watu ambao matendo yao ya ajabu yaliifanya dunia kuabudu akili zao, lakini ni watu ambao ukatili na mavumbuzi yao maovu yalisababisha Mungu awafute kwenye uumbaji wake. Watakuwepo wafalme na majenerali ambao hawakuwahi kushindwa katika pambano hata moja. Walipokuwa wamekufa hawakupitia mabadiliko yoyote. Watakapotoka makaburini watahamasishwa na nia ileile ya kushinda iliyowatawala wakati walipoanguka.

## Shambulizi la Mwisho Dhidi ya Mungu

Shetani atashauriana na watu hawa wenye nguvu. Watasema kwamba jeshi lililo ndani ya mji ni dogo likilinganishwa na la kwao na kwamba wataweza kulishinda. Mafundi wenye ujuzi watatengeneza zana za vita. Viongozi wa kijeshi watawapanga watu wapenda vita katika makundi na vikosi.

Hatimaye amri ya kusonga mbele itatolewa, na jeshi lisilohesabika litasonga mbele, jeshi hili litakuwa kubwa kiasi kwamba muungano wa majeshi ya zama zote hautalingana nalo. Shetani, ataongoza kikosi cha mstari wa mbele, Wafalme na mashujaa wake watakuwa kwenye msururu wake. Kwa umakini wa kijeshi wanajeshi wakiwa wamejipanga kwenye mistari kulingana na vyeo vyao, watasonga mbele juu ya uso wa nchi uliobomolewa, wakiuelekea mji wa Mungu.. Kwa amri ya Yesu, malango ya Yerusalemu Mpya yatafungwa, na majeshi ya Shetani yatajipanga tayari kwa mapambano.

Sasa Kristo ataonekana mbele za adui zake. Mbali juu ya mji, juu ya msingi wa dhahabu itakayokuwa iking'aa kutakuwa na kiti cha enzi. Juu ya kiti hiki cha enzi atakaa Mwana wa Mungu, na kumzunguka kutakuwa na watu wa ufalme wake. Utukufu wa Baba wa milele utamfunika Mwana wake. Mng'ao wa uwepo wake utavuka malango, na kuifunika dunia kwa nuru yake.

Karibu na kiti cha cnzi watakuwapo wale ambao hapo zamani walikuwa na bidii katika kazi za Shetani, lakini wakatolewa kama vinga vya moto, wakamfuata Mwokozi wao kwa kujitoa kikamilifu. Baada yao ni wale waliokuwa wakamilifu katika tabia zao katikati ya uwongo na ukafiri, walioiheshimu sheria ya Mungu ulimwengu ulipotangaza kuwa rasmi kuwa haikuwa halali, na mamilioni, wa zama zote waliouawa kwa sababu ya imani yao. Baada ya hao ni "mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, . . . wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao." Ufunuo 7:9. Vita vyao vitakuwa vimekoma, ushindi wao watakuwa wameupata. Tawi la mtende ni ishara ya ushindi, mavazi meupe yanawakilisha haki ya Kristo ambayo sasa ni yao [398]

Katika mkutano huo mkubwa hakuna hata mmoja atakayedai kuwa amejipatia wokovu kwa wema wake mwenyewe. Hakuna kitakachosemwa kuhusu mateso waliyoyapitia; ujumbe wa kila wimbo mkuu ni, Wokovu ni kwa Mungu wetu na kwa Mwana- Kondoo wake.

## Hukumu Yatolewa Dhidi Ya Waasi

Kutawazwa kwa Kristo kutafanyika mbele ya mkutano wa wakazi wa duniani na wa mbinguni. Na sasa akiwa amevikwa enzi na nguvu, Mfalme wa wafalme atatoa hukumu kwa waasi ambao waliasi sheria na kuwatesa watu wake. "Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao." Ufunuo 20:11,12.

Macho ya Yesu yatakapowaangalia waovu, wataitambua kila dhambi ambayo waliwahi kuitenda. Wataona ni wapi miguu yao ilitanga pembeni mbali na njia ya utakatifu. Majaribu yenye kushawishi ambayo waliyawezesha kwa kuendekeza dhambi, wajumbe wa Mungu waliopuuzwa, maonyo yaliyokataliwa, mawimbi ya rehema

yaliyorudishwa nyuma kwa ukaidi, moyo usiotubu-yote yataonekana kana kwamba yaliandikwa kwa herufi za moto.

[399] Juu ya kiti cha enzi, msalaba utafunuliwa. Kama kulivyo kuonekana kwa sinema, yataonekana mazingira ya anguko la Adamu na hatua zilizofuata za mpango wa ukombozi. Kuzaliwa kwa unyenyekevu kwa Mwokozi; maisha yake ya kawaida; ubatizo wake Yordani; kufunga na kujaribiwa jangwani; huduma yake akiwafunulia watu baraka za mbinguni; siku zilizojazwa na matendo mengi ya rehema, siku ambazo alitumia usiku mzima akiomba milimani, mitego ya husuda na roho ya chuki ambayo iligeuka kuwa faida kwake; uchungu usioelezeka katika bustani ya Gethsemane akibeba uzito wa dhambi za ulimwengu; usaliti uliomtia mikononi mwa kundi la wauaji; matukio katika usiku ule wa kutisha - mfungwa asiye na upinzani aliyeachwa na wanafunzi wake, akiwa mtuhumiwa mbele ya behewa la kuhani mkuu, ndani ya ukumbi wa hukumu wa Pilato, mbele ya Herode mwoga, kufanyiwa mzaha, kutukanwa, kuteswa na kuhukumiwa kifo -yote yataoneshwa wazi.

Na sasa mbele ya makutano wanaosukwasukwa yatafunuliwa matukio ya mwisho: mteswaji mwenye subira akipita njia ya kwenda Kalvari; Mfalme wa mbinguni akining'inia msalabani; makuhani na walimu wa sheria wakidhihaki mateso yake; giza lisilokuwa la kawaida ambalo lililionesha alama ya wakati ambapo mkombozi wa ulimwengu alitoa uhai wake.

Mambo ya kutisha yataonekana jinsi yalivyo. Shetani na wafuasi wake hawatakuwa nguvu ya kuacha kuiangalia picha nzima. Kila mhusika ataikumbuka sehemu yake aliyohusika. Herode aliyewachinja watoto wasiokuwa na hatia wa Bethlehemu; Herodia mwovu, ambaye damu ya Yohana Mbatizaji inadaiwa katika nafsi yake; Pilato, mtu dhaifu, aliyetumika kujaza wakati tu; askari wenye kudhihaki; halaiki ya watu iliyokuwa na hasira iliyopiga kelele, "damu yake iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu!" -wote watatafuta kujificha mbali na uso wa mwenye enzi wa mbinguni bila mafanikio, wakati waliokombolewa wakitupa taji zao miguuni pa Mwokozi, wakisema, "alikufa kwa ajili yangu!"

Atakuwapo Nero, jitu la kutisha kwa ukatili na tabia mbaya, akitazama kutukuzwa kwa wale ambao aliwahi kuwatesa, na ambao katika kuteseka kwao yeye alipata furaha yake ya kishetani. Mama yake ataishuhudia kazi yake, jinsi tamaa iliyohamasishwa na mvuto

namfano wake ilivyozaa matunda ya uhalifu ulioufanya ulimwengu utetemeke.

Watakuwape makasisi wa Kikatoliki na wasaidizi wao waliodai kuwa ni mabalozi Wakristo, lakini bado walitumia magereza ya chini ya ardhi, vitanda vya kutesea na kuchoma watu kwenye nguzo za moto ili kuwatawala watu wake. Watakuwapo pia wale maaskofu wenye kiburi waliojitukuza juu ya Mungu na wakajichukulia madaraka ya kuibadili sheria ya Mungu aliye juu. Makasisi hawa waliojidai watakuwa na kesi ya kujibu mbele za Mungu. Wakiwa wamechelewa sana ndipo wataona kuwa Yeye mwenye kujua yote anao wivu kwa sheria yake. Sasa ndipo watajifunza kwamba Kristo anatambua mambo mazuri yaliyo kwa watu wake wanaoteseka. [400]

Ulimwengu wote wa waovu utasimama ukishitakiwa kwa makosa ya uhaini wa hali ya juu dhidi ya serikali ya mbinguni. Hawatakuwa na yeyote wa kumsihi awasaidie; hawatakuwa na udhuru; na hukumu ya kifo cha milele itatolewa dhidi yao.

Waovu wataona kile walichopoteza kwa sababu ya uasi wao. “yote haya” roho zilizopotea zitalia, ” ningekuwa nayo. Ah nimepumbazwa ajabu! Nimebadilisha amani, furaha, na heshima kwa kuchukua huzuni, aibu na kukata tamaa.” Wote wataona kuwa kutengwa kwao na mbingu ni haki. Kwa maisha yao walitamka, “Mtu huyu Yesu hatatutawala.”

## Shetani Ameshindwa

Kama walio ndotoni, waovu watatazama kutawazwa kwa Mwana wa Mungu. Wataona mikononi mwake mbao za sheria ya mbinguni waliyoipuuza. Watashuhudia sauti kubwa ya kutukuza kutoka kwa waliookolewa, na wimbi la sauti linapopaa juu ya makutano hadi kufika nje ya jiji, wote watasema, “Ni makuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi.” Ufunuo 15:3. Wataanguka kifudifudi, wakimwabudu Mfalme wa uzima.

Shetani ataonekana kupooza. Yeye aliyekuwa kerubi afunikaye, sasa atakumbuka pale alipoanguka. Kutoka kwenye halmashauri ambapo alikuwa anaheshimiwa sasa ameondolewa milele. Atamwona mwingine sasa akisimama karibu na Baba, malaika mwenye enzi. Atajua kwamba nafasi hii ya kutukuka ya malaika huyu ingekuwa yake..

[401] Kumbukumbu zitamjia za hapa ambapo palikuwa nyumbani akiwa hana hatia, , amani na ridhaa alivyokuwa navyo mpaka wakati wa uasi wake. Atakumbuka kazi aliyoifanya kati ya wanadamu na matokeo yake, audui wa mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake, uharibifu mbaya wa maisha, mapinduzi ya watawala, machafiiko, migogoro, na mapinduzi. Atakumbuka jitihada zake ambazo hazikukoma katika kuipinga kazi ya Kristo. Atapoangalia matunda ya kazi yake ataona kushindwa tu. Tena na tena katika pambano kuu amekuwa akishindwa na kulazimika kukubali..

Kusudi la mwasi mkuu daima limekuwa ni kuthibitisha kwamba serikali ya mbinguni inawajibika kwa uasi. Amewaongoza makutano wengi kukubali maelezo yake. Kwa miaka mingi kiongozi huyu wa udanganyifu amebadilisha ukweli kwa kuweka uongo. Lakini sasa muda utakuwa umefika ambapo historia na tabia ya Shetani itafichuliwa. Katika jitihada zake za mwisho za kumpindua Kristo, kuwaangamiza watu wake na kuutwaa mji wa Mungu, mdanganyifu mkuu amefunuliwa kikamilifu. Wale walioungana naye wataona kushindwa kabisa kwa makusudi yake.

Shetani ataona kuwa kuasi kwake kwa hiari kumemfanya asifae kuwa mbinguni. Amezizoeza nguvu zake kufanya vita dhidi ya Mungu. Sasa usafi na upatanifu uliopo mbinguni kwake ungekuwa ni mateso. Atasujudu na kukiri haki ya hukumu yake.

Kila swali la ukweli na makosa katika pambano la muda mrefu sasa litakuwa limewekwa wazi. Matokeo ya kuweka pembeni utaratibu wa mbinguni yatakuwa yamewekwa wazi na kuonekana kwa ulimwengu wote. Historia ya dhambi itakuwepo milele zote kama ushahidi kwamba uwepo wa sheria ya Mungu umefungamana na furaha ya viumbe wote aliowaumba. Ulimwengu wote, wale walio waaminifu na waasi kwa sauti moja watasema, "Ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa watakatifu"

Saa itakuwa imefika ambapo Kristo atatukuzwa juu ya kila jina linalojulikana. Kwa sababu furaha iliyokuwa mbele yake-ili kwamba awalete wana wengi kwenye utukufu-aliuvumilia msalaba, atawaangalia waliokombolewa, wakiwa wamefanywa upya katika sura yake. Ataona ndani yao matokeo ya maumivu yake, na ataridhika. Isaya 53:11. Kwa sauti itakayowafikia makutano wenye haki na waovu atasema: "Tazama gharama ya damu yangu, kwa ajili ya hawa niliteseka, kwa ajili ya hawa nilikufa."

### Mwisho Mbaya wa Waovu [402]

Tabia ya Shetani haitbadilika. Kwa mara nyingine, Uasi kama mkondo wa maji wenye nguvu unaibuka. Ataazimu kutoacha jitihada zake za mwisho dhidi ya Mfalme wa mbinguni. Lakini sasa, katika mamilioni wasiohesabika aliowashawishi kuasi, hakuna atakayetambua ukuu wake. Waovu watakuwa wamejazwa na chuki ile ile ya Mungu inayomchochea Shetani, lakini wataona kwamba hali yao haina namatumaini. "Kwa kuwa umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu. basi, tazama, nitaleta wageni juu yako, watu wa mataifa wenye kutisha; nao watafuta panga zao juu ya uzuri wa hekima yako, nao watautia uchafu mwangaza wako. Watakushusha hata shimoni. . . . nami nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto. . . . nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama. . . nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao. . .umekuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwapo tena hata milele." Ezekieli 28:6-8,16-19.

"Maana Bwana ana ghadhabu juu ya mataifa yote" "Awanyeshee wasio haki mitego, Moto na kiberiti na upepo wa hari, Na viwe fungu la kikombe chao." Isaya34:2; Zaburi 11:6. Moto utashukakutoka mbinguni kwa Mungu. Dunia itavunjika. Miali ya moto ulao unaoteketeza utaibuka kutoka kwenye nyufa ardhini. Miamba yenyewe itashika moto. Vitu vitaunguzwa kwa moto mkali, dunia pia na matendo yaliyomo humo yataunguzwa. 2 Petro3:10. Uso wa dunia unaonekana kama tope kubwa, ziwa kubwa la moto. Ni "siku ya kisasi cha Bwana, mwaka wa malipo, ili kushindania Sayuni." Isaya 34:8.

Waovu wanaadhibiwa "sawasawa na matendo yao." Shetani atateseka sio tu kwa uasi wake lakini kwa dhambi zote alizosababisha watu wa Mungu kutenda. Hatimaye katika moto waovu wataangamizwa, mzizi na tawi-Shetani ndiye mzizi na wafuasi wake ni matawi. Adhabu kamili kwa uasi wa sheria imekwisha kutolewa; hitaji la haki yamekwisha kutimizwa. Kazi ya Shetani ya uharibifu imekomeshwa milele. Sasa viumbe wa Mungu wamekombolewa milele kutoka kwenye majaribu yake.

Wakati dunia itakupokuwa imefunikwa kwa moto, wenye haki [403]
wataendelea kukaa salama katika Mji wa Mtakatifu. Wakati Mungu

ni moto ulao kwa waovu, kwa watu wake yeye ni ngao. Angalia Ufunuo 20:6; Zaburi 84:11.

"Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita." Ufunuo 21:1. Moto utakaowaangamiza waovu utaitakasa dunia. Kila dalili ya laana itaondolewa. Hakuna moto wa kuzimu unaowaka milele utakaowafanya waliokombolewa kuwa na hofu ya matokeo mabaya ya dhambi.

### Mambo Yanayotukumbusha Kusulubishwa kwa Mwokozi

Jambo moja linalotukumbusha kusulubishwa litabakia: Mkombozi wetu daima atakuwa na alama za kusulubiwa kwake. Alama pekee za kazi ya ukatili iliyosababishwa na dhambi. Katika kipindi chote cha milele majeraha aliyoyapata Kalvari yataonesha sifa zake na kutangaza uwezo wake.

Kristo aliwahakikishia wanafunzi wake kwamba alikwenda kuwaandalia makao kwenye nyumba ya Baba yake. Lugha ya binadamu haitoshelezi kuelezea ujira wa wenye haki. Utajulikana tu kwa wale watakaouona. Hakuna akili ya mwanadamu yeyote inayoweza kufahamu utukufu wa Paradiso ya Mungu.

Katika Biblia urithi wa waliokombolewa unaitwa "nchi" Waebrania 11 : 14-16. Hapo Mchungaji wa mbinguni atawaongoza kondoo wake kwenye vijito vya maji ya uzima. Pale kuna vijito vinavyotiririka vilivyo angavu kama bilauri, na pembeni mwa vijito hivyo miti itakuwa inapepea na kutupa vivuli vyao kwenye njia zilizoandaliwa kwa ajili ya waliokombolewa na Bwana. Tambarare kubwa zinainuka na kuwa vilima vizuri, na vilele vya milima ya Mungu inasimama kwa fahari. Kwenye tambarare zile zilizokuwa zimetulia, kando ya vijito vya uzima, watu wa Mungu, ambao kwa muda mrefu hawakuwa na makao wenye kutangatanga watapata mahali pa kuishi.

"Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu, na kula matunda yake." "Hawatajenga, akakaa mtu mwingine ndani yake; hawatapanda, akala mtu mwingine: . . . "wateule
[404] wangu wataifurahia kazi ya mikono yao" . .. Nyika na mahali palipo ukiwa patafurahi; jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi." "Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na

chui atalala pamoja na mwana- mbuzi; . . na mtoto mdogo atawaongoza.". .Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; Isaya 65:21,22; 35:1; 11:6,9.

Maumivu hayawezi kuwepo mbinguni. Hakutakuwa tena na machozi, wala misafara ya mazishi "Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, . . .kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." "Wala hapana mwenyeji atakayesema, Mimi mgonjwa; watu wakaao humo watasamehewa uovu wao." Ufunuo 21:4; Isaya 33:24.

Kuna Yerusalemu Mpya, makao makuu ya dunia mpya na yenye utukufu. "Mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi, safi kama bilauri." "Na mataifa ya waliokombolewa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake." "Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao." Ufunuo 21:11, 24,3.

Katika mji wa Mungu "hapatakuwa na usiku" Ufunuo 22:5. Hapatakuwa na kuchoka. Daima tutajisikia kuwa na nguvu ya asubuhi na kuendelea kuwa katika hali hiyo. Mwanga wa jua utazidiwa na mng'ao usiopungua, ambayo unapita mng'ao wa mwezi. Waliokombolewa watatembea katika utukufii wa siku isiyo kuwa na ukomo.

"Nami sikuona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo, ndio hekalu lake." Ufunuo 21:22. Watu wa Mungu wanapata fursa ya kuwa na mazungumzo ya wazi na Baba na Mwana. Sasa tunaitazama sura ya Mungu kama vile kwenye kioo, lakini tutakapomwona uso kwa uso, bila kuwa na utaji katikati.

### Kushinda Kwa Upendo Wa Mungu

Kule upendo na huruma ambazo Mungu mwenyewe ameweka kwenye mioyo vitapata uzoefu mtamu na wa kweli. Usharika halisi pamoja na viumbe watakatifu na waaminifu wa zama zote uhu- [405]
siano mtakatifu unaowaweka pamoja. "ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa." (Waefeso 3:15) -hawa wanasaidia kuleta furaha ya waliokombolewa.

Pale akili zisizoflkwa na mauti zitaelewa furaha isiyoshindwa ya maajabu ya nguvu ya uumbaji, siri ya upendo wa ukombozi. Kila sehemu itaendelezwa, kila uwezo kuongezeka. Kupatikana kwa maarifa hakutachosha nguvu. Biashara kubwa zinaweza kufanyika, matarajio makubwa yanaweza kufikiwa, na shauku kubwa zinaweza kufikiwa. Na bado kutainuka viwango vya juu kufikia, maajabu mapya ya kustaajabia, kweli mpya za kuelewa, vitu vipya vya kuonesha uwezo wa akili, mwili na roho.

Hazina zote za ulimwengu zitafunguliwa kwa waliokobolewa na Mungu. Hawatatawaliwa na kifo. Wataaruka pasipo kuchoka kwenda ulimwengu wa mbali. Watoto wa dunia wataingia katika furaha na hekima ya viumbe wasioanguka na watashiriki hazina za maarifa walizozipata vizazi na vizazi. Kwa kuona bila kukoma wanashangaa utukufu wa uumbaji-jua na nyota na mifumo, yote katika utaratibu uliopangwa vikizunguka kiti cha enzi cha Mungu.

Na miaka ya milele inapoendelea, italeta ufunuo wa utukufu zaidi wa Mungu na Wakristo. Kwa kadri watu watakapojifunza zaidi kuhusu Mungu ndivyo watakavyozidi kuishangaa tabia yake. Wakati Yesu atakapofungua mbele yao utajiri wa ukombozi wao na mafanikio ya kushangaza katika pambano kuu dhidi ya Shetani, mioyo ya waliokombolewa itasisimuka kwa kujitoa, na elfu kumi mara elfu kumi sauti zinainua kiitikio cha sifa.

[406] "Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele." Ufunuo 5:13 Pambano kuu limekwisha. Dhambi na wenye dhambi hawapo tena. Ulimwengu wote ni safi. Pigo moja la usawa na furaha linasambaa katika uumbaji wote. Kuoka kwake yeye aliyeumba vyote, unatiririka uzima na mwanga katika ulimwengu usio na kikomo. Kuanzia kwenye chembe ndogo hadi kwenye ulimwengu mkubwa, vitu vyote vyenye uhai na visivyo na uhai katika uzuri wake halisi vinatangaza Mungu ni upendo.